JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# HALI YA UCHUMI WA TAIFA KATIKA MWAKA 2020

Kimetolewa na:
**Wizara ya Fedha na Mipango**
**DODOMA - TANZANIA**
**Juni 2021**

# HALI YA UCHUMI WA TAIFA KATIKA MWAKA 2020

## YALIYOMO

**ORODHA YA MAJEDWALI** ........ **viii**
**KIREFU/TAFSIRI YA MANENO** ........ **xiii**
**MATUKIO MUHIMU YA KIUCHUMI KWA MWAKA 2020** ........ **xvii**

**SURA YA I** ........ **1**
**HALI YA UCHUMI WA TAIFA** ........ **1**
UKUAJI WA UCHUMI ........ 1
MWENENDO WA BEI ........ 6
UKUZAJI RASILIMALI ........ 9

**SURA YA 2** ........ **35**
**FEDHA NA TAASISI ZA FEDHA** ........ **35**
UJAZI WA FEDHA ........ 35
MWENENDO WA MIKOPO KWA SERIKALI KUU NA SEKTA BINAFSI ........ 35
AMANA KATIKA BENKI ZA BIASHARA ........ 36
MWENENDO WA VIWANGO VYA RIBA ........ 36
MAENDELEO KATIKA SEKTA YA FEDHA ........ 37
HUDUMA ZA BENKI ........ 37
HUDUMA NDOGO ZA FEDHA ........ 38
MAMLAKA YA MASOKO YA MITAJI NA DHAMANA ........ 39
MFUKO WA HIFADHI YA JAMII KWA WATUMISHI WA UMMA ........ 40
MFUKO WA FIDIA KWA WAFANYAKAZI ........ 41
MFUKO WA TAIFA WA BIMA YA AFYA ........ 42

**SURA YA 3** ........ **53**
**FEDHA ZA SERIKALI** ........ **53**
UTANGULIZI ........ 53
MWENENDO WA MAPATO ........ 54
MAPATO YA NDANI ........ 54
MIKOPO YA NDANI ........ 54
MIKOPO YENYE MASHARTI YA KIBIASHARA ........ 55
MWENENDO WA MATUMIZI ........ 55
DENI LA SERIKALI ........ 56
DENI LA NJE ........ 57
DENI LA NJE KWA WAKOPESHAJI ........ 57
DENI LA NDANI ........ 58
DENI LA NDANI KWA WAKOPESHAJI ........ 58
TATHMINI YA UHIMILIVU WA DENI ........ 59

**SURA YA 4** ........ **64**
**SEKTA YA NJE** ........ **64**
BIDHAA ZILIZOUZWA NJE ........ 64
BIDHAA ASILIA ........ 64

BIDHAA ZISIZO ASILIA ........ 65
MAPATO YA HUDUMA ........ 68
BIDHAA ZILIZOAGIZWA KUTOKA NJE YA NCHI ........ 68
MALIPO YA HUDUMA ........ 69
MWENENDO WA BIASHARA BAINA YA TANZANIA NA NCHI MBALIMBALI ........ 69
MIZANIA YA MALIPO NA NCHI ZA NJE ........ 74

**SURA YA 5 ........ 88**
**HALI YA UCHUMI WA DUNIA ........ 88**
UKUAJI WA UCHUMI ........ 88
MWENENDO WA BEI ........ 89
MWENENDO WA BIASHARA DUNIANI ........ 90
USHIRIKIANO WA UCHUMI KIMATAIFA ........ 90
USHIRIKIANO WA KIUCHUMI BARANI AFRIKA ........ 91
USHIRIKIANO WA KIUCHUMI KATIKA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI ........ 92
UTEKELEZAJI WA HIMAYA MOJA YA FORODHA ........ 92
MAPITIO YA WIGO WA PAMOJA WA USHURU WA FORODHA ........ 92
ITIFAKI YA UMOJA WA FEDHA WA AFRIKA MASHARIKI ........ 93
USHIRIKIANO BAINA YA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI NA KANDA NYINGINE ........ 94
SEKTA ZA MIUNDOMBINU NA HUDUMA ZA JAMII KATIKA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI ........ 94

**SURA YA 6 ........ 95**
**RASILIMALI WATU ........ 95**
IDADI YA WATU ........ 95
MGAWANYIKO WA WATU KIMKOA ........ 95
NGUVU KAZI NA AJIRA ........ 97
WAKALA WA HUDUMA ZA AJIRA TANZANIA ........ 99

**SURA YA 7 ........ 102**
**UENDELEZAJI WA SEKTA BINAFSI ........ 102**
MGAWANYIKO WA USAJILI WA MIRADI KISEKTA ........ 102
MGAWANYIKO WA MIRADI KIMKOA ........ 103
RIPOTI YA UWEKEZAJI TANZANIA YA MWAKA 2020 ........ 104
JUMLA YA UWEKEZAJI WA SEKTA BINAFSI KUTOKA NJE ........ 104
UWEKEZAJI WA SEKTA BINAFSI KWA MIAKA HUSIKA ........ 104
AJIRA KUTOKANA NA UWEKEZAJI KUTOKA NJE ........ 105
URAHISI WA KUWEKEZA NA KUFANYA BIASHARA NCHINI ........ 105
UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI ........ 105
UBIA KATI YA SEKTA YA UMMA NA SEKTA BINAFSI ........ 107

**SURA YA 8 ........ 109**
**MASUALA MTAMBUKA ........ 109**
UKIMWI ........ 109

MAPAMBANO DHIDI YA VIRUSI VYA UKIMWI NA UKIMWI ........ 109
MAZINGIRA ........ 109
ULINZI NA USALAMA WA RAIA ........ 111
VITAMBULISHO VYA TAIFA ........ 112
USAJILI, UFILISI NA UDHAMINI ........ 113
UTAWALA BORA ........ 113

**SURA YA 9 ........ 115**
**HALI YA UMASKINI NA MAENDELEO YA WATU ........ 115**
UTANGULIZI ........ 115
HALI YA UMASKINI ........ 115
MPANGO WA KUNUSURU KAYA MASKINI ........ 116
MAENDELEO YA WATU ........ 117

**SURA YA 10 ........ 120**
**TANZANIA KUINGIA HADHI YA UCHUMI WA KATI WA CHINI ........ 120**
UTANGULIZI ........ 120
VIASHIRIA VYA UCHUMI WA TANZANIA KUELEKEA HADHI YA UCHUMI WA KATI... 121
UKUAJI WA UCHUMI NA IDADI YA WATU ........ 121
MFUMUKO WA BEI ........ 122
THAMANI YA SHILINGI ........ 122
MAUZO NJE ........ 122
DENI LA SERIKALI NA UHIMILIVU WA DENI ........ 123
MAENDELEO YA WATU ........ 123
HALI YA UMASKINI ........ 124
TOFAUTI ZA KIPATO ........ 125
MWENENDO WA MAPATO NA MATUMIZI ........ 125
MAPATO YA NDANI ........ 125
MISAADA NA MIKOPO NAFUU ........ 126
MIKOPO YA KIBIASHARA ........ 126
UGHARAMIAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ........ 127
WASTANI WA PATO KWA MTU ........ 128
MISAADA NA MIKOPO KUTOKA TAASISI NA MASHIRIKA YA FEDHA YA KIMATAIFA 130
BENKI YA DUNIA ........ 131
SHIRIKA LA FEDHA LA KIMATAIFA ........ 132
BENKI YA MAENDELEO YA AFRIKA ........ 132
FURSA NA CHANGAMOTO ZA TANZANIA KUWA NCHI YA UCHUMI WA PATO LA KATI LA CHINI ........ 133
FURSA ZA NCHI KUWA NA HADHI YA UCHUMI WA PATO LA KATI ........ 133
CHANGAMOTO ZA NCHI KUWA HADHI YA UCHUMI WA PATO LA KATI ........ 135
MIKAKATI ENDELEVU YA KUBAKI KATIKA UCHUMI WA PATO LA KATI ........ 136
HITIMISHO ........ 137

**SURA YA 11** 140
**KILIMO NA USHIRIKA** 140
UZALISHAJI WA MAZAO YA KILIMO 140
MAZAO YA CHAKULA 140
MAZAO YA BIASHARA 140
MAZAO YA BUSTANI 141
MAZAO YA MBEGU ZA MAFUTA 141
UPATIKANAJI WA PEMBEJEO ZA KILIMO 142
MWENENDO WA BEI NA MASOKO YA MAZAO 143
HUDUMA ZA UGANI 143
UTAFITI 143
MAFUNZO YA KILIMO 144
UMWAGILIAJI 144
MIFUGO 144
UZALISHAJI WA MALISHO NA UTENGENEZAJI WA VYAKULA VYA MIFUGO 145
BIASHARA YA MIFUGO NA MAZAO YAKE 146
VYUO VYA MAFUNZO YA MIFUGO 148
UTAFITI WA MIFUGO 149
HUDUMA ZA UGANI KATIKA MIFUGO 149
MAENDELEO YA USHIRIKA 150
UVUVI 151
USIMAMIZI WA RASILIMALI ZA UVUVI 151
UZALISHAJI VIFARANGA VYA SAMAKI, SAMAKI NA VIUMBE MAJI 151
UVUNAJI WA SAMAKI 152
UDHIBITI WA UBORA NA USALAMA WA MAZAO YA UVUVI 153
UWEKEZAJI KATIKA SEKTA YA UVUVI 153
MWENENDO WA UUZAJI NA UINGIZAJI WA MAZAO YA UVUVI NJE YA NCHI 153
**SURA YA 12** 164
**MALIASILI NA UTALII** 164
MISITU NA NYUKI 164
WANYAMAPORI 165
UTALII 166
MALIKALE 168
**SURA YA 13** 175
**MADINI** 175
UTAFUTAJI MADINI 175
VIBALI VYA UUZAJI WA MADINI 175
DHAHABU 175
ALMASI 176
VITO VYA THAMANI 176
TANZANITE 176

MAKAA YA MAWE ........ 176
MADINI MENGINE ........ 177
MADINI UJENZI ........ 177
MASOKO YA MADINI ........ 177
**SURA YA 14........ 181**
**VIWANDA NA BIASHARA........ 181**
UZALISHAJI WA BIDHAA VIWANDANI ........ 181
UENDELEZAJI WA VIWANDA VIDOGO NA BIASHARA NDOGO ........ 181
MIUNDOMBINU YA MASOKO YA BIDHAA ZA MAZAO NA MIFUGO ........ 184
USAJILI WA BIASHARA NA VIWANDA ........ 185
MAONESHO YA KIBIASHARA YA KIMATAIFA ........ 185
UDHIBITI WA UBORA WA VIWANGO NA VIPIMO ........ 186
USAWA WA USHINDANI NA UDHIBITI WA BIDHAA BANDIA ........ 187
SHIRIKA LA MAENDELEO LA TAIFA ........ 188
MAMLAKA YA MAENEO MAALUM YA UWEKEZAJI ........ 188
**SURA YA 15........ 195**
**UJENZI NA MAENDELEO YA ARDHI ........ 195**
UJENZI ........ 195
MTANDAO WA BARABARA NCHINI ........ 195
BARABARA, MADARAJA, VIVUKO NA MAGARI ........ 196
MTANDAO WA BARABARA ZA VIJIJINI NA MIJINI ........ 197
MFUKO WA BARABARA ........ 198
NYUMBA NA MAJENGO YA SERIKALI ........ 198
USAJILI WA MAKANDARASI ........ 198
USAJILI WA WAHANDISI ........ 199
WABUNIFU MAJENGO NA WAKADIRIAJI MAJENZI ........ 200
BARAZA LA TAIFA LA UJENZI ........ 200
TAASISI YA TEKNOLOJIA YA UJENZI ........ 201
MAENDELEO YA ARDHI ........ 201
UTAYARISHAJI WA HATIMILIKI, UKAGUZI NA UHAKIKI MILKI ........ 201
USAJILI WA HATIMILIKI ZA ARDHI NA NYARAKA ZA KISHERIA ........ 202
UTHAMINI WA MALI ........ 202
UPIMAJI WA MASHAMBA NA VIWANJA ........ 202
MIPANGO YA MATUMIZI YA ARDHI ........ 203
URASIMISHAJI WA MAKAZI HOLELA ........ 204
MABARAZA YA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA ........ 204
UJENZI WA NYUMBA ZA MAKAZI NA BIASHARA ........ 205
**SURA YA 16........ 206**
**MAWASILIANO NA UCHUKUZI ........ 206**

**UCHUKUZI** .......... **206**
USAFIRI WA BARABARA .......... 206
USAFIRI KWA NJIA YA RELI .......... 206
USAFIRI WA ANGA .......... 208
KAMPUNI YA NDEGE TANZANIA .......... 209
USAFIRI KWA NJIA YA MAJI .......... 210
MAMLAKA YA USIMAMIZI WA BANDARI TANZANIA .......... 211
UCHUKUZI KWENYE MAZIWA .......... 213
MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA .......... 214
UDHIBITI WA MIONZI .......... 215
**HUDUMA ZA MAWASILIANO** .......... **215**
HUDUMA ZA POSTA .......... 215
HUDUMA ZA SIMU .......... 217
HUDUMA ZA INTANETI .......... 217
HUDUMA ZA UTANGAZAJI .......... 218
UTOAJI WA LESENI ZA MAWASILIANO .......... 218
MKONGO WA TAIFA WA MAWASILIANO .......... 219
HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO .......... 219
SEKTA YA HABARI .......... 219
**MAENDELEO YA SANAA** .......... **219**
USAJILI WA WABUNIFU NA KAZI ZA SANAA .......... 220
BARAZA LA KISWAHILI LA TAIFA .......... 220
MAENDELEO YA KISWAHILI KATIKA JUMUIYA YA MAENDELEO KUSINI MWA AFRIKA .......... 221
MAENDELEO YA MICHEZO .......... 221
**SURA YA 17** .......... **232**
**NISHATI** .......... **232**
UFUAJI WA UMEME .......... 232
UTAFUTAJI WA MAFUTA NA GESI .......... 236
GESI ASILIA .......... 236
UAGIZAJI MAFUTA .......... 237
MAFUTA YALIYOINGIZWA NCHINI KWENDA NCHI JIRANI .......... 237
MWENENDO WA BEI ZA MAFUTA .......... 238
NISHATI JADIDIFU .......... 239
NISHATI MBADALA YA GESI INAYOTOKANA NA PETROLI .......... 239
NISHATI YA MIONZI YA JUA .......... 240
**SURA YA 18** .......... **241**
**MAJI** .......... **241**
USIMAMIZI NA UENDELEZAJI WA RASILIMALI ZA MAJI .......... 241
HUDUMA YA MAJI VIJIJINI .......... 242
HUDUMA YA MAJI MIJINI .......... 242

UCHIMBAJI WA VISIMA ..... 243
UONDOAJI WA MAJITAKA ..... 243

**SURA YA 19 ..... 246**
**ELIMU MAFUNZO YA UFUNDI NA TEKNOLOJIA ..... 246**
ELIMU YA AWALI ..... 246
ELIMU YA MSINGI ..... 246
ELIMU YA SEKONDARI ..... 247
ELIMU KATIKA VYUO VYA UALIMU ..... 248
UKAGUZI WA SHULE NA VYUO VYA UALIMU ..... 248
ELIMU YA UFUNDI NA MAFUNZO ..... 248
ELIMU YA UFUNDI STADI NA VYUO VYA MAENDELEO YA WANANCHI ..... 249
ELIMU YA JUU ..... 249
TEKNOLOJIA NA UBUNIFU ..... 249

**SURA YA 20 ..... 257**
**AFYA NA MAENDELEO YA JAMII ..... 257**
AFYA ..... 257
VITUO VYA KUTOLEA HUDUMA ZA AFYA ..... 257
HUDUMA ZA CHANJO KWA WATOTO CHINI YA MWAKA MMOJA ..... 257
DAWA NA VIFAA TIBA ..... 257
AFYA YA UZAZI NA MTOTO ..... 258
HUDUMA ZA MATIBABU YA KIBINGWA ..... 259
UDHIBITI WA MALARIA ..... 259
UDHIBITI WA KIFUA KIKUU ..... 259
UVIKO - 19 ..... 260
LISHE ..... 260
MAFUNZO KATIKA KADA ZA AFYA ..... 261
MAENDELEO YA JAMII ..... 261
MAFUNZO YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII ..... 261
MAENDELEO YA WANAWAKE NA JINSIA ..... 262
HUDUMA ZA USTAWI NA MAENDELEO YA WATOTO ..... 262
HUDUMA YA MALEZI, MAKUZI NA MAENDELEO YA AWALI YA MTOTO ..... 263
HUDUMA ZA USTAWI KWA WAZEE ..... 263
MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI ..... 264

**Ukurasa**

## ORODHA YA MAJEDWALI


Jedwali A: Takwimu Muhimu Katika Uchumi – Tanzania Bara ................................xviii

Jedwali B: Mwenendo wa Viashiria vya Kiuchumi, 2013-2019……...........................xix

Jedwali 1: Pato la Taifa kwa shughuli za kiuchumi, kwa Bei za Soko (Bei za miaka inayohusika) ..........................................................................................10

Jedwali 1A Pato la Taifa kwa shughuli za kiuchumi, kwa Bei za Soko – Sehemu inayouzika na isiyouzika (Bei za miaka inayohusika).................................11

Jedwali 2: Mchango wa shughuli za kiuchumi kwa Pato la Taifa kwa Bei za Soko (Bei za miaka inayohusika) ...................................................................12

Jedwali 2A: Mchango wa shughuli za kiuchumi kwa Pato la Taifa kwa Bei za Soko-Sehemu inayouzika na isiyouzika (Bei za miaka inayohusika) …………...13

Jedwali 2B: Pato la Taifa na Matumizi yake, kwa bei za soko (Bei za miaka inayohusika) ..................................................................................................14

Jedwali 3: Pato la Taifa kwa shughuli za kiuchumi, (Kwa Bei za mwaka 2015)........15

Jedwali 3A: Pato la Taifa kwa shughuli za kiuchumi, kwa Bei za Soko - Sehemu inayouzika na isiyouzika (Kwa Bei za mwaka 2015)................................16

Jedwali 4: Ukuaji wa Pato la Taifa kwa shughuli za kiuchumi, (Kwa Bei za mwaka 2015) ..........................................................................................................17

Jedwali 4A: Ukuaji wa Pato la Taifa kwa shughuli za kiuchumi, kwa Bei za Soko - Sehemu inayouzika na isiyouzika (Bei za mwaka 2015) ............................19

Jedwali 4B: Pato la Taifa (PLT) na matumizi yake, kwa bei za soko (Bei za mwaka 2015) ..................................................................................................20

Jedwali 5: Ukuzaji Rasilimali kwa aina ya shughuli (bei za miaka inayohusika)......... 21

Jedwali 6: Ukuzaji Rasilimali kwa aina ya shughuli (Bei za mwaka 2015)………......22

Jedwali 7A: Mchango katika Ukuzaji Rasilimali kwa aina ya Shughuli (Kwa Bei za Miaka inayohusika) ........................ ............................................................23

Jedwali 7B: Ukuzaji wa Rasilimali katika Sehemu za Uchumi wa Kitaifa na Binafsi (Kwa bei za Miaka inayohusika).................................................................24

Jedwali 8: Fahirisi za bei za rejereja ya bidhaa zitumiwazo na watu wa kipato cha chini Dar es Salaam (Des. 2015=100)……… ....................................................25

Jedwali 9: Fahirisi za Bei za rejereja ya bidhaa zitumiwazo na watu wa kipato cha chini D'Salaam (Des. 2015=100) ..........................................................................26

Jedwali 10: Fahirisi za bei za bidhaa na huduma zitumiwazo na wafanyakazi wa kima cha kati Dar es Salaam (Des. 2015= 100)..........................................................27

Jedwali 11: Fahirisi ya Bei za bidhaa na huduma zitumiwazo na wafanyakazi wa kima cha kati D'Salaam (Des. 2015=100). ........................................................28

Jedwali 12: Fahirisi ya Bidhaa na Huduma zitumiwazo na wenye kipato cha juu Dar es Salaam (Des. 2015=100) ............................................................................ 29

Jedwali 13: Fahirisi ya gharama ya maisha ya wenye kipato cha juu Dar es Salaam (Des. 2015=100) ...............................................................................................30

Jedwali 14: Fahirisi ya bei ya bidhaa na huduma zitumiwazo na wakazi wa mijini - Tanzania Bara (2015=100)……..................................................................31

Jedwali 15: Fahirisi ya Bei ya Bidhaa na huduma zitumiwazo na wakazi wa mijini - Tanzania Bara (Des. 2015=100) .................................................................32

Jedwali 16: Fahirisi mbali mbali za bidhaa na huduma zitumiwazo na wakazi wa mijini – Tanzania Bara (Des. 2015=100) .................................................................33

Jedwali 17: Mwenendo wa karadha na ujazi wa fedha - Tanzania Bara .........................48

Jedwali 18: Viwango vya ukuaji wa karadha na ujazi wa fedha - Tanzania Bara ......... 49

Jedwali 19: Mwenendo wa Viwango vya ubadilishaji kati ya Shilingi na Dola ya Marekani ..............................................................................................50

Jedwali 20: Mikopo ya benki za biashara kwa Shughuli za Kiuchumi............................50

Jedwali 21: Mwenendo wa amana katika benki za biashara .........................................51

Jedwali 22: Viwango vya wastani vya riba (asilimia) ..................................................51

Jedwali 23: Mwenendo wa mapato na matumizi ya Serikali .........................................59

Jedwali 24: Mgawanyo wa Matumizi ya Serikali kwa huduma za Serikali (Sh. Milioni) ...................................................................................................................61

Jedwali 25: Thamani ya Bidhaa za biashara baina ya Tanzania na nchi za nje (Sh. Milioni) ..........................................................................................76

Jedwali 26: Kiasi na thamani ya bidhaa muhimu zilizouzwa nchi za nje (Sh. Milioni) ..........................................................................................................77

Jedwali 27: Kiasi na thamani ya bidhaa za asilia na zisizo asilia zilizouzwa nchi za nje ..........................................................................................................78

Jedwali 28: Wastani wa bei za bidhaa muhimu zilizouzwa nchi za nje (Sh./tani) ……...82

Jedwali 29: Wastani wa bei za bidhaa muhimu zilizouzwa nchi za nje (US$/tani) .........83

Jedwali 30: Mizania ya malipo na nchi za nje (US$ milioni) ............…………….......85

Jedwali 31: Idadi ya watu nchini Tanzania kimkoa (2012-2020) ...................................99

Jedwali 32: Kituo cha Uwekezaji Tanzania - TIC: Miradi ya uwekezaji iliyosajiliwa …..................................................................................................107

Jedwali 33: Uzalishaji wa miwa na sukari nchini..........................................................152

Jedwali 34: Pamba iliyonunuliwa na mauzo nchini.......................................................153

Jedwali 35: Eneo lililopandwa michai na majani mabichi yaliyopatikana …………....154

Jedwali 36: Kahawa iliyonunuliwa na mauzo nchini ....................................................155

Jedwali 37: Eneo lililopandwa mkonge na katani iliyopatikana ..................................156

Jedwali 38: Maua ya pareto yaliyonunuliwa na mauzo ya bidhaa za pareto nchini ......157

Jedwali 39: Muhtasari wa kiasi cha mazao muhimu ya biashara yaliyonunuliwa ........158

Jedwali 40: Uzalishaji katika sekta ya uvuvi (2000-2019)……………………………159

Jedwali 40A: Mwenendo wa uuzaji wa samaki nje ya nchi 2011-2020 ...........................160

Jedwali 40B: Mwenendo wa ukuzaji viumbe maji 2015 - 2020 ...................................160

Jedwali 41: Idadi ya wageni waliotembelea Hifadhi za Taifa na Mapato yaliyopatikana ..........................................................................................................167

Jedwali 42: Mauzo ya bidhaa za misitu katika masoko ya nje......................................168

Jedwali 43: Idadi na Mapato yatokanayo na Uwindaji wa Kitalii ................................169

Jedwali 44: Mwenendo wa Biashara ya Utalii ............................................................170

Jedwali 45: Watalii waliotembelea Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro……………171

Jedwali 46: Uchimbaji wa madini: Kiasi kilichopatikana ............................................176

Jedwali 47: Madini yaliyouzwa nchi za nje (2016-2020) .............................................177

Jedwali 48: Matumizi ya saruji nchini .........................................................................186

Jedwali 49: Uzalishaji wa baadhi ya bidhaa za viwandani .................………………187

Jedwali 50: Viwanda - Idadi ya Watu walioajiriwa ......................................................188

Jedwali 51: Viwanda - Gharama za kazi .....................................................................189

Jedwali 52: Viwanda - Muhtasari wa Matokeo ............................................................190

Jedwali 53: Viwanda - Muhtasari wa Matokeo Kimkoa ..............................................191

Jedwali 54: Shirika la Reli Tanzania (TRL) ................................................................220

Jedwali 55: Reli ya Uhuru (TAZARA) ........................................................................221

Jedwali 56A: Usafirishaji kwa Meli: Dar Es Salaam ......................................................222

Jedwali 56B: Usafirishaji kwa Meli: Tanga ....................................................................223

Jedwali 56C: Usafirishaji kwa Meli: Mtwara .................................................................224

Jedwali 57: Huduma za Posta .......................................................................................225

Jedwali 58: Idadi ya Wanaotumia Simu za Mezani na Viganjani.................................226

Jedwali 59: Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) ..........................................................227

Jedwali 60: Uwezo wa Mitambo ya Umeme na Kiasi cha Umeme Uliotengenezwa kwa Vituo…………………………………………………………...............230

Jedwali 61: Mauzo ya Umeme kwa Watumiaji Mbalimbali .......................................231

Jedwali 62: Mauzo ya Umeme kwa Mikoa .................................................................231

Jedwali 63: Uzalishaji wa maji na mapato yatokanayo na maji Mijini………………..240

Jedwali 64: Mahitaji na Upatikanaji wa Maji katika Miji ............................................241

Jedwali 65: Shule za sekondari za Serikali - Idadi ya wanafunzi kwa kidato ..............247

Jedwali 65A: Idadi ya wanafunzi na walimu katika shule za msingi na sekondari kwa jinsia.........................................................................................................248

Jedwali 65B: Idadi ya taasisi za elimu………………………………………...................249

Jedwali 65C: Mafunzo ya walimu katika vyuo vya ualimu……………........................250

Jedwali 66: Shule za sekondari za binafsi - Idadi ya wanafunzi kwa kidato .................251

Jedwali 67: Idadi ya Vituo vya Kutolea Huduma za Afya………………………........260

Jedwali 68: Idadi ya Wagonjwa katika Vituo vya Afya................................................261

Jedwali 69: Idadi ya Vitanda katika Hospitali zote Nchini...........................................262

Jedwali 70: Udahili wa Wanafunzi katika Taasisi za Ustawi na Maendeleo ya Jamii…263

## KIREFU/TAFSIRI YA MANENO

| | |
|---|---|
| ARV | Antiretroviral Drugs |
| ATCL | Air Tanzania Company Limited (Kampuni ya Ndege Tanzania) |
| BAKITA | Baraza la Kiswahili la Taifa |
| BRELA | Business Registrations and Licensing Agency (Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni) |
| CAMARTEC | Centre for Agricultural Mechanization and Rural Technology (Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini) |
| CBE | College of Business Education |
| CFS | Container Freight Station (Yadi ya Kupakia Makasha) |
| CNC | Computer Numerical Control |
| COASCO | Co-operative Audit and Supervision Corporation (Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika) |
| COMESA | The Common Market for Eastern and Southern Africa (Jumuiya ya soko la pamoja la nchi za mashariki na kusini mwa Afrika) |
| COSOTA | Chama cha Hakimiliki Tanzania |
| CT | Computed Tomography |
| DSE | Dar es Salaam Stock Exchange (Soko la Hisa la Dar es Salaam) |
| EAC | The East African Community (Jumuiya ya Afrika Mashariki) |
| ECD | Empty Container Depot (Yadi ya Kuhifadhi Makasha Matupu) |
| EMS | Express Mail Service (Huduma ya Kutuma Fedha, Nyaraka na Vifurushi kwa njia ya Haraka) |
| EPZ | Export Processing Zone (Maeneo Maalumu ya Uwekezaji) |
| EPZA | Export Processing Zones Authority (Mamlaka ya Mauzo Nje) |
| FCC | Fair Competition Commission (Tume ya Ushindani) |
| GWh | Saa za Gigawati |
| HDI | Human Development Index (Farihisi ya Maendeleo ya Watu) |
| HPV | Human Papillomavirus Infection |
| ICD | Inland Container Depot (Yadi ya Bandari Kavu) |
| KPI | Key Performance Indicator |

| | |
|---|---|
| LITA | Livestock Training Agency (Wakala wa Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo) |
| LPG | Liquified Petroleum Gas (Gesi inayotokana na Petroli) |
| M1 | Narrow Money Supply (Ujazi wa fedha kwa Tafsiri Finyu) |
| M2 | Broad Money Supply (Ujazi wa Fedha kwa Tafsiri Pana) |
| M3 | Extended Broad Money Supply (Ujazi wa Fedha kwa Tafsiri Pana Zaidi) |
| MAKISATU | Mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu |
| MRI | Magnetic Resonance Imaging |
| MUST | Mbeya University of Science and Technology (Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya) |
| MV | Merchant Vessel |
| MW | Megawati |
| NBC | National Bank of Commerce |
| NEEC | National Economic Empowerment Council (Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi) |
| NHIF | National Health Insurance Fund (Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya) |
| NIC | National Insurance Corporation (Shirika la Bima la Taifa) |
| NIDA | National Identification Authority (Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa) |
| NSE | Nairobi Stock Exchange (Soko la Hisa la Nairobi) |
| NSSF | National Social Security Fund (Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii) |
| OPV | Oral Polio Vaccine |
| PCP | Programme for Country Partnership (Programu Shirikishi baina ya Nchi na Washirika wa Maendeleo) |
| pCUM | City Urgent Mail |
| PET | Positron Emmission Tomography |
| PSSSF | Public Service Social Security Fund (Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma) |
| PWP | Public Works Programme |
| SADC | The Southern African Development Community (Jumuiya ya maendeleo Kusini mwa Afrika) |
| SAT | Sustainable Agriculture Tanzania (Shirika la Kilimo Endelevu |

| | |
|---|---|
| | Tanzania) |
| SEZ | Special Economic Zone (Maeneo Maalumu ya Uwekezaji) |
| SGR | Standard Gauge Railway (Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa) |
| SIDO | Small Industries Development Organization (Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo) |
| SITE | Swahili International Tourism Expo |
| TaESA | Tanzania Employment Services Agency (Wakala ya Huduma za Ajira Tanzania) |
| TAHUDE | Tanzania Human Development Foundation |
| TAKUKURU | Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa |
| TAM | Tathimini ya Athari katika Mazingira |
| TANESCO | Shirika la Umeme Tanzania |
| TANROADS | Tanzania National Roads Agency (Wakala wa Barabara Tanzania) |
| TANTRADE | Tanzania Trade Development Authority (Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania) |
| TARI | Tanzania Agricultural Research Institute (Taaasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania) |
| TARURA | Tanzania Rural and Urban Roads Agency (Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini) |
| TASAF | Tanzania Social Action Fund (Mfuko wa Maendeleo ya Jamii) |
| TAWA | Tanzania Wildlife Management Authority (Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori) |
| TAZARA | Tanzania Zambia Railway Authority (Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia) |
| TBA | Tanzania Buildings Agency (Wakala wa Majengo Tanzania) |
| TBS | Tanzania Bureau of Standards (Shirika la Viwango Tanzania) |
| TCDC | Tanzania Cooperative Development Commission (Tume ya Maendeleo ya Ushirika) |
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TEMDO | Tanzania Engineering and Manufacturing Design Organisation |
| TEMESA | Tanzania Electrical, Mechanical and Electronics Services Agency (Wakala wa Ufundi na Umeme) |
| TEUs | Twenty Equivalent Units (Urefu wa Futi Ishirini) |
| TI | Transparency International |

| | |
|---|---|
| TIA | Tanzania Institute of Accountancy (Chuo cha Taasisi ya Uhasibu Tanzania) |
| TIC | Tanzania Investment Centre (Kituo cha Uwekezaji) |
| TICTS | Tanzania International Container Terminal Services (Kampuni ya Kupakua na Kupakia Makasha Tanzani) |
| TIN | Taxpayer Identification Number (Utambulisho wa Mlipa Kodi) |
| TIRA | Tanzania Insurance Regulatory Authority (Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima Tanzania) |
| TIRDO | Tanzania Industrial Research and Development Organization (Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania) |
| TMK | Tathmini ya Mazingira Kimkakati |
| TMRC | Tanzania Mortgage Refinance Company (Kampuni ya Mikopo ya Nyumba Tanzania) |
| TPA | Tanzania Ports Authority (Mamlaka ya Bandari Tanzania) |
| TPSF | Tanzania Private Sector Foundation (Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania) |
| TRA | Tanzania Revenue Authority (Mamlaka ya Mapato Tanzania) |
| UKIMWI | Upungufu wa Kinga Mwilini |
| UNDP | United Nations Development Programme (Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa) |
| UNIDO | The United Nations Industrial Development Organization (Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda) |
| USAID | United States Agency for International Development |
| UVIKO | Ugonjwa wa Virusi vya Korona |
| VETA | Vocational Education and Training Authority (Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi) |
| VVU | Virusi vya Ukimwi |
| WCF | Workers Compensation Fund (Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi) |
| WHC | Watumishi Housing Company (Kampuni ya Nyumba kwa Watumishi) |
| WMA | Weight and Measurement Agency (Wakala wa Vipimo) |

## MATUKIO MUHIMU YA KIUCHUMI KWA MWAKA 2020

| TAREHE | MWEZI | MATUKIO |
|---|---|---|
| 6 | Februari | Serikali yazindua Kipindi cha Pili cha Awamu ya Tatu ya TASAF. |
| 17 | Machi | Serikali yatangaza kusitishwa kwa muda kwa baadhi ya shughuli za kiuchumi kufuatia mlipuko wa UVIKO-19. |
| 23 | Mei | Maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii iliyopo Mabibo, Dar es salaam yenye uwezo wa kupima sampuli 1,800 za magonjwa ya mlipuko ndani ya masaa 24 yaanza kazi baada ya kukamilika kwa zoezi la upanuzi wa jingo la Maabara. |
| 11 | Juni | Serikali za nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zasoma Bajeti za mwaka 2020/21. |
| 01 | Julai | Benki ya Dunia yaitangaza Tanzania kuwa Nchi ya Hadhi ya Uchumi wa Kipato cha Kati cha Chini. |
| 04 | Julai | Serikali yazindua Baraza la Tano la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. |
| 10 | Julai | Serikali yazindua Mpango wa Uendelezaji wa Viwanda Vidogo na Kati. |

Jedwali Na. A

## TAKWIMU MUHIMU KATIKA UCHUMI-TANZANIA BARA

| Maelezo | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020p | 2020/19 Badiliko (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watu (Milioni) | 46.1 | 47.4 | 48.7 | 51.0 | 52.6 | 54.3 | 55.9 | 2.9 |
| Pato la Taifa kwa Bei za miaka inayohusika (Sh. Milioni) | 82,603,388 | 94,349,316 | 108,362,324 | 118,744,498 | 129,043,901 | 139,641,854 | 148,522,111 | 6.4 |
| Pato la Taifa kwa Bei za mwaka 2015 (Sh. Milioni) | 88,874,111 | 94,349,316 | 100,828,393 | 107,657,405 | 115,141,329 | 123,196,736 | 129,095,844 | 4.8 |
| Wastani Pato kwa Kila Mtu kwa bei za miaka inayohusika (Sh.) | 1,793,387 | 1,990,492 | 2,225,099 | 2,327,395 | 2,452,406 | 2,573,324 | 2,653,790 | 3.1 |
| Wastani Pato kwa Kila Mtu kwa bei za 2015 (Sh.) | 1,929,529 | 1,990,492 | 2,070,398 | 2,110,088 | 2,188,195 | 2,269,888 | 2,306,682 | 1.6 |
| Kasi ya Upandaji Bei (asilimia) | 6.1 | 5.6 | 5.2 | 5.3 | 3.5 | 3.4 | 3.3 | -2.9 |
| Urari wa Biashara ya Bidhaa (US$ milioni) | -5723.7 | -5016.3 | -3589.8 | -3040.95 | -3853.51 | -3415.5 | 1,517.2 | -55.6 |
| Urari wa Bidhaa, Huduma na Uhamisho wa Mali (US$ milioni) | -5,048.6 | -4,477.4 | -2,740.5 | -1,827.1 | -2248.3 | -1490.9 | -994.8 | -0.33 |
| Saruji Iliyotumika (Tani '000) | 4,082,681 | 4,404,187 | 6,028,794 | 4,359,163 | 4,577,117 | 6,104,108 | 6,777,008 | 11.0 |
| Umeme Uliouzwa (GWH)[r] | 5,051.5 | 5,297.1 | 5,496.1 | 5,565.8 | 5,876.6 | 6,161.0 | 6,199.4 | 0.6 |
| Utalii (Mapato US$ milioni) | 1,983.0 | 1,901.9 | 2,131.6 | 2,199.8 | 2,432.9 | 2,604.5 | 714.5 | -72.6 |
| Reli: Uchukuzi Mizigo (Tani '000) | 160.0 | 363.6 | 198.0 | 341.0 | 379.3 | 355.1 | 339.7 | -4.3 |
| Elimu: Wanafunzi katika Shule za Msingi ('000) * | 8222.7 | 8298.3 | 8639.2 | 9317.8 | 10,112 | 10,605 | 10,925 | 3.0 |
| Elimu: Wanafunzi katika Shule za Sekondari ('000) * | 1947.3 | 1774.4 | 1807.0 | 1908.9 | 2,149 | 2,338 | 2,473 | 5.8 |
| Hospitali: Idadi ya Vitanda | 50,670 | - | 59,757 | 60,952 | 62,203 | 80,164 | 84,162 | 5.0 |
| **Mauzo Nje ya Mazao Muhimu ya Biashara (Mil. US$)** | | | | | | | | |
| **Bidhaa Asilia** | | | | | | | | |
| Kahawa | 130.52 | 160.88 | 153.69 | 126.27 | 148.00 | 152.2 | 145.2 | -4.6 |
| Pamba | 52.31 | 28.16 | 46.76 | 36.76 | 68.38 | 91.8 | 87.5 | -4.6 |
| Katani | 16.76 | 26.53 | 17.23 | 28.73 | 32.54 | 19.3 | 17.6 | -8.9 |
| Chai | 57.10 | 47.21 | 44.79 | 49.13 | 45.82 | 45.7 | 32.4 | -29.1 |
| Tumbaku | 137.79 | 214.79 | 339.20 | 195.81 | 269.95 | 146.5 | 148.7 | 1.5 |
| Korosho | 212.09 | 196.42 | 320.24 | 529.70 | 109.56 | 353.1 | 359.6 | 1.8 |
| Karafuu | 15.91 | 25.49 | 10.47 | 55.42 | 0.36 | 9.1 | 17.1 | 87.9 |
| **Bidhaa zisizo Asilia** | | | | | | | | |
| Madini | 1926.32 | 1893.92 | 1930.02 | 1694.48 | 1615.40 | 2,326.7 | 3,369.1 | 44.8 |
| Bidhaa za Viwanda | 1139.10 | 785.44 | 684.86 | 676.27 | 894.29 | 851.8 | 908.6 | 6.7 |
| Samaki na Mazao ya Samaki | 167.91 | 161.48 | 143.70 | 193.01 | 181.85 | 168.0 | 139.6 | -16.9 |
| Mazao ya Mboga na Maua | 19.29 | 193.27 | 274.10 | 148.65 | 147.70 | 202.4 | 274.1 | 35.4 |
| Bidhaa zilizouzwa tena (Re-export) | 219.77 | 339.08 | 194.07 | 143.16 | 186.71 | 242.8 | 87.7 | -63.9 |
| Bidhaa nyinginezo | 500.68 | 315.25 | 271.64 | 223.29 | 340.40 | 394.3 | 474.2 | -20.3 |
| **Ujazi wa Fedha** | | | | | | | | |
| Ujazi wa Fedha-M3 (Sh. bilioni) | 18,614.2 | 22,115.3 | 22,877.8 | 24,714.3 | 25,823.5 | 28,313.1 | 29,918.2 | 5.7 |
| Karadha (Sh. bilioni) | 18,863.7 | 22,505.5 | 23,775.8 | 24,977.2 | 26,249.3 | 28,103.3 | 26,139.6 | -7.0 |
| **Fedha za serikali** | **2014/15** | **2015/16** | **2016/17** | **2017/18** | **2018/19p** | **2019/20** | **2020/21** | **2020/21 Badiliko** |
| Mapato ya Ndani ya Serikali (Sh. milioni) | 10,957,765.3 | 14,048,034.0 | 16,639,831.5 | 17,944,887.0 | 18,529,558.0 | 21,069,956.8 | 24,065,543 | 14.2 |
| Matumizi ya Kawaida ya Serikali (Sh. milioni) | 10,893,486.1 | 13,420,045.1 | 11,625,865.8 | 12,852,304.0 | 13,806,788.9 | 14,201,148 | 16,321,179 | 14.9 |
| Matumizi ya Maendeleo ya Serikali (Sh. milioni) | 3,710,228.2 | 4,339,552.9 | 7,272,824.3 | 7,615,768.3 | 8,493,838.5 | 9,301,503 | 12,779,255 | 37.4 |

**Chanzo:** Wizara ya Fedha na Mipango

[1]Takwimu imeboreshwa

Jedwali Na. B **MWENENDO WA VIASHIRIA VYA UCHUMI MKUU NA BAJETI (2013 - 2020)**

| Mwaka wa Kalenda | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| PATO LA TAIFA | | | | | | | | |
| Ukuaji halisi wa Pato la Taifa (mp) | 6.8% | 6.7% | 6.2% | 6.9% | 6.8% | 7.0% | 7.0% | 4.8% |
| Ukuaji wa Pato la Taifa kwa Bei za Miaka Husika (mp) | 17.1% | 13.2% | 14.2% | 14.9% | 9.6% | 8.7% | 8.2% | 6.4% |
| Uwiano wa Uwekezaji na Pato la Taifa (Investment/GDP) | 37.5% | 37.7% | 32.8% | 32.2% | 34.0% | 38.4% | 39.9% | 39.7% |
| Uwiano wa Akiba kwenye Benki na Pato la Taifa (Savings/GDP) | 10.7% | 13.0% | 13.2% | 17.2% | 15.8% | 16.3% | 18.0% | 18.3% |
| MWENENDO WA BEI NA VIWANGO VYA RIBA | | | | | | | | |
| Kasi ya Upandaji wa Bei (mwisho wa kipindi) | 5.6% | 4.8% | 6.8% | 6.5% | 4.0% | 3.3% | 3.8% | 3.2% |
| Kasi ya Upandaji wa Bei (wastani wa mwaka) | 7.9% | 6.1% | 5.6% | 5.2% | 5.3% | 3.5% | 3.4% | 3.3% |
| GDP deflator Inflation (bp) | 10.7% | 4.8% | 6.1% | 7.1% | 2.5% | 2.0% | 0.9% | 0.7% |
| GDP deflator Inflation (MP) | 9.7% | 6.1% | 7.6% | 7.5% | 2.6% | 1.6% | 1.1% | 1.1% |
| Riba za Mikopo (mwaka mmoja) | 14.0% | 14.7% | 14.2% | 13.7% | 18.3% | 18.2% | 16.7% | 15.7% |
| Riba za Amana za muda maalum (miezi 12) | 11.6% | 10.8% | 10.8% | 11.5% | 11.7% | 8.8% | 8.8% | 8.3% |
| Tofauti ya riba za amana na za mikopo (mwaka) | 2.44% | 3.86% | 3.45% | 2.19% | 6.64% | 9.47% | 7.89% | 7.45% |
| Kiwango cha ubadilishanaji fedha kwa Dola (wastani wa mwaka) | 1,605.4 | 1,661.2 | 2,007.0 | 2,188.0 | 2,240.8 | 2,275.4 | 2,299.8 | 2,305.6 |
| UJAZI WA FEDHA | | | | | | | | |
| Kiwango cha ukuaji wa M3 | 10.0% | 15.6% | 18.8% | 3.4% | 8.0% | 4.5% | 9.6% | 5.7% |
| Kiwango cha ukuaji wa M2 | 10.9% | 17.0% | 13.4% | 5.3% | 10.4% | 3.8% | 11.8% | 8.2% |
| Mikopo Chechefu | 6.6% | 6.8% | 6.6% | 10.3% | 11.5% | 10.7% | 9.8% | 9.3% |
| Kiwango cha ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi | 15.3% | 19.4% | 24.8% | 7.2% | 1.7% | 4.9% | 11.1% | 3.1% |
| UWIANO WA MIZANIA YA MALIPO YA NJE NA PATO LA TAIFA | | | | | | | | |
| Bidhaa zilizouzwa nje | 11.9% | 12.4% | 11.1% | 10.0% | 8.6% | 7.9% | 8.8% | 10.0% |
| Bidhaa na huduma zilizouzwa nje | 19.2% | 20.6% | 19.0% | 17.4% | 15.9% | 15.0% | 15.8% | 14.0% |
| Bidhaa zilizonunuliwa kutoka nje | 25.0% | 26.2% | 22.7% | 17.4% | 14.4% | 14.7% | 14.1% | 12.0% |
| Bidhaa na huduma zilizonunuliwa kutoka nje | 30.6% | 32.6% | 28.8% | 21.9% | 18.3% | 18.1% | 17.0% | 14.0% |
| Urari wa malipo ya kawaida | -11.3% | -12.2% | -10.3% | -5.6% | -3.5% | -3.4% | -2.1% | -0.8% |
| Akiba ya fedha za kigeni (miezi) | 4.5 | 4.7 | 5.1 | 5.0 | 6.6 | 4.9 | 6.4 | 5.6 |
| UWIANO WA BAJETI YA SERIKALI NA PATO LA TAIFA | | | | | | | | |
| Mwaka wa fedha | 2012/13 | 2013/14 | 2014/15 | 2015/16 | 2016/17 | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 |
| Mapato ya ndani | 12.5% | 13.1% | 12.4% | 13.9% | 14.7% | 14.6% | 13.9% | 14.7% |
| Mapato ya kodi | 11.4% | 11.9% | 11.2% | 12.2% | 12.4% | 12.3% | 11.6% | 12.2% |
| Matumizi (Bila rollover) | 18.8% | 17.9% | 16.5% | 17.5% | 16.6% | 16.7% | 16.8% | 16.4% |
| Matumizi ya kawaida | 13.4% | 12.9% | 12.3% | 13.2% | 10.2% | 10.5% | 10.4% | 9.9% |
| Matumizi ya maendeleo | 5.4% | 5.0% | 4.2% | 4.3% | 6.4% | 6.2% | 6.4% | 6.5% |
| Misaada | 2.3% | 2.0% | 1.3% | 0.4% | 0.9% | 0.8% | 0.7% | 0.6% |
| Nakisi (kabla ya misaada) | -6.5% | -4.2% | -4.9% | -3.0% | -1.3% | -2.5% | -3.2% | -2.6% |
| Nakisi (baada ya misaada) | -4.2% | -2.3% | -3.6% | -2.6% | -0.3% | -1.7% | -2.5% | -2.0% |
| Mikopo ya nje | 2.6% | 2.0% | 2.7% | 0.4% | 0.4% | 1.2% | 0.2% | 1.7% |
| Mikopo ya ndani (kutoka benki) | 1.0% | 1.2% | 0.6% | 1.5% | -0.9% | -0.3% | 1.8% | -0.3% |

**Chanzo:** Wizara ya Fedha na Mipango

# SEHEMU YA KWANZA
# MAENDELEO YA UCHUMI JUMLA




## SURA YA I

## HALI YA UCHUMI WA TAIFA

### Ukuaji wa Uchumi

1. Mwaka 2020, Pato la Taifa lilikua kwa asilimia 4.8 ikilinganishwa na asilimia 7.0 mwaka 2019. Kupungua kwa kasi ya ukuaji kulitokana na: mvua zilizozidi wastani ambazo zilisababisha uharibifu wa miundombinu ya usafirishaji nchini na kuchelewesha utekelezaji wa baadhi ya miradi; na athari za hatua zilizochukuliwa na mataifa mbalimbali duniani ambao ni washirika wakubwa wa biashara wa Tanzania katika kukabiliana na janga la UVIKO-19. Miongoni mwa hatua zilizochukuliwa na mataifa hayo ni pamoja na kufunga mipaka, kusitisha safari za ndege za kimataifa na kusitisha baadhi ya shughuli za kiuchumi zinazohusisha mikusanyiko. Hatua hizo zilisababisha uchumi wa dunia kuporomoka mwaka 2020 ambapo nchi nyingi zilikuwa na ukuaji hasi na kwa nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, ni nchi 11 tu zilikuwa na ukuaji chanya kati ya nchi 45. Pamoja na kupungua kwa kasi ya ukuaji, Tanzania iliweza kuwa na ukuaji chanya kutokana na kutochukua hatua za kuzuia kufanyika kwa shughuli za kiuchumi isipokuwa kwa kipindi kifupi tu cha robo ya pili ya mwaka 2020 ambapo ilisitisha kwa muda baadhi ya shughuli zinazohusisha mikusanyiko ya watu kama shule, sanaa na burudani. Athari za janga la UVIKO-19 zilijitokeza zaidi katika shughuli za kiuchumi za malazi na huduma ya chakula pamoja na sanaa na burudani ambazo zilikuwa na ukuaji hasi mwaka 2020. Mwenendo wa ukuaji kwa baadhi ya sekta ni kama unavyoonekana katika **Kielelezo Na. 1.1**

**Kielelezo Na.1.1: Mwenendo wa Ukuaji kwa Baadhi ya Sekta**



2. Pato ghafi la Taifa lililozalishwa nchini lilikuwa shilingi milioni 148,522,111 mwaka 2020 ikilinganishwa na shilingi milioni 139,641,854 mwaka 2019. Aidha, Tanzania Bara ilikadiriwa kuwa na watu 55,966,030 mwaka 2020 ambapo Wastani wa Pato kwa Mtu (GDP per capita) lilifikia shilingi 2,653,790 kutoka shilingi 2,573,324 mwaka 2019, sawa na ongezeko la wastani wa asilimia 3.1. Kiasi hicho cha Wastani wa Pato kwa Mtu kwa mwaka 2020 ni sawa na dola za Marekani 1,151.0 ikilinganishwa na dola za Marekani 1,118.9 mwaka 2019.

3. Shughuli za kiuchumi za kilimo ambazo zinajumuisha kilimo cha mazao, mifugo, misitu na uvuvi zilikua kwa asilimia 4.9 mwaka 2020, ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 4.4 mwaka 2019. Ukuaji huo ulitokana na uwepo wa mvua za kutosha katika maeneo ya uzalishaji wa mazao na upatikanaji wa maji na malisho ya kutosha kwa ajili ya mifugo. Mchango wa shughuli za kilimo katika Pato la Taifa uliongezeka na kufikia asilimia 26.9 mwaka 2020 ikilinganishwa na asilimia 26.6 mwaka 2019.

4. Kiwango cha ukuaji wa shughuli ndogo za uzalishaji mazao na uvuvi kiliongezeka kufikia asilimia 5.0 na asilimia 6.7 mwaka 2020 kutoka ukuaji wa asilimia 4.4 na asilimia 1.5 mtawalia mwaka 2019. Aidha, shughuli za mazao zilichangia asilimia 15.4 katika Pato la Taifa mwaka 2020 na uvuvi ilichangia asilimia 1.7. Kiwango cha ukuaji wa shughuli za kiuchumi za mifugo kilikuwa asilimia 5.0 mwaka 2020 kama ilivyokuwa mwaka 2019 na sekta ndogo hii ilichangia asilimia 7.1 katika Pato la Taifa mwaka 2020. Kiwango cha ukuaji wa shughuli za misitu kilipungua kufikia asilimia 3.2 mwaka 2020 kutoka asilimia 4.8 mwaka 2019. Mchango wa shughuli za misitu katika Pato la Taifa uliendelea kubaki asilimia 2.7 mwaka 2020 kama ilivyokuwa mwaka 2019.

5. Mwaka 2020, shughuli za kilimo sehemu inayouzika zilikua kwa asilimia 5.0 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 4.5 mwaka 2019 na sehemu isiyouzika zilikua kwa asilimia 4.2 mwaka 2020 ikilinganishwa na asilimia 3.9 mwaka 2019. Kiwango cha ukuaji wa shughuli ndogo za kiuchumi za mazao, uvuvi, mifugo na misitu kwa sehemu inayouzika kilikuwa asilimia 5.1, asilimia 6.7, asilimia 5.2 na asilimia 3.2 mwaka 2020 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 4.6, asilimia 1.5, asilimia 5.0 na asilimia 4.8 mwaka 2019 mtawalia. Kwa upande mwingine, kiwango cha ukuaji wa shughuli ndogo za kiuchumi za mazao, uvuvi, mifugo na misitu kwa sehemu isiyouzika kilikuwa asilimia 4.6, asilimia 3.7, asilimia 3.7 na asilimia 3.4 mwaka 2020 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 3.4, asilimia 1.4, asilimia 4.6 na asilimia 4.6 mwaka 2019 mtawalia.

6. Mwaka 2020, shughuli za kiuchumi za uchimbaji madini na mawe zilikuwa na kiwango cha ukuaji wa asilimia 6.7 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 17.7 mwaka 2019. Ukuaji huo ulitokana na kuimarika kwa usimamizi na udhibiti wa biashara ya madini nchini. Pamoja na kasi ndogo ya ukuaji, mchango wa shughuli za uchimbaji

madini na mawe katika Pato la Taifa uliongezeka kufikia asilimia 6.7 mwaka 2020 kutoka asilimia 5.2 mwaka 2019.

7. Mwaka 2020, shughuli za uzalishaji bidhaa viwandani zilikua kwa asilimia 4.5 ikilinganishwa na asilimia 5.8 mwaka 2019. Kupungua kwa kasi ya ukuaji kulitokana na uhaba wa malighafi za uzalishaji viwandani zinazoagizwa kutoka nje ya nchi kufuatia athari za janga la UVIKO-19. Mchango wa shughuli za uzalishaji bidhaa viwandani katika Pato la Taifa ulipungua kidogo kufikia asilimia 8.4 mwaka 2020 kutoka asilimia 8.5 mwaka 2019.

8. Mwaka 2020, shughuli za uzalishaji na usambazaji umeme zilikua kwa asilimia 5.5 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 7.2 mwaka 2019. Kasi ndogo ya ukuaji ilitokana na kupungua kwa mahitaji ya umeme kufuatia kusitishwa kwa baadhi ya shughuli za kiuchumi. Hata hivyo, mchango wa shughuli hizi katika Pato la Taifa umeendelea kuwa asilimia 0.3 kwa mwaka wa nne (4) mfululizo.

9. Mwaka 2020, shughuli za usambazaji maji na udhibiti majitaka zilikua kwa asilimia 5.8 ikilinganishwa na asilimia 6.9 mwaka 2019. Hii ilitokana na hatua zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali za kuimarisha miundombinu ya majisafi na majitaka na kuongezeka kwa uwezo wa miundombinu ya kuzalisha na kusambaza maji. Katika kipindi hicho, mchango wa shughuli za usambazaji maji katika Pato la Taifa uliongezeka na kufikia asilimia 0.5 kutoka asilimia 0.4 mwaka 2019. Aidha, shughuli za usambazaji maji na udhibiti wa majitaka sehemu inayouzika na isiyouzika zilikua kwa asilimia 6.2 na asilimia 4.4 mwaka 2020 ikilinganishwa na asilimia 7.2 na asilimia 5.8 mwaka 2019, mtawalia.

10. Mwaka 2020, shughuli za kiuchumi za ujenzi zilikua kwa asilimia 9.1 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 13.7 mwaka 2019. Ukuaji huo ulitokana na kuendelea kwa ujenzi wa miundombinu mbalimbali ikiwemo barabara, madaraja, viwanja vya ndege na reli. Aidha, baadhi ya miradi ya ujenzi iliyokuwa inatekelezwa kwa kutumia wakandarasi na vifaa kutoka nje ilisimama kwa muda kutokana na janga la UVIKO-19 hivyo kuathiri kasi ya ukuaji wa sekta ya ujenzi. Shughuli za ujenzi sehemu inayouzika na isiyouzika zilikua kwa asilimia 9.1 na asilimia 8.8 mwaka 2020 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 13.9 na asilimia 11.3 mwaka 2019, mtawalia. Pamoja na kupungua kwa kasi ya ukuaji, mchango wa shughuli za kiuchumi za ujenzi katika Pato la Taifa uliongezeka kufikia asilimia 14.4 mwaka 2020 kutoka asilimia 14.2 mwaka 2019.

11. Mwaka 2020, shughuli za biashara na matengenezo zilikua kwa asilimia 2.1 ikilinganishwa na asilimia 5.5 mwaka 2019. Hii ilitokana na athari za UVIKO-19 katika uchumi ambazo zilipelekea wateja kubadili mwenendo wa matumizi kwa kupendelea

zaidi bidhaa muhimu na zenye gharama ndogo. Aidha, mchango wa shughuli za biashara na matengenezo katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 8.7 ikilinganishwa na asilimia 8.8 mwaka 2019.

12. Mwaka 2020, shughuli za uchukuzi na uhifadhi mizigo zilikua kwa asilimia 8.4 ikilinganishwa na asilimia 8.7 mwaka 2019. Mwenendo huo ulitokana na kupungua kwa idadi ya abiria na mizigo iliyosafirishwa kwa njia ya anga, reli na barabara kufuatia zuio la safari za anga katika nchi mbalimbali duniani kulikosababishwa na athari za janga la UVIKO-19. Aidha, mchango wa huduma za uchukuzi na uhifadhi mizigo katika Pato la Taifa uliongezeka kutoka asilimia 6.9 mwaka 2019 na kufikia asilimia 7.5 mwaka 2020.

13. Shughuli za kiuchumi za malazi na huduma ya chakula ziliathiriwa kwa kiwango kikubwa na UVIKO-19, hali iliyopelekea kuporomoka hadi kufikia kiwango hasi cha ukuaji cha asilimia 13.7 mwaka 2020 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 2.6 mwaka 2019. Ukuaji huo ulitokana na kupungua kwa idadi ya watumiaji wa huduma hizo kutoka nje ya nchi hususan watalii kufuatia nchi nyingi duniani kuweka zuio la kusafiri ili kukabiliana na maambukizi ya UVIKO-19. Aidha, mchango wa sekta hii katika Pato la Taifa ulipungua kutoka asilimia 1.3 mwaka 2019 hadi kufikia asilimia 1.0 mwaka 2020.

14. Mwaka 2020, shughuli za kiuchumi za huduma za habari na mawasiliano zilikua kwa asilimia 8.4 ikilinganishwa na asilimia 7.2 mwaka 2019. Ukuaji huu ulitokana na kuongezeka kwa matumizi ya huduma za simu za viganjani na mitandao ya kijamii nchini katika kuwasiliana na kupata habari na matukio mbalimbali pamoja na kuongezeka kwa matumizi ya njia za mitandao katika kufanya mikutano, hususan katika kipindi cha mlipuko wa UVIKO-19. Aidha, mchango wa shughuli za huduma za habari na mawasiliano katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 1.5 kama ilivyokuwa mwaka 2019.

15. Shughuli za utoaji huduma za fedha na bima zilikua kwa asilimia 3.1 mwaka 2020, ikilinganishwa na asilimia 4.5 mwaka 2019. Ongezeko hilo lilitokana na juhudi za Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania kuchukua hatua mbalimbali za kukabiliana na changamoto zilizokuwa zinaikabili sekta hii ikiwemo ongezeko la mikopo chechefu. Aidha, kasi ndogo ya ukuaji ilitokana na kupungua kwa kasi ya ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi na kupungua kwa amana kutokana na athari za UVIKO-19 kwenye uchumi. Mchango wa shughuli za utoaji huduma za fedha na bima katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 3.5 mwaka 2020 kama ilivyokuwa mwaka 2019.

16. Shughuli za kiuchumi za huduma za upangishaji nyumba zilikua kwa asilimia 4.5 mwaka 2020 sawa na ukuaji wa mwaka 2019. Ukuaji huo ulitokana na kuendelea kuongezeka kwa mahitaji ya nyumba kwa ajili ya makazi, biashara na ofisi, hususan

katika maeneo ya mijini. Shughuli za upangishaji nyumba katika sehemu inayouzika na sehemu isiyouzika zilikua kwa asilimia 4.5 na asilimia 4.6 mwaka 2020 mtawalia. Aidha, shughuli za kiuchumi za huduma za upangishaji nyumba zilichangia asilimia 2.9 katika Pato la Taifa mwaka 2020 ikilinganishwa na asilimia 2.7 mwaka 2019.

17. Mwaka 2020, shughuli za kitaaluma, sayansi na ufundi zilikuwa na ukuaji wa asilimia 7.3 ikilinganishwa na asilimia 7.6 mwaka 2019. Hii ilitokana na ongezeko la mahitaji ya shughuli za kitaaluma, kisheria na kiuhasibu. Katika kipindi hicho, shughuli hizo zilichangia asilimia 0.7 katika Pato la Taifa ikilinganishwa na asilimia 0.6 mwaka 2019. Kwa upande mwingine, shughuli za huduma zinazohusiana na utawala zikiwemo ukodishaji wa vifaa, mashine na mitambo, utafutaji wa ajira, huduma za utalii, ulinzi wa mali na watu, utoaji huduma ofisini, na haki ya kutumia matokeo ya kitaaluma zilikua kwa asilimia 7.8 ikilinganishwa na asilimia 8.4 mwaka 2019. Mchango wa shughuli hizo katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 2.7 mwaka 2020 ikilinganishwa na asilimia 2.6 mwaka 2019.

18. Shughuli za utawala na ulinzi zinajumuisha shughuli zinazofanywa na Serikali kwa maana ya sekta ya umma, shughuli za mahakama, uhamiaji, mambo ya nje, ulinzi na usalama pamoja na usimamizi wa programu za Serikali. Shughuli za kiuchumi za utawala na ulinzi zilikua kwa asilimia 3.8 mwaka 2020 ikilinganishwa na asilimia 3.4 mwaka 2019. Shughuli hizo zilichangia asilimia 3.7 katika Pato la Taifa ikilinganishwa na asilimia 3.8 mwaka 2019.


19. Mwaka 2020, shughuli za utoaji huduma za elimu zilikua kwa asilimia 3.3 ikilinganishwa na asilimia 6.9 mwaka 2019. Kupungua kwa kasi ya ukuaji kulitokana na athari za janga la UVIKO-19 ambapo Serikali ilifunga shule za msingi, sekondari na vyuo vikuu kwa muda ili kupunguza kasi ya maambukizi. Aidha, shughuli za huduma za elimu zilichangia asilimia 2.3 katika Pato la Taifa ikilinganishwa na asilimia 2.4 mwaka 2019. Kwa upande mwingine, shughuli za afya na huduma za ustawi wa jamii zilikua kwa asilimia 6.5 ikilinganishwa na asilimia 5.0 mwaka 2019. Ukuaji huo ulitokana na jitihada za wadau mbalimbali za kugharamia mahitaji ya sekta ya afya katika kukabiliana na magonjwa ya mlipuko, magonjwa ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza. Mchango wa shughuli za afya na utoaji huduma kwa jamii katika Pato la Taifa umeendelea kubaki asilimia 1.4 kwa mwaka wa tano (5) mfululizo.

20. Mwaka 2020, shughuli za kiuchumi za sanaa na burudani zilikuwa na ukuaji hasi wa asilimia 4.4 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 11.2 mwaka 2019. Hii ilitokana na kupungua kwa mauzo ya bidhaa za kitamaduni kwa watalii kulikosababishwa na kupungua kwa watalii waliotembelea vivutio mbalimbali katika kipindi husika. Aidha, zuio la mikusanyiko nchini katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2020 kufuatia mlipuko wa UVIKO-19 liliathiri kwa kiasi kikubwa tasnia ya sanaa na burudani.

Mchango wa shughuli za sanaa na burudani katika Pato la Taifa umeendelea kuwa asilimia 0.3.

21. Mwaka 2020, kiwango cha ukuaji wa shughuli za kaya binafsi katika kuajiri kilikuwa asilimia 3.1 kama ilivyokuwa mwaka 2019. Aidha, mchango wa shughuli hizo katika Pato la Taifa uliendelea kuwa asilimia 0.2. Kwa upande wa shughuli za huduma nyingine za kijamii, kiwango cha ukuaji kilikuwa asilimia 5.0 mwaka 2020 ikilinganishwa na asilimia 6.7 mwaka 2019. Mchango wa shughuli hizi katika Pato la Taifa umeendelea kuwa asilimia 0.8.

**Kielelezo Na. 1.2: Mchango wa Sekta katika Pato la Taifa**




**Mwenendo wa Bei**

22. Mwaka 2020, mfumuko wa bei uliendelea kushuka na kufikia asilimia 3.3 kutoka asilimia 3.4 mwaka 2019. Kushuka kwa kiwango cha mfumuko wa bei kulitokana na sababu mbalimbali zikiwemo: Utekelezaji madhubuti wa sera za fedha na bajeti; kutengamaa kwa bei ya mafuta ya petroli katika soko la dunia; na kuimarika kwa thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya sarafu nyingine duniani.

23. Mwaka 2020, uchambuzi wa mwenendo wa bei kwa makundi makuu ya bidhaa na huduma ulionesha kuwa idadi kubwa ya makundi hayo ilikuwa na ongezeko dogo la bei ikilinganishwa na mwaka 2019. Katika kipindi hicho, mfumuko wa bei uliongezeka katika makundi mawili ambayo ni vyakula na vinywaji baridi pamoja na mawasiliano. Mfumuko wa bei wa vyakula na vinywaji baridi uliongezeka kufikia asilimia 4.1 mwaka 2020 kutoka asilimia 2.9 mwaka 2019. Aidha, baada ya miaka minne mfululizo ya kupungua kwa kasi ya upandaji bei, kundi la mawasiliano lilianza kuwa na ongezeko

la kasi ya kupanda kwa wastani wa bei kufikia asilimia 0.4 mwaka 2020. Kundi la vinywaji vyenye kilevi na bidhaa za tumbaku ndio pekee ambalo kasi ya upandaji bei ilipungua mwaka 2020. Kasi ya upandaji bei kwa makundi yaliyobaki ilipungua mwaka 2020 ikilinganishwa na ilivyokuwa mwaka 2019. Pamoja na kupungua kwa kasi ya ongezeko la bei katika kundi la nishati, maji na malazi kutoka asilimia 7.9 mwaka 2019 hadi asilimia 7.6 mwaka 2020, kundi hilo ndilo lililokuwa na kiwango kikubwa cha mfumuko wa bei ikilinganishwa na makundi mengine. Kupungua kwa mfumuko wa bei katika kundi hilo kulitokana na kushuka kwa bei za mafuta katika soko la dunia pamoja na jitihada za Serikali za kuimarisha huduma za maji mijini na vijijini. Mwenendo wa bei kwa makundi makuu ya bidhaa na huduma ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 1.1.**

**Jedwali Na. 1.1: Fahirisi na Mfululizo wa Bei ya Bidhaa na Huduma Zitumiwazo na Wakazi wa Mijini – Tanzania Bara (2001-100)**

| Mwaka | | Vyakula na vinywaji baridi | Vinywaji vyenye kilevi na bidhaa za tumbaku | Mavazi ya nguo na viatu | Nishati, Maji na Makazi | Samani, vifaa vya nyumbani na ukarabati wa nyumba | Gharama za Afya | Usafirishaji | Mawasiliano | Utamaduni na Burudani | Elimu | Hoteli na Migahawa | Bidhaa na huduma nyinginezo | FAHIRISI BIDHAA ZOTE |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2015 | Fahirisi za bei | 96.8 | 99.2 | 98.4 | 100.9 | 98.2 | 97.9 | 98.8 | 99.8 | 98.4 | 99.6 | 99.1 | 98.4 | 97.9 |
| 2016 | | 103.8 | 103.2 | 102.2 | 107.3 | 101.7 | 103.4 | 99.5 | 99.1 | 101.1 | 102.3 | 103.1 | 101.7 | 102.9 |
| 2017 | | 113.3 | 106.6 | 105.8 | 115.4 | 104.7 | 106.0 | 99.9 | 98.2 | 102.3 | 103.2 | 104.4 | 105.0 | 108.4 |
| 2018 | | 116.6 | 108.4 | 108.9 | 129.2 | 107.4 | 107.4 | 102.5 | 96.6 | 102.8 | 105.8 | 105.7 | 106.7 | 112.2 |
| 2019 | | 120.0 | 111.0 | 112.1 | 139.4 | 111.5 | 109.3 | 105.7 | 96.5 | 104.3 | 107.6 | 110.2 | 109.3 | 116.1 |
| 2020 | | 124.9 | 110.8 | 114.5 | 150.0 | 113.5 | 110.2 | 107.2 | 96.8 | 104.7 | 109.0 | 111.9 | 110.3 | 119.9 |
| 2015 | Mwenendo wa bei | 8.7% | 3.6% | 4.1% | 1.6% | 1.6% | 3.0% | -0.6% | 0.3% | 1.6% | 2.9% | 4.6% | 2.9% | 5.6% |
| 2016 | | 7.2% | 4.0% | 3.9% | 6.3% | 3.6% | 5.6% | 0.6% | -0.7% | 2.7% | 2.7% | 4.1% | 3.4% | 5.2% |
| 2017 | | 9.1% | 3.3% | 3.5% | 7.6% | 2.9% | 2.6% | 0.5% | -0.9% | 1.3% | 0.9% | 1.2% | 3.2% | 5.3% |
| 2018 | | 3.0% | 1.6% | 2.9% | 12.0% | 2.5% | 1.3% | 2.5% | -1.6% | 0.5% | 2.4% | 1.3% | 1.6% | 3.5% |
| 2019 | | 2.9% | 2.4% | 3.0% | 7.9% | 3.9% | 1.8% | 3.1% | -0.2% | 1.5% | 1.8% | 4.2% | 2.4% | 3.4% |
| 2020 | | 4.1% | -0.1% | 2.2% | 7.6% | 1.8% | 0.8% | 1.4% | 0.4% | 0.4% | 1.3% | 1.5% | 0.9% | 3.3% |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

24. Uchambuzi wa mwenendo wa bei kwa makundi mengine maalumu unaonesha kuwa wastani wa ongezeko la bei ya chakula kinachojumuisha vyakula vinavyoliwa majumbani na hotelini ulikuwa asilimia 5.0 mwaka 2020 ikilinganishwa na asilimia 4.3 mwaka 2019. Hii ilitokana na athari za mvua zilizozidi wastani na kusababisha uharibifu wa miundombinu ya usafirishaji na hivyo kusababisha bei ya chakula kupanda. Kwa upande mwingine, wastani wa ongezeko la bei ya bidhaa zisizokuwa za chakula ulikuwa asilimia 2.8 mwaka 2020 ikilinganishwa na asilimia 4.0 mwaka 2019. Aidha, wastani wa ongezeko la bei ya nishati ulipungua na kufikia asilimia 5.0 mwaka 2020 kutoka asilimia 9.0 mwaka 2019. Hali hii ilitokana na kuimarika kwa bei za petroli, dizeli na mafuta ya taa katika soko la ndani kufuatia kushuka kwa bei za mafuta katika soko la dunia pamoja na gharama za usafirishaji. Vilevile, mfumuko wa bei

usiojumuisha chakula na nishati ulipungua kufikia asilimia 2.3 mwaka 2020 kutoka asilimia 3.0 mwaka 2019 kutokana na utekelezaji madhubuti wa sera za fedha na bajeti. Kundi hili lilichangia asilimia 54.3 katika kapu la walaji na ndilo linaloweza kudhibitiwa kwa kutumia nyenzo za sera za fedha.

25. Fahirisi ya bei za bidhaa na huduma kwa makundi ya watu wa tabaka la kipato cha juu, kati na chini ilipungua mwaka 2020 na kufikia asilimia 2.4, asilimia 3.5 na asilimia 2.1 kutoka asilimia 3.6, asilimia 4.5 na asilimia 3.8 mwaka 2019, mtawalia. Hii ilitokana na kupungua kwa wastani wa bei za bidhaa na huduma zinazotumika kwa wingi na makundi hayo zikiwemo mavazi ya nguo na viatu; gharama za afya; na usafirishaji. Kwa ujumla, mwenendo wa fahirisi ya bei ya bidhaa na huduma uliendana na mahitaji ya kundi husika kimapato kama inavyoonekana katika. **Jedwali Na. 1.2.**

**Jedwali Na. 1.2: Mfumuko wa Bei za Bidhaa na Huduma Zitumiwazo na Walaji Kulingana na Tabaka la Kipato**

| Mwaka | Tabaka la Kipato | Vyakula na vinywaji baridi | Vinywaji vyenye kilevi na bidhaa za tumbaku | Mavazi ya nguo na viatu | Nishati, Maji na Makazi | Samani, vifaa vya nyumbani na ukarabati wa nyumba | Gharama za Afya | Usafirishaji | Mawasiliano | Utamaduni na Burudani | Elimu | Hoteli na Migahawa | Bidhaa na huduma nyinginezo | FAHIRISI BIDHAA ZOTE |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2015 | Kipato cha juu | 8.8% | 6.5% | 0.9% | 7.1% | 0.7% | 1.2% | 3.6% | 2.9% | 0.8% | 2.1% | 8.4% | -0.7% | 6.5% |
| 2016 | | 8.6% | 3.3% | 1.8% | 8.8% | 3.3% | 14.1% | -2.3% | 2.4% | 1.1% | -1.6% | 5.1% | 3.5% | 4.8% |
| 2017 | | 9.2% | 2.1% | 1.8% | 1.3% | 5.4% | 2.5% | 4.9% | 0.6% | -1.2% | -0.1% | 0.8% | 3.2% | 4.2% |
| 2018 | | 7.0% | 0.2% | 2.5% | 5.6% | 1.1% | 0.1% | 6.4% | 0.4% | 0.8% | 7.8% | 1.0% | 0.6% | 4.7% |
| 2019 | | 4.4% | 0.0% | 2.4% | 8.1% | 2.0% | 4.1% | 2.8% | 1.5% | 0.7% | 1.5% | 3.7% | 0.4% | 3.6% |
| 2020 | | 7.6% | 0.2% | 1.4% | 6.7% | 0.5% | 0.6% | -1.8% | 0.6% | -0.1% | 0.0% | 0.6% | -0.2% | 2.4% |
| 2015 | Kipato cha kati | 2.9% | 7.4% | 2.1% | 14.6% | 4.5% | 3.1% | 4.4% | 0.5% | 3.9% | 5.5% | 11.4% | 5.0% | 5.6% |
| 2016 | | 3.3% | 2.5% | 1.1% | 12.4% | 1.4% | 13.4% | 0.3% | 0.6% | 2.9% | -2.3% | 8.3% | 5.4% | 4.5% |
| 2017 | | 4.6% | 2.3% | 1.4% | 2.2% | 3.3% | 2.4% | 0.7% | 0.5% | 0.5% | -0.1% | 1.2% | 1.1% | 2.6% |
| 2018 | | 7.0% | -0.5% | 2.1% | 4.1% | 1.3% | 0.3% | -18.8% | -0.1% | 0.1% | 8.6% | -0.5% | 1.5% | 1.9% |
| 2019 | | 5.6% | 0.4% | 3.5% | 6.6% | 2.2% | 4.5% | 5.6% | 1.4% | 2.0% | 0.0% | 2.7% | 2.6% | 4.5% |
| 2020 | | 4.5% | 0.1% | 1.3% | 9.7% | 0.5% | 0.7% | -0.8% | 0.6% | -0.2% | 0.0% | 0.7% | 0.2% | 3.5% |
| 2015 | Kipato cha chini | 5.9% | 14.2% | 9.0% | 3.4% | 6.0% | 5.6% | -0.2% | 0.0% | 5.6% | -0.3% | 7.1% | 2.7% | 5.4% |
| 2016 | | 3.6% | 8.2% | -2.4% | 7.1% | 2.7% | 12.1% | 0.9% | 0.6% | 1.2% | -5.2% | 6.8% | 6.0% | 4.3% |
| 2017 | | 3.4% | 2.9% | 1.3% | 0.9% | 3.1% | 1.6% | -0.1% | 0.4% | 1.7% | 3.9% | 0.5% | 0.9% | 1.9% |
| 2018 | | 4.5% | 0.0% | 3.1% | 5.7% | 1.9% | 0.1% | -12.5% | -0.1% | 1.1% | 5.5% | 0.1% | 1.6% | 2.0% |
| 2019 | | 4.6% | 0.8% | 4.0% | 5.6% | 1.9% | 3.1% | 4.9% | 1.0% | 2.3% | -0.1% | 2.2% | 2.5% | 3.8% |
| 2020 | | 1.1% | 0.0% | 1.2% | 9.4% | 0.6% | 0.9% | -0.2% | 0.2% | -0.1% | -0.1% | 0.6% | 0.3% | 2.1% |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Ukuzaji Rasilimali**

26. Mwaka 2020, ukuzaji rasilimali kwa bei za miaka husika ulifikia shilingi bilioni 59,235.4 kutoka shilingi bilioni 55,762.4 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 6.2. Aidha, ukuzaji rasilimali kwa bei za mwaka 2015 uliongezeka kwa asilimia 4.8 na kufikia shilingi bilioni 51,708.0 kutoka shilingi bilioni 49,349.3 mwaka 2019. Uwiano wa ukuzaji rasilimali kwa Pato la Taifa kwa bei za miaka husika ulifikia asilimia 39.9 sawa na ilivyokuwa mwaka 2019.

27. Ukuzaji rasilimali za kudumu kwa bei za mwaka 2015 unaojumuisha majengo; vifaa vya usafiri; mitambo na vifaa vingine; rasilimali za mazao na mifugo; na haki za umiliki, utafiti na maendeleo na huduma za kitaalamu ulifikia shilingi bilioni 57,519.8 mwaka 2020 kutoka shilingi bilioni 53,777.6 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 7.0. Aidha, ukuzaji rasilimali za kudumu kwa bei za miaka husika uliongezeka kwa asilimia 7.8 kutoka shilingi bilioni 59,440.5 mwaka 2019 hadi shilingi bilioni 64,049.9 mwaka 2020. Kwa upande mwingine, thamani ya limbikizo la rasilimali kwa bei za mwaka 2015 ilipungua kwa shilingi bilioni 5,811.7 mwaka 2020 ikilinganishwa na upungufu wa thamani wa shilingi bilioni 4,428.3 mwaka 2019. Vile vile, thamani ya limbikizo la rasilimali kwa bei za miaka husika ilipungua kwa shilingi bilioni 4,814.5 mwaka 2020 ikilinganishwa na upungufu wa thamani wa shilingi bilioni 3,678.2 mwaka 2019.

28. Ukuzaji rasilimali katika shughuli za ujenzi wa majengo kwa bei za mwaka 2015 uliongezeka kwa asilimia 5.1 kutoka shilingi bilioni 45,205.6 mwaka 2019 hadi shilingi bilioni 47,526.3 mwaka 2020. Aidha, ukuzaji rasilimali katika shughuli za ujenzi wa majengo kwa bei za miaka husika uliongezeka kwa asilimia 5.6 na kufikia shilingi bilioni 53,000.5 mwaka 2020 kutoka shilingi bilioni 50,182.0 mwaka 2019. Hii ilitokana na kuendelea kuongezeka kwa ujenzi wa nyumba za makazi na biashara katika maeneo mbalimbali nchini. Katika kipindi cha mwaka 2020, thamani ya uagizaji wa vifaa vya usafiri; mitambo na vifaa; aina nyingine za mitambo na vifaa; rasilimali za mazao ya mifugo; na haki ya umiliki, utafiti na maendeleo na huduma za kitaalamu kwa bei za mwaka 2015 iliongezeka kwa asilimia 2.9, asilimia 25.6, asilimia 20.2, asilimia 13.2 na asilimia 14.7 na kwa bei za miaka husika thamani iliongezeka kwa asilimia 16.0, asilimia 23.2, asilimia 20.2, asilimia 14.6 na asilimia 15.3 mtawalia.

29. Ukuzaji rasilimali katika sekta ya umma inayojumuisha Serikali Kuu, mashirika na taasisi za Serikali kwa bei za miaka husika uliongezeka kwa asilimia 12.1 na kufikia shilingi bilioni 19,791.4 mwaka 2020 kutoka shilingi bilioni 17,653.8 mwaka 2019. Aidha, ukuzaji rasilimali katika sekta binafsi kwa bei za miaka husika ulifikia shilingi bilioni 44,258.5 mwaka 2020 ikilinganishwa na shilingi bilioni 41,786.7 mwaka 2019,

sawa na ongezeko la asilimia 5.9. Sekta ya umma ilichangia asilimia 30.9 katika rasilimali za kudumu na sekta binafsi ilichangia asilimia 69.1 mwaka 2020.

I

**PATO LA TAIFA (GDP) KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI KWA BEI ZA SOKO**
**(Bei za Miaka Inayohusika)**

**Jedwali Na.1** **Sh. Milioni**

| | SHUGHULI YA KIUCHUMI | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| A | **Kilimo, Misitu na Uvuvi** | **25,234,560** | **29,739,111** | **34,154,594** | **35,962,728** | **37,192,537** | **39,965,062** |
| | Kilimo cha Mazao | 13,279,392 | 16,474,729 | 19,703,004 | 21,003,720 | 20,686,963 | 22,867,959 |
| | Mifugo | 7,158,457 | 8,205,007 | 8,857,939 | 9,240,100 | 10,345,069 | 10,609,888 |
| | Misitu | 2,920,425 | 3,094,767 | 3,310,076 | 3,459,581 | 3,738,360 | 3,947,993 |
| | Uvuvi | 1,843,401 | 1,929,747 | 2,245,558 | 2,218,731 | 2,379,172 | 2,494,162 |
| | Huduma za katika shughuli za Kilimo | 32,886 | 34,861 | 38,017 | 40,596 | 42,973 | 45,060 |
| | **Viwanda na Ujenzi** | **23,103,647** | **26,937,139** | **29,735,584** | **34,851,874** | **39,944,212** | **44,932,190** |
| B | Uchimbaji Madini na Mawe | 4,055,619 | 5,299,362 | 5,206,217 | 6,573,059 | 7,213,403 | 9,921,721 |
| C | Viwanda | 7,411,672 | 8,467,126 | 9,102,282 | 10,418,776 | 11,860,403 | 12,539,107 |
| D | Umeme | 798,801 | 472,868 | 413,351 | 348,527 | 369,917 | 398,086 |
| E | Maji safi na Maji taka | 390,758 | 433,132 | 519,909 | 566,562 | 628,187 | 745,222 |
| F | Ujenzi | 10,446,797 | 12,264,650 | 14,493,826 | 16,944,950 | 19,872,302 | 21,328,055 |
| | **Huduma** | **38,146,529** | **42,747,407** | **45,066,596** | **48,059,561** | **51,417,505** | **55,201,494** |
| G | Biashara na Matengenezo | 8,747,862 | 9,861,678 | 10,843,499 | 11,793,201 | 12,264,511 | 12,933,035 |
| H | Usafirishaji na Uhifadhi mizigo | 6,929,895 | 7,549,484 | 7,897,993 | 8,381,276 | 9,622,792 | 11,172,778 |
| I | Malazi na Huduma ya chakula | 1,421,916 | 1,523,035 | 1,602,543 | 1,653,792 | 1,764,898 | 1,506,711 |
| J | Habari na Mawasiliano | 1,681,098 | 1,739,556 | 1,829,360 | 1,948,180 | 2,052,242 | 2,196,751 |
| K | Fedha na Bima | 4,189,021 | 5,268,866 | 4,789,632 | 4,947,301 | 4,927,613 | 5,259,757 |
| L | Upangishaji Majengo | 2,949,598 | 3,162,290 | 3,334,171 | 3,553,630 | 3,834,061 | 4,253,836 |
| M | Sughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundi | 518,123 | 617,914 | 726,707 | 817,442 | 903,234 | 986,133 |
| N | Huduma zinazohusiana na Utawala | 2,183,917 | 2,661,978 | 3,027,384 | 3,306,554 | 3,640,720 | 3,992,260 |
| O | Utawala na Ulinzi | 4,548,604 | 4,846,491 | 4,986,287 | 5,131,630 | 5,354,893 | 5,531,515 |
| P | Elimu | 2,413,306 | 2,673,289 | 2,864,290 | 3,081,718 | 3,322,028 | 3,439,015 |
| Q | Afya na Huduma za Jamii | 1,419,090 | 1,540,484 | 1,681,353 | 1,816,738 | 1,920,963 | 2,044,830 |
| R | Sanaa na Burudani | 248,510 | 285,626 | 322,353 | 374,924 | 427,887 | 416,049 |
| S | Huduma nyingine za Kijamii | 717,898 | 831,216 | 959,152 | 1,037,612 | 1,140,417 | 1,217,190 |
| T | Shughuli za Kaya katika kuajiri | 177,691 | 185,501 | 201,872 | 215,564 | 241,246 | 251,635 |
| | **Jumla ya Ongezeko la Thamani** | **86,484,736** | **99,423,658** | **108,956,774** | **118,874,163** | **128,554,255** | **140,098,746** |
| | Ongeza kodi katika bidhaa | 7,864,579 | 8,938,667 | 9,787,724 | 10,169,738 | 11,087,600 | 8,423,365 |
| | **Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko** | **94,349,316** | **108,362,324** | **118,744,498** | **129,043,901** | **139,641,854** | **148,522,111** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**PATO LA TAIFA (GDP) KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI KWA BEI ZA SOKO - SEHEMU INAYOUZIKA NA ISIYOUZIKA**
**(Bei za Miaka Inayohusika)**

Jedwali Na. 1A | Sh. Milioni

| | SHUGHULI YA KIUCHUMI | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **A: SEHEMU INAYOUZIKA** | | | | | | |
| | **Jumla ya Pato la Taifa (GDPmp)** | **84,275,963** | **97,295,383** | **106,025,246** | **114,220,803** | **124,491,292** | **132,130,577** |
| A | ***Kilimo, Misitu na Uvuvi*** | ***16,020,386*** | ***19,628,661*** | ***22,561,096*** | ***22,410,625*** | ***23,371,988*** | ***24,989,034*** |
| | Kilimo cha Mazao | 7,176,326 | 9,729,649 | 11,822,710 | 11,350,635 | 11,179,456 | 12,358,090 |
| | Mifugo | 5,160,608 | 6,322,457 | 6,877,739 | 6,661,287 | 7,457,872 | 7,648,783 |
| | Misitu | 1,882,033 | 1,706,926 | 1,680,599 | 2,229,486 | 2,409,141 | 2,544,237 |
| | Uvuvi | 1,768,534 | 1,834,769 | 2,142,032 | 2,128,621 | 2,282,546 | 2,392,865 |
| | Huduma za katika shughuli za Kilimo | 32,886 | 34,861 | 38,017 | 40,596 | 42,973 | 45,060 |
| | ***Viwanda na Ujenzi*** | ***22,361,768*** | ***26,111,436*** | ***28,749,158*** | ***33,722,200*** | ***38,766,672*** | ***43,685,850*** |
| B | Uchimbaji Madini na Mawe | 4,055,619 | 5,299,362 | 5,206,217 | 6,573,059 | 7,213,403 | 9,921,721 |
| C | Viwanda | 7,411,672 | 8,467,126 | 9,102,282 | 10,418,776 | 11,860,403 | 12,539,107 |
| D | Umeme | 798,801 | 472,868 | 413,351 | 348,527 | 369,917 | 398,086 |
| E | Maji safi na Maji taka | 272,990 | 301,821 | 372,032 | 395,810 | 438,862 | 525,028 |
| F | Ujenzi | 9,822,685 | 11,570,259 | 13,655,276 | 15,986,029 | 18,884,087 | 20,301,908 |
| | ***Huduma*** | ***38,029,229*** | ***42,616,618*** | ***44,927,268*** | ***47,918,240*** | ***51,265,032*** | ***55,032,328*** |
| G | Biashara na Matengenezo | 8,747,862 | 9,861,678 | 10,843,499 | 11,793,201 | 12,264,511 | 12,933,035 |
| H | Usafirishaji na Uhifadhi mizigo | 6,929,895 | 7,549,484 | 7,897,993 | 8,381,276 | 9,622,792 | 11,172,778 |
| I | Malazi na Huduma ya chakula | 1,421,916 | 1,523,035 | 1,602,543 | 1,653,792 | 1,764,898 | 1,506,711 |
| J | Habari na Mawasiliano | 1,681,098 | 1,739,556 | 1,829,360 | 1,948,180 | 2,052,242 | 2,196,751 |
| K | Fedha na Bima | 4,189,021 | 5,268,866 | 4,789,632 | 4,947,301 | 4,927,613 | 5,259,757 |
| L | Upangishaji Majengo | 2,832,298 | 3,031,501 | 3,194,842 | 3,412,309 | 3,681,588 | 4,084,669 |
| M | Sughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundi | 518,123 | 617,914 | 726,707 | 817,442 | 903,234 | 986,133 |
| N | Huduma zinazohusiana na Utawala | 2,183,917 | 2,661,978 | 3,027,384 | 3,306,554 | 3,640,720 | 3,992,260 |
| O | Utawala na Ulinzi | 4,548,604 | 4,846,491 | 4,986,287 | 5,131,630 | 5,354,893 | 5,531,515 |
| P | Elimu | 2,413,306 | 2,673,289 | 2,864,290 | 3,081,718 | 3,322,028 | 3,439,015 |
| Q | Afya na Huduma za Jamii | 1,419,090 | 1,540,484 | 1,681,353 | 1,816,738 | 1,920,963 | 2,044,830 |
| R | Sanaa na Burudani | 248,510 | 285,626 | 322,353 | 374,924 | 427,887 | 416,049 |
| S | Huduma nyingine za Kijamii | 717,898 | 831,216 | 959,152 | 1,037,612 | 1,140,417 | 1,217,190 |
| T | Shughuli za Kaya katika kuajiri | 177,691 | 185,501 | 201,872 | 215,564 | 241,246 | 251,635 |
| | **Jumla ya Ongezeko la Thamani** | **76,411,383** | **88,356,716** | **96,237,522** | **104,051,065** | **113,403,692** | **123,707,212** |
| | Ongeza kodi katika bidhaa | 7,864,579 | 8,938,667 | 9,787,724 | 10,169,738 | 11,087,600 | 8,423,365 |
| | **B: SEHEMU ISIYOUZIKA** | | | | | | |
| | **Jumla ya Pato la Taifa (GDPmp)** | **10,073,353** | **11,066,941** | **12,719,252** | **14,823,098** | **15,150,563** | **16,391,535** |
| A | Kilimo, Misitu na Uvuvi | 9,214,174 | 10,110,449 | 11,593,497 | 13,552,103 | 13,820,550 | 14,976,028 |
| | Mazao | 6,103,066 | 6,745,080 | 7,880,294 | 9,653,085 | 9,507,507 | 10,509,869 |
| | Mifugo | 1,997,848 | 1,882,549 | 1,980,200 | 2,578,812 | 2,887,197 | 2,961,106 |
| | Misitu | 1,038,392 | 1,387,841 | 1,629,477 | 1,230,096 | 1,329,219 | 1,403,757 |
| | Uvuvi | 74,867 | 94,978 | 103,526 | 90,110 | 96,626 | 101,296 |
| | **Viwanda na Ujenzi** | **741,880** | **825,703** | **986,427** | **1,129,674** | **1,177,540** | **1,246,340** |
| E | Usambazaji maji safi na udhibiti maji taka | 117,768 | 131,311 | 147,877 | 170,752 | 189,325 | 220,194 |
| F | Ujenzi | 624,112 | 694,392 | 838,550 | 958,922 | 988,215 | 1,026,146 |
| | **Huduma** | **117,300** | **130,789** | **139,328** | **141,321** | **152,473** | **169,167** |
| L | Upangishaji Majengo | 117,300 | 130,789 | 139,328 | 141,321 | 152,473 | 169,167 |
| | **Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko** | **94,349,316** | **108,362,324** | **118,744,498** | **129,043,901** | **139,641,854** | **148,522,111** |

**Chanzo**:Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**PATO LA TAIFA (GDP) KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI KWA BEI ZA SOKO**
**(Bei za Miaka Inayohusika)**

Jedwali Na. 2 Asilimia

| | SHUGHULI YA KIUCHUMI | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| A | ***Kilimo, Misitu na Uvuvi*** | ***26.7*** | ***27.4*** | ***28.8*** | ***27.9*** | ***26.6*** | ***26.9*** |
| | Kilimo cha Mazao | 14.1 | 15.2 | 16.6 | 16.3 | 14.8 | 15.4 |
| | Mifugo | 7.6 | 7.6 | 7.5 | 7.2 | 7.4 | 7.1 |
| | Misitu | 3.1 | 2.9 | 2.8 | 2.7 | 2.7 | 2.7 |
| | Uvuvi | 2.0 | 1.8 | 1.9 | 1.7 | 1.7 | 1.7 |
| | Huduma za katika shughuli za Kilimo | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| B | Uchimbaji Madini na Mawe | 4.3 | 4.9 | 4.4 | 5.1 | 5.2 | 6.7 |
| C | Viwanda | 7.9 | 7.8 | 7.7 | 8.1 | 8.5 | 8.4 |
| D | Umeme | 0.8 | 0.4 | 0.3 | 0.3 | 0.3 | 0.3 |
| E | Maji safi na Maji taka | 0.4 | 0.4 | 0.4 | 0.4 | 0.4 | 0.5 |
| F | Ujenzi | 11.1 | 11.3 | 12.2 | 13.1 | 14.2 | 14.4 |
| G | Biashara na Matengenezo | 9.3 | 9.1 | 9.1 | 9.1 | 8.8 | 8.7 |
| H | Usafirishaji na Uhifadhi mizigo | 7.3 | 7.0 | 6.7 | 6.5 | 6.9 | 7.5 |
| I | Malazi na Huduma ya chakula | 1.5 | 1.4 | 1.3 | 1.3 | 1.3 | 1.0 |
| J | Habari na Mawasiliano | 1.8 | 1.6 | 1.5 | 1.5 | 1.5 | 1.5 |
| K | Fedha na Bima | 4.4 | 4.9 | 4.0 | 3.8 | 3.5 | 3.5 |
| L | Upangishaji Majengo | 3.1 | 2.9 | 2.8 | 2.8 | 2.7 | 2.9 |
| M | Shughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundi | 0.5 | 0.6 | 0.6 | 0.6 | 0.6 | 0.7 |
| N | Huduma zinazohusiana na Utawala | 2.3 | 2.5 | 2.5 | 2.6 | 2.6 | 2.7 |
| O | Utawala na Ulinzi | 4.8 | 4.5 | 4.2 | 4.0 | 3.8 | 3.7 |
| P | Elimu | 2.6 | 2.5 | 2.4 | 2.4 | 2.4 | 2.3 |
| Q | Afya na Huduma za Jamii | 1.5 | 1.4 | 1.4 | 1.4 | 1.4 | 1.4 |
| R | Sanaa na Burudani | 0.3 | 0.3 | 0.3 | 0.3 | 0.3 | 0.3 |
| S | Huduma nyingine za Kijamii | 0.8 | 0.8 | 0.8 | 0.8 | 0.8 | 0.8 |
| T | Shughuli za Kaya katika kuajiri | 0.2 | 0.2 | 0.2 | 0.2 | 0.2 | 0.2 |
| | **Jumla ya Ongezeko la Thamani** | **91.7** | **91.8** | **91.8** | **92.1** | **92.1** | **94.3** |
| | Ongeza kodi katika bidhaa | 8.3 | 8.2 | 8.2 | 7.9 | **7.9** | **5.7** |
| | **Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**PATO LA TAIFA (GDP) KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI KWA BEI ZA SOKO - SEHEMU INAYOUZIKA NA ISIYOUZIKA**
**(Bei za Miaka Inayohusika)**

Jedwali Na. 2A

Asilimia

| | SHUGHULI YA KIUCHUMI | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **A: SEHEMU INAYOUZIKA** | | | | | | |
| | **Jumla ya Pato la Taifa (GDPmp)** | | | | | | |
| A | ***Kilimo, Misitu na Uvuvi*** | ***17.0*** | ***18.1*** | ***19.0*** | ***17.4*** | ***16.7*** | ***16.8*** |
| | Kilimo cha Mazao | 7.6 | 9.0 | 10.0 | 8.8 | 8.0 | 8.3 |
| | Mifugo | 5.5 | 5.8 | 5.8 | 5.2 | 5.3 | 5.1 |
| | Misitu | 2.0 | 1.6 | 1.4 | 1.7 | 1.7 | 1.7 |
| | Uvuvi | 1.9 | 1.7 | 1.8 | 1.7 | 1.6 | 1.6 |
| | Huduma za katika shughuli za Kilimo | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| B | Uchimbaji Madini na Mawe | 4.3 | 4.9 | 4.4 | 5.1 | 5.2 | 6.7 |
| C | Viwanda | 7.9 | 7.8 | 7.7 | 8.1 | 8.5 | 8.4 |
| D | Umeme | 0.8 | 0.4 | 0.3 | 0.3 | 0.3 | 0.3 |
| E | Maji safi na Maji taka | 0.3 | 0.3 | 0.3 | 0.3 | 0.3 | 0.4 |
| F | Ujenzi | 10.4 | 10.7 | 11.5 | 12.4 | 13.5 | 13.7 |
| G | Biashara na Matengenezo | 9.3 | 9.1 | 9.1 | 9.1 | 8.8 | 8.7 |
| H | Uchukuzi na Uhifadhi mizigo | 7.3 | 7.0 | 6.7 | 6.5 | 6.9 | 7.5 |
| I | Malazi na Huduma ya chakula | 1.5 | 1.4 | 1.3 | 1.3 | 1.3 | 1.0 |
| J | Habari na Mawasiliano | 1.8 | 1.6 | 1.5 | 1.5 | 1.5 | 1.5 |
| K | Fedha na Bima | 4.4 | 4.9 | 4.0 | 3.8 | 3.5 | 3.5 |
| L | Upangishaji Majengo | 3.0 | 2.8 | 2.7 | 2.6 | 2.6 | 2.8 |
| M | Shughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundi | 0.5 | 0.6 | 0.6 | 0.6 | 0.6 | 0.7 |
| N | Huduma zinazohusiana na Utawala | 2.3 | 2.5 | 2.5 | 2.6 | 2.6 | 2.7 |
| O | Utawala na Ulinzi | 4.8 | 4.5 | 4.2 | 4.0 | 3.8 | 3.7 |
| P | Elimu | 2.6 | 2.5 | 2.4 | 2.4 | 2.4 | 2.3 |
| Q | Afya na Huduma za Jamii | 1.5 | 1.4 | 1.4 | 1.4 | 1.4 | 1.4 |
| R | Sanaa na Burudani | 0.3 | 0.3 | 0.3 | 0.3 | 0.3 | 0.3 |
| S | Huduma nyingine za Kijamii | 0.8 | 0.8 | 0.8 | 0.8 | 0.8 | 0.8 |
| T | Shughuli za Kaya katika kuajiri | 0.2 | 0.2 | 0.2 | 0.2 | 0.2 | 0.2 |
| | **Jumla ya Ongezeko la Thamani** | **81.0** | **81.5** | **81.0** | **80.6** | **81.2** | **83.3** |
| | Ongeza kodi katika bidhaa | 8.3 | 8.2 | 8.2 | 7.9 | 7.9 | 5.7 |
| | **B: SEHEMU ISIYOUZIKA** | | | | | | |
| | **Jumla ya Pato la Taifa (GDPmp)** | **10.7** | **10.2** | **10.7** | **11.5** | **10.8** | **11.0** |
| A | Kilimo, Misitu na Uvuvi | 9.8 | 9.3 | 9.8 | 10.5 | 9.9 | 10.1 |
| | Mazao | 6.5 | 6.2 | 6.6 | 7.5 | 6.8 | 7.1 |
| | Mifugo | 2.1 | 1.7 | 1.7 | 2.0 | 2.1 | 2.0 |
| | Misitu | 1.1 | 1.3 | 1.4 | 1.0 | 1.0 | 0.9 |
| | Uvuvi | 0.1 | 0.1 | 0.1 | 0.1 | 0.1 | 0.1 |
| E | Usambazaji maji safi na udhibiti maji taka | 0.1 | 0.1 | 0.1 | 0.1 | 0.1 | 0.1 |
| F | Ujenzi | 0.7 | 0.6 | 0.7 | 0.7 | 0.7 | 0.7 |
| L | Upangishaji Majengo | 0.1 | 0.1 | 0.1 | 0.1 | 0.1 | 0.1 |
| | **Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** |

**Chanzo**: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**PATO LA TAIFA NA MATUMIZI YAKE KWA BEI ZA SOKO**
**(Bei za Miaka inayohusika)**

Jedwali Na. 2B **Sh. Milioni**

| **Aina ya Matumizi** | **2015** | **2016** | **2017** | **2018** | **2019** | **2020** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Pato la Taifa kwa Bei za Soko (GDPmp)** | **94,349,316** | **108,362,324** | **118,744,498** | **129,043,901** | **139,641,854** | **148,522,111** |
| **Matumizi ya Mwisho (Final consumption)** | **69,619,572** | **74,761,715** | **81,577,249** | **87,731,958** | **93,002,322** | **99,965,192** |
| Serikali | 9,366,334 | 9,824,677 | 10,097,404 | 10,468,798 | 10,978,620 | 11,195,316 |
| Binafsi | 60,047,089 | 64,699,505 | 71,211,545 | 76,966,654 | 81,712,049 | 88,445,302 |
| Taasisi binafsi Zinazotoa huduma za kijamii | 206,149 | 237,532 | 268,299 | 296,506 | 311,653 | 324,574 |
| **Ukuzaji rasilimali** | **30,907,602** | **34,865,346** | **40,427,427** | **49,493,556** | **55,762,365** | **59,235,366** |
| Rasilimali za kudumu | 30,070,195 | 35,492,828 | 42,141,921 | 50,387,086 | 59,440,540 | 64,049,913 |
| Ongezeko la limbikizo la Vito vya Thamani | 903,043 | 1,105,406 | 1,006,179 | 1,215,104 | 1,273,337 | 1,838,290 |
| Ongezeko la limbikizo | -65,636 | -1,732,887 | -2,720,674 | -2,108,634 | -4,951,512 | -6,652,837 |
| Mauzo nje | **16,138,367** | **17,717,213** | **17,993,324** | **19,160,137** | **22,160,020** | **20,813,548** |
| Bidhaa-fob | 8,708,690 | 9,177,377 | 8,924,522 | 10,066,069 | 12,305,060 | 14,617,648 |
| Huduma | 7,429,677 | 8,539,835 | 9,068,803 | 9,094,069 | 9,854,960 | 6,195,900 |
| Uagizaji | **22,316,226** | **20,665,232** | **20,320,749** | **23,103,332** | **24,152,270** | **21,051,375** |
| Bidhaa-fob | 16,955,419 | 15,602,694 | 15,816,338 | 18,797,200 | 20,120,379 | 18,098,427 |
| Huduma | 5,360,807 | 5,062,538 | 4,504,411 | 4,306,132 | 4,031,891 | 2,952,948 |
| Makosa na Mapungufu | 0 | 1,683,283 | -932,752 | -4,238,418 | -7,130,583 | -10,440,620 |

**Chanzo**: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**PATO LA TAIFA KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI**
**(Bei za mwaka 2015)**

Jedwali Na. 3 **Sh. Milioni**

| | **SHUGHULI YA KIUCHUMI** | **2015** | **2016** | **2017** | **2018** | **2019** | **2020** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| A | **Kilimo, Misitu na Uvuvi** | **25,234,560** | **26,436,338** | **28,008,976** | **29,504,198** | **30,802,027** | **32,321,327** |
| | Kilimo cha Mazao | 13,279,392 | 13,996,348 | 14,895,622 | 15,659,175 | 16,351,312 | 17,174,752 |
| | Mifugo | 7,158,457 | 7,506,593 | 7,876,592 | 8,266,049 | 8,676,074 | 9,107,854 |
| | Misitu | 2,920,425 | 3,034,569 | 3,180,379 | 3,334,791 | 3,495,187 | 3,608,190 |
| | Uvuvi | 1,843,401 | 1,864,627 | 2,020,292 | 2,206,242 | 2,239,892 | 2,389,915 |
| | Huduma za katika shughuli za Kilimo | 32,886 | 34,201 | 36,091 | 37,941 | 39,562 | 40,615 |
| | **Viwanda na Ujenzi** | **23,103,647** | **25,817,955** | **28,565,774** | **31,344,128** | **34,976,982** | **37,507,952** |
| B | Uchimbaji Madini na Mawe | 4,055,619 | 4,356,709 | 4,588,624 | 4,659,195 | 5,485,112 | 5,850,231 |
| C | Viwanda | 7,411,672 | 8,213,364 | 8,889,818 | 9,623,501 | 10,184,558 | 10,646,279 |
| D | Umeme | 798,801 | 869,262 | 877,667 | 928,174 | 994,879 | 1,049,611 |
| E | Maji safi na Maji taka | 390,758 | 417,899 | 444,660 | 477,510 | 510,411 | 540,159 |
| F | Ujenzi | 10,446,797 | 11,960,720 | 13,765,005 | 15,655,747 | 17,802,021 | 19,421,672 |
| | **Huduma** | **38,146,529** | **40,549,564** | **42,689,011** | **45,369,789** | **48,114,453** | **50,173,139** |
| G | Biashara na Matengenezo | 8,747,862 | 9,260,703 | 9,821,248 | 10,396,691 | 10,965,038 | 11,194,534 |
| H | Usafirishaji na Uhifadhi mizigo | 6,929,895 | 7,324,856 | 7,815,845 | 8,736,561 | 9,493,191 | 10,293,276 |
| I | Malazi na Huduma ya chakula | 1,421,916 | 1,480,052 | 1,525,619 | 1,604,391 | 1,645,950 | 1,419,654 |
| J | Habari na Mawasiliano | 1,681,098 | 1,718,548 | 1,824,471 | 1,989,717 | 2,133,312 | 2,313,033 |
| K | Fedha na Bima | 4,189,021 | 4,235,515 | 4,115,393 | 4,094,972 | 4,281,167 | 4,412,967 |
| L | Upangishaji Majengo | 2,949,598 | 3,077,086 | 3,211,895 | 3,354,518 | 3,505,485 | 3,663,972 |
| M | Shughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundi | 518,123 | 606,207 | 694,291 | 763,332 | 821,636 | 881,833 |
| N | Huduma zinazohusiana na Utawala | 2,183,917 | 2,611,498 | 2,892,463 | 3,054,288 | 3,311,753 | 3,569,800 |
| O | Utawala na Ulinzi | 4,548,604 | 4,793,820 | 4,907,113 | 5,064,968 | 5,238,491 | 5,438,923 |
| P | Elimu | 2,413,306 | 2,665,336 | 2,859,171 | 3,046,789 | 3,257,406 | 3,363,845 |
| Q | Afya na Huduma za Jamii | 1,419,090 | 1,497,896 | 1,611,999 | 1,746,731 | 1,833,514 | 1,952,425 |
| R | Sanaa na Burudani | 248,510 | 280,131 | 307,907 | 350,027 | 389,225 | 372,120 |
| S | Huduma nyingine za Kijamii | 717,898 | 814,529 | 912,404 | 971,690 | 1,037,083 | 1,089,265 |
| T | Shughuli za Kaya katika kuajiri | 177,691 | 183,387 | 189,193 | 195,113 | 201,203 | 207,492 |
| | **Jumla ya Ongezeko la Thamani** | **86,484,736** | **92,803,857** | **99,263,761** | **106,218,115** | **113,893,462** | **120,002,418** |
| | Ongeza kodi katika bidhaa | 7,864,579 | 8,024,535 | 8,393,644 | 8,923,215 | 9,303,274 | 9,093,427 |
| | **Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko** | **94,349,316** | **100,828,393** | **107,657,405** | **115,141,329** | **123,196,736** | **129,095,844** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwiimu

## PATO LA TAIFA KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI, KWA BEI ZA SOKO - SEHEMU INAYOUZIKA NA ISIYOUZIKA
### (Bei za mwaka 2015)

Jedwali Na. 3A — Sh. Milioni

| | SHUGHULI YA KIUCHUMI | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **A: SEHEMU INAYOUZIKA** | | | | | | |
| | **Jumla ya Pato la Taifa (GDPmp)** | **90,262,677** | **96,464,568** | **103,029,270** | **110,210,543** | **118,007,109** | **123,641,315** |
| A | ***Kilimo, Misitu na Uvuvi*** | ***21,953,873*** | ***22,914,869*** | ***24,357,439*** | ***25,671,332*** | ***26,820,733*** | ***28,171,298*** |
| | Kilimo cha Mazao | 11,330,959 | 11,852,633 | 12,666,159 | 13,361,566 | 13,975,902 | 14,689,561 |
| | Mifugo | 6,131,537 | 6,458,453 | 6,797,008 | 7,080,239 | 7,435,167 | 7,820,592 |
| | Misitu | 2,629,474 | 2,720,412 | 2,853,656 | 3,002,559 | 3,147,670 | 3,248,720 |
| | Uvuvi | 1,829,018 | 1,849,169 | 2,004,525 | 2,189,028 | 2,222,432 | 2,371,811 |
| | Huduma za katika shughuli za Kilimo | 32,886 | 34,201 | 36,091 | 37,941 | 39,562 | 40,615 |
| | ***Viwanda na Ujenzi*** | ***22,391,185*** | ***25,070,677*** | ***27,685,960*** | ***30,352,531*** | ***33,879,613*** | ***36,319,467*** |
| B | Uchimbaji Madini na Mawe | 4,055,619 | 4,356,709 | 4,588,624 | 4,659,195 | 5,485,112 | 5,850,231 |
| C | Viwanda | 7,411,672 | 8,213,364 | 8,889,818 | 9,623,501 | 10,184,558 | 10,646,279 |
| D | Umeme | 798,801 | 869,262 | 877,667 | 928,174 | 994,879 | 1,049,611 |
| E | Maji safi na Maji taka | 302,407 | 326,898 | 350,019 | 369,545 | 396,149 | 420,891 |
| F | Ujenzi | 9,822,685 | 11,304,444 | 12,979,833 | 14,772,116 | 16,818,914 | 18,352,455 |
| | ***Huduma*** | ***38,053,040*** | ***40,454,486*** | ***42,592,227*** | ***45,263,466*** | ***48,003,489*** | ***50,057,123*** |
| G | Biashara na Matengenezo | 8,747,862 | 9,260,703 | 9,821,248 | 10,396,691 | 10,965,038 | 11,194,534 |
| H | Usafirishaji na Uhifadhi mizigo | 6,929,895 | 7,324,856 | 7,815,845 | 8,736,561 | 9,493,191 | 10,293,276 |
| I | Malazi na Huduma ya chakula | 1,421,916 | 1,480,052 | 1,525,619 | 1,604,391 | 1,645,950 | 1,419,654 |
| J | Habari na Mawasiliano | 1,681,098 | 1,718,548 | 1,824,471 | 1,989,717 | 2,133,312 | 2,313,033 |
| K | Fedha na Bima | 4,189,021 | 4,235,515 | 4,115,393 | 4,094,972 | 4,281,167 | 4,412,967 |
| L | Upangishaji Majengo | 2,856,109 | 2,982,008 | 3,115,112 | 3,248,194 | 3,394,521 | 3,547,957 |
| M | Shughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundi | 518,123 | 606,207 | 694,291 | 763,332 | 821,636 | 881,833 |
| N | Huduma zinazohusiana na Utawala | 2,183,917 | 2,611,498 | 2,892,463 | 3,054,288 | 3,311,753 | 3,569,800 |
| O | Utawala na Ulinzi | 4,548,604 | 4,793,820 | 4,907,113 | 5,064,968 | 5,238,491 | 5,438,923 |
| P | Elimu | 2,413,306 | 2,665,336 | 2,859,171 | 3,046,789 | 3,257,406 | 3,363,845 |
| Q | Afya na Huduma za Jamii | 1,419,090 | 1,497,896 | 1,611,999 | 1,746,731 | 1,833,514 | 1,952,425 |
| R | Sanaa na Burudani | 248,510 | 280,131 | 307,907 | 350,027 | 389,225 | 372,120 |
| S | Huduma nyingine za Kijamii | 717,898 | 814,529 | 912,404 | 971,690 | 1,037,083 | 1,089,265 |
| T | Shughuli za Kaya katika kuajiri | 177,691 | 183,387 | 189,193 | 195,113 | 201,203 | 207,492 |
| | **Jumla ya Ongezeko la Thamani** | **82,398,098** | **88,440,032** | **94,635,626** | **101,287,328** | **108,703,835** | **114,547,888** |
| | Ongeza kodi katika bidhaa | 7,864,579 | 8,024,535 | 8,393,644 | 8,923,215 | 9,303,274 | 9,093,427 |
| | **B: SEHEMU ISIYOUZIKA** | | | | | | |
| | **Jumla ya Pato la Taifa (GDPmp)** | **4,086,638** | **4,363,825** | **4,628,135** | **4,930,787** | **5,189,627** | **5,454,529** |
| A | Kilimo, Misitu na Uvuvi | 3,280,687 | 3,521,469 | 3,651,537 | 3,832,866 | 3,981,294 | 4,150,029 |
| | Mazao | 1,948,433 | 2,143,714 | 2,229,463 | 2,297,609 | 2,375,410 | 2,485,191 |
| | Mifugo | 1,026,920 | 1,048,140 | 1,079,584 | 1,185,810 | 1,240,908 | 1,287,262 |
| | Misitu | 290,951 | 314,157 | 326,723 | 332,233 | 347,517 | 359,470 |
| | Uvuvi | 14,383 | 15,458 | 15,767 | 17,214 | 17,459 | 18,104 |
| | **Viwanda na Ujenzi** | **712,462** | **747,278** | **879,814** | **991,597** | **1,097,369** | **1,188,485** |
| E | Usambazaji maji safi na udhibiti maji taka | 88,351 | 91,001 | 94,641 | 107,966 | 114,262 | 119,268 |
| F | Ujenzi | 624,112 | 656,276 | 785,173 | 883,632 | 983,107 | 1,069,217 |
| | **Huduma** | 93,489 | 95,078 | 96,783 | 106,323 | 110,964 | 116,016 |
| L | Upangishaji Majengo | 93,489 | 95,078 | 96,783 | 106,323 | 110,964 | 116,016 |
| | **Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko** | **94,349,316** | **100,828,393** | **107,657,405** | **115,141,329** | **123,196,736** | **129,095,844** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**PATO LA TAIFA KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI**


**(Bei za mwaka 2015)**

Jedwali NA. 4 **Asilimia**

| | **SHUGHULI YA KIUCHUMI** | **2015** | **2016** | **2017** | **2018** | **2019** | **2020** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| A | Kilimo, Misitu na Uvuvi | **5.4** | **4.8** | **5.9** | **5.4** | 4.4 | 4.9 |
| | Kilimo cha Mazao | 7.6 | 5.4 | 6.4 | 5.2 | 4.4 | 5.0 |
| | Mifugo | 4.9 | 4.9 | 4.9 | 4.9 | 5.0 | 5.0 |
| | Misitu | 3.4 | 3.9 | 4.8 | 4.9 | 4.8 | 3.2 |
| | Uvuvi | -4.5 | 1.2 | 8.4 | 9.2 | 1.5 | 6.7 |
| | Huduma za katika shughuli za Kilimo | 4.5 | 4.0 | 5.5 | 5.2 | 4.3 | 2.7 |
| B | Uchimbaji Madini na Mawe | 10.0 | 7.4 | 5.3 | 1.5 | 17.7 | 6.7 |
| C | Viwanda | 7.1 | 10.8 | 8.2 | 8.3 | 5.8 | 4.5 |
| D | Umeme | -2.0 | 8.8 | 1.0 | 5.8 | 7.2 | 5.5 |
| E | Maji safi na Maji taka | 2.4 | 6.9 | 6.4 | 7.4 | 6.9 | 5.8 |
| F | Ujenzi | 12.9 | 14.5 | 15.1 | 13.8 | 13.7 | 9.1 |
| G | Biashara na Matengenezo | 3.6 | 5.9 | 6.1 | 5.9 | 5.5 | 2.1 |
| H | Usafirishaji na Uhifadhi mizigo | 5.4 | 5.7 | 6.7 | 11.8 | 8.7 | 8.4 |
| I | Malazi na Huduma ya chakula | 1.7 | 4.1 | 3.1 | 5.2 | 2.6 | -13.7 |
| J | Habari na Mawasiliano | 7.8 | 2.2 | 6.2 | 9.1 | 7.2 | 8.4 |
| K | Fedha na Bima | 11.3 | 1.1 | -2.8 | -0.5 | 4.5 | 3.1 |
| L | Upangishaji Majengo | 4.3 | 4.3 | 4.4 | 4.4 | 4.5 | 4.5 |
| M | Shughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundi | 15.7 | 17.0 | 14.5 | 9.9 | 7.6 | 7.3 |
| N | Huduma zinazohusiana na Utawala | 10.5 | 19.6 | 10.8 | 5.6 | 8.4 | 7.8 |
| O | Utawala na Ulinzi | 7.2 | 5.4 | 2.4 | 3.2 | 3.4 | 3.8 |
| P | Elimu | 10.4 | 10.4 | 7.3 | 6.6 | 6.9 | 3.3 |
| Q | Afya na Huduma za Jamii | 5.1 | 5.6 | 7.6 | 8.4 | 5.0 | 6.5 |
| R | Sanaa na Burudani | 7.7 | 12.7 | 9.9 | 13.7 | 11.2 | -4.4 |
| S | Huduma nyingine za Kijamii | 4.7 | 13.5 | 12.0 | 6.5 | 6.7 | 5.0 |
| T | Shughuli za Kaya katika kuajiri | 3.2 | 3.2 | 3.2 | 3.1 | 3.1 | 3.1 |
| | **Jumla ya Ongezeko la Thamani** | **6.9** | **7.3** | **7.0** | **6.9** | **7.2** | **5.4** |
| | Ongeza kodi katika bidhaa | -1.7 | 2.0 | 4.6 | 6.3 | 4.3 | -2.3 |
| | **Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko** | **6.2** | **6.9** | **6.8** | **7.0** | **7.0** | **4.8** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Kielelezo 1.3: UKUAJI HALISI WA PATO LA TAIFA** (Kwa bei za mwaka 2015)



**PATO LA TAIFA KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI, KWA BEI ZA SOKO - SEHEMU INAYOUZIKA NA ISIYOUZIKA (Bei za mwaka 2015)**

Jedwali Na.4A Sh. Milioni

| | SHUGHULI YA KIUCHUMI | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **A: SEHEMU INAYOUZIKA** | | | | | | |
| | **Jumla ya Pato la Taifa (GDPmp)** | | | | | | |
| A | ***Kilimo, Misitu na Uvuvi*** | **6.9** | **4.4** | **6.3** | **5.4** | **4.5** | **5.0** |
| | Kilimo cha Mazao | 10.4 | 4.6 | 6.9 | 5.6 | 4.6 | 5.1 |
| | Mifugo | 5.9 | 5.3 | 5.2 | 4.2 | 5.0 | 5.2 |
| | Misitu | 3.7 | 3.5 | 4.9 | 5.2 | 4.8 | 3.2 |
| | Uvuvi | -4.5 | 1.1 | 8.4 | 9.2 | 1.5 | 6.7 |
| | Huduma za katika shughuli za Kilimo | 4.5 | 4.0 | 5.5 | 5.2 | 4.3 | 2.7 |
| B | Uchimbaji Madini na Mawe | 10.0 | 7.4 | 5.3 | 1.5 | 17.7 | 6.7 |
| C | Viwanda | 7.1 | 10.8 | 8.2 | 8.3 | 5.8 | 4.5 |
| D | Umeme | -2.0 | 8.8 | 1.0 | 5.8 | 7.2 | 5.5 |
| E | Maji safi na Maji taka | 2.0 | 8.1 | 7.1 | 5.6 | 7.2 | 6.2 |
| F | Ujenzi | 12.5 | 15.1 | 14.8 | 13.7 | 13.9 | 9.1 |
| G | Biashara na Matengenezo | 3.6 | 5.9 | 6.1 | 5.9 | 5.5 | 2.1 |
| H | Usafirishaji na Uhifadhi mizigo | 5.4 | 5.7 | 6.7 | 11.8 | 8.7 | 8.4 |
| I | Malazi na Huduma ya chakula | 1.7 | 4.1 | 3.1 | 5.2 | 2.6 | - 13.7 |
| J | Habari na Mawasiliano | 7.8 | 2.2 | 6.2 | 9.1 | 7.2 | 8.4 |
| K | Fedha na Bima | 11.3 | 1.1 | -2.8 | -0.5 | 4.5 | 3.1 |
| L | Upangishaji Majengo | 4.4 | 4.4 | 4.5 | 4.3 | 4.5 | 4.5 |
| M | Shughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundi | 15.7 | 17.0 | 14.5 | 9.9 | 7.6 | 7.3 |
| N | Huduma zinazohusiana na Utawala | 10.5 | 19.6 | 10.8 | 5.6 | 8.4 | 7.8 |
| O | Utawala na Ulinzi | 7.2 | 5.4 | 2.4 | 3.2 | 3.4 | 3.8 |
| P | Elimu | 10.4 | 10.4 | 7.3 | 6.6 | 6.9 | 3.3 |
| Q | Afya na Huduma za Jamii | 5.1 | 5.6 | 7.6 | 8.4 | 5.0 | 6.5 |
| R | Sanaa na Burudani | 7.7 | 12.7 | 9.9 | 13.7 | 11.2 | - 4.4 |
| S | Huduma nyingine za Kijamii | 4.7 | 13.5 | 12.0 | 6.5 | 6.7 | 5.0 |
| T | Shughuli za Kaya katika kuajiri | 3.2 | 3.2 | 3.2 | 3.1 | 3.1 | 3.1 |
| | **Jumla ya Ongezeko la Thamani** | **7.3** | **7.3** | **7.0** | **6.9** | **7.3** | **5.4** |
| | Ongeza kodi katika bidhaa | -1.7 | 2.0 | 4.5 | 6.3 | **4.3** | **- 2.3** |
| | **B: SEHEMU ISIYOUZIKA** | | | | | | |
| | **Jumla ya Pato la Taifa (GDPmp)** | **-0.6** | **6.8** | **6.1** | **6.4** | **5.2** | **5.1** |
| A | Kilimo, Misitu na Uvuvi | -3.9 | 7.3 | 3.7 | 5.0 | 3.9 | 4.2 |
| | Mazao | -6.2 | 10.0 | 4.0 | 3.1 | 3.4 | 4.6 |
| | Mifugo | -0.6 | 2.1 | 3.0 | 9.8 | 4.6 | 3.7 |
| | Misitu | 0.7 | 8.0 | 4.0 | 1.7 | 4.6 | 3.4 |
| | Uvuvi | -5.1 | 7.5 | 2.0 | 9.2 | 1.4 | 3.7 |
| E | Usambazaji maji safi na udhibiti maji taka | 3.4 | 3.0 | 4.0 | 14.1 | 5.8 | 4.4 |
| F | Ujenzi | 19.5 | 5.2 | 19.6 | 12.5 | 11.3 | 8.8 |
| L | Upangishaji Majengo | 1.5 | 1.7 | 1.8 | 9.9 | 4.4 | 4.6 |
| | **Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko** | **6.2** | **6.9** | **6.8** | **7.0** | **7.0** | **4.8** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

## PATO LA TAIFA NA MATUMIZI YAKE KWA BEI ZA SOKO
## (Bei za mwaka 2015)

Jedwali Na. 4B — Sh. Milioni

| Aina ya Matumizi | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Pato la Taifa kwa Gharama zake (GDPbp)** | **86,484,736** | **92,803,857** | **99,263,761** | **106,218,115** | **113,893,462** | **120,002,418** |
| **Kodi za uzalishaji** | **7,864,579** | **8,024,535** | **8,393,644** | **8,923,215** | **9,303,274** | **9,093,427** |
| **Pato la Taifa kwa Bei za Soko (GDPmp)** | **94,349,316** | **100,828,393** | **107,657,405** | **115,141,329** | **123,196,736** | **129,095,844** |
| **MATUMIZI YA PATO LA TAIFA** | | | | | | |
| **Pato la Taifa kwa Bei za Soko (GDPmp)** | **94,349,316** | **100,828,393** | **107,657,405** | **115,141,329** | **123,196,736** | **129,095,844** |
| **Matumizi ya Mwisho** | **69,619,572** | **70,594,782** | **73,603,189** | **77,376,434** | **79,848,346** | **83,205,811** |
| Serikali | 9,366,334 | 9,667,251 | 9,771,806 | 9,965,992 | 10,310,060 | 10,647,864 |
| Binafsi | 60,047,089 | 60,697,766 | 63,578,381 | 67,135,273 | 69,253,213 | 72,259,048 |
| Taasisi binafsi Zinazotoa huduma za kijamii | 206,149 | 229,766 | 253,003 | 275,169 | 285,073 | 298,899 |
| **Ukuzaji rasilimali** | **30,907,602** | **33,795,169** | **38,338,123** | **44,669,633** | **49,349,298** | **51,708,028** |
| Rasilimali za kudumu | 30,070,195 | 34,878,462 | 40,376,858 | 46,705,540 | 53,777,604 | 57,519,761 |
| Ongezeko la limbikizo la Vito vya Thamani | 903,043 | 902,490 | 858,566 | 776,123 | 925,034 | 1,096,591 |
| Ongezeko la limbikizo | -65,636 | -1,985,783 | -2,897,301 | -2,812,030 | -5,353,340 | -6,908,325 |
| Mauzo nje | **16,138,367** | **16,137,713** | **15,480,491** | **15,316,635** | **17,905,766** | **15,683,119** |
| Bidhaa-fob | 8,708,690 | 8,060,826 | 7,805,507 | 7,608,448 | 9,797,768 | 10,233,451 |
| Huduma | 7,429,677 | 8,076,886 | 7,674,984 | 7,708,187 | 8,107,998 | 5,449,668 |
| Uagizaji | **22,316,226** | **20,331,252** | **18,879,441** | **22,025,703** | **22,051,517** | **19,922,411** |
| Bidhaa-fob | 16,955,419 | 15,631,116 | 15,311,240 | 18,593,941 | 18,940,515 | 17,554,120 |
| Huduma | 5,360,807 | 4,700,136 | 3,568,202 | 3,431,761 | 3,111,002 | 2,368,291 |
| Makosa na Mapungufu | 0 | 631,981 | -884,958 | -195,670 | -1,855,158 | -1,578,703 |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**UKUZAJI RASILIMALI KWA AINA YA SHUGHULI**
**(Bei za Miaka Inayohusika)**

Jedwali Na. 5 Shs.Milioni

| **Aina** | **2015** | **2016** | **2017** | **2018** | **2019** | **2020** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Majengo | 22,807,556 | 27,721,670 | 33,872,241 | 41,694,655 | 50,181,960 | 53,000,466 |
| Vifaa vya Usafiri | 1,663,027 | 1,514,772 | 1,413,888 | 1,763,519 | 1,933,144 | 2,241,710 |
| Mitambo na Vifaa | 3,194,486 | 3,430,297 | 3,756,643 | 3,400,915 | 3,508,102 | 4,323,098 |
| Aina nyingine za Mitambo na Vifaa | 1,172,391 | 1,366,982 | 1,441,018 | 1,688,577 | 1,785,118 | 2,146,447 |
| Rasilimali za Mazao ya Mifugo | 375,399 | 425,361 | 461,511 | 510,723 | 566,744 | 649,209 |
| Haki ya Umiliki, Utafiti na Maendeleo na Huduma za Kitaalamu | 857,335 | 1,033,744 | 1,196,620 | 1,328,698 | 1,465,471 | 1,688,984 |
| Rasilimali za kudumu | 30,070,195 | 35,492,828 | 42,141,921 | 50,387,086 | 59,440,540 | 64,049,913 |
| Ongezeko la limbikizo la Vito vya Thamani | 903,043 | 1,105,406 | 1,006,179 | 1,215,104 | 1,273,337 | 1,838,290 |
| Ongezeko la limbikizo | -65,636 | -1,732,887 | -2,720,674 | -2,108,634 | -4,951,512 | -6,652,837 |
| **Jumla ya Ukuzaji Rasilimali** | **30,907,602** | **34,865,346** | **40,427,427** | **49,493,556** | **55,762,365** | **59,235,366** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

## UKUZAJI RASILIMALI KWA AINA YA SHUGHULI
## (Bei za Mwaka 2015)

Jedwali Na. 6 Shs.Milioni

| Aina | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Majengo | 22,807,556 | 27,512,753 | 32,836,681 | 38,590,978 | 45,205,617 | 47,526,349 |
| Vifaa vya Usafiri | 1,663,027 | 1,373,682 | 1,173,050 | 1,778,192 | 2,128,145 | 2,189,915 |
| Mitambo na Vifaa | 3,194,486 | 3,268,709 | 3,473,892 | 3,136,401 | 3,075,952 | 3,862,605 |
| Mitambo na Vifaa vingine | 1,172,391 | 1,323,953 | 1,335,724 | 1,525,517 | 1,563,289 | 1,878,735 |
| Rasilimali za Mazao ya Mifugo | 375,399 | 385,150 | 414,428 | 434,150 | 472,426 | 534,673 |
| Haki ya Umiliki, Utafiti na Maendeleo na Huduma za Kitaalamu | 857,335 | 1,014,215 | 1,143,083 | 1,240,303 | 1,332,176 | 1,527,483 |
| Rasilimali za kudumu | 30,070,195 | 34,878,462 | 40,376,858 | 46,705,540 | 53,777,604 | 57,519,761 |
| Ongezeko la limbikizo la Vito vya Thamani | 903,043 | 902,490 | 858,566 | 776,123 | 925,034 | 1,096,591 |
| Ongezeko la limbikizo | -65,636 | -1,985,783 | -2,897,301 | -2,812,030 | -5,353,340 | -6,908,325 |
| **Jumla ya Ukuzaji Rasilimali** | **30,907,602** | **33,795,169** | **38,338,123** | **44,669,633** | **49,349,298** | **51,708,028** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**MCHANGO KATIKA RASILIMALI KWA AINA YA SHUGHULI**
**(Bei za Miaka Inayohusika)**

Jedwali Na. 7a

Asilimia

| **Aina** | **2015** | **2016** | **2017** | **2018** | **2019** | **2020** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Majengo | 73.8 | 79.5 | 83.8 | 84.2 | 90.0 | 89.5 |
| Vifaa vya Usafiri | 5.4 | 4.3 | 3.5 | 3.6 | 3.5 | 3.8 |
| Mitambo na Vifaa | 10.3 | 9.8 | 9.3 | 6.9 | 6.3 | 7.3 |
| Aina nyingine za Mitambo na Vifaa | 3.8 | 3.9 | 3.6 | 3.4 | 3.2 | 3.6 |
| Rasilimali za Mazao ya Mifugo | 1.2 | 1.2 | 1.1 | 1.0 | 1.0 | 1.1 |
| Haki ya Umiliki, Utafiti na Maendeleo na Huduma za Kitaalamu | 2.8 | 3.0 | 3.0 | 2.7 | 2.6 | 2.9 |
| Rasilimali za kudumu | 97.3 | 101.8 | 104.2 | 101.8 | 106.6 | 108.1 |
| Ongezeko la limbikizo la Vito vya Thamani | 2.9 | 3.2 | 2.5 | 2.5 | 2.3 | 3.1 |
| Ongezeko la limbikizo | -0.2 | -5.0 | -6.7 | -4.3 | -8.9 | -11.2 |
| **Jumla ya Ukuzaji Rasilimali** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

## UKUZAJI WA RASILIMALI KATIKA SEHEMU ZA UCHUMI WA KITAIFA NA BINAFSI
**(Bei za Miaka Inayohusika)**

Jedwali Na. 7B — Sh. Milioni

| Sekta | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| A. Rasilimali za kudumu | 30,070,195 | 35,492,828 | 42,141,921 | 50,387,086 | 59,440,540 | 64,049,913 |
| 1. Serikali: | 7,219,843 | 8,944,186 | 10,914,757 | 13,124,780 | 14,979,006 | 16,588,928 |
| 2. Mashirika: | 589,169 | 745,349 | 1,011,406 | 1,106,303 | 1,248,250 | 1,537,198 |
| 3. Taasisi: | 812,232 | 851,827 | 1,095,690 | 1,056,017 | 1,426,572 | 1,665,298 |
| 4. Sekta binafsi | 21,448,950 | 24,951,465 | 29,120,067 | 35,099,986 | 41,786,712 | 44,258,490 |
| C: Ongezeko la limbikizo la Vito vya Thamani | 903,043 | 1,105,406 | 1,006,179 | 1,215,104 | 1,273,337 | 1,838,290 |
| D. Ongezeko la Limbikizo | -65,636 | -1,732,887 | -2,720,674 | -2,108,634 | -4,951,512 | -6,652,837 |
| **E. Jumla la Ukuzaji Rasilimali** | **30,907,602** | **34,865,346** | **40,427,427** | **49,493,556** | **55,762,365** | **59,235,366** |

**Chanzo**: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**FAHIRISI ZA BEI ZA REJAREJA ZA BIDHAA ZITUMIWAZO NA WATU WA KIPATO CHA CHINI DAR-ES-SALAAM (Des.2015=100)**

Jedwali Na.8

| Mwaka | Bidhaa zote | | Chakula | |
|---|---|---|---|---|
| | Fahirisi | Badiliko Asilimia | Fahirisi | Badiliko Asilimia |
| 2003 | 28.4 | 5.8 | 26.3 | 5.4 |
| 2004 | 30.2 | 6.4 | 28.1 | 6.8 |
| 2005 | 32.7 | 8.3 | 30.1 | 7.3 |
| 2006 | 36.5 | 11.5 | 33.2 | 10.3 |
| 2007 | 39.9 | 9.3 | 36.3 | 9.3 |
| 2008 | 46.8 | 17.3 | 41.9 | 15.2 |
| 2009 | 54.7 | 16.8 | 50.0 | 19.4 |
| 2010 | 61.9 | 13.2 | 59.0 | 18.0 |
| 2011 | 66.5 | 7.4 | 63.2 | 7.1 |
| 2012 | 79.0 | 18.8 | 77.8 | 23.2 |
| 2013 | 86.3 | 9.3 | 86.0 | 10.5 |
| 2014 | 93.0 | 7.7 | 92.2 | 7.3 |
| 2015* | 98.0 | 5.4 | 97.7 | 5.9 |
| 2016 | 102.2 | 4.3 | 101.2 | 3.6 |
| 2017 | 104.1 | 1.9 | 104.7 | 3.4 |
| 2018 | 106.1 | 2.0 | 109.4 | 4.5 |
| 2019 | 110.1 | 3.8 | 114.4 | 4.6 |
| 2020 | 112.4 | 2.1 | 115.6 | 1.1 |

**Chanzo**: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

*Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika Des. 2015=100

## FAHIRISI ZA BEI ZA REJA REJA ZA BIDHAA ZITUMIKAZO NA WATU WA KIPATO CHA CHINI DAR ES SALAAM (2001= 100)

Jedwali Na.9

| Mwaka | Chakula | Vinywaji na Sigara | Kodi ya Nyumba | Umeme, Mafuta ya Taa, Maji | Nguo na Viatu | Fenicha, Vyombo Vya Ny-umbani | Huduma Mahitaji ya Nyumbani | Huduma za Afya | Michezo na Starehe | Usafiri | Elimu | Vingine vyo | Fahirisi Bidhaa Zote |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2004 | 123.5 | 122.9 | 100.0 | 142.0 | 97.2 | 137.4 | 80.5 | 85.1 | 99.4 | 104.1 | 191.1 | 123.0 | 121.9 |
| 2005 | 125.7 | 120.0 | 113.6 | 162.3 | 108.7 | 115.7 | 110.0 | 113.6 | 110.4 | 109.8 | 115.0 | 121.1 | 126.5 |
| 2006 | 138.6 | 141.8 | 132.8 | 193.7 | 108.0 | 115.4 | 109.6 | 118.8 | 113.5 | 134.0 | 93.3 | 139.3 | 126.1 |
| 2007 | 151.5 | 159.5 | 146.1 | 209.1 | 124.1 | 131.7 | 119.1 | 114.8 | 148.5 | 114.9 | 104.0 | 128.4 | 154.2 |
| 2008 | 174.6 | 175.1 | 199.3 | 269.8 | 139.3 | 160.5 | 138.4 | 134.0 | 110.8 | 179.5 | 99.2 | 137.2 | 180.9 |
| 2009 | 208.5 | 210.8 | 206.6 | 276.6 | 152.8 | 173.3 | 167.1 | 163.8 | 124.7 | 225.9 | 111.3 | 147.7 | 211.3 |

**FAHIRISI ZA BEI ZA REJA REJA ZA BIDHAA ZITUMIWAZO NA WATU WA KIPATO CHA CHINI DAR ES SALAAM (Des. 2015 = 100)**

| Mwaka | Vyakula na vinywaji baridi | Vinywaji vyenye kilevi na bidhaa za tumbaku | Mavazi ya nguo na viatu | Nishati, Maji na Makazi | Samani, vifaa vya nyumbani na ukarabati wa nyumba | Gharam a za Afya | Usafirishaji | Mawasiliano | Utamaduni na Burudani | Elimu | Hoteli na Migahawa | Bidhaa na huduma nyinginezo | Fahirisi Bidhaa Zote |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2013 | 85.98 | 75.34 | 85.60 | 88.69 | 88.81 | 90.62 | 86.32 | 100.00 | 90.84 | 102.73 | 85.16 | 84.36 | 86.34 |
| 2014 | 92.22 | 81.64 | 93.45 | 94.93 | 92.39 | 91.24 | 100.08 | 100.00 | 94.70 | 102.72 | 91.76 | 94.05 | 92.95 |
| 2015* | 97.67 | 93.26 | 101.90 | 98.12 | 97.91 | 96.35 | 99.91 | 100.00 | 100.00 | 102.40 | 98.24 | 96.61 | 97.97 |
| 2016 | 101.19 | 100.89 | 99.41 | 105.13 | 100.55 | 108.05 | 100.84 | 100.57 | 101.22 | 97.07 | 104.92 | 102.41 | 102.21 |
| 2017 | 104.67 | 103.85 | 100.71 | 106.08 | 103.70 | 109.73 | 100.74 | 100.95 | 102.92 | 100.84 | 105.48 | 103.38 | 104.10 |
| 2018 | 109.36 | 103.85 | 103.87 | 112.15 | 105.67 | 109.80 | 88.19 | 100.86 | 104.08 | 106.36 | 105.60 | 105.01 | 106.15 |
| 2019 | 114.38 | 104.67 | 107.98 | 118.42 | 107.72 | 113.26 | 92.54 | 101.84 | 106.52 | 106.25 | 107.91 | 107.62 | 110.13 |
| 2020 | 115.62 | 104.69 | 109.30 | 129.54 | 108.35 | 114.26 | 92.33 | 102.06 | 106.37 | 106.12 | 108.61 | 107.93 | 112.39 |

**Chanzo**: Ofisi yaTaifa ya Takwimu

NB. Wastani (Average) wa mwaka (kuanzia mwaka 2003, Fahirisi (Index) imekuwa ikitolewa kila mwezi katika miezi yote 12 ya mwaka

*Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika Des. 2015=100

Fahirisi za Bei kuanzia mwaka 2005 hadi 2009 zilitumia mgawanyo wa makundi kwa tafsiri ya Kitaifa (National Classification) hivyo fahirisi hizi haziwezi kuungwa na fahirisi zilizonzia mwaka 2010 zilizotumia mgawanyo wa makundi kwa mfumo wa kimataifa wa COICOP

## FAHIRISI YA BEI YA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WAFANYAKAZI WA KIMA CHA KATI - DAR-ES-SALAAM (Des. 2015 =100)

Jedwali Na.10

| Mwaka | Robo ya Kwanza | Robo ya Pili | Robo ya Tatu | Robo ya Nne | Wastani | Badiliko Asilimia |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2003 | 30.4 | 30.4 | 30.9 | 31.7 | 30.8 | 2.3 |
| 2004 | 32.8 | 33.1 | 33.5 | 34.2 | 33.4 | 8.2 |
| 2005 | 34.9 | 35.3 | 36.7 | 37.3 | 36.0 | 7.9 |
| 2006 | 38.3 | 39.4 | 39.5 | 40.2 | 39.3 | 9.2 |
| 2007 | 41.7 | 43.3 | 44.4 | 46.0 | 43.9 | 11.5 |
| 2008 | 48.5 | 49.9 | 51.2 | 52.7 | 50.6 | 15.3 |
| 2009 | 55.7 | 57.3 | 60.3 | 62.3 | 58.9 | 16.4 |
| 2010 | 63.9 | 64.6 | 65.1 | 65.6 | 64.8 | 10.0 |
| 2011 | 67.9 | 69.3 | 70.3 | 72.1 | 69.9 | 7.9 |
| 2012 | 78.4 | 81.6 | 82.7 | 83.4 | 81.5 | 16.6 |
| 2013 | 87.6 | 88.6 | 88.5 | 88.4 | 88.3 | 8.3 |
| 2014 | 92.8 | 94.2 | 94.5 | 93.5 | 93.7 | 6.2 |
| 2015* | 96.5 | 98.9 | 100.6 | 100.0 | 99.0 | 5.6 |
| 2016 | 102.1 | 104.3 | 103.8 | 103.8 | 103.5 | 4.5 |
| 2017 | 104.5 | 106.7 | 106.7 | 107.0 | 106.2 | 2.6 |
| 2018 | 105.7 | 108.5 | 108.7 | 109.8 | 108.2 | 1.9 |
| 2019 | 111.9 | 113.5 | 113.0 | 114.0 | 113.1 | 4.5 |
| 2020 | 116.9 | 117.0 | 117.3 | 116.9 | 117.0 | 3.5 |

**Chanzo**: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

*Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika Des. 2015=100

## FAHIRISI YA BEI ZA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WAFANYAKAZI WA KIMA CHA KATI DAR ES SALAAM (DES. 2015=100)

Jedwali Na.11

| Mwaka | | Vyakula na vinywaji baridi | Vinywaji vyenye kilevi na bidhaa za tumbaku | Mavazi ya nguo na viatu | Nishati, Maji na Makazi | Samani, vifaa vya nyumbani na ukarabati wa nyumba | Gharama za Afya | Usafirishaji | Mawasiliano | Utamaduni na Burudani | Elimu | Hoteli na Migahawa | Bidhaa na huduma nyinginezo | FAHIRISI BIDHAA ZOTE |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2013 | Robo ya kwanza | 94.6 | 82.5 | 94.0 | 70.7 | 90.1 | 90.0 | 78.0 | 98.7 | 90.0 | 83.5 | 80.0 | 85.4 | 87.6 |
| | Robo ya pili | 94.6 | 83.5 | 94.7 | 73.7 | 90.4 | 90.1 | 83.6 | 99.0 | 90.8 | 84.2 | 80.7 | 86.0 | 88.6 |
| | Robo ya tatu | 92.7 | 86.2 | 95.6 | 76.2 | 90.8 | 91.3 | 88.0 | 99.2 | 91.5 | 85.9 | 81.6 | 88.2 | 88.5 |
| | Robo ya nne | 91.7 | 88.0 | 95.7 | 77.5 | 91.3 | 91.7 | 89.5 | 99.2 | 92.2 | 86.8 | 82.5 | 88.8 | 88.4 |
| 2014 | Robo ya kwanza | 98.1 | 88.8 | 96.0 | 80.3 | 92.1 | 92.2 | 93.5 | 99.3 | 92.6 | 91.8 | 83.5 | 90.2 | 92.8 |
| | Robo ya pili | 99.1 | 89.0 | 96.6 | 82.8 | 93.2 | 94.8 | 94.2 | 99.5 | 93.2 | 94.3 | 85.8 | 90.6 | 94.2 |
| | Robo ya tatu | 97.3 | 92.9 | 97.3 | 86.8 | 96.7 | 97.0 | 96.3 | 100.0 | 95.0 | 95.9 | 88.0 | 93.6 | 94.5 |
| | Robo ya nne | 93.7 | 97.0 | 98.0 | 89.6 | 99.0 | 97.8 | 97.7 | 100.0 | 97.2 | 95.9 | 90.5 | 95.7 | 93.5 |
| 2015* | Robo ya kwanza | 97.3 | 97.9 | 98.5 | 93.4 | 99.6 | 97.8 | 98.6 | 100.2 | 97.2 | 99.0 | 93.8 | 96.0 | 96.5 |
| | Robo ya pili | 100.1 | 98.1 | 98.9 | 96.7 | 99.3 | 97.8 | 99.3 | 100.3 | 97.3 | 99.9 | 96.4 | 96.6 | 98.9 |
| | Robo ya tatu | 101.8 | 98.9 | 99.0 | 99.4 | 99.4 | 98.4 | 100.5 | 100.2 | 98.2 | 100.0 | 98.0 | 96.7 | 100.6 |
| | Robo ya nne | 100.4 | 100.0 | 99.8 | 99.5 | 99.9 | 99.6 | 100.1 | 100.0 | 100.1 | 100.0 | 99.0 | 99.2 | 100.0 |
| 2016 | Robo ya kwanza | 101.81 | 100.94 | 99.84 | 108.37 | 99.89 | 106.44 | 99.44 | 100.00 | 100.34 | 97.77 | 100.70 | 101.37 | 102.05 |
| | Robo ya pili | 104.35 | 100.23 | 100.67 | 111.35 | 101.13 | 111.18 | 99.79 | 100.65 | 100.98 | 97.34 | 105.93 | 102.20 | 104.35 |
| | Robo ya tatu | 103.90 | 101.28 | 99.83 | 107.36 | 100.24 | 113.92 | 100.57 | 101.22 | 101.05 | 97.34 | 106.92 | 102.16 | 103.81 |
| | Robo ya nne | 102.52 | 102.55 | 100.25 | 110.34 | 102.43 | 114.81 | 99.94 | 101.34 | 101.94 | 97.34 | 105.83 | 103.52 | 103.79 |
| 2017 | Robo ya kwanza | 105.73 | 103.07 | 100.93 | 105.30 | 104.32 | 114.49 | 101.20 | 101.35 | 101.16 | 97.34 | 106.10 | 102.99 | 104.48 |
| | Robo ya pili | 110.22 | 103.61 | 101.49 | 108.85 | 104.02 | 114.00 | 102.03 | 101.35 | 101.70 | 97.34 | 105.91 | 103.44 | 106.72 |
| | Robo ya tatu | 107.86 | 103.86 | 101.84 | 115.20 | 104.13 | 114.10 | 99.40 | 101.34 | 101.41 | 97.34 | 106.27 | 103.89 | 106.65 |
| | Robo ya nne | 107.75 | 103.85 | 101.95 | 117.53 | 104.36 | 114.48 | 99.98 | 101.28 | 101.91 | 97.34 | 106.27 | 103.25 | 107.02 |
| 2018 | Robo ya kwanza | 111.38 | 103.06 | 101.58 | 112.37 | 104.56 | 114.41 | 80.57 | 101.28 | 101.05 | 105.74 | 104.96 | 103.43 | 105.75 |
| | Robo ya pili | 117.46 | 103.06 | 102.80 | 114.81 | 105.34 | 114.57 | 80.87 | 101.18 | 101.75 | 105.74 | 104.97 | 104.92 | 108.50 |
| | Robo ya tatu | 116.84 | 103.06 | 104.34 | 116.35 | 105.73 | 114.65 | 81.26 | 101.12 | 101.55 | 105.74 | 105.55 | 105.35 | 108.73 |
| | Robo ya nne | 115.96 | 103.21 | 106.12 | 121.73 | 106.68 | 114.80 | 84.15 | 101.17 | 102.12 | 105.74 | 106.91 | 106.24 | 109.82 |
| 2019 | Robo ya kwanza | 119.35 | 103.50 | 106.54 | 123.10 | 107.69 | 118.59 | 85.96 | 102.55 | 103.36 | 105.74 | 108.48 | 107.91 | 111.91 |
| | Robo ya pili | 123.24 | 103.50 | 107.13 | 122.92 | 107.94 | 120.09 | 86.49 | 103.03 | 103.56 | 105.74 | 108.62 | 108.00 | 113.48 |
| | Robo ya tatu | 121.21 | 103.50 | 107.82 | 124.54 | 107.77 | 120.10 | 86.49 | 102.29 | 104.49 | 105.74 | 108.59 | 107.40 | 112.96 |
| | Robo ya nne | 123.84 | 103.50 | 107.79 | 125.41 | 108.11 | 120.21 | 86.11 | 102.45 | 103.13 | 105.74 | 108.15 | 107.64 | 113.96 |
| 2020 | Robo ya kwanza | 129.28 | 103.50 | 108.53 | 131.29 | 108.35 | 120.24 | 86.38 | 102.69 | 103.41 | 105.71 | 108.16 | 107.21 | 116.89 |
| | Robo ya pili | 127.07 | 103.50 | 108.65 | 138.02 | 108.42 | 120.64 | 84.99 | 103.32 | 103.43 | 105.71 | 108.16 | 107.85 | 117.03 |
| | Robo ya tatu | 126.63 | 103.50 | 108.64 | 139.25 | 108.47 | 120.73 | 85.17 | 103.32 | 103.46 | 105.71 | 110.24 | 108.26 | 117.35 |
| | Robo ya nne | 126.71 | 104.11 | 108.95 | 135.44 | 108.46 | 120.73 | 85.78 | 103.32 | 103.47 | 105.71 | 110.24 | 108.54 | 116.91 |

**Chanzo**: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

*Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika Des. 2015=100

Fahirisi za Bei kuanzia mwaka 2004 hadi 2009 zilitumia mgawanyo wa makundi kwa tafsiri ya Kitaifa (National Classification) hivyo fahirisi hizi haziwezi kuungwa na fahirisi zilizonzia mwaka 2010 zilizotumia mgawanyo wa makundi kwa mfumo wa kimataifa wa COICOP

**FAHIRISI YA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WATU WENYE KIPATO CHA JUU DAR ES SALAAM (Des. 2015=100)**

Jedwali Na.12

| Mwaka | Vyakula na vinywaji baridi | Vinywaji vyenye kilevi na bidhaa za tumbaku | Mavazi ya nguo na viatu | Nishati, Maji na Makazi | Samani, vifaa vya nyumbani na ukarabati wa nyumba | Gharama za Afya | Usafirishaji | Mawasiliano | Utamaduni na Burudani | Elimu | Hoteli na Migahawa | Bidhaa na huduma nyinginezo | FAHIRISI BIDHAA ZOTE |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2013 Robo ya kwanza | 83.1 | 81.4 | 93.8 | 83.9 | 96.1 | 94.8 | 86.4 | 95.5 | 93.9 | 84.4 | 84.9 | 96.4 | 85.5 |
| Robo ya pili | 81.7 | 82.1 | 95.2 | 83.4 | 96.3 | 94.8 | 94.1 | 95.7 | 96.1 | 84.4 | 85.3 | 96.8 | 85.6 |
| Robo ya tatu | 82.8 | 87.7 | 96.3 | 84.3 | 97.1 | 94.8 | 95.6 | 95.7 | 96.3 | 84.4 | 85.8 | 97.2 | 86.6 |
| Robo ya nne | 84.2 | 90.4 | 96.4 | 86.4 | 97.7 | 94.8 | 96.2 | 95.7 | 96.0 | 84.7 | 87.4 | 97.2 | 87.9 |
| 2014Robo ya kwanza | 88.5 | 90.4 | 97.5 | 87.6 | 97.7 | 95.5 | 96.6 | 95.7 | 98.8 | 95.7 | 87.9 | 99.0 | 90.6 |
| Robo ya pili | 87.9 | 90.4 | 97.6 | 88.1 | 98.5 | 97.7 | 97.6 | 95.7 | 98.9 | 98.6 | 88.0 | 99.8 | 90.7 |
| Robo ya tatu | 88.0 | 92.9 | 97.5 | 92.7 | 97.8 | 97.5 | 98.7 | 95.7 | 99.3 | 98.6 | 90.4 | 101.2 | 91.8 |
| Robo ya nne | 89.7 | 95.6 | 97.3 | 95.1 | 98.2 | 97.3 | 99.3 | 95.6 | 99.8 | 98.6 | 92.5 | 99.9 | 93.3 |
| 2015*Robo ya kwanza | 92.5 | 96.7 | 97.8 | 95.2 | 98.3 | 97.5 | 101.2 | 97.6 | 99.7 | 100.0 | 95.4 | 100.2 | 95.1 |
| Robo ya pili | 95.1 | 98.1 | 97.8 | 96.0 | 98.2 | 97.5 | 102.5 | 97.7 | 100.0 | 100.0 | 97.5 | 98.6 | 96.8 |
| Robo ya tatu | 97.6 | 99.0 | 98.5 | 97.1 | 98.7 | 98.4 | 102.6 | 98.5 | 100.2 | 100.0 | 97.5 | 98.7 | 98.3 |
| Robo ya nne | 100.0 | 99.6 | 99.3 | 101.1 | 99.6 | 99.3 | 99.9 | 100.0 | 100.1 | 100.0 | 98.4 | 99.6 | 100.0 |
| 2016Robo ya kwanza | 102.6 | 100.4 | 99.8 | 105.2 | 100.2 | 107.3 | 98.6 | 100.0 | 100.4 | 98.6 | 100.4 | 101.4 | 101.0 |
| Robo ya pili | 105.3 | 100.9 | 100.7 | 107.2 | 103.0 | 111.9 | 98.9 | 100.6 | 101.3 | 98.4 | 103.1 | 102.0 | 102.5 |
| Robo ya tatu | 106.0 | 102.3 | 99.7 | 104.3 | 100.1 | 114.0 | 99.7 | 101.2 | 101.0 | 98.4 | 102.9 | 102.7 | 102.4 |
| Robo ya nne | 104.4 | 102.8 | 100.2 | 106.9 | 104.4 | 115.0 | 99.8 | 101.3 | 101.9 | 98.4 | 102.4 | 105.0 | 102.8 |
| 2017 Robo ya kwanza | 107.4 | 102.9 | 101.3 | 105.5 | 107.3 | 115.2 | 101.7 | 101.3 | 100.1 | 98.4 | 102.5 | 105.3 | 104.0 |
| Robo ya pili | 112.6 | 103.8 | 102.0 | 105.8 | 107.7 | 114.7 | 103.2 | 101.3 | 100.6 | 98.4 | 103.1 | 105.4 | 105.8 |
| Robo ya tatu | 116.9 | 104.1 | 102.1 | 107.7 | 107.3 | 114.2 | 104.8 | 101.3 | 99.4 | 98.4 | 103.4 | 106.3 | 107.4 |
| Robo ya nne | 119.9 | 104.1 | 102.4 | 110.0 | 107.2 | 115.2 | 106.8 | 101.5 | 99.8 | 98.4 | 103.0 | 107.3 | 108.9 |
| 2018 Robo ya kwanza | 120.6 | 104.1 | 102.8 | 110.4 | 107.6 | 115.1 | 107.8 | 101.7 | 100.4 | 101.4 | 103.0 | 105.2 | 109.5 |
| Robo ya pili | 121.9 | 104.1 | 103.9 | 112.9 | 108.6 | 115.1 | 110.4 | 101.8 | 100.9 | 107.6 | 103.2 | 106.6 | 111.2 |
| Robo ya tatu | 123.3 | 103.8 | 105.2 | 113.8 | 108.9 | 115.0 | 111.6 | 101.8 | 101.3 | 107.6 | 103.9 | 107.5 | 112.1 |
| Robo ya nne | 122.9 | 103.8 | 105.9 | 115.9 | 109.2 | 114.9 | 113.4 | 101.8 | 100.7 | 107.6 | 106.1 | 107.7 | 113.0 |
| 2019 Robo ya kwanza | 124.8 | 103.9 | 106.1 | 116.4 | 110.4 | 118.4 | 113.5 | 103.3 | 101.3 | 107.6 | 108.2 | 107.7 | 113.9 |
| Robo ya pili | 128.5 | 103.9 | 106.8 | 123.5 | 110.8 | 120.1 | 114.4 | 103.8 | 101.8 | 107.6 | 108.3 | 107.7 | 116.0 |
| Robo ya tatu | 127.5 | 103.9 | 107.4 | 124.5 | 110.6 | 120.0 | 114.1 | 103.0 | 102.5 | 107.6 | 107.5 | 107.3 | 115.7 |
| Robo ya nne | 129.4 | 103.9 | 107.5 | 125.4 | 110.9 | 120.1 | 113.6 | 103.2 | 100.7 | 107.6 | 107.8 | 105.9 | 116.1 |
| 2020 Robo ya kwanza | 136.7 | 103.9 | 108.3 | 128.0 | 111.1 | 120.1 | 113.9 | 103.4 | 101.4 | 107.5 | 108.0 | 105.6 | 118.2 |
| Robo ya pili | 136.1 | 103.9 | 108.4 | 131.7 | 111.2 | 120.5 | 111.1 | 104.1 | 101.4 | 107.5 | 108.0 | 107.1 | 117.9 |
| Robo ya tatu | 137.2 | 103.9 | 108.4 | 132.6 | 111.3 | 120.5 | 111.1 | 104.1 | 101.5 | 107.5 | 109.3 | 107.4 | 118.3 |
| Robo ya nne | 139.0 | 104.8 | 108.6 | 130.5 | 111.3 | 120.5 | 111.3 | 104.1 | 101.5 | 107.5 | 109.3 | 107.5 | 118.5 |

**Chanzo**: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

*Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika Des. 2015=100

Fahirisi za Bei kuanzia mwaka 2004 hadi 2009 zilitumia mgawanyo wa makundi kwa tafsiri ya Kitaifa (National Classification) hivyo fahirisi hizi haziwezi kuungwa na fahirisi zilizonzia mwaka 2010 zilizotumia mgawanyo wa makundi kwa mfumo wa kimataifa wa COICOP

## FAHIRISI YA GHARAMA YA MAISHA YA WATU WENYE KIPATO CHA JUU DAR-ES-SALAAM (Des. 2015=100)

Jedwali Na. 13

| Mwaka | Miezi | | | | Wastani | Badiliko |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Machi | Juni | Sept. | Desemba | | Asilimia |
| 2003 | 29.92 | 30.22 | 30.19 | 30.24 | 30.14 | 4.2 |
| 2004 | 30.98 | 31.77 | 32.30 | 33.02 | 32.02 | 6.2 |
| 2005 | 33.62 | 33.88 | 34.76 | 36.80 | 34.77 | 8.6 |
| 2006 | 37.88 | 38.51 | 38.90 | 40.13 | 38.86 | 11.8 |
| 2007 | 42.19 | 43.45 | 44.68 | 45.76 | 44.02 | 13.3 |
| 2008 | 48.86 | 50.13 | 53.91 | 55.41 | 52.08 | 18.3 |
| 2009 | 57.72 | 58.40 | 61.62 | 63.21 | 60.24 | 15.7 |
| 2010 | 63.41 | 64.89 | 65.82 | 66.29 | 65.10 | 8.1 |
| 2011 | 68.73 | 70.77 | 72.83 | 75.67 | 72.00 | 10.6 |
| 2012 | 78.04 | 79.50 | 80.40 | 82.20 | 80.04 | 11.2 |
| 2013 | 85.48 | 85.58 | 86.64 | 87.93 | 86.41 | 8.0 |
| 2014 | 90.61 | 90.68 | 91.84 | 93.27 | 91.60 | 6.0 |
| 2015* | 95.14 | 96.78 | 98.27 | 100.00 | 97.55 | 6.5 |
| 2016 | 101.02 | 102.52 | 102.43 | 102.81 | 102.20 | 4.8 |
| 2017 | 104.01 | 105.76 | 107.37 | 108.93 | 106.52 | 4.2 |
| 2018 | 109.52 | 111.24 | 112.15 | 113.00 | 111.48 | 4.7 |
| 2019 | 113.92 | 115.99 | 115.74 | 116.09 | 115.44 | 3.6 |
| 2020 | 118.15 | 117.85 | 118.31 | 118.52 | 118.21 | 2.4 |

**Chanzo**: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

*Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika Des. 2015=100

**FAHIRISI YA BEI YA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WAKAZI WA MIJINI - TANZANIA BARA (Des. 2015=100)**

Jedwali Na.14

| Mwaka | | Vyakula na vinywaji baridi | Vinywaji vyenye kilevi na bidhaa za tumbaku | Mavazi ya nguo na viatu | Nishati, Maji na Makazi | Samani, vifaa vya nyumbani na ukarabati wa nyumba | Gharama za Afya | Usafirishaji | Mawasiliano | Utamaduni na Burudani | Elimu | Hoteli na Migahawa | Bidhaa na huduma nyingine zo | FAHIRISI BIDHAA ZOTE |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2013 | Robo ya kwanza | 83.4 | 87.6 | 90.5 | 86.1 | 94.4 | 91.0 | 90.7 | 98.7 | 95.6 | 91.7 | 91.8 | 88.6 | 86.7 |
| | Robo ya pili | 82.9 | 88.3 | 91.2 | 90.1 | 94.6 | 91.7 | 96.1 | 98.5 | 96.0 | 91.9 | 92.2 | 89.4 | 87.3 |
| | Robo ya tatu | 81.6 | 92.4 | 92.3 | 90.7 | 95.0 | 91.9 | 97.8 | 99.0 | 96.4 | 92.1 | 92.3 | 90.9 | 86.9 |
| | Robo ya nne | 83.7 | 93.5 | 92.8 | 92.0 | 95.6 | 92.0 | 98.4 | 99.1 | 96.4 | 92.1 | 92.9 | 91.7 | 88.4 |
| 2014 | Robo ya kwanza | 88.9 | 93.8 | 93.8 | 96.8 | 96.1 | 92.8 | 98.8 | 99.2 | 96.6 | 96.8 | 93.3 | 92.6 | 91.9 |
| | Robo ya pili | 89.7 | 93.8 | 94.1 | 98.7 | 96.8 | 95.2 | 99.4 | 99.5 | 96.7 | 96.8 | 94.5 | 96.6 | 92.9 |
| | Robo ya tatu | 88.6 | 96.8 | 94.5 | 100.5 | 96.9 | 95.8 | 100.0 | 99.9 | 96.9 | 96.8 | 95.2 | 96.6 | 92.7 |
| | Robo ya nne | 89.2 | 98.6 | 95.5 | 101.1 | 96.9 | 96.2 | 99.6 | 99.7 | 97.0 | 96.8 | 96.1 | 96.7 | 93.3 |
| 2015* | Robo ya kwanza | 93.5 | 98.8 | 97.0 | 101.6 | 97.4 | 96.6 | 97.5 | 99.8 | 97.1 | 98.6 | 97.6 | 97.4 | 95.7 |
| | Robo ya pili | 97.3 | 98.8 | 97.8 | 99.8 | 97.4 | 97.1 | 97.6 | 99.8 | 97.5 | 100.0 | 98.9 | 97.8 | 97.8 |
| | Robo ya tatu | 97.5 | 99.4 | 99.1 | 101.1 | 98.7 | 98.4 | 100.3 | 99.7 | 98.9 | 100.0 | 99.8 | 98.5 | 98.5 |
| | Robo ya nne | 98.9 | 99.8 | 99.7 | 100.9 | 99.3 | 99.5 | 99.8 | 100.0 | 100.1 | 100.0 | 100.0 | 99.8 | 99.4 |
| 2016 | Robo ya kwanza | 102.1 | 100.4 | 101.0 | 103.8 | 100.5 | 101.6 | 99.1 | 99.5 | 100.4 | 101.8 | 100.5 | 100.8 | 101.4 |
| | Robo ya pili | 104.2 | 103.2 | 101.9 | 107.3 | 101.5 | 103.2 | 98.9 | 98.8 | 100.9 | 102.3 | 103.6 | 101.4 | 103.0 |
| | Robo ya tatu | 103.9 | 104.4 | 102.8 | 107.8 | 101.9 | 104.0 | 99.8 | 99.1 | 101.2 | 102.6 | 104.4 | 101.9 | 103.3 |
| | Robo ya nne | 105.1 | 104.9 | 103.3 | 110.1 | 103.1 | 104.6 | 100.0 | 99.1 | 101.7 | 102.6 | 104.1 | 102.6 | 104.2 |
| 2017 | Robo ya kwanza | 111.4 | 105.5 | 104.4 | 112.5 | 104.2 | 105.3 | 100.0 | 98.7 | 101.5 | 102.9 | 104.3 | 103.4 | 107.1 |
| | Robo ya pili | 115.7 | 106.5 | 105.8 | 113.6 | 104.7 | 105.8 | 100.1 | 98.1 | 102.0 | 103.1 | 104.4 | 105.5 | 109.1 |
| | Robo ya tatu | 113.2 | 107.0 | 106.4 | 116.7 | 104.8 | 106.2 | 99.5 | 98.1 | 102.7 | 103.4 | 104.4 | 105.7 | 108.6 |
| | Robo ya nne | 112.9 | 107.5 | 106.5 | 118.8 | 105.1 | 106.7 | 100.1 | 98.1 | 103.2 | 103.5 | 104.5 | 105.4 | 108.9 |
| 2018 | Robo ya kwanza | 117.4 | 107.9 | 107.6 | 122.3 | 106.1 | 107.0 | 101.2 | 98.2 | 103.1 | 105.5 | 105.2 | 105.7 | 111.4 |
| | Robo ya pili | 119.4 | 107.6 | 108.3 | 128.7 | 107.1 | 107.3 | 101.9 | 97.3 | 102.8 | 105.6 | 105.3 | 106.8 | 113.1 |
| | Robo ya tatu | 115.9 | 108.4 | 109.4 | 131.4 | 107.8 | 107.5 | 102.4 | 95.5 | 102.7 | 106.0 | 105.7 | 107.0 | 112.2 |
| | Robo ya nne | 113.9 | 109.6 | 110.2 | 134.4 | 108.5 | 107.7 | 104.5 | 95.5 | 102.6 | 106.0 | 106.7 | 107.5 | 112.3 |
| 2019 | Robo ya kwanza | 118.0 | 110.8 | 111.4 | 137.4 | 110.4 | 108.6 | 105.0 | 96.3 | 103.3 | 107.5 | 109.1 | 108.6 | 114.7 |
| | Robo ya pili | 121.5 | 111.5 | 112.0 | 141.2 | 111.6 | 109.5 | 106.1 | 96.9 | 105.3 | 107.7 | 110.4 | 109.5 | 117.0 |
| | Robo ya tatu | 119.9 | 110.9 | 112.3 | 139.6 | 111.9 | 109.5 | 105.8 | 96.3 | 104.6 | 107.7 | 110.5 | 109.6 | 116.2 |
| | Robo ya nne | 120.5 | 110.7 | 112.7 | 139.6 | 112.2 | 109.5 | 105.8 | 96.4 | 104.1 | 107.7 | 110.7 | 109.7 | 116.4 |
| 2020 | Robo ya kwanza | 124.6 | 110.8 | 113.7 | 143.8 | 112.8 | 109.5 | 107.1 | 96.8 | 104.4 | 108.9 | 111.1 | 110.1 | 118.9 |
| | Robo ya pili | 126.7 | 111.3 | 114.5 | 151.8 | 113.6 | 110.0 | 107.0 | 97.1 | 104.8 | 109.0 | 111.3 | 110.5 | 120.8 |
| | Robo ya tatu | 124.3 | 111.1 | 114.7 | 151.9 | 113.8 | 110.5 | 107.2 | 96.7 | 104.9 | 109.0 | 112.5 | 110.4 | 120.0 |
| | Robo ya nne | 124.2 | 110.2 | 115.1 | 152.4 | 113.8 | 110.6 | 107.3 | 96.8 | 104.8 | 109.1 | 112.6 | 110.4 | 120.0 |

**Chanzo**: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

*Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika Des. 2015=100

Fahirisi za Bei kuanzia mwaka 2005 hadi 2009 zilitumia mgawanyo wa makundi kwa tafsiri ya Kitaifa (National Classification) hivyo fahirisi hizi haziwezi kuungwa na fahirisi zilizonzia mwaka 2010 zilizotumia mgawanyo wa makundi kwa mfumo wa kimataifa wa COICOP

## FAHIRISI YA BEI YA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WAKAZI WA MIJINI TANZANIA BARA (Des 2015=100)

Jedwali Na.15

| Mwaka | Robo ya Mwaka | | | | Wastani wa Fahirisi | Badiliko Asilimia |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Robo ya Kwanza | Robo ya Pili | Robo ya Tatu | Robo ya Nne | | |
| 2003 | 37.1 | 37.6 | 37.4 | 38.3 | 37.6 | 5.3 |
| 2004 | 39.0 | 39.0 | 39.1 | 40.4 | 39.4 | 4.7 |
| 2005 | 40.6 | 41.2 | 41.3 | 42.4 | 41.4 | 5.0 |
| 2006 | 43.8 | 44.9 | 43.7 | 45.1 | 44.4 | 7.3 |
| 2007 | 46.9 | 47.5 | 47.4 | 48.2 | 47.5 | 7.0 |
| 2008 | 51.1 | 51.9 | 52.3 | 54.2 | 52.4 | 10.3 |
| 2009 | 57.7 | 57.8 | 58.4 | 61.0 | 58.7 | 12.1 |
| 2010 | 61.3 | 62.1 | 61.9 | 62.4 | 61.9 | 5.5 |
| 2011 | 65.8 | 68.2 | 71.0 | 74.2 | 69.8 | 12.7 |
| 2012 | 78.6 | 80.5 | 81.4 | 83.4 | 81.0 | 16.0 |
| 2013 | 86.7 | 87.3 | 86.9 | 88.4 | 87.3 | 7.9 |
| 2014 | 91.9 | 92.9 | 92.7 | 93.3 | 92.7 | 6.1 |
| 2015* | 95.7 | 97.8 | 98.5 | 99.4 | 97.9 | 5.6 |
| 2016 | 101.4 | 103.0 | 103.3 | 104.2 | 102.9 | 5.2 |
| 2017 | 107.1 | 109.1 | 108.6 | 108.9 | 108.4 | 5.3 |
| 2018 | 111.4 | 113.1 | 112.2 | 112.3 | 112.2 | 3.5 |
| 2019 | 114.7 | 117.0 | 116.2 | 116.4 | 116.1 | 3.4 |
| 2020 | 118.9 | 120.8 | 120.0 | 120.0 | 119.9 | 3.3 |

**Chanzo**: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

*Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika Des. 2015=100

**FAHIRISI MBALIMBALI ZA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WAKAZI WA MIJINI-TANZANIA BARA (Des.2015=100)**

Jedwali Na.16

| Mwaka | Fahirisi | | | | Badiliko % | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kipato cha | | | Wakazi mijini Tanz. Bara | Kipato cha | | | Wakazi mijini Tanz. Bara |
| | Chini | Kati | Juu | | Chini | Kati | Juu | |
| 2003 | 28.4 | 30.8 | 30.1 | 37.6 | 5.8 | 2.3 | 4.3 | 5.3 |
| 2004 | 30.2 | 33.4 | 32.0 | 39.4 | 6.4 | 8.2 | 6.2 | 4.7 |
| 2005 | 32.7 | 36.0 | 34.8 | 41.4 | 8.3 | 7.9 | 8.6 | 5.0 |
| 2006 | 36.5 | 39.3 | 38.9 | 44.4 | 11.5 | 9.2 | 11.8 | 7.3 |
| 2007 | 39.9 | 43.9 | 44.0 | 47.5 | 9.3 | 11.5 | 13.3 | 7.0 |
| 2008 | 46.8 | 50.6 | 52.1 | 52.4 | 17.3 | 15.3 | 18.3 | 10.3 |
| 2009 | 54.7 | 58.9 | 60.2 | 58.7 | 16.8 | 16.4 | 15.7 | 12.1 |
| 2010* | 61.9 | 64.8 | 65.1 | 61.9 | 13.2 | 10.0 | 8.1 | 5.5 |
| 2011 | 66.5 | 69.9 | 72.0 | 69.8 | 7.4 | 7.9 | 10.6 | 12.7 |
| 2012 | 79.0 | 81.5 | 80.0 | 81.0 | 18.8 | 16.6 | 11.2 | 16.0 |
| 2013 | 86.3 | 88.3 | 86.4 | 87.3 | 9.3 | 8.3 | 8.0 | 7.9 |
| 2014 | 93.0 | 93.7 | 91.6 | 92.7 | 7.7 | 6.2 | 6.0 | 6.1 |
| 2015* | 98.0 | 99.0 | 97.5 | 97.9 | 5.4 | 5.6 | 6.5 | 5.6 |
| 2016 | 102.2 | 103.5 | 102.2 | 102.9 | 4.3 | 4.5 | 4.8 | 5.2 |
| 2017 | 104.1 | 106.2 | 106.5 | 108.4 | 1.9 | 2.6 | 4.2 | 5.3 |
| 2018 | 106.1 | 108.2 | 111.5 | 112.2 | 2.0 | 1.9 | 4.7 | 3.5 |
| 2019 | 110.1 | 113.1 | 115.4 | 116.1 | 3.8 | 4.5 | 3.6 | 3.4 |
| 2020 | 112.4 | 117.0 | 118.2 | 119.9 | 2.1 | 3.5 | 2.4 | 3.3 |

**Chanzo**: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

*Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika Des. 2015=100

## SURA YA 2

## FEDHA NA TAASISI ZA FEDHA

### Ujazi wa Fedha

30. Mwaka 2020, ujazi wa fedha uliendelea kukua kwa kasi ya kuridhisha inayoendana na mahitaji halisi ya shughuli mbalimbali za kiuchumi licha ya changamoto ya mlipuko wa UVIKO-19. Katika kipindi hicho, Benki Kuu ya Tanzania ilichukua hatua mbalimbali katika kuhakikisha kunakuwa na ukwasi unaokidhi mahitaji mbalimbali ya shughuli za kiuchumi wakati wote ikiwa ni pamoja na: kupunguza kiwango cha kisheria cha sehemu ya amana kinachotakiwa kuwekwa Benki Kuu ya Tanzania na benki za biashara kutoka asilimia 7 hadi asilimia 6; kupunguza kiwango cha riba kinachotozwa kwa benki za biashara zinapokopa Benki Kuu ya Tanzania (*discount rate*) kutoka asilimia 7 hadi asilimia 5; kupunguza kiwango cha dhamana na hati fungani za Serikali zinazotumika na sekta ndogo ya benki kama dhamana wakati wa kukopa kutoka Benki Kuu kutoka asimilia 10 hadi asilimia 5 kwa dhamana za muda mfupi, na kutoka asilimia 40 hadi 20 kwa hatifungani. Pamoja na hatua hizi, Benki Kuu iliendelea kuongeza ukwasi katika sekta ndogo ya benki kwa kutoa mikopo ya muda mfupi na kununua fedha za kigeni kutoka katika soko la ndani.


31. Kutokana na utekezaji thabiti wa sera ya fedha, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) uliongezeka kwa asilimia 5.7 na kufikia shilingi bilioni 29,918.2 mwaka 2020 kutoka shilingi bilioni 28,313.1 mwaka 2019. Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2) ulikua kwa asilimia 8.2 kutoka kiasi cha shilingi bilioni 21,280.3 mwaka 2019 hadi shilingi bilioni 23,015.2 mwaka 2020. Aidha, ujazi wa fedha kwa tasfiri finyu (M1) nao pia uliongezeka kufikia shilingi bilioni 14,313.6 mwaka 2020 kutoka shilingi bilioni 13.325.1 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 7.4. Vile vile, mzunguko wa fedha katika uchumi (currency in circulation) uliongezeka kwa asilimia 6.6 mwaka 2020 na kufikia shilingi bilioni 4,500.5. Mwenendo huo ni matokeo ya ukuaji wa mikopo kwa Serikali na sekta binafsi iliyotolewa na sekta ndogo ya benki. Kwa ujumla, hatua zilizochukuliwa na Benki kuu ya Tanzania zilichangia kuimarika kwa ukwasi katika sekta ya benki kulikosababisha kupungua kwa viwango vya riba katika masoko ya fedha na hivyo, kuongeza upatikanaji wa mikopo kwa Serikali na sekta binafsi kwa gharama nafuu.

### Mwenendo wa Mikopo kwa Serikali Kuu na Sekta Binafsi

32. Mwaka 2020, mikopo kutoka sekta ndogo ya benki kwenda Serikali Kuu kupitia ununuzi wa dhamana na hati fungani za Serikali iliongezeka kwa asilimia 48.7 ikilinganishwa na kushuka kwa asilimia 13.1 mwaka 2019. Pamoja na ongezeko kubwa, Serikali iliendelea kuzingatia kiwango cha ukomo wa ukopaji katika soko la ndani

kisichozidi asilimia moja ya Pato ghafi la Taifa ili kutoathiri fursa za ukopaji kwa sekta binafsi. Mikopo kwa sekta binafsi ilikuwa shilingi bilioni 20,308.3 mwaka 2020 ikilinganishwa na shilingi bilioni 19,695.4 mwaka 2019 sawa na ongezeko la asilimia 3.1. Kasi ndogo ya ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi ilitokana na athari hasi za UVIKO-19 katika uchumi wa dunia ulioathri baadhi ya biashara nchini, hususan shughuli zinazohusiana na utalii na usafirishaji na hivyo kusababisha mahitaji ya mikopo mipya kupungua. Katika kipindi hicho, maeneo yaliyokuwa na kasi kubwa ya ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi ni pamoja na mikopo binafsi, uchukuzi na mawasiliano na uchimbaji wa madini. Aidha, sehemu kubwa ya mchango wa mikopo kwa sekta binafsi iliendelea kushikiliwa na shughuli binafsi, biashara, viwanda na kilimo kwa asilimia 33.5, asilimia 15.1, asilimia 9.3 na asilimia 8.5 mtawalia.

**Kielelezo Na 2.1: Mchango wa Mikopo ya Benki za Biashara kwa Shughuli za Kiuchumi**




**Amana katika Benki za Biashara**

33. Mwaka 2020, amana katika benki za biashara zilikuwa shilingi bilioni 23,722.1 ikilinganishwa na shilingi bilioni 22,758.9 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 4.2. Kati ya hizo, amana za sekta binafsi zilikuwa shilingi bilioni 23,069.2 sawa na asilimia 97.2. Ongezeko la amana lilitokana na juhudi za benki za biashara kuhimiza wananchi kuweka akiba katika mfumo rasmi wa benki, kuendelea kuongeza wigo wa utoaji huduma kwa kuongeza matawi ya benki pamoja na matumizi ya mawakala. Aidha, uwiano wa amana za fedha za kigeni ukilinganishwa na amana zote ulikuwa asilimia 27.2 mwaka 2020 ikilinganishwa na asilimia 27.1 mwaka 2019.

**Mwenendo wa Viwango vya Riba**

34. Mwaka 2020, wastani wa viwango vya riba katika soko la fedha baina ya benki ulipungua hadi asilimia 4.50 kutoka asilimia 5.13 mwaka 2019. Aidha, riba ya dhamana

za Serikali za muda mfupi ilipungua hadi wastani wa asilimia 4.42 mwaka 2020 kutoka asilimia 7.71 mwaka 2019. Vile vile, viwango vya riba za mikopo inayotolewa na benki za biashara vilipungua na kufikia wastani wa asilimia 16.66 mwaka 2020 kutoka wastani wa asilimia 16.97 mwaka 2019. Katika kipindi hicho, riba za mikopo ya mwaka mmoja zilipungua hadi wastani wa asilimia 15.73 kutoka asilimia 16.69 mwaka 2019. Kupungua kwa riba za mikopo kulitokana na juhudi mbalimbali zinazoendelea kutekelezwa na Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania katika kupunguza mikopo chechefu, kuhakikisha uwepo wa ukwasi wa kutosha katika uchumi ili kuwezesha benki na taasisi za fedha kuongeza utoaji wa mikopo kwa sekta binafsi pamoja na kuendelea kuboreshwa kwa mazingira ya biashara nchini. Kwa upande mwingine, riba za amana za muda maalum kwa ujumla zilipungua hadi wastani wa asilimia 6.70 mwaka 2020 kutoka asilimia 7.25 mwaka 2019, na riba za mwaka mmoja zilipungua na kufikia wastani wa asilimia 8.28 kutoka asilimia 8.80 mwaka 2019. Kutokana na mwenendo huo, tofauti kati ya viwango vya riba za amana na mikopo ya mwaka mmoja ilipungua kutoka wastani wa asilimia 7.89 mwaka 2019 hadi wastani wa asilimia 7.45 mwaka 2020.

## MAENDELEO KATIKA SEKTA YA FEDHA

### Huduma za Benki

35. Mwaka 2020 kulikuwa na benki na taasisi nyingine za fedha zipatazo 55 (benki 46 na taasisi nyingine za fedha 9) ikilinganishwa na taasisi za fedha 60 (benki 51 na taasisi nyingine za fedha 9) mwaka 2019. Upungufu huo ulitokana na Benki Kuu ya Tanzania kuridhia na kuunganisha benki kama ifuatavyo: NIC Bank Tanzania Limited na Commercial Bank of Africa (Tanzania) Limited na kuunda benki inayoitwa NCBA Bank Tanzania Limited; TIB Corporate Bank Limited na Tanzania Postal Bank na kuunda benki inayoitwa TPB Bank Plc; na HAKIKA Microfinance Bank Limited, EFC Tanzania Microfinance Bank Limited na Mwanga Rural Community Bank Limited na kuunda benki inayoitwa Mwanga Hakika Microfinance Bank Limited. Aidha, hadi Desemba 2020 kulikuwa na matawi ya benki 969 ikilinganishwa na matawi 941 katika kipindi kama hicho mwaka 2019.

36. Hadi Desemba 2020, jumla ya benki 23 zilitoa huduma kwa njia ya uwakala ikilinganishwa na benki 21 Desemba 2019. Aidha, idadi ya mawakala wa utoaji huduma za kibenki ilifikia 40,410 kutoka mawakala 28,358 Desemba 2019, sawa na ongezeko la asilimia 42.50. Ongezeko hilo lilichangiwa na kuendelea kwa utekelezaji wa Mpango wa Huduma Jumuishi za Fedha 2018 - 2022 ambao uliwezesha upatikanaji wa huduma za fedha mijini na vijijini zikichangiwa kwa sehemu kubwa na matumizi ya simu za mikononi pamoja na mawakala wa benki.

37. Mwaka 2020, miamala ya kuweka amana kupitia huduma za benki kwa njia ya uwakala ilikuwa 9,860,061 yenye thamani ya shilingi bilioni 6,763.9 ikilinganishwa na miamala 7,522,863 yenye thamani ya shilingi bilioni 5,464.9 mwaka 2019, sawa na ongezeko la miamala kwa asilimia 31.1. Aidha, idadi ya miamala ya kutoa fedha ilikuwa 6,704,709 yenye thamani ya shilingi bilioni 2,548.28 mwaka 2020 ikilinganishwa na miamala 5,377,436 yenye thamani ya shilingi bilioni 1,833.06 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 24.7.

38. Mwaka 2020, sekta ya ndogo ya benki iliendelea kuwa imara, salama na yenye kutengeneza faida ikiwa na mitaji na ukwasi wa kutosha juu ya ukomo unaohitajika kisheria. Viashiria vya sekta ndogo ya benki vinaonesha kuwa uwiano kati ya mali inayoweza kubadilishwa kuwa fedha taslimu na amana zinazohitajika kwa muda mfupi uliendelea kuwa juu ya uwiano unaohitajika kisheria wa asilimia 20 japokuwa ulipungua na kufikia asilimia 30.24 Desemba 2020 kutoka asilimia 31.01 kipindi kama hicho mwaka 2019. Aidha, uwiano wa mtaji wa msingi na rasilimali za benki ulikuwa asilimia 17.17 Desemba 2020 ikilinganishwa na asilimia 16.73 katika kipindi kama hicho mwaka 2019, ambao ni zaidi ya uwiano wa chini unaohitajika kisheria wa asilimia 10. Vilevile, rasilimali za sekta ya kibenki ziliimarika zaidi kutokana na kupungua kwa uwiano wa mikopo chechefu na kufikia asilimia 9.32 Decemba 2020 kutoka asilimia 9.84 ya mikopo yote mwezi Decemba 2019. Katika kufikia lengo la asilimia 5 la uwiano wa mikopo chechefu, hatua zilizoendelea kuchukuliwa na Benki Kuu ni pamoja na kuzitaka benki na taasisi za fedha: kuboresha usimamizi katika utoaji mikopo; kutekeleza mpango kazi wa kupunguza uwiano wa mikopo chechefu kwa benki zilizokuwa na uwiano mkubwa; na kutumia taarifa ya historia za wakopaji zilizopo kwenye kanzidata kabla ya utoaji wa mikopo. Katika kipindi hicho, faida kabla ya kodi katika sekta ndogo ya benki ilikuwa shilingi bilioni 636.58 ikilinganishwa na faida kabla ya kodi ya shilingi bilioni 577.39 ya mwaka 2019.

**Huduma Ndogo za Fedha**

39. Mwaka 2020, Serikali iliendelea kutekeleza sera, sheria na kanuni za huduma ndogo za fedha kwa kutoa mafunzo kwa wadau mbalimbali wakiwemo maafisa maendeleo ya jamii, maafisa tehama, wahariri wa vyombo vya habari na waratibu wa biashara ya huduma ndogo za fedha katika ngazi ya wizara, mikoa na halmashauri zote nchini. Kwa upande mwingine, Benki Kuu ilipokea maombi ya leseni 698 ya watoa huduma ndogo za fedha daraja la pili, ambapo watoa huduma 215 walipata leseni. Aidha, maombi 241 ya leseni kwa watoa huduma ndogo za fedha wa daraja la tatu yalipokelewa na leseni 56 zilitolewa.

**Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana**

40. Hadi Desemba 2020, leseni zilizotolewa na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana kwa watendaji na washauri wa uwekezaji zilifikia 144 kutoka leseni 76 katika kipindi kilichoishia Desemba 2019. Aidha, Mamlaka kupitia masoko ya awali ilifanya uchambuzi na kuidhinisha maombi ya: Kuorodheshwa kwa hisa 2,164,349 za kampuni ya JATU zenye thamani ya shilingi bilioni 1.08 katika Soko la Hisa la Dar es Salaam; Kuuza hisa 16,808,412 za Benki ya Biashara ya Akiba zenye thamani ya shilingi bilioni 24.7; kuuza hisa 24,509,804 za Benki ya Wananchi Mufindi zenye thamani ya shilingi bilioni 5; na kuuza hisa 174,500,000 za Benki ya Biashara ya NMB zenye thamani ya shilingi bilioni 420.5 kutoka Kampuni ya Rabobank kwenda Kampuni ya Arise.

41. Mwaka 2020, mauzo ya hisa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam -DSE yalikuwa shilingi bilioni 591.2 ikilinganishwa na shilingi bilioni 624.8 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 5.4. Hii ilichangiwa na kupungua kwa uwekezaji kulikotokana na athari za UVIKO-19 zilizosababisha wawekezaji kuhamisha uwekezaji wa hisa uliokuwa na uwezekano mkubwa wa kupata athari za kiuchumi na kwenda uwekezaji wa hatifungani za Serikali.

42. Katika kipindi kilichoishia Desemba 2020, mtaji wa Soko la Hisa kwa kampuni za ndani uliongezeka kwa asilimia 2.2 na kufikia shilingi trilioni 9.2 ikilinganishwa na shilingi trilioni 9.0 katika kipindi kama hicho mwaka 2019. Hii ilitokana na kuongezeka kwa bei ya hisa za baadhi ya kampuni zilizoorodheshwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam na kuorodheshwa kwa hisa za Kampuni ya JATU PLC. Hata hivyo, mtaji wa jumla wa Soko la Hisa ulipungua kwa asilimia 11.7 kufikia shilingi trilioni 15.1 katika kipindi kilichoishia Desemba 2020 kutoka shilingi trilioni 17.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2019. Kupungua kwa mtaji wa jumla wa Soko la Hisa kulitokana na kushuka kwa bei za hisa za kampuni zilizoorodheshwa Soko la Hisa la Dar es Salaam kutoka Soko la Hisa la Nairobi (NSE) ambazo ni Jubilee Holdings, Kenya Airways, Kenya Commercial Bank, National Media Group na East African Breweries Ltd.

43. Hadi Desemba 2020, mauzo ya hatifungani za Serikali zilizoorodheshwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam yaliongezeka kwa asilimia 90.9 na kufikia shilingi trilioni 2.1 kutoka mauzo ya shilingi trilioni 1.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2019. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uwekezaji katika hatifungani za Serikali kulikosababishwa na wawekezaji kuhamisha uwekezaji kutoka kwenye uwekezaji unaoonekana unaweza kupata athari za kiuchumi. Aidha, mauzo ya hatifungani za kampuni yaliongezeka kwa asilimia 72.4 na kufikia shilingi bilioni 1.31 Desemba 2020 ikilinganishwa na mauzo ya shilingi bilioni 0.76 katika kipindi kama hicho mwaka 2019.

44. Hadi Desemba 2020, jumla ya thamani ya Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja ilikuwa shilingi bilioni 476.9 ikilinganishwa na shilingi bilioni 329.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 44.7. Thamani ya mifuko yote iliongezeka mwaka 2020 isipokuwa thamani ya Mfuko wa Jikimu ambao ulipungua kufikia shilingi bilioni 17.96 katika kipindi kilichoishia Desemba 2020 kutoka shilingi bilioni 19.77 katika kipindi kama hicho mwaka 2019. Kupungua kwa thamani ya Mfuko wa Jikimu kulitokana na malipo kwa baadhi ya wawekezaji kufuatia kuiva kwa uwekezaji na kuwekeza kwenye Mifuko ya Hatifungani na Ukwasi.

**Jedwali Na. 2.1: Thamani ya Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja Mwaka 2019-2020 (Shilingi)**

| Jina la Mfuko | 2019 | 2020 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|
| Umoja | 217,343,594,420.1 | 237,355,417,114.1 | 9.2 |
| Wekeza Maisha | 1,175,287,918.8 | 1,430,985,515.8 | 21.8 |
| Watoto | 3,205,688,248.0 | 3,686,050,079.0 | 15.0 |
| Ukwasi | 62,690,472,220.1 | 152,620,440,938.4 | 143.5 |
| Jikimu | 19,775,644,400.1 | 17,964,415,714.4 | -9.2 |
| Hatifungani | 25,445,083,010.8 | 63,929,897,105.9 | 151.2 |
| **Jumla** | **329,635,770,217.8** | **476,987,206,467.5** | **44.7** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana

**Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma**

45. Mwaka 2020, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma - PSSSF ulisajili wanachama wapya 14,615 ikilinganishwa na wanachama 12,809 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 14.1. Aidha, Mfuko ulikusanya shilingi trilioni 1.4 kutokana na michango ya wanachama mwaka 2020 ikilinganishwa na shilingi trilioni 1.3 mwaka 2019. Vile vile, Mfuko ulilipa mafao yenye thamani ya shilingi trilioni 1.2 kwa wanachama 38,104 mwaka 2020 ikilinganishwa na mafao yenye thamani ya shilingi trilioni 1.5 kwa wanachama 23,504 mwaka 2019. Kwa upande mwingine, mapato yaliyotokana na uwekezaji wa Mfuko yalikuwa shilingi bilioni 415.4 mwaka 2020 ikilinganishwa na shilingi bilioni 429.9 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 3.4. Hii ilitokana na kupungua kwa mapato ya uwekezaji kulikosababishwa na kushuka kwa riba katika soko la fedha na kupungua kwa mapato yalitokanayo na kodi za majengo kufuatia mlipuko wa UVIKO – 19 kwani baadhi ya wapangaji walisitisha biashara. Hadi Desemba 2020, thamani ya Mfuko ilikuwa shilingi trilioni 5.7 ikilinganishwa na shilingi trilioni 5.5 mwaka 2019.

**Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii**

46. Mwaka 2019/20, wanachama wachangiaji wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii – NSSF walifikia 797,564 kutoka wanachama 583,354 mwaka 2018/19, sawa na

ongezeko la asilimia 36.7. Aidha, Mfuko ulikuwa na wastaafu 22,042 mwaka 2019/20 ikilinganishwa na wastaafu 18,838 mwaka 2018/19, sawa na ongezeko la asilimia 17.0. Kwa upande mwingine, Mfuko ulikusanya michango ya wanachama kiasi cha shilingi trilioni 1.1 ikilinganishwa na shilingi bilioni 920.6 zilizokusanywa mwaka 2018/19, sawa na ongezeko la asilimia 19.5. Vile vile, mafao yaliyolipwa kwa wanachama yalikuwa shilingi bilioni 461.9 ikilinganishwa na shilingi bilioni 375.7 mwaka 2018/19, sawa na ongezeko la asilimia 22.9.

47. Mwaka 2019/20, mapato ya Mfuko yatokanayo na uwekezaji yalifikia shilingi bilioni 337.8 ikilinganishwa na shilingi bilioni 115.9 mwaka 2018/19. Kuongezeka kwa mapato kulitokana na kuimarishwa kwa ukusanyaji wa mapato yatokanayo na uwekezaji na udhibiti wa mifumo ya fedha. Kwa upande mwingine, thamani ya Mfuko iliongezeka kwa asilimia 18.9 kutoka shilingi trilioni 3.7 mwaka 2018/19 na kufikia shilingi trilioni 4.4 mwaka 2019/20.

**Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi**

48. Hadi Desemba 2020, waajiri waliosajiliwa na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi – WCF walifikia 22,796 kutoka waajiri 20,102 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 13.4. Aidha, michango kutoka kwa waajiri ilipungua na kufikia shilingi bilioni 106.4 ikilinganishwa na shilingi bilioni 108.9 mwaka 2019. Upungufu huo ulitokana na baadhi ya waajiri kufunga biashara na kupunguza wafanyakazi wanaochangiwa kwenye Mfuko kulikosababishwa na athari za maambukizi ya UVIKO-19.

49. Mwaka 2020, mapato yatokanayo na uwekezeji wa Mfuko yalifikia shilingi bilioni 42.3 kutoka shilingi bilioni 25.02 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 69.1. Hii ilitokana na uwekezaji mapato yanayotokana na michango ya waajiri katika hati fungani za Serikali. Aidha, mapato yaliyotokana na shughuli nyingine za kiuchumi ikiwemo mapato ya huduma yalikuwa shilingi milioni 445.6 ikilinganishwa na shilingi milioni 82.6.

50. Mwaka 2020, Mfuko ulitumia shilingi bilioni 9.1 kulipi matibabu na fidia kwa wafanyakazi walioumia au kufariki wakiwa kazini ikilinganishwa na shilingi bilioni 4.9 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asimilia 85.7. Hii ilitokana na kutolewa kwa elimu kwa umma kuhusu masuala ya fidia kwa wafanyakazi na taratibu za kudai mafao kulikosababisha kuongezeka kwa madai ya wafanyakazi walioumia, kuugua au kufariki wakiwa kazini. Kwa upande mwingine, thamani ya Mfuko ilifikia shilingi bilioni 333.5 mwaka 2020 ikilinganishwa na shilingi bilioni 278.1 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 19.9. Hii ilitokana na kuongezeka kwa makusanyo ya michango ya waajiri na mapato yatokanayo na uwekezaji pamoja na shughuli nyingine za kiuchumi. Aidha, Mfuko uliwekeza katika amana za Serikali  shilingi bilioni 264.0, amana za benki

shilingi bilioni 14.8) amana za Kampuni shilingi bilioni 2.9, Mfuko wa Umoja UTT shilingi bilioni 16.0, Hisa za kampuni shilingi bilioni 23.8 na Kiwanja Dodoma shilingi milioni 2.6.

**Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya**

51. Mwaka 2019/20, wanachama wachangiaji katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya – NHIF waliongezeka kwa asilimia 9.2 na kufikia wanachama 1,055,555 kutoka wanachama 966,792 mwaka 2018/19. Aidha, Mfuko ulihudumia wanufaika 4,403,581 ikilinganishwa na wanufaika 4,025,693 mwaka 2018/19, sawa na ongezeko la asilimia 9.4. Ongezeko la wanufaika lilitokana na utoaji wa elimu kwa umma na kuongeza makundi mbalimbali kupitia vyama vya ushirika, makundi mengine ya sekta isiyo rasmi ikiwemo bodaboda na mwanachama mmoja mmoja kupitia vifurushi vya bima ya afya.

**Jedwali Na.2.2: Wanachama Wachangiaji na Wanufaika wa Mfuko**

| **Mwaka** | **Idadi ya wanachama** | **Wanufaika Waliohudumiwa** |
|---|---|---|
| 2016/17 | 753,832 | 3,491,400 |
| 2017/18 | 858,446 | 3,918,999 |
| 2018/19 | 966,792 | 4,025,693 |
| 2019/20 | 1,055,555 | 4,403,581 |
| **Badiliko (asilimia)** | **9.2** | **9.4** |

**Chanzo:** Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya

52. Mwaka 2019/20, vituo vya kutolea huduma za afya vilivyosajiliwa na Mfuko vilifikia 8,970 kutoka vituo 7,606 mwaka 2018/2019, sawa na ongezeko la asilimia 17.9. Kati ya hivyo, vituo 6,202 sawa na asilimia 69 vilikuwa vya Serikali, madhehebu ya dini vituo 905 (asilimia10) na vituo binafsi 1,863 (asilimia 21).

**Jedwali Na. 2.3: Idadi ya Vituo vya Kutolea Huduma za Afya Vilivyosajiliwa na Mfuko Mwaka 2016/17-2019/20**

| **Vituo vya Kutolea Huduma ya Afya** | **2016/17** | **2017/18** | **2018/19** | **2019/20** | **Badiliko (Asilimia)** |
|---|---|---|---|---|---|
| Zahanati | 5,360 | 5,401 | 5,753 | 6,485 | 12.7 |
| Vituo vya Afya | 705 | 713 | 766 | 853 | 11.4 |
| Hospitali | 278 | 286 | 298 | 346 | 15.8 |
| Maduka ya dawa | 320 | 349 | 449 | 597 | 33.0 |
| Maduka ya dawa maalumu | 434 | 202 | 200 | 461 | 130.5 |
| Cliniki Maalum | 37 | 73 | 130 | 211 | 62.3 |
| Vituo vya Uchunguzi | 6 | 6 | 9 | 16 | 77.8 |
| Vituo vya Uokozi | - | 1 | 1 | 1 | 0.0 |
| **Jumla** | **7,140** | **7,031** | **7,606** | **8,970** | **17.9** |

**Chanzo:** Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya

53. Mwaka 2019/20, mapato ya Mfuko yalikuwa shilingi bilioni 550.4 ikilinganishwa na shilingi bilioni 502.9 mwaka 2018/2019, sawa na ongezeko la asilimia 9.5. Hii ilitokana na mikakati mbalimbali ya kusajili makundi mbalimbali

kutoka sekta rasmi na isiyo rasmi. Aidha, thamani ya Mfuko ilipungua kwa asilimia 7.7 na kufikia shilingi bilioni 1.2 mwaka 2019/20 kutoka shilingi bilioni 1.3 mwaka 2018/19. Upungufu huo ulisababishwa na ongezeko la malipo ya madai pamoja na kushuka kwa mapato yatokanayo na uwekezaji kulikosababishwa na kushuka kwa riba katika soko la fedha.

**Jedwali Na. 2.4: Mchanganuo wa Mapato ya Mfuko kwa aina ya Chanzo**

| Mwaka wa Fedha | Shilingi Bilioni | | | Jumla ya Mapato |
|---|---|---|---|---|
| | Mapato ya Michango | Mapato ya Vitega Uchumi | Mapato Mengineyo | |
| 2016/17 | 367.6 | 109.5 | 1.9 | 479.0 |
| 2017/18 | 394.9 | 107.4 | 1.5 | 503.8 |
| 2018/19 | 431.0 | 84.8 | 3.1 | 518.9 |
| 2019/20 | 467.8 | 79.5 | 3.2 | 550.4 |
| **Badiliko (Asilimia)** | **8.5** | **-6.2** | **1.8** | **6.1** |

**Chanzo:** Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya

**Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima Tanzania**

54. Hadi Desemba 2020, kampuni za bima zilizosajiliwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima Tanzania - TIRA kufanya biashara ya bima zilikuwa 32 kama ilivyokuwa mwaka 2019. Katika kipindi hicho, Mamlaka ilisajili kampuni za udalali wa bima 77, udalali wa bima mtawanyo nne (4), wakala wa bima 756 na wakadiriaji hasara 60 ikilinganishwa na kampuni za udalali wa bima 101, udalali wa bima mtawanyo tatu (3), wakala wa bima 643 na wakadiriaji hasara 58 mwaka 2019. Aidha, benki-wakala wa bima 14 zilisajiliwa kuanza kutoa huduma za bima na kampuni tatu (3) za sayansi ya uthaminishaji zilisajiliwa na kupewa leseni mwaka 2020. Mwaka 2020, mikataba ya bima iliyotolewa na kampuni za bima iliongezeka kwa asilimia 5.1 na kufikia mikataba 1,694,666 kutoka mikataba 1,611,853 mwaka 2019.

55. Mwaka 2020, watumiaji wa huduma za bima waliongezeka kwa asilimia 17.1 kutoka watumiaji 5,709,878 mwaka 2019 hadi watumiaji 6,686,267. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uelewa wa wananchi kuhusu umuhimu wa kuwa na bima. Aidha, madai ya bima za kawaida yaliyolipwa yaliongezeka kwa asilimia 7.6 kutoka shilingi milioni 268,393 mwaka 2019 kufikia shilingi milioni 288,916 mwaka 2020. Hii ilitokana na kuongezeka kwa madai katika bima za ajali, vyombo vya moto, anga na majini. Vile vile, malipo ya madai ya bima za maisha yaliongezeka kufikia shilingi milioni 64,227 mwaka 2020 kutoka shilingi milioni 50,573 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 27.0.

**Jedwali Na. 2.5: Thamani ya Madai ya Bima za Kawaida (Shilingi Milioni)**

| Aina za Bima | Mwaka 2019 | Mwaka 2020 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---:|---:|:---:|
| Moto | 48,657 | 55,170 | 13.4 |
| Uhandisi | 7,418 | 7,097 | -4.3 |
| Vyombo vya moto | 88,060 | 93,920 | 6.7 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Ajali | 11,212 | 13,360 | 19.2 |
| Majini | 7,066 | 8,967 | 26.9 |
| Anga | 2,965 | 13,394 | 351.7 |
| Afya | 96,023 | 88,451 | -7.9 |
| Vinginevyo | 6,990 | 8,559 | 22.4 |
| **Jumla** | **268,393** | **288,916** | **7.6** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima Tanzania

56. Mwaka 2020, mauzo katika soko la bima yaliongezeka kwa asilimia 1.6 na kufikia shilingi bilioni 827.9 kutoka shilingi bilioni 814.5 mwaka 2019. Aidha, mauzo ya bima za kawaida yalipungua hadi shilingi bilioni 690.0 mwaka 2020 kutoka shilingi bilioni 694.9 mwaka 2019. Hii ilitokana na kupungua kwa mauzo ya bima za uhandisi kulikosababishwa na kushuka kwa uwekezaji katika miradi ya kigeni ya moja kwa moja kutokana na athari za UVIKO-19. Vile vile, mauzo ya bima za maisha yalifikia shilingi bilioni 137.9 mwaka 2020 kutoka shilingi bilioni 119.6 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 15.3. Bima za kawaida zilichangia asilimia 83.3 ya mauzo yote na bima za maisha asilimia 16.7 mwaka 2020.

57. Mwaka 2020, thamani ya mali za kampuni za bima zilifikia shilingi bilioni 1,181.0 kutoka shilingi bilioni 1,047.0 kwa mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 12.8. Ongezeko hilo lilitokana na kukua kwa mauzo ya bima na mitaji ya kampuni za bima. Aidha, uwekezaji wa kampuni za bima ulikuwa na thamani ya shilingi bilioni 858.7 ikilinganishwa na shilingi bilioni 750.8 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 14.4. Uwekezaji huo ulijumuisha amana katika taasisi za fedha na benki na fedha taslimu asilimia 46.4, dhamana za Serikali (asilimia 31.8), hisa (asilimia 10.0), mali zisizohamishika (asilimia 9.8), na uwekezaji kwenye maeneo mengine (asilimia 2.0). Kwa upande mwingine, madeni ya kampuni za bima yalifikia shilingi bilioni 764.9 mwaka 2020 kutoka shilingi bilioni 719.8 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 6.3. Mitaji ya makampuni hayo iliongezeka kwa asilimia 27.1 kutoka shilingi bilioni 327.2 mwaka 2019 hadi shilingi bilioni 416.1 kwa mwaka 2020.

**Jedwali Na. 2.6: Thamani za Mali na Madeni ya Kampuni za Bima (Shilingi Milioni)**

| Maelezo | Mwaka 2019 | Mwaka 2020 | Badiliko (asilimia) |
|---|---|---|---|
| Mali | 1,047,040 | 1,180,960 | 12.8 |
| Madeni | 719,801 | 764,904 | 6.3 |
| Ziada ya Mali | 327,240 | 416,056 | 27.2 |
| Mali Zilizowekezwa | 750,828 | 858,717 | 14.4 |

**Chanzo**: Mamlaka ya Bima Tanzania

58. Mwaka 2020, mapato yatokanayo na uwekezaji wa kampuni za bima za kawaida yalikuwa shilingi bilioni 52.5 ikilinganishwa na shilingi bilioni 32.0 mwaka 2019. Katika kipindi hicho, Kampuni za bima za kawaida zilipata faida ya shilingi bilioni 50.1 ikilinganishwa na shilingi bilioni 45.8 mwaka 2019 sawa na ongezeko la asilimia 9.4.

59. Mwaka 2019/20, Shirika la Bima la Taifa - NIC liliendelea kutoa huduma za bima ya maisha na bima nyingine kupitia matawi na wakala waliopo nchi nzima. Katika kipindi hicho, mapato ya Shirika la Bima la Taifa - NIC yalikuwa shilingi bilioni 76.44 ikilinganishwa na shilingi bilioni 44.59 mwaka 2018/19, sawa na ongezeko la asiliamia 71.4. Thamani ya mali za Shirika iliongezeka na kufikia shilingi bilioni 72.16 mwaka 2019/20 kutoka shilingi bilioni 48.72 mwaka 2018/19, sawa na ongezeko la asilimia 48.1. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uwekezaji wa Shirika katika hati fungani. Vile vile, thamani ya fidia iliyotolewa na Shirika iliongezeka na kufikia shilingi bilioni 18.09 mwaka 2019/20 ikilinganishwa na shilingi bilioni 12.52 mwaka 2018/19. Kuongezeka kwa kiwango cha fidia iliyolipwa kulitokana na utekelezaji wa mkakati wa Shirika uliolenga kupunguza malimbikizo ya madai utakaongeza imani katika soko na kuvutia wateja.

**Mwenendo wa Soko la Mikopo ya Nyumba Tanzania**

60. Mwaka 2020, Kampuni ya Mikopo ya Nyumba Tanzania - TMRC ilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 1.0 kwa benki ya First Housing Finance kwa mara ya kwanza ikilinganishwa na mikopo ya shilingi bilioni 47.4 iliyotelewa kwa benki saba (7) mwaka 2019. Kupungua kwa utoaji wa mikopo kulitokana na benki kuendelea kulipa deni la mikopo ya nyuma iliyotolewa na Kampuni na upatikanaji mdogo wa mikopo yenye masharti nafuu kwa ajili ya kukopesha benki na taasisi za fedha zinatoa mikopo ya nyumba. Katika kipindi hicho, thamani ya mikopo kutoka TMRC iliyokuwepo katika benki na taasisi za fedha zilizotoa mikopo ya nyumba ilikuwa shilingi bilioni 134.7.

**Jedwali Na. 2.5: Thamani ya Mikopo kutoka TMRC iliyopo katika Benki na Taasisi za Fedha mwaka 2020**

| Na. | Benki | Kiasi cha Mkopo (shilingi Milioni) | Asilimia |
|---|---|---|---|
| 1 | CRDB Bank Plc | 27,000 | 20 |
| 2 | Azania Bank Limited | 15,700 | 12 |
| 3 | National Bank of Commerce Limited | 13,000 | 10 |
| 4 | Absa Bank (T) Limited | 12,000 | 9 |
| 5 | NMB Bank Plc | 11,700 | 9 |
| 6 | Bank of Africa (T) Limited | 10,750 | 8 |
| 7 | NCBA Bank (T) Limited | 3,000 | 2 |
| 8 | KCB Bank (T) Limited | 10,000 | 7 |
| 9 | African Banking Corporation (T) Limited | 6,400 | 5 |
| 10 | Exim Bank (T) Limited | 6,000 | 4 |
| 11 | Mkombozi Commercial Bank Plc | 3,000 | 2 |
| 12 | Stanbic Bank (T) Limited | 5,900 | 4 |
| 13 | DCB Commercial Bank Plc | 3,500 | 3 |
| 14 | I & M Bank (T) Limited | 3,250 | 2 |

| Na. | Benki | Kiasi cha Mkopo (shilingi Milioni) | Asilimia |
|---|---|---|---|
| 15 | First National Bank (T) Limited | 2,500 | 2 |
| 16 | First Housing Finance | 1,000 | 1 |
| | **Jumla** | **134,700** | **100** |

**Chanzo**: Kampuni ya Mikopo ya Nyumba Tanzania

61. Mwaka 2020, thamani ya mali za Kampuni ya Mikopo ya Nyumba Tanzania ilipungua na kufikia shilingi bilioni 187.6 ikilinganishwa na shilingi bilioni 201.4 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 6.8. Hii ilitokana na benki na taasisi za fedha zilizokuwa zikitoa mikopo ya nyumba kupitia TMRC kurejesha mkopo Benki Kuu ya Tanzania kiasi cha shilingi bilioni 15.8. Aidha, Kampuni ilipata faida ya shilingi bilioni 2.8 mwaka 2020 ikilinganishwa na shilingi bilioni 1.0 mwaka 2019. Kwa upande mwingine, wanufaika wa mikopo iliyotolewa na benki na taasisi za fedha walikuwa 1,345 ambapo wanaume walikuwa 889, wanawake 389 na waliokopa kwa pamoja walikuwa 67.

**Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania**

62. Hadi Desemba 2020, mtaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania uliongezeka kwa asilimia 12 kufikia shilingi bilioni 77.4 kutoka shilingi bilioni 69.1 mwaka 2019. Katika kipindi hicho, amana za benki zilipungua hadi shilingi bilioni 416.8 kutoka shilingi bilioni 680.2 mwaka 2019. Kupungua kwa amana kulitokana na benki hiyo kulipa madai ya wakulima wa korosho katika mikoa ya Mtwara na Lindi.

63. Mwaka 2020, Benki ya Maendeleo ya Kilimo ilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 86.7 ikilinganishwa na shilingi bilioni 59.6 mwaka 2019. Mikopo hii iliwanufaisha wakulima 2,487,722 ikilinganishwa na wakulima 2,130,849, sawa na ongezeko la asilimia 16.7. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya mikopo katika shughuli za kiuchumi za kilimo. Kati ya mikopo hiyo, shilingi bilioni 43.69 zilitolewa kwa vyama vitatu vya ushirika katika Mkoa wa Kagera kwa ajili ya ununuzi wa kahawa. Aidha, benki ilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 32.0 kwa ajili miradi mbalimbali ya uchakataji wa mazao ikiwemo: Kiwanda cha Sukari Bagamoyo; Mawese–Kigoma; Maziwa–Tanga; Mahindi–Arusha na Rukwa; Mafuta ya Alizeti na Pamba–Shinyanga; Usindikaji wa Zabibu-Dodoma; Mpunga–Mara; Pamba–Shinyanga; na Samaki-Kagera. Vilevile, mikopo ya shilingi bilioni 6.6 ilitolewa kwa ajili ya ununuzi wa matrekta na mashine ya kupanda na kuvuna (combine harvester) na shilingi bilioni 4.9182 kununua zana za kilimo za uzalishaji wa mazao ya pamba, mahindi na mpunga.

64. Mwaka 2020, Benki ya Maendeleo ya Kilimo ilipata faida ya shilingi bilioni 8.9 ikilinganishwa na faida ya shilingi bilioni 3.1 mwaka 2019. Hii ilitokana na

kuongezeka kwa jitihada za benki katika kufuatilia urejeshwaji wa mikopo na kupunguza gharama za uendeshaji. Kwa upande mwingine, benki kupitia Mfuko wa Dhamana kwa Wakulima Wadogo - SCGS ilitoa mikopo ya shilingi bilioni 27.7 kupitia benki nane (8) za biashara na kuwanufaisha wakulima 749,377 katika mikoa 26 ya Tanzania Bara na mkoa mmoja (1) wa Zanzibar. Kati ya wanufaika hao, wanawake walikuwa 137,402, sawa na asilimia 18.4.

**Benki ya TPB**

65. Mwaka 2020, amana za wateja katika Benki ya TPB zilifikia shilingi milioni 665,496 kutoka shilingi milioni 498,200 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 33.6. Hii ilitokana na kuongezeka kwa wateja 41,922 kulikosababishwa na kuunganishwa kwa TPB Bank PLC na TIB Corporate na kufanya jumla ya wateja kufikia 623,508 hadi Desemba 2020. Aidha, Benki ya TPB ilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi milioni 616,512 ikilinganishwa na shilingi milioni 420,200 mwaka 2019. Kwa upande mwingine, uwekezaji wa benki katika dhamana za Serikali ulipungua na kufikia shilingi milioni 100,455 mwaka 2020 kutoka shilingi milioni 100,588 mwaka 2019. Katika kipindi hicho, mikopo chechefu iliongezeka na kufikia shilingi milioni 86,867, sawa na asilimia 14.1 ya mikopo yote kutoka shilingi milioni 36,133 mwaka 2019. Kuongezeka kwa mikopo chechefu kulitokana na Benki ya TPB kuungana na Benki ya TIB Corporate na kurithi mikopo chechefu iliyokuwa katika benki hiyo. Pato ghafi la Benki ya TPB liliongezeka kwa asilimia 17.2 na kufikia shilingi milioni 152,110 kutoka shilingi milioni 129,800 mwaka 2019. Ongezeko hilo lilichangiwa na benki kuweka kipaumbele katika utoaji wa mikopo ya kimkakati kwa mikopo inayofanya vizuri katika marejesho na ulipaji wa riba pamoja na kuongezeka kwa wigo wa vyanzo vya mapato.

**Soko la Bidhaa Tanzania**

66. Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi ilianzisha Kampuni ya Soko la Bidhaa Tanzania iliyosajiliwa mwaka 2014 chini ya Sheria ya Kampuni ya mwaka 2002. Aidha, Kampuni hiyo ilipewa leseni na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana Desemba 2016 kwa mujibu wa Sheria ya Masoko ya Bidhaa ya mwaka 2015 na Kanuni zake za mwaka 2016.

67. Soko la Bidhaa ni mahali ambapo wauzaji na wanunuzi hukutana kwa kuwakilishwa na mawakala walioidhinishwa kufanya biashara ya mikataba ya bidhaa. Mawakala hawa wanapaswa kuwa na leseni kutoka Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana na kuidhinishwa na Bodi ya Soko la Bidhaa kufanya kazi hiyo. Aidha, Soko la Bidhaa huwaleta pamoja wanunuzi wengi wa ndani na nje ya nchi ambao sio lazima

wafike kwenye soko la bidhaa au nchini kwa kuwa miamala hufanyika kwa njia za kielektroniki na husimamiwa kisheria ili kulinda wanunuzi na wauzaji. Katika utaratibu huo, muuzaji huwa na uhakika wa kupata malipo yake baada ya mauzo na mnunuzi huwa na uhakika wa kupata bidhaa yenye ubora na uzito uliokubalika katika mkataba wa mauzo. Hadi Desemba 2020 mazao yaliyokuwa yakiuzwa katika soko la bidhaa yalijumuisha ufuta, korosho, choroko na dengu.

68. Mwaka 2019/20, vikao mbalimbali vya mashauriano na mafunzo vilifanyika kwa lengo la kuandaa miongozo na utaratibu utakaotumika kuuza mazao katika Soko la Bidhaa kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala. Vikao hivyo vilifanyika katika mikoa ya Mtwara, Pwani, Morogoro, Dodoma, Manyara, Singida, Mwanza, Shinyanga, Tabora, Katavi, Lindi, Ruvuma, na Simiyu. Elimu iliendelea kutolewa kwa wadau wengine kama Bodi za mazao, wafanyabiashara wa mazao ya kilimo, wadau wa mazao yakiwemo ya kimkakati na waendesha ghala.

69. Mwaka 2019/20, wakulima kupitia vyama vya ushirika waliwezeshwa kufanya mauzo kwa njia ya kielektroniki katika Soko la Bidhaa ambapo tani 19,790 za ufuta ziliuzwa na shilingi milioni 37,651 zililipwa kwa washiriki katika mikoa ya Mtwara, Pwani, Dodoma, Katavi, Morogoro, Manyara na Singida. Kwa upande mwingine, tani 19,868 za korosho ziliuzwa na shilingi milioni 42,507 zililipwa kwa washiriki wa mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma na Pwani. Aidha, tani 104 za dengu ziliuzwa na shilingi milioni 122.7 zililipwa kwa washiriki mkoani Shinyanga.

Jedwali Na. 17 **MWENENDO WA KARADHA NA UJAZI WA FEDHA - TANZANIA BARA**

| | Kipindi kinachoishia mwezi Desemba (Sh. Bilioni) | | | | | | Badiliko (2019-2020) | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **2015** | **2016** | **2017** | **2018** | **2019** | **2020** | **Kiasi** | **%** |
| **Fedha ya msingi (M0)** | **6,833.1** | **6,854.4** | **6,954.4** | **6,992.9** | **7,466.4** | **7,169.3** | **-297.1** | **-4.0** |
| **Ujazi wa fedha, kwa tafsiri finyu (M1)** | **9,575.7** | **10,083.8** | **11,155.3** | **11,723.7** | **13,325.1** | **14,321.7** | **996.6** | **7.5** |
| Amana za Akiba na za muda maalum | 6,204.4 | 6,536.5 | 7,194.6 | 7,316.7 | 7,955.1 | 8,711.0 | 755.9 | 9.5 |
| **Ujazi wa fedha, kwa tafsiri pana (M2)** | **15,780.1** | **16,620.3** | **18,349.9** | **19,040.4** | **21,280.3** | **23,032.6** | **1,752.3** | **8.2** |
| Amana za fedha za kigeni | 6,335.2 | 6257.5 | 6364.4 | 6783.1 | 7032.9 | 6,887.9 | -145.0 | -2.1 |
| **Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3)** | **22,115.3** | **22,877.8** | **24,714.3** | **25,823.5** | **28,313.1** | **29,918.2** | **1,605.1** | **5.7** |
| **Rasilimali halisi katika fedha za kigeni kwenye benki (Net foreign assets)** | **8,244.0** | **8186.3** | **11596.1** | **10629.8** | **12034.5** | **10,722.5** | **-1,312.0** | **-10.9** |
| Rasilimali halisi katika fedha za kigeni Benki Kuu | | | | 10,692.3 | 12,063.1 | 10,308.8 | -1,754.3 | -14.5 |
| Rasilimali halisi katika fedha za kigeni kwenye mabenki | | | | -62.5 | -28.5 | 413.8 | 442.3 | |
| **Rasilimali halisi katika fedha za ndani kwenye benki (Net domestic assets)** | **13,871.3** | **14,691.6** | **13,118.2** | **15,193.7** | **16,278.6** | **19,198.0** | **2,919.4** | **17.9** |
| Karadha Nchini | 22,505.5 | 23,775.8 | 24,977.2 | 26,249.3 | 28,103.3 | 26,139.6 | -1,963.7 | -7.0 |
| Madai halisi kwa serikali kuu | 4,881.6 | 4,282.0 | 3,275.7 | 4,481.6 | 3,893.9 | 5,831.3 | 1,937.4 | 49.8 |
| Mikopo kwa serikali kuu | 7,012.8 | 7,166.9 | 8,081.8 | 8,522.5 | 8,408.0 | 12,599.1 | 4,191.1 | 49.8 |
| Mikopo kwa sekta binafsi | 15,492.7 | 16608.9 | 16895.4 | 17726.8 | 19695.4 | 20,308.3 | 612.9 | 3.1 |
| Amana za Serikali zilizopo Benki Kuu na Benki za Biashara | 2131.1 | 2,884.9 | 4,806.1 | 4,040.9 | 4,514.1 | 6767.7 | 2,253.6 | 49.9 |
| Rasilimali nyinginezo (Other Items Net) | -6,503.1 | -6,199.3 | -7,052.9 | -7,014.7 | -7,310.7 | -6,941.6 | 369.1 | -5.0 |

**Chanzo**: Benki Kuu ya Tanzania

Jedwali 18 **VIWANGO VYA UKUAJI WA KARADHA NA UJAZI WA FEDHA - TANZANIA BARA**

| | Kipindi kinachoishia mwezi Desemba | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | **2015** | **2016** | **2017** | **2018** | **2019** | **2020** |
| **Fedha ya msingi (M0)** | **15.6%** | **0.3%** | **1.5%** | **0.6%** | **6.8%** | **-4.0%** |
| **Ujazi wa fedha, kwa tafsiri finyu (M1)** | **15.6%** | **5.3%** | **10.6%** | **5.1%** | **13.7%** | **7.5%** |
| Amana za Akiba na za muda maalum | 10.1% | 5.4% | 10.1% | 1.7% | 8.7% | 9.5% |
| **Ujazi wa fedha, kwa tafsiri pana (M2)** | **13.4%** | **5.3%** | **10.4%** | **3.8%** | **11.8%** | **8.2%** |
| Amana za fedha za kigeni | 34.9% | -1.2% | 1.7% | 6.6% | 3.7% | -2.1% |
| **Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3)** | **18.8%** | **3.4%** | **8.0%** | **4.5%** | **9.6%** | **5.7%** |
| **Rasilimali halisi katika fedha za kigeni kwenye benki (Net foreign assets)** | **25.8%** | **-0.7%** | **41.7%** | **-8.3%** | **13.2%** | **-10.9%** |
| **Rasilimali halisi katika fedha za ndani kwenye benki (Net domestic assets)** | **15.0%** | **5.9%** | **-10.7%** | **15.8%** | **7.1%** | **17.9%** |
| Karadha Nchini | 19.3% | 5.6% | 5.1% | 5.1% | 7.1% | -7.0% |
| Mikopo kwa serikali kuu | 8.7% | 2.2% | 12.8% | 5.5% | -1.3% | 49.80% |
| Mikopo kwa sekta Binafsi | 24.8% | 7.2% | 1.7% | 4.9% | 11.1% | 3.1% |
| Rasilimali nyinginezo (Other Items Net) | 62.5% | -4.7% | 13.8% | -0.5% | 4.2% | -5.0% |

**Chanzo**: Benki Kuu ya Tanzania

Jedwali Na.19 **MWENENDO WA VIWANGO VYA UBADILISHAJI KATI YA SHILINGI NA DOLA YA MAREKANI**

| | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Shs/Dola (mwisho wa mwaka) | 2,153.1 | 2,181.3 | 2,242.2 | 2,291.3 | 2,300.0 | 2,309.8 |
| Badiliko la thamani ya shilingi (%) | 24.9 | 1.3 | 2.8 | 2.2 | 0.4 | 0.4 |
| Shs/Dola (wastani wa mwaka) | 2,007.0 | 2,188.0 | 2,240.8 | 2,275.4 | 2,299.8 | 2,305.6 |
| Badiliko la wastani wa thamani ya shilingi (%) | 20.8 | 9.0 | 2.4 | 1.5 | 1.1 | 0.3 |

**Chanzo**: Benki Kuu ya Tanzania

Jedwali Na. 20 **MIKOPO YA BENKI ZA BIASHARA KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI**

| Aina ya Shughuli | Kipindi kinachoishia mwezi Desemba (Sh. Billioni) | | | | | | Ukuaji (%) | Mchango (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019[r] | 2020[p] | | |
| Uzalishaji katika Kilimo | 1,174 | 1,108 | 1,135 | 953 | 1,824 | 1,726 | -5.4 | 8.5 |
| Huduma za Kifedha | 405 | 389 | 292 | 173 | 202 | - | - | - |
| Madini na Uchimbaji Mawe | 275 | 329 | 293 | 375.2 | 425 | 429 | 1.1 | 2.1 |
| Viwanda | 1,696 | 1,628 | 1,778 | 1,938 | 2,087 | 1,878.4 | -10.0 | 9.3 |
| Majengo na Ujenzi | 741 | 741 | 837 | 643 | 1,130 | 1,072.3 | -5.1 | 5.3 |
| Uchukuzi na Mawasiliano | 1,232 | 1,181 | 976 | 930 | 1,060 | 1,142.4 | 7.8 | 5.6 |
| Biashara | 3,078 | 3,349 | 3,307 | 3,277 | 3,375 | 3,054.9 | -9.5 | 15.1 |
| Utalii | 177 | 198 | 176 | 141 | 144 | - | - | - |
| Mahoteli na Migahawa | 515 | 526 | 595 | 583 | 555 | 549.5 | -1.0 | 2.7 |
| Umeme | 440 | 430 | 335 | 356 | 225 | 114.7 | -49.1 | 0.6 |
| Watu Binafsi | 2,732 | 2,982 | 3,259 | 4,923 | 5,486 | 6,793.9 | 23.9 | 33.5 |
| Sekta Nyinginezo | 3,029 | 3,749 | 3,913 | 3,451 | 3,525 | 3,530.4 | 0.2 | 17.4 |
| **Jumla** | **15,492.7** | **16,608.9** | **16,895.4** | **17,741.2** | **20,036.5** | **20,291.4** | **1.3** | **100.0** |

**Chanzo**: Benki Kuu ya Tanzania
r - Takwimu zimeboreshwa
- Takwimu hazikupatikana

Jedwali Na. 21 **MWENENDO WA AMANA KATIKA BENKI ZA BIASHARA** Sh. Billioni

| | Kipindi Kinachoishia mwezi Desemba | | | | | | Badiliko% | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **2015** | **2016** | **2017** | **2018** | **2019** | **2020** | **2019** | **2020** |
| **Amana za Sekta Binafsi** | | | | | | | | |
| Amana za Hundi/Zinazaohamishika | 5,772.1 | 5,941.5 | 6,685.3 | 7,031.7 | 7,866.5 | 8,117.1 | 11.9 | 3.2 |
| Amana za Akiba na za Muda Maalum | 6,086.8 | 6,415.6 | 7,052.2 | 7,154.7 | 7,750.4 | 8,510.0 | 8.3 | 9.8 |
| Amana za fedha za kigeni | 6,301.8 | 5,831.5 | 6,087.1 | 6,376.3 | 6,160.6 | 6,442.2 | -3.4 | 4.6 |
| **Jumla** | **18,160.7** | **18,188.7** | **19,824.6** | **20,562.8** | **21,777.5** | **23,069.2** | **5.9** | **5.9** |
| Amana za Serikali | 857.0 | 577.8 | 560.6 | 358.5 | 981.3 | 652.9 | - | -33.5 |
| **Jumla za Amana zote** | **19,017.7** | **18,766.5** | **20,385.1** | **20,921.3** | **22,758.9** | **23,722.1** | **8.8** | **4.2** |

**Chanzo**: Benki Kuu ya Tanzania

Jedwali Na. 22 **VIWANGO VYA WASTANI WA RIBA** Asilimia

| **Aina ya Riba** | **2015** | **2016** | **2017** | **2018** | **2019** | **2020** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Riba ya Benki kuu (Discount rate) | 16.00 | 16.00 | 16.00 | 7.00 | 7.00 | 5.00 |
| Riba katika soko la fedha kati ya benki za biashara kwa ujumla | 11.23 | 13.47 | 6.00 | 2.21 | 5.13 | 4.50 |
| Riba za dhamana za serikali kwa ujumla | 12.91 | 16.17 | 11.10 | 6.43 | 7.71 | 4.42 |
| Siku 91 | 8.80 | 7.85 | 5.49 | 2.89 | 4.17 | 2.37 |
| Siku 182 | 13.04 | 15.84 | 10.01 | 4.13 | 5.07 | 2.88 |
| Siku 364 | 13.92 | 16.56 | 11.79 | 7.08 | 8.04 | 2.32 |
| **Riba za hati fungani** | | | | | | |
| Miaka miwili | 14.78 | 17.44 | 14.52 | 9.42 | 11.45 | 8.14 |
| Miaka mitano | 15.15 | 17.79 | 15.78 | 11.64 | 12.56 | 11.24 |
| Miaka saba | 16.60 | 17.69 | 16.31 | 12.62 | 13.09 | 11.48 |
| Miaka kumi | 17.14 | 18.11 | 16.79 | 14.39 | 15.04 | 12.51 |
| Miaka kumi na tano | 17.71 | 18.85 | 17.54 | 14.69 | 15.52 | 14.05 |
| Miaka ishirini | | | | 17.70 | 17.35 | 15.79 |
| **Riba za amana** | | | | | | |
| Amana za akiba | 3.45 | 3.35 | 3.03 | 2.52 | 2.44 | 2.34 |
| Amana za muda maalum kwa ujumla | 8.89 | 9.19 | 10.04 | 8.24 | 7.25 | 6.70 |
| Mwaka mmoja | 10.80 | 11.47 | 11.66 | 8.78 | 8.80 | 8.28 |
| **Riba za mikopo** | | | | | | |
| Mikopo kwa ujumla | 16.10 | 15.96 | 17.77 | 17.43 | 16.97 | 16.66 |
| Mikopo ya muda mfupi hadi mwaka mmoja | 14.25 | 13.66 | 18.30 | 18.25 | 16.69 | 15.73 |

**Chanzo:** Benki Kuu ya Tanzania

## SURA YA 3

## FEDHA ZA SERIKALI

**Utangulizi**

70. Bajeti ya mwaka 2020/21 ilizingatia vipaumbele vilivyoainishwa katika Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 - 2020/21 wenye dhima ya **“kujenga uchumi wa viwanda utakaochochea ajira na ustawi endelevu wa jamii”**. Licha ya kuwepo kwa athari za mvua nyingi na mlipuko wa janga la UVIKO-19, bajeti ilizingatia fursa zilizoibuka ikiwemo kushuka kwa bei za mafuta, kuongezeka kwa bei ya dhahabu na mwanya wa kuzalisha vifaa na vifaa tiba katika viwanda vya ndani ili kukabiliana na janga la UVIKO - 19. Aidha, kama ilivyo kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, dhima ya bajeti ya 2020/21 ilikuwa ni “**kuchochea ukuaji wa uchumi ili kulinda na kuboresha maisha ya wananchi, ajira na biashara pamoja na kufufua viwanda**”.

71. Bajeti ya mwaka 2020/21 ambayo ni ya mwisho katika utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21 ilipanga kutekeleza vipaumbele vifuatavyo: Kukarabati miundombinu iliyoharibiwa na mvua zilizozidi wastani pamoja na kupambana na janga la UVIKO-19; kuendelea kugharamia utekelezaji wa miradi ya kitaifa ya kimkakati ikiwemo ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa (*Standard Gauge Railway - SGR*), Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere - MW 2,115 na kuboresha Shirika la Ndege Tanzania; kuboresha upatikanaji wa huduma za afya, elimu na ujuzi pamoja na huduma za majisafi na majitaka; kuendeleza ujenzi wa msingi wa uchumi wa viwanda; kuendelea kuboresha mazingira wezeshi ya uendeshaji biashara na uwekezaji nchini; na kuboresha maisha ya wananchi wa hali ya chini kwa kuendelea na utekelezaji wa mpango wa kunusuru kaya maskini kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

72. Shabaha za bajeti ya mwaka 2020/21 zililenga: kuwa na ukuaji wa Pato halisi la Taifa wa asilimia 5.5 mwaka 2020; kuendelea kudhibiti mfumuko wa bei kuwa katika wigo wa tarakimu moja kati ya asilimia 3.0 hadi 4.5 katika kipindi cha muda wa kati; mapato ya ndani ikijumuisha mapato ya halmashauri kuwa asilimia 14.7 ya Pato la Taifa; mapato ya kodi kufikia asilimia 12.9 ya Pato la Taifa; matumizi ya Serikali kufikia asilimia 22.1 ya Pato la Taifa; nakisi ya bajeti kufikia asilimia 2.6 ya Pato la Taifa; na kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4).

73. Mwaka 2020/21, Serikali ilitarajia kukusanya jumla ya shilingi bilioni 34,879.8 kutoka vyanzo vya ndani na nje. Jumla ya mapato ya ndani ikijumuisha mapato ya Halmashauri yalitarajiwa kuwa shilingi bilioni 24,065.5, sawa na asilimia 69.0 ya bajeti

yote. Kati ya mapato ya ndani, mapato ya kodi yalikadiriwa kuwa shilingi bilioni 20,325.8, sawa na asilimia 12.9 ya Pato la Taifa. Mapato yasiyo ya kodi yalikadiriwa kuwa shilingi bilioni 2,924.8 na mapato kutoka vyanzo vya Halmashauri shilingi bilioni 815.0. Misaada na mikopo nafuu kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ilikadiriwa kuwa shilingi bilioni 2,874.4, sawa na asilimia 8.2 ya bajeti yote. Aidha, Serikali ilitarajia kukopa shilingi bilioni 4,904.2 kutoka soko la ndani na shilingi bilioni 3,035.4 kutoka soko la nje kwa masharti ya kibiashara.

**Mwenendo wa Mapato**

**Mapato ya Ndani**

74. Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, makusanyo ya ndani yalifikia shilingi bilioni 15,467.8, sawa na asilimia 86.7 ya lengo la kipindi hicho la shilingi bilioni 17,832.3. Kati ya mapato hayo; mapato yaliyokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania yalifikia shilingi bilioni 13,274.3, sawa na asilimia 87.4 ya lengo la shilingi bilioni 15,183.8; makusanyo ya maduhuli yalifikia shilingi bilioni 1,622.7, sawa na asilimia 80.1 ya lengo la shilingi bilioni 2,026.7; na mapato kutoka vyanzo vya Halmashauri yalifikia shilingi bilioni 570.8, sawa na asilimia 91.8 ya lengo la shilingi bilioni 621.8. Kutofikiwa kwa malengo ya mapato ya ndani kulichangiwa na: ukwepaji kodi unaofanywa na wafanyabiashara wasio waaminifu ikiwa ni pamoja na kuingiza bidhaa nchini kwa njia za magendo na kutotoa stakabadhi za kielektroniki wanapofanya mauzo; na athari za mlipuko wa UVIKO-19 ulioenea Duniani kote na kuathiri mapato yatokanayo na biashara na huduma, hususan utalii, uhamiaji na ushuru wa forodha.

**Misaada na Mikopo Nafuu**

75. Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, misaada na mikopo nafuu iliyopokelewa kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ilikuwa shilingi bilioni 1,680.6, sawa na asilimia 75.2 ya lengo la kipindi hicho. Kati ya kiasi hicho, misaada na mikopo nafuu ya kibajeti ilikuwa shilingi bilioni 210.5 ikiwa ni asilimia 232.2 ya makadirio ya kipindi hicho; mifuko ya kisekta shilingi bilioni 199.1, sawa na asilimia 82.5 ya makadirio katika kipindi hicho; na miradi ya maendeleo shilingi bilioni 1,270.7, sawa na asilimia 66.8 ya makadirio. Kutofikiwa kwa lengo la misaada na mikopo nafuu kulitokana na kuchelewa kusainiwa kwa makubaliano kati ya Serikali na Washirika wa Maendeleo (*Side Agreement*) kulikosababishwa na changamoto za kufungwa kwa baadhi ya ofisi za Washirika wa Maendeleo kufuatia mlipuko wa UVIKO-19.

**Mikopo ya Ndani**

76. Hadi Machi 2021, Serikali ilikopa jumla ya shilingi bilioni 3,488.7 kutoka soko la ndani, sawa na asilimia 71.1 ya shilingi bilioni 4,904.2 zilizopangwa kukopwa mwaka 2020/21. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 2,266.9 zilikopwa kwa ajili ya kulipia hati fungani na dhamana za Serikali zilizoiva na shilingi bilioni 1,221.8 zilikopwa kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo.

**Mikopo yenye Masharti ya Kibiashara**

77. Mwaka 2020/21, Serikali ilipanga kukopa shilingi bilioni 3,035.6 kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo. Hadi Machi 2021, Serikali ilikopa shilingi bilioni 1,138.8, sawa na asilimia 37.5 ya lengo la mwaka. Hii ilitokana na uhaba wa mikopo katika masoko ya fedha ya kimataifa uliochangiwa na athari za janga la UVIKO-19. Aidha, kiasi kilichobaki kinatarajiwa kukopwa katika kipindi cha robo ya nne (4) ya mwaka 2020/21.

**Mwenendo wa Matumizi**

78. Mwaka 2020/21, sera za matumizi ya Serikali zililenga: Kuendelea kusimamia nidhamu ya matumizi ya fedha za umma kwa kudhibiti matumizi yasiyo ya lazima; kuhakikisha nakisi ya bajeti haizidi asilimia 3.0 ya Pato la Taifa kuendana na makubaliano ya Jumuiya ya Afrika Mashariki; kuelekeza fedha kwenye maeneo ya kipaumbele yatakayochochea ukuaji wa uchumi; kuhakikisha miradi inayoendelea inapewa kipaumbele kabla ya miradi mipya; kudhibiti ulimbikizaji wa madai; na kuongeza kasi ya matumizi ya TEHAMA katika miamala na shughuli za Serikali. Katika kuhakikisha malengo ya sera hizo yanafikiwa, bajeti ya mwaka 2020/21 ililenga kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2020/21 ikiwa ni pamoja na: Kukarabati miundombinu iliyoharibiwa na mvua zilizozidi wastani na kupambana na janga la UVIKO-19; kuendelea kutekeleza miradi ya kielelezo; kuboresha huduma za jamii; na kuendeleza ujenzi wa msingi wa uchumi wa viwanda.

79. Mwaka 2020/21, Serikali ilikadiria kutumia jumla ya shilingi bilioni 34,879.8 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 22,100.5 zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikiwa ni asilimia 63.0 ya bajeti na shilingi bilioni 12,779.3 zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo, sawa na asilimia 37.0 ya bajeti. Aidha, katika bajeti ya fedha za maendeleo, kiasi cha shilingi bilioni 10,043.2 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 2,736.0 ni fedha za nje.

80. Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, ridhaa ya matumizi iliyotolewa ilikuwa shilingi bilioni 22,263.3, sawa na asilimia 88.5 ya lengo la kipindi hicho. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 15,692.4 ilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 6,570.9 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo, ambapo shilingi bilioni 5,014.6 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 1,556.3 ni fedha za nje. Kiasi kilichotolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida kinajumuisha malipo ya riba kwa madeni ya ndani na nje ya shilingi bilioni 1,836.0, sawa na asilimia 93.1 ya makadirio ya shilingi bilioni 1,972.3. Aidha, malipo ya mtaji kwa deni la ndani na nje yalifikia shilingi bilioni 4,305.4, sawa na asilimia 100 ya lengo. Kati ya malipo hayo, shilingi bilioni 2,675.6 ilikuwa ni kwa ajili ya malipo ya dhamana na amana za Serikali zilizoiva. Matumizi mengine ya Mfuko Mkuu yalikuwa shilingi bilioni 1,196.7.

81. Matumizi ya kawaida yanajumuisha pia malipo ya mishahara ya watumishi wa Serikali kiasi cha shilingi bilioni 5,489.1, sawa na asilimia 94.4 ya lengo la kipindi hicho la shilingi bilioni 5,815.5. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 1,890.9 zililipwa kwa watumishi wa Serikali Kuu, shilingi bilioni 52.6 kwa watumishi wa Sekretarieti za Mikoa na shilingi bilioni 2,649.5 kwa watumishi wa Halmashauri za Majiji, Manispaa, Miji na Wilaya. Aidha, Serikali ililipa mishahara ya Taasisi na Mashirika ya Umma jumla ya shilingi bilioni 896.1.

82. Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, Serikali ilipanga kutumia jumla ya shilingi bilioni 8,867.8 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali. Kati ya hizo, shilingi bilioni 6,725.3 zilikuwa fedha za ndani na shilingi bilioni 2,142.5 fedha za nje. Hadi Machi 2021, ridhaa ya matumizi ya fedha za maendeleo kiasi cha shilingi bilioni 6,570.9 ilitolewa, sawa na asilimia 74.1 ya makadirio. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 5,014.6 zilikuwa fedha za ndani na shilingi bilioni 1,556.3 fedha za nje. Kutofikiwa kwa malengo ya utoaji wa fedha za maendeleo kulitokana na kutofikiwa kwa malengo ya upatikanaji wa mapato kama ilivyokadiriwa.


83. Baadhi ya mahitaji yaliyopewa kipaumbele zaidi katika utoaji wa fedha za matumizi ya maendeleo katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021 ni pamoja na: Utekelezaji wa miradi ya miundombinu ya barabara, reli na viwanja vya ndege ambapo jumla ya shilingi trilioni 2.21 zilitolewa; Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere shilingi bilioni 481.2; ulipaji wa madeni yaliyohakikiwa ya Wakandarasi na Washauri Elekezi shilingi bilioni 301.3; kugharamia Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 jumla ya shilingi bilioni 268.5; kuendelea na Awamu ya Tatu ya Mradi wa Kupeleka Umeme Vijijini kupitia Wakala wa Nishati Vijijini shilingi bilioni 256.5; kugharamia elimumsingi bila ada shilingi bilioni 187.2; utekelezaji wa miradi ya maji mijini na vijijini shilingi bilioni 150.2; kugharamia mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu shilingi bilioni 138.1; ununuzi wa ndege mpya na uimarishaji wa Shirika la Ndege la Tanzania shilingi bilioni 31.6; uimarishaji wa vyuo vya VETA na kukuza ujuzi kwa vijana shilingi bilioni 31.1; kuendeleza ujenzi na ukarabati wa meli katika maziwa makuu shilingi bilioni 26.3; na kugharamia shughuli za Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo shilingi bilioni 11.

**Deni la Serikali**

84. Hadi Machi 2021, Deni la Serikali lilikuwa shilingi bilioni 59,852.6 ikilinganishwa na shilingi bilioni 54,976.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 8.9. Kati ya kiasi hicho, deni la ndani lilikuwa shilingi bilioni 16,116.5 na deni la nje lilikuwa shilingi bilioni 43,736.1. Ongezeko la deni lilitokana na kupokelewa kwa mikopo mipya kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo. Vile vile, ongezeko hilo lilichangiwa na malimbikizo ya riba

ya deni la nje, hususan kwa nchi zisizo wanachama wa kundi la Klabu ya Paris. **Kielelezo Na. 3.1** kinaonesha mwenendo wa Deni la Serikali.

**Kielelezo Na. 3.1: Mwenendo wa Deni la Serikali kwa kipindi cha Machi 2012 - Machi 2021 (Shilingi Bilioni)**




**Deni la Nje**

85. Hadi Machi 2021, Deni la Serikali la Nje lilikuwa dola za Marekani milioni 18,933.7 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 17,488.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 8.3. Ongezeko hilo lilitokana na kupokelewa kwa mikopo mipya kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo.

**Deni la Nje kwa Wakopeshaji**

86. Hadi Machi 2021, mchanganuo wa deni la nje ulionesha kuwa, mashirika ya fedha ya kimataifa yalichangia asilimia 58.7 ya deni la nje ikilinganishwa na asilimia 57.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Aidha, Benki za Kibiashara zilichangia asilimia 29.7 na nchi wahisani zilichangia asilimia 11.6 ya deni lote la nje. **Jedwali Na. 3.1** linaonesha mchanganuo wa deni la nje kwa wakopeshaji. Kwa upande mwingine, kati ya kiasi chote cha deni la nje, mikopo nafuu ilichangia dola za Marekani milioni 13,316.4 sawa na asilimia 70.3 na mikopo yenye masharti ya kibiashara ilichangia dola za Marekani milioni 5,617.3 sawa asilimia 29.7.

**Jedwali Na. 3.1: Mchanganuo wa Deni la Nje kwa Wakopeshaji (Dola za Marekani Milioni)**


| Taasisi | Machi 2019 | Mchango kwa asilimia | Machi 2020 | Mchango kwa asilimia | Machi 2021 | Mchango kwa asilimia |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mashirika ya Fedha | 9,561.9 | 58.2 | 10,091.5 | 57.7 | 11,121.7 | 58.7 |
| Washirika wa Mendeleo | 1,930.8 | 11.9 | 2,038.5 | 11.7 | 2,194.7 | 11.6 |
| Benki za kibiashara | 4,865.8 | 29.9 | 5,358.2 | 30.6 | 5,617.3 | 29.7 |
| **Jumla** | **16,358.6** | **100.0** | **17,488.2** | **100.0** | **18,933.7** | **100.0** |

**Chanzo**: Wizara ya Fedha na Mipango

## Deni la Ndani

87. Hadi Machi 2021, deni la ndani lilikuwa shilingi bilioni 16,116.5 ikilinganishwa na shilingi bilioni 14,730.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 9.4. Ongezeko hilo lilitokana na Serikali kuendelea kukopa kutoka kwenye soko la ndani ili kulipa mikopo ya ndani iliyoiva pamoja na kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo. Aidha, sehemu kubwa ya deni la ndani ilikuwa ni mikopo ya hati fungani ambayo ilikuwa ni asilimia 81.4 ya deni lote la ndani ikifuatiwa na dhamana za Serikali za muda mfupi asilimia 9.5, hati fungani maalum asilimia 7.6 na madeni mengine asilimia 1.5. **Kielelezo Na. 3.2** kinaonesha mwenendo wa madeni ya ndani.

**Kielelezo Na. 3.2: Mwenendo wa Deni la Ndani (Shilingi Bilioni)**




## Deni la Ndani kwa Wakopeshaji

88. Hadi Machi 2021, benki za biashara ziliongoza kwa kuhodhi asilimia 39.2 ya deni la ndani ikilinganishwa na asilimia 40.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Aidha, mifuko ya hifadhi ya jamii ilihodhi asilimia 34.3 ikifuatiwa na kampuni za bima asilimia 9.7. **Jedwali Na. 3.2** linaonesha mchanganuo wa deni la ndani kwa wakopeshaji.

**Jedwali Na. 3.2: Mchanganuo wa Deni la Ndani kwa Wakopeshaji hadi Machi 2021 (Shilingi Bilioni)**

| Taasisi | Machi 2019 | Mchango kwa asilimia | Machi 2020 | Mchango kwa asilimia | Machi 2021 | Mchango kwa asilimia |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Benki za Biashara | 4,866.3 | 42.4 | 5,346.5 | 40.7 | 5,600.7 | 39.2 |
| Taasisi za Fedha | 139.0 | 1.2 | 189.5 | 1.4 | 79.8 | 0.6 |
| Mifuko ya Jamii | 3,782.1 | 32.9 | 4,318.3 | 32.9 | 4,908.9 | 34.3 |
| Kampuni za Bima | 1,310.6 | 11.4 | 1,305.3 | 10 | 1,383.3 | 9.7 |
| Taasisi za Kigeni | 502.4 | 4.4 | 877.2 | 6.7 | 967.7 | 6.8 |
| Mashirika Madogo | 230.3 | 2 | 296.6 | 2.3 | 429.7 | 3 |
| Watu binafsi | 656.9 | 5.7 | 790.7 | 6 | 926.2 | 6.5 |
| **Jumla** | **11,487.6** | **100** | **13,278.6** | **100** | **14,296.4** | **100** |

**Chanzo:** Wizara ya Fedha na Mipango

**Tathmini ya Uhimilivu wa Deni**

89. Tathmini ya Uhimilivu wa Deni ilifanyika Desemba 2020 kwa kuzingatia vigezo vya uhimilivu ambavyo ni uwiano wa deni halisi kwa Pato la Taifa, uwiano wa deni halisi kwa malipo ya nje na uwiano wa malipo ya deni kwa mapato ya ndani na mapato yatokanayo na mauzo ya nje. Matokeo ya tathmini hiyo yalionesha kuwa deni ni himilivu kwa kipindi cha muda mfupi, wa kati na mrefu. Tathmini hiyo ilionesha kuwa: Thamani ya deni la nje kwa Pato la Taifa ni asilimia 17.3 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 55; thamani ya deni la nje kwa mauzo ya nje ni asilimia 113.2 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 240 na ulipaji wa deni la nje kwa kutumia mapato ya ndani ni asilimia 13.7 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 23. Matokeo hayo yanamaanisha kuwa nchi ina uwezo wa kukopa nje na ndani na kulipa mikopo hiyo kadiri inavyoiva bila kuleta athari kwenye ukuaji wa uchumi. Hali hii ya uhimilivu wa deni inatokana na Serikali kusimamia kwa karibu mchakato mzima wa ukopaji na kuhakikisha kuwa mikopo inaelekezwa kwenye miradi inayochochea ukuaji wa uchumi na kuzalisha mapato. **Jedwali Na. 3.3** linaonesha viashiria vya uhimilivu wa deni la Serikali

**Jedwali Na.3.3: Tathmini ya Viashiria vya Deni la Taifa**

| **Viashiria vya deni la nje** | **2020/21** | **2021/22** | **2022/23** | **2023/24** | **2024/25** | **2030/31** | **2040/41** | **Ukomo** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Deni (PV(1))/Pato la Taifa | 17.3 | 17.5 | 17.9 | 17.9 | 17.2 | 14.0 | 7.2 | 55 |
| Deni (PV)/uuzaji wa bidhaa nje | 113.2 | 109.7 | 103.5 | 94.3 | 87.9 | 68.0 | 34.9 | 240 |
| Ulipaji wa deni la nje/Uuuzaji wa bidhaa nje | 14.0 | 13.4 | 10.6 | 10.3 | 10.9 | 11.1 | 7.0 | 21 |
| Ulipaji wa deni /Mapato ya ndani | 13.7 | 13.8 | 11.8 | 12.5 | 13.3 | 14.1 | 8.3 | 23 |
| **Viashiria vya deni la nje na ndani** | **2020/21** | **2021/22** | **2022/23** | **2023/24** | **2024/25** | **2030/31** | **2040/41** | **Ukomo** |
| Deni (PV)/ Pato la Taifa | 27.9 | 27.7 | 27.9 | 28.0 | 27.8 | 33.1 | 19.0 | 70 |
| Deni (PV)/ Mapato ya ndani | 171.1 | 172.0 | 173.6 | 174.7 | 173.7 | 202.5 | 110.0 | - |
| Ulipaji wa deni/ Mapato ya ndani | 34.5 | 31.6 | 29.4 | 24.6 | 29.0 | 44.3 | 29.5 | - |

**Chanzo:** Wizara ya Fedha na Mipango

## MWENENDO WA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI


Jedwali Na. 23

**Shilingi milioni**

| | 2017/18 Halisi | 2018/19 Halisi | 2019/20 Halisi | 2020/21 Bajeti | 2020/21 Matokeo hadi Machi | 2020/21 Matarajio hadi Juni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| A. MAPATO YA NDANI (yakijumuisha Halmashauri) | 17,944,886.98 | 18,529,558.0 | 21,069,956.8 | 24,065,543.3 | 15,467,777.8 | 21,441,795.3 |
| MAPATO YA NDANI | 17,403,387.93 | 17,868,195.0 | 20,352,708.1 | 23,250,582.3 | 14,897,008.3 | 20,697,192.6 |
| 1. Mapato yatokanayo na Kodi | 15,191,421.33 | 15,511,330.1 | 17,622,822.1 | 20,325,779.3 | 13,274,264.8 | 18,416,133.2 |
| Ushuru wa Forodha na Excise Duty | 3,313,671.46 | 3,585,509.0 | 3,781,641.1 | 4,613,657.1 | 3,037,408.9 | 4,195,777.3 |
| Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) | 4,478,850.59 | 4,781,633.0 | 5,184,322.0 | 6,146,401.4 | 3,870,507.4 | 5,446,669.6 |
| Bidhaa toka nje | 2,054,675.39 | 2,259,827.4 | 2,421,392.8 | 2,875,319.5 | 1,820,931.5 | 2,557,214.6 |
| Bidhaa za ndani | 2,424,175.20 | 2,521,805.6 | 2,762,929.2 | 3,271,081.8 | 2,049,575.9 | 2,889,455.1 |
| Kodi ya Mapato | 5,157,886.30 | 5,148,191.5 | 6,523,795.2 | 7,200,183.7 | 4,534,932.8 | 6,678,667.0 |
| Kodi nyingine | 2,299,242.38 | 2,130,594.5 | 2,379,568.6 | 2,773,280.3 | 1,938,656.6 | 2,315,000.2 |
| Marejesho (Refunds Accounts) | (58,229.40) | (134,597.9) | (246,504.8) | (407,743.1) | (107,240.9) | (219,981.0) |
| 2. Mapato yasiyotokana na Kodi | 2,211,966.60 | 2,356,864.9 | 2,729,886.0 | 2,924,802.9 | 1,622,743.5 | 2,281,059.4 |
| 3. Mapato ya Halmashauri | 541,499.05 | 661,363.0 | 717,248.7 | 814,961.0 | 570,769.5 | 744,602.7 |
| B. JUMLA YA MATUMIZI | 20,468,072.32 | 22,300,627.4 | 23,509,931.6 | 29,100,434.0 | 17,449,865.6 | 24,450,598.5 |
| 1. Matumizi ya Kawaida | 12,852,304.02 | 13,806,788.9 | 14,201,147.8 | 16,321,179.0 | 10,516,839.3 | 15,505,120.0 |
| 2. Matumizi ya Maendeleo | 7,615,768.31 | 8,493,838.5 | 9,308,783.8 | 12,779,255.0 | 6,933,026.3 | 8,945,478.5 |
| Fedha za ndani | 5,397,033.55 | 6,535,879.2 | 6,840,103.8 | 10,043,206.1 | 5,376,763.5 | 7,030,244.3 |
| Fedha za nje | 2,218,734.76 | 1,957,959.3 | 2,468,679.9 | 2,736,048.9 | 1,556,262.8 | 1,915,234.2 |
| C. NAKISI/SALIO (A-B) | (2,523,185.35) | (3,771,069.4) | (2,439,974.8) | (5,034,890.7) | (1,982,087.8) | (3,008,803.2) |
| D. KUZIBA NAKISI | 2,523,185.35 | 3,771,069.4 | 2,439,974.8 | 5,034,890.7 | 1,982,087.8 | 3,008,803.2 |
| 1. Fedha kutoka nje | 2,461,430.08 | 1,743,562.6 | 3,353,986.9 | 3,446,721.5 | 1,307,748.2 | 2,695,518.2 |
| Ruzuku | 882,391.98 | 707,797.3 | 746,757.2 | 752,784.2 | 363,860.3 | 498,561.2 |
| Basket support | 117,166.12 | 181,377.8 | 181,091.0 | 196,538.3 | 147,524.4 | 68,617.6 |
| Mikopo ya uagizaji bidhaa/OGL | 74,680.98 | 169,677.0 | 292,121.2 | 79,004.6 | 262,098.1 | 262,098.1 |
| Mikopo ya miradi | 1,220,480.55 | 1,115,041.4 | 2,340,231.7 | 1,846,045.1 | 906,794.7 | 1,293,891.9 |
| Mikopo ya masharti ya kibiashara | 1,474,281.58 | 1,144,822.3 | 1,822,093.1 | 3,035,630.0 | 1,138,831.7 | 3,035,630.0 |
| Kulipia madeni ya nje (Amortization Foreign) | (1,307,571.11) | (1,575,153.1) | (2,028,307.3) | (2,463,280.6) | (1,511,361.0) | (2,463,280.6) |
| 2. Fedha za Ndani | 61,755.26 | 2,027,506.8 | (914,012.1) | 1,588,169.2 | 674,339.6 | 313,285.0 |
| Mikopo isiyo ya mabenki | (343,325.54) | 653,774.1 | 781,780.6 | 168,258.2 | 956,254.9 | 168,258.2 |
| Mikopo ya mabenki | 941,973.00 | 2,383,403.3 | (404,856.6) | 1,419,911.0 | (45,379.8) | 1,419,911.0 |
| Mikopo ya ndani (Rollover) | 4,835,199.26 | 3,718,008.3 | 3,976,811.2 | 3,316,078.4 | 2,675,630.5 | 3,316,078.4 |
| Marekebisho (Adjustment to Cash) | (465,124.32) | (1,009,670.7) | (1,275,185.8) | | (229,217.4) | (1,267,566.2) |
| Kulipia madeni ya ndani (amortization) | (4,835,199.26) | (3,718,008.3) | (3,976,811.2) | (3,316,078.4) | (2,675,630.5) | (3,316,078.4) |
| Expenditure float | (71,767.88) | - | (15,750.3) | - | (7,318.0) | (7,318.0) |

Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

**Kielelezo Na. 3.3: MWENENDO WA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI**




**Chanzo:** Wizara ya Fedha na Mipango

**Jedwali Na. 24** **MGAWANYO WA MATUMIZI YA SERIKALI KWA HUDUMA ZA SERIKALI** **Sh. Milioni**

| Fungu | Maelezo | 2019/2020 (Halisi) | | | 2020/2021 (Bajeti) | | | 2021/2022 (Makadirio) | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Matumizi ya Kawaida | Matumizi ya Maendeleo | Jumla | Matumizi ya Kawaida | Matumizi ya Maendeleo | Jumla | Matumizi ya Kawaida | Matumizi ya Maendeleo | Jumla |
| **701** | **Huduma za Kawaida** | **11,786,405** | **893,035** | **12,679,440** | **13,513,521** | **2,061,540** | **15,575,062** | **13,800,690** | **2,618,461** | **16,419,152** |
| 70111 | Utawala na Shughuli za Bunge | 900,945 | 46,962 | 947,907 | 836,974 | 85,135 | 922,109 | 928,945 | 61,234 | 990,179 |
| 70112 | Fedha na Masuala ya Kodi | 390,374 | 15,376 | 405,750 | 941,138 | 601,487 | 1,542,624 | 952,180 | 788,228 | 1,740,408 |
| 70113 | Mambo ya Nje | 97,736 | 0 | 97,736 | 156,469 | 0 | 156,469 | 159,815 | 0 | 159,815 |
| 70121 | Misaada ya Kiuchumi kutoka Nje | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70122 | Misaada ya Kiuchumi kupitia Mashirika ya Kimataifa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70131 | Huduma za Umma | 74,247 | 3,306 | 77,553 | 112,645 | 12,688 | 125,333 | 52,165 | 10,030 | 62,194 |
| 70132 | Huduma za Mipango na Takwimu | 417,325 | 257,423 | 674,748 | 421,000 | 402,718 | 823,718 | 437,849 | 830,655 | 1,268,503 |
| 70133 | Huduma nyingine za Kawaida | 83,356 | 297,936 | 381,292 | 104,045 | 544,380 | 648,425 | 120,421 | 601,141 | 721,561 |
| 70140 | Utafiti wa Msingi | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70150 | Utafiti na Maendeleo Huduma za Umma | 323 | 68 | 391 | 532 | 20,100 | 20,632 | 270 | 15,300 | 15,570 |
| 70160 | Huduma za Umma zisizotajwa hapo Juu | 12,634 | 161,172 | 173,805 | 11,953 | 187,030 | 198,983 | 13,872 | 11,692 | 25,564 |
| 70170 | Deni la Taifa | 9,394,345 | 0 | 9,394,345 | 10,487,787 | 0 | 10,487,787 | 10,673,518 | 0 | 10,673,518 |
| 70180 | Uhamishaji Fedha Ndani ya Serikali | 415,120 | 110,792 | 525,912 | 440,978 | 208,002 | 648,981 | 461,656 | 300,183 | 761,839 |
| **702** | **Ulinzi** | **2,024,941** | **110790** | **2,135,731** | **1,956,294** | **128,400** | **2,084,694** | **2,160,844** | **133,928** | **2,294,773** |
| 70210 | Huduma za Ulinzi wa Kijeshi | 2,024,747 | 2515 | 2,027,263 | 1,955,986 | 14,000 | 1,969,986 | 2,160,536 | 36,578 | 2,197,115 |
| 70220 | Huduma za Ulinzi wa Kiraia | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70230 | Misaada ya Nje ya Ulinzi | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70240 | Utafiti na Maendeleo ya Ulinzi | 194 | 108274 | 108,469 | 308 | 114,400 | 114,708 | 308 | 97,350 | 97,658 |
| 70250 | Huduma za Ulinzi zisizotajwa hapo Juu | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **703** | **Usalama wa Raia** | **923,458** | **40,904** | **964,362** | **831,089** | **104,856** | **935,946** | **832,573** | **68,604** | **901,176** |
| 70310 | Huduma za Polisi | 662,999 | 0 | 662,999 | 562,091 | 2,034 | 564,125 | 319,072 | 2,000 | 321,072 |
| 70320 | Huduma za Zimamoto | 32,315 | 737 | 33,052 | 35,100 | 3,500 | 38,600 | 36,604 | 3,500 | 40,104 |
| 70330 | Mahakama | 133,905 | 31,232 | 165,137 | 167,792 | 73,871 | 241,662 | 191,413 | 45,184 | 236,597 |
| 70340 | Magereza | 80,187 | 269 | 80,456 | 46,511 | 14,590 | 61,101 | 43,001 | 7,840 | 50,841 |
| 70350 | Huduma za utafiti na Maendeleo Usalama wa Raia | 40 | 0 | 40 | 64 | 0 | 64 | 79 | 0 | 79 |
| 70360 | Huduma Usalama wa Raia zisizotajwa hapo juu | 14,012 | 8,665 | 22,677 | 19,532 | 10,862 | 30,394 | 242,404 | 10,080 | 252,484 |
| **704** | **Shughuli za Kiuchumi** | **389,568** | **4,910,977** | **5,300,545** | **438,928** | **7,227,791** | **7,666,719** | **792,133** | **6,552,199** | **7,344,332** |
| 70411 | Shughuli za Kiuchumi na Biashara | 12,203 | 109,425 | 121,628 | 8,405 | 163,964 | 172,369 | 11,950 | 148,724 | 160,674 |
| 70412 | Masuala ya Kazi | 7,466 | 17,085 | 24,551 | 9,251 | 10,165 | 19,416 | 9,055 | 12,058 | 21,113 |
| 70421 | Kilimo | 119,427 | 33,543 | 152,970 | 138,758 | 135,881 | 274,639 | 153,079 | 88,839 | 241,918 |
| 70422 | Misitu | 19,260 | 502 | 19,762 | 19,964 | 13,641 | 33,605 | 23,000 | 3,478 | 26,478 |
| 70423 | Uvuvi na Uwindaji | 24,679 | 3,720 | 28,399 | 34,130 | 13,523 | 47,653 | 361,884 | 212,659 | 574,543 |
| 70431 | Makaa ya Mawe na Nishati nyingine | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70432 | Petroli na Gesi Asilia | 16,988 | 1,191,856 | 1,208,844 | 20,810 | 2,166,587 | 2,187,397 | 19,252 | 2,355,788 | 2,375,040 |
| 70433 | Nishati ya Nyukilia | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70434 | Nishati nyingine | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70435 | Umeme | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70436 | Nishati isiyo ya umeme | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70441 | Uchimbaji Madini yasiyo Nishati | 34,633 | 4,154 | 38,787 | 43,683 | 8,500 | 52,183 | 41,326 | 15,000 | 56,326 |
| 70442 | Uzalishaji Viwandani | 11,837 | - | 11,837 | 12,390 | 16,958 | 29,348 | 11,859 | 19,538 | 31,397 |
| 70443 | Ujenzi | 13,016 | 25,033 | 38,049 | 15,830 | 82,635 | 98,466 | 14,983 | 86,990 | 101,973 |
| 70451 | Usafiri wa Barabara | 16,904 | 1,888,226 | 1,905,130 | 20,044 | 1,402,763 | 1,422,808 | 19,753 | 1,406,271 | 1,426,025 |
| 70452 | Usafiri wa Majini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70453 | Usafiri wa Reli | 84,105 | 1,508,455 | 1,592,560 | 81,413 | 3,045,058 | 3,126,471 | 82,802 | 1,812,083 | 1,894,885 |
| 70454 | Usafiri wa Anga | 121 | 101,503 | 101,623 | 60 | 91,885 | 91,945 | 255 | 95,123 | 95,378 |
| 70455 | Usafirishaji kwa njia ya Bomba na njia nyingine za usafiri | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70460 | Mawasiliano | 1,738 | - | 1,738 | 2,226 | 11,000 | 13,226 | 2,730 | 211400 | 214,129 |
| 70471 | Huduma za Biashara na Utunzaji Mizigo | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |

**Jedwali Na. 24 linaendelea**

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 70472 | Hoteli na Migahawa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70473 | Utalii | 14,402 | 170 | 14,572 | 10,681 | - | 10,681 | 19,559 | 700 | 20,259 |
| 70474 | Miradi ya Maendeleo | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70481 | Utafiti katika shughuli za Kiuchumi, Biashara na Kazi | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70482 | Utafiti na Maendeleo ya Kilimo, Misitu, Uvuvi na | 16 | 0 | 16 | 84 | 0 | 84 | 285 | 0 | 285 |
| 70483 | Utafiti na Maendeleo ya Mafuta na Nishati | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70484 | Utafiti na Maendeleo ya Uchimbaji Madini, Uzalishaji Viwandani na Ujenzi | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70485 | Utafiti na Maendeleo ya Usafiri | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70486 | Utafiti na Maendeleo ya Mawasiliano | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70487 | Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Vingine | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70490 | Shughuli nyingine za Kiuchumi zisizotajwa hapo juu | 12,774 | 27,305 | 40,078 | 21,201 | 65,231 | 86,431 | 20,362 | 83,547 | 103,909 |
| **705** | **Hifadhi ya Mazingira** | **7,062** | **780** | **7,841** | **10,264** | **12,688** | **22,951** | **10,879** | **4,257** | **15,136** |
| 70510 | Hifadhi ya Taka | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70520 | Hifadhi ya Maji Taka | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70530 | Kupunguza Uharibifu wa Mazingira | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70540 | Hifadhi ya Viumbehai na Mazingira | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70550 | Utafiti na Maendeleo ya Hifadhi ya Mazingira | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70560 | Huduma nyingine za Hifadhi ya Mazingira zisizotajwa hapo juu | 7,062 | 780 | 7,841 | 10,264 | 12,688 | 22,951 | 10,879 | 4,257 | 15,136 |
| **706** | **Nyumba na Huduma za Jamii** | **67,584** | **490,062** | **557,647** | **90,359** | **1,097,044** | **1,187,403** | **97,572** | **1,081,205** | **1,178,778** |
| 70610 | Maendeleo ya Nyumba | 30,253 | 8,815 | 39,068 | 41,182 | 90,874 | 132,056 | 58,077 | 30,473 | 88,549 |
| 70620 | Maendeleo ya Jamii | 13,083 | 11,649 | 24,732 | 16,455 | 305,048 | 321,502 | 4,304 | 410,589 | 414,893 |
| 70630 | Usambazaji Maji | 22,358 | 469,598 | 491,956 | 30,078 | 699,622 | 729,700 | 32,579 | 638,643 | 671,222 |
| 70640 | Taa za Barabarani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70650 | Utafiti wa Nyumba na Maendeleo ya Jamii | 65 | 0 | 65 | 151 | 0 | 151 | 133 | 0 | 133 |
| 70660 | Nyumba na Huduma za Jamii zisizotajwa hapo juu | 1,825 | 0 | 1,825 | 2,493 | 1,500 | 3,993 | 2,480 | 1,500 | 3,980 |
| **707** | **Afya** | **2,692,878** | **454,195** | **3,147,073** | **3,164,456** | **735,125** | **3,899,582** | **3,211,050** | **783,346** | **3,994,396** |
| 70711 | Madawa | 93 | 39,698 | 39,791 | 532 | 200,000 | 200,532 | 1,115 | 218,100 | 219,215 |
| 70712 | Bidhaa nyingine za madawa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70713 | Huduma za Tiba na Vifaa vya Tiba | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70721 | Huduma za Tiba za Jumla | 144449 | 17976 | 162425 | 156309 | 46466 | 202775 | 153097 | 63775 | 216872 |
| 70722 | Huduma Maalumu za Tiba | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70723 | Huduma za Meno | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70724 | Huduma za Wakunga Wasaidizi | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70731 | Huduma za Hospitali | 1,100,281 | 3,743 | 1,104,023 | 1,266,417 | 11,496 | 1,277,913 | 1,111,078 | 20,045 | 1,131,123 |
| 70732 | Huduma za Hospitali Maalumu | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70733 | Huduma za Vifaa vya Kujifungulia Wajawazito | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70734 | Huduma za Wakunga na Wakunga wa Jadi | 144 | 0 | 144 | 472 | 0 | 472 | 661 | 0 | 661 |
| 70740 | Huduma za Afya | 104,710 | 301,474 | 406,183 | 142,986 | 398,325 | 541,311 | 141,189 | 343,395 | 484,584 |
| 70750 | Utafiti na Maendeleo ya Huduma za Afya | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70760 | Huduma za Afya zisizotajwa hapo juu | 1,343,202 | 91,305 | 1,434,507 | 1,597,741 | 78,838 | 1,676,579 | 1,803,911 | 138,031 | 1,941,942 |
| **708** | **Burudani, Utamaduni na Dini** | **20,566** | **799** | **21,365** | **28,183** | **7,465** | **35,648** | **31,085** | **20,465** | **51,550** |
| 70810 | Huduma za Burudani na Michezo | 1,606 | - | 1,606 | 2,825 | 950 | 3,775 | 2,703 | 12449 | 15,152 |
| 70820 | Huduma za Utamaduni | 5,290 | - | 5,290 | 6,717 | 515 | 7,232 | 10,395 | 2015 | 12,410 |
| 70830 | Huduma za Utangazaji na Uchapishaji | 13,617 | 799 | 14,416 | 18,455 | 6,000 | 24,455 | 17,744 | 6,001 | 23,745 |
| 70840 | Dini na Huduma nyingine za Kijamii | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70850 | Utafiti na Maendeleo katika Burudani, Utamaduni na Dini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70860 | Huduma nyingine za Burudani, Utamaduni na Dini zisizotajwa hapo juu | 54 | 0 | 54 | 186 | 0 | 186 | 243 | 0 | 243 |
| **709** | **Elimu** | **1,751,872** | **937,334** | **2,689,205** | **1,915,257** | **1,400,394** | **3,315,651** | **1,904,863** | **1,982,646** | **3,887,508** |
| 70911 | Elimu ya Awali | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70912 | Elimu ya Msingi | 827,092 | 221,677 | 1,048,769 | 945,574 | 360,575 | 1,306,149 | 926,080 | 469,238 | 1,395,319 |
| 70921 | Elimu ya Sekondari (Kidato cha I - IV) | 438,800 | 140,378 | 579,178 | 506,299 | 251,332 | 757,630 | 488,940 | 682,181 | 1,171,121 |
| 70922 | Elimu ya Sekondari (Kidato cha V - VI) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70930 | Elimu baada ya Sekondari isiyo ya Chuo Kikuu | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70941 | Daraja la Awali Elimu ya Chuo Kikuu | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70942 | Daraja linalofuata Elimu ya Chuo Kikuu | 19,450 | 4,974 | 24,424 | 21,717 | 24,294 | 46,010 | 21,154 | 34,996 | 56,149 |
| 70950 | Elimu isiyopambanuliwa | - | 0 | - | - | 0 | - | 0 | 0 | 0 |
| 70960 | Huduma za Ziada kwa Elimu | 466,530 | 570,304 | 1,036,834 | 441,668 | 764,193 | 1,205,861 | 468,689 | 796,231 | 1,264,920 |
| 70970 | Utafiti na Maendeleo ya Elimu | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70980 | Huduma za Elimu zisizotajwa hapo juu | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **710** | **Kinga ya Jamii** | **197,955** | **150,633** | **348,588** | **152,274** | **3,952** | **156,226** | **160,954** | **11,164** | **172,118** |
| 71011 | Ugonjwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 71012 | Ulemavu | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 71020 | Wazee | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 71030 | Waathirika | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 71040 | Familia na Watoto | 141,925 | 234 | 142,159 | 143,458 | 2,149 | 145,607 | 149,208 | 1,918 | 151,126 |
| 71050 | Ukosefu wa Ajira | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 71060 | Nyumba | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 71070 | Huduma za Jamii zisizotajwa hapo juu | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 71080 | Utafiti na Maendeleo ya Kinga ya Jamii | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 71090 | Huduma za Kinga ya Jamii zisizotajwa hapo juu | 56,031 | 150,399 | 206,430 | 8,816 | 1,803 | 10,619 | 11,746 | 9,246 | 20,992 |
| **7** | **JUMLA** | **19,862,289** | **7,989,509** | **27,851,798** | **22,100,627** | **12,779,255** | **34,879,882** | **23,002,644** | **13,256,275** | **36,258,918** |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

CS: Huduma za umma zinazotolewa na serikali na wanufaika ni watu wote

IS: Huduma za umma zinazotolewa na serikali na wanufaika ni wanakaya

## SURA YA 4

## SEKTA YA NJE

**Bidhaa Zilizouzwa Nje**

90. Thamani ya mauzo ya bidhaa nje ilikuwa dola za Marekani milioni 6,371.7 mwaka 2020 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 5,377.6 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 18.5 Hii ilitokana na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa zisizo asilia, hususan dhahabu, bidhaa za viwandani, na mazao ya mbogamboga. Bidhaa zisizo asilia zilichangia asilimia 82.3 ya mauzo ya bidhaa nje wakati mauzo ya bidhaa asilia yalichangia asilimia 12.7

**Bidhaa Asilia**

91. Thamani ya mauzo ya bidhaa asilia ilipungua na kufikia dola za Marekani milioni 808.1 mwaka 2020 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 817.7 mwaka 2019, sawa na punguzo la asilimia 1.2. Hii ilitokana na kushuka kwa thamani ya mauzo ya mazao ya chai, katani, kahawa na pamba katika soko la dunia kulikosababishwa na madhara UVIKO-19.

**Korosho**

92. Thamani ya mauzo ya korosho nje ilikuwa dola za Marekani milioni 359.6 mwaka 2020 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 353.1 mwaka 2019. Hii ilitokana na kuongezeka kwa kiasi cha korosho kilichouzwa nje kutoka tani 295,600 mwaka 2019 hadi tani 320,900 mwaka 2020. Aidha, bei ya korosho kwa tani ilipungua kwa asilimia 6.2 kutoka dola za Marekani 1,194.6 mwaka 2019 hadi dola za Marekani 1,120.3 mwaka 2020.

**Kahawa**

93. Thamani ya mauzo ya kahawa nje ilipungua hadi dola za Marekani milioni 145.2 mwaka 2020 kutoka dola za Marekani milioni 152.2 mwaka 2019, sawa na punguzo la asilimia 4.6. Hii ilitokana na kupungua kwa kiasi cha mauzo ya kahawa nje, ambapo tani 64,000 ziliuzwa mwaka 2020 ikilinganishwa na tani 76,200 mwaka 2019. Hata hivyo, wastani wa bei ya kahawa uliongezeka kwa asilimia 13.6 na kufikia dola za Marekani 2,268.9 kwa tani mwaka 2020.

**Pamba**

94. Thamani ya mauzo ya pamba nje ilikuwa dola za Marekani milioni 87.5 mwaka 2020, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 91.8 mwaka 2019, sawa na punguzo la asilimia 4.6. Hii ilitokana na kupungua kwa kiasi cha pamba kilichouzwa nje, ambapo tani 72,600 ziliuzwa mwaka 2020 ikilinganishwa na tani 79,000 mwaka 2019. Aidha, wastani wa bei ya pamba katika soko la dunia uliongezeka na kufikia dola za Marekani 1,206.4 kwa tani mwaka 2020 kutoka dola za Marekani 1,162.2 kwa tani mwaka 2019.

**Katani**

95. Thamani ya mauzo ya katani nje ilikuwa dola za Marekani milioni 17.6 mwaka 2020 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 19.3 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 8.9. Hii ilitokana na kushuka kwa kiasi cha katani kilichouzwa nje kutoka tani 12,200 mwaka 2019 hadi tani 11,200 mwaka 2020. Aidha, wastani wa bei ya katani ulipungua kufikia dola za Marekani 1,566.2 kwa tani mwaka 2020 kutoka dola 1,581.7 kwa tani mwaka 2019.

**Chai**

96. Thamani ya mauzo ya chai nje ilikuwa dola za Marekani milioni 32.4 mwaka 2020 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 45.7 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 29.1. Hii ilitokana na kushuka kwa bei ya chai katika soko la dunia kwa asilimia 6.8 kutoka dola za Marekani 1,444.2 kwa tani mwaka 2019 hadi dola 1,345.5 kwa tani mwaka 2020. Aidha, kiasi cha chai kilichouzwa nje kilipungua kutoka tani 31,700 mwaka 2019 hadi tani 24,100 mwaka 2020.

**Tumbaku**

97. Thamani ya mauzo ya tumbaku nje iliongezeka kwa asilimia 1.5 na kuwa dola za Marekani milioni 148.7 mwaka 2020 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 146.5 mwaka 2019. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa wastani wa bei ya tumbaku katika soko la dunia kutoka dola za Marekani 3,440.9 kwa tani mwaka 2019 hadi dola za Marekani 3,494.2 kwa tani mwaka 2020. Aidha, mwaka 2020 kiasi cha tumbaku kilichouzwa nje kilikuwa tani 42,600 kama ilivyokuwa mwaka 2019.

**Bidhaa Zisizo Asilia**

98. Thamani ya mauzo nje ya bidhaa zisizo asilia ilikuwa dola za Marekani milioni 5,253.3 mwaka 2020 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 4,186.0 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 25.5. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mauzo ya madini, bidhaa za viwandani, mbogamboga na bidhaa nyinginezo.

**Madini**

99. Thamani ya mauzo ya madini nje ilikuwa dola za Marekani milioni 3,369.1 mwaka 2020 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 2,326.7 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 44.8. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mauzo ya dhahabu na madini mengine isipokuwa almasi. Thamani ya mauzo ya dhahabu iliongezeka kwa asilimia 33.5 na kufikia dola za Marekani milioni 2,957.5 mwaka 2020 kutoka dola za Marekani milioni 2,215.1 mwaka 2019. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mauzo na kupanda kwa bei ya dhahabu katika soko la dunia kufuatia uwepo wa mahitaji makubwa ya madini hayo. Wawekezaji wengi walinunua madini hayo na kuyahifadhi kama akiba benki ili kunusuru thamani ya fedha zao kutoka katika masoko ya fedha na mitaji ambayo mengi yaliporomoka katika kipindi cha mlipuko wa UVIKO-19. Bei ya dhahabu katika soko la dunia iliongezeka kutoka wastani wa dola za Marekani 1,392.60

kwa wakia moja mwaka 2019 hadi dola 1,769.64 mwaka 2020. Mapato ya mauzo ya madini yalichangia asilimia 63.6 ya mapato yote ya bidhaa zisizo asilia mwaka 2020 na dhahabu ilichangia asilimia 87.8 katika mapato ya madini.

**Bidhaa za Viwandani**

100. Thamani ya mauzo ya bidhaa za viwandani ilikuwa dola za Marekani milioni 908.6 mwaka 2020 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 851.8 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 6.7. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa za viwandani nje hususan, chuma na bidhaa za chuma, vioo na bidhaa za vioo, vigae na bidhaa za plastiki. Aidha, bidhaa za viwandani zilichangia asilimia 17.3 ya mapato ya bidhaa zisizo asilia mwaka 2020.

**Samaki na Mazao ya Samaki**

101. Thamani ya mauzo ya samaki na mazao yake nje ilipungua kwa asilimia 16.9 kutoka dola za Marekani milioni 168.0 mwaka 2019 hadi dola za Marekani milioni 139.6 mwaka 2020. Hii ilichangiwa na kupungua kwa kiasi cha samaki na mazao ya samaki kilichouzwa nje.

**Mbogamboga na Maua**

102. Thamani ya mauzo ya mbogamboga na maua yaliongezeka kwa asilimia 35.4 kutoka dola za Marekani milioni 202.4 mwaka 2019 hadi dola za Marekani milioni 274.1 mwaka 2020 Sehemu kubwa ya ongezeko hilo ilitokana na mauzo ya matunda na mbogamboga katika nchi jirani.

**Bidhaa Nyinginezo Zilizouzwa Nje**

103. Thamani ya mauzo ya bidhaa nyinginezo zilizouzwa nje ilikuwa dola za Marekani milioni 474.2 mwaka 2020 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 394.3 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 20.3. Bidhaa zinazojumuishwa katika kundi hili ni pamoja na mbegu za mafuta, kakao, ngozi na nafaka kama mahindi, mchele na mtama. Sehemu kubwa ya bidhaa hizi ziliuzwa katika nchi jirani.

**Jedwali Na. 4.1: Thamani, Kiasi na Bei ya Bidhaa Zilizouzwa Nje**

| Bidhaa | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | Badiliko Asilimia |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Bidhaa Asilia** | | | | | | | | |
| **Kahawa** | | | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 121.5 | 162.2 | 153.7 | 126.3 | 147.9 | 152.2 | 145.2 | -4.6 |
| Kiasi ('000 tani) | 44.1 | 51.9 | 58.7 | 41.8 | 56.6 | 76.2 | 64.0 | -16.0 |
| Bei (US$ kwa tani) | 2,756.2 | 3,123.0 | 2,616.8 | 3,019.5 | 2,612.0 | 1,996.5 | 2,268.9 | 13.6 |
| **Pamba** | | | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 54.7 | 30.2 | 46.8 | 36.8 | 68.4 | 91.8 | 87.5 | -4.6 |
| Kiasi ('000 tani) | 49.5 | 29.1 | 33.0 | 25.3 | 47.4 | 79.0 | 72.6 | -8.1 |
| Bei (US$ kwa tani) | 1,104.9 | 1,037.8 | 1,416.1 | 1,450.3 | 1,444.2 | 1,162.2 | 1,206.4 | 3.8 |
| **Katani** | | | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 16.8 | 26.5 | 17.2 | 28.7 | 32.5 | 19.3 | 17.6 | -8.9 |
| Kiasi ('000 tani) | 11.5 | 15.2 | 8.6 | 17.0 | 20.3 | 12.2 | 11.2 | -8.0 |
| Bei (US$ kwa tani) | 1,459.7 | 1,748.8 | 2,002.1 | 1,686.7 | 1,604.5 | 1,581.7 | 1,566.2 | -1.0 |
| **Chai** | | | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 45.7 | 44.0 | 44.8 | 49.1 | 45.9 | 45.7 | 32.4 | -29.1 |
| Kiasi ('000 tani) | 29.2 | 27.5 | 26.3 | 27.5 | 26.9 | 31.7 | 24.1 | -23.9 |
| Bei (US$ kwa tani) | 1,568.1 | 1,600.9 | 1,700.8 | 1,783.6 | 1,707.4 | 1,444.2 | 1,345.5 | -6.8 |
| **Tumbaku** | | | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 315.0 | 287.6 | 339.2 | 195.8 | 270.3 | 146.5 | 148.7 | 1.5 |
| Kiasi ('000 tani) | 67.4 | 66.3 | 74.3 | 48.3 | 72.2 | 42.6 | 42.6 | -0.1 |
| Bei (US$ kwa tani) | 4,673.5 | 4,336.5 | 4,562.7 | 4,055.6 | 3,741.9 | 3,440.9 | 3,494.2 | 1.5 |
| **Korosho** | | | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 222.2 | 218.8 | 320.2 | 529.6 | 196.5 | 353.1 | 359.6 | 1.8 |
| Kiasi ('000 tani) | 172.2 | 171.7 | 217.5 | 329.4 | 120.2 | 295.6 | 320.9 | 8.5 |
| Bei (US$ kwa tani) | 1,290.7 | 1,273.8 | 1,472.4 | 1,607.7 | 1,634.2 | 1,194.6 | 1,120.6 | -6.2 |
| **Karafuu** | | | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 52.9 | 24.1 | 39.3 | 54.4 | 10.5 | 9.1 | 17.1 | 86.9 |
| Kiasi ('000 tani) | 4.7 | 2.8 | 4.9 | 6.9 | 1.3 | 1.8 | 3.6 | 97.8 |
| Bei (US$ kwa tani) | 11,231.3 | 8,653.1 | 7,976.0 | 7,886.6 | 8,031.7 | 5,047.8 | 4,770.0 | -5.5 |
| **Jumla (Bidhaa Asilia)** | **828.8** | **793.3** | **961.2** | **1,020.7** | **772.1** | **817.7** | **808.1** | **-1.2** |
| **Bidhaa Zisizo Asilia (US$ millioni)** | | | | | | | | |
| **Madini** | **1,469.2** | **1,285.4** | **1,930.0** | **1,694.5** | **1,615.3** | **2,326.7** | **3,369.1** | **44.8** |
| Dhahabu | 1,324.1 | 1,183.3 | 1,508.8 | 1,541.1 | 1,524.0 | 2,215.1 | 2,957.5 | 33.5 |
| Almasi | 78.2 | 53.2 | 38.9 | 64.4 | 81.8 | 81.3 | 20.2 | -75.1 |
| Madini mengine | 66.9 | 48.9 | 382.3 | 88.9 | 9.5 | 30.3 | 391.3 | -- |
| **Bidhaa za Viwandani** | **1,239.6** | **1,277.0** | **714.2** | **693.7** | **794.6** | **851.8** | **908.6** | **6.7** |
| Nyuzi za Pamba | 10.8 | 11.9 | 16.8 | 16.1 | 16.8 | 6.7 | 6.9 | 4.0 |
| Kahawa iliyozalishwa | 1.2 | 0.3 | 0.5 | 1.2 | 2.0 | 1.4 | 5.2 | -- |
| Tumbaku iliyozalishwa | 33.6 | 33.0 | 31.6 | 22.3 | 21.6 | 24.5 | 18.3 | -25.5 |
| Mazao ya Katani | 10.5 | 17.4 | 22.3 | 26.3 | 21.4 | 23.4 | 23.2 | -0.6 |
| Mazao mengine ya Viwandani | 1,183.4 | 1,214.4 | 643.1 | 627.9 | 732.8 | 795.9 | 855.0 | 7.4 |
| **Samaki na Mazao ya Samaki** | **195.0** | **173.5** | **143.7** | **193.0** | **158.4** | **168.0** | **139.6** | **-16.9** |
| **Mazao ya Mboga na Maua** | **30.5** | **24.4** | **24.8** | **27.2** | **33.0** | **202.4** | **274.1** | **35.4** |
| **Bidhaa zilizouzwa tena (re-exports)** | **177.0** | **385.8** | **187.7** | **126.5** | **175.6** | **242.8** | **87.7** | **-63.9** |
| **Bidhaa nyinginezo** | **687.2** | **894.0** | **538.1** | **357.1** | **432.5** | **394.3** | **474.2** | **20.3** |
| **Jumla (Bidhaa zisizo Asilia)** | **3,798.6** | **4,040.1** | **3,538.5** | **3,091.9** | **3,209.3** | **4,186.0** | **5,253.3** | **25.5** |
| Bidhaa zisizo rekodiwa | 566.8 | 483.3 | 450.0 | 411.3 | 398.1 | 373.8 | 310.4 | -17.0 |
| **JUMLA KUU (BIDHAA ZOTE)** | **5,194.1** | **5,316.8** | **4,949.7** | **4,523.9** | **4,379.6** | **5,377.6** | **6,371.7** | **18.5** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Mapato Tanzania na Benki Kuu ya Tanzania

**Mapato ya Huduma**

104. Mapato yatokanayo na biashara ya huduma yalikuwa na thamani ya dola za Marekani milioni 2,182.9 mwaka 2020 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 4,281.0 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 49.0. Upungufu huo ulichangiwa na kushuka kwa mapato yatokanayo na huduma za safari (hususani utalii) na huduma za usafirishaji. Mapato yatokanayo na huduma za safari za utalii yalipungua kwa asilimia 72.6 na kufikia thamani ya dola za Marekani milioni 714.5 mwaka 2020 kutoka dola za Marekani milioni 2,604.5 mwaka 2019. Aidha, mapato yatokanayo na huduma ya usafirishaji yalipungua na kufikia dola za Marekani milioni 1,284.5 mwaka 2020 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,355.9 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 5.3. Hii ilitokana na hatua mbalimbali zilizochukuliwa na nchi nyingi duniani kudhibiti kuenea kwa maambukizi ya UVIKO-19 ikiwemo kuzuia watu kusafiri, kusimamishwa kwa ndege za abiria za kimataifa na kufungwa kwa mipaka hususan ya nchi jirani.

**Bidhaa Zilizoagizwa Kutoka Nje ya Nchi**

105. Thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nje ilipungua kwa asilimia 10.3 hadi dola za Marekani milioni 7,889.0.4 mwaka 2020 kutoka dola za Marekani milioni 8,793.1 mwaka 2019. Punguzo hilo lilitokana na kupungua kwa thamani ya uagizaji wa bidhaa za kukuza mitaji na bidhaa za kati kutoka nje.

**Bidhaa za Kukuza Mitaji**

106. Thamani ya bidhaa za kukuza mitaji zilizoingizwa nchini ilipungua kwa asilimia 13 na kufikia dola za Marekani milioni 3,220.7 mwaka 2020 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 3,703.9 mwaka 2019. Punguzo hilo lilichangiwa na kushuka kwa thamani ya uingizaji wa vifaa vya usafirishaji, majengo na ujenzi, na mitambo kutoka nje. Aidha, thamani ya vifaa vya usafirishaji ilipungua kwa asilimia 27.5 na kufikia dola za Marekani milioni 782.8 mwaka 2020.

**Bidhaa za Kati**

107. Thamani ya bidhaa za kati zilizoagizwa kutoka nje ilipungua kwa asilimia 16.8 na kufikia dola za Marekani milioni 2,231.8 mwaka 2020 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 2,682.7 mwaka 2019. Hii ilitokana na kushuka kwa thamani ya uagizaji wa bidhaa za mafuta ya petroli. Thamani ya bidhaa za mafuta ya petroli zilizoagizwa kutoka nje ilipungua kwa asilimia 26.8 na kufikia dola za Marekani milioni 1,281.3 mwaka 2020 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,793.8 mwaka 2019. Hii ilitokana na kupungua kwa kiasi cha mafuta ya petroli kilichoagizwa toka nje sambamba na kupungua kwa bei ya mafuta katika soko la dunia.

**Bidhaa za Matumizi ya Kawaida**

108. Thamani ya bidhaa za matumizi ya kawaida zilizoagizwa kutoka nje iliongezeka kwa asilimia 1.2 na kufikia dola za Marekani milioni 2,436.4 mwaka 2020

kutoka dola za Marekani milioni 2,406.5 mwaka 2019. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uagizaji wa bidhaa nyingine za matumizi ya kawaida isipokuwa bidhaa za chakula. Uagizaji wa bidhaa za chakula ulipungua kwa asilimia 6.2 na kufikia dola za Marekani milioni 386.7 mwaka 2020 kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa chakula nchini.

### Malipo ya Huduma

109. Thamani ya malipo ya huduma ilipungua kwa asilimia 30.5 kufikia dola za Marekani milioni 1,239.2 mwaka 2020 kutoka dola za Marekani milioni 1,782.5 mwaka 2019. Hii ilitokana na kushuka kwa thamani ya malipo ya huduma za usafirishaji, utalii na huduma nyinginezo.

**Jedwali Na. 4.2: Thamani ya Bidhaa Zilizoagizwa kutoka Nje (Dola za Marekani Milioni) Mwaka 2015-2020**

| Bidhaa | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | Badiliko, % |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Bidhaa za Kukuza Mitaji** | **3,813.0** | **3,497.4** | **2,688.4** | **3,405.8** | **3,703.9** | **3,220.7** | **-13.0** |
| Vifaa vya Usafirishaji | 1,096.5 | 907.7 | 694.2 | 1,193.0 | 1,079.9 | 782.8 | **-27.5** |
| Majengo na Ujenzi | 908.0 | 817.2 | 581.8 | 840.3 | 1,006.7 | 936.8 | **-6.9** |
| Mitambo | 1,808.4 | 1,772.5 | 1,412.5 | 1,372.5 | 1,617.4 | 1,501.2 | **-7.2** |
| **Bidhaa za Kati** | **3,696.6** | **2,863.2** | **2,704.4** | **2,549.8** | **2,682.7** | **2,231.8** | **-16.8** |
| Uagizaji Mafuta | 2,760.7 | 1,807.7 | 1,850.6 | 1,613.2 | 1,793.8 | 1,281.3 | **-28.6** |
| Mbolea | 145.6 | 118.6 | 124.9 | 176.5 | 129.9 | 186.3 | **43.5** |
| Malighafi za Viwanda | 790.4 | 937.0 | 728.9 | 760.2 | 759.0 | 764.2 | **0.7** |
| **Bidhaa za Matumizi ya Kawaida** | **2,331.3** | **2,100.8** | **2,156.7** | **2,111.0** | **2,406.5** | **2,436.4** | **1.2** |
| Bidhaa za Vyakula | 541.7 | 445.5 | 405.3 | 264.3 | 412.1 | 386.7 | **-6.2** |
| Bidhaa Nyingine | 1,789.6 | 1,655.4 | 1,751.4 | 1,848.9 | 1,994.4 | 2,049.8 | **2.8** |
| **Jumla (FoB)** | **9,843.1** | **8,463.6** | **7,551.7** | **8,066.6** | **8,793.1** | **7,889.0** | **10.3** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Mapato na Benki Kuu ya Tanzania

### Mwenendo wa Biashara Baina ya Tanzania na Nchi Mbalimbali

110. Mwaka 2020, Tanzania iliendelea kuboresha mahusiano ya kibiashara na nchi mbalimbali duniani. Katika kipindi hicho, thamani ya bidhaa zilizouzwa kwenye soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) iliongezeka kwa asilimia 19.8 na kufikia dola za Marekani milioni 807.9 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 674.4 mwaka 2019. Hali hii ilichangiwa na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa za chai, mahindi, ngano, alizeti, mchele, mbogamboga, karatasi, bidhaa za chuma, vigae, vyandarua, kemikali (methyl bromide), saruji na mafuta ya kupaka kwenda katika nchi hizo.

111. Thamani ya bidhaa zilizouzwa katika soko la Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) iliongezeka kwa asilimia 7.9 na kufikia dola za Marekani milioni 1,458.3 mwaka 2020 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,350.9 mwaka 2019. Sehemu kubwa ya mauzo ya bidhaa hizo ziliuzwa kwa nchi ya Afrika Kusini, Jamhuri

ya Kidemokrasia ya Kongo, Zambia na Malawi. Bidhaa zilizouzwa kwa wingi katika nchi hizo ni pamoja na madini, pamba, chai, kahawa, vigae, vyandarua, kemikali (methly bromide), *petroleum coke*, saruji, sabuni, na mafuta ya kupaka.


112. Mwaka 2020 thamani ya mauzo ya bidhaa kwenda katika soko la Ulaya iliongezeka hadi dola za Marekani milioni 1,511.6 kutoka dola za Marekani 823.9 mwaka 2019, Sawa na ongezeko la asilimia 83.5. Hii ilitonakana na kuongezeka kwa mauzo hususan ya dhahabu kwenda nchi za Uswisi, Uhispania, Ubelgiji, Uholanzi, Ujerumani na Italy.

113. Mwaka 2020 thamani ya mauzo ya bidhaa kwenda nchi za Bara la Asia iliongezeka kwa asilimia 15.0 hadi kufikia dola za Marekani milioni 2,193.8 kutoka dola za Marekani 1,906.9 mwaka 2019. Hii ilitonakana na kuongezeka kwa mauzo kwenda nchi za Umoja wa Falme za Kiarabu, India, China na Vietnam. Aidha, uagizaji wa bidhaa kutoka nchi za Bara la Asia uliongezeka kwa asilimia 5.9 hadi kufikia dola za Marekani 5,974.5 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 5,643.0 mwaka 2019. Hii ilitokana na kuongezeka kwa bidhaa za mtaji, bidhaa za usafirirshaji na bidhaa za kawaida zilizoagizwa kutoka katika nchi hizo.

114. Mwaka 2020, nchi ambazo Tanzania iliuza bidhaa zake kwa kiasi kikubwa zilikuwa ni Afrika Kusini, Uswisi, Umoja wa Falme za Kiarabu, India, China na Kenya ambazo kwa pamoja zilichangia asilimia 62.4 ya bidhaa zote zilizouzwa nje ya nchi. Aidha, bidhaa zilizouzwa Umoja wa Falme za Kiarabu, China, India na Japani ni pamoja na mbegu za mafuta, tumbaku, kahawa na korosho. Kwa upande mwingine, dhahabu iliuzwa Afrika Kusini, India na Uswisi. Bidhaa zilizouzwa Kenya ni pamoja na nafaka (mahindi na mchele), mazao ya mboga mboga.

**Kielelezo Na. 4.1: Mchanganuo wa Masoko ya Bidhaa za Tanzania Nje ya Nchi, Mwaka 2020**

Asilimia




**Chanzo:** Mamlaka ya Mapato na Benki Kuu ya Tanzania

## Jedwali Na. 4.3: Mauzo ya Bidhaa Kwenda Nchi Mbalimbali Duniani

**(Dola za Marekani Milioni)**

| JUMUIYA/ NCHI | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | 2019/20 Badiliko% |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| JUMUIYA YA ULAYA NA USWISI | 898.4 | 791.7 | 615.4 | 629.8 | 510.5 | 657.3 | 725.9 | 1475.9 | 103.3 |
| NCHI NYINGINE ZA ULAYA | 16.9 | 77.5 | 176.4 | 784.7 | 26.2 | 92.7 | 98.0 | 35.8 | -63.5 |
| **JUMLA- BARA LA ULAYA** | **915.3** | **869.2** | **791.8** | **1414.5** | **536.7** | **750.1** | **823.9** | **1511.6** | **83.5** |
| **AFRIKA** | | | | | | | | | |
| **JUMUIYA YA NCHI ZA KUSINI MWA AFRIKA (SADC)** | | | | | | | | | |
| AFRIKA YA KUSINI | 760.0 | 689.1 | 673.2 | 692.2 | 693.3 | 730.6 | 971.6 | 1161.6 | 19.6 |
| Zambia | 90.6 | 135.3 | 44.1 | 35.7 | 48.3 | 50.2 | 63.6 | 54.1 | -14.9 |
| Swaziland | 4.0 | 1.2 | 9.1 | 0.1 | 0.5 | 2.0 | 5.9 | 0.1 | -99.0 |
| Zimbabwe | 6.5 | 7.1 | 6.3 | 7.0 | 8.3 | 8.7 | 18.8 | 21.1 | 12.6 |
| Msumbiji | 66.4 | 68.1 | 18.6 | 13.5 | 13.0 | 6.8 | 32.6 | 21.0 | -35.6 |
| Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo | 236.2 | 281.5 | 197.7 | 319.8 | 101.4 | 133.7 | 164.1 | 144.2 | -12.1 |
| **Nchi nyingine za SADc** | **44.9** | **53.7** | **79.1** | **44.4** | **89.7** | **61.7** | **94.3** | **56.2** | -40.4 |
| **Jumla-SADC** | **1208.6** | **1236.0** | **1028.1** | **1112.7** | **954.6** | **993.6** | **1350.9** | **1458.3** | **7.9** |
| **JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI (EAC)** | | | | | | | | | |
| Burundi | 45.0 | 43.0 | 39.1 | 52.1 | 50.5 | 47.4 | 87.9 | 177.7 | 102.1 |
| Kenya | 227.1 | 445.9 | 731.4 | 313.8 | 174.4 | 212.0 | 269.9 | 230.2 | -14.7 |
| Rwanda | 81.1 | 35.8 | 41.2 | 6.5 | 60.1 | 79.0 | 190.9 | 205.3 | 7.5 |
| Uganda | 66.1 | 73.3 | 50.3 | 58.2 | 104.9 | 104.9 | 123.7 | 191.2 | 54.6 |
| Sudan ya Kusini | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 1.0 | 1.0 | 2.0 | 3.4 | 68.2 |
| **JUMLA-EAC** | **419.3** | **598.0** | **862.0** | **430.6** | **590.9** | **444.3** | **674.4** | **807.9** | **19.8** |
| **Nchi nyingine za Afrika** | **3.5** | **219.1** | **337.5** | **202.8** | **24.8** | **102.7** | **59.5** | **56.2** | **-5.6** |
| **JUMLA-AFRIKA** | **1631.4** | **2053.1** | **2227.6** | **1746.1** | **1570.3** | **1540.6** | **2084.8** | **2322.3** | **11.4** |
| **BARA LA AMERIKA** | | | | | | | | | |
| Marekani | 60.5 | 143.0 | 50.6 | 57.0 | 61.7 | 59.7 | 52.4 | 47.0 | -10.4 |
| Canada | 12.9 | 7.1 | 6.0 | 4.7 | 3.6 | 6.9 | 3.7 | 3.2 | -13.6 |
| **Nchi nyingine za bara la Amerika** | **2.7** | **6.2** | **84.7** | **9.3** | **98.7** | **69.0** | **69.7** | **2.8** | -96.0 |
| **JUMLA - BARA LA AMERIKA** | **76.1** | **156.3** | **77.1** | **71.0** | **164.0** | **135.5** | **125.8** | **53.0** | **-57.9** |
| **BARA LA ASIA** | | | | | | | | | |
| China | 307.8 | 583.9 | 560.5 | 354.1 | 141.0 | 143.0 | 233.7 | 238.9 | 2.2 |
| India | 748.2 | 1084.1 | 1145.8 | 702.8 | 974.1 | 727.1 | 867.8 | 528.7 | -39.1 |
| Japan | 220.0 | 247.8 | 229.7 | 138.5 | 73.9 | 66.0 | 64.2 | 55.8 | -13.0 |
| Umoj wa falme za kiarabu | 84.2 | 85.5 | 157.1 | 63.5 | 87.3 | 84.9 | 395.1 | 754.9 | 91.1 |
| Honkong | 30.4 | 35.6 | 33.9 | 30.0 | 42.9 | 38.7 | 49.6 | 128.3 | 158.6 |
| Singapore | 55.7 | 15.9 | 6.6 | 10.5 | 5.4 | 2.8 | 7.6 | 43.7 | 477.7 |
| Nchi nyingine za Asia | 64.7 | 121.9 | 160.2 | 193.0 | 811.8 | 288.3 | 289.1 | 443.5 | 53.4 |
| **JUMLA-ASIA** | **1511.0** | **2174.7** | **2293.8** | **1492.4** | **2136.5** | **1350.8** | **1906.9** | **2193.8** | **15.0** |
| Nchi nyinginezo | 1124.3 | 65.5 | 12.0 | 964.8 | 783.7 | 668.1 | 436.1 | 291.0 | -33.3 |
| **JUMLA KUU** | **5258.1** | **5318.8** | **5402.3** | **5688.8** | **5191.2** | **4445.1** | **5377.6** | **6371.7** | **18.5** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Mapato Tanzania na Benki Kuu ya Tanzania


115. Mwaka 2020, bidhaa zenye thamani ya dola za Marekani milioni 324.3 ziliagizwa kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki ikilinganishwa na bidhaa zenye thamani ya dola milioni 329.2 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 1.5. Aidha, bidhaa

zilizoagizwa kutoka Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika zilikuwa na thamani ya dola za Marekani milioni 492.4 ikilinganishwa na dola milioni 594.0 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 17.1. Upungufu huo ulitokana na kuimarika kwa viwanda vya ndani vinavyozalisha bidhaa zilizokuwa zinaagizwa kutoka nchi wanachama zikiwemo juisi mchanganyiko, mabati na bidhaa za chuma. Uagizaji wa bidhaa kutoka Jumuiya ya Ulaya ulipungua kwa asilimia 20.2 na kufikia dola za Marekani milioni 1,191.2 mwaka 2020 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1492.3 mwaka 2019. Hii ilitokana na kuendelea kuimarika kwa upatikanaji wa bidhaa zinazozalishwa hapa nchini.

116. Mwaka 2020, nchi ambazo Tanzania iliagiza bidhaa zake kwa kiasi kikubwa zilikuwa ni China, India, Umoja wa Falme za Kiarabu, Japan, Afrika Kusini na Saudi Arabia ambazo kwa pamoja zilichangia asilimia 60.06 ya thamani ya bidhaa zote zilizoagizwa kutoka nje ya nchi. Sehemu kubwa ya bidhaa zilizoagizwa ni pamoja na mitambo, matrekta na bidhaa za kielektroniki kutoka China pamoja na mafuta ya petroli kutoka nchi za Saudi Arabia na Umoja wa Falme za Kiarabu. Aidha, magari na vyuma viliagizwa kutoka India na Afrika Kusini.

**Kielelelezo Na. 4.2: Mchanganuo wa Vyanzo vya Bidhaa Zilizoingia Nchini, Mwaka 2020**

Asilimia




**Chanzo:** Mamlaka ya MapatoTanzania na Benki Kuu ya Tanzania

## Jedwali Na. 4.4: Uagizaji wa Bidhaa Kutoka Nchi Mbalimbali Duniani

**(Dola za Marekani Milioni)**

| **JUMUIYA/ NCHI** | **2013** | **2014** | **2015** | **2016** | **2017** | **2018** | **2019** | **2020** | **2019/20 Badiliko%** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| JUMUIYA YA ULAYA NA USWISI | 2759 | 2795 | 1007 | 977.8 | 1085.6 | 982.4 | 1069.9 | 1072.0 | 0.2 |
| NCHI NYINGINE ZA ULAYA | 218 | 499.1 | 673.6 | 323.6 | 311.5 | 442.5 | 422.4 | 119.3 | -71.8 |
| **JUMLA – ULAYA** | **2977** | **3294** | **1680** | **1301.4** | **1397.1** | **1424.9** | **1492.3** | **1191.2** | -20.2 |
| **AFRIKA** | | | | | | | | | |
| **JUMUIYA YA NCHI ZA KUSINI MWA AFRIKA (SADC)** | | | | | | | | | |
| Afrika ya Kusini | 660.1 | 603.3 | 514.1 | 472.2 | 414.7 | 437.2 | 438.8 | 345.8 | -21.2 |
| Zambia | 46.2 | 63.3 | 32.6 | 2.1 | 53.7 | 51.0 | 47.3 | 51.2 | 8.2 |
| Swaziland | 33.9 | 47.1 | 37.3 | 33.5 | 37.1 | 38.5 | 48.7 | 26.4 | -45.9 |
| Zimbabwe | 3.4 | 4.8 | 5.7 | 41.2 | 1.1 | 1.2 | 1.0 | 4.7 | 375.2 |
| Msumbiji | 66.9 | 18.3 | 33.3 | 12.0 | 9.2 | 24.0 | 8.4 | 2.4 | -71.5 |
| Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo | 0.1 | 0.8 | 0.6 | 0.4 | 1.0 | 0.6 | 1.3 | 2.1 | 66.7 |
| **Nchi nyingine za SADc** | **25.3** | **35.3** | **45.6** | **54.2** | **45.6** | **51.7** | **48.5** | **59.9** | 23.3 |
| **JUMLA-SADC** | **835.9** | **772.9** | **669.2** | **615.6** | **562.5** | **604.2** | **594.0** | **492.4** | -17.1 |
| **JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI (EAC)** | | | | | | | | | |
| Burundi | 1.5 | 0.6 | 1.1 | 0.8 | 0.2 | 1.0 | 0.4 | 0.3 | -23.4 |
| Kenya | 303.6 | 379.6 | 238.6 | 267.7 | 201.0 | 247.5 | 267.0 | 247.7 | -7.2 |
| Rwanda | 1.5 | 3.2 | 1.1 | 1.1 | 1.3 | 1.4 | 1.5 | 2.2 | 49.9 |
| Uganda | 52.5 | 48 | 39.4 | 30.7 | 34.1 | 52.7 | 60.3 | 74.0 | 22.8 |
| Sudan ya Kusini | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 0.0 | 0.2 | 0.0 | 0.0 | 100.0 |
| **JUMLA-EAC** | **359.1** | **431.4** | **280.2** | **300.3** | **236.6** | **302.8** | **329.2** | **324.3** | -1.5 |
| Nchi nyingine za Afrika | 60.6 | 53.3 | 62.7 | 69.0 | 88.6 | 83.8 | 113.7 | 41.5 | -63.5 |
| **JUMLA-AFRIKA** | **1256** | **1258** | **1012** | **984.9** | **887.7** | **990.8** | **1037.0** | **858.2** | -17.2 |
| **BARA LA AMERIKA** | | | | | | | | | |
| Marekani | 211.9 | 269.8 | 323.3 | 252.0 | 201.8 | 237.7 | 320.6 | 217.0 | -32.3 |
| Canada | 91.8 | 93.7 | 60.2 | 100.9 | 39.5 | 34.7 | 30.3 | 31.0 | 2.3 |
| **Nchi nyingine za bara la Amerika** | **34.5** | **44.4** | **47.3** | **48.6** | **95.3** | **50.3** | 100.3 | 59.2 | -41.0 |
| **JUMLA - BARA LA AMERIKA** | **338.2** | **407.9** | **430.8** | **401.5** | **336.7** | **322.6** | **451.2** | **307.3** | -31.9 |
| **BARA LA ASIA** | | | | | | | | | |
| China | 1444 | 1571 | 1700 | 1638.4 | 1499.6 | 1762.0 | 1987.7 | 1940.3 | -2.4 |
| India | 2088 | 1749 | 1154 | 1428.7 | 1165.0 | 1217.3 | 1258.5 | 980.6 | -22.1 |
| Japan | 466.7 | 559.3 | 363 | 371.0 | 410.6 | 398.0 | 485.2 | 338.4 | -30.3 |
| Umoja wa falme za kiarabu | 1079 | 1095 | 769 | 592.3 | 592.2 | 871.6 | 949.9 | 824.3 | -13.2 |
| Honkong | 32.7 | 53.2 | 41.6 | 51.6 | 51.3 | 60.0 | 47.6 | 47.7 | 0.2 |
| Singapore | 200.7 | 39.2 | 84.3 | 52.6 | 61.5 | 30.2 | 65.6 | 30.8 | -53.0 |
| Nchi nyingine za Asia | 1871 | 1052 | 2497 | 1566.6 | 961.0 | 822.4 | 848.5 | 1363.2 | 60.7 |
| **JUMLA-ASIA** | **7183** | **6119** | **6609** | **5701.2** | **4741.2** | **5161.6** | **5643.0** | **5525.3** | -2.1 |
| **Nchi nyinginezo** | **-725** | **3.4** | **111.3** | **74.6** | **189.1** | **482.5** | 283.4 | 48.5 | -82.9 |
| **JUMLA KUU** | **11029** | **11082** | **9843** | **8463.6** | **7551.7** | **8298.7** | **8793.1** | **7889.0** | -10.3 |

**Chanzo:** Mamlaka ya Mapato Tanzania na Benki Kuu ya Tanzania

**Mizania ya Malipo na Nchi za Nje**

**Urari wa Malipo Yote**

117. Urari wa malipo yote nje ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 764.9 mwaka 2020 ikilinganishwa na ziada ya dola za Marekani milioni 587.0 mwaka 2019. Matokeo haya yalichangiwa na kupungua kwa ziada katika urari wa biashara ya huduma.

**Urari wa Biashara ya Bidhaa**

118. Urari wa biashara ya bidhaa ulipungua hadi kufikia nakisi ya dola za Marekani milioni 1,517.2 mwaka 2020 kutoka nakisi ya dola za Marekani milioni 3,415.5 mwaka 2019, sawa na upungufu wa nakisi kwa asilimia 55.6. Kupungua huko kulitokana na kuongezeka kwa thamani ya mauzo ya bidhaa nje ya nchi sambamba na kupungua kwa thamani ya uagizaji wa bidhaa kutoka nje.

**Urari wa Biashara ya Huduma**

119. Mwaka 2020, urari wa biashara ya huduma ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 943.7 ikilinganishwa na ziada ya dola milioni 2,498.5 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 62.2. Hii ilitokana na kupungua kwa mapato yatokanayo na huduma hususan, utalii na usafirishaji.

**Urari wa Biashara ya Bidhaa na Huduma**

120. Mwaka 2020, urari wa biashara ya bidhaa na huduma ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 573 ikilingnishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 917.0 mwaka 2019, sawa na punguzo la nakisi kwa asilimia 37.5. Punguzo hilo la nakisi lilitokana na kupungua kwa nakisi katika biashara ya bidhaa.

**Urari wa Mapato ya Vitega Uchumi**

121. Urari wa mapato ya vitega uchumi ambayo yanajumuisha kiasi cha malipo yatokanayo na ajira kwa wafanyakazi, mapato ya uwekezaji na malipo ya riba ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 854.5 mwaka 2020 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 992.5 mwaka 2019, sawa na upungufu wa nakisi kwa asilimia 13.9.

**Urari wa Uhamisho Mali wa Kawaida**

122. Urari wa uhamisho mali wa kawaida unaojumuisha uhamisho wa fedha unaofanywa na sekta binafsi, misaada na unafuu wa kulipa deni ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 433.6 mwaka 2020 ikilinganishwa na ziada ya dola za Marekani milioni 418.5 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 3.6. Hii ilitokana na kuongezeka kwa misaada kutoka kwa washirika wa maendeleo iliyoelekezwa kwenye miradi mbalimbali ya kisekta.

**Urari wa Malipo ya Kawaida**

123. Urari wa malipo ya kawaida unaojumuisha biashara ya bidhaa, huduma, mapato ya vitega uchumi na uhamisho mali wa kawaida ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 961.2 mwaka 2020 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,009.8 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 31.6 Hii ilitokana na kupungua kwa nakisi ya biashara ya bidhaa na huduma.

**Urari wa Uhamisho wa Mitaji**

124. Urari wa uhamisho wa mitaji unaojumuisha misaada ya vitega uchumi na misamaha ya madeni ya nje kutoka kwa mashirika ya fedha ya kimataifa na nchi wahisani ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 303.6 mwaka 2020 ikilinganishwa na ziada ya dola milioni 481.2 mwaka 2019 swa na upungufu wa asilimia 36.9. Hii ilitokana na kupungua kwa misaada kwa ajili ya miradi mbalimbali ya kimkakati kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

**Urari wa Rasilimali Fedha**

125. Urari wa malipo katika rasilimali fedha, unaojumuisha uwekezaji wa moja kwa moja na mikopo ya fedha kutoka nje ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 1,282.2 mwaka 2020 ikilinganishwa na ziada ya dola milioni 1,315.8 mwaka 2019, sawa na punguzo la asilimia 197.4 Kushuka kwa urari wa malipo katika rasilimali fedha kulitokana na kupungua kwa uwekezaji wa moja kwa moja na mapato ya huduma.

**Akiba ya Fedha za Kigeni**

126. Akiba ya fedha za kigeni imebakia katika viwango vya kuridhisha na vyenye kukidhi mahitaji ya nchi ya kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Desemba 2020, akiba ya fedha za kigeni ilifikia dola za Marekani milioni 4,767.7, kiwango ambacho kinatosheleza kulipia uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi cha takriban miezi 5.6. Aidha, kiwango hiki ni zaidi ya lengo la nchi la kukidhi uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa muda wa miezi 4.0, ikiwa pia, ni juu ya lengo lililokubalika katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki la miezi isiyopungua 4.5.

**Soko la Fedha za Kigeni kwa Mabenki**

127. Viwango vya ubadilishanaji fedha za kigeni katika soko la jumla la fedha za kigeni vimeendelea kuamuliwa na nguvu ya soko katika kipindi chote cha mwaka 2020. Katika mwaka 2020, kiasi cha dola za Marekani milioni 618.8 kiliuzwa katika soko la jumla la fedha za kigeni ikilinganishwa na dola milioni 1,280.4 kwa mwaka 2019. Aidha, Benki Kuu ya Tanzania iliendelea kushiriki katika soko hilo la fedha za kigeni kama moja ya nyenzo za utekelezaji wa sera ya fedha katika kusimamia ukwasi na

kukidhi mahitaji ya uagizaji bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi, kwa kuuza jumla ya dola za Marekani milioni 224.6, sawa na asilimia 36.3 ya mauzo yote, pamoja na kununua dola za Marekani milioni 87.0.

**Mwenendo wa Thamani ya Shilingi ya Tanzania**

128. Thamani ya shilingi iliendelea kuwa imara na thabiti dhidi ya fedha za kigeni za washirika wetu wakuu wa kibiashara ulimwenguni katika kipindi chote cha mwaka 2020. Katika soko la jumla la fedha za kigeni, dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa shilingi za Tanzania 2,305.6 ikilinganishwa na shilingi 2,299.8 kwa dola ya Marekani mwaka 2019. Kuimarika kwa shilingi ya Tanzania kulitokana na mfumuko mdogo wa bei, utekelezaji wa sera thabiti za fedha na bajeti, bei ndogo ya mafuta katika soko la dunia na nakisi ndogo ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho mali nchi za nje. Aidha, dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa shilingi 2,309.8 mwishoni mwa mwaka 2020 ikilinganishwa na wastani wa shilingi 2,300.0 mwishoni mwa mwaka 2019.

**THAMANI YA BIDHAA ZA BIASHARA BAINA YA TANZANIA NA NCHI ZA NJE**

Jedwali Na.25 Shs. Milioni

| Aina ya Bidhaa | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019r | 2020 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Zilizouzwa Nje | 8,223,206 | 8,527,450 | 9,582,943 | 10,610,721 | 10,053,844 | 10,064,249 | 11,378,808 | 13,882,711.95 |
| Bidhaa Halisi | 7,012,100 | 7,060,772 | 7,979,691 | 9,303,457 | 8,779,726 | 8,307,170 | 10,824,002 | 13,673,643.32 |
| Zilizouzwa Tena | 1,211,106 | 363,174 | 673,214 | 422,502 | 319,086 | 422,733 | 554,806 | 209,068.63 |
| Zilizoagizwa | 19,904,472 | 18,041,771 | 19,542,294 | 18,425,925 | 16,831,696 | 18,789,124 | 20,939,079 | 19,631,817.90 |
| **Jumla** | 28,127,678 | 26,569,220 | 29,125,237 | 29,036,647 | 26,885,540 | 28,853,373 | 32,317,886 | 33,514,529.85 |
| Urari | -11,681,266 | -9,514,321 | -9,959,352 | -7,815,204 | -6,777,852 | -8,724,875 | -9,560,271 | -5749105.95 |

**Chanzo**: Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Idara ya forodha na Benki Kuu ya Tanzania
**r** -Takwimu zimeboreshwa

## KIASI NA THAMANI YA BIDHAA MUHIMU ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE

Jedwali Na. 26

| | Kiasi (000" Tani) | | | | | | Thamani (sh. Milioni) | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Bidhaa** | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | Badiliko (%) 2019/20 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | Badiliko (%) 2019/20 |
| Kahawa | 51.9 | 58.7 | 41.8 | 56.6 | 76.2 | -16.0 | 334,594 | 281,441 | 335,102 | 349,423 | 331453.3 | -5.1 |
| Pamba | 29.1 | 33.0 | 25.3 | 47.4 | 79.0 | -8.1 | 101,792 | 81,940 | 154,811 | 212,310 | 199,823 | -5.9 |
| Katani | 15.2 | 8.6 | 17.0 | 20.3 | 12.2 | -8.0 | 37,509 | 64,046 | 73,686 | 53,829 | 40,071 | -25.6 |
| Chai | 27.5 | 26.3 | 27.5 | 26.9 | 31.7 | -23.9 | 97,512 | 109,515 | 103,745 | 104,044 | 73,987 | -28.9 |
| Tumbaku | 66.3 | 74.3 | 48.3 | 72.2 | 42.6 | -0.1 | 738,458 | 436,423 | 611,201 | 389,502 | 339,428 | -12.9 |
| Korosho | 171.7 | 217.5 | 329.4 | 120.2 | 295.6 | 8.5 | 697,193 | 1,180,627 | 248,063 | 821,945 | 824,634 | 0.3 |
| Karafuu | 2.8 | 4.9 | 6.9 | 1.3 | 1.8 | 97.8 | 22,801 | 123,518 | 821 | 20,807 | 38,916 | 87.0 |
| Almasi (Carat) | 235,951 | 282,032 | 408,656 | 590,000 | 154,331 | -73.8 | 84,625 | 143,628 | 185,166 | 184,967 | 46,080 | -75.1 |
| Dhahabu(gms) | 81,561,000 | 54,660,377 | 60,784,383 | 81,098,466 | 66,871,115 | -17.5 | 3,284,790 | 3,434,956 | 3,450,863 | 5,043,077 | 6,752,407 | 33.9 |


**Chanzo**: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Idara ya forodha, TRA

**KIASI NA THAMANI YA BIDHAA ZA ASILIA NA ZISIZO ZA ASILIA ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE**


Jedwali Na. 27

| | Kiasi (000" Tani) | | | | | | Badiliko (%) | Thamani (Milioni US$) | | | | | | Badiliko (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Bidhaa** | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019r | 2020 | 2019/20 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | 2019/20 |
| Bidhaa Asilia: | | | | | | | | | | | | | | |
| Kahawa | 51.9 | 58.7 | 41.8 | 56.6 | 76.2 | 64.0 | -16.0 | 162.2 | 153.7 | 126.3 | 147.9 | 152.2 | 145.2 | -4.6 |
| Pamba | 29.1 | 33.0 | 25.3 | 47.4 | 79.0 | 72.6 | -8.1 | 30.2 | 46.8 | 36.8 | 68.4 | 91.8 | 87.5 | -4.6 |
| Katani | 15.2 | 8.6 | 17.0 | 20.3 | 12.2 | 11.2 | -8.0 | 26.5 | 17.2 | 28.7 | 32.5 | 19.3 | 17.6 | -8.9 |
| Chai | 27.5 | 26.3 | 27.5 | 26.9 | 31.7 | 24.1 | -23.9 | 44.0 | 44.8 | 49.1 | 45.9 | 45.7 | 32.4 | -29.1 |
| Tumbaku | 66.3 | 74.3 | 48.3 | 72.2 | 42.6 | 42.6 | -0.1 | 287.6 | 339.2 | 195.8 | 270.3 | 146.5 | 148.7 | 1.5 |
| Korosho | 171.7 | 217.5 | 329.4 | 120.2 | 295.6 | 320.9 | 8.5 | 218.8 | 320.2 | 529.6 | 196.5 | 353.1 | 359.6 | 1.8 |
| Karafuu | 2.8 | 4.9 | 6.9 | 1.3 | 1.8 | 3.6 | 97.8 | 24.1 | 39.3 | 54.4 | 10.5 | 9.1 | 17.1 | 87.9 |
| **Jumla** | | | | | | | | **793.3** | **961.2** | **1,020.7** | **772.1** | **817.7** | **808.1** | **-1.2** |
| Bidhaa zisizo asilia: | | | | | | | | | | | | | | |
| Madini | | | | | | | | 1,285.4 | 1,930.0 | 1,694.5 | 1,615.3 | 2,326.7 | 3,369.1 | 44.8 |
| Bidhaa za Viwanda | | | | | | | | 1,277.0 | 714.2 | 693.7 | 794.6 | 851.8 | 908.6 | 6.7 |
| Samaki na Mazao ya Samaki | | | | | | | | 173.5 | 143.7 | 193.0 | 158.4 | 168.0 | 139.6 | -16.9 |
| Mazao ya Mboga na Maua | | | | | | | | 24.4 | 24.8 | 27.2 | 33.0 | 202.4 | 274.1 | 35.4 |
| Bidhaa zilizouzwa tena | | | | | | | | 385.8 | 187.7 | 126.5 | 175.6 | 242.8 | 87.7 | -63.9 |
| Bidhaa nyinginezo | | | | | | | | 894.0 | 538.1 | 357.1 | 432.5 | 394.3 | 474.2 | -20.3 |
| **Jumla** | | | | | | | | **4,040.1** | **3,538.5** | **3,091.9** | **3,209.3** | **4,186.0** | **5,253.3** | **25.5** |
| Bidhaa Zisizorekodiwa | | | | | | | | 483.3 | 450.0 | 411.3 | 398.1 | 373.8 | 310.4 | -17.0 |
| **JUMLA KUBWA** | | | | | | | | **5,316.8** | **4,949.7** | **4,523.9** | **4,379.6** | **5,377.6** | **6,371.7** | **18.5** |


**Kielelezo Na.4.3: MWENENDO WA THAMANI YA BIDHAA ASILIA NA ZISIZO ASILIA ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE (MILIONI)**



**Kielelezo Na.4.4: KIASI CHA PAMBA NA KAHAWA ILIYOUZWA NCHI ZA NJE**



**Kielelezo Na.4.5: MCHANGO WA BIDHAA ASILIA NA ZISIZO ASILIA ZILIZOUZWA NJE**



**WASTANI WA BEI YA BIDHAA MUHIMU ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE**

Jedwali Na. 28 Sh./Tani*

| **Bidhaa** | **2014** | **2015** | **2016** | **2017** | **2018** | **2019r** | **2020** | Badiliko (%) 2019/20 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kahawa | 4,620,772 | 5,440,481 | 5,696,882 | 6,729,323 | 5,910,939 | 4,585,610 | 5,178,939 | 12.9 |
| Pamba | 1,056,627 | 1,810,254 | 3,082,925 | 3,232,598 | 3,269,171 | 2,690,875 | 2,753,527 | 2.3 |
| Katani | 2,412,232 | 3,471,979 | 4,358,643 | 3,759,421 | 3,632,793 | 3,901,618 | 3,575,866 | -8.3 |
| Chai | 3,227,164 | 3,199,976 | 3,702,858 | 3,975,372 | 3,865,620 | 3,292,541 | 3,070,579 | -6.7 |
| Tumbaku | 3,111,126 | 6,468,558 | 9,933,320 | 9,039,462 | 8,468,137 | 9,143,243 | 7,975,654 | -12.8 |
| Korosho | 1,802,912 | 2,277,753 | 3,205,456 | 3,582,971 | 3,537,608 | 2,759,651 | 2,570,147 | -6.9 |
| Karafuu | 16,901,202 | 16,449,051 | 17,393,365 | 17,530,187 | 12,011,337 | 16,005,679 | 10,868,651 | -32.1 |
| Almasi (kwa carat) | 309,019 | 353,121 | 786,301 | 507,080 | 453,109 | 313,503 | 298,578 | -4.8 |
| Dhahabu (kwa gramu) | 62,795 | 56,146 | 37,527 | 62,555 | 56,767 | 62,185 | 100,976 | 62.4 |

**Chanzo**: Idara ya Forodha, Mamlaka ya Mapato Tanzania
**r** - Takwimu zimeboreshwa
* Isipokuwa kwa almasi na dhahabu


**WASTANI WA BEI YA BIDHAA MUHIMU ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE**

Jedwali Na. 29 US$/Tani*

| **Bidhaa** | **2014** | **2015** | **2016** | **2017** | **2018** | **2019r** | **2020** | **Badiliko (%) 2019/20** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kahawa | 2,796 | 2,740 | 2,617 | 3,019 | 2,611 | 2,017 | 2,269 | 12.5 |
| Pamba | 639 | 912 | 1,416 | 1,450 | 1,444 | 1,147 | 1,206 | 5.2 |
| Katani | 1,460 | 1,749 | 2,002 | 1,687 | 1,604 | 2,109 | 1,566 | -25.7 |
| Chai | 1,953 | 1,612 | 1,701 | 1,784 | 1,707 | 1,446 | 1,346 | -6.9 |
| Tumbaku | 1,883 | 3,258 | 4,563 | 4,056 | 3,740 | 3,441 | 3,494 | 1.5 |
| Korosho | 1,091 | 1,147 | 1,472 | 1,608 | 1,562 | 1,193 | 1,121 | -6.1 |
| Karafuu | 10,228 | 8,285 | 7,989 | 7,865 | 5,305 | 7,000 | 4,770 | -31.9 |
| Almasi (kwa carat) | 187 | 178 | 361 | 228 | 200 | 138 | 131 | -4.9 |
| Dhahabu (kwa gramu) | 38 | 28 | 17 | 28 | 25 | 27 | 44 | 61.1 |

**Chanzo**: Idara ya forodha, TRA
*  Isipokuwa kwa almasi na dhahabu
**r** - Takwimu zimeboreshwa

**Kielelezo Na. 4.6: MWENENDO WA BEI YA PAMBA NA KAHAWA ILIYOUZWA NJE (US$/TANI)**




## MIZANIA YA MALIPO

Jedwali Na. 30 Dola za Marekani

| | 2015 Halisi | 2016 Halisi | 2017 Halisi | 2018 Halisi | 2019 Halisi | 2020 Halisi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Urari wa Biashara** | **-5016.3** | **-3589.8** | **-3041.0** | **-4190.4** | **-3415.5** | **-1517.2** |
| Zilizouzwa nje (fob) | 4826.7 | 4873.9 | 4510.8 | 4292.7 | 5377.6 | 6371.7 |
| Zilizonunuliwa toka nje (fob)* | 9843.1 | 8463.6 | 7551.7 | 8483.1 | 8793.1 | 7889 |
| | | | | | | |
| **Urari wa Huduma** | **783.3** | **1422.9** | **1792.0** | **2098.8** | **2498.5** | **943.7** |
| Mapato | 3412.4 | 3599.3 | 3831.9 | 4014.7 | 4281.0 | 2182.9 |
| Malipo | 2629.1 | 2176.4 | 2039.9 | 1915.9 | 1782.5 | 1239.2 |
| | | | | | | |
| **Urari wa Mapato ya Vitega Uchumi** | -724.3 | -955.1 | -980.1 | -625.2 | -992.5 | -854.8 |
| Yaliyoingia | 110.3 | 98.5 | 125.3 | 155.9 | 212.4 | 111.19 |
| Yaliyotoka | 834.6 | 1053.6 | 1105.4 | 781.1 | 1204.9 | 966.01 |
| **Urari wa Uhamisho Mali wa Kawaida** | 479.9 | 381.5 | 402.0 | 468.5 | 418.5 | 433.6 |
| Iliyoingia | 560.1 | 452.7 | 485.2 | 535.8 | 474.9 | 486.29 |
| Serikalini | 194.8 | 81.1 | 121.8 | 170.3 | 103.5 | 183.06 |
| Sekta nyingine | 365.3 | 371.6 | 363.4 | 365.5 | 371.4 | 303.23 |
| Iliyotoka | 80.2 | 71.2 | 83.2 | 67.3 | 56.4 | 52.701 |
| **Urari wa Biashara ya Bidhaa, Huduma na Uhamisho Mali** | **-4477.4** | **-2740.5** | **-1827.1** | **-2248.3** | **-1490.9** | **-994.8** |
| | | | | | | |
| **Urari wa Uhamisho wa Mitaji** | **380.1** | **446.2** | **376.8** | **464.1** | **481.2** | **303.6** |
| Iliyoingia | 380.1 | 446.2 | 376.8 | 464.1 | 481.2 | 303.61 |
| Iliyotoka | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| | | | | | | |
| **Urari katika uwekezaji** | **2586.0** | **1734.9** | **1811.1** | **1668.1** | **2599.5** | **682.8** |
| Uwekezaji katika miradi | 1506.0 | 864.0 | 937.7 | 971.6 | 1217.2 | 684.89 |
| Uwekezaji katika hisa | 27.6 | -5.0 | 2.9 | -3.7 | 36.8 | -2.0771 |
| Uwekezaji aina nyingine | 1052.3 | 875.8 | 870.4 | 700.3 | 1345.5 | |
| | | | | | | |
| Makosa na Masahihisho | 1286.5 | 839.3 | 1183.3 | -635.2 | -728.8 | -664.78 |
| | | | | | | |
| **Urari wa Malipo yote** | **-224.8** | **279.8** | **1643.9** | **-790** | **587** | **-764.9** |

**Chanzo**: Benki Kuu ya Tanzania

**Kielelezo Na. 4.7: MWENENDO WA URARI KATIKA MIZANIA YA MALIPO NA NCHI ZA NJE (Milioni)**



## SURA YA 5

## HALI YA UCHUMI WA DUNIA NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA

### HALI YA UCHUMI WA DUNIA

#### Ukuaji wa Uchumi

129. Mwaka 2020, uchumi wa dunia uliporomoka na kufikia ukuaji hasi wa asilimia 3.3 ikilinganishwa na ukuaji chanya wa asilimia 2.8 mwaka 2019. Kuporomoka kwa uchumi wa dunia kulisababishwa na kupungua kwa shughuli za kiuchumi duniani hususan, biashara, usafirishaji na utalii kutokana na athari za UVIKO-19. Aidha, hatua mbalimbali zilizochukuliwa na mataifa mengi duniani kukabiliana na athari za maambukizi ya ugojwa huu zikiwemo kufungia raia ndani wasijihusishe na shughuli za kiuchumi (lockdown), kufunga mipaka ya nchi na shughuli za kibiashara ndani na nje ya nchi zilisababisha uchumi wa dunia kuporomoka hususan kwa nchi zinazotegemea utalii na biashara ya nje.

130. Mwaka 2020, nchi zilizoendelea zilikuwa na ukuaji hasi wa asilimia 4.7 ikilinganishwa na ukuaji chanya wa asilimia 1.6 mwaka 2019. Kushuka kwa kasi ya ukuaji kulitokana na athari za UVIKO-19 ambapo nchi zilizoendelea zilisitisha shughuli za kiuchumi na kijamii kwa lengo la kudhibiti maambukizi.

131. Mwaka 2020, nchi zinazoendelea zilikuwa na ukuaji hasi wa asilimia 2.2 ikilinganishwa na ukuaji chanya wa asilimia 3.6 mwaka 2019. Katika kipindi hicho, ukuaji wa uchumi katika nchi za Asia zinazoendelea ikijumuisha China na India zilikuwa na ukuaji hasi wa asilimia 1.0 ikilinganishwa na ukuaji chanya wa asilimia 5.4 mwaka 2019. Ukuaji hasi wa uchumi kwa nchi zinazoendelea ulitokana na athari za UVIKO-19 zilizosababisha kusimama kwa shughuli za kiuchumi. Aidha, nchi zilizoathirika zaidi ni zile zilizokuwa na milipuko mikubwa ya ndani, kuwa na sera za ndani zisizotabirika na zinazotegemea sana utalii na usafirishaji. Vile vile, majanga ya asili ikiwemo kimbunga cha kitropiki cha Harold nchini Fiji na ukame mkali nchini Thailand yaliongeza athari za kiuchumi katika nchi hizo.

132. Mwaka 2020, nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara zilikuwa na ukuaji hasi wa uchumi wa asilimia 1.9 ikilinganishwa na ukuaji chanya wa asilimia 3.2 mwaka 2019. Ukuaji hasi ulitokana na kupungua kwa mauzo ya bidhaa nje na shughuli za utalii kulikosababishwa na athari za UVIKO-19. Aidha, nchi zinazotegemea utalii kama chanzo kikubwa cha ukuaji wa uchumi zikiwemo Carpe Verde na Mauritius na zile zinazotegemea mafuta (Angola, Cameroon, Chad, Congo, Jamhuri ya Guinea, Gabon, Nigeria na Sudan ya Kusini) zilipata athari kubwa kutokana na UVIKO-19 na kuchangia ukuaji hasi wa nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara. Kwa ujumla mwaka 2020, nchi 32 kati ya 45 za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara zilikuwa na ukuaji hasi wa

uchumi, sawa na asilimia 71.1 ya nchi zote, nchi mbili zilikuwa na ukuaji wa asilimia sifuri na nchi kumi na moja (11) ikiwemo Tanzania zilikuwa na ukuaji chanya wa uchumi.

**Jedwali Na 5.1: Pato la Dunia Mwaka 2016 – 2020**

| | **2016** | **2017** | **2018** | **2019** | **2020** |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Ukuaji (Asilimia)** | | | | |
| Pato la Dunia | 3.1 | 3.8 | 3.6 | 2.8 | -3.3 |
| Nchi zilizoendelea | 1.6 | 2.4 | 2.2 | 1.6 | -4.7 |
| Nchi zinazoendelea | 4.1 | 4.8 | 4.5 | 3.6 | -2.2 |
| Nchi za Asia Zinazoendelea | 6.3 | 6.6 | 6.3 | 5.4 | -1.0 |
| Afrika Kusini ya Jangwa la Sahara | 1.6 | 2.9 | 3.3 | 3.2 | -1.9 |

**Chanzo:** Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), WEO Aprili 2021

**Mwenendo wa Bei**

133. Mwaka 2020, mfumuko wa bei wa dunia ulipungua na kufikia wastani wa asilimia 3.2 ikilinganishwa na asilimia 3.5 mwaka 2019. Hii ilitokana na kupungua kwa shughuli za usafirishaji na hivyo kupunguza mahitaji ya mafuta duniani kulikosababishwa na athari za UVIKO-19. Aidha, sababu za kupungua kwa kasi ya mfumuko wa bei wa dunia zinawiana na zile za nchi zilizoendelea na nchi zinazoendelea za Asia ambapo mfumuko wa bei kwa nchi zilizoendelea ulikuwa wastani wa asilimia 0.7 mwaka 2020 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 1.4 mwaka 2019. Vile vile, wastani wa mfumuko wa bei kwa nchi zinazoendelea za Asia ulikuwa asilimia 3.1 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.3 mwaka 2019.

134. Mwaka 2020, kasi ya ukuaji wa mfumuko wa bei kwa nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara iliongezeka kutoka wastani wa asilimia 8.5 mwaka 2019 na kufikia wastani wa asilimia 10.8. Ongezeko hilo lilisababishwa na upungufu wa chakula kutokana na ukame kwa baadhi ya nchi ikiwemo Burkina Faso, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Mali, Niger na Zimbabwe. Mwaka 2020, wastani wa mfumuko wa bei kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ulikuwa asilimia 11.0 kama ulivyokuwa mwaka 2019. Katika kipindi hicho, nchi ya Rwanda ilikuwa na kiwango kikubwa cha mfumuko wa bei wa asilimia 8.0 na Tanzania ilikuwa na kiwango kidogo cha mfumuko wa bei wa asilimia 3.3.

**Jedwali Na. 5.2: Viwango vya Mfumuko wa Bei katika Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki**

| **Nchi** | **2019** | **2020** |
|---|---|---|
| | Mfumuko wa Bei (Asilimia) | |
| Tanzania | 3.4 | 3.3 |
| Uganda | 2.9 | 3.8 |
| Kenya | 5.2 | 5.3 |
| Rwanda | 2.4 | 8.0 |
| Burundi | 0.7 | 7.3 |
| Sudan ya Kusini | 51.2 | 38.0 |
| **Wastani kwa Afrika Mashariki** | **11.0** | **11.0** |

**Chanzo:** Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), WEO Aprili 2021

**Mwenendo wa Biashara Duniani**

135. Mwaka 2020, biashara ya bidhaa duniani ilikuwa na ukuaji hasi wa asilimia 5.3 ikilinganishwa na ukuaji chanya wa asilimia 0.2 mwaka 2019. Hii ilitokana na hatua za nchi mbalimbali kuzuia shughuli za kiuchumi na kijamii kwa lengo la kudhibiti maambukizi ya UVIKO-19. Athari za ugonjwa huo zilijidhihirisha zaidi katika uuzaji na uagizaji wa bidhaa katika kanda mbalimbali duniani. Aidha, uuzaji wa bidhaa nje ya Bara la Afrika ulikuwa na ukuaji hasi wa asilimia 8.1 mwaka 2020 ikilinganishwa na ukuaji hasi wa asilimia 0.5 mwaka 2019. Vile vile, uagizaji wa bidhaa nje ya Bara la Afrika ulikuwa na ukuaji hasi wa asilimia 8.8 ikilinganishwa na ukuaji chanya wa asilimia 2.6 mwaka 2019.

**Ushirikiano wa Uchumi Kimataifa**

136. Mwaka 2020, Tanzania iliendelea kushirikiana kikamilifu na Jumuiya ya Kimataifa kupitia Umoja wa Mataifa, mashirika ya fedha na biashara ya kimataifa na majukwaa mengine ya kimataifa. Katika kipindi hicho, Tanzania ilijumuishwa katika Programu Shirikishi baina ya Nchi na Washirika wa Maendeleo (Programme for Country Partnership - PCP) ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda (UNIDO). Programu hii inalenga kuzisaidia Nchi Wanachama wa Shirika hilo kujiletea maendeleo jumuishi na endelevu ya viwanda kwa kusaidia utekelezaji wa vipaumbele vya nchi kwa ajili ya maendeleo ya sekta ya viwanda.

137. Mwaka 2020, Tanzania ilishiriki kwenye mijadala ya mikutano ya Kikao cha 75 cha Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa. Ushiriki wa Tanzania kwenye mikutano hiyo ulitoa fursa ya kuieleza jumuiya ya kimataifa hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali katika kuboresha huduma za kijamii, kuongeza fursa za kiuchumi na hivyo kuleta maendeleo kwa mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla. Aidha, mikutano ya Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa imekuwa ikitumika kupigania kuondolewa vikwazo vya kiuchumi kwa nchi wanachama. Katika kipindi hicho, wakati Tanzania ikiwa Mwenyekiti wa Mkutano wa 39 wa SADC, Nchi Wanachama wa Jumuiya hiyo

zilipitisha kwa kauli moja tarehe 25 Oktoba kila mwaka kuwa siku ya kupaza sauti ya kuondolewa kwa vikwazo vya kiuchumi dhidi ya Zimbabwe. Mwaka 2002 nchi ya Zimbabwe iliwekewa vikwazo na Umoja wa Nchi za Ulaya na Marekani kwa madai ya ukiukwaji wa haki za binadamu katika zoezi la mageuzi ya umilikaji wa ardhi.

138. Mwaka 2020, Tanzania ilishiriki kwenye mijadala ya mikutano ya Kikao cha 43 cha Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa. Kupitia mijadala hiyo, jumuiya ya kimataifa ilielezwa kuhusu msimamo wa Tanzania wa kutambua haki za binadamu, ikiwemo haki ya kupata elimu, huduma za afya, maji safi na salama pamoja na nishati. Hatua hizi zimeimarisha mtazamo chanya wa jumuiya ya kimataifa kuhusu Tanzania.

**Ushirikiano wa Kiuchumi Barani Afrika**

139. Mwaka 2020, Rais wa Jamhuri ya Burundi na Rais wa Jamhuri ya Malawi walifanya ziara nchini kwa nyakati tofauti. Baadhi ya masuala yaliyohimizwa katika ziara hizo ni pamoja na kufanyika kwa Mikutano ya Tume ya Pamoja ya Kudumu ya Ushirikiano kati ya nchi hizo na Tanzania, kudumisha ujirani mwema na kukuza uchumi. Aidha, ziara hizo zilitoa fursa ya kuimarisha ushirikiano katika sekta za uchukuzi, utalii, nishati, madini pamoja na huduma za bandari na masuala ya ulinzi na usalama. Vile vile, viongozi wa nchi hizo pamoja na mambo mengine walihimiza Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania kufungua ofisi nchini Malawi na Burundi ili kusogeza huduma katika nchi hizo. Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari ilifungua ofisi Jijini Bujumbura na inaendelea na hatua za kufungua ofisi nchini Malawi.

140. Mwaka 2020, Tanzania iliendelea kushiriki katika majadiliano ya Mkataba wa Eneo Huru la Biashara la Bara la Afrika (African Continental Free Trade Area - AfCFTA). Mkataba huo ulizinduliwa rasmi tarehe 21 Machi, 2018 Kigali, Rwanda, kwenye Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali baada ya nchi 54 kati ya nchi 55 Wanachama wa Umoja wa Afrika ikiwemo Tanzania kusaini Mkataba huo. Nchi pekee ambayo haijasaini Mkataba ni Eritrea. Mkataba huu unahusisha maeneo ya ushirikiano katika biashara ya bidhaa na huduma, uwekezaji, hakimiliki na ubunifu na sera za ushindani. Hadi mwishoni mwa mwaka 2020. jumla ya nchi 18 Wanachama wa Umoja wa Afrika zilikuwa zimewasilisha mapendekezo ya ufunguaji wa soko la bidhaa katika Kamisheni ya Umoja wa Afrika (Africa Union Commission - AUC) kwa lengo la ufunguaji wa soko la bidhaa. Tanzania pia ilishawasilisha mapendekezo yake kwa Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo yalijumuishwa na mapendekezo ya nchi nyingine za Afrika Mashariki (isipokuwa Sudani ya Kusini) na kuwasilishwa Kamisheni ya Umoja wa Afrika.

141. Katika kutekeleza Mkataba huo, nchi za Afrika zilikubaliana kufungua soko la bidhaa (Tariff Offer) kwa kuondoleana ushuru wa forodha kwa makubaliano yafuatayo: asilimia 90 ya bidhaa zitaingizwa katika nchi husika bila kulipiwa ushuru, na utekelezaji wake utafanyika ndani ya miaka 10 kuanzia mwaka 2020/21; asilimia 7 ya bidhaa nyeti

(sensitive list) zitaingia katika nchi mwanachama bila kutozwa ushuru baada ya mwaka wa 5 wa kuanza utekelezaji wa mkataba; na asilimia 3 ya bidhaa hazitafunguliwa (exclusion list) kwa maana zitaendelea kutozwa ushuru. Bidhaa ambazo zitaendelea kutozwa ushuru wa forodha ni pamoja na: vifaranga vya kuku, nyama, matunda na juisi za matunda, mbogamboga, maziwa na bidhaa za maziwa, baadhi ya bidhaa za mafuta ya kula, unga wa ngano na mahindi, sukari, karafuu, saruji na *Clinker*, karatasi na bidhaa za karatasi, nyuzi na vitambaa vya pamba, viatu vya ngozi, vigae (tiles) samani, bidhaa za nondo na mabati.

## USHIRIKIANO WA KIUCHUMI KATIKA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI

### Utekelezaji wa Himaya Moja ya Forodha

142. Mwaka 2020, thamani ya bidhaa zilizouzwa kutoka Tanzania kwenda nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ilifikia dola za Marekani milioni 807.9 kutoka dola za Marekani milioni 674.4 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 19.8. Ongezeko hilo lilitokana na Tanzania kuendelea na shughuli za uzalishaji wakati nchi nyingine wanachama zilifungia raia ndani (lockdown) kwa lengo la kudhibiti kuenea kwa ugonjwa wa homa kali ya mapafu hivyo kuwa na fursa zaidi ya kuuza nje. Bidhaa zilizouzwa kwa wingi ni pamoja na mahindi, mchele, maziwa, chuma na malighafi ya kutengeneza saruji. Aidha, bidhaa zilizonunuliwa kutoka nchi wanachama mwaka 2020 zilikuwa na thamani ya dola za Marekani milioni 324.3 ikilinganishwa na bidhaa zenye thamani ya dola za Marekani milioni 329.2 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 1.5. Upungufu huo ulitokana na athari za ugonjwa wa homa kali ya mapafu katika nchi wananchama. Kutokana na mwenendo huo, urari wa biashara baina ya Tanzania na nchi nyingine za Jumuiya ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 488.3 mwaka 2020 ikilinganishwa na ziada ya dola milioni 345.2 mwaka 2019.

143. Mwaka 2020, muda wa kusafirisha shehena kutoka katika bandari ya Dar-es-Salaam kwenda Rusumo mpakani mwa Rwanda na Tanzania ulifikia siku 7 kutoka siku 3 mwaka 2019. Aidha, muda wa usafirishaji wa shehena kutoka Bandari ya Dar-es-Salaam kwenda mpaka wa Mutukula na Kabanga ulifikia siku 7 mwaka 2020 kutoka siku 4 mwaka 2019. Ongezeko hilo lilitokana na nchi wanachama kutokuwa na itifaki ya pamoja ya upimaji wa madereva wa usafirishaji shehena mipakani ili kukabiliana na maambukizi ya UVIKO-19.

### Mapitio ya Wigo wa Pamoja wa Ushuru wa Forodha

144. Mwaka 2020, Tanzania iliendelea kushiriki katika zoezi la kufanya mapitio ya viwango vya pamoja vya ushuru wa forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Lengo la mapitio hayo ni kuhakikisha viwango vya ushuru wa forodha katika Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki vinaendana na mabadiliko ya kiuchumi katika nchi wanachama sambamba na kulinda viwanda na wazalishaji wa ndani dhidi ya bidhaa zinazoagizwa kutoka nje ya Jumuiya. Viwango vya ushuru wa forodha vinavyotumika katika Jumuiya

ya Afrika Mashariki kwa sasa ni: Asilimia 0 kwa malighafi na bidhaa za mitaji; asilimia 10 kwa bidhaa zilizosindikwa kwa kiwango cha kati; na kiwango cha asilimia 25 kwa bidhaa za mwisho za mlaji.

**Itifaki ya Umoja wa Fedha wa Afrika Mashariki**

145. Itifaki ya Umoja wa Fedha wa Afrika Mashariki imeweka vigezo vya kufikia muungano wa kifedha thabiti na kuwa na sarafu moja ifikapo mwaka 2024. Hadi Juni 2019/20, Tanzania pekee kati ya nchi sita (6) wanachama ilikidhi vigezo vya msingi vya kuingia katika Umoja wa Fedha wa Afrika Mashariki. Katika kipindi hicho, mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 3.3 ikilinganishwa na lengo la mfumuko wa bei usiozidi asilimia 8, deni la Serikali la asilimia 27.1 ya Pato la Taifa kwa viwango vya sasa vya thamani ikilinganishwa na lengo la lisilozidi asilimia 50 na akiba ya fedha za kigeni ilikidhi uagizaji wa bidhaa kwa miezi 6.0 ikilinganishwa na lengo lisilopungua miezi 4.5.

**Jedwali Na. 5.3: Vigezo vya Muunganiko wa Uchumi Jumla na Hatua Iliyofikiwa na Nchi Wanachama**

| **Kigezo** | **Nchi** | **2016/17** | **2017/18** | **2018/19** | **2019/20** |
|---|---|---|---|---|---|
| Mfumuko wa bei usiozidi asilimia 8 | Burundi | 16.1 | -2.6 | -0.8 | |
| | Kenya | 6.6 | 6.5 | 8.1 | 5.2 |
| | Rwanda | 6.8 | 2.3 | 0.8 | 6.3 |
| | Sudani ya Kusini | 117.7 | 40.1 | 69.0 | 37.7 |
| | Tanzania | 5.3 | 4.3 | 3.2 | 3.5 |
| | Uganda | 5.7 | 3.4 | 3.1 | 3.0 |
| Nakisi ya bajeti (pamoja na misaada) isiyozidi asilimia 3 ya Pato la Taifa | Burundi | -4.6 | -4.5 | -4.3 | |
| | Kenya | -8.1 | -7.1 | -9.1 | -7.8 |
| | Rwanda | -4.5 | -4.6 | -5.6 | -7.2 |
| | Sudani ya Kusini | | | | |
| | Tanzania | -1.4 | -1.9 | -3.2 | -1.4 |
| | Uganda | -3.9 | -4.1 | -4.9 | -7.2 |
| Deni la umma lisilozidi asilimia 50 ya Pato la Taifa kwa viwango vya sasa vya thamani | Burundi | 42.5 | 47.3 | 52.2 | |
| | Kenya | 45.8 | 48.7 | 49 | 48.6 |
| | Rwanda | 26.7 | 27.9 | 29 | 34.7 |
| | Sudani ya Kusini | | | | |
| | Tanzania | 34.4 | 33 | 27.2 | 27.1 |
| | Uganda | 27.7 | 30.7 | 26.8 | 30.9 |
| Akiba ya fedha za kigeni isiyopungua miezi 4.5 ya uagizaji bidhaa | Burundi | 1.7 | 1.0 | 1.5 | |
| | Kenya | 4.5 | 5.4 | 5.7 | 5.8 |
| | Rwanda | 4.0 | 4.4 | 4.5 | 5.7 |
| | Sudani ya Kusini | 0.00 | 0.00 | 0.01 | 0.00 |
| | Tanzania | 5.7 | 6.1 | 4.3 | 6.0 |
| | Uganda | 5.7 | 4.2 | 4.3 | 5.2 |

**Chanzo:** Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki

146. Mwaka 2020, Tanzania iliendelea kushiriki katika majadiliano ya Miswada ya Sheria za kuanzisha Taasisi za Umoja wa Fedha ambapo majadiliano hayo yalikamilika katika ngazi ya wataalamu. Kwa upande wa urasinishaji wa sera na sheria za Jumuiya, Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zilifanikiwa kurasinisha kodi za

ndani na hivyo kupatikana kwa Sera ya Kodi za Ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Sera hii inawezesha Jumuiya kuwa na viwango vya kodi za ndani vyenye uwiano ili kuwa ni ukanda tulivu wa kifedha na uwekezaji.

**Ushirikiano Baina ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Kanda Nyingine**

147. Mwaka 2020, majadiliano kuhusu Mkataba wa Eneo Huru la Biashara la Utatu wa COMESA-EAC-SADC yalifanyika. Majadiliano hayo yalihusu viambatisho vya mkataba vilivyosalia katika awamu ya kwanza ikiwemo ufunguaji wa biashara ya bidhaa, kanuni za utambuzi wa uasilia wa bidhaa, masuala ya afya za wanyama, mimea na binadamu, vikwazo vya biashara visivyo vya kiforodha na vikwazo vya kiufundi vya kibiashara.

**Sekta za Miundombinu na Huduma za Jamii katika Jumuiya ya Afrika Mashariki**

148. Mwaka 2020, nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ziliendelea na utekelezaji wa maazimio ya Soko la Pamoja na uendelezaji wa miundombinu hususan Mpango wa Kuendeleza Mtandao wa Barabara za Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika kipindi hicho, Tanzania iliendelea na ujenzi wa Barabara za Kikanda za Nyakanazi- Kasulu-Manyovu/Rumonge-Rutunga-Bujumbura ambapo hadi kufikia Desemba 2020 ujenzi wa barabara kipande cha Nyakanazi-Kabingo chenye urefu wa kilometa 50 ulifikia asilimia 97. Aidha, hatua za awali za ujenzi wa barabara kipande cha Kabingo-Kasulu-Manyovu chenye urefu wa kilometa 260 ulianza.

149. Mwaka 2020, ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Utoaji Huduma Mipakani katika mpaka wa Songwe/Kasumulu unaounganisha nchi za Tanzania na Malawi ulifikia asilimia 44. Katika kipindi hicho, Ripoti ya Utafiti wa Awali ya Hali ya Usafiri wa Majini na Sekta ya Bandari ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki iliandaliwa. Kwa mujibu wa Ripoti hiyo, Nchi Wanachama ziliendelea kutekeleza miradi ya kuendeleza Sekta ya Bandari.

## SURA YA 6

## RASILIMALI WATU

**Idadi ya Watu**

150. Mwaka 2020, idadi ya watu Tanzania iliongezeka kwa asilimia 3.1 na kufikia watu 57,637,628 ikilinganishwa na watu 55,890,747 mwaka 2019. Tanzania Bara ilikadiriwa kuwa na watu 55,966,030, sawa na asilimia 97.1 ya watu wote na Tanzania Zanzibar ilikadiriwa kuwa na watu 1,671,598. Aidha, wanaume walikadiriwa kuwa 28,229,599, sawa na asilimia 49.0 ya watu wote na wanawake walikadiriwa kuwa 29,408,029. Makadirio haya yalitokana na maoteo ya idadi ya watu kwa kutumia matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012 pamoja na viashiria muhimu vya mabadiliko ya idadi ya watu vikijumuisha uzazi, vifo na uhamiaji.

**Mgawanyiko wa Watu Kimkoa**

151. Mwaka 2020, mkoa wa Dar es Salaam ulikadiriwa kuwa na watu 5,401,814, sawa na asilimia 9.7 ya watu wote Tanzania Bara ambayo ni idadi kubwa ikilinganishwa na mikoa mingine ukifuatiwa na mkoa wa Mwanza uliokadiriwa kuwa na watu 3,826,573, sawa na asilimia 6.8. Idadi kubwa ya watu katika mkoa wa Dar es Salaam ilichangiwa na upatikanaji wa huduma muhimu za kijamii na fursa za kiuchumi zilizosababisha watu kuhamia kutoka mikoa mingine. Aidha, mkoa wa Katavi ulikuwa na idadi ndogo zaidi ya watu wapatao 805,887, sawa na asilimia 1.4 ya watu wote Tanzania Bara ukifuatiwa na mkoa wa Njombe uliokuwa na watu 837,557 sawa na asilimia 1.5 na Lindi 1,025,800 sawa na asilimia 1.8. Kwa upande wa Tanzania Zanzibar, mkoa wa Mjini Magharibi ulikuwa na idadi kubwa ya watu wapatao 733,914, sawa na asilimia 43.9 ya watu wote Tanzania Zanzibar. Mkoa wa Kaskazini Pemba ulikadiriwa kuwa na watu 294,267 (asilimia 17.6) na mkoa wa Kusini Unguja ulikadiriwa kuwa na idadi ndogo zaidi ya watu wapatao 138,589, sawa na asilimia 8.3.

152. Msongamano wa watu kwa Tanzania ulikuwa wastani wa watu 65 kwa kila kilometa ya mraba mwaka 2020 ikilinganishwa na wastani wa watu 63 mwaka 2019. Aidha, msongamano wa watu Tanzania Bara ulikuwa wastani wa watu 63 kwa kila kilometa ya mraba. Mkoa wa Dar es Salaam ulikuwa na msongamano mkubwa zaidi ukiwa na wastani wa watu 3,878 kwa kila kilometa ya mraba, ukifuatiwa na Mwanza (wastani wa watu 404), Kilimanjaro (wastani wa watu 147) na Kagera (wastani wa watu 128). Aidha, mkoa wa Lindi ulikuwa na msongamano mdogo zaidi ukiwa na wastani wa watu 16 kwa kila kilometa ya mraba, ukifuatiwa na mkoa wa Katavi wastani wa watu 18 kwa kila kilometa ya mraba. Kwa upande wa Tanzania Zanzibar, Mkoa wa Mjini Magharibi ulikuwa na msongamano mkubwa wa wastani wa watu 3,191 kwa kila kilometa ya mraba ukifuatiwa na Mkoa wa Kusini Pemba uliokuwa na wastani wa watu

820 kwa kila kilometa ya mraba. Mkoa wa Kusini Unguja ulikuwa na msongamano mdogo zaidi ukiwa na wastani wa watu 162 kwa kila kilometa ya mraba.


153. Mwaka 2020, idadi ya watoto wenye umri chini ya miaka minne ilikuwa 9,851,027, sawa na asilimia 17.1 ya watu wote Tanzania. Watu wenye umri wa miaka mitano (5) hadi tisa (9) walikuwa 7,982,216 sawa na asilimia 13.8. Aidha, idadi ya watu wenye umri wa miaka 15 hadi 19 walikuwa 6,055,232 sawa na asilimia 10.5 ya watu wote; watu wenye umri wa miaka 25 hadi 29 ilikuwa 4,375,259, sawa na asilimia 7.6; watu wenye umri wa miaka 40 hadi 44 walikuwa 2,572,072, sawa na asilimia 4.5; na watu wenye umri zaidi ya miaka 80 walikuwa 306,986, sawa na asilimia 0.5. Katika kipindi hicho, watu wenye umri wa miaka 15 hadi 64 ambao ni nguvukazi ya Taifa walikuwa 30,947,502, sawa na asilimia 53.7 ya watu wote nchini. Wazee wa zaidi ya miaka 65 na wategemezi wenye chini ya umri wa miaka 14 walikuwa asilimia 46.3 ya watu wote.

**Jedwali Na. 6.1: Mchanganuo wa Idadi ya Watu kwa Makundi ya Umri na Jinsi Tanzania kwa Mwaka 2020**

| **Umri** | **Jinsi** | | | **Asilimia** |
|---|---|---|---|---|
| | **Wanaume** | **Wanawake** | **Jumla** | |
| 0 - 4 | 4,972,289 | 4,878,738 | 9,851,027 | 17.1 |
| 5 - 9 | 4,013,263 | 3,968,953 | 7,982,216 | 13.8 |
| 10-14 | 3,582,899 | 3,568,790 | 7,151,689 | 12.4 |
| 15 - 19 | 3,014,118 | 3,041,114 | 6,055,232 | 10.5 |
| 20 - 24 | 2,656,362 | 2,674,122 | 5,330,484 | 9.2 |
| 25 - 29 | 2,042,003 | 2,333,256 | 4,375,259 | 7.6 |
| 30 - 34 | 1,642,384 | 1,971,517 | 3,613,901 | 6.3 |
| 35 - 39 | 1,464,246 | 1,732,225 | 3,196,471 | 5.5 |
| 40 - 44 | 1,241,782 | 1,330,290 | 2,572,072 | 4.5 |
| 45 - 49 | 1,032,732 | 1,113,792 | 2,146,524 | 3.7 |
| 50 - 54 | 758,908 | 762,341 | 1,521,249 | 2.6 |
| 55 - 59 | 605,139 | 713,099 | 1,318,238 | 2.3 |
| 60 - 64 | 411,344 | 406,728 | 818,072 | 1.4 |
| 65 - 69 | 312,655 | 351,895 | 664,550 | 1.2 |
| 70 - 74 | 199,196 | 211,801 | 410,997 | 0.7 |
| 75 - 79 | 141,944 | 180,717 | 322,661 | 0.6 |
| 80+ | 138,335 | 168,651 | 306,986 | 0.5 |
| **Jumla** | **28,229,599** | **29,408,029** | **57,637,628** | **100** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Kielelezo Na. 6.1: Idadi ya Watu kwa Umri Tanzania (2020)**




**Jedwali Na. 6.2: Mchanganuo wa Idadi ya Watu kwa Makundi ya Umri na Jinsi Tanzania Bara kwa Mwaka 2020**

| Umri | Jinsi | | Jumla | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| | Wanaume | Wanawake | | |
| 0 - 4 | 4,836,109 | 4,745,067 | 9,581,176 | 17.1 |
| 5 - 9 | 3,896,605 | 3,853,979 | 7,750,584 | 13.8 |
| 10-14 | 3,483,136 | 3,469,159 | 6,952,295 | 12.4 |
| 15 - 19 | 2,931,131 | 2,957,201 | 5,888,332 | 10.5 |
| 20 - 24 | 2,577,994 | 2,594,298 | 5,172,292 | 9.2 |
| 25 - 29 | 1,979,967 | 2,259,850 | 4,239,817 | 7.6 |
| 30 - 34 | 1,591,792 | 1,909,217 | 3,501,009 | 6.3 |
| 35 - 39 | 1,423,310 | 1,681,374 | 3,104,684 | 5.5 |
| 40 - 44 | 1,206,784 | 1,290,655 | 2,497,439 | 4.5 |
| 45 - 49 | 1,002,335 | 1,077,881 | 2,080,216 | 3.7 |
| 50 - 54 | 735,851 | 738,648 | 1,474,499 | 2.6 |
| 55 - 59 | 584,421 | 687,078 | 1,271,499 | 2.3 |
| 60 - 64 | 396,931 | 394,965 | 791,896 | 1.4 |
| 65 - 69 | 302,407 | 342,363 | 644,770 | 1.2 |
| 70 - 74 | 193,180 | 206,753 | 399,933 | 0.7 |
| 75 - 79 | 137,807 | 176,320 | 314,127 | 0.6 |
| 80+ | 135,680 | 165,782 | 301,462 | 0.5 |
| **Jumla Kuu** | **27,415,440** | **28,550,590** | **55,966,030** | **100.0** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

## Nguvu Kazi na Ajira

154. Mwaka 2020, asilimia 72.7 ya watu wenye umri wa zaidi ya miaka 15 walikuwa katika ajira na baadhi ya waliobakia walikuwa hawana ajira na wengine walikuwa hawana kazi lakini hawakuwa tayari kufanya kazi kutokana aidha na ugonjwa, walikuwa masomoni au kwa sababu nyingine.

**Jedwali Na:6.3: Mchanganuo wa Uwiano wa Ajira kwa Idadi ya Watu**

| | 2019 | | | 2020 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Wanawake** | **Wanaume** | **Jumla** | **Wanawake** | **Wanaume** | **Jumla** |
| Idadi ya watu (15+) | 16,067,308 | 14,529,859 | 30,597,167 | 16,636,966 | 15,045,009 | 31,681,975 |
| Ajira (15+) | 10,888,559 | 11,562,986 | 22,451,545 | 11,043,823 | 11,986,131 | 23,029,954 |
| Uwiano wa ajira kwa idadi ya watu (Asilimia) | 67.8 | 79.6 | 73.4 | 66.4 | 79.7 | 72.7 |

**Chanzo**: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

155. Mwaka 2020, jumla ya watu 23,029,954 kati ya watu 25,436,904 waliokuwa katika soko la ajira walikuwa wameajiriwa katika sekta mbalimbali za kiuchumi ikilinganishwa na watu 22,451,545 mwaka 2019. Kati ya hizo, ajira 11,043,823 sawa na asilimia 48.0 zilikuwa ajira za wanawake na ajira 11,986,131 wanaume. Aidha, asilimia 5.8 ya ajira zote zilikuwa kwa ajili ya watu wenye ulemavu. Katika kipindi hicho, sekta ya kilimo, misitu na uvuvi ilitoa asilimia 61.5 ya ajira zote ikifuatiwa na sekta ya biashara na matengenezo (asilimia 14.5). Kwa upande mwingine, sekta ya upangishaji majengo ilichangia asilimia 0.04 ya ajira zote ikiwa na mchango mdogo kuliko sekta nyingine.

**Jedwali Na. 6.4: Mchanganuo wa Ajira kwa Sekta**

| **Sekta** | **Wanaume** | **Wanawake** | **Jumla** | **Mchango wa Sekta (Asilimia)** |
|---|---|---|---|---|
| Kilimo, misitu na uvuvi | 7,390,435 | 6,778,951 | 14,169,386 | 61.5 |
| Uchimbaji wa madini na mawe | 224,524 | 108,952 | 333,476 | 1.4 |
| Viwanda | 487,227 | 366,133 | 853,360 | 3.7 |
| Usambazaji wa umeme | 22,387 | 3,018 | 25,405 | 0.1 |
| Maji safi na maji taka | 14,076 | 4,347 | 18,423 | 0.1 |
| Ujenzi | 697,402 | 26,991 | 724,393 | 3.1 |
| Biashara na matengenezo | 1,298,969 | 2,047,781 | 3,346,750 | 14.5 |
| Uchukuzi na uhifadhi mizigo | 709,000 | 31,715 | 740,715 | 3.2 |
| Malazi na huduma ya chakula | 180,389 | 771,697 | 952,086 | 4.1 |
| Habari na mawasiliano | 40,432 | 7,163 | 47,595 | 0.2 |
| Fedha na bima | 66,626 | 50,009 | 116,635 | 0.5 |
| Upangishaji majengo | 6,685 | 2,627 | 9,312 | 0.04 |
| Shughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundi | 34,280 | 18,802 | 53,082 | 0.2 |
| Huduma zinazohusiana na utawala | 139,562 | 90,317 | 229,879 | 1 |
| Utawala na ulinzi | 119,788 | 42,777 | 162,565 | 0.7 |
| Elimu | 328,750 | 199,295 | 528,045 | 2.3 |
| Afya na Huduma za jamii | 53,255 | 171,588 | 224,843 | 1 |
| Sanaa na Burudani | 15,739 | 17,037 | 32,776 | 0.1 |
| Huduma nyingine | 125,516 | 162,860 | 288,376 | 1.3 |
| Shughuli za kaya katika kuajiri | 31,089 | 141,763 | 172,852 | 0.8 |
| **Jumla** | **11,986,131** | **11,043,823** | **23,029,954** | **100** |

**Chanzo**: Ofisi ya Taifa ya takwimu

156. Mwaka 2020, kiwango cha ukosefu wa ajira nchini kilikuwa asilimia 9.5 sawa na watu 2,406,950 ya idadi ya watu waliokuwa katika soko la ajira. Aidha, Serikali kupitia Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi iliwawezesha vijana 18,956 kupata mafunzo ya ujuzi unaohitajika katika soko la ajira ili waweze kujiajiri na kuajirika ikilinganishwa na vijana 23,755 mwaka 2019. Kati ya hao, vijana 5,538 walipata mafunzo ya uanagenzi; wahitimu 3,240 walipata mafunzo kwa vitendo mahala pa kazi; na vijana 10,178 walipata mafunzo ya ufundi stadi na kurasimishiwa ujuzi waliopa nje ya mfumo rasmi.

**Jedwali Na. 6.5: Mwenendo wa Kiwango cha Ukosefu wa Ajira**

| | **2016** | **2017** | **2018** | **2019** | **2020** |
|---|---|---|---|---|---|
| Watu walio katika soko la ajira (15+) | 23,311,917 | 23,826,427 | 24,354,215 | 24,889,028 | 25,436,904 |
| Walioajiriwa (15+) | 20,984,596 | 21,478,747 | 21,984,534 | 22,501,559 | 23,029,954 |
| Wasioajiriwa (15+) | 2,327,321 | 2,347,680 | 2,369,681 | 2,387,469 | 2,406,950 |
| **Kiwango cha ukosefu wa ajira (asilimia)** | **10.0** | **9.9** | **9.7** | **9.6** | **9.5** |

**Chanzo**: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

### Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania

157. Mwaka 2020, Serikali kupitia Wakala wa Huduma za Ajira - TaESA ilisajili watafutakazi 12,230 (wanaume 6,524 na wanawake 5,706) na kuwapatia ushauri nasihi kuhusu uchaguzi wa kazi ikilinganishwa na watafutakazi 14,884 mwaka 2019. Katika kipindi hicho, watafutakazi 2,861 (wanaume 1,456 na wanawake 1,405) walipata mafunzo ya kuwajengea uwezo wa kutafuta kazi, kushindania fursa za ajira ndani na nje ya nchi pamoja na mafunzo ya kujenga maadili ya kazi yanayohitajika na waajiri mbalimbali ikilinganishwa na watafutakazi 7,979 mwaka 2019.

158. Mwaka 2020, Wakala iliwaunganisha vijana wahitimu 1,230 (wanaume 665 na wanawake 565) wa ngazi mbalimbali za elimu na mafunzo kwenye fursa za mafunzo ya uzoefu wa kazi ili kuwajengea ujuzi wa kazi, kukuza maadili ya kazi, kuwajengea mtazamo chanya kuhusu kazi pamoja na kukuza ubunifu na tija mahali pa kazi. Aidha, vijana 923 (wanaume 504 na wanawake 419) waliunganishwa na fursa za kazi kwa waajiri mbalimbali nchini ikilinganishwa na vijana 2,268 mwaka 2019.

Jedwali Na. 31

**IDADI YA WATU NCHINI TANZANIA KIMKOA: 2012-2020**

| **Mkoa** | **2012**** | **2013** | **2014** | **2015** | **2016** | **2017** | **2018** | **2019** | **2020** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Dodoma | 2,083,588 | 2,127,416 | 2,172,165 | 2,217,856 | 2,264,508 | 2,419,941 | 2,492,989 | 2,568,514 | 2,647,410 |
| Arusha | 1,694,310 | 1,741,396 | 1,789,791 | 1,839,531 | 1,890,653 | 1,948,219 | 1,999,907 | 2,051,852 | 2,104,074 |
| Kilimanjaro | 1,640,087 | 1,669,051 | 1,698,526 | 1,728,522 | 1,759,048 | 1,823,151 | 1,864,329 | 1,906,978 | 1,951,252 |
| Tanga | 2,045,205 | 2,091,341 | 2,138,517 | 2,186,757 | 2,236,086 | 2,284,712 | 2,337,053 | 2,391,791 | 2,449,235 |
| Morogoro | 2,218,492 | 2,271,310 | 2,325,386 | 2,380,750 | 2,437,431 | 2,531,268 | 2,596,287 | 2,662,468 | 2,730,058 |
| Pwani | 1,098,668 | 1,122,685 | 1,147,227 | 1,172,306 | 1,197,933 | 1,236,481 | 1,265,504 | 1,295,267 | 1,325,852 |
| Dar es Salaam | 4,364,541 | 4,617,000 | 4,884,061 | 5,166,570 | 5,465,420 | 5,017,294 | 5,147,070 | 5,275,315 | 5,401,814 |
| Lindi | 864,652 | 872,758 | 880,939 | 889,197 | 897,533 | 963,465 | 983,738 | 1,004,439 | 1,025,800 |
| Mtwara | 1,270,854 | 1,286,501 | 1,302,340 | 1,318,374 | 1,334,606 | 1,397,723 | 1,424,083 | 1,451,078 | 1,478,874 |
| Ruvuma | 1,376,891 | 1,406,411 | 1,436,563 | 1,467,362 | 1,498,821 | 1,543,869 | 1,579,811 | 1,616,991 | 1,655,443 |
| Iringa | 941,238 | 951,964 | 962,813 | 973,784 | 984,882 | 1,068,695 | 1,095,172 | 1,122,131 | 1,149,481 |
| Mbeya | 2,707,410 | 2,781,971 | 2,858,585 | 2,937,310 | 1,883,024 | 2,006,072 | 2,070,412 | 2,136,614 | 2,204,543 |
| Singida | 1,370,637 | 1,402,820 | 1,435,758 | 1,469,469 | 1,503,972 | 1,569,304 | 1,612,854 | 1,658,086 | 1,705,182 |
| Tabora | 2,291,623 | 2,359,642 | 2,429,679 | 2,501,796 | 2,576,053 | 2,769,093 | 2,870,522 | 2,974,427 | 3,081,263 |
| Rukwa | 1,004,539 | 1,037,259 | 1,071,044 | 1,105,931 | 1,141,953 | 1,160,568 | 1,195,550 | 1,231,959 | 1,270,049 |
| Kigoma | 2,127,930 | 2,179,598 | 2,232,520 | 2,286,727 | 2,342,250 | 2,528,708 | 2,616,200 | 2,706,831 | 2,800,919 |
| Shinyanga | 1,534,808 | 1,566,734 | 1,599,325 | 1,632,593 | 1,666,554 | 1,816,316 | 1,874,709 | 1,933,768 | 1,993,589 |
| Kagera | 2,458,023 | 2,537,021 | 2,618,558 | 2,702,715 | 2,789,577 | 2,919,942 | 3,022,037 | 3,127,908 | 3,238,347 |
| Mwanza | 2,772,509 | 2,856,258 | 2,942,537 | 3,031,422 | 3,122,992 | 3,393,620 | 3,532,378 | 3,676,300 | 3,826,573 |
| Mara | 1,743,830 | 1,787,279 | 1,831,810 | 1,877,451 | 1,924,230 | 2,123,683 | 2,209,143 | 2,298,317 | 2,391,845 |
| Manyara | 1,425,131 | 1,471,083 | 1,518,516 | 1,567,479 | 1,618,020 | 1,692,667 | 1,750,864 | 1,810,929 | 1,873,105 |
| Njombe | 702,097 | 707,698 | 713,345 | 719,036 | 724,772 | 786,347 | 803,299 | 820,355 | 837,557 |
| Katavi | 564,604 | 583,160 | 602,325 | 622,121 | 642,567 | 706,472 | 738,237 | 771,287 | 805,887 |
| Simiyu | 1,584,157 | 1,613,580 | 1,643,549 | 1,674,075 | 1,705,168 | 1,998,224 | 2,094,798 | 2,196,449 | 2,304,228 |
| Geita | 1,739,530 | 1,785,824 | 1,833,350 | 1,882,141 | 1,932,230 | 2,148,409 | 2,239,949 | 2,335,134 | 2,434,800 |
| Songwe | | | | | 1,136,415 | 1,166,094 | 1,202,419 | 1,239,970 | 1,278,850 |
| **Tanzania Mainland** | **43,625,354** | **44,827,757** | **46,069,230** | **47,351,275** | **48,676,698** | **51,020,337** | **52,619,314** | **54,265,158** | **55,966,030** |
| Kaskazini Unguja | 187,455 | 193,551 | 199,844 | 206,343 | 213,053 | 216,697 | 222,066 | 227,317 | 232480 |
| Kusini Unguja | 115,588 | 117,923 | 120,305 | 122,736 | 125,215 | 131,162 | 133,767 | 136,235 | 138589 |
| Mjini Magharibi | 593,678 | 619,144 | 645,701 | 673,398 | 702,283 | 683,833 | 700,791 | 717,468 | 733914 |
| Kaskazini Pemba | 211,732 | 214,502 | 217,309 | 220,153 | 223,033 | 260,884 | 271,594 | 282,716 | 294267 |
| Kusini Pemba | 195,116 | 197,274 | 199,456 | 201,662 | 203,893 | 241,715 | 251,631 | 261,853 | 272348 |
| **Zanzibar** | **1,303,569** | **1,342,394** | **1,382,616** | **1,424,292** | **1,467,477** | **1,534,291** | **1,579,849** | **1,625,589** | **1,671,598** |
| **Tanzania** | **44,928,923** | **46,170,151** | **47,451,847** | **48,775,567** | **50,144,175** | **52,554,628** | **54,199,163** | **55,890,747** | **57,637,628** |

**Chanzo**: Ofisi ya Taifa ya Takwimu
**Takwimu za matokeo ya sensa mwaka 2012
- Not Available

# SEHEMU YA PILI

## UENDELEZAJI SEKTA BINAFSI

## SURA YA 7

## UENDELEZAJI WA SEKTA BINAFSI

### Usajili wa Miradi ya Uwekezaji

159. Mwaka 2020, Serikali kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania ilisajili miradi 203 ikilinganishwa na miradi 269 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 24.5. Hii ilitokana na athari za UVIKO-19 kwa nchi nyingi duniani na kutokuwepo kwa miradi ya mwendelezo katika kipindi hicho. Kati ya miradi iliyosajiliwa, miradi 64 ilikuwa ya watanzania, miradi 74 ya wageni, miradi 65 ya ubia kati ya watanzania na wageni ikilinganishwa na miradi 86 ya watanzania, 107 ya wageni na miradi 76 ya ubia mwaka 2019. Kwa upande mwingine, thamani ya miradi iliyosajiliwa ilipungua kwa asilimia 59.1 kutoka dola za Marekani bilioni 2.6 mwaka 2019 hadi dola za Marekani bilioni 1.1 mwaka 2020. Aidha, fursa za ajira zilizotokana na miradi hiyo iliyosajiliwa zilipungua kwa asilimia 63.4 mwaka 2020 kufikia 17,084 ikilinganishwa na fursa za ajira 46,703 mwaka 2019. Hii ilitokana na kupungua kwa miradi iliyosajiliwa.

### Mgawanyiko wa Usajili wa Miradi Kisekta

160. Mwaka 2020, sekta ya uzalishaji viwandani ilivutia uwekezaji wenye thamani ya dola za Marekani milioni 635.9; ikifuatiwa na nishati dola za Marekani milioni 158.7; usafirishaji wa mizigo dola za Marekani milioni 94.5; utalii dola za Marekani milioni 46.8; na kilimo dola za Marekani milioni 46.3. Katika kipindi hicho, sekta ya uzalishaji viwandani ilisajili miradi 130 ikifuatiwa na usafirishaji mizigo miradi 17; utalii miradi 12; kilimo miradi 12; majengo ya biashara na huduma miradi 10 kila mmoja; na rasilimalimali watu miradi 5 ikilinganishwa na miradi 156 sekta ya uzalishaji viwandani, usafirishaji mizigo miradi 34, huduma miradi 19, kilimo miradi 18, utalii miradi 16 na majengo ya biashara miradi 11 mwaka 2019.

**Jedwali Na. 7.1: Miradi ya Uwekezaji Iliyosajiliwa Mwaka 2020**

| Sekta | Miradi yote | Miradi mipya | Miradi ya mwendelezo | Miradi ya Wazawa | Miradi ya Wageni | Miradi ya Ubia | Ajira | Thamani dola za marekani milioni |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kilimo | 12 | 12 | 0 | 4 | 5 | 3 | 802 | 46.30 |
| Maliasili | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 2 | 185 | 5.55 |
| Utalii | 12 | 12 | 0 | 3 | 5 | 4 | 834 | 46.79 |
| Uzalishaji Viwandani | 130 | 130 | 0 | 41 | 47 | 42 | 11,303 | 635.85 |
| Madini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Majengo ya Biashara | 10 | 10 | 0 | 2 | 6 | 2 | 789 | 44.97 |
| Usafirishaji | 17 | 17 | 0 | 6 | 5 | 6 | 2,004 | 94.47 |
| Huduma | 10 | 10 | 0 | 4 | 4 | 2 | 656 | 35.54 |
| Kompyuta | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Taasisi za Kifedha | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Raslimali Watu | 5 | 5 | 0 | 3 | 1 | 1 | 206 | 3.90 |
| Mawasiliano | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Nishati | 4 | 4 | 0 | 0 | 1 | 3 | 285 | 158.72 |
| Miundombinu | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Utangazaji | 1 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 20 | 0.9 |
| **Jumla** | **203** | **203** | **0** | **64** | **74** | **65** | **17,084** | **1,072.99** |

**Chanzo:** Kituo cha Uwekezaji Tanzania

## Mgawanyiko wa Miradi Kimkoa

161. Mwaka 2020, Mkoa wa Dar es Salaam uliendelea kuongoza kwa kuvutia uwekezaji ambapo miradi 97 ilisajiliwa. Hii ilitokana na kuwepo kwa mazingira wezeshi ya uwekezaji hususan miundombinu ikilinganishwa na mikoa mingine. Aidha, mkoa wa Pwani ulifuatia kwa kusajili miradi 35, Mwanza miradi 17, Arusha miradi 8 na Iringa na Shinyanga miradi 7 kila mmoja.

**Jedwali Na. 7.2: Mgawanyiko wa Miradi iliyosajiliwa Kimkoa Mwaka 2020**

| Mkoa | Kilimo | Utangazaji | Majengo ya Biashara | Kompyuta | Miundombinu | Nishati | Taasisi za Kifedha | Raslimali watu | Uzalishaji Viwandani | Maliasili | Huduma | Mawasiliano | Utalii | Usafirishaji | Idadi ya Mradi Kimkoa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Arusha** | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 5 | 1 | **8** |
| **Dar-es-salaam** | 3 | 0 | 7 | 0 | 0 | 1 | 0 | 2 | 64 | 1 | 6 | 0 | 2 | 11 | **97** |
| **Dodoma** | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | **3** |
| **Geita** | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **1** |
| **Iringa** | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | **7** |
| **Kagera** | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **2** |
| **Katavi** | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **1** |
| **Kigoma** | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | **4** |
| **Kilimanjaro** | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **1** |
| **Lindi** | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| **Manyara** | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **1** |
| **Mara** | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 3 | 0 | **4** |
| **Mbeya** | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **1** |
| **Morogoro** | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | **3** |
| **Mtwara** | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **3** |
| **Mwanza** | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 11 | 1 | 2 | 0 | 0 | 1 | **17** |
| **Njombe** | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **2** |
| **Pwani** | 3 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 27 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | **35** |
| **Rukwa** | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **1** |
| **Ruvuma** | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | **3** |
| **Shinyanga** | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | **7** |
| **Simiyu** | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Singida** | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Songwe** | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Tabora** | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Tanga** | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **2** |
| **Jumla ya miradi** | **12** | **1** | **10** | **0** | **0** | **4** | **0** | **5** | **130** | **2** | **10** | **0** | **12** | **17** | **203** |

**Chanzo:** Kituo cha Uwekezaji Tanzania

## RIPOTI YA UWEKEZAJI TANZANIA YA MWAKA 2020

162. Serikali hufanya utafiti wa hali ya uwekezaji nchini kila mwaka kwa lengo la kubaini aina za uwekezaji kutoka nje na mchango wa uwekezaji huo katika uchumi wa Taifa. Mwaka 2019, utafiti huo ulifanyika ambapo Ripoti ya Uwekezaji Tanzania inayojumuisha taarifa za uwekezaji wa moja kwa moja na hisa kutoka nje, uwekezaji mwingine na ajira kutokana na uwekezaji kutoka nje ilitolewa mwaka 2020 na ifuatayo ni sehemu ya matokeo ya utafiti huo.

### Jumla ya Uwekezaji wa Sekta Binafsi Kutoka Nje

163. Hadi Desemba 2019, uwekezaji wa sekta binafsi kutoka nje kwa ujumla ulifikia dola za Marekani milioni 20,369.7 kutoka dola za Marekani milioni 19,356.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 5.2. Hii ilichangiwa na uwepo wa sera nzuri za uchumi, amani, utulivu, pamoja na kuimarika kwa mazingira ya uwekezaji. Kati ya uwekezaji huo, uwekezaji wa moja kwa moja ulifikia dola za Marekani milioni 15,099.9, sawa na asilimia 74.1 ya uwekezaji wa sekta binafsi kutoka nje, uwekezaji wa hisa asilimia 0.2 na uwekezaji mwingine asilimia 25.7.

### Uwekezaji wa Sekta Binafsi kwa Miaka husika

164. Thamani ya mitaji iliyowekezwa kwenye sekta binafsi kutoka nje ya nchi mwaka 2019 ilikuwa dola za Marekani milioni 1,240.0 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,214.4 mwaka 2018. Kati ya hizo, Tanzania ilipokea uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje wenye thamani ya dola za Marekani milioni 1,217.2 mwaka 2019 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 971.6 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 25.3. Ongezeko la thamani ya mtaji iliyowekezwa lilichangiwa na kuendelea kuboreshwa kwa mazingira ya uwekezaji hususan utekelezaji wa miradi ya kimkakati ya miundombinu ikiwemo barabara, reli na umeme. Aidha, katika kipindi hicho, Tanzania ilipokea dola za Marekani milioni 5.5 kwenye uwekezaji wa hisa ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1.6 mwaka 2018. Vile vile, Tanzania ilipokea dola za Marekani milioni 17.3 kupitia uwekezaji mwingine mwaka 2019 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 241.3 mwaka 2018. Uwekezaji mwingine unajumuisha mikopo ya muda mrefu na mfupi, mikopo ya mali na huduma kutoka kwenye taasisi na mashirika yasiyokuwa na uhusiano wa kihisa na makampuni au taasisi zilizowekeza nchini. Kushuka kwa uwekezaji mwingine kulichangiwa na kupungua kwa mikopo ya muda mrefu kutoka dola za Marekani milioni 243.8 mwaka 2018 hadi dola za Marekani milioni 1.3 Mwaka 2019.

**Jedwali Na.7.3: Uwekezaji kwenye Sekta Binafsi kutoka Nje ya Nchi (Dola za Marekani Milioni) Mwaka 2015-2019**

| Aina ya uwekezaji | Kiasi kilichowekezwa | | | | | Limbikizo lililowekezwa | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 |
| Uwekezaji wa moja kwa moja | 1,560.60 | 755 | 937.7 | 971.6 | 1,217.20 | 12,572.60 | 12,839.20 | 13,274.40 | 14,092.00 | 15,099.90 |
| Uwekezaji wa hisa | 1.5 | 2.8 | 0.8 | 1.6 | 5.5 | 31.4 | 128 | 176.6 | 30.6 | 39.6 |
| Uwekezaji mwingine | 2.7 | 237.7 | 113.2 | 241.3 | 17.3 | 1,100.70 | 1,667.10 | 2,058.70 | 5,233.70 | 5,230.20 |
| **Jumla** | **1,564.80** | **995.5** | **1,051.70** | **1,214.40** | **1,240.00** | **13,704.60** | **14,634.30** | **15,392.70** | **19,356.30** | **20,369.70** |

**Chanzo:** Benki Kuu ya Tanzania

## Ajira kutokana na Uwekezaji kutoka Nje

165. Uwekezaji wa moja kwa moja ulitoa ajira kwa watu 140,415 mwaka 2019 ikilinganishwa na watu 140,256 mwaka 2018. Kati ya hao, wafanyakazi wataalamu walikuwa 43,931 sawa na asilimia 31 ya waajiriwa wote na wasiokuwa wataalamu walikuwa 96,484. Aidha, wafanyakazi wataalamu waliendelea kuajiriwa zaidi kwenye sekta za mawasiliano, fedha na bima.

## Urahisi wa kuwekeza na Kufanya Biashara Nchini

166. Mwaka 2020, Serikali iliendelea kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Kufanya Biashara na Uwekezaji nchini - *BluePrint* kwa lengo la kuboresha mazingira ya biashara nchini. Katika kipindi hicho, utekelezaji wa *Blueprint* ulikuwa na mafanikio mbalimbali yakiwemo: kufutwa au kupunguzwa kwa jumla ya tozo na ada 60; kutungwa kwa Sheria ya Usuluhishi wa Migogoro (Arbitration Act 2020); kufutwa kwa kipengele cha 16(2) cha Sheria ya makampuni ili kupunguza urasimu na gharama za kupata tamko la kutimiza matakwa ya sheria hiyo wakati wa kufungua kampuni au kuhuisha usajili; kuuganishwa na kuwezesha kuwasiliana kwa baadhi ya mifumo ya kieletroniki ikiwemo mfumo ya Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) uliounganishwa na mfumo wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), mfumo wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) wa utoaji wa namba za Utambulisho wa Mlipa Kodi (TIN); na kuimarisha mfumo wa Huduma za Mahala Pamoja (One Stop Centre) katika Kituo cha Uwekezaji (TIC) na Mamlaka ya Mauzo Nje (EPZA).

## Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

167. Mwaka 2020, Serikali kupitia Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi iliendelea kuwawezesha wananchi kiuchumi kupitia utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Hadi Desemba 2020, mifuko ya uwezeshaji wananchi kiuchumi inayotoa mikopo moja kwa moja kwa kushirikiana na mifuko inayotoa dhamana ilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 898.1 kwa wajasiriamali wadogo 3,614,857 ikilinganisha na mikopo yenye thamani ya shilingi trilioni 1.24 kwa wajasiliamali 1,150,741 mwaka 2019. Katika kipindi hicho, shilingi bilioni 381.2 zilitolewa kwa wanawake 1,882,376, sawa na asilimia 52.0 ya wanufaika

wote na shilingi bilioni 490.3 zilitolewa kwa wanaume 1,603,503, sawa na asilimia 44.0. Vile vile, shilingi bilioni 26.6 zilitolewa kwa watu wenye ulemavu 128,978, sawa na asilimia 4.0 ya wanufaika wote. Ongezeko la wanufaika wa mikopo lilichangiwa na kuwepo kwa idadi kubwa ya wajasiriamali wanaojishughulisha na shughuli za uchumi katika sekta mbalimbali ikiwemo viwanda, afya, elimu, biashara, madini, uvuvi, ufugaji na kilimo.

168. Mwaka 2020, ajira 60,329 za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja zilizalishwa katika miradi ya kimkakati na uwekezaji ikilinganishwa na ajira 18,363 mwaka 2019. Ongezeko hilo lilichangiwa na idadi kubwa ya miradi iliyofanyiwa tathmini. Aidha, wazawa waliopata ajira katika miradi hiyo ni 56,921 na wageni 3,408 mwaka 2020 ikilinganishwa na wazawa 16,908 na wageni 1,455 mwaka 2019. Katika kipindi hicho, makandarasi wa miradi ya kimkakati waliingia mikataba na kampuni 1,015 za watanzania kwa ajili ya huduma za chakula, ulinzi, usafiri, bima, mafuta na bidhaa za ujenzi kama vile saruji, nondo, kokoto na mchanga ikilinganishwa na kampuni 71 mwaka 2019. Kuongezeka kwa kampuni za watanzania zilizoingia mikataba kulitokana na utekelezaji wa Mpango wa Ushiriki wa Watanzania katika Uwekezaji na Miradi ya Kimkakati.

169. Mwaka 2020, Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi lilitoa mafunzo ya ujasiriamali kwa wajasiriamali 191,418 kwa lengo la kuwaunganisha na fursa za kiuchumi ikilinganishwa na wajasiriamali 7,924 mwaka 2019. Katika kipindi hicho, Baraza lilianza kutoa mafunzo ya ubunifu na ujasiriamali kwa wanafunzi 623,482 wa vyuo vikuu na vyuo vya elimu ya juu wanaoendelea na waliohitimu. Mafunzo hayo yalilenga: kuongeza ujuzi wa wajasiriamali katika kuanzisha na kuendeleza shughuli za kiuchumi; kuwaunganisha na fursa za mitaji kutoka mifuko ya uwezeshaji, benki na taasisi za fedha; umuhimu wa kurasimisha biashara na kuunda vikundi; na utafutaji wa masoko ya ndani na ya kimataifa.

170. Mwaka 2020, Serikali ilianza kutekeleza Mpango wa Uendelezaji wa Viwanda Vidogo na vya Kati unaolenga kutatua changamoto ya upatikanaji wa ujuzi, masoko na mitaji katika miradi midogo na ya kati ya viwanda kwa wajasiriamali ulizinduliwa Julai 2020. Mpango huo unasimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu na unatekelezwa na taasisi tano ambazo ni Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo-SIDO, Benki ya Azania, Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii - NSSF, Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi - VETA na Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi -NEEC. Katika kipindi hicho, mikopo yenye thamani ya shillingi milioni 934.5 ilitolewa kwa kampuni 13 kutoka katika mikoa ya Mwanza, Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Mbeya, Kilimanjaro na Geita kwa ajili ya kuwezesha upatikanaji wa mitaji ya kuanzisha na kuendeleza shughuli za uzalishaji na biashara.

171. Mwaka 2020, Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi lilianzisha Vituo 10 vya uwezeshaji katika mikoa ya Geita, Singida, Kigoma na Dodoma ikilinganishwa na Vituo 6 mwaka 2019. Vituo hivyo vinatoa huduma mbalimbali zikiwemo elimu ya uandishi wa mpango wa biashara, elimu ya masuala ya kodi na upatikanaji wa masoko kwa lengo la kuwawezesha wananchi kutumia fursa za kiuchumi katika maeneo yao au maeneo mengine.

**Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi**

172. Mwaka 2020, Serikali iliendelea kupokea na kuchambua miradi inayotarajiwa kutekelezwa kwa utaratibu wa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi. Katika kipindi hicho, miradi iliyopokelewa na kuchambuliwa ilikuwa: Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Tozo yenye urefu wa kilometa 158 kutoka Kibaha-Chalinze-Morogoro; Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Tozo yenye urefu wa kilometa 258 kutoka Morogoro–Dodoma; Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Mchepuko yenye urefu wa kilometa 48.9 kutoka Uyole-Songwe; Mradi wa Kujenga na Kuendesha Kiwanda cha Kutengeneza Simu za Kiganjani; na Mradi wa Kuimarisha Huduma za Saratani. Aidha, miradi hii imekidhi vigezo vya kutekelezwa kwa utaratibu wa Ubia Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi.

173. Mwaka 2020, maandiko ya miradi yaliyopo katika hatua mbalimbali za uchambuzi ni pamoja na: mradi wa Ujenzi wa Hosteli za wanafunzi katika Chuo cha Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA); miradi ya Ujenzi wa Hoteli ya Nyota Tano, Ujenzi wa Jengo la Abiria na Ujenzi wa Kituo cha Biashara katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa Kilimanjaro ambayo ipo katika hatua ya Andiko Dhana; Miradi ya Ujenzi wa Hosteli za wanafunzi katika Chuo cha Elimu ya Biashara (Kampasi za Dar es Salaam na Dodoma) na Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini ipo katika hatua ya Upembuzi Yakinifu wa Awali ; Ujenzi wa Hoteli ya Nyota Nne na Ujenzi wa Kituo cha biashara katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere; na Mradi wa Kuzalisha Dawa Muhimu na Vifaa Tiba wa Bohari Kuu ya Dawa ipo katika hatua ya ununuzi wa Mbia

Jedwali Na.32 **KITUO CHA UWEKEZAJI TANZANIA (TIC): MIRADI YA UWEKEZAJI ILIYOSAJILIWA**

| Sekta | 2019 | | | | | | | | 2020 | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | A | B | C | D | E | F | G | H | A | B | C | D | E | F | G | H |
| Kilimo | 18 | 18 | - | 6 | 6 | 6 | 19,428 | 463 | 12 | - | - | 4 | 5 | 3 | 802 | 46.3 |
| Maliasili | 2 | 2 | - | - | - | 2 | 195 | 2 | 2 | - | - | 0 | 0 | 2 | 185 | 5.55 |
| Uzalishaji Viwandani | 156 | 156 | - | 41 | 70 | 45 | 17,713 | 1,159 | 130 | - | - | 41 | 47 | 42 | 11303 | 635.852 |
| Majengo ya biashara | 11 | 11 | - | 2 | 6 | 3 | 1,101 | 159 | 10 | - | - | 2 | 6 | 2 | 789 | 44.97 |
| Usafirishaji Mizigo | 34 | 34 | - | 22 | 7 | 5 | 3,876 | 375 | 17 | - | - | 6 | 5 | 6 | 2004 | 94.47 |
| Huduma za Biashara | 19 | 19 | - | 1 | 9 | 9 | 1,828 | 38 | 10 | - | - | 4 | 4 | 2 | 656 | 35.54 |
| Nishati | 6 | 6 | - | 4 | 2 | - | 669 | 28 | 4 | - | - | 0 | 1 | 3 | 285 | 158.72 |
| Rasilimali watu | 2 | 2 | - | 2 | - | - | 308 | 64 | 5 | - | - | 3 | 1 | 1 | 206 | 3.9 |
| Utalii | 16 | 16 | - | 7 | 7 | 2 | 1,260 | 60 | 12 | - | - | 3 | 5 | 4 | 834 | 46.79 |
| Utangazaji | 1 | 1 | - | 1 | - | - | 212 | 12 | 1 | - | - | 1 | 0 | 0 | 20 | 0.9 |
| **Jumla** | **269** | **269** | **-** | **86** | **107** | **76** | **46,703** | **2,623** | **203** | **-** | **-** | **64** | **74** | **65** | **17,084.0** | **1,072.99** |

**Chanzo:** Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC)
A Jumla ya Miradi Iliyosajiliwa
B Miradi Mipya
C Miradi ya Maendeleo
D Miradi ya Wazawa
E Miradi ya Wageni
F Miradi ya Ubia
G Jumla ya Ajira
H Jumla ya Thamani ya Uwekezaji (USD. Milioni)
\- Takwimu Hazikupatikana

## SURA YA 8

## MASUALA MTAMBUKA

### Ukimwi

### Mapambano Dhidi ya Virusi Vya UKIMWI na UKIMWI

174. Mwaka 2020, Serikali iliendelea kutekeleza Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI kwa kutekeleza mikakati mbalimbali ya kupambana na UKIMWI ili kuweza kufikia malengo yaliyoainishwa katika Mkakati wa Nne wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI 2018/19-2022/23. Aidha, moja ya lengo la mkakati huo ni kufikia malengo ya Tiba ya Tisini Tatu (90-90-90) ifikapo Desemba 2020. Dhana hii inamaanisha: asilimia 90 ya watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI (WAVIU) wawe wamepimwa na kujua hali yao ya uambukizo ya VVU; asilimia 90 kati ya waliotambua hali zao za maambukizi wawe wanatumia tiba endelevu ya ARV; na asilimia 90 ya walio kwenye tiba wawe wamefubaza VVU kwenye damu.

175. Mwaka 2020, Tanzania ilikadiriwa kuwa na watu milioni 1.7 wanaoishi na virusi vya UKIMWI ikilinganishwa na watu milioni 1.6 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 6.3. Kati ya watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI, watu milioni 1.4, sawa na asilimia 82.4 walikuwa wanatambua hali zao ikilinganishwa na watu milioni 1.3 waliokuwa wanatambua hali zao mwaka 2019. Katika kipindi hicho, watu milioni 1.36 wanaotambua hali zao, sawa na asilimia 98 walikuwa katika tiba endelevu ya ARV na asilimia 92 ya wanaotumia tiba endelevu walikuwa wamefubaza virusi vya UKIMWI. Aidha, asilimia 91 ya walioanzishiwa dawa za ARV kinga zao za mwili ziliimarika na wamefanikiwa kupunguza wingi wa VVU mwilini na hivyo kupunguza uwezekano wa kuwaambukiza wenzi wao.

176. Mwaka 2020, Serikali iliendelea kuimarisha huduma za upimaji VVU kwa kufanya marekebisho ya Sheria ya UKIMWI ya mwaka 2008 kwa kuruhusu upimaji binafsi wa VVU na kushusha umri wa kuhitaji ridhaa ya mzazi au mlezi kwa ajili ya kupima VVU kutoka miaka 18 hadi miaka 15. Hadi Desemba 2020, vituo vilivyokuwa vinatoa huduma na tiba ya kufubaza VVU viliongezeka na kufikia 6,829 kutoka vituo 6,529 mwaka 2019. Vile vile, Serikali iliongeza mashine za kupima wingi wa VVU kutoka mashine 40 mwaka 2019 hadi mashine 77 mwaka 2020.

### Mazingira

177. Mwaka 2020, Serikali iliendelea kuhakikisha kuwa utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo unazingatia Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 ambapo miradi 780 ilipata hati za Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) baada ya kukidhi vigezo ikilinganishwa na miradi 720 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 8.3. Ongezeko hilo lilitokana na uhamasishaji uliofanyika kuhusu umuhimu

wa kufanya tathmini ya athari kwa mazingira kabla ya kuanza utekelezaji wa miradi na maelekezo yaliyotolewa kwa taasisi za fedha kutotoa mikopo kwa miradi isiyokuwa na vyeti vya TAM. Aidha, Serikali iliendelea kuhakikisha kuwa utekelezaji wa sera, mikakati, miswada na programu unazingatia hifadhi ya mazingira kwa kutoa hati za Tathmini ya Athari Kwa Mazingira Kimkakati (TMK) ambapo hati moja (1) ya TMK ilitolewa mwaka 2020 ikilinganishwa na hati tatu (3) zilizotolewa mwaka 2019.

178. Mwaka 2020, vibali 215 vilitolewa kwa wafanyabiashara wanaojihusisha na shughuli za ukusanyaji, uhifadhi, usafirishaji, uingizaji na usafirishaji nje ya nchi wa taka hatarishi ambazo hurejelezwa na kutumika kama malighafi katika shughuli za uzalishaji viwandani ikilinganishwa na vibali 20 vilivyotolewa mwaka 2019. Kuongezeka kwa vibali hivyo kulitokana na kuendelea na utekelezaji wa Kanuni ya Udhibiti na Usimamizi Taka Hatarishi ya Mwaka 2009 yaliyolenga kuweka utaratibu wenye tija wa kusimamia taka hatarishi pamoja na kuhamasisha wazalishaji wakubwa wa taka hizo kama vile Makampuni ya simu, Migodi, Bandari na Shirika la Reli katika kusimamia na kufuata matakwa ya kisheria ya kuhakikisha yanatoa tenda za ukusanyaji wa taka hatarishi kwa makampuni yenye vibali. Aidha, wakusanyaji wadogo wanaokusanya taka hatarishi chini ya tani tatu (taka ngumu) na lita 600 (taka maji) walifuata matakwa ya Kanuni.

**Jedwali Na. 8.1: Vibali vya Taka Hatarishi Vilivyotolewa Mwaka 2020**

| Na. | Aina ya Taka Hatarishi | Idadi ya vibali |
|---|---|---|
| 1 | Vyuma chakavu | 127 |
| 2 | Mafuta machafu | 23 |
| 3 | Taka za kielektroniki | 20 |
| 4 | taka za plastiki | 1 |
| 5 | Betri chakavu | 26 |
| 6 | Mipira chakavu | 8 |
| 7 | Vibali vya kusafirisha taka nje ya nchi | 7 |
| 8 | Vibali vya kuingiza taka ngumu nje | 3 |
| | **Jumla** | **215** |

**Chanzo:** Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira

179. Mwaka 2020, Serikali ilifanikisha utekelezaji wa katazo la matumizi ya mifuko ya plastiki ambapo jumla ya tani 294.5 za mifuko mbadala ziliingizwa nchini ikilinganishwa na tani 1,082.3 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 72.8. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa mifuko mbadala katika viwanda vya ndani. Hadi Desemba 2020, kulikuwa na viwanda 17 vya ndani vinavyozalisha mifuko mbadala ya plastiki aina ya *non - woven* na mifuko ya karatasi ikilinganishwa na viwanda 14 mwaka 2019. Aidha, viwanda hivyo vilizalisha ajira 545 ikilinganishwa na ajira 345 mwaka 2019.

**Ulinzi na Usalama wa Raia**

180. Mwaka 2020, jumla ya makosa ya jinai yaliyoripotiwa yalikuwa 50,689 ikilinganishwa na makosa 58,590 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 13.5. Upungufu huo ulitokana na elimu iliyotolewa kwa umma juu ya madhara ya uhalifu na hivyo jamii kuhamasika kudhibiti uhalifu kupitia ulinzi shirikishi. Kati ya makosa yaliyoripotiwa: makosa dhidi ya binadamu yalikuwa 11,001 ikilinganishwa na makosa 12,223 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 10.0; makosa ya kuwania mali yalikuwa 24,056 ikilinganishwa na makosa 27,635 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 13.0; makosa 905 ya uhalifu wa fedha yaliripotiwa ikilinganishwa na makosa 1,218 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 27.7; na makosa dhidi ya uhalifu wa jamii yalikuwa 14,727 ikilinganishwa na makosa 17,514 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 15.9.

181. Mwaka 2020 kulikuwa na jumla ya matukio ya ajali 1,933 ambapo kati ya hayo, ajali 1,031 zilisababisha vifo vya watu 1,384 na majeruhi 2,362 ikilinganishwa na jumla ya matukio ya ajali 2,924 ambapo matukio ya ajali 1,208 yalisababisha vifo vya watu 1,536 na majeruhi 3,123 mwaka 2019.

182. Mwaka 2020, magereza nchini yalikuwa na jumla ya wafungwa na mahabusu 32,398 ambao ni asilimia 8.3 zaidi ya uwezo wa magereza wa kuhifadhi wafungwa na mahabusu 29,902. Kati ya hao, wafungwa walikuwa 16,712 (asilimia 51.6) na mahabusu walikuwa 15,686 (asilimia 48.4) ikilinganishwa na wafungwa 14,503 na mahabusu 17,845 mwaka 2019. Katika jitihada za kupunguza msongamano gerezani, Bodi ya Parole ilifanya kikao kimoja (1) kilichojadili wafungwa 79 ambapo wafungwa 73 waliachiwa huru na wafungwa 6 walikataliwa. Aidha, katika jitihada hizo za kupunguza msongamano wa wafungwa, Serikali ilitoa msamaha kwa wafungwa 3,973 wakati wa sherehe za miaka 56 ya Muungano tarehe 26 Aprili 2020 na wafungwa wengine 3,316 walisamehewa ama kupunguziwa adhabu zao wakati wa siku ya maadhimisho ya miaka 59 ya Uhuru wa Tanganyika tarehe 9 Desemba 2020.

183. Mwaka 2020, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji liliendelea kukabiliana na majanga ya moto na majanga mengine ambapo idadi ya miito 2,001 ya matukio ya moto ilipokelewa ikilinganishwa na idadi ya miito 2,023 mwaka 2019. Kupungua kwa matukio hayo kulitokana na jamii kuwa na uelewa wa kinga na tahadhari dhidi ya majanga ya moto. Katika kipindi hicho, miito ya maokozi ilikuwa 876 ikilinganishwa na miito ya maokozi 853 mwaka 2019. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uelewa wa wananchi katika matumizi ya namba ya dharura 114 pindi tukio linapotokea.

184. Mwaka 2020, Serikali kupitia Idara ya Uhamiaji ilitoa hati za kusafiria 123,113 ikilinganishwa na hati 198,498 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 38.0. Hii ilitokana na kupungua kwa uhitaji wa watanzania kusafiri nje ya nchi kulikosababishwa

na athari za UVIKO-19. Katika kipindi hicho, jumla ya wageni 614,838 waliingia nchini kwa vibali halali ikilinganishwa na wageni 1,457,597 walioingia nchini mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 60.6. Vile vile, wageni 563,230 walitoka nchini mwaka 2020 ikilinganishwa na wageni 1,174,411 waliotoka nchini mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 63.4. Hii ilitokana kupungua kwa shughuli za usafirishaji kulikosababishwa na athari za UVIKO-19.

185. Mwaka 2020, idadi ya waomba hifadhi na wakimbizi ilikuwa 275,430 ikilinganishwa na waomba hifadhi na wakimbizi 291,647 mwaka 2019. Kati ya hao, waomba hifadhi na wakimbizi 196,976 walitoka Burundi, 78,014 Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, 150 Somalia na 290 mataifa mengine. Aidha, wakimbizi waliohamishiwa nchi ya tatu walikuwa 1,365 (Marekani 1,286, Canada 16, Australia 60, na Finland 3) mwaka 2020 ikilinganishwa na wakimbizi 4,078 waliohamishiwa nchi ya tatu mwaka 2019. Katika kipindi hicho, wakimbizi 30,644 walirejeshwa kwenye nchi zao za asili kwa hiari yao ikilinganishwa na wakimbizi 20,936 waliorejeshwa mwaka 2019.

**Vitambulisho vya Taifa**

186. Mwaka 2020, Serikali kupitia Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa iliendelea na zoezi la usajili na utambuzi wa wananchi katika mikoa yote Tanzania. Hadi Desemba 2020, jumla ya wananchi 22,280,625 walitambuliwa na kusajiliwa ikilinganishwa na wananchi 21,511,321 waliotambuliwa na waliosajiliwa katika kipindi kama hicho mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 3.6. Aidha, Mamlaka ilisajili wageni wakaazi 32,062 na wakimbizi 212,608 mwaka 2020 ikilinganishwa na wageni wakaazi 19,311 na Wakimbizi 200,074 waliosajiliwa mwaka 2019. Wageni na wakimbizi waliosajiliwa walitoka katika kambi za Mtendeli, Nduta na Nyarugusu (Kigoma), makazi ya Katumba na Mishamo (Katavi), kambi ya Ulyankulu (Tabora), Mtambaswala (Mtwara) pamoja na wakimbizi wenye vibali vya kuishi katika Jiji la Dar es Salaam.

187. Hadi Desemba 2020, Mamlaka ilizalisha namba za utambulisho 18,543,158 ikilinganishwa na namba za utambulisho 16,211,654 zilizozalishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 14.4. Aidha, vitambulisho vilivyotolewa viliongezeka na kufikia 6,296,037 kutoka vitambulisho 5,787,869 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 8.8. Ongezeko hilo lilitokana na Mamlaka kununua na kuanza kutumia mashine za kuzalisha vitambulisho zenye uwezo mkubwa.

188. Mwaka 2020, Mamlaka iliunganisha vituo vya usajili 137 na huduma ya mtandao wa mawasiliano ili kurahisisha usafirishaji wa taarifa baina ya vituo hivyo na makao makuu ya Mamlaka ikilinganishwa na vituo 126 mwaka 2019. Katika kipindi hicho, Mamlaka iliziunganisha taasisi 69 katika mfumo wa usajili na utambuzi ikilinganishwa na taasisi 57 zilizounganishwa mwaka 2019.

**Usajili, Ufilisi na Udhamini**

189. Mwaka 2020, Serikali kupitia Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini ilisajili vizazi 1,434,279 ikilinganishwa na vizazi 2,164,982 vilivyosajiliwa mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 33.8. Katika kipindi hicho, vifo 28,531 vilisajiliwa ikilinganishwa na vifo 35,708 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 20. Aidha, Wakala ulisajili ndoa 48,193, talaka 210 na hati za watoto wa kuasili 33 mwaka 2020 ikilinganishwa na ndoa 44,562, talaka 295 na hati za watoto wa kuasili 34 mwaka 2019. Vile vile, kupitia mpango wa usajili kwa watoto walio na umri wa chini ya miaka mitano, jumla ya watoto 668,842 walisajiliwa katika mikoa ya Morogoro, Pwani, Dodoma na Singida. mwaka 2020 ikilinganishwa na watoto 1,141,029 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 41.4. Upungufu huo ulitokana na uwepo wa idadi ndogo ya watoto waliotakiwa kusajiliwa katika mikoa hiyo.

190. Mwaka 2020, mfumo wa usajili wa vizazi na vifo na uhakiki wa nyaraka kwa kutumia mtandao (E-Huduma) ulianza kutumika. Hadi Desemba, 2020 maombi 117,923 yalipokelewa na vyeti vya vizazi na vifo 112,487 vya wanafunzi wanaoomba mikopo katika Bodi ya Elimu ya Juu vilihakikiwa kupitia mfumo wa usajili.

191. Mwaka 2020, Wakala ulitoa hati 79 za miunganisho ya wadhamini ikilinganishwa na hati 98 mwaka 2019. Aidha, wosia 113 ziliandikwa na kuhifadhiwa mwaka 2020 ikilinganishwa na wosia 65 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 73.8. Hii ilitokana na kuendelea kutolewa kwa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kuandika na kutunza wosia ili kuepusha migogoro ya wanafamilia mwenye mali anapofariki.

**Utawala Bora**

192. Mwaka 2020, Serikali kupitia Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ilikamilisha uchunguzi wa majalada 412 ambapo majalada 72 yalipata kibali cha watuhumiwa kufikishwa mahakamani ikilinganishwa na uchunguzi wa majalada 916 ambapo majalada 51 yalipata kibali cha watuhumiwa kufikishwa mahakamani mwaka 2019. Aidha, kesi mpya 214 zilifunguliwa mahakamani na kufanya jumla ya kesi zilizoendeshwa kufikia 909 mwaka 2020. Vile vile, kesi 259 ziliamuliwa mahakamani ambapo kesi 91 watuhumiwa waliachiwa huru na kesi 168 watuhumiwa walipatikana na hatia na kuhukumiwa vifungo au kulipa faini.

193. Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 ulifanyika kwa ufanisi, kidemokrasia, amani na utulivu na kwa kutumia fedha za ndani ambapo jumla ya shilingi bilioni 268.6 zilitumika. Katika uchaguzi huo, Rais, wabunge na madiwani waliweza kupatikana kwa njia ya kidemokrasia ambapo CCM iliendelea kupata ridhaa ya wananchi kuongoza nchi. Aidha, wabunge wanaume walikuwa asilimia 63.3 na wanawake asilimia 36.7 kama ilivyokuwa katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015. Kwa upande mwingine,

wanawake katika Baraza la Mawaziri waliongezeka kutoka asilimia 21.1 mwaka 2016 hadi asilimia 21.7 mwaka 2020.

194. Mwaka 2020, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma iliendelea kutekeleza majukumu yake ambapo viongozi wa umma 14,724, sawa na asilimia 97 ya viongozi 15,110 walirejesha Fomu za Tamko la Rasilimali na Madeni ikilinganishwa na viongozi 14,878 mwaka 2019. Aidha, Sekretarieti ilipokea na kuchambua malalamiko 88 ya ukiukwaji wa maadili dhidi ya viongozi wa umma ambapo malalamiko 43 yalihusu sheria ya maadili ya viongozi na malalamiko 45 hayakuhusu sheria hiyo.

## SURA YA 9

## HALI YA UMASKINI NA MAENDELEO YA WATU


**Utangulizi**

195. Mwaka 2020, Serikali kupitia Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21) iliendelea na juhudi za kujenga misingi thabiti ya uchumi wa viwanda kwa kuhakikisha maendeleo jumuishi ya jamii kwa kuboresha huduma za msingi hususan, elimu, afya na maji. Kutokana na juhudi hizo, Tanzania imeingia katika kundi la nchi za uchumi wa kati wa chini kutoka kundi la nchi maskini. Aidha, Serikali iliendelea kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030 na Malengo ya Agenda ya Afrika ya Mwaka 2063 kwa lengo la kuhakikisha umaskini wa aina zote ikiwa ni pamoja na umaskini uliokithiri unatokomezwa ili kufikia malengo hayo.

**Hali ya Umaskini**

196. Kwa mujibu wa Taarifa ya mwenendo wa umaskini kwa kipindi cha mwaka 1991 hadi 2020 kiwango cha umaskini wa mahitaji ya msingi kilikadiriwa kupungua kutoka asilimia 26.4 mwaka 2018 hadi asilimia 25.7 mwaka 2020. Aidha, kiwango cha umaskini wa chakula kilipungua kutoka asilimia 8.0 mwaka 2018 hadi asilimia 7.3 mwaka 2020. Kupungua kwa viwango vya umaskini nchini kulichangiwa na upatikanaji wa umeme na maji, uboreshwaji wa huduma za afya, kuendeleza utoaji wa elimumsingi bila ada pamoja na kaya maskini kuwezeshwa kupitia Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini.

**Kielelezo Na. 9.1: Mwenendo wa Kiwango cha Umaskini wa Mahitaji ya Msingi na Chakula Mwaka 1992 hadi 2020**



**Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini**

197. Mwaka 2020, Serikali iliendelea kuboresha hali za maisha ya watu wanaoishi katika umaskini uliokithiri kupitia programu mbalimbali ikiwemo Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini. Mpango huo ulitekelezwa kupitia maeneo matatu ambayo ni: kuhawilisha fedha kwa kaya maskini ili ziweze kukidhi matumizi ya kaya ikiwa ni pamoja na kuboresha lishe, kujenga uwezo wa uzalishaji na kulinda rasilimali watu; kutoa ajira za muda kwa kaya za walengwa ili kuongeza kipato kwa kushiriki kufanya kazi katika miradi iliyoibuliwa na jamii; na kujenga uchumi wa kaya kwa kuhamasisha uundaji wa vikundi vya kuweka akiba, kukopeshana na kuwekeza kwenye miradi ya uzalishaji mali kupitia vikundi vitakavyoundwa.

198. Hadi Desemba 2020, kaya 1,087,622 zenye jumla ya wanufaika 5,641,008 zilinufaika na Mpango huo ikilinganishwa na kaya 1,067,041 zenye wanufaika 5,474,231 mwaka 2019. Kati ya wanufaika hao, wanawake walikuwa 2,858,523 sawa na asilimia 50.8 na wanaume walikuwa 2,782,485. Aidha, watoto wenye umri chini ya miaka mitano wanaotakiwa kuhudhuria kliniki walikuwa 473,844 sawa na asilimia 8.4 ya wanufaika wote, wanufaika waliokuwa katika shule za msingi na sekondari wenye umri kati ya miaka 6 hadi 18 walikuwa 2,228,198, sawa na asilimia 39.5 ya wanufaika wote na wanufaika wenye umri kati ya miaka 19 hadi 60 walikuwa 2,177,429 sawa na asilimia 38.6 ya wanufaika wote. Vile vile, wazee wenye umri wa zaidi ya miaka 60 walikuwa 761,537, sawa na asilimia 13.5 ya wanufaika wote.

**Jedwali Na. 9.1: Wanufaika wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini Mwaka 2019 - 2020**

| Jinsia/ Mwaka | Idadi ya Wanufaika | | Miaka 0-2 | Miaka 3-5 | Miaka 6-18 | Miaka 19-60 | Zaidi ya 60 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2019 | 2020 | | | | | |
| Wanaume | 2,635,238 | 2,782,485 | 97,470 | 185,234 | 1,174,859 | 1,006,655 | 313,847 |
| Wanawake | 2,838,993 | 2,858,523 | 66,119 | 125,021 | 1,053,339 | 1,170,774 | 447,690 |
| **Jumla** | 5,474,231 | 5,641,008 | 163,589 | 310,255 | 2,228,198 | 2,177,429 | 761,537 |
| **Asilimia ya wanufaika wote** | | | 2.9 | 5.5 | 39.5 | 38.6 | 13.5 |

**Chanzo:** Mfuko wa Maendeleo ya Jamii

199. Hadi Desemba 2020, shilingi bilioni 858.4 zilitolewa kupitia uhawilishaji fedha kwa wanufaika wote ikilinganishwa na shilingi bilioni 728.5 zilizotolewa mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 17.8. Katika kipindi hicho, kaya 253,117 zilinufaika na utekelezaji wa miradi 7,775 kwa kupata ajira za muda mfupi ambapo shilingi bilioni 83.5 zilitumika kulipa ujira ikilinganishwa na kaya 220,212 zilizonufaika na utekelezaji wa miradi 6,608 kupitia ajira za muda mfupi ambapo shilingi bilioni 70.9 zilitumika kulipa ujira hadi Desemba 2019. Miradi iliyotekelezwa ni pamoja na ujenzi na ukarabati wa barabara za vijijini, ujenzi na ukarabati wa malambo, uanzishwaji wa vitalu vya miche na ujenzi wa makinga maji.

200. Mwaka 2020, vikundi 23,618 kutoka katika kaya maskini vyenye wanachama 319,940 viliundwa na kuweka akiba ya shilingi bilioni 5.9 ikilinganishwa na vikundi


18,232 vyenye wanachama 253,448 na akiba ya shilingi bilioni 3.6 mwaka 2019, sawa na ongezeko la vikundi kwa asilimia 29.5. Ongezeko hilo lilitokana na uhamasishaji kwa wananchi kuunda vikundi vya kuweka akiba na kukopeshana na kutambua umuhimu wa kuweka akiba kwa ajili kwa ajili ya maendeleo ya shughuli za uzalishaji mali zinazofanywa na walengwa. Katika kipindi hicho, jumla ya shilingi bilioni 2.5 zilikopeshwa kwa wanachama wa vikundi kwa ajili ya kuanzisha au kuendeleza shughuli za uzalishaji mali ambapo wastani wa marejesho ya mikopo hiyo ni asilimia 86.5. Aidha, wanachama wa vikundi hivyo walipewa mafunzo ya kuwawezesha kuzalisha kwa tija katika shughuli za uchumi wanazofanya hususan kilimo. Vile vile, kaya maskini zenye nguvu kazi zilipatiwa mafunzo ya kuendeleza uchumi wa kaya.

201. Kupitia ruzuku zilizotolewa kwa wanufaika na mikopo ya vikundi, walengwa wameweza kuboresha maisha yao kwa kuanzisha shughuli za kiuchumi zikiwemo ufugaji, kilimo cha mazao, uvuvi na biashara ndogondogo. Hadi Desemba 2020, kaya 562,934 ziliweza kuanzisha miradi ya kilimo, kaya 33,613 miradi ya ufugaji na kaya 210,755 biashara ndogondogo. Aidha, katika miradi ya ufugaji kulikuwa na jumla ya ng’ombe 51,299, mbuzi 2,745,000, kuku 12,053,000, nguruwe 781,400, kondoo 193,608, na bata 207,176. Vile vile, Mpango umewajengea uwezo wanawake ambapo wanauwezo wa kushiriki katika shughuli mbalimbali za kijamii na kiuchumi.

**Maendeleo ya Watu**


202. Kwa mujibu wa Taarifa ya Dunia ya Maendeleo ya Watu ya Mwaka 2020 ya Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa - UNDP, Tanzania ilipanda kwa nafasi moja na kushika nafasi ya 163 kati ya nchi 189 mwaka 2019 ikilinganishwa na nafasi ya 164 mwaka 2018. Farihisi ya Maendeleo ya Watu - HDI hupima maendeleo ya watu kwa kuzingatia vigezo vya elimu, afya na hali ya Maisha. Kipimo hiki kinatafsiriwa kuwa kadiri tarakimu inavyokaribia moja (1), inaashiria kuimarika kwa maendeleo ya watu. Hivyo, kwa mujibu wa Taarifa hiyo, Farihisi ya Maendeleo ya Watu iliongezeka kutoka 0.524 mwaka 2018 hadi 0.529 mwaka 2019. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa Pato la wastani kwa mtu kwa kuzingatia uwezo wa kufanya manunuzi na wastani wa umri wa kuishi kwa mtanzania kutoka miaka 65 mwaka 2018 hadi miaka 65.5 mwaka 2019. Aidha, Taarifa hiyo ilionesha kuwa Fahirisi ya Maendeleo ya Kijinsia iliendelea kuimarika kutoka 0.936 mwaka 2018 hadi 0.948 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 1.28. Hii inamaanisha kuwa Tanzania imeendelea kupunguza pengo la tofauti ya kijinsia katika vigezo vya maendeleo ya watu. Kipimo cha Farihisi ya Maendeleo ya Kijinsia kinatafsiriwa kuwa kadri tarakimu inavyokaribia moja, ndivyo pengo la tofauti ya kijinsia linapungua.

**Kielelezo Na. 9.2: Mwenendo wa Farihisi ya Maendeleo ya Watu Nchini**




203. Mwaka 2020, Serikali iliendelea kupambana na vitendo vya rushwa katika sekta na mashirika ya umma ili kuboresha ufanisi katika matumizi ya rasilimali za umma pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa huduma muhimu katika jamii. Kutokana na juhudi hizo, Taarifa ya *Transparency International* (TI) ya mwaka 2020, ilionesha kuwa Tanzania ilipata alama 38 kati ya alama 100 ya Fahirisi ya Rushwa ikilinganishwa na alama 37 mwaka 2019. Alama hii ipo juu ya wastani wa alama 36 ambayo Nchi za Ulaya Mashariki na Asia ya Kati zilipata pamoja na alama 32 ambayo Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara zilipata ambayo inaashiria kuendelea kuimarika kwa jitihada za kupambana na vitendo vya rushwa nchini. Kutokana na Taarifa ya *Transparency International*, nafasi ya Tanzania katika kupambana na vitendo vya rushwa iliimarika na kufikia nafasi ya 94 kati ya nchi 180 mwaka 2020 ikilinganishwa na nafasi ya 96 mwaka 2019.

**Kielelezo Na. 9.3: Fahirisi ya Rushwa katika Sekta za Umma**



# SEHEMU YA TATU
## SUALA MAALUMU KIMAENDELEO

## SURA YA 10

## TANZANIA KUINGIA HADHI YA UCHUMI WA KATI WA CHINI

**Utangulizi**

204. Wastani wa Pato kwa Mtu ni uwiano wa Pato ghafi la nchi kwa idadi ya watu. Pato ghafi linaweza kupimwa kwa namna mbili: Kwanza ni Pato ghafi lililozalishwa na raia wa nchi husika waliopo ndani na nje ya nchi (Gross National Income - GNI) na pili ni Pato ghafi lililozalishwa ndani ya nchi na raia na wageni walioko ndani ya nchi husika (Gross Domestic Product - GDP). Katika kukokotoa wastani wa pato kwa mtu, Benki ya Dunia hufanya tathmini ya mwenendo wa uchumi wa nchi zote duniani kwa kuchambua viashiria mbalimbali ikiwemo pato ghafi, mwenendo wa mfumuko wa bei, idadi ya watu na thamani ya sarafu ya nchi husika. Tathmini hiyo hutumika katika upangaji wa nchi katika makundi manne ya hadhi za kiuchumi ambayo ni nchi zenye uchumi wa pato la juu, pato la kati la juu, pato la kati la chini na pato la chini. Kigezo kikuu kinachotumika kufanya upangaji huo ni wastani wa Pato Ghafi la Taifa linalozalishwa na wananchi wa Taifa husika waliopo ndani na nje ya nchi kwa mtu (GNI per capita).

205. Tanzania ni moja ya nchi ambazo uchumi wake unakua kwa kasi barani Afrika, ikiwa na wastani wa asilimia 6.4 ya ukuaji wa Pato la Taifa katika kipindi cha mwaka 2000 hadi 2020. Ukuaji huu ulitokana na utekelezaji wa miradi mikubwa ya miundombinu ya kiuchumi ikiwemo ujenzi, uchukuzi, nishati pamoja na ugharamiaji wa huduma za jamii hususan afya, elimu na maji. Sekta zilizoongoza kwa ukuaji katika kipindi hicho ni pamoja na madini, ujenzi, habari na mawasiliano na usafirishaji na uhifadhi mizigo.

206. Katika kipindi cha mwaka 2000 hadi 2020, mfumuko wa bei ulidhibitiwa na kubaki katika wigo wa tarakimu moja isipokuwa katika kipindi cha mwaka 2008 na 2009 kutokana na kupanda kwa bei ya mafuta na mdororo wa sekta ya fedha duniani na mwaka 2011 na 2012 kutokana na ukame ulioathiri uzalishaji na upatikanaji wa mazao ya chakula. Pamoja na changamoto hizo, wastani wa mfumuko wa bei kati ya mwaka 2000 hadi 2020 ulikuwa tarakimu moja ya asilimia 6.7. Kwa upande wa thamani ya sarafu ya Tanzania dhidi ya dola ya Marekani katika kipindi hicho ilikuwa na vipindi vingi vya kupungua ingawa kwa sehemu kubwa ilipungua kwa kasi ndogo ya wastani wa chini ya asilimia 3.0. Vile vile, kwa mujibu wa matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012, idadi ya watu nchini ilikuwa inaongezeka kwa wastani wa asilimia 2.7 kwa mwaka kwa kipindi cha mwaka 2002 hadi 2012. Hata hivyo, katika kipindi cha mwaka 2013 hadi 2020, idadi ya watu ilikadiriwa kuongezeka kwa wastani wa asilimia 3.2 kwa mwaka.

207. Mnamo Julai 2020, Benki ya Dunia iliitangaza Tanzania kuingia katika kundi la nchi za hadhi ya uchumi wa pato la kati la chini, ikiwa na wastani wa Pato kwa Mtu wa dola za Marekani 1,080 mwaka 2019 kutoka dola za Marekani 1,020 mwaka 2018. Wastani huo ni zaidi ya kigezo cha wastani wa dola za Marekani 1,036 kilichowekwa na Benki ya Dunia kwa nchi kufikia hadhi hiyo. Aidha, thamani ya Pato Ghafi la Taifa kwa bei za mwaka husika ilikuwa dola za Marekani milioni 55,194 mwaka 2019 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 51,878 mwaka 2018. Mafanikio ya Tanzania kukidhi vigezo vya kuingia katika kundi hilo yalitokana na kuongezeka kwa kasi ya ukuaji wa uchumi; utulivu wa thamani wa shilingi; na mfumuko mdogo wa bei katika kipindi cha mwaka 2013 hadi 2019. Nchi kupanda daraja kulingana na kigezo cha wastani wa Pato kwa Mtu kuna fursa na changamoto zake na pia ikumbukwe kuwa nchi inaweza kupanda na kushuka kutoka kundi moja kwenda lingine kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo mabadiliko ya viasharia vya uchumi katika kipindi husika.

**Viashiria vya Uchumi wa Tanzania Kuelekea Hadhi ya Uchumi wa Kati**

208. Sehemu hii inabainisha mwenendo wa viashiria mbalimbali vya uchumi kufikia hadhi ya uchumi wa kati wa chini. Viashiria hivyo ni kama ifuatavyo:

**Ukuaji wa Uchumi na Idadi ya Watu**

209. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2016 – 2020), Tanzania iliendelea kuwa na uchumi imara ambapo Pato halisi la Taifa lilikua kwa wastani wa asilimia 6.5 kwa mwaka. Ukuaji huo ulitokana na kuboreshwa kwa huduma za usafiri na usafirishaji pamoja na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa barabara, reli, viwanja vya ndege, miradi ya nishati ya umeme pamoja na ujenzi na ukarabati wa vituo vya kutolea huduma za afya. Aidha, Pato halisi la Taifa lilikua kwa wastani wa asilimia 4.8 mwaka 2020 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 7.0 mwaka 2019. Kasi ndogo ya ukuaji ilichangiwa na mvua zilizozidi wastani na kusababisha mafuriko yaliyoharibu miundombinu ya usafirishaji na kuchelewesha utekelezaji wa baadhi ya miradi pamoja na athari za janga la UVIKO-19 ulioenea katika nchi washirika wa kibiashara.

210. Kwa upande wa idadi ya watu, Sensa ya Watu na Makazi iliyofanyika mwaka 2012 ilionesha kuwa idadi ya watu nchini ilikuwa ikiongezeka kwa wastani wa asilimia

211. 2.9 kwa mwaka ambapo jumla ya watu wote ilikuwa 44,928,923. Aidha, idadi ya watu ilikadiriwa kuongezeka kwa wastani wa asilimia 3.2 kati ya mwaka 2013 hadi 2020. Ongezeko kubwa la idadi ya watu huchangia kupungua kwa wastani wa pato kwa mtu na kuongeza bajeti ya Serikali kwa ajili ya kugharamia mahitaji mbalimbali yakiwemo huduma za jamii kama vile elimu, afya na maji.

**Mfumuko wa Bei**

212. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2016 – 2020), mfumuko wa bei ulikuwa tulivu na wa kuridhisha ukiwa wa wastani wa asilimia 4.2. Kuimarika kwa mfumuko wa bei kulitokana na usimamizi madhubuti wa sera za fedha na bajeti, kuimarika kwa bei za mafuta katika soko la dunia pamoja na upatikanaji wa chakula cha kutosha katika masoko ya ndani na nchi jirani. Utulivu wa mfumuko wa bei huimarisha uwezo wa wananchi kumudu gharama za maisha, huchochea shughuli za uzalishaji, na kuongeza ushindani wa bidhaa zinazozalishwa ndani na nje ya nchi na hivyo kuchangia ukuaji wa Pato la Taifa na kuongezeka kwa Pato la Wastani kwa Mtu.


**Thamani ya Shilingi**

213. Thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya dola ya Marekani iliendelea kuwa tulivu katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita (2017 – 2020) ambapo ilishuka kwa kiwango kisichozidi wastani wa asilimia 1.3. Utulivu wa thamani ya shilingi ulitokana na utekelezaji madhubuti wa sera ya fedha, kuongezeka uzalishaji wa bidhaa za viwandani, kuimarika kwa akiba ya fedha za kigeni, mfumuko mdogo wa bei na kuimarika kwa ukuaji wa uchumi. Utulivu wa thamani ya shilingi huvutia uwekezaji na mauzo nje ambayo huchangia katika ukuaji wa uchumi.

**Mauzo Nje**

214. Thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi kwa muongo mmoja uliopita ilikuwa inaongezeka mwaka hadi mwaka isipokuwa kwa miaka michache. Mwenendo mzuri wa mauzo ulitokana na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa asilia ikiwemo pamba, korosho na karafuu na bidhaa zisizo asilia ikiwemo bidhaa za viwandani, mbogamboga, maua pamoja na madini hususan dhahabu. Hata hivyo, mapato ya huduma yalipungua mwaka 2020 kutokana na kupungua kwa idadi ya watalii kufuatia hatua zilizochukuliwa na nchi washirika wetu kibiashara kusitisha safari ili kukabiliana na maambukizi ya UVIKO – 19. Masoko makubwa ya bidhaa za Tanzania ni nchi za Afrika Kusini, India, Kenya, Umoja wa Falme za Kiarabu, Uswisi, Vietnam na China. Ukuaji wa mauzo nje ni kiashiria cha kuongezeka kwa uzalishaji wa ndani, ukuaji wa Pato la Taifa na ongezeko la akiba ya fedha za kigeni.

**Kielelezo Na.10.1: Mwenendo wa Mauzo Nje (Dola za Marekani Milioni)**




**Deni la Serikali na Uhimilivu wa Deni**

215. Serikali imeendelea kukopa mikopo nafuu kutoka kwa nchi wahisani pamoja na mikopo ya kibiashara ya ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kugharamia ujenzi wa miradi ya maendeleo ambayo ni chachu ya ukuaji wa uchumi. Hadi Desemba 2020, deni la Serikali lilifikia shilingi bilioni 59,009.8 ambapo deni la ndani lilikuwa shilingi bilioni 16,179.6 na deni la nje shilingi bilioni 42,830.2. Aidha, sehemu kubwa ya deni la nje ilikuwa ni mikopo nafuu kutoka nchi wahisani lakini sura ya deni imebadilika ambapo mikopo ya kibiashara imeongezeka kufikia asilimia 44.5 ya deni lote la nje mwaka 2019/20 kutoka asilimia 7.2 mwaka 2010/11 na wakati huo huo mikopo ya masharti nafuu ilipungua kufikia asilimia 55.5 kutoka asilimia 92.8 katika kipindi hicho. Hata hivyo, tathmini ya Uhimilivu wa Deni la Taifa iliyofanyika mwaka 2020 ilionesha kuwa deni la Taifa ni himilivu katika kipindi cha muda mfupi, wa kati na mrefu kwa kuzingatia ukomo wa viashiria vyote vinavyokubalika kimataifa. Serikali itaendelea kuhakikisha kuwa inaelekeza fedha zinazotokana na mikopo ya kibiashara katika miradi inayochochea kasi ya ukuaji wa uchumi ili kuwa na uwezo wa kurejesha mikopo hiyo kulingana na masharti ya mikopo husika.

**Maendeleo ya Watu**

216. Shirika la Maendeleo Duniani (UNDP) hutoa ripoti ya maendeleo ya watu duniani katika nchi 189 kwa kuzingatia fahirisi ya maendeleo ya watu duniani (Human Development Index - HDI). Fahirisi katika ripoti hiyo huonesha mwenendo wa viashiria vya maendeleo ya watu duniani kwa kuangazia nyanja kuu tatu ambazo ni: maisha yanayoambatana na afya bora; kiwango na upatikanaji wa maarifa; na kiwango cha maisha bora. Maisha yenye afya bora hupimwa kwa kuangalia wastani wa muda wa mtu kuishi; Kiwango cha maarifa hupimwa kwa kuangalia wastani wa muda wa kuwepo shuleni kwa kundi la watu wazima ambao ni wastani wa muda unaotumiwa na mtu kuwepo shuleni kwa kundi la watu wenye umri kuanzia miaka 25 na kuendelea. Aidha,

upatikanaji wa maarifa hupimwa kwa kuangalia muda tarajiwa wa kuwepo shuleni kwa watoto walio na umri wa kuanza shule. Vilevile, kiwango cha maisha bora hupimwa kwa wastani wa pato la taifa kwa mtu.

217. Kati ya mwaka 1990-2019, fahirisi ya maendeleo ya watu kwa Tanzania iliongezeka kwa asilimia 43.8 kutoka 0.368 hadi 0.529. Mwaka 2019, viwango vya wastani wa muda wa kuishi na wastani wa muda wa kuwepo shuleni vilikuwa miaka 65.5 na miaka 6.1 mtawalia. Viwango hivyo ni juu ya viwango vya wastani kwa nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara vya miaka 61.5 kwa umri wa kuishi na miaka 5.8 kwa muda wa kuwepo shuleni**. Jedwali Na. 10.1** linaonesha mwenendo wa viashiria vya fahirisi ya maendeleo ya watu kwa Tanzania kati ya mwaka 1990 na 2019.

**Jedwali Na. 10.1: Mwenendo wa Viashiria vya Fahirisi ya Maendeleo ya Watu kwa Tanzania Kati ya Mwaka 1990 - 2019**

| Mwaka | Wastani wa muda wa kuishi (Miaka) | Muda tarajiwa wa kuwepo shuleni (Miaka) | Wastani wa muda wa kuwepo shuleni (Miaka) | Maendeleo ya Watu-HDI (Fahirisi) |
|---|---|---|---|---|
| 1990 | 50.2 | 5.5 | 3.6 | 0.368 |
| 1995 | 49.3 | 5.4 | 4.1 | 0.367 |
| 2000 | 50.8 | 6.2 | 4.2 | 0.39 |
| 2005 | 54.3 | 7.6 | 4.8 | 0.437 |
| 2010 | 58.6 | 8.8 | 5.1 | 0.481 |
| 2015 | 63.1 | 8.5 | 5.9 | 0.514 |
| 2016 | 63.8 | 8.5 | 6 | 0.52 |
| 2017 | 64.5 | 8.3 | 6 | 0.523 |
| 2018 | 65 | 8.1 | 6 | 0.524 |
| 2019 | 65.5 | 8.1 | 6.1 | 0.529 |

**Chanzo**: Shirika la Maendeleo Duniani

### Hali ya Umaskini

218. Kipimo kingine cha maendeleo ya nchi ni hali ya umasikini. Kwa mujibu wa Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya (HBS) kiwango cha umaskini wa mahitaji ya msingi kilipungua kutoka asilimia 28.2 mwaka 2011/12 kufikia asilimia 25.7 mwaka 2020 wakati umaskini wa chakula ulipungua kutoka asilimia 9.7 mwaka 2011/12 hadi kufikia asilimia 7.3 mwaka 2020. Haya ni matokeo ya juhudi endelevu za Serikali za kuboresha hali ya maisha, ustawi wa jamii, kupunguza umaskini na kuboresha maendeleo ya watu ikijumuisha upatikanaji wa huduma za msingi na mali zinazotumika katika uzalishaji kama vile nishati, barabara unganishi, masoko na maji, huduma za afya na elimu. Kama ilivyokuwa kwa tafiti zilizotangulia, uchambuzi wa Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya mwaka 2017/18 unaonesha kuwa hali ya umaskini wa mtu mmoja

mmoja kwa mahitaji ya msingi katika maeneo ya vijijini ambayo ni asilimia 31.3 ipo juu ikilinganishwa na asilimia 15.8 maeneo ya mijini.

**Tofauti za Kipato**

219. Tofauti ya kipato hupimwa kwa kutumia kipimo cha *Gini coefficient* ambacho huanzia sifuri (0) kama hakuna tofauti ya kipato mpaka moja (1) kama kuna tofauti kubwa ya kipato. Pamoja na wastani wa pato kwa mtu kuongezeka, ni vizuri nchi kuwa na mgawanyiko mzuri wa kipato baina ya wananchi ili kufikia maendeleo endelevu na shirikishi. Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya (2017/18) unaonesha kuwa kuna ongezeko la tofauti ya kipato kutokana na kipimo cha *Gini* (*Gini Coefficient)* kutoka 0.34 mwaka 2011/12 hadi 0.38 mwaka 2017/18. Aidha, tofauti ya kipato imekuwa kubwa katika maeneo ya miji mikubwa kama Dar es Salaam iliyosababishwa na watu wengi wa vijijini kuhamia Dar es Salaam kutafuta ajira za viwandani na maisha bora zaidi. Njia ya kudhibiti hali hii ni kuongeza upatikanaji wa fursa na huduma bora za kijamii katika maeneo ya vijijini. **Jedwali Na. 10.2** linaonesha mwenendo wa tofauti za kipato Tanzania bara.

**Jedwali Na. 10.2: Mwenendo wa Tofauti za Kipato Tanzania**

| Mwaka | Dar es Salaam | Miji Mingine | Vijijini | Tanzania Bara |
|---|---|---|---|---|
| 1991/92 | 0.30 | 0.35 | 0.33 | 0.34 |
| 2000/01 | 0.36 | 0.36 | 0.33 | 0.35 |
| 2007/08 | 0.34 | 0.35 | 0.33 | 0.35 |
| 2011/12 | 0.35 | 0.37 | 0.29 | 0.34 |
| 2017/18 | 0.42 | 0.38 | 0.32 | 0.38 |

**Chanzo**: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Mwenendo wa Mapato na Matumizi**

220. Upatikanaji wa mapato huiwezesha Serikali kugharamia shughuli za msingi katika kutoa huduma mbalimbali kwa wananchi. Matumizi haya yanahusisha ugharamiaji miradi ya maendeleo, ulipaji wa deni la Serikali na matumizi ya kawaida. Hata hivyo, mapato ya ndani ya Serikali yamekuwa hayatoshi kugharamia utekelezaji wa bajeti ya Serikali na kuilazimu Serikali kutafuta vyanzo vingine vya mapato kwa ajili ya kuziba nakisi ya bajeti. Vyanzo hivyo ni pamoja na misaada, mikopo nafuu na mikopo yenye masharti ya kibiashara.

**Mapato ya Ndani**

221. Mapato halisi ya ndani yaliongezeka kutoka shilingi bilioni 17,944.8 mwaka 2016/17 hadi shilingi bilioni 21,146.7 mwaka 2019/20. Wastani wa mapato ya kodi kwa mwezi uliongezeka kutoka shilingi bilioni 825 kwa mwezi mwaka 2014/15 hadi shilingi trilioni 1.5 kwa mwezi mwaka 2019/20. Ongezeko la mapato lilitokana na juhudi

zilizofanywa na Serikali kudhibiti upotevu wa mapato kwa kuimarisha usimamizi wa sheria za kodi na matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika ukusanyaji wa mapato. Kwa wastani, mapato ya ndani hugharamia asilimia 66.0 ya bajeti yote ya Serikali.

**Misaada na Mikopo Nafuu**

222. Chanzo kingine cha kugharamia bajeti ya Serikali ni misaada na mikopo nafuu kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Utegemezi wa mikopo na misaada nafuu katika bajeti ya Serikali umepungua kutoka wastani wa asilimia 20.7 ya bajeti yote kati ya mwaka 2010/11 na 2014/15 hadi wastani wa asilimia 9.2 kati ya mwaka 2015/16 na 2019/20. Hii ilitokana na juhudi za Serikali za kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani. Baada ya Tanzania kuwa na hadhi ya uchumi wa pato la kati la chini, utegemezi huo unatarajia kushuka zaidi kutokana na kubadilika kwa vigezo na masharti ya upatikanaji wa misaada na mikopo hiyo.

**Jedwali Na. 10.3: Utegemezi wa Misaada na Mikopo nafuu kwa Bajeti ya Serikali**

**(Shilingi Bilioni)**

| Mwaka | Bajeti ya Serikali (Halisi) | Misaada (Halisi) | Mikopo ya Masharti nafuu (Halisi) | Jumla (Misaada na mikopo nafuu) | Uwiano wa Misaada na Mikopo nafuu katika Bajeti ya Serikali (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|
| 2010/11 | 10,203 | 1,622 | 1,058 | 2,680 | 26.3 |
| 2011/12 | 12,172 | 1,849 | 963 | 2,812 | 23.1 |
| 2012/13 | 15,404 | 1,585 | 1,390 | 2,975 | 19.3 |
| 2013/14 | 15,668 | 1,520 | 1,719 | 3,239 | 20.7 |
| 2014/15 | 17,489 | 442 | 1,998 | 2,440 | 14.0 |
| 2015/16 | 22,544 | 361 | 1,387 | 1,748 | 7.8 |
| 2016/17 | 25,418 | 1,032 | 1,442 | 2,474 | 9.7 |
| 2017/18 | 26,611 | 1,166 | 1,300 | 2,466 | 9.3 |
| 2018/19 | 28,963 | 802 | 1,280 | 2,082 | 7.2 |
| 2019/20 | 29,935 | 928 | 2,632 | 3,560 | 11.9 |

**Chanzo:** Wizara ya Fedha na Mipango

**Mikopo ya kibiashara**

223. Tanzania ilivyokuwa nchi ya pato la chini ilikuwa ikinufaika na mikopo yenye masharti nafuu na misaada kutoka taasisi za fedha za kimataifa na nchi wahisani. Mikopo nafuu na misaada hiyo imefanya nchi kuwa na sura nzuri ya deni (debt portifolio) ambapo kwa mujibu wa Mkakati wa Kati wa Kusimamia Deni wa mwaka 2019, muda wa wastani wa kulipa mikopo (Average Time to Maturiy) ni miaka 11, muda wa wastani wa kubadilika kwa riba (Average Time to Refixing) ni miaka 10.8 na asilimia 88.0 ya deni la Serikali ina riba isiyobadilika (fixed rate debt). Sifa hizi za sura

ya deni la Serikali (debt portifolio) zilitokana na nchi kunufaika na mikopo nafuu kutoka taasisi za fedha za kimataifa na nchi wahisani. Sifa hizi zimesababisha deni la Serikali kuwa na athari kidogo ikilinganishwa na nchi nyingine ambazo sehemu kubwa ya mikopo yake ni yenye masharti ya kibiashara.

224. Mwaka 2011, Serikali ilianza kukopa mikopo ya nje yenye masharti ya kibiashara kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya kugharamia miradi ya maendeleo na kupungua kwa upatikanaji wa misaada na mikopo yenye masharti nafuu. Baadhi ya masharti ya mikopo ya kibiashara ni pamoja na muda mfupi wa kuiva kati ya miaka 5 hadi 10, viwango vya riba vya soko vya wastani wa asilimia 7, riba inayo badilika na muda mfupi wa kutolipa mtaji yaani *grace period*.

225. Tanzania kuwa na uchumi wa kati kutasababisha kupungua zaidi kwa misaada na mikopo yenye masharti nafuu, hivyo kulazimu Serikali kukopa zaidi mikopo yenye masharti ya kibiashara kutoka katika masoko ya fedha ya kimataifa ambayo pamoja na kuiongezea Serikali gharama za kulipia mikopo hiyo pia itasababisha kubadilika kwa sura ya deni (debt portifolio) ambapo muda wa wastani wa kulipa mikopo (Average Time to Maturity) na muda wa wastani wa kubadilika kwa riba (Average time to Refixing) utapungua na mikopo yenye riba zinazobadilika itaongezeka. Kubadilika kwa sura ya deni kutasababisha kuongezeka kwa athari mbalimbali katika deni la Serikali pamoja na kuongezeka kwa gharama za ulipaji wa mikopo hiyo. Pamoja na Tathmini ya Deni la Serikali iliyofanyika Desemba 2020 kuonesha kuwa deni la Serikali ni himilivu, Serikali itaendelea kuchukua tahadhari katika ukopaji kutokana na hali hii ya kubadilika kwa sura ya deni.

226. Kwa upande mwingine, Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa pato la kati kunasababisha nchi kuaminika zaidi na wakopeshaji wa mikopo yenye masharti ya kibiashara (creditworth) kutoka taasisi za kifedha za kimataifa na nchi wahisani. Aidha, kuongezeka kwa uaminifu katika uwezo wa kurejesha mkopo kutasaidia kiwango cha riba kupungua na kupelekea Serikali kupata kwa urahisi fedha za kugharamia miradi ya maendeleo. Kwa upande wa mikopo ya ndani, Serikali imekuwa inakopa mikopo ya ndani kwa nia ya kukuza soko la mitaji, kulipia amana za Serikali zilizoiva na kuziba nakisi ya kibajeti. Hata hivyo, mikopo ya ndani imewekewa ukomo wa asilimia moja ya Pato la Taifa ili Serikali isikope zaidi katika soko la ndani na kuibana sekta binafsi (*to avoid crowd out effect*).

**Ugharamiaji wa Miradi ya Maendeleo**

227. Katika kipindi cha mwaka 2015/16 hadi mwaka 2019/20, Serikali ililenga kuhakikisha kuwa asilimia 40 ya bajeti yote ya Serikali inaelekezwa katika utekelezaji wa miradi ya kielelezo na kimkakati. Miradi hiyo ni pamoja na: Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Mwalimu Julius Nyerere; ujenzi wa miundombinu ya reli, barabara, bandari, na viwanja vya ndege; uboreshaji wa shirika la ndege Tanzania;

uboreshaji na uimarishaji wa huduma za jamii ikiwemo afya, elimu, umeme vijijini na maji; pamoja na kuimarisha sekta za uzalishaji. Mwenendo halisi wa utekelezaji unaonesha kuwa bajeti ya maendeleo ilikuwa inaongezeka mwaka hadi mwaka kutoka asilimia 22.5 ya bajeti yote mwaka 2015/16 hadi asilimia 32 mwaka 2019/20.

**Jedwali Na. 10.4: Matumizi Halisi ya Fedha katika Miradi ya Maendeleo (Bilioni) mwaka 2015/16 – 2019/20**

| | 2015/16 | 2016/17 | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 |
|---|---|---|---|---|---|
| Jumla ya Matumizi ya Serikali | 22,544 | 25,418 | 26,440 | 28,962 | 30,208 |
| Matumizi ya Maendeleo | 4,340 | 7,272 | 7,445 | 8,494 | 10,002 |
| Fedha za Ndani | 2,905 | 5,141 | 5,397 | 6,536 | 6,833 |
| Fedha za Nje | 1,435 | 2,131 | 2,048 | 1,958 | 3,169 |
| Uwiano wa fedha za nje kwa Matumizi ya maendeleo (Asilimia) | 33.1 | 29.3 | 27.5 | 23.1 | 31.7 |
| **Uwiano wa Matumizi ya maendeleo kwa Matumizi yote (Asilimia)** | **19.3** | **28.6** | **28.2** | **29.3** | **33.1** |

**Chanzo:** Wizara ya Fedha na Mipango

### Wastani wa Pato kwa Mtu

228. Benki ya Dunia hukokotoa wastani wa Pato kwa Mtu kila mwaka kwa nchi zote duniani kwa kutumia Mbinu ya *Atlas*. Mbinu hii hupunguza tofauti ya takwimu inayoweza kujitokeza hasa kutokana na tofauti ya kiwango cha ubadilishaji fedha na mfumuko wa bei. Takwimu muhimu zinazotumika katika Mbinu hii ni idadi ya watu, Pato ghafi lililozalishwa na wananchi wa nchi husika walioko ndani na nje ya nchi (GNI) mfumuko wa bei na thamani ya sarafu ya nchi husika. Kwa kuzingatia Mbinu ya ukokotoaji ya *Atlas*, Benki ya Dunia kila mwaka mwezi Julai hufanya mapitio ya ukomo wa wastani wa pato kwa mtu kwa nchi na kuzigawa nchi katika makundi ya kiuchumi kulingana na Pato kwa Mtu. Mgawanyo wa makundi ya nchi kimapato na ukomo ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 10.5**


**Jedwali Na. 10.5: Kundi la Nchi kwa Wastani wa Pato kwa Mtu**

| Na. | Aina ya Kundi | Ukomo - 2019 (dola za Marekani) | Ukomo - 2020 (dola za Marekani) |
|---|---|---|---|
| 1 | Pato la chini | Chini ya 1,025 | Chini ya 1,036 |
| 2 | Pato la kati la chini | 1,026 – 3,995 | 1,036 – 4,045 |
| 3 | Pato la kati la juu | 3,996 – 12,375 | 4,046 – 12,535 |
| 4 | Pato la juu | Zaidi ya 12,375 | Zaidi ya 12,535 |

**Chanzo**: Benki ya Dunia

229. Kufuatia matokeo ya ukokotoaji yaliyotolewa na Benki ya Dunia Julai 2020, nchi saba (7) zilipanda hadhi, tatu (3) zilishuka hadhi na nyingine zilizosalia zilibaki kama zilivyokuwa awali. Matokeo hayo yalionesha kuwa Tanzania ilifanikiwa kuingia katika kundi la nchi za uchumi wa pato la kati la chini (lower middle income) ikiwa na wastani wa Pato kwa Mtu wa dola za Marekani 1,080 mwaka 2019 ambao ni zaidi ya ukomo uliowekwa wa dola za Marekani 1,036. Aidha, Tanzania iliingia katika kundi hilo mapema ikilinganishwa na malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya kufikia uchumi wa kipato cha kati ifikapo mwaka 2025. Tanzania kuingia katika kundi hilo kulitokana na matokeo chanya katika vigezo vya kiuchumi ikiwemo kuongezeka kwa kasi ya ukuaji wa uchumi, utulivu wa thamani ya shilingi, na mfumuko wa bei uliobaki katika wigo wa tarakimu moja.

**Kielelezo Na. 10.2: Mwenendo wa Wastani wa Pato la Mtu mwaka 2012-2019**




230. Nchi nyingine za Afrika zilizopanda daraja ni pamoja na Benin kutoka uchumi wa pato la chini wa dola za Marekani 870 kwa mtu mwaka 2018 kufikia uchumi wa pato la kati la chini wa dola za marekani 1,250 kwa mtu mwaka 2019 na Mauritius iliyotoka uchumi wa pato la kati la juu wa dola za Marekani 12,050 kwa mtu mwaka 2018 kufikia uchumi wa pato la juu wa dola za Marekani 12,740 kwa mtu mwaka 2019. Kwa upande mwingine, Algeria na Sri Lanka zilishuka kutoka uchumi wa pato la kati la

juu na kuwa nchi za uchumi wa pato la kati la chini. Pato la wastani kwa mtu kwa nchi hizo lilishuka kutoka dola za Marekani 4,060 mwaka 2018 hadi dola za Marekani 3,970 kwa Algeria na dola za Marekani 4,020 kwa Sri Lanka mwaka 2019. Tathmini hii inaonesha kuwa nchi zinaweza kupanda hadhi au kushuka kulingana na jinsi zinavyosimamia uchumi jumla au kukabiliana na matukio ya dharura kama vile magonjwa ya mlipuko, majanga ya asili na vita.

231. Nchi kumi zinazoongoza duniani kuwa na wastani mkubwa wa pato kwa mtu kama ilivyotangazwa Julai 2020 ni; Switzerland (dola za Marekani 85,500), Norway (dola za Marekani 82,500), Luxembourg (dola za Marekani 73,910), Iceland (dola za Marekani 72,850), Marekani (dola za Marekani 65,850), Ireland (dola za Marekani 64,000), Denmark (dola za Marekani 63,950), Qatar (dola za Marekani 61,180), Singapore (dola za Marekani 59,590) na Sweden (dola za Marekani 55,780). Kwa upande wa Afrika, nchi kumi zinazoongoza kuwa na wastani mkubwa wa pato kwa mtu ni pamoja na : Seychelles (dola za Marekani 16,900), Mauritius (dola za Marekani 12,900), Botswana (dola za Marekani 7,650), Gabon (dola za Marekani 7, 170), Guinea ya Ikweta (dola za Marekani 6,460), Afrika Kusini (dola za Marekani 6,040), Namibia (dola za Marekani 5,060), Algeria (dola za Marekani 4,040), Eswatini (dola za Marekani 3,670) na Tunisia (dola za Marekani 3,370). Ni vema ikaeleweka kuwa ukokotoaji wa wastani wa pato kwa mtu ulitumia takwimu za mwaka 2019 na hivyo athari za UVIKO-19 hazikuzingatiwa kwenye matokeo ya tathmini hii. Kwa ujumla, wastani wa pato kwa mtu duniani ni dola za Marekani 11,566 kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 10.6.**

**Jedwali Na. 10.6: Mchanganuo wa Baadhi ya Viashiria kwa Matabaka ya Kipato mwaka 2019**

| Tabaka la Kipato | Pato Ghafi (GDP - dola za Marekani Bilioni) | Asilimia ya Pato Ghafi la Dunia | Idadi ya watu (Milioni) | Asilimia ya watu Duniani | Pato la Wastani kwa Mtu (dola za Marekani) |
|---|---|---|---|---|---|
| Pato la juu | 55,517 | 62.8 | 1,235.9 | 16.1 | 45,348 |
| Pato la kati la juu | 25,393 | 29.4 | 2,855.9 | 37.2 | 9,050 |
| Pato la Kati | 31,679 | 36.6 | 5,769.2 | 75.2 | 5,580 |
| Pato la Kati cha Chini | 6,276 | 7.2 | 2,913.4 | 38.0 | 2,176 |
| Pato la Chini | 533 | 0.6 | 668.5 | 8.7 | 820 |
| Nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara | 1,709 | 2.0 | 1,107.0 | 14.4 | 1,555 |
| **Jumla** | **87,693** | **100** | **7,673.5** | **100** | **11,566** |

**Chanzo:** Benki ya Dunia

## Misaada na Mikopo Kutoka Taasisi na Mashirika ya Fedha ya Kimataifa

232. Tanzania hushirikiana na taasisi na mashirika mbalimbali ya kimataifa katika nyanja mbalimbali za kiuchumi na kijamii ikiwemo upatikanaji wa misaada na mikopo

kwa ajili ya kusaidia urari wa malipo (BOP) na utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Miongoni mwa mashirika hayo ni Benki ya Dunia, Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB). Aidha, taasisi na mashirika hayo yana taratibu na miongozo ya upatikanaji wa misaada na mikopo kwa wanachama kulingana na hadhi ya uchumi wa nchi husika. Hivyo, Tanzania kuingia katika uchumi wa pato la kati kutabadilisha vigezo na masharti ya ushirika wa nchi na taasisi/mashirika hayo hususan katika upatikanaji wa misaada na mikopo kama ifuatavyo:

**Benki ya Dunia**

233. Benki ya Dunia ina jumla ya nchi wanachama 189 na inaundwa na taasisi tano ambazo ni: Shirikisho la Kimataifa la Maendeleo – IDA, Benki ya Kimataifa ya Marekebisho na Maendeleo -IBRD, Taasisi ya Fedha ya Kimataifa - IFC, Shirika la Uwekezaji na Dhamana - MIGA na Kituo cha kimataifa cha utatuzi wa mizozo ya kiuwekezaji -ICSID. Benki hiyo hutoa mikopo na misaada kwa nchi wanachama kwa kuzingatia wastani wa pato kwa mtu na uhimilivu wa deni la Serikali kupitia madirisha ya: Shirikisho la Kimataifa la Maendeleo- IDA; Benki ya Kimataifa ya Marekebisho na Maendeleo -IBRD; na Kundi la nchi mchanganyiko -*Blended Countries*.

234. Dirisha la Shirikisho la Kimataifa la Maendeleo - IDA hutoa mikopo na misaada nafuu kwa nchi zenye uwezo mdogo wa kukopesheka, viashiria hatarishi vya deni na wastani wa pato kwa mtu wa chini ya ukomo wa Shirikisho la Kimataifa la Maendeleo (IDA's operational threshold) ambapo kwa mwaka 2020 ukomo ulikuwa dola za Marekani 1,185. Aidha, Dirisha la Benki ya Kimataifa ya Marekebisho na Maendeleo - IBRD hutoa mikopo ya kibiashara kwa nchi za pato la kati zenye deni himilivu na wastani wa pato kwa mtu ulio juu ya ukomo uliowekwa na IDA. Kwa upande mwingine, dirisha la nchi Mchanganyiko - *Blend Countries* linajumuisha nchi zenye deni himilivu na wastani wa pato kwa mtu ulio chini ya ukomo uliowekwa na IDA ambapo nchi hizo hunufaika na misaada na mikopo yenye masharti nafuu kupitia IDA na mikopo ya kibiashara kupitia IBRD.

235. Kabla ya Tanzania kuingia hadhi ya uchumi wa pato la kati la chini ilikuwa ikinufaika na misaada na mikopo nafuu kutoka Benki ya Dunia kupitia dirisha la IDA ambapo baada ya kuingia uchumi wa pato la kati la chini Tanzania imewekwa katika kundi la Blend Countries linalojumuisha misaada na mikopo yenye masharti nafuu kutoka IDA na mkopo ya kibiashara kutoka IBRD. Hii imesababisha masharti ya kukopa kutoka Benki ya Dunia kuwa magumu hususan kupitia dirisha la IBRD ambapo riba ya mkopo huzingatia bei ya soko, muda wa msamaha wa kutolipa mtaji chini ya miaka sita (6) na mkopo kulipwa katika kipindi cha miaka 25 hadi 35 ikilinganishwa na mikopo inayotolewa kupitia dirisha la IDA ambayo ina riba ya asilimia sifuri (0), muda wa kutolipa mtaji wa miaka sita (6) na kipindi cha miaka 38 cha kulipa mkopo. Aidha, Tanzania itaendelea kunufaika na misaada na mikopo yenye masharti nafuu kupitia

dirisha la IDA kwa kuwa wastani wa pato kwa mtu wa dola za Marekani 1,080 upo chini ya ukomo uliwekwa na IDA wa dola za Marekani 1,185 kwa mwaka 2020.

**Shirika la Fedha la Kimataifa**

236. Shirika la Fedha la Kimataifa - IMF hutoa misaada na mikopo kwa nchi wanachama ambayo inaweza kuwa nyenzo (instruments) au programu kulingana na mazingira na hadhi ya uchumi wa nchi. Nchi zote wanachama zina haki ya kukopa kupitia dirisha la *General Resources Account* - GRA kwa viwango vya riba ya soko wakati nchi masikini huruhusiwa kukopa mikopo yenye masharti nafuu kupitia dirisha la Mpango wa Kupunguza Umaskini na Kukuza Uchumi (Poverty Reduction and Growth Trust - PRGT). Nchi inakoma kupata mikopo yenye masharti nafuu kupitia dirisha la PRGT endapo wastani wa pato kwa mtu unakua juu ya ukomo uliowekwa na IDA. Hivyo, Tanzania itaendelea kutumia fursa za mikopo kutoka dirisha la PRGT kwa kuwa wastani wa pato kwa mtu wa dola za Marekani 1,080 upo chini ya ukomo wa IDA wa dola za Marekani 1,185 kwa mwaka 2020. Nyenzo (instruments) zinazotumiwa na IMF kukopesha au kusaidia nchi wanachama ni pamoja na:

(i) Dirisha la Mkopo wa Dharura *(Standby Credit Facility - SCF):* Dirisha hili hutumika kukabiliana na changamoto za muda mfupi za urari wa malipo kwa nchi maskni kupitia dirisha la PRGT ambapo muda wa kutolipa mtaji ni miaka minne (4) na muda wa kulipa mkopo na riba ni miaka nane (8). Aidha, Nyenzo kama hii kwa nchi zisizo maskini inajulikana kama *Stand-by Arrangement (SBA)* ambayo muda wa kutolipa mtaji ni kati ya mwaka mmoja (1) hadi mitatu (3) na muda wa mkopo ni kati ya miaka mitatu (3) hadi mitano (4).

(ii) Dirisha la Mkopo wa Haraka **(***Rapid Credit Facility* – RCF) hutoa usaidizi wa haraka wa fedha kwa nchi maskini wakati wa majanga ambapo muda wa kutolipa mtaji ni miaka mitano (5) na muda wa kulipa mkopo ni miaka 10. Aidha, *Rapid Financing Instrument* (RFI) ni dirisha maalum kwa nchi zisizo maskini la kutoa mkopo wa haraka wa fedha wakati wa majanga ambapo mkopo hulipwa katika kipindi cha kati ya miaka mitatu (3) hadi mitano (5).

(iii) Misaada ya Kukabiliana na Maafa (Catastrophe Containment and Relief Trust - CCRT) hutoa misaada kwa nchi maskini kwa njia ya msamaha wa deni la Serikali ili kuziwezesha nchi zilizokumbwa na maafa kutumia fedha ambazo zingetumika kulipa deni kukabilina na maafa hayo. Tanzania ni miongoni mwa nchi zilizonufaika na mpango huu ambapo mwaka 2020 nchi ilipata msamaha wa IMF wa dola za Marekani milioni 25.6 ili kukabiliana na janga la UVIKO-19

**Benki ya Maendeleo ya Afrika**

237. Benki ya Maendeleo ya Afrika -AfDB inajumuisha nchi wanachama 53 za Afrika na nchi wanachama 25 kutoka nje ya Bara la Afrika. Benki ya Maendeleo ya

Afrika hutoa misaada na mikopo kwa wanachama kwa kuzingatia vigezo vya ukuaji wa uchumi na uwezo wa kukopesheka wa nchi kupitia mdirisha matano ambayo ni:

(i) Mfuko wa Maendeleo wa Afrika (Africa Development Fund - ADF-only) ambao unatoa misaada na mikopo yenye masharti nafuu kwa nchi wanachama wenye uwezo mdogo wa kukopesheka na wastani wa pato kwa mtu chini ya ukomo wa IDA ;
(ii) *ADF-gap countries* hutoa misaada na mikopo yenye masharti nafuu kwa nchi wanachama wenye uwezo mdogo wa kukopesheka na wastani wa pato kwa mtu ulio juu ya ukomo uliowekwa na IDA kwa miaka miwili mfululizo;
(iii) Kundi la nchi mchanganyiko (Blend countries) hutoa misaada na mikopo yenye masharti nafuu pamoja na mikopo ya kibiashara kwa nchi wanachama wenye uwezo wa kukopesheka na wastani wa pato kwa mtu chini ya ukomo uliowekewa na IDA;
(iv) *ADB-only countries* hutoa mikopo ya kibiashara kwa nchi wanachama wenye uwezo wa kukopesheka na wastani wa pato kwa mtu ulio juu ya ukomo uliowekwa na IDA; na
(v) Nchi zilizofuzu *(*Graduating counties*)* hutoa mikopo kwa nchi ambazo zipo kwenye kipindi cha mpito kuelekea dirisha la *ADB only* zenye uwezo wa kukopesheka na wastani wa pato kwa mtu ulio juu ya ukomo uliowekwa na IDA.

238. Kabla ya Tanzania kuingia hadhi ya uchumi wa pato la kati la chini ilikuwa katika dirisha la ADF only. Kutokana na kupanda kwa hadhi ya uchumi, Tanzania itakuwa katika dirisha la *Blend Countries* pindi taratibu za kubadilisha dirisha zitakapo kamilika ili kuendana na hadhi ya uchumi wa nchi. Endapo Tanzania itaingia katika kundi la *Blend countries*, masharti ya ukopaji kutoka AfDB yatakuwa magumu ikiwemo muda wa kulipa mkopo wa miaka 30, muda wa kutolipa mtaji wa miaka mitano (5), kiwango cha unafuu wa ulipaji cha asilimia 35 na riba ya asilimia moja (1) ikilinganishwa na mika 40 ya muda wa kulipa mkopo, miaka 10 ya muda wa kutolipa mtaji, asilimia 61 ya kiwango cha unafuu wa ulipaji na riba ya asilimia sifuri (0) katika dirisha la *ADF only*.

**Fursa na changamoto za Tanzania kuwa Nchi ya Uchumi wa Pato la Kati la Chini**

239. Tanzania kuingia kwenye kundi la nchi za uchumi wa pato la kati la chini kunaambatana na fursa pamoja na changamoto mbalimbali kama ifuatavyo:

**Fursa za Nchi kuwa na Hadhi ya Uchumi wa Pato la Kati**

240. Tanzania baada ya kupanda daraja na kuwa nchi ya uchumi wa pato la kati la chini, zipo fursa zitakazojitokeza ambazo ni pamoja na: -

(i) **Kuongezeka kwa wigo wa upatikanaji wa fedha za mikopo ya kibiashara kwa ajili ya miradi ya maendeleo:** Taasisi na mashirika ya fedha ya kimataifa yana

madirisha tofauti ya utoaji wa misaada na mikopo kulingana na hadhi ya nchi kimapato. Kwa Tanzania kupanda hadhi, fursa za kupata misaada zinapungua na madirisha ya fursa za upatikanaji wa mikopo yanaongezeka. Hivyo, Serikali inaweza kupata rasilimali fedha zaidi kupitia mikopo yenye masharti ya kibiashara kwa kuzingatia uwezo wa kulipa ili kutekeleza miradi ya maendeleo inayoipa nchi fursa ya kuendelea kubaki katika nchi za uchumi wa pato la kati.

(ii) **Uhuru wa kupanga matumizi:** Tanzania kuingia katika uchumi wa kati inaongeza wigo wa upatikanaji wa fedha za mikopo ya kibiashara isiyo na kibali au masharti maalum ya jinsi ya kutumia fedha hizo ikilinganishwa na fedha za misaada na mikopo yenye masharti nafuu ambazo huikosesha Serikali fursa ya kuelekeza fedha hizo kwenye maeneo mengine ya msingi zaidi. Fedha zinazotokana na mikopo ya kibiashara zinatoa fursa kwa nchi kuchagua makandarasi na washauri elekezi wazawa kutekeleza miradi ya maendeleo bila masharti yanayotolewa na nchi zinazotoa misaada na mikopo yenye masharti nafuu.

(iii) **Kuchochea uwekezaji**. Ukuaji wa wastani wa pato kwa mtu ni moja ya vigezo muhimu ambavyo wawekezaji huangalia kabla ya kuwekeza katika nchi husika ili kujiridhisha na uwezo wa kipato cha watu wa kununua bidhaa au huduma itakayotolewa na **mwekezaji** husika. Kutokana na kigezo hiki, kupanda kwa wastani wa pato kwa mtu kutavutia uwekezaji kwani huwapa uhakika wa uwepo wa wateja wenye uwezo wa kununua bidhaa na huduma zao.

(iv) **Kuondokana na utegemezi:** Moja ya fursa tarajiwa baada ya nchi kuingia katika kundi la nchi za uchumi wa kati ni pamoja na kuondokana na utegemezi unaotokana na vibali au masharti maalum ya jinsi ya kutumia fedha za misaada na mikopo yenye masharti nafuu pamoja na masharti ya kutumia kampuni za makandarasi na washauri elekezi waliopendekezwa kutekeleza miradi inayogharamiwa na fedha hizo. Hii inatoa fursa kwa Serikali kuongeza wigo wa vyanzo vipya vya kuongeza mapato ya ndani kwa ajili ya kuendelea kutekeleza miradi ya **kielelezo** na kimkakati ambayo ilikua inategemea fedha za misaada na mikopo yenye masharti nafuu.

(v) **Kuaminika katika taasisi za kifedha za kimataifa:** Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa pato la kati inaongeza imani ya wakopeshaji (creditworthiness) wa mikopo yenye **masharti** ya kibiashara kutoka katika masoko ya mitaji ya kimataifa, taasisi za kifedha za kimataifa na Washirika wa Maendeleo kutokana na kutengamaa kwa viashiria vya uchumi.

**Changamoto za Nchi kuwa Hadhi ya Uchumi wa Pato la Kati**

241. Pamoja na fursa mbalimbali zinazoweza kujitokeza, zipo pia changamoto za nchi kuwa na hadhi ya uchumi wa pato la kati la chini. Changamoto hizo ni pamoja na:

(i) **Kupungua upatikanaji wa misaada na mikopo yenye masharti nafuu:** Benki ya Dunia na Benki ya Maendeleo ya Afrika zina madirisha maalum ya kutoa misaada na mikopo yenye masharti nafuu kwa nchi changa za kipato cha chini. Kupandishwa hadhi kwa Tanzania kutasababisha fursa hizo kupungua na hivyo nchi **kulazimika** kukopa mikopo yenye masharti ya kibiashara kupitia madirisha yaliyoko katika taasisi hizo.

(ii) **Gharama kubwa za marejesho ya mkopo:** Serikali hutumia wastani wa asilimia 30 ya bajeti ya mwaka kwa ajili ya kugharamia Deni la Serikali. Baada ya Tanzania kuingia uchumi wa kati, uwiano huu utaongezeka pindi nchi itakapoanza kutegemea zaidi mikopo ya kibiashara na hivyo, kuathiri ugharamiaji wa shughuli nyingine katika bajeti. Hii inatokana na riba za mikopo ya kibiashara kuwa kubwa ambazo ni wastani wa asilimia saba kwa mwaka na muda wa marejesho ni mfupi (chini ya miaka saba) ikilinganishwa na mikopo nafuu ambayo ina riba ya wastani wa asilimia moja kwa mwaka na ina muda mrefu wa marejesho wa zaidi ya miaka 30.

(iii) **Uhimilivu wa deni:** Tanzania kuwa nchi yenye kipato cha kati ina nafasi ya kukopa zaidi mikopo ya kibiashara ambayo huambatana na riba kubwa na marejesho ya muda mfupi. Kupungua kwa mikopo yenye masharti nafuu na kuongezeka kwa mikopo yenye masharti ya kibiashara kunaweza kusababisha deni la Serikali kutokuwa himilivu.

(iv) **Kuondolewa kwa fursa za kibiashara zenye upendeleo maalum (preferential access to regional trading blocs):** Tanzania imekuwa ikipata fursa ya kuuza baadhi ya bidhaa katika masoko ya nje yanayotoa upendeleo maalum wa kuondolewa vikwazo vya kiushuru na ukomo wa kiwango cha kuuza bidhaa kwa nchi za kipato cha chini na nchi maskini. Hivyo, Tanzania kuingia katika kundi la nchi zenye hadhi ya uchumi wa pato la kati kutaikosesha fursa hiyo na bidhaa kuanza kuingia katika masoko hayo kwa utaratibu mpya wa ushuru.

(v) **Michango ya Baadhi ya Washirika wa Maendeleo kwenye Jumuiya za Kikanda:** Baadhi ya Washirika wa Maendeleo wanaochangia bajeti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki mfano Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya Dunia, Benki ya Uwekezaji ya Ulaya, Ujerumani, Marekani na Uingereza wanaweza kubadilisha vigezo vya kuchangia bajeti ya EAC kwa kutoa misaada na kupendekeza njia ya mikopo kwa nchi zenye uchumi wa Pato la Kati.

(vi) **Kuondolewa katika kundi la nchi zinazopata upendeleo wa misaada kupitia mifuko mbalimbali:** Kabla ya Tanzania kuingia katika nchi ya uchumi wa kipato

cha kati cha chini ilikuwa ikipata misaada kupitia mifuko maalumu kwa nchi maskini ikiwemo mifuko ya mabadiliko ya tabianchi na mifuko ya afya. Baadhi ya mifuko hiyo ni Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi (Global Fund na Green Climate Fund) na Mfuko wa nchi Maskini Duniani (Least Developed Countries Fund ). Kuondolewa katika kundi la nchi ya uchumi wa pato la chini kutaifanya Tanzania kukosa fursa za mifuko hiyo na kuilazimu Serikali kugharamia shughuli zilizokuwa zinatekelezwa na miradi hiyo kupitia vyanzo vingine vya fedha.

(vii) **Kuongezeka michango kwa taasisi na mashirika mbalimbali ya kimataifa: Tanzania** kupandishwa hadhi kutokana na Pato la nchi kuongezeka kutasababisha mchango wa Tanzania katika Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) na Umoja wa Afrika (AU) kuongezeka kwani mfumo wa uchangiaji hufanyika kwa kuzingatia uwezo wa nchi kulipia michango kwa kutumia kigezo cha Pato la Taifa.

**Mikakati endelevu ya kubaki katika Uchumi wa Pato la Kati**

242. Taarifa ya mapitio ya uchumi wa Tanzania toleo la 15 iliyotolewa na Benki ya Dunia Februari 2021 inaonesha kuwa katika kipindi cha muongo mmoja uliopita kulikuwa na nchi 23 zilizoshuka hadhi yao ama kutoka daraja la kati kwenda la chini au la juu kwenda la kati. Sababu kubwa za anguko zinatajwa kuwa ni majanga ya asili, magonjwa ya mlipuko, vita na usimamizi duni wa uchumi. Mwaka 2020, Tanzania ilikuwa ni miongoni mwa nchi zilizoathiriwa na janga la UVIKO – 19 ambapo utalii, usafiri wa anga na biashara za nje ni miongoni mwa sekta zilizoathirika na janga hilo na hivyo, kupunguza kasi ya ukuaji wa uchumi. Hivyo, mafanikio ya Tanzania kupanda hadhi yanaweza kuathiriwa na sababu zilizo nje ya uwezo wa Serikali na kwa ujumla inahitajika mikakati madhubuti ya kuweza kustahimili changamoto zozote ili kuliwezesha Taifa kuendelea kubaki katika hadhi ya kipato cha kati cha chini.

243. Katika kuhakikisha Taifa linaendelea kubaki katika tabaka la nchi ya pato la kati la chini na ikiwezekana kupanda zaidi, Serikali itaendelea kuzingatia masuala makuu matatu. Masuala hayo ni: kuimarisha viashiria vya uchumi mpana na kuhakikisha ukuaji endelevu wa uchumi; kuhakikikisha ukuaji wa uchumi unakuwa shirikishi ili kupunguza umaskini; na kujenga na kuimarisha tabaka la watu wa pato la kati kwa kuendeleza rasilimali watu na uboreshaji wa huduma muhimu za msingi.

244. **Katika kuimarisha viashiria vya uchumi mpana na kujenga ukuaji endelevu wa uchumi,** Serikali itahakikisha kuwa inaendelea: kuzingatia uwepo wa deni la taifa himilivu; kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani na kupanua wigo wa mapato ili kutosheleza mahitaji ya kibajeti; kuongeza nidhamu ya matumizi katika utekelezaji wa bajeti ya Serikali; kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji; kuimarisha uzalishaji viwandani ili kuongeza mauzo nje; na kuongeza tija katika sekta za uzalishaji ikiwemo kufanya mageuzi ya kilimo kuwa cha kisasa na kibiashara.

245. **Katika kujenga uchumi shirikishi,** Serikali itaendelea kuweka mikakati mbalimbali katika kuhakikisha wananchi wanafaidi matunda ya kukua kwa uchumi. Lengo ni kuhakikisha kuwa tofauti ya kipato inapungua kutoka kiwango cha sasa cha fahirisi ya 0.38 na kuongeza kasi ya kupungua kwa kiwango cha umaskini. Mikakati hiyo ni pamoja na azma ya Serikali ya kujenga uchumi wa viwanda vitakavyotumia rasilimali (malighafi na watu) zinazopatikana kwa wingi hapa nchini, kuwekeza kwa katika rasilimali watu (ufundi, ujuzi, na ubunifu), kuimarisha miundombinu ya masoko; kuendelea kuwekeza katika ujenzi wa miundombinu wezeshi, kuendelea kuimarisha ubora na upatikanaji wa huduma za jamii (elimu, afya, maji, umeme vijijini) na kuendelea kugharamia miradi ya maendeleo itakayotoa fursa za ajira kwa watanzania wengi.

246. **Uendelezaji wa rasilimali watu** kupitia uwekezaji katika elimu, afya na ujuzi ni muhimu ili kuhakikisha kuwa Taifa linakuwa na tabaka la watu wengi wa kipato cha kati wenye ujuzi na maarifa ya kuweza kutumia ipasavyo fursa za kiuchumi zinazojitokeza zikiwemo kujiari na fursa za ajira zenye staha. Mikakati ya Serikali katika eneo hili inalenga kuendeleza maarifa na ujuzi wa rasimali watu nchini, kuanzia ngazi za elimu ya awali hadi elimu ya juu ikiwemo kuwawezesha vijana kujiajiri. Vile vile, eneo hili linajumuisha hatua za kuboresha viwango vya utoaji wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi pamoja na ujuzi adimu kwa lengo la kuongeza tija na ushindani wa wananchi katika kutumia rasimali zilizopo nchini ili kuleta maendeleo. Eneo hili pia litahusu upatikanaji wa huduma muhimu za kifedha ili kuiwezesha jamii kutumia kikamilifu fursa za kiuchumi zinazoweza kujitokeza kuwekeza na hivyo kuepusha kutumbukia katika umaskini. Kwa ujumla, kufanikiwa kwa mikakati hii kunategemea utekelezaji wa sera mbalimbali za uchumi na ushiriki wa sekta binafsi, jambo ambalo litaendelea kutiliwa mkazo na Serikali.

**Hitimisho**

247. Tanzania imekuwa nchi ya kipato cha chini tangu uhuru na kwa miaka ya hivi karibuni ilikuwa ni moja ya nchi ambazo uchumi wake unakua kwa kasi barani Afrika. Kutokana na mwenendo mzuri wa uchumi, Tanzania ilifanikiwa kuingia kwenye kundi la nchi za kipato cha kati cha chini ikiwa na wastani wa pato kwa mtu wa dola za Marekani 1,080 mwaka 2019 ikiwa imevuka ukomo uliowekwa wa dola za Marekani 1,036. Mafanikio ya Tanzania kuvuka kutoka hadhi ya nchi ya uchumi wa pato la chini na kufikia nchi ya uchumi wa pato la kati la chini ni hatua muhimu ambayo ina fursa na changamoto zinazoambatana na hadhi hiyo. Miongoni mwa fursa za kuwa nchi ya hadhi ya uchumi wa kati ni pamoja na kuongezeka kwa wigo wa upatikanaji wa fedha za mikopo ya kibiashara kwa ajili ya miradi ya maendeleo; uhuru wa kupanga matumizi; kuchochea uwekezaji nchini; na kuaminika katika taasisi za kifedha za kimataifa.Aidha, changamoto za Nchi kuwa na hadhi ya uchumi wa pato la kati ni pamoja na: kupungua upatikanaji wa misaada na mikopo nafuu; kuondolewa katika

kundi la nchi zinazopata upendeleo wa misaada kupitia mifuko mbalimbali; gharama kubwa za kugharamia mikopo ya kibiashara; na uwezekano wa kushuka kwa uhimilivu wa deni kutokana na gharama kubwa za madeni.

248. Kupanda hadhi kwa Tanzania bado ni mwanzo wa hatua za mafanikio na kwa vile kiwango cha pato kwa mtu kipo karibu kabisa na kiwango cha ukomo, ipo haja ya kuongeza juhudi za kuimarisha viashiria vya uchumi jumla na kujenga uchumi shirikishi ili kuepuka kushuka hadhi kama ilivyowahi kutokea kwa mataifa mengine. Kwa mantiki hiyo, hatua muhimu zitakazochukuliwa na Serikali ili kuliwezesha Taifa kuendelea kubaki katika hadhi ya uchumi wa kati ni pamoja na: kuendelea kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani na kupanua wigo wa mapato ili kutosheleza mahitaji ya kibajeti; kuhakikisha kuwa deni la taifa linaendelea kuwa himilivu; kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara ikiwemo ujenzi wa miundombinu wezeshi ili kuvutia uwekezaji wa ndani na nje; kujenga uchumi shindani wa viwanda na kukuza mauzo ya nje; kujenga na kuimarisha tabaka la watu wa kipato cha kati kwa kuendeleza rasilimali watu (ufundi, ujuzi, na ubunifu); na kuendelea kuimarisha ubora na upatikanaji wa huduma za jamii (elimu, afya, maji, umeme vijijini).



# SEHEMU YA NNE

## MAENDELEO YA SEKTA MBALIMBALI

# SURA YA 11

# KILIMO NA USHIRIKA

## Uzalishaji wa Mazao ya Kilimo

### Mazao ya Chakula

249. Mwaka 2020, uzalishaji wa mazao makuu ya chakula ulikuwa tani 18,196,733 ikilinganishwa na tani 16,293,637 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 11.7. Kati ya kiasi hicho, tani 10,869,596 zilikuwa za mazao ya nafaka na tani 7,327,137 mazao yasiyo ya nafaka. Ongezeko la uzalishaji lilichangiwa na: matumizi ya teknolojia na pembejeo bora katika uzalishaji; kuwepo kwa hali nzuri ya hewa katika maeneo ya uzalishaji; kufutwa kwa baadhi ya kodi, tozo na ada kulikovutia uwekezaji katika shughuli za uzalishaji wa mazao ya kilimo; kuimarika kwa usimamizi wa mazao baada ya kuvuna; na kuimarika kwa huduma za ugani. Aidha, uzalishaji wa mtama, uwele, ulezi na muhogo ulipungua kutokana na uwepo wa mvua nyingi katika maeneo ya uzalishaji.

**Jedwali Na 11.1 Mwenendo wa Uzalishaji wa Mazao ya Chakula (Tani `000) Mwaka 2015-2020**

| Mazao ya Chakula | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mahindi | 5,908 | 6,149 | 6,681 | 6,273 | 5,652 | 6,711 | **18.7** |
| Mchele | 1,937 | 2,229 | 1,594 | 2,220 | 2,063 | 3,038 | **47.3** |
| Ngano | 72 | 76 | 50 | 57 | 63 | 77 | **22.2** |
| Mtama, uwele na ulezi | 1,007 | 1,003 | 1,064 | 988 | 1,117 | 1,043 | **-6.6** |
| Muhogo(mkavu) | 1,962 | 2,205 | 1,342 | 2,791 | 2,728 | 2,427 | **-11.0** |
| Maharage na mikunde | 1,808 | 1,959 | 2,318 | 1,823 | 1,888 | 1,895 | **0.4** |
| Ndizi (kavu) | 1,195 | 1,061 | 845 | 1,132 | 1,135 | 1,358 | **19.6** |
| Viazi (Vitamu na mviringo) (kavu) | 1,645 | 1,491 | 2,008 | 1,608 | 1,644 | 1,647 | **0.1** |
| **Jumla** | **15,534** | **16,173** | **15,902** | **16,892** | **16,290** | **18,197** | **11.7** |

**Chanzo:** Wizara ya Kilimo

250. Mwaka 2020, mahitaji ya chakula yalikuwa tani 14,404,171 (mazao ya nafaka tani 9,191,116 na yasiyo ya nafaka tani 5,213,055) ikilinganishwa na mahitaji ya tani 13,819,863 (mazao ya nafaka tani 8,730,677 na yasiyo ya nafaka tani 5,089,186) mwaka 2019. Mahitaji hayo yakilinganishwa na uzalishaji yalionesha nchi ilikuwa na ziada ya tani 3,792,562 za chakula na hivyo, kiwango cha utoshelevu wa chakula kilikuwa asilimia 126 ikilinganishwa na asilimia 118 mwaka 2019.

### Mazao ya Biashara

251. Mwaka 2020, uzalishaji wa mazao makuu ya biashara ulipungua kwa asilimia 7.5 na kufikia tani 1,058,798 ikilinganishwa na tani 1,144,631 mwaka 2019. Upungufu

huo ulitokana na mvua zilizozidi wastani katika maeneo ya uzalishaji na mlipuko wa wadudu na magonjwa ya mazao. Aidha, uzalishaji wa mazao ya pareto na mkonge uliongezeka kwa asilimia 24.6 na asilimia 9.3 mtawalia. Ongezeko hilo lilitokana na uwepo wa hali nzuri ya hewa kwa mazao husika. Kwa upande mwingine, uzalishaji wa mazao ya tumbaku na chai ulipungua kwa asilimia 47.0 na asilimia 22.8 mtawalia. Upungufu huo ulitokana na: mvua zilizozidi wastani zilizoathiri uzalishaji na ubora wa tumbaku na kupungua kwa mahitaji katika soko la dunia; na kuanguka kwa barafu katika ukanda wa nyanda za juu kusini zilizoathiri uzalishaji wa chai.

**Jedwali Na 11.2: Mwenendo wa Uzalishaji wa Mazao ya Biashara (Tani) Mwaka 2017-2020**

| Zao | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|
| Pamba | 132,934 | 222,039 | 348,910 | 348,958 | 0.01 |
| Kahawa | 48,329 | 45,245 | 68,147 | 60,651 | -11.0 |
| Chai | 26,975 | 34,010 | 37,193 | 28,715 | -22.8 |
| Pareto | 2,150 | 2,400 | 2,014 | 2,510 | 24.6 |
| Tumbaku | 58,639 | 50,522 | 70,824 | 37,546 | -47.0 |
| Korosho | 265,238 | 313,826 | 225,053 | 232,681 | 3.4 |
| Mkonge | 36,533 | 40,635 | 33,271 | 36,379 | 9.3 |
| Sukari | 330,843 | 303,752 | 359,219 | 311,357.61 | -13.3 |
| **Jumla** | **901,641** | **1,012,429** | **1,144,631** | **1,058,798** | **-7.5** |

**Chanzo:** Wizara ya Kilimo

## Mazao ya Bustani

252. Uzalishaji wa mazao ya bustani ulikuwa tani 7,560,010 mwaka 2020 ikilinganishwa na tani 6,597,863.2 mwaka 2019 sawa na ongezeko la asilimia 14.6. Aidha, uzalishaji wa viungo na matunda uliongezeka kwa asilimia 53 na 22 mtawalia. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa uhitaji wa viungo pamoja na matunda ambayo hutumika katika mapishi na tiba mbadala hususan katika kukabiliana na athari za mlipuko wa UVIKO-19. Kwa upande mwingine, uzalishaji wa maua ulishuka kwa asilimia 87.1. Upungufu huo ulitokana na kushuka kwa uhitaji wa maua kwenye soko la dunia kulikosababishwa na athari za UVIKO-19.

**Jedwali Na 11.3: Uzalishaji wa Mazao ya Bustani (Tani) Mwaka 2017-2020**

| Zao | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|
| Matunda | 5,243,343 | 3,703,124 | 4,576,948 | 5,582,117 | 22 |
| Mboga | 1,298,388 | 1,595,489 | 1,926,927 | 1,852,676 | -3.8 |
| Maua | 11,615 | 12,622 | 13,240 | 1,710 | -87.1 |
| Viungo | 22,062 | 22,062 | 80,748 | 123,508 | 53 |
| **Jumla** | **6,575,408** | **5,333,297** | **6,597,863** | **7,560,010** | **14.6** |

**Chanzo:** Wizara ya Kilimo

## Mazao ya Mbegu za mafuta

253. Uzalishaji wa mazao ya mbegu za mafuta uliongezeka kwa asilimia 28.7 na kufikia tani 1,583,669.28 mwaka 2020 ikilinganishwa na tani 1,230,767 mwaka 2019.

Ongezeko hilo lilitokana na matumizi ya kanuni bora za kilimo, hali nzuri ya hewa katika maeneo ya uzalishaji pamoja na kuongezeka kwa mahitaji ya mafuta nchini.

**Jedwali Na 11.4 Uzalishaji wa Mbegu za Mafuta (Tani) Mwaka 2017-2020**

| Zao | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|
| Alizeti | 352,902 | 543,261 | 561,297 | 649,437.3 | 15.7 |
| Karanga | 216,167 | 370,356 | 376,520 | 631,465.3 | 67.7 |
| Ufuta | 56,846 | 133,704 | 227,821 | 228,919.8 | 0.5 |
| Mawese | 42,277 | 40,500 | 42,176 | 42,386.9 | 0.5 |
| Soya | 6,135 | 21,321 | 22,953 | 31,460 | 37.1 |
| **Jumla** | **674,327** | **1,109,142** | **1,230,767** | **1,583,669.3** | **28.7** |

**Chanzo:** Wizara ya Kilimo

### Upatikanaji wa Pembejeo za Kilimo

254. Mwaka 2020, upatikanaji wa mbolea ulifikia tani 633,197 ikilinganishwa na tani 492,394 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 28.6. Ongezeko hilo lilitokana na matumizi ya Mfumo wa Ununuzi wa Mbolea wa Pamoja uliowezesha bei ya mbolea kwa mkulima kupungua kwa kati ya asilimia 6 hadi asilimia 17 kulingana na eneo husika. Aidha, Serikali kupitia Wakala wa Mbolea ilifanya ukaguzi wa usajili, leseni, uingizaji wa mbolea, biashara, utunzaji wa mbolea na matumizi ya bei elekezi kwa wafanyabiashara 1,148. Vile vile, Wakala ulisajili wafanyabiashara wa mbolea 387 na kuhuisha usajili wa wafanyabiashara 533 na hivyo, kuwa na jumla ya wafanyabiashara wa mbolea 920 mwaka 2020.

255. Mwaka 2020, Mfuko wa Pembejeo ulitoa mikopo 48 yenye thamani ya shilingi milioni 2,128.4 ikilinganishwa na mikopo 44 yenye thamani ya shilingi milioni 2,283.0 mwaka 2019. Mikopo hiyo ilinufaisha wakulima 175 ikilinganishwa na wakulima 158 walionufaika mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 10.8. Mikopo hiyo ilijumuisha: mikopo 20 ya matrekta; mikopo ya fedha za uendeshaji (9); pembejeo za kilimo (8); miundombinu ya kilimo, mifugo na uvuvi (6); mitambo ya mashambani (2); matrekta ya mikono (1); ukarabati wa matrekta (1); na mashine za kusindika na vifungashio (1).

256. Mwaka 2020, uzalishaji wa mbegu bora za nafaka, mikunde na mazao ya mafuta ulikuwa tani 69,173.2 ikilinganishwa na tani 38,507.9 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 79.6. Hii ilitokana na kuongezeka kwa eneo la uzalishaji wa mbegu kutoka hekta 10,887 hadi hekta 94,365 na kufutwa kwa ada na tozo 12 zinazohusu uzalishaji wa mbegu bora. Aidha, Serikali imeendelea kuimarisha maabara ya Taasisi ya Udhibiti wa Mbegu Bora Tanzania ambapo ilipata ithibati ya Shirika la Kimataifa la Uthibiti wa Ubora wa Mbegu na kujiunga katika Skimu za Mbegu za Shirika la Kimataifa. Hatua hizo ziliwezesha uuzaji wa mbegu za mahindi jumla ya tani 756 katika nchi za Kenya na Burundi mwaka 2020.

**Mwenendo wa Bei na Masoko ya Mazao**

257. Mwaka 2020, Serikali iliendelea kuboresha mifumo ya masoko ya mazao ya kilimo kwa kufanya tafiti za mahitaji ya masoko, kuimarisha vyama vya ushirika na kusimamia mifumo mbalimbali ya masoko ya mazao ikiwemo Tigo Kilimo, G-Soko na kukamilisha mfumo wa M-Kilimo kwa lengo la kuwezesha wakulima kupata taarifa mbalimbali za masuala ya kilimo kwa wakati. Kufuatia jitihada hizo, bei za mazao ya kilimo ziliimarika katika soko la ndani mwaka 2020 ikilinganishwa na bei za mwaka 2019 kama ifuatvyo: bei ya kakao kutoka shilingi 4,800 kwa kilo hadi shilingi 5,000 kwa kilo; bei ya mkonge daraja UG (Under Grade) iliongezeka kutoka shilingi milioni 3.5 kwa tani hadi shilingi milioni 3.6 kwa tani. Aidha, bei ya kahawa aina ya Arabika kwa gunia la kilo 50 katika soko la ndani ilikuwa dola za Marekani 112.0 ikilinganishwa na dola 107.04 katika soko la dunia. Vile vile, bei ya kahawa aina ya Robusta kwa gunia la kilo 50 katika soko la ndani ilikuwa dola za Marekani 87.13 ikilinganishwa na dola 73.90 katika soko la dunia.

**Huduma za Ugani**

258. Mwaka 2020, Serikali imeendelea kuimarisha huduma za ugani kwa kuanzisha mfumo wa M-Kilimo ambapo jumla ya maafisa Ugani 1,344 na wakulima 20,318 walisajiliwa. Kati ya hao maafisa ugani 1,085 na wakulima 5,141 kutoka mikoa ya Dodoma, Tanga, Iringa, Arusha, Morogoro na Mara walipata mafunzo ya kutumia mfumo huo. Mfumo huo uliwezesha wakulima kupata taarifa sahihi na kwa wakati kuhusiana na masoko na namna ya kuongeza tija katika shughuli za kilimo.

259. Mwaka 2020, Serikali kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Kituo cha Usambazaji wa Teknolojia (Nyakabindi AgriTecH) ilitoa mafunzo kupitia vituo vyake 11 kwa wakulima 34,229 na maafisa ugani 895 kuhusu teknolojia bora za kilimo. Vile vile, katika kuhamasisha matumizi ya teknolojia na ubunifu, Taasisi iliwasilisha matokeo ya tafiti mbalimbali kupitia vipindi 269 vya luninga na radio, machapisho 140, makala 54 na hadithi 17 za mafanikio ya teknolojia zilizofanyiwa utafiti kupitia mitandao ya kijamii.

**Utafiti**

260. Mwaka 2020, Serikali kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo - TARI iligundua na kuzalisha aina 20 za mbegu bora za mazao zenye ukinzani dhidi ya magugu na magonjwa ikilinganishwa na mbegu 22 mwaka 2019. Mbegu hizo zinajumuisha mtama (2), Migomba (4), viazi vitamu (2), miwa (6) na maharage (6). Aidha, mbegu mama kilogramu 930, mbegu za msingi kilogramu 9,870 na mbegu za awali Kilogramu 329 za mazao ya nafaka na mbegu za mafuta zilizalishwa mwaka 2020. Katika kipindi hicho, Taasisi ilizalisha na kusambaza: miche 2,672,000 ya mkonge, michikichi (3,748,425), miembe (300), parachichi (4,482), mizabibu (4,710), minazi (5,000), mipapai (5,000); vipando vya mihogo 388,436, viazi vitamu (926,000), miwa (46,000), pareto (8,986); na

vikonyo vya mihogo 24,089. Kwa upande mwingine, Taasisi ya Utafiti wa Kahawa ilizalisha na kusambaza miche bora ya kahawa 10,367,548 ikilinganishwa na miche 7,284,735 mwaka 2019.

**Mafunzo ya Kilimo**

261. Mwaka 2020, Serikali kupitia vyuo 14 vya kilimo ilidahili wanafunzi 2,788 ikilinganishwa na wanafunzi 2,856 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 2.4. Kati ya wanafunzi hao, wanafunzi 2,491 walifadhiliwa na Serikali na wanafunzi 297 walijigharamia wenyewe mwaka 2020 ikilinganishwa na wanafunzi 2,359 waliofadhiliwa na Serikali na wanafunzi 497 waliojigharamia mwaka 2019.

262. Mwaka 2020, Serikali ilifadhili watumishi 12 wa shahada ya uzamili na watumishi sita (6) wa shahada ya kwanza ikilinganishwa na watumishi 19 wa shahada ya uzamili na watumishi wanne (4) wa shahada ya kwanza mwaka 2019 kwa lengo la kuongeza ufanisi katika ufundishaji Aidha, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Kilimo Endelevu Tanzania - SAT na Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania -TPSF ilihuisha mitaala sita (6) ya mafunzo ya kilimo ili kuendana na mahitaji ya soko la ajira na mabadiliko ya teknolojia. Mitaala hiyo inayohusu kilimo cha maua na mboga mboga (*Horticulture)*, usanifu wa kilimo (*Agromechanization)*, ufundi sanifu wa mitambo ya umwagiliaji (*irrigation engineering)*, mipango na usimamizi wa matumizi bora ya ardhi ya kilimo (*Agricultural Land Use Planning and Management)*, kilimo cha mazao (*Crop Production),* Technolojia ya chakula na Lishe (*Food Technology and Human Nutrition*)

**Umwagiliaji**

263. Mwaka 2020, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji iliongeza eneo la umwagiliaji na kufikia hekta 694,715 kutoka hekta 561,383 mwaka 2019. Aidha, Serikali ilikamilisha ujenzi na ukarabati wa skimu 15 za umwagiliaji nchini ikilinganishwa na jumla ya skimu sita (6) zilizokamilishwa mwaka 2019. Hadi Desemba 2020, idadi ya vyama vya umwagiliaji vilivyosajiliwa na Tume iliongezeka na kufikia vyama 196 ikilinganishwa na vyama 169 kipindi kama hicho mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 16.0. Ongezeko lilichangiwa na kuhamasika kwa wakulima kujiunga au kuanzisha vyama vya umwagiliaji.

## MIFUGO

**Uzalishaji wa Mifugo na Mazao yake**

264. Mwaka 2020, idadi ya mifugo nchini ilikadiriwa kuwa ng’ombe milioni 33.9, mbuzi milioni 24.1, kondoo milioni 8.5, nguruwe milioni 3.2 na kuku milioni 87.7 ikilinganishwa na ng’ombe milioni 32.2, mbuzi milioni 20.0, kondoo milioni 5.5, nguruwe milioni 2.0 na kuku milioni 79.1 mwaka 2019. Aidha, uzalishaji wa maziwa ulikuwa lita milioni 3,100.1 ikilinganishwa lita milioni 2,678.4 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 15.7. Kati ya kiasi kilichozalishwa, lita milioni 969.7 zilitokana na ng’ombe wa kisasa na lita milioni 2,130.4 zilitokana na ng’ombe wa asili. Kuongezeka

kwa uzalishaji wa maziwa kulitokana na kuendelea na uboreshaji wa mbari za mifugo kupitia uhimilishaji. Kwa upande mwingine, usindikaji wa maziwa ulifikia lita milioni 74.3 katika viwanda 91 vilivyokuwa vinafanya kazi mwaka 2020 ikilinganishwa na lita milioni 63.6 zilizosindikwa katika viwanda 90 mwaka 2019.

265. Mwaka 2020, uzalishaji wa nyama ulikuwa tani 701,679.0 ikilinganishwa na tani 681,501 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 3.0. Hii ilitokana na kuendelea kudhibiti utoroshaji wa mifugo na mazao yake pamoja na kuongezeka kwa idadi ya mifugo na mahitaji ya nyama. Kati ya nyama zilizozalishwa: tani 486,736.1 zilikuwa nyama ya ng'ombe, tani 95,964.2 mbuzi na kondoo, tani 80,601.3 kuku na tani 38,377.4 nguruwe ikilinganishwa na tani 506,798 za nyama ya ng'ombe, tani 110,563 mbuzi na kondoo, tani 41,000 kuku na tani 23,140 nguruwe mwaka 2019. Aidha, jumla ya mayai milioni 4,051.2 yalizalishwa mwaka 2020 ikilinganishwa na mayai milioni 3,575.6 yaliyozalishwa mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 13.3. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mahitaji sambamba na vituo vya kutotolesha vifaranga vya kuku.

**Jedwali Na. 11.5: Uzalishaji wa Mazao Yanayotokana na Mifugo Mwaka 2015-2020**

| Aina ya zao | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Uzalishaji Maziwa (Lita 000)** | | | | | | |
| Ng'ombe wa Asili | 1,381,451 | 1,423,288 | 1,490,000 | 1,608,099 | 1,874,923 | 2,130,408 |
| Ng'ombe wa kisasa | 677,275 | 703,979 | 626,100 | 792,044 | 803,538 | 969,666 |
| **jumla** | **2,058,726** | **2,217,267** | **2,116,100** | **2,400,134** | **2,678,461** | **3,100,074** |
| **Uzalishaji Nyama (Tani)** | | | | | | |
| Ng'ombe | 319,112 | 323,775 | 394,604 | 471,692 | 506,798 | 486,736 |
| Mbuzi na kondoo | 124,745 | 129,292 | 81,064 | 92,999 | 110,563 | 95,964 |
| Nguruwe | 54,360 | 91,451 | 18,899 | 37,191 | 23,140 | 38,377 |
| Kuku | 99,540 | 104,292 | 63,597 | 78,110 | 41,000 | 80,601 |
| **Jumla** | **597,757** | **648,810** | **558,164** | **679,992** | **681,501** | **701,679** |
| **Uzalishaji mayai (000)** | | | | | | |
| Mayai | 4,153,800 | 4,353,182 | 2,758,000 | 3,156,692 | 3,575,621 | 4,051,179 |

**Chanzo:** Wizara ya Mifugo na Uvuvi

### Uzalishaji wa Malisho na Utengenezaji wa Vyakula vya Mifugo

266. Mwaka 2020, uzalishaji wa mbegu bora za malisho ya mifugo katika mashamba ya Serikali ulikuwa tani 127.3 ikilinganishwa na tani 12.1 mwaka 2019. Ongezeko hilo lilitokana na Serikali kuendelea kuboresha mashamba ya malisho kwa kuyapatia vitendea kazi ikiwemo matrekta na *harrow* pamoja na uwepo wa mvua za kutosha katika misimu ya vuli na masika uliowezesha kuongezeka kwa uzalishaji wa vipandikizi. Katika kipindi hicho, uzalishaji wa hei katika mashamba ya Serikali ulikuwa marobota 326,655 ikilinganishwa na marobota 550,919 mwaka 2019, sawa na

upungufu wa asilimia 40.7. Upungufu huo ulichangiwa na kuwepo kwa mvua nyingi za vuli na masika zilizoathiri uvunaji wa majani yanayotumika kutengeneza hei. Kwa upande wa sekta binafsi, tani 900,000 za vyakula vya mifugo zilizalishwa mwaka 2020 ikilinganishwa na tani 600,120 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 50.0. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa vifaranga vya kuku wa mayai na nyama kufuatia kuongezeka kwa mahitaji ya nyama na mayai katika soko.

267. Mwaka 2020, viwanda vya kutengeneza vyakula vya mifugo vilifikia 105 ikilinganishwa na viwanda 94 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 11.7. Ongezeko hilo lilitokana na uhamasishaji uliofanywa na Serikali kwa wananchi kuhusu fursa za uwekezaji katika sekta ya viwanda. Katika kuhakikisha upatikanaji wa vyakula vya mifugo vyenye ubora na viwango stahiki, Serikali ilifanya kaguzi katika maeneo 11 ya kuzalisha vyakula na maeneo matano (5) ya kuhifadhi vyakula mwaka 2020 ikilinganishwa na maeneo 20 ya kuzalisha vyakula na maeneo 14 ya kuhifadhia chakula mwaka 2019. Kadhalika, maeneo 36 ya kuuzia vyakula vya mifugo yalifanyiwa ukaguzi. Kufuatia kaguzi hizo, wadau 36 (Dar es salaam 8, Arusha 12, Kilimanjaro 3, Pwani 3, Mwanza 9 na Iringa mmoja) walipata vyeti vya usajili wa kuuza vyakula vya mifugo baada ya kukidhi vigezo.

**Biashara ya Mifugo na Mazao yake**

268. Mwaka 2020, ng’ombe 1,023,200, mbuzi 987,867 na kondoo 205,161 wenye jumla ya thamani ya shilingi bilioni 865 waliuzwa katika soko la ndani ikilinganishwa na ng’ombe 1,427,212, mbuzi 1,062,324, na kondoo 122,390 wenye thamani ya shilingi bilioni 947.4 mwaka 2019, sawa na kushuka kwa thamani ya mauzo kwa asilimia 8.7. Hii ilitokana na mvua nyingi iliyosababisha uharibifu wa miundombinu ya barabara na minada ya awali katika kipindi hicho. Aidha, idadi ya mifugo hai iliyouzwa nje ya nchi ilifikia ng’ombe 3,574, mbuzi na kondoo 49,184 wenye thamani ya shilingi bilioni 1.9 mwaka 2020 ikilinganishwa na ng’ombe 11,670, mbuzi na kondoo 44,790 wenye thamani ya shilingi bilioni 22.9 mwaka 2019, sawa na kushuka kwa thamani ya mauzo kwa asilimia 91.7. Kupungua kwa thamani ya mauzo nje ya nchi kulitokana na athari za janga la UVIKO-19 na hivyo kuathiri shughuli za minada mipakani.

269. Mwaka 2020, jumla ya tani 692.4 za nyama zenye thamani ya shilingi bilioni 2.99 (dola za Marekani milioni 1.3) ziliuzwa nje katika nchi za Dubai, Iraq, Omani, Comoro, Hongkong na Vietnam ikilinganishwa na tani 1,207.9 zenye thamani ya shilingi bilioni 5.2 mwaka 2019. Kati ya tani za nyama zilizouzwa nje ya nchi, nyama ya ng’ombe ilikuwa tani 142.2, mbuzi tani 36.1, kondoo tani 1.1 na punda tani 513. Aidha, jumla ya tani 243.7 za nyama zenye thamani ya shilingi bilioni 4.1 (Dola za Marekani milioni 1.8) ziliingizwa nchini kutoka Kenya, Afrika Kusini, Ubelgiji na Uingereza ikilinganishwa na tani 516.6 zenye thamani ya shilingi bilioni 5.0 (Dola za

Marekani Milioni 2.2) zilizoingizwa nchini mwaka 2019. Kati ya nyama zilizoagizwa kutoka nje, nyama ya ng'ombe ilikuwa tani 195.1 na nguruwe tani 48.5

270. Mwaka 2020, ukusanyaji wa ngozi ulikuwa vipande 10,492,156 ikilinganishwa na vipande 10,435,355 mwaka 2019. Kati ya hivyo, vipande 3,022,995 vilikuwa vya ngozi ya ng'ombe na vipande 7,469,160 vya ngozi ya mbuzi na kondoo ikilinganishwa na vipande 3,010,224 vya ngozi ya ng'ombe na vipande 7,425,131 vya ngozi ya kondoo na mbuzi. Aidha, jumla ya vipande 677,867 vya ngozi za ng'ombe, mbuzi na kondoo viliuzwa nje ya nchi ikilinganishwa na vipande 665,177 mwaka 2019. Katika kipindi hicho, tani 2,929.2 za ngozi ghafi na tani 102.7 za ngozi zilizosindikwa kwa kiwango cha kati ziliuzwa nje ikilinganishwa na tani 2,871.2 za ngozi ghafi na tani 156.0 za ngozi zilizosindikwa kwa kiwango cha kati mwaka 2019. Upungufu wa mauzo nje ya ngozi zilizosindikwa ulitokana na wasindikaji wa ndani kuwa katika kipindi cha mpito cha kubadilisha teknolojia ya usindikaji kwa kutumia kemikali aina ya chrome na kuanza kutumia mimea aina ya mimosa (vegetable tanning) inayoendana na viwango vinavyokubalika katika soko la Ulaya.

**Jedwali Na. 11.6: Ukusanyaji wa Vipande vya Ngozi**

| Mwaka | Ngozi za Ng'ombe | Ngozi za mbuzi na kondoo | Jumla |
|---|---|---|---|
| 2009 | 1,223,668 | 6,983,999 | 8,207,667 |
| 2010 | 2,456,540 | 3,678,294 | 6,134,834 |
| 2011 | 2,378,235 | 4,978,000 | 7,356,235 |
| 2012 | 3,022,400 | 4,928,000 | 7,950,400 |
| 2013 | 2,567,340 | 6,325,525 | 8,892,865 |
| 2014 | 2,263,472 | 3,567,321 | 5,830,793 |
| 2015 | 2,543,914 | 5,983,210 | 8,527,124 |
| 2016 | 2,654,400 | 6,132,212 | 8,786,612 |
| 2017 | 2,790,560 | 6,643,998 | 9,434,558 |
| 2018 | 2,896,796 | 7,022,908 | 9,919,704 |
| 2019 | 3,010,224 | 7,425,131 | 10,435,355 |
| 2020 | 3,022,995 | 7,469,160 | 10,492,155 |

**Chanzo:** Wizara ya Mifugo na Uvuvi

**Jedwali Na. 11.7: Uuzaji wa Vipande vya Ngozi Nje ya Nchi**

| Mwaka | Ngozi za Ng'ombe | Ngozi za Mbuzi na Kondoo | Jumla |
|---|---|---|---|
| 2009 | 982,668 | 3,469,936 | 4,452,604 |
| 2010 | 739,315 | 2,088,582 | 2,827,897 |
| 2011 | 1,719,506 | 1,561,000 | 3,280,506 |
| 2012 | 2,000,000 | 3,600,000 | 5,600,000 |
| 2013 | 1,269,060 | 2,582,525 | 3,851,585 |
| 2014 | 1,263,472 | 2,716,436 | 3,979,908 |
| 2015 | 1,388,139 | 1,020,000 | 2,408,139 |
| 2016 | 1,575,139 | 1,124,000 | 2,699,139 |
| 2017 | 1,215,030 | 928,115 | 2,143,145 |
| 2018 | 828,079 | 1,009,202 | 1,837,281 |
| 2019 | 614,743 | 50,434 | 665,177 |
| 2020 | 629,202 | 48,665 | 677,867 |

**Chanzo:** Wizara ya Mifugo na Uvuvi

**Jedwali Na. 11.8: Mwenendo wa Mauzo ya Ngozi Nje ya Nchi**

| Mwaka | Ngozi ghafi | | Ngozi zilizosindikwa | | Jumla thamani (Ngozi ghafi na zilisindikwa) (Shilingi Milioni) |
|---|---|---|---|---|---|
| | Kiasi Kg (000) | Thamani Shilingi milioni | Kiasi (000) | Thamani (Shilingi Milioni) | |
| 2009 | 1,666 | 1,433 | 5,026 | 6,797 | 8,230 |
| 2010 | 3,241 | 2,438 | 7,217 | 8,672 | 11,110 |
| 2011 | 8,141 | 6,831 | 7,904 | 17,005 | 23,836 |
| 2012 | 2,887 | 3,445 | 5,011 | 17,375 | 20,820 |
| 2013 | 2 | 3 | 7,061 | 22,686 | 22,689 |
| 2014 | 1,559 | 2,231 | 11,186 | 33,372 | 35,603 |
| 2015 | 372 | 1,185 | 6,594 | 20,878 | 22,063 |
| 2016 | 1,758 | 2,397 | 2,592 | 5,097 | 7,494 |
| 2017 | 4,835 | 6,592 | 6,482 | 9,452 | 16,044 |
| 2018 | 3,650 | 5,064 | 4,840 | 8,794 | 13,858 |
| 2019 | 2,871.20 | 4,971.40 | 156 | 230 | 5,201.4 |
| 2020 | 2,929.20 | 5,029.90 | 102.7 | 197.3 | 5,227.2 |

**Chanzo:** Mamlaka ya Mapato Tanzania

### Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo

271. Mwaka 2020, Serikali kupitia Wakala wa Mafunzo ya Mifugo - LITA ilidahili wanafunzi 3,574 katika ngazi ya astashahada na stashahada ikilinganishwa na wanafunzi 3,634 mwaka 2019. Mafunzo yaliyotolewa kwa wanafunzi yalijumuisha fani za afya na uzalishaji mifugo, ufundi sanifu wa maabara ya vetenari na utunzaji wa nyanda za malisho na udhibiti wa ndorobo. Mafunzo hayo yalitolewa katika Kampasi za Morogoro, Tengeru (Arusha), Mpwapwa (Dodoma), Kikulula (Kagera), Madaba

(Songea), Mabuki (Mwanza), Temeke (Dar es Salaam) na Buhuri (Tanga). Aidha, Wakala ulitoa mafunzo kwa wafugaji 2,078 kuhusu mbinu bora za uzalishaji mifugo na malisho mwaka 2020 ikilinganishwa na wafugaji 1,468 waliofikiwa mwaka 2019.

**Utafiti wa Mifugo**

272. Mwaka 2020, Serikali kupitia Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania iliendelea na tafiti za uzalishaji wa mifugo zilizowezesha kuzalisha na kusambaza ng'ombe chotara wa nyama 56, ng'ombe chotara wa maziwa 78 na mbuzi chotara 304 kwa wadau wa mifugo ikilinganishwa na ng'ombe chotara wa nyama 93, ng'ombe chotara wa maziwa 48 na mbuzi chotara 134 mwaka 2019. Aidha, vifaranga vya kuku chotara 4,801 aina ya Kuroiler na vifaranga 600 aina ya Sasso vilisambazwa katika halmashauri za Mpwapwa na Meatu mwaka 2020 ikilinganishwa na vifaranga vya kuku chotara 642 aina ya Sasso na 2,412 aina ya Kuroiler viliosambazwa katika Halmashauri ya Mpwapwa mwaka 2019. Vile vile, mayai 240 ya kuku chotara aina ya Sasso na mayai 3,251 ya kuku aina ya kroiler yalirutubishwa na kusambazwa kwa wafugaji katika Halmashauri ya Mpwapwa mwaka 2020 ikilinganishwa na mayai 359 ya kuku aina ya sasso na mayai 720 ya kuku aina ya kroiler yaliyosambazwa mwaka 2019. Katika kipindi hicho, kilogramu 1,041 za mbegu bora za malisho na kilogramu 758.5 za vishina vya malisho zilizalishwa na kusambazwa kwa wafugaji ikilinganishwa na kilogramu 6,029 za mbegu bora za malisho na kilogramu 3,250 za vishina vya malisho zilizalishwa na kusambazwa mwaka 2019.

273. Mwaka 2020, Taasisi ilisindika na kusambaza marobota 21,124 ya malisho makavu ikilinganishwa na marobota 20,748 mwaka 2019. Marobota hayo yalisambazwa katika maeneo ya Mbeya, Rungwe, Misungwi, Sengerema, Tarime, Ilemela, Nyamagana, Dodoma na Tanga. Aidha, wafugaji 11,571 waliopokea teknolojia za mifugo walipatiwa mafunzo na huduma za ushauri wa kitaalam ikilinganishwa na wafugaji 8,350 mwaka 2019. Mafunzo hayo yalifanyika katika mikoa ya; Mbeya, Songwe, Simiyu, Geita, Dodoma, Tanga, Manyara, Arusha, Morogoro, Njombe, Mwanza, Mtwara, Lindi, Iringa, Kilimanjaro na Pwani.

**Huduma za Ugani katika Mifugo**

274. Mwaka 2020, Serikali ilitoa mafunzo kwa maafisa ugani 3,914 ikilinganishwa na wafugaji na maafisa ugani 19,839 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 80.3. Upungufu huo ulitokana na kubadilishwa kwa mfumo wa utoaji mafunzo rejea ambapo mafunzo hayo yalilenga maafisa ugani katika ngazi za wilaya/halmashauri. Mafunzo hayo yalifanyika katika mikoa ya Rukwa kwa wafugaji 1,412, Mbeya (1,201), Songwe (653) na Katavi (648). Mafunzo rejea yalitolewa kwa maafisa ugani washauri wa mikoa 26 na afisa ugani mmoja kwa kila halmashauri 18 za mikoa ya Dodoma (halmashauri 10) na Singida halmashauri nane (8). Mafunzo hayo yalihusu ufugaji bora wa ng'ombe

wa nyama na maziwa, uendelezaji wa nyanda za malisho, udhibiti wa magonjwa ya mifugo na uzalishaji wa malisho.

275. Mwaka 2020, Serikali ilianzisha mashamba darasa 12 ya malisho ya mifugo katika wilaya ya Kishapu (4), Kahama (3), Bahi (3), Bihawana (1) na Nzega (1) ikilinganishwa na mashamba darasa 20 mwaka 2019. Aidha, wafugaji 43 walipata mafunzo kwa vitendo kuhusu kilimo cha malisho kupitia mashamba darasa hayo ikilinganishwa na wafugaji 260 mwaka 2019. Upungufu huo ulisababishwa na changamoto ya baadhi ya mashamba darasa kujaa maji kutokana na mvua nyingi katika kipindi hicho.

**Maendeleo ya Ushirika**

276. Mwaka 2020, Serikali kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika iliendelea kudhibiti, kusimamia na kuhamasisha ushirika katika shughuli za kilimo cha mazao, mifugo na uvuvi ili kuchochea ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini. Katika kipindi hicho, vyama vya ushirika vilipungua na kufikia 9,185 (vyama vya masoko ya mazao 4,039, vyama vya akiba na mikopo 3,831, vyama vya aina nyingine 1,215, vyama vikuu 58 na miradi ya pamoja 42) kutoka vyama 11,626 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 21.0. Upungufu huo ulitokana na baadhi ya vyama kukosa vigezo na kufutwa baada ya uhakiki. Aidha, idadi ya wanachama wa vyama vya ushirika iliongezeka kutoka wanachama 5,880,736 mwaka 2019 na kufikia wanachama 6,050,324 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 2.9. Ongezeko hilo lilitokana na uhamasishwaji wa wananchi kuhusu umuhimu wa kujiunga na ushirika katika kujikomboa kiuchumi ikiwemo ununuzi wa pembejeo kwa pamoja ili kupunguza gharama za uzalishaji.

277. Mwaka 2020, viwanda vya kuchakata mazao vinavyomilikiwa na vyama vya ushirika vilikuwa 452 ikilinganishwa na viwanda 374 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 20.9. Ongezeko hilo lilitokana na kuendelea uhamasishaji wa uanzishwaji wa viwanda nchini unaofanywa na Serikali ikiwa ni pamoja na kutoa motisha za kikodi. Katika kipindi hicho, vyama vya ushirika vilitoa ajira 100,100 ikilinganishwa na ajira 90,090 mwaka 2019. Aidha, mikopo yenye thamani ya shilingi trilioni 1.63 ilitolewa kwa wanachama wa vyama vya ushirika vya akiba na mikopo ikilinganishwa na mikopo yenye thamani ya shilingi trilioni 1.5 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 8.7. Thamani ya hisa na akiba za wanachama ziliongezeka kutoka shilingi bilioni 819 mwaka 2019 hadi shilingi bilioni 891 mwaka 2020.

278. Mwaka 2020, Serikali kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika - TCDC ilikagua vyama vya ushirika 4,494 ikilinganishwa na vyama 2,964 vilivyokaguliwa mwaka 2019. Aidha, vyama 35 vilifanyiwa kaguzi maalumu mwaka 2020 ikilinganishwa na vyama 28 mwaka 2019. Katika kipindi hicho, Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika - COASCO lilikagua hesabu za vyama vya ushirika 6,021 ambapo

vyama 289 vilipata hati inayoridhisha, vyama 3,114 hati yenye shaka, vyama 948 hati isiyoridhisha na vyama 1,670 hati chafu. Kufuatia kaguzi hizo, watendaji wa vyama vya ushirika walipewa mafunzo kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kuandaa hesabu na taarifa za fedha za vyama kwa ufanisi zaidi. Kupitia kaguzi hizo vyama vya ushirika vilivyokuwa na mapungufu vilichukuliwa hatua stahiki kwa lengo la kuboresha utendaji kazi

**UVUVI**

**Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi**

279. Mwaka 2020, Serikali ilifanya ulinzi na usimamizi shirikishi wa rasilimali za uvuvi uliowezesha kukamatwa kwa vifaa na zana zinazotumika kwenye uvuvi haramu zikiwemo; kamba za kokoro zenye urefu wa mita 89,225, nyavu za makila 16,445, ndoano 5,601, nyavu za timba 1,689, kokoro 592, mitumbwi 552, nyavu za dagaa 382, nyavu za mtando 204, injini za boti 201, boti 78, nyavu aina ya gonga 35, kasia 24, vyandarua 22, magari 14, pikipiki 12, viatu vya kuzamia jozi tisa (9), katuli nane (8), nyavu za gizagiza sita (6) na tanki moja (1) la mafuta. Aidha, samaki wachanga kilo 22,977 na mabondo kilo 37 yalikamatwa. Kwa upande mwingine, Kikosi Kazi cha Taifa cha Kudhibiti Vitendo Haramu na Uhalifu wa Kimazingira kiliendelea kufanya ulinzi shirikishi wa rasilimali za uvuvi katika Ukanda wa Pwani na Ziwa Tanganyika mwaka 2020 uliowezesha kukamatwa kwa vifaa na zana zilizotumika katika uvuvi haramu zikiwemo kamba za kokoro zenye urefu wa mita 20,705, nyavu za makila 8,445, nyavu za timba 201, kokoro 105, nyavu za mtando 55, mitumbwi 30, mitungi ya gesi 20, na magari matano (5). Vile vile, watuhumiwa 1,400 walikamatwa na kesi 5 ziliwasilishwa mahakamani.

**Uzalishaji Vifaranga vya Samaki, Samaki na Viumbe Maji**

280. Mwaka 2020, idadi ya vizimba vya kuzalishia samaki katika maziwa na malambo iliongezeka na kufikia 431 kutoka vizimba 408 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 5.6. Kati ya hivyo, vizimba 370 vilikuwa katika Ziwa Victoria, tisa (9) Ziwa Tanganyika na vizimba 115 kwenye malambo mbalimbali. Aidha, idadi ya mabwawa ya kufugia samaki iliongezeka na kufikia 27,979 mwaka 2020 kutoka mabwawa 26,445 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 2.4. Hii ilitokana na wananchi kuhamasika kuwekeza katika tasnia ya ukuzaji wa viumbe maji pamoja na upatikanaji wa mikopo nafuu kutoka katika taasisi za fedha.

281. Mwaka 2020, jumla ya vifaranga vya samaki 21,676,187 vilizalishwa katika vituo vitotoleshi vya Serikali na sekta binafsi ikilinganishwa na vifaranga 17,301,076 vilivyozalishwa mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 25.3. Ongezeko hilo lilitokana na kuimarishwa kwa vituo vitotoleshi kwa kuwezesha upatikanaji wa pembejeo zikiwemo mbegu bora, vyakula na vitotoleshi vya samaki. Katika kipindi hicho, uzalishaji wa samaki (sato na kambale) ulikuwa tani 18,716.6 zenye thamani ya

shilingi bilioni 103.4 ikilinganishwa na tani 18,073.6 zenye thamani ya shilingi bilioni 97.7 mwaka 2019, sawa na ongezeko la tani kwa asilimia 3.6. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uwekezaji katika ukuzaji wa viumbe maji ikiwemo ufugaji samaki katika vizimba. Aidha, uzalishaji wa mwani ulikuwa tani 1,410 zenye thamani ya shilingi milioni 705.0 mwaka 2020 ikilinganishwa na tani 1449.0 zenye thamani ya shilingi milioni 724.5 mwaka 2019. Vile vile, uzalishaji wa kambamiti ulikuwa tani 73.6 zenye thamani ya shilingi bilioni 1.8 ikilinganishwa na tani 336 zenye thamani ya shilingi bilioni 8.4 mwaka 2019.

**Jedwali Na. 11.9 Uzalishaji wa Samaki wa Maji Baridi (Sato na Kambale) kwenye Mabwawa, Mwani na Kambamiti**

| Mwaka | Idadi ya Vifaranga | Uzalishaji wa Sato na Kambale (Tani) | Thamani ya Sato na Kambale Shilingi (000,000) | Uzalishaji wa Mwani (Tani) | Thamani ya Mwani Shilingi (000,000) | Uzalishaji wa Kambamiti (Tani) | Thamani ya Kambamiti Shilingi (000,000) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2015 | 19,692,000 | 3,118.0 | 18,753.6 | 222.8 | 111.4 | 391 | 8,525.0 |
| 2016 | 18,000,000 | 3,613.6 | 21,681.6 | 1176.5 | 588.25 | 407 | 9,082.5 |
| 2017 | 14,119,272 | 11,000.0 | 66,000.0 | 1197.5 | 598.75 | 248 | 9,292.5 |
| 2018 | 15,119,757 | 14,800.0 | 88,800.0 | 1329.7 | 664.85 | 371.7 | 9,372.5 |
| 2019 | 21,173,226 | 18,073.6 | 97,728.0 | 1449.0 | 724.5 | 336 | 8,410.0 |
| 2020 | 17,301,076 | 18,716.6 | 103,398.0 | 1410.0 | 705 | 73.6 | 1,840.0 |

**Chanzo**: Wizara ya Mifugo na Uvuvi - Uvuvi

## Uvunaji wa Samaki

282. Mwaka 2020, tani 473,592 za samaki zenye thamani ya shilingi trilioni 2.4 zilivunwa ikilinganishwa na tani 470,309 zenye thamani ya trilioni 2.2 mwaka 2019. Kati ya hizo, tani 409,828 zilivunwa katika maji baridi na tani 63,764 katika maji chumvi ikilinganishwa na tani 365,104 za maji baridi na tani 105,205 za maji chumvi mwaka 2019. Kuongezeka kwa uvunaji wa samaki kulitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa samaki kulikochangiwa na kuendelea kupungua kwa vitendo vya uvuvi haramu ambavyo kwa kiasi kikubwa huharibu mazalia ya Samaki.

**Jedwali Na. 11.10: Mwenendo wa Uvunaji wa Samaki (Tani)**

| Mwaka | Maji baridi | Maji chumvi | Jumla |
|---|---|---|---|
| 2011 | 290,474 | 50,592 | **341,066** |
| 2012 | 314,944 | 50,079 | **365,023** |
| 2013 | 315,008 | 52,846 | **367,854** |
| 2014 | 314,062 | 51,912 | **365,974** |
| 2015 | 309,922 | 52,723 | **362,645** |
| 2016 | 308,772 | 53,823 | **362,595** |
| 2017 | 332,373 | 55,170 | **387,543** |
| 2018 | 323,120 | 53,231 | **376,351** |
| 2019 | 409,333 | 60,977 | **470,309** |
| 2020 | 409,828 | 63,764 | **473,592** |

**Chanzo:** Wizara ya Mifugo na Uvuvi

**Udhibiti wa Ubora na Usalama wa Mazao ya Uvuvi**

283. Mwaka 2020, Serikali ilifanya kaguzi 7,341 kwa lengo la kuhakiki ubora na usalama wa mazao ya uvuvi ikilinganishwa na kaguzi 3,724 mwaka 2019. Kaguzi hizo zilifanyika katika viwanda 51 vikubwa na vya kati vya kuchakata samaki, mialo 124, masoko 31, maghala 52, na vyombo 541 vya kusafirisha mazao ya uvuvi. Aidha, vibali 3,385 vilitolewa kwa wafanyabiashara wa ndani kwa ajili ya uuzaji wa tani 38,221.3 katika masoko ya ndani ikilinganishwa na vibali 5,943 vilivyotolewa kwa ajili ya uuzaji wa tani 93,314.9 mwaka 2019. Vile vile, vyeti vya afya 2,733 vilitolewa kwa wafanyabiashara wanaosafirisha samaki na mazao yake nje ya nchi ikilinganishwa na vyeti 2,879 mwaka 2019. Katika kulinda ubora na usalama wa chakula, Maabara ya Taifa ya Uvuvi Nyegezi ilifanya uchunguzi wa kimaabara wa vimelea na kemikali katika sampuli 3,271 za mazao ya uvuvi mwaka 2020 ikilinganishwa na sampuli 4,608 mwaka 2019 ambapo sampuli zote zilikidhi viwango vya ubora vinavyokubalika.

**Uwekezaji katika Sekta ya Uvuvi**

284. Serikali iliendelea kuhamasisha uwekezaji katika sekta ya uvuvi ambapo hadi Desemba 2020, kulikuwa na jumla ya viwanda vikubwa 18 vya samaki, viwanda vitano (5) vya kutengeneza nyavu, maghala 90 ya kuhifadhi mazao ya uvuvi ikilinganishwa na viwanda vikubwa 15, viwanda vinne (4) vya kutengeneza nyavu na maghala 56 ya kuhifadhi mazao ya uvuvi mwaka 2019. Katika kipindi hicho, kulikuwa na viwanda vidogo 34 vya kuchakata mazao ya uvuvi na viwanda vitatu (3) vya kutengeneza boti kama ilivyokuwa mwaka 2019. Aidha, Serikali kupitia Kitengo cha Hifadhi ya Bahari na Maeneo Tengefu iliweza kuvutia uwekezaji katika shughuli za hoteli ambapo hadi Desemba 2020 kulikuwa na hoteli 22 za kitalii zilizopo karibu na maeneo yaliyohifadhiwa ikilinganishwa na hoteli 18 za kitalii mwaka 2019. Kati ya hizo, 12 zipo Mafia, Tanga sita (6), Dar es Salaam tatu (3) na Mtwara moja (1). Ongezeko hilo lilitokana na kuanzishwa kwa hoteli tatu zilizopo mkoa wa Dar es Salaam na moja mkoa wa Mtwara.

**Mwenendo wa Uuzaji na uingizaji wa Mazao ya Uvuvi nje ya Nchi**

285. Mwaka 2020, tani 40,478.0 za mazao ya uvuvi na samaki hai wa mapambo 128,316 wenye thamani ya shilingi bilioni 386.4 waliuzwa nje ya nchi ikilinganishwa na tani 45,775 za mazao ya uvuvi na samaki hai wa mapambo 136,915 wenye thamani ya shilingi bilioni 376.8 waliouzwa nje mwaka 2019. Aidha, thamani ya mazao ya uvuvi yaliyouzwa nje ilikuwa kubwa kutokana na kuongezeka kwa bei ya mazao hayo katika mialo. Katika kipindi hicho, mauzo ya mazao ya uvuvi na samaki hai wa mapambo yaliliingizia Taifa mapato ya shilingi bilioni 21.7 kama mrabaha ikilinganishwa na shilingi bilioni 25.6 mwaka 2019. Aidha, jumla ya tani 706.05 za mabondo zenye thamani ya shilingi bilioni 129.9 ziliuzwa nje ya nchi na kuliingizia Taifa mapato ya shilingi bilioni 4.60 kama mrabaha ikilinganishwa na tani 541.5 za mabondo zenye thamani ya shilingi bilioni 111.5 zilizouzwa nje ya nchi mwaka 2019 na kuliingizia taifa

mapato ya shilingi bilioni 3.9 kama mrabaha. Kupungua kwa kiasi cha mabondo yaliouzwa nje kulitokana na kuyumba kwa soko la mabondo katika nchi za Hong Kong na China. Kwa upande mwingine, jumla ya tani 5.3 za samaki wenye thamani ya shilingi milioni 114.9 ziliingizwa nchini na kuliingizia taifa mapato ya shilingi milioni 27.2 kama mrabaha ikilinganishwa na tani 6.0 za samaki wenye thamani ya shilingi milioni 116.6 zilizoingizwa nchini mwaka 2019 na kuliingizia Taifa mapato ya shilingi milioni 37.0 kama mrabaha. Kupungua kwa kiasi cha samaki kilichoingizwa nchini kulitokana kuongezeka kwa uzalishaji wa samaki ndani ya nchi.

**UZALISHAJI WA MIWA NA SUKARI NCHINI**

Jedwali Na. 33

| Msimu[1] | Miwa | | | | Sukari | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wakulima | | | | | iliyotumika[3] | |
| | Umma (000 Tani) | Binafsi (000 Tani) | Jumla (000 Tani) | Bei[2] (Sh./Tani) | Iliyozalishwa Tani | Jumla Tani | Kilo kwa kila mtu[4] |
| 2001/02 | 1,134 | 389 | 1,523 | 14,700 | 164,498 | 142,398 | 10.10 |
| 2002/03 | 1,402 | 411 | 1,813 | 15,000 | 190,120 | 167,300 | 10.42 |
| 2003/04 | 1,672 | 670 | 2,342 | 16,800 | 223,839 | 290,711 | 10.90 |
| 2004/05 | 1,594 | 752 | 2,346 | 20,568 | 229,617 | 328,005 | 10.90 |
| 2005/06 | 1,545 | 956 | 2,501 | 22,383 | 263,317 | 343,292 | 12.00 |
| 2006/07 | 1,430 | 611 | 2,041 | 29,000 | 192,095 | 366,708 | 12.00 |
| 2007/08 | 1,967 | 799 | 2,766 | 32,767 | 265,434 | 382,518 | 13.00 |
| 2008/09 | 2,056 | 693 | 2,749 | 32,771 | 279,850 | 396,113 | 13.40 |
| 2009/10 | 1,972 | 598 | 2,570 | 42,046 | 263,461 | 398,070 | 13.68 |
| 2010/11 | 2,357 | 661 | 3,018 | 43,865 | 304,135 | 410,259 | 12.00 |
| 2011/12 | 2,036 | 680 | 2,716 | 48,833 | 262,879 | 439,307 | 12.00 |
| 2012/13 | 2,242 | 711 | 2,953 | 52,167 | 296,698 | 468,000 | 12.00 |
| 2013/14 | 2,198 | 602 | 2,800 | 50,500 | 294,300 | 434,782 | 12.00 |
| 2014/15 | 2,466 | 697 | 3,163 | 51,333 | 304,007 | 511,680 | 12.00 |
| 2015/16 | 2,270 | 569 | 2,839 | 59,707 | 293,075 | 525,784 | 12.00 |
| 2016/17 | 2,504 | 557 | 3,061 | 72,667 | 324,930 | 456,000 | 12.75 |
| 2017/18 | 2,550 | 626 | 3,175 | 72,667 | 303,752 | 515,004 | 13.50 |
| 2018/19 | 2,792 | 797 | 3,589 | 72,667 | 359,219 | 524,772 | 13.50 |
| 2019/20 | 2,659 | 728 | 3,387 | 77,333 | 311,358 | 372,787 | 12.75 |
| Badiliko (%) 2018/19-2019/20 | -4.78 | -8.65 | -5.64 | | -13.32 | -28.96 | -5.56 |
| Ongezeko (%) 2001/02-2019/20 | 134.5 | 87.2 | 122.4 | 426.1 | 89.3 | 161.8 | 26.2 |

**Chanzo**: Bodi ya Sukari Tanzania

1 Msimu ni Kati ya Julai na Juni

2 Bei ya Mimea ni ile iliyo na asilimia 10 za Sucrose

3 Ni pamoja na Sukari iliyopelekwa Zanzibar

4 Ni kwa Tanzania bara

* Sukari yote huzalishwa na wakulima/mashirika binafsi

**PAMBA ILIYONUNULIWA NA MAUZO NCHINI**

Jedwali Na. 34

| Msimu [1] | Pamba yenye mbegu | | | | | Pamba iliyoondolewa mbegu | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Uzalishaji Kiasi (tani) | | | Bei ya wastani (Shs/Kilo) | | Kiasi (tani) | | | Mauzo nchini | | |
| | | | | | | | | | Kiasi (tani) | Bei ya wastani (000'Shs/tani) | |
| | AR | BR | Jumla | AR | BR | AR | BR | Jumla | Jumla [2] | AR | BR |
| 2001/02 | 148,180 | .. | 148,180 | 165 | .. | 49,668 | - | 49,668 | .. | .. | .. |
| 2002/03 | 187,908 | 781 | 188,689 | 180 | 50 | 62,983 | 262 | 63,245 | .. | .. | .. |
| 2003/04 | 139,756 | 213 | 139,969 | 280 | 100 | 46,843 | 72 | 46,915 | .. | .. | .. |
| 2004/05 | 341,589 | .. | 341,589 | 250 | .. | 114,496 | .. | 114,496 | .. | .. | .. |
| 2005/06 | 376,591 | .. | 376,591 | 220 | .. | 126,228 | .. | 126,228 | .. | .. | .. |
| 2006/07 | 130,585 | .. | 130,585 | 350 | .. | 43,770 | .. | 43,770 | .. | .. | .. |
| 2007/08 | 200,662 | .. | 200,662 | 450 | | 70,773 | .. | 70,773 | 37,488 | .. | .. |
| 2008/09 | 368,697 | .. | 368,697 | 480 | .. | 123,582 | .. | 123,582 | 66,554 | .. | .. |
| 2009/10 | 267,644 | .. | 267,644 | 480 | .. | 54,851 | .. | 54,851 | .. | .. | .. |
| 2010/11 | 163,518 | . | 163,518 | 900 | .. | 54,809 | - | 54,809 | .. | .. | .. |
| 2011/12 | 225,938 | .. | 225,938 | 1,000 | .. | 75,731 | .. | 75,731 | .. | .. | .. |
| 2012/13 | 351,156 | .. | 351,156 | 660 | .. | 117,702 | .. | 117,702 | .. | .. | .. |
| 2013/14 | 245,815 | .. | 245,815 | 700 | .. | 82,394 | .. | 82,394 | .. | .. | .. |
| 2014/15 | 202,312 | .. | 202,312 | 750 | .. | 67,812 | .. | 67,812 | | | .. |
| 2015/16 | 149,765 | .. | 149,765 | 800 | | 50,199 | .. | 50,199 | 525,784 | 12 | .. |
| 2016/17 | 132,934 | .. | 132,934 | 1,000 | .. | 42,203 | .. | 42,203 | | | |
| 2017/18 | 222,790 | .. | 222,790 | 1,100 | .. | 80,575 | .. | 80,575 | 39,244 | 3,667 | .. |
| 2018/19 | 348,901 | .. | 348,901 | 1,200 | .. | 129,408 | .. | 129,408 | 51,942 | 3,123 | |
| 2019/20 | 348,958 | .. | 348,958 | 1,200 | .. | 129408 | .. | 129,408 | 25,910 | 3,123 | .. |
| Badiliko (%) 2018/19-2019/20 | 0.02 | | 0.02 | 0 | | 0 | | 0 | -50 | | |

**Chanzo:** Bodi ya Mauzo ya Pamba

1 Msimu ni kati ya Juni na Mei

2 Ni jumla ya AR na BR

.Takwimu hazikupatikani

Pamba ya Tanzania hainunuliwi wala kuuzwa katika madaraja kwa sasa

## ENEO LILILOPANDWA MICHAI NA MAJANI MABICHI YALIYOPATIKANA

Jedwali Na. 35

| Msimu [1] | Eneo lililopandwa (hekta): mashamba | | | Majani Mabichi yaliyopatikana (tani) | | | | | | Bei kwa mkulima (Shs/ Kilo) | Mauzo[2] Nchini (tani) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Kiumilikaji: mashamba | | | Kikanda: mashamba | | | | |
| | Makubwa | Madogo | Jumla | Makubwa | Madogo | Jumla | Kaskazini | Kusini | Jumla | | |
| 2001/02 | 10,811 | 10,364 | 21,175 | 97,297 | 13,999 | 111,296 | 22,794 | 88,502 | 111,296 | 80 | 2,683 |
| 2002/03 | 11,097 | 9,762 | 20,889 | 100,677 | 31,718 | 132,395 | 28,679 | 103,716 | 132,395 | 85 | 3,158 |
| 2003/04 | 11,485 | 10,801 | 22,286 | 95,986 | 31,993 | 127,979 | 26,384 | 101,595 | 127,979 | 86 | 3,225 |
| 2004/05 | 11,271 | 11,442 | 22,713 | 94,172 | 39,246 | 133,418 | 20,649 | 112,769 | 133,418 | 86 | 4,004 |
| 2005/06 | 11,310 | 10,977 | 22,287 | 91,337 | 31,881 | 123,218 | 29,046 | 94,172 | 123,218 | 93 | 3,881 |
| 2006/07 | 11,271 | 11,956 | 23,227 | 109,632 | 49,024 | 158,656 | 39,673 | 118,983 | 158,656 | 100 | 4,737 |
| 2007/08 | 11,272 | 11,449 | 22,722 | 97,310 | 51,160 | 148,470 | 33,456 | 115,015 | 148,471 | 111 | 4,253 |
| 2008/09 | 11,271 | 11,449 | 22,722 | 100,644 | 41,167 | 141,811 | 31,677 | 110,134 | 141,811 | 118 | 4,464 |
| 2009/10 | 11,272 | 11,449 | 22,722 | 106,021 | 44,716 | 150,737 | 33,309 | 117,428 | 150,737 | 124 | 5,084 |
| 2010/11 | 11,272 | 11,449 | 22,722 | 95,511 | 47,616 | 143,127 | 112,368 | 30,759 | 143,127 | 152 | 6,065 |
| 2011/12 | 11,272 | 11,449 | 22,722 | 88,582 | 52,359 | 140,941 | 27,009 | 113,932 | 140,941 | 200 | 4,839 |
| 2012/13 | 11,272 | 11,449 | 22,722 | 113,628 | 54,872 | 168,500 | 30,997 | 137,503 | 168,500 | 206 | 5,498 |
| 2013/14 | 11,272 | 11,449 | 22,722 | 101,489 | 47,001 | 148,490 | 27,935 | 120,555 | 148,490 | 225 | 5,672 |
| 2014/15 | 11,272 | 11,449 | 22,722 | 100,018 | 52,467 | 152,485 | 23,283 | 129,202 | 152,485 | 176 | 6,302 |
| 2015/16 | 11,272 | 11,449 | 22,721 | 96,759 | 44,605 | 141,364 | 25,413 | 115,915 | 141,328 | 230 | 10,257 |
| 2016/17 | 11,272 | 11,449 | 22,722 | 78,929 | 41,495 | 120,424 | 20,592 | 99,832 | 120,424 | 285 | 4,648 |
| 2017/18 | 11,322 | 11,705 | 23,028 | 97,428 | 55,620 | 153,048 | 31,599 | 121,449 | 153,048 | 299 | 5,434 |
| 2018/19 | 11,322 | 11,705 | 23,027 | 104,203 | 61,081 | 165,284 | 36,506 | 128,778 | 165,284 | 312 | 3,926 |
| 2019/20 | 12,275 | 11,127 | 23,403 | 78,579 | 54,973 | 133,552 | 23,700 | 109,852 | 133,552 | 312 | 3,767 |
| Badiliko (%) 2018/19-2019/20 | -8.42 | 4.94 | 1.63 | -24.59 | -10 | -19 | 35 | -14 | -19.20 | 4.7 | -27.7 |

**Chanzo**: Bodi ya Chai Tanzania

1 Msimu ni kati ya Julai na Juni

2 Chai iliyotengenezwa

Jedwali Na. 36

**KAHAWA ILIYONUNULIWA NA MAUZO NCHINI**

| Msimu[1] | Iliyonunuliwa (Tani) | | | | Bei (Sh./kilo) | | | Mauzo nchini[+] | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | ARABICA | | ROBUSTA | JUMLA | ARABICA | | ROBUSTA | KIASI | THAMANI |
| | Laini | Ngumu | | | Laini | Ngumu | Maganda | (Tani) | (shs'000) |
| 2003/04 | 20,716 | 1,850 | 16,138 | 38,704 | 1,800.0 | 1,200.0 | 600.0 | 38,704.0 | 46,670.0 |
| 2004/05 | 23,870 | 888 | 9,133 | 33,891 | 2,593.5 | 1,976.0 | 1,235.0 | 33,891.0 | 62,566.0 |
| 2005/06 | 24,116 | 1,362 | 8,856 | 34,334 | 1,200.0 | 420.0 | 270.0 | 33,300.0 | 793,042.5 |
| 2006/07 | 33,345 | 2,417 | 19,076 | 54,838 | 2,840.0 | 1,796.0 | 1,616.0 | 548.4 | 129,867.5 |
| 2007/08 | 26,330 | 1,588 | 15,606 | 43,524 | 2,995.0 | 1,875.0 | 1,734.0 | 43,523.0 | 89,099.3 |
| 2008/09 | 37,207 | 1,727 | 29,643 | 68,577 | 2,887.0 | 2,172.0 | 1,836.0 | 68,577.0 | 165,615.6 |
| 2009/10 | 22,217 | 915 | 11,467 | 34,599 | 3,988.0 | 2,475.0 | 1,563.0 | 34,599.0 | 108,741.1 |
| 2010/11 | 30,309 | 2,013 | 24,348 | 56,670 | 4,500.0 | 1,300.0 | 1,200.0 | 56,670.0 | 264,143.6 |
| 2011/12 | 20,775 | 941 | 11,590 | 33,306 | 8,144.4 | 5,436.4 | 3,276.9 | 33,306.0 | 212,292.6 |
| 2012/13 | 33,204 | 1,655 | 36,150 | 71,009 | 4,850.0 | 3,600.0 | 3,200.0 | 71,009.0 | 281,781.8 |
| 2013/14 | 28,212 | 1,115 | 18,875 | 48,202 | 4,314.0 | 3,272.9 | 3,074.6 | 48,202.0 | 183,708.9 |
| 2014/15 | 26,335 | 810 | 18,788 | 45,933 | 5,848.0 | 4,515.0 | 3,848.5 | - | - |
| 2015/16 | 21,517 | 460 | 17,526 | 39,503 | 7,249.6 | 5,943.4 | 4,092.9 | 39,503.0 | 105,760.8 |
| 2016/17 | 27,023 | 681 | 19,989 | 47,693 | 7,636.0 | 6,164.0 | 4,347.0 | 47,693.0 | 129,428,710.0 |
| 2017/18 | 36,551 | 633 | 11,897 | 43,193 | 2,980.0 | 2,980.0 | 2,980.0 | 43,193.3 | 116,587,271.0 |
| 2018/19 | 30,664 | 2,068 | 27,927 | 66,546 | 2,210.0 | 2,210.0 | 2,210.0 | 66,546.2 | 123,185,587.0 |
| 2019/20 | 31,379 | 883 | 27,056 | 59,318 | 5,014.8 | 4,515.2 | 4,056.8 | 59,318.0 | 258,364,970.6 |
| Badiliko (%) | | | | | | | | | |
| 2018/19-2019/20 | 2.33 | -57.30 | -3.12 | -10.86 | 126.91 | 104.31 | 83.57 | -10.86 | 109.74 |

**Chanzo**: Bodi ya Kahawa Tanzania

\+ Kahawa iliyosafishwa

1 Msimu ni kati ya Julai na Juni

2 Ni ya muda

\- Takwimu hazikupatikana

**ENEO LILILOPANDWA MKONGE NA KATANI ILIYOPATIKANA**

Jedwali Na. 37

| | Eneo (Hekta) | | | Katani iliyopatikana | | Mauzo nchini+ | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Msimu[1] | Uliokomaa | Usiokomaa | Jumla | Kiasi (tani) | Bei kwa Mkulima (shs/tani) | Kiasi (tani) | Thamani (Sh. milioni) |
| 2001/02 | 34,645 | 11,473 | 46,118 | 23,641 | 337,732 | 4,947 | 1,671 |
| 2002/03 | 39,462 | 10,611 | 50,073 | 23,280 | 450,000 | 6,300 | 2,835 |
| 2003/04 | 29,493 | 12,204 | 41,697 | 26,758 | 540,000 | 6,370 | 4,027 |
| 2004/05 | 45,079 | 14,500 | 59,579 | 27,794 | 617,342 | 8,213 | 5,070 |
| 2005/06 | 26,384 | 13,264 | 39,648 | 30,934 | 810,000 | 10,767 | 8,613 |
| 2006/07 | 28,273 | 13,608 | 41,882 | 33,327 | 975,000 | 11,010 | 10,152 |
| 2007/08 | 28,577 | 15,622 | 44,199 | 34,057 | 1,000,000 | 16,997 | 15,800 |
| 2008/09 | 35,751 | 18,023 | 53,774 | 25,996 | 1,000,000 | 11,496 | 10,100 |
| 2009/10 | 30,556 | 11,849 | 42,405 | 24,092 | 1,200,000 | 12,761 | 10,375 |
| 2010/11 | 31,117 | 12,169 | 43,286 | 25,090 | 1,300,000 | 11,617 | 13,154 |
| 2011/12 | 32,601 | 14,302 | 46,902 | 36,600 | 1,500,000 | 11,511 | 14,390 |
| 2012/13 | 33,649 | 11,994 | 45,643 | 34,874 | 1,600,000 | 11,466 | 16,823 |
| 2013/14 | 35,266 | 11,044 | 46,310 | 37,805 | 1,724,864 | 9,160 | 16 |
| 2014/15 | 35,946 | 12,494 | 48,440 | 38,872 | 2,071,446 | 8,972 | 17,513 |
| 2015/16 | 34,723 | 13,231 | 47,954 | 41,795 | 2,700,000 | 9,075 | 20,342 |
| 2016/17 | 41,661 | 12,850 | 54,511 | 36,533 | 2,700,000 | 9,559 | 21,541 |
| 2017/18 | 40,635 | 14,389 | 55,024 | 43,280 | 3,000,000 | 12,111 | 30,803 |
| 2018/19 r | 43,406 | 18,567 | 61,973 | 33,271 | 3,300,000 | 13,043 | 39,607 |
| 2019/20 | 41,461 | 17,044 | 58,505 | 35,923 | 3,500,000 | 12645 | 38,322 |
| Badiliko (%) 2018/19-2019/20 | -4.5 | -8.2 | -5.6 | -8.0 | 6.1 | -3.1 | -3.2 |

**Chanzo**: Bodi ya Katani

+ Katani aina ya Line fibre, Tow na Flume Tow

1 Msimu ni kati ya Julai na Juni - Takwimu hazikupatikana

r - Takwimu zimeboreshwa

## MAUA YA PARETO YALIYONUNULIWA NA MAUZO YA BIDHAA ZA PARETO NCHINI

Jedwali Na. 38

| Msimu [1] | Maua yaliyonunuliwa (tani) | | | | Mauzo Nchini: Kiasi (tani) | | | Mauzo Nchini: Thamani (Sh.'000) | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kaskazini | Kusini | Jumla | Bei[2] (Sh./kg) | Utomvu (Crude Extract) | Poda | Dawa (Dry Mack) | Utomvu Crude Extract | Poda | Dawa (Dry Mack) |
| 2001/02 | 36 | 1,699.0 | 1,735.0 | 420.0 | - | - | - | - | - | - |
| 2002/03* | 111 | 979.0 | 1,090.0 | 380.0 | 2.0 | 90.0 | - | 106,920.0 | 99,891.0 | - |
| 2003/04 | 85 | 751.0 | 842.0 | 360.0 | - | - | - | - | - | - |
| 2004/05 | 90 | 910.0 | 1,000.0 | 360.0 | - | - | - | - | - | - |
| 2005/06 | - | 2,800.0 | 2,800.0 | 360.0 | - | - | - | - | - | - |
| 2006/07 | - | 1,600.0 | 1,600.0 | 700.0 | - | - | - | - | - | - |
| 2007/08 | - | 1,470.0 | 1,470.0 | 1,050.0 | - | - | - | - | - | - |
| 2008/09 | - | 1,600.0 | 1,600.0 | 1,500.0 | 36.4 | 105.0 | 624.0 | - | - | - |
| 2009/10 | - | 1,780.0 | 1,780.0 | 1,500.0 | 57.0 | 69.0 | 1,035.0 | 37,361.0 | 1,473.0 | 248.0 |
| 2010/11 | - | 1,786.8 | 1,786.8 | 1,500.0 | 57.2 | 69.3 | 69.3 | 37,503.7 | 1,478.6 | 246.9 |
| 2011/12 | 0 | 5,700.0 | 5,700.0 | 1,700.0 | 82.0 | - | 750.0 | - | 204.0 | 360,919.0 |
| 2012/13 | 0 | 6,100.0 | 6,100.0 | 2,400.0 | 84.0 | - | 2,000.0 | - | - | 462,000.0 |
| 2013/14 | 34 | 2,691.8 | 2,726.2 | 2,000.0 | 90.0 | 60.0 | 830.0 | 6,900,000.0 | 160,500.0 | 233,000.0 |
| 2014/15 | 31 | 2,255.0 | 2,286.0 | 2,500.0 | 76.0 | 30.0 | 430.0 | 133.6 | 116,048.0 | 235,612.7 |
| 2015/16 | 25 | 1,987.0 | 2,012.4 | 2,100.0 | 59.9 | 6.0 | 480.0 | 9,450,000.0 | 30,240.0 | 282,240.0 |
| 2016/17 | 39 | 2,111.8 | 2,151.0 | 2,050.0 | 53.2 | 162.0 | 727.0 | 6,782,016.0 | 651,810.0 | 436,232.0 |
| 2017/18 | 43 | 2,355.9 | 2,400.0 | 2,500.0 | 16.0 | 204.0 | 700.0 | 13,932,947.0 | 869,418.1 | 390,864.0 |
| 2018/19 | 68 | 2050 | 2118 | 3200 | - | - | - | 144,487.0 | 844,213.9 | 409,299.4 |
| 2019/20 | 69 | 2441 | 2510 | 3200 | - | - | - | - | - | - |
| Badiliko (%) 2018/19-2019/20 | 1.47% | 19.07% | 18.51 | 0 | - | - | - | - | - | |

**Chanzo**: Bodi ya Pareto Tanzania

1 Msimu ni kati ya Julai na Juni

2 Bei ni kwa maua ya daraja la tano

- Takwimu hazikupatikana

* Takwimu hizi hadi December 30 2002, Msimu bado unaendelea

## MUHTASARI WA KIASI CHA MAZAO MUHIMU YA BIASHARA YALIYONUNULIWA

Jedwali Na. 39 (Tani)

| Mazao | 2011/12 | 2012/13 | 2013/14 | 2014/15 | 2015/16 | 2016/17 | 2017/18 | 2018/19r | 2019/20 | Badiliko % 2017/18 - 2018/19 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Katani | 36,600 | 34,874 | 37,805 | 38,872 | 41,795 | 36,533 | 43,280 | 33,271 | 35,923 | 8.0 |
| Kahawa | 33,306 | 71,009 | 48,202 | 45,933 | 39,503 | 47,693 | 43,193 | 66,546 | .. | .. |
| Pamba[1] | 225,938 | 351,156 | 245,815 | 202,312 | 149,765 | 132,934 | 222,790 | 348,901 | 122,833 | -64.8 |
| Tumbaku | 74,239 | 86,343 | 105,803 | 87,281 | 60,691 | 85,861 | 50,522 | 72,325 | 37,546 | -48.1 |
| Pareto | 5,700 | 6,100 | 2,726 | 2,286 | 2,011 | 2,151 | 2,400 | 2,118 | 2,510 | 18.5 |
| Chai[2] | 140,941 | 168,500 | 148,490 | 152,485 | 141,328 | 120,424 | 153,048 | 61,081 | 54,973 | -10.0 |
| Korosho | 121,946 | 124,924 | 174,695 | 197,933 | 231,864 | 265,238 | 313,826 | 225,116 | .. | … |
| Miwa | 2,716 | 2,953 | 2,800 | 3,163 | 2,839 | 556,522 | 625,743 | 797,016 | .. | … |

**Chanzo**: Bodi zinazohusika
1 Yenye mbegu
2 Majani mabichi
.. Takwimu hazikupatikana
r Takwimu zimeboreshwa

Jedwali Na. 40

**UZALISHAJI KATIKA SEKTA YA UVUVI 2003-2020**

| Mwaka | Idadi ya Wavuvi | Idadi ya Vyombo | | | Uzalishaji na Mapato | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Maji baridi | | Maji Chumvi | | Jumla | |
| | | Maji baridi | Maji Chumvi | Jumla ya Vyombo | Uzito (tani) | Thamani (Sh..) | Uzito (tani) | Thamani (Sh. ) | Uzito (tani) | Thamani (Sh. ) |
| 2003 | 124,570 | 31,225 | 4,927 | 36,152 | 301,855 | 141,073,500 | 49,270 | 34,489,000 | 351,125 | 175,562,500 |
| 2004 | 122,514 | 32,248 | 4,927 | 37,175 | 312,040 | 147,743,000 | 50,470 | 40,376,000 | 362,510 | 188,119,000 |
| 2005 | 133,197 | 32,248 | 7,190 | 39,438 | 320,566 | 256,452,800 | 54,969 | 82,452,930 | 375,535 | 338,905,730 |
| 2006 | 156,544 | 44,362 | 7,190 | 51,552 | 292,519 | 248,640,904 | 48,591 | 37,077,637 | 341,109 | 285,718,540 |
| 2007 | 163,037 | 44,362 | 7,489 | 51,851 | 284,348 | 252,525,198 | 43,499 | 39,210,207 | 327,847 | 291,735,405 |
| 2008 | 170,038 | 44,838 | 7,489 | 52,327 | 281,691 | 194,725,416 | 43,130 | 40,563,641 | 324,821 | 235,289,057 |
| 2009 | 172,090 | 45,234 | 7,664 | 52,898 | 288,059 | 351,394,073 | 47,616 | 56,633,436 | 335,675 | 408,027,509 |
| 2010 | 163,601 | 42,337 | 7,664 | 50,001 | 294,474 | 684,844,020 | 52,683 | 89,639,934 | 347,157 | 774,483,954 |
| 2011 | 177,527 | 47,635 | 7,664 | 55,299 | 290,474 | 1,031,883,681 | 50,592 | 166,954,953 | 341,066 | 1,198,838,634 |
| 2012 | 182,741 | 49,321 | 7,664 | 56,985 | 314,944 | 1,129,349,925 | 50,079 | 177,781,799 | 365,023 | 1,307,131,724 |
| 2013 | 183,431 | 49,721 | 7,664 | 57,385 | 315,008 | 1,248,903,393 | 52,846 | 195,529,127 | 367,854 | 1,444,432,520 |
| 2014 | 183,800 | 49,627 | 7,664 | 57,291 | 314,062 | 1,287,248,813 | 51,912 | 207,649,600 | 365,974 | 1,494,898,413 |
| 2015 | 183,800 | 49,627 | 7,664 | 57,291 | 309,922 | 1,270,856,680 | 52,723 | 210,892,897 | 362,645 | 1,481,749,577 |
| 2016 | 203,529 | 49,688 | 9,650 | 59,338 | 308,772 | 1,274,485,404 | 53,823 | 211,891,899 | 362,595 | 1,486,377,303 |
| 2017 | 203,529 | 49,688 | 9,650 | 59,338 | 332,373 | 1,495,678,680 | 55,170 | 248,262,840 | 387,543 | 1,743,941,520 |
| 2018 | 202,053 | 49,688 | 9,242 | 58,930 | 323,120 | 1,518,667,619 | 53,231 | 250,190,118 | 376,351 | 1,768,857,737 |
| 2019 | 202,053 | 49,688 | 9,242 | 58,930 | 365,104 | 1,715,988,903 | 105,205 | 494,464,498 | 470,309 | 2,210,453,400 |
| 2020 | 202,539 | 50,116 | 9,242 | 59,358 | 409,828 | 2,049,141,547 | 63,764 | 318,819,664 | 473,592 | 2,367,961,211 |

**Chanzo**: Wizara ya Mifugo na Uvuvi

## MWENENDO WA UUZAJI WA SAMAKI NJE YA NCHI 2011-2020

Jedwali Na. 40A

| Mwaka | Uzito (Mt) | Samaki wa mapambo | Thamani katika dola za Marekani | Thamani katika Shilingi | Ushuru |
|---|---|---|---|---|---|
| 2011 | 37,996.43 | 61,215 | 152,973,356.80 | 233,714,590,010.80 | 6,153,278,023.30 |
| 2012 | 41,394.27 | 45,550 | 163,299,365.50 | 254,901,017,111.31 | 6,819,926,007.14 |
| 2013 | 38,573.61 | 44,260 | 147,659,778.56 | 234,884,628,955.92 | 6,117,769,193.74 |
| 2014 | 43,354.40 | 42,100 | 188,101,262.01 | 314,489,903,877.12 | 7,490,632,355.15 |
| 2015 | 41,059.45 | 87,630 | 259,286,762.20 | 547,228,222,095.53 | 13,097,411,199.19 |
| 2016 | 39,691.46 | 65,841 | 257,257,100.48 | 526,985,019,569.27 | 14,302,761,906.89 |
| 2017 | 36,063.23 | 101,110 | 182,450,277.75 | 406,568,122,271.47 | 10,446,850,538.58 |
| 2018 | 44,939.79 | 63,978 | 239,680,014.56 | 546,993,779,393.01 | 13,520,367,822.26 |
| 2019 | 45,775.17 | 136,915 | 158,657,945.58 | 376,763,802,642.91 | 25,567,600,872.63 |
| 2020 | 40,477.97 | 128,316 | 169,111,837.12 | 386,369,197,733.30 | 21,678,640,820.11 |

**Chanzo:** Wizara ya Mifugo na Uvuvi - Idara ya Uvuvi

## MWENENDO WA UKUZAJI VIUMBE MAJI 2015 - 2020

Jedwali Na. 40B

| Mwaka | Idadi ya Wakuzaji viumbe maji | Idadi ya mabwawa ya samaki | Idadi ya vizimba | Idadi ya vifaranga | Uzalishaji wa samaki | Uzalishaji wa mwani |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2015 | 17,725 | 21,300 | 50 | 19,090,000 | 3,118 | 222.8 |
| 2016 | 18,843 | 22,545 | 109 | 18,000,000 | 3,613.6 | 1,176.5 |
| 2017 | 20,370 | 24,302 | 150 | 14,119,272 | 11,000 | 1,197.5 |
| 2018 | 22,598 | 24,302 | 315 | 15,119,757 | 14,800 | 1,329.5 |
| 2019 | 26,474 | 26,445 | 408 | 17,301,076 | 16,288 | 1,449 |
| 2020 | 28,009 | 27,979 | 431 | 21,676,187 | 17,233 | 1,410 |

**Chanzo:** Wizara ya Mifugo na Uvuvi - Idara ya Uvuvi

## SURA YA 12

## MALIASILI NA UTALII

### Misitu na Nyuki

286. Mwaka 2020, tani 30,037 za asali zilizalishwa ikilinganishwa na tani 30,622 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 1.9. Kati ya hizo, tani 2,032.4 zenye thamani ya shilingi milioni 13,413.7 ziliuzwa nje ya nchi ikilinganishwa na tani 607.6 zenye thamani ya shilingi milioni 4,860.8 mwaka 2019. Kuongezeka kwa thamani ya mauzo ya asali nje kulitokana na kuongezeka kwa kiasi cha mauzo na kupanda kwa wastani wa bei ya asali katika soko la dunia kutoka dola za Marekani 2.2 kwa kilo mwaka 2019 hadi dola za Marekani 3.5 kwa kilo mwaka 2020. Aidha, tani 1,884 za nta zilizalishwa mwaka 2020 ikilinganishwa na tani 1,897 za nta zilizozalishwa mwaka 2019. Kati ya hizo, tani 251 za nta zenye thamani ya shilingi milioni 3,865.4 ziliuzwa nje ya nchi ikilinganishwa na tani 179.3 zenye thamani ya shilingi milioni 1,437.9 mwaka 2019. Kuongezeka kwa kiasi na thamani ya nta iliyouzwa nje ya nchi kulitokana na kuimarika kwa bei ya nta katika soko la dunia ambapo wastani wa bei ya nta iliongezeka kutoka dola za Marekani 7.5 kwa kilo mwaka 2019 hadi dola za Marekani 8.0 kwa kilo mwaka 2020. Sehemu kubwa ya asali na nta iliyozalishwa nchini iliuzwa katika nchi za Marekani, Ujerumani na Japan.

**Jedwali Na 12.1: Mauzo ya Mazao ya Nyuki Nje ya Nchi**

| Mwaka | Asali | | Nta | |
|---|---|---|---|---|
| | Uzito (Tani) | Thamani (Shilingi) | Uzito (Tani) | Thamani (Shilingi) |
| 2011 | 343 | 2,181,319,119 | 534 | 3,898,239,826 |
| 2012 | 103.8 | 262,043,582 | 277 | 2,582,805,057 |
| 2013 | 83 | 287,368,000 | 384 | 4,659,954,408 |
| 2014 | 108.2 | 539,927,831 | 271 | 3,849,466,035 |
| 2015 | 152.6 | 983,848,159 | 220.2 | 3,238,346,723 |
| 2016 | 259.9 | 1,222,045,655 | 251.9 | 4,549,643,832 |
| 2017 | 240.8 | 1,292,017,450 | 203.9 | 6,879,170,450 |
| 2018 | 1,095.9 | 9,342,538,000 | 143 | 1,287,099,000 |
| 2019 | 607.6 | 4,860,834,400 | 179.3 | 1,437,865,600 |
| 2020 | 2,032.4 | 13,413,721,200 | 251 | 3,865,400,000 |

**Chanzo:** Wizara ya Maliasili na Utalii

287. Serikali kupitia Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania uliotesha miche ya miti 20,689,369 mwaka 2020 ikilinganishwa na miche 21,824,600 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 5.2. Miche hiyo ilipandwa katika maeneo mapya yenye hekta 3,583; maeneo yaliyovunwa (hekta 4,543); na maeneo mapya ambayo miti haikuota (hekta 3,303) ikilinganishwa na maeneo yenye hekta 1,893; hekta 615; na hekta 251,

mtawalia, mwaka 2019. Aidha, mashamba ya miti yenye ukubwa wa hekta 37,469 yalisafishwa ikilinganishwa na hekta 18,101 mwaka 2019. Vile vile, Wakala ulipogoa miti katika mashamba yenye hekta 9,647 na kupunguzia miti katika mashamba yenye hekta 3,317 ikilinganishwa na hekta 6,244 na hekta 1,293, kwa mtiririko huo, mwaka 2019. Wakala uliongeza mashamba mapya yenye ukubwa wa hekta 56,500 kwa ajili ya upandaji miti katika jitihada za kuongeza upatikanaji wa mazao ya misitu.

**Jedwali Na. 12.2: Kazi Zilizofanyika katika Kuendeleza Mashamba ya Miti ya Kupandwa**

| Mwaka | Kuotesha miche ya miti | Kuandaa mashamba | Kurudishia miti | Kupanda miti | Kurudishia maeneo yasiyoota vizuri | Kuondoa magugu | Kupogoa | Kupunguzia miti |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (Hekta) | | | | | | |
| **2016** | 17,944,569 | 6,186.2 | 4,378.4 | 4,644 | 1,946.5 | 31,103.0 | 5,896.5 | 9,439.7 |
| **2017** | 19,181,213 | 9,162 | 2,987 | 4,825 | 2,966 | 41,056 | 7,969 | 1,262 |
| **2018** | 20,435,500 | 7,408 | 3,732 | 4,927 | 2,664 | 36,989 | 9,019 | 4,658 |
| **2019** | 21,824,600 | 4,438 | 615 | 1,893 | 251 | 18,101 | 6,244 | 1,293 |
| **2020** | 20,689,369 | 7,604 | 4,543 | 3,583 | 3,303 | 37,469 | 9,647 | 3,317 |

**Chanzo**: Wizara ya Maliasili na Utalii

288. Mwaka 2020, jumla ya miche 22,270 ilioteshwa na kupandwa katika maeneo ya misitu ya asili iliyoharibiwa kutokana na shughuli za binadamu ikilinganishwa na miche 1,692,421 iliyopandwa katika maeneo hayo mwaka 2019. Kupungua kwa idadi ya miche iliyooteshwa na kupandwa kulitokana kuimarika kwa ulinzi wa maeneo ya misitu pamoja na elimu iliyotolewa kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kuhifadhi na kutunza mazingira na hivyo, kupunguza maeneo ya misitu ya asili iliyoharibiwa. Aidha, mipango ya usimamizi wa misitu ya hifadhi 13 iliandaliwa na mipaka ya hifadhi ya misitu yenye urefu wa kilomita 1,652.8 ilisafishwa na kuwekwa maboya/vigingi 2,765 na mabango 749 kwa lengo la kupunguza migogoro ya mipaka na wananchi.

### Wanyamapori

289. Mwaka 2020, doria 540,553 zilifanyika kwa ajili ya kudhibiti ujangili na uvamizi wa maeneo yaliyohifadhiwa ikilinganishwa na doria 529,679 mwaka 2019. Kati ya hizo, doria 278,289 zilifanyika katika Hifadhi za Taifa; doria 75,000 hifadhi ya eneo la Ngorongoro; na doria 187,264 katika mapori ya akiba na mapori tengefu. Aidha, doria hizo ziliwezesha kukamatwa kwa nyara mbalimbali zikiwemo: meno ya tembo 59; bunduki 493 na risasi 2,952 za aina mbalimbali. Kutokana na doria hizo, idadi ya mizoga ya tembo katika mapori ya akiba, tengefu, ardhioevu na maeneo ya hifadhi ya wanyamapori ilipungua. Vile vile, katika kuimarisha jeshi la Uhifadhi wa Wanyapori na Misitu, watumishi wapatao 6,473 wa kada za wanyamapori na misitu walipatiwa mafunzo ikilinganishwa na watumishi 4,556 waliopatiwa mafunzo mwaka 2019.

290. Mwaka 2020, shilingi milioni 154,390.1 zilikusanywa na sekta ndogo ya wanyamapori ikilinganishwa na shilingi milioni 460,446.9 zilizokusanywa mwaka

2019, sawa na upungufu wa asilimia 66.5. Kati ya fedha hizo, Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania lilikusanya shilingi milioni 85,614.7; Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (shilingi milioni 47,862.2); na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (shilingi milioni 20,913.2). Kushuka kwa mapato hayo kulichangiwa na kupungua kwa idadi ya watalii kutoka nje ya nchi kulikosababishwa na athari za janga la UVIKO-19.

**Jedwali Na. 12.3: Mchanganuo wa Mapato Yatokanayo na Sekta Ndogo ya Wanyamapori**

| Mwaka | Hifadhi za Taifa | Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro | Mapato yatokanayo na Uwindaji wa Kitalii (TAWA) | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| 2016 | 175,089,696,000 | 70,863,972,000 | 29,136,885,800 | 275,090,553,800 |
| 2017 | 207,587,218,000 | 103,090,458,000 | 19,202,957,607 | 329,880,633,607 |
| 2018 | 214,486,751,736 | 108,149,417,000 | 20,109,785,000 | 342,745,953,736 |
| 2019 | 292,539,502,030 | 147,043,375,161 | 20,864,030,536 | 460,446,907,727 |
| 2020 | 85,614,710,442 | 47,862,177,819 | 20,913,213,013 | 154,390,101,274 |

**Chanzo**: Wizara ya Maliasili na Utalii

### Utalii

291. Mwaka 2020, watalii 620,867 walitembelea vivutio mbalimbali vya utalii nchini ikilinganishwa na watalii 1,527,230 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 59.3. Upungufu huo ulisababishwa na nchi nyingi duniani kuweka zuio la kusafiri ili kukabiliana na maambukizi ya UVIKO-19. Aidha, watalii 507,177 walitembelea Hifadhi za Taifa ikilinganishwa na watalii 1,257,952 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 59.7. Kati ya hao, watalii 288,867 walitoka ndani ya nchi na watalii 218,310 walitoka nje ya nchi.

292. Mwaka 2020, watalii waliotembelea Hifadhi ya Ngorongoro walipungua kwa asilimia 65.7 na kufikia watalii 248,181 kutoka watalii 724,538 mwaka 2019. Kati ya hao, watalii 122,228 walitoka nje ya nchi na watalii 125,953 walikuwa wa ndani ikilinganishwa na watalii 445,283 na watalii 279,255 mtawalia mwaka 2019. Kutokana na kupungua kwa idadi ya watalii, mapato yatokanayo na utalii nayo yalipungua kwa asilimia 59.3 kufikia dola za Marekani milioni 1,058.8 kutoka dola za Marekani milioni 2,604.5 mwaka 2019. Kufuatia kupungua kwa mapato yatokanayo na utalii kulikosababishwa na athari za UVIKO-19, Serikali ilichukua jukumu la kugharamia uendeshaji wa taasisi zinazosimamia sekta ya utalii nchini ambazo ni Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori, Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro na Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania. Taasisi hizo zilitengewa fedha kwa ajili ya mishahara ya watumishi, matumizi mengineyo na matumizi ya maendeleo kupitia bajeti ya Serikali.

**Jedwali Na. 12.4: Watalii Waliotembelea Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro**

| **Mwaka/Mwezi** | **2018** | | **2019** | | **2020** | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Nje ya Nchi** | **Ndani ya Nchi** | **Nje ya Nchi** | **Ndani ya Nchi** | **Nje ya Nchi** | **Ndani ya Nchi** |
| Januari | 30,000 | 18,692 | 32,913 | 21,348 | 35,482 | 22,605 |
| Februari | 38,598 | 19449 | 41,753 | 22,215 | 44,003 | 23,367 |
| Machi | 23,936 | 15,946 | 19,506 | 15,399 | 12,205 | 11,931 |
| Aprili | 12,497 | 10,384 | 14,539 | 14,519 | 202 | 2,812 |
| Mei | 16,748 | 12,065 | 17,150 | 14,245 | 184 | 2,447 |
| Juni | 33,608 | 20,954 | 37,240 | 24,368 | 672 | 3,731 |
| Julai | 55,513 | 40,559 | 69,211 | 33,100 | 1,971 | 6,410 |
| Agosti | 59,635 | 36,394 | 65,903 | 34,257 | 3,384 | 7,144 |
| Septemba | 41,706 | 25,148 | 42,693 | 26,949 | 3,278 | 6,878 |
| Oktoba | 39,537 | 23,467 | 43,396 | 25,921 | 5,967 | 8,152 |
| Novemba | 23,507 | 18,102 | 24,378 | 19,167 | 4,754 | 7,494 |
| Desemba | 35,289 | 27,720 | 36,601 | 27,767 | 10,126 | 22,982 |
| Jumla | **410,574** | **268,880** | **445,283** | **279,255** | **122,228** | **125,953** |

**Chanzo**: Wizara ya Maliasili na Utalii

293. Mwaka 2020, Idadi ya hifadhi za Taifa iliongezeka na kufikia hifadhi 22 ikilinganishwa na hifadhi 16 mwaka 2019. Hii ilitokana na kuongezwa kwa hifadhi mpya za Burigi Chato, Ibanda Kyerwa, Kigosi, Nyerere, Rumanyika Karagwe na Ugalla. Katika kipindi hicho, Serikali iliendelea kuboresha miundombinu ndani ya maeneo ya Hifadhi za Taifa kwa kujenga kivuko cha kubeba watalii katika Hifadhi ya Taifa iliyopo Kisiwa cha Rubondo na hoteli ya kitalii yenye hadhi ya nyota tatu (3) katika eneo la Rubambagwe - Chato. Aidha, Serikali ilianzisha mazao mapya ya utalii pamoja na kukarabati na kujenga maeneo ya malazi katika Hifadhi za Taifa za Saadani, Tarangire na Mkomazi.

294. Mwaka 2020, Serikali iliendelea kutangaza vivutio mbalimbali vya utalii ndani na nje ya nchi kwa: kuboresha *channel* maalum iitwayo *Tanzania Safari Channel*; kutumia watu maarufu, mabalozi wa hiari na Ofisi za Balozi zetu nje ya nchi; kushiriki katika maonesho ya utalii ya Marekani (New York Times), Jamhuri ya Czech (GO International Tourism Fair-Brno), Uholanzi (Vakantiebeurs) na Uholanzi (Utrecht) Januari 2020; kushiriki maonesho ya Ubelgiji (Holiday Fair) , Afrika Kusini (Meetings Africa) na Uganda (Pearl of Africa Tourism Expo) Februari 2020. Aidha, Serikali kupitia Bodi ya Utalii iliendelea kutoa elimu ya masuala ya utalii kupitia matamasha, matukio ya michezo na maonesho mbalimbali yakiwemo Serengeti Marathon, Kilimanjaro Marathon, Ngorongoro Marathon na Selous Marathon; Onesho la SITE; Sabasaba; Nanenane; Karibu Kusini, Kumbukizi ya Vita vya Majimaji; Onesho la Utalii Nyasa na Onesho la Utalii Hydom. Vile vile, Serikali kwa kushirikiana na shirika la

USAID la Marekani ilikamilisha maandalizi ya video mpya ijulikanayo kama *Tanzania Unforgettable* itakayotumika kutangaza na kutambulisha vivutio vya utalii na fursa nyingine zilizopo nchini

295. Mwaka 2020, Serikali iliendelea kukagua na kupanga huduma za malazi katika viwango vya ubora wa nyota (nyota 1 hadi 5) kwa kutumia vigezo vilivyowekwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mwaka 2020, jumla ya huduma za malazi 11 zilipangwa katika madaraja katika Mkoa wa Dodoma. Hatua hiyo imepelekea huduma za malazi zilizopangwa katika madaraja ya ubora nchini kuongezeka kutoka 297 za mwaka 2019 hadi kufikia 308 mwaka 2020. Huduma hii haikuweza kufanyika nchi nzima kutokana na athari za UVIKO 19.

**Malikale**

296. Mwaka 2020, wageni 44,488 wa ndani na nje ya nchi walitembelea vivutio vya malikale ikilinganishwa na wageni 86,095 waliotembelea vivutio hivyo mwaka 2019, sawa na upungufu wa 48.3. Hii ilitokana na kupungua kwa idadi ya watalii waliotembelea vivutio hivyo kutokana na athari za UVIKO-19. Aidha, mapato yaliyotokana na viingilio vya wageni katika vituo vya malikale yalipungua kwa asilimia 43.7 na kufikia shilingi milioni 128.7 mwaka 2020 ikilinganishwa na mapato ya shilingi milioni 228.4 za mwaka 2019**.**

**Jedwali Na. 12.5**: **Mapato Yatokanayo na Wageni Waliotembelea Vivutio vya Malikale**

| Kituo | Mwaka 2019 | | Mwaka 2020 | |
|---|---|---|---|---|
| | Wageni | Mapato (shilingi) | Wageni | Mapato (shilingi) |
| Magomeni | 38 | 94,000 | 102 | 38,940 |
| Kaole | 34,226 | 70,863,000 | 12,400 | 25,000,000 |
| Isimila | 2,520 | 7,476,000 | 4,754 | 10,429,860 |
| Mji Mkongwe | 18,392 | 50,793,624 | 9,573 | 21,602,000 |
| Kalenga | 2,258 | 4,579,300 | 945 | 1,797,020 |
| Kilwa | 3,813 | 33,389,000 | 2,994 | 26,848,000 |
| Mbozi | 3,441 | 6,359,460 | 2,008 | 4,516,290 |
| Amboni | 9,537 | 16,627,000 | 5,019 | 17,736,827 |
| Tongoni | 238 | 880,000 | 102 | 400,000 |
| Ujiji | 3,429 | 9,237,340 | 2,699 | 7,627,340 |
| Kwihara | 506 | 919,000 | 190 | 251,000 |
| Kolo | 2,765 | 17,543,000 | 2,319 | 9,390,000 |
| Caravan Serai | 4,932 | 9,660,160 | 1,383 | 3,059,740 |
| **Jumla** | **86,095** | **228,420,884** | **44,488** | **128,697,017** |

**Chanzo**: Wizara ya Maliasili na Utalii

297. Mwaka 2020, wageni 65,989 (ndani ya nchi 11,869 na nje ya nchi 54,120) walitembelea vituo vya Makumbusho ya Taifa ikilinganishwa na wageni 67,382 (ndani

ya nchi 52,697 na nje ya nchi 14,685) mwaka 2019. Katika kipindi hicho, mapato yaliyotokana na viingilio vya wageni katika Makumbusho ya Taifa yalipungua kwa asilimia 44.7 na kufikia shilingi milioni 269.6 ikilinganishwa na shilingi milioni 487.3 mwaka 2019.

**Jedwali Na. 12.6: Mapato Yatokanayo na Wageni Waliotembelea Vivutio vya Makumbusho**

| Kituo | 2019 | | | | 2020 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Nje ya nchi** | **Ndani ya nchi** | **Jumla** | **Mapato** | **Nje ya nchi** | **Ndani ya nchi** | **Jumla** | **Mapato** |
| Makumbusho na Nyumba ya Utamaduni | 8,497 | 15,769 | 24,266 | 323,779,084 | 11,170 | 4,858 | 16,028 | 64,711,044 |
| Kijiji cha Makumbusho | 3,378 | 8,363 | 11,741 | 76,829,500 | 8,925 | 3,660 | 12,585 | 51,229,577 |
| Makumbusho ya Azimio la Arusha | 327 | 5,594 | 5,921 | 19,133,900 | 1,274 | 84 | 1,358 | 5,392,587 |
| Makumbusho ya Elimu Viumbe | 2,322 | 6,252 | 8,574 | 46,696,700 | 9,565 | 3,053 | 12,618 | 53,925,869 |
| Makumbusho ya Mwalimu Nyerere | 100 | 9,104 | 9,204 | 12,452,850 | 6,008 | 36 | 6,044 | 24,266,642 |
| Makumbusho ya Vita ya Majimaji | 61 | 7615 | 7,676 | 8,424,000 | 17,178 | 178 | 17,356 | 70,103,631 |
| **Jumla** | **14,685** | **52,697** | **67,382** | **487,316,034** | **54,120** | **11,869** | **65,989** | **269,629,350** |

**Chanzo**: Wizara ya Maliasili na Utalii

**IDADI YA WAGENI WALIOTEMBELEA HIFADHI ZA TAIFA NA MAPATO YALIYOPATIKANA**

Jedwali Na. 41

| Mwaka | Idadi ya Watalii | | | Mapato (Tshs.) |
|---|---|---|---|---|
| | Nje | Ndani | Jumla | |
| 2015 | 432,124 | 526,110 | 958,234 | 149,957,485,000 |
| 2016 | 439,119 | 518,457 | 957,576 | 175,089,696,000 |
| 2017 | 386,529 | 595,811 | 982,340 | 207,587,218,000 |
| 2018 | 726,003 | 442,543 | 1,168,546 | 214,486,751,736 |
| 2019 | 763,276 | 494,676 | 1,257,952 | 292,539,502,030 |
| 2020 | 218,310 | 288,867 | 507,177 | 85,614,710,442 |
| **JUMLA KUU** | **2,965,361** | **2,866,464** | **5,831,825** | **1,125,275,363,208** |

**Chanzo**: Wizara ya Maliasili na Utalii, Makumbusho ya Taifa

**MAUZO YA BIDHAA ZA MISITU KATIKA MASOKO YA NJE – 2020**

Jedwali Na. 42

| Zao | Kiasi | | Thamani (Dola za Marekani) |
|---|---|---|---|
| | Uzito (kg) | Ujazo (Mita za Ujazo) | |
| Mbao | - | 69,198 | 34,598,998 |
| Maji/Utomvu wa Miwati | 1,834,821 | - | 3,302,678 |
| Vinyago | 8,815 | - | 102,073 |
| Mbao za Mpingo (Clarinets) | - | 74 | 368,805 |
| Mafuta ya Msandali | 3,075 | - | 922,500 |
| Utomvu wa Misindano | 131,285 | - | 170,670 |
| Nguzo za Umeme | - | 994 | 218,789 |
| Unga wa Ubuyu | 61,188 | - | 4,895 |
| Gundi ya Arabika | 103,740 | - | 36,309 |
| Fito (Withies) | 112,179 | - | 112,179 |
| Venia (Veneer) | - | 13,752 | 2,750,400 |
| Mafuta ya Msambu | - | 83,800 | 46,090 |
| Mbao zilizogundishwa (Plywood) | - | 6,776 | 2,371,583 |
| Asali | 1,406,883 | - | 7,034,415 |
| Nta | 17,750 | - | 136,320 |
| Ukwaju | 70,000 | - | 7,000 |
| Vikapu | 919 | - | 13,778 |
| Dawa za asili | 2,250 | - | 11,250 |
| Vifaa vya kuchonga (Hand crafts) | 4,089 | - | 81,776 |
| Mkaa endelevu (Briquettes) | 49,720 | - | 12,927 |
| Mazao mengine | 17,707 | - | 914,620 |
| **Jumla** | **3,824,419** | **174,594** | **53,218,053** |

**Chanzo:** Wizara ya Maliasili na Utalii

-Takwimu hazikupatikana

Jedwali Na. 43 **IDADI YA WATALII NA MAPATO YATOKANAYO NA UWINDAJI WA KITALII**

| Mwaka | Idadi ya Watalii | | | Mapato (Shs.) |
|---|---|---|---|---|
| | Wawindaji | Watazamaji | Jumla | |
| 2015 | 608 | 393 | 1,001 | 28,802,391,200.00 |
| 2016 | 495 | 297 | 792 | 29,136,885,800.00 |
| 2017 | 473 | 291 | 764 | 19,202,957,607.00 |
| 2018 | 503 | 280 | 783 | 20,109,785,000.00 |
| 2019 | 519 | 483 | 1,002 | 20,864,030,536.00 |
| 2020 | 251 | 185 | 436 | 15,590,640,205 |
| **Jumla Kuu** | **2,849** | **1,929** | **4,778** | **133,706,690,348.00** |

**Chanzo:** Wizara ya Maliasili na Utalii, Idara ya Wanyamapori

**MWENENDO WA BIASHARA YA UTALII 2013-2020**

Jedwali Na. 44

| **Maelezo** | **Kipimo** | **2013** | **2014** | **2015** | **2016** | **2017** | **2018** | **2019[r]** | **2020** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Jumla ya Watalii | Idadi | 1,095,884 | 1,140,156 | 1,137,182 | 1,284,279 | 1,327,143 | 1,505,702 | 1,527,230 | 620,867 |
| Watalii wa hotelini | Idadi | 1,021,766 | 1,005,058 | 1,033,555 | 1,155,851 | 1,163,752 | 1,404,672 | 1,353,279 | 563,779 |
| Mapato | US $ Milion | 1,853 | 1,983 | 1,902 | 2,132 | 2,200 | 2,433 | 2,604 | 715 |
| Wastani wa siku za kukaa watalii hotelini | Siku | 10 | 10 | 10 | 10 | 9 | 10 | 13 | 10 |
| Wastani wa matumizi ya fedha kwa mtalii kwa siku (US $) | *Package Tour* | 372 | 378 | 305 | 351 | 410 | 331 | 379 | 312 |
| | *Non - Package Tour* | 201 | 210 | 141 | 145 | 136 | 135 | 216 | 115 |

**Chanzo**: Wizara ya Maliasili na Utalii, Idara ya Utalii
r-Takwimu zimeboreshwa

## WATALII WALIOTEMBELEA MAMLAKA YA HIFADHI YA NGORONGORO

Jedwali Na. 45

| Mwaka | Wageni kutoka Nje | Watanzania | Jumla ya Watalii |
|---|---|---|---|
| 2010 | 281,513 | 242,133 | 523,646 |
| 2011 | 281,513 | 307,086 | 588,599 |
| 2012 | 310,537 | 254,730 | 565,267 |
| 2013 | 350,970 | 296,763 | 647,733 |
| 2014 | 332,469 | 278,221 | 610,690 |
| 2015 | 289,061 | 278,922 | 567,983 |
| 2016 | 284,794 | 265,845 | 550,639 |
| 2017 | 391,030 | 249,428 | 640,458 |
| 2018 | 410,574 | 268,880 | 679,454 |
| 2019 | 445,283 | 279,255 | 724,538 |
| 2020 | 122,228 | 125,953 | 248,181 |

**Chanzo**: Wizara ya Maliasili na Utalii, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro

# SURA YA 13

# MADINI

## Utafutaji Madini

298. Mwaka 2020, leseni 4,978 za utafutaji wa madini, uchimbaji wa kati, uchimbaji mdogo, uchenjuaji, uyeyushaji na usafishaji wa madini zilitolewa ikilinganishwa na leseni 3,002 zilizotolewa mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 65.8. Ongezeko hilo lilitokana na maboresho ya Sheria ya Madini, kuendelea kutoa elimu kwa wadau hasa kwa wachimbaji wadogo na kuboreshwa kwa taratibu za upatikanaji wa leseni za madini. Kati ya leseni zilizotolewa, leseni 111 zilikuwa za utafutaji wa madini, leseni 19 za uchimbaji wa kati, leseni 4,815 za uchimbaji mdogo, leseni 29 za uchenjuaji wa madini, leseni mbili (2) za uyeyushaji madini na leseni mbili (2) za usafishaji wa madini. Aidha, maombi 11,161 ya leseni mbalimbali za madini yaliidhinishwa mwaka 2020 ikilinganishwa na maombi 8,801 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 26.8. Ongezeko hilo lilitokana na mwamko wa uwekezaji katika utafutaji madini hususan uchimbaji mdogo na wa kati pamoja na uwepo wa masoko ya madani uliosababisha kuongezeka kwa maombi ya leseni za biashara ya madini.

## Vibali vya Uuzaji wa Madini

299. Mwaka 2020, madini yaliyopata vibali vya kuuzwa nje ya nchi yalikuwa na thamani ya dola za Marekani milioni 3,310.7 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 2,280.5 mwaka 2019, sawa na ongezeko asilimia 45.2. Hii ilitokana na kuimarika kwa usimamizi na udhibiti wa biashara ya madini pamoja na kuongezeka kwa uzalishaji wa madini hususan dhahabu na vito vya thamani.

## Dhahabu

300. Mwaka 2020, uzalishaji wa dhahabu ulifikia kilogramu 55,805 ikilinganishwa na kilogramu 48,408 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 15.3. Hii ilitokana na kuimarika kwa usimamizi wa biashara ya madini, udhibiti wa utoroshaji na biashara haramu ya madini katika maeneo ya uzalishaji na uchenjuaji hususan kwa wachimbaji wadogo na wa kati na uwepo wa masoko na vituo vya ununuzi na uuzaji wa madini. Aidha, kilogramu 49,812 za dhahabu zilipata vibali vya kusafirishwa nje ya nchi mwaka 2020 ikilinganishwa na kilogramu 42,108 zilizopata vibali mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 18.3. Thamani ya dhahabu iliyopata vibali vya kuuzwa nje ya nchi kwa mwaka 2020 iliongezeka kwa asilimia 49.4 na kufikia dola za Marekani milioni 2,845.0 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,904.1 mwaka 2019. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa dhahabu, kuendelea kutoa elimu kuhusu sheria, kanuni na taratibu na kuimarika kwa bei ya dhahabu katika soko la dunia. Katika kipindi hicho, wastani wa bei ya dhahabu katika soko la dunia ilikuwa dola za Marekani

1,769.6 kwa wakia moja ikilinganishwa na dola za Marekani 1,392.6 kwa wakia moja kwa mwaka 2019

**Almasi**

301. Mwaka 2020, uzalishaji wa madini ya almasi ulikuwa karati 147,191 zenye thamani ya dola za Marekani milioni 20.1 ikilinganishwa na karati 416,749.5 zenye thamani ya dola za Marekani milioni 89.3 mwaka 2019, sawa na upungufu wa uzalishaji kwa asilimia 64.7. Upungufu huo ulisababishwa na mgodi wa Kampuni ya Williamson's Diamond Limited kusitisha uzalishaji kutokana na kushuka kwa bei ya almasi katika soko la dunia. Aidha, wastani wa bei ya almasi katika soko la dunia ilikuwa dola za Marekani 136.6 kwa karati moja mwaka 2020 ikilinganishwa na dola za Marekani 214.3 kwa karati moja kwa mwaka 2019.

**Vito vya Thamani**

302. Mwaka 2020, uzalishaji wa vito vya thamani (isipokuwa Tanzanite na Almasi) ulikuwa kilogramu 23,564,525 ikilinganishwa na kilogramu 1,929,714 zilizozalishwa mwaka 2019. Kiasi hicho kinajumuisha madini mbalimbali yakiwemo *spinel, chrysoprase ruby, sapphire, garnets, moonstones, sunstones na tourmaline*. Ongezeko la uzalishaji wa vito vya thamani ulitokana na uzalishaji mkubwa wa madini ya vito yenye ubora wa chini (Low grade) pamoja na kuendelea kutoa elimu kuhusu sheria, kanuni na taratibu zinazosimamia sekta ya madini.

**Tanzanite**

303. Mwaka 2020, uzalishaji wa madini ya *Tanzanite* ghafi ulikuwa kilogramu 51,542 ikilinganishwa na kilogramu 2,772.2 mwaka 2019. Kuimarika kwa uzalishaji kulitokana na kuongezeka kwa wazalishaji wa Tanzanite ghafi, kujumuisha kiwango cha ubora wa kati na cha chini wa madini ya Tanzanite na kuendelea kuimarika kwa udhibiti wa madini kutokana na kuwepo kwa ukuta wa Mirerani.

304. Mwaka 2020, karati 118,773 za madini ya Tanzanite yenye thamani ya dola za Marekani milioni 10.9 yalikatwa na kusanifiwa ikilinganishwa na karati 160,387 zenye thamani ya dola za Marekani milioni 12.6 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 25.9. Upungufu huo ulitokana na kushuka kwa bei ya madini ya vito katika soko la dunia kulikosababishwa na kusitishwa kwa shughuli za kiuchumi kufuatia mlipuko wa UVIKO-19.

**Makaa ya Mawe**

305. Mwaka 2020, uzalishaji wa makaa ya mawe ulikuwa tani 689,959 ikilinganishwa na tani 712,136.4 zilizozalishwa mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 3.1. Upungufu huo ulitokana na wachimbaji wakubwa wa makaa ya mawe kupunguza uzalishaji kutokana na janga la UVIKO-19. Aidha, thamani ya makaa ya

mawe yaliyozalishwa ilikuwa shilingi bilioni 204.6 mwaka 2020 ikilinganishwa na shilingi bilioni 116.7 mwaka 2019.

**Madini Mengine**

306. Mwaka 2020, uzalishaji wa madini ya fedha ulikuwa kilogramu 13,187 ikilinganishwa na kilogramu 12,550 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 5.1. Madini ya fedha yaliyopata vibali vya mauzo nje yalikuwa na thamani ya dola za Marekani milioni 8.8 mwaka 2020 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 6.5 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 35.4. Aidha, uzalishaji wa madini ya bati ulikuwa tani 47.0 mwaka 2020 ikilinganishwa na tani 24.3 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 93.4. Jumla ya vibali 12 vyenye thamani ya shilingi bilioni 1.1 vilitolewa kwa ajili ya mauzo ya madini ya bati nje ya nchi mwaka 2020 ikilinganishwa na vibali 10 vyenye thamani ya shilingi milioni 414.7 mwaka 2019.

307. Mwaka 2020, Uzalishaji wa madini ya jasi ulikuwa tani 443,926 ikilinganishwa na tani 256,529 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 73.1. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya madini hayo katika nchi jirani. Katika kipindi hicho, vibali 86 vyenye thamani ya dola za Marekani milioni 0.45 vilitolewa kwa ajili ya uuzaji wa tani 4,252 za madini ya jasi nje ya nchi ikilinganishwa na vibali 41 vyenye thamani ya dola za Marekani milioni 0.32 kwa ajili ya uuzaji wa tani 2,916 mwaka 2019.

**Madini Ujenzi**

308. Mwaka 2020, tani 38,300.4 za madini ujenzi zenye thamani ya shilingi bilioni 591.2 zilizalishwa ikilinganishwa na tani 30,206.4 zenye thamani shilingi bilioni 477.36 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 27.0. hii ilitokana na kuongezeka kwa shughuli za ujenzi na utekelezaji wa miradi ya kimkakati ikiwemo mradi wa Kufua Umeme wa Julius Nyerere, ujenzi wa bandari, viwanja vya ndege na Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa.

**Masoko ya Madini**

309. Mwaka 2020, Serikali iliendelea kusimamia uendeshaji wa masoko na vituo vya madini ili kuhakikisha yanafanya kazi kwa ufanisi. Katika kipindi hicho, kulikuwa na masoko ya madini 39 na vituo vya ununuzi wa madini 41 ikilinganishwa na masoko 30 na vituo 27 mwaka 2019. Jumla ya tani 15.5 za madini ya dhahabu zenye thamani ya shillingi trilioni 1.78 ziliuzwa katika masoko hayo mwaka 2020 ikilinganishwa na tani 8.9 zenye thamani ya shillingi bilioni 844.0 mwaka 2019. Aidha, jumla ya karati 15,426.7 za madini ya almasi zenye thamani ya shillingi bilioni 6. 5 ziliuzwa katika masoko mwaka 2020 ikilinganishwa na karati 12,055.5 zenye thamani ya shillingi bilioni 6.3 mwaka 2019. Vile vile, jumla ya tani 1,062.8 za vito ghafi na vito vilivyoongezewa thamani karati 137,756.9 zenye jumla ya thamani ya shillingi bilioni 43.9 ziliuzwa katika masoko ya madini mwaka 2020 ikilinganishwa na tani 1,064.4 ya

vito ghafi na karati 96,512.3 za vito vilivyoongezewa thamani vyenye thamani ya shillingi bilioni 48.1 mwaka 2019. Kadhalika, jumla ya tani 47.5 za madini ya bati zenye thamani ya shillingi  bilioni 1.1 ziliuzwa katika masoko hayo mwaka 2020 ikilinganishwa na tani 20.7 zenye thamani ya shillingi milioni 456.1 mwaka 2019. Katika kipindi hicho,shilingi bilioni 109.4 zilikusanywa kama mrabaha na shilingi bilioni 18.3 zilikusanywa kama ada ya ukaguzi wa madini katika masoko na vituo hivyo.

Jedwali Na.46

## UCHIMBAJI WA MADINI: KIASI KILICHOPATIKANA

| MADINI | Kipimo | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Almasi | Carat | 252,875 | 216,491 | 237,685 | 304,456 | 381,302 | 416,750 | 147,191 |
| Dhahabu | Kg | 40,481 | 43,293 | 45,155 | 43,490 | 39,304 | 48,408 | 55,805 |
| Tanzanite ghafi | | | | | | | | 51,542 |
| Tanzanite (iliyochakatwa) | | | | | | | | 118,773 |
| Gemstones | Kg | 3,083,765 | 1,872,915 | 2,554,932 | 1,185,697 | 284,321 | 1,929,714 | 23,564,525 |
| Chumvi | Tani | 54,757 | 92,158 | 145,718 | 100,017 | 36,392 | 99,510 | 83,974 |
| Phosphate | Tani | 738,000 | 222,800 | 23,658 | 1,351 | - | - | 28,376 |
| Limestone | 000 Tani | 873 | 2,945 | 4,170 | 3,301 | 2,944 | 5,527 | 6,788 |
| Tin Ore | Tani | 79 | 179 | 138 | 91 | 8 | 24 | 47 |
| Gypsum | Tani | 200,179 | 239,302 | 213,744 | 123,645 | 241,260 | 256,529 | 443,926 |
| Makaa ya mawe | Tani | 246,128 | 257,321 | 276,030 | 563,053 | 627,652 | 712,136 | 689,959 |
| Pozolana | Tani | 68,925 | 342,628 | 230,045 | 79,085 | 91,645 | 263,064 | 160,078 |
| Kaolin | Tani | 3,809 | 1,953 | 656 | 13,816 | 129,383 | 15,343 | 98,454 |
| Madini ya fedha | Kg | 14,493 | 15,569 | 17,984 | 10,911 | 12,041 | 12,550 | 13,187 |
| Shaba | Pound | 14,027,008 | 14,252,341 | 15,762,430 | 2,933,941 | - | - | 3,761,086 |
| Chuma | Tani | | | | | | | 28,431 |
| Bauxite | Tani | 25,641,201 | 204,956 | 72,779 | 12,090 | 7,140 | - | 25,995 |
| Madini ya Ujenzi | 000 Tani | 10,480 | 12,960 | 15,460 | 5,601 | 10,375 | 20,188 | 31,892 |
| Madini mengine ya viwanda | | | | | | | | 2,161 |

**Chanzo**: Wizara ya Madini
- Takwimu hazikupatikana
Carat = 0.205 gm

Jedwali Na. 47

**THAMANI YA MADINI YALIYOTOLEWA VIBALI KWAAJILI YA KUUZWA NJE YA NCHI 2016- 2020**

| **Aina ya madin** | **Kipimo** | **Kiasi cha Madini** | | | | | **Thamani ('000 US $)** | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **2016** | **2017** | **2018** | **2019** | **2020** | **2016** | **2017** | **2018** | **2019** | **2020** |
| Almasi (Rough) | '000 Carats | 239,305 | 304,456 | 383,391 | 416,750 | 143,471 | 85,090 | 67,510 | 96,066 | 89,335 | 20,065 |
| Almasi (iliyokatwa) | '000 Carats | - | - | - | - | | - | - | - | - | |
| Almasi (Contruct goods) | '000 Carats | - | - | - | - | | - | - | - | - | |
| Dhahabu | '000 Gramu | 45,155 | 43,490 | 35,864 | 48,408 | 49,812 | 1,824,815 | 1,636,575 | 1,454,879 | 2,123,035 | 2,844,960 |
| *Germstones (Cut)* | | | | | | 128,461 | | | | | 19,215 |
| Mawe ya thamani | '000 Gramu | 2,944,107 | 1,185,697 | 284,321 | 761,814 | 1,435,273 | 60,483 | 53,596 | 28,006 | 27,314 | 19215 |
| Chumvi | Tani | 145,718 | 100,017 | 36,392 | 99,510 | | 4,806 | 3,803 | 1,207 | 5,576 | 1,927 |
| Phosphate | Tani | 23,658 | 1,351 | - | - | 14,241 | 721 | 585 | - | - | 1,945 |
| Bati | Tani | 138 | 91 | 8 | - | 41 | 1,499 | 1,037 | - | - | 420 |
| Jasi | Tani | 213,744 | 123,645 | 241,260 | 2,916 | 4,252 | 6,279 | 3,187 | - | 317 | 446 |
| Grafiti | Tani | 1,180 | 128 | 27,810 | 9,271 | 2,250 | 2,132 | 18 | 2,418 | 4,420 | 1,071 |
| Fedha | 000Grams | 17,984 | 10,911 | 12,041 | 12,550 | 13,187 | 9,901 | 5,850 | 6,045 | 6,537 | 8,748 |
| Shaba | 0001b | 16,247 | 2,934 | - | - | - | 35,421 | 7,741 | - | - | - |
| Makinikia ya shaba | | - | - | - | - | 38,683 | | | | | 346,673 |
| Madini ya viwandani | Tani | 4,769,577 | 708,047 | 783,180 | 336,844 | 7,419 | 78,491 | 29,896 | 35,783 | 23,994 | 374 |
| Bauxite | Tani | 74,660 | 12,090 | 7,140 | | 25,995 | 1,242 | 898 | 335 | - | 1,349 |
| Makaa ya mawe | Tani | | | | | 162,648 | | | | | 60,212 |
| Madini ya Ujenzi | Tani | | | | | 4,300,002,564 | | | | | 298,013 |
| Jumla ('000 US $) | | | | | | | 2,110,877 | 1,810,697 | 1,624,739 | 2,280,529 | 3,605,418 |

**Chanzo**: Wizara ya Madini

- Takwimu hazikupatikana

## SURA YA 14

## VIWANDA NA BIASHARA

**Uzalishaji wa Bidhaa Viwandani**

310. Mwaka 2020, uzalishaji wa baadhi ya bidhaa za viwandani uliongezeka kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na mwitikio wa wananchi kutumia bidhaa zinazozalishwa nchini. Bidhaa hizo ni pamoja na: biskuti na tambi (asilimia 23.8), nguo (asilimia 16.9), unga wa ngano (asilimia 12.8), betri (asilimia 10.0), bati (asilimia 6.8), chibuku (asilimia 6.7), dawa za pareto (asilimia 6.2), konyagi (asilimia 2.9), nyavu za uvuvi (asilimia 2.8), na chuma (asilimia 1.9). Kwa upande mwingine, uzalishaji ulipungua kwa bidhaa za tabaka la mbao (asilimia 19.56), rangi (asilimia 16.83), sigara (asilimia 12.53), kamba za katani (asilimia 11.84), bia (asilimia 1.39) na saruji (asilimia 0.28). Aidha, gharama za uzalishaji bidhaa viwandani ziliongezeka kwa asilimia 10.0 na kuwa shilingi bilioni 9,565.8 mwaka 2020 ikilinganishwa na shilingi bilioni 8,696.2 mwaka 2019. Hii illitokana na kuongezeka kwa bei za malighafi hususan zinazoagizwa kutoka nje ya nchi.

**Uendelezaji wa Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo**

311. Mwaka 2020, Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo - SIDO lilitoa mafunzo kwa wajasiriamali 19,036 ikilinganishwa na wajasiriamali 17,831 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 6.8. Ongezeko hilo lilitokana na mwamko wa wajasiriamali kutumia fursa mbalimbali ikiwemo zile zilizotokana na athari za UVIKO-19. Mafunzo yaliyotolewa yalihusu: utengenezaji wa vifaa na vitakasa mikono kwa ajili ya kujikinga na maambukizi ya UVIKO-19; usindikaji wa mazao ya kilimo; utengenezaji wa bidhaa za ngozi; usindikaji wa mazao ya nyuki; ubunifu wa mavazi na ushonaji; njia za kuzuia upotevu wa mazao kabla na baada ya kuvuna; na utengenezaji wa mashine, zana na bidhaa mbalimbali.

312. Mwaka 2020, Serikali kupitia vituo vya maendeleo ya teknolojia vilivyo chini ya SIDO ilitengeneza na kusambaza mashine 509 ikilinganishwa na mashine 338 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 50.6. Ongezeko hilo lilichangiwa na uhitaji wa mashine na vifaa mbalimbali kwa ajili ya: kujikinga na maambukizi ya UVIKO-19; kusindika mazao ya kilimo, mifugo na bidhaa zake; uvunaji na uhifadhi wa mazao; kupunguza matumizi ya miti na mazao yake kama vyanzo vya nishati; kufungashia vyakula vilivyosindikwa; na kutengeneza matofali.

313. Mwaka 2020, Serikali kupitia Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Wajasiriamali ilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 6.3 ikilinganishwa na shilingi bilioni 5.4 zilizotolewa mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 17.9. Aidha, wajasiriamali 2,862 walinufaika na mikopo iliyotolewa mwaka 2020 ikilinganishwa na wajasiriamali

2,763 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 3.6. Ongezeko hilo lilitokana na fursa iliyojitokeza ya uhitaji wa mashine na vifaa vya kujikinga na maambukizi ya UVIKO-19. Mikopo iliyotolewa iliwezesha upatikanaji wa fursa za ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja 8,264 mwaka 2020 ikilinganishwa na fursa 7,594 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 8.8.

314. Mwaka 2020, Serikali kupitia Chuo cha Elimu ya Biashara - CBE ilitoa huduma za mafunzo kwa wajasiriamali wadogo 465 ikilinganishwa na wajasiriamali 98 waliopatiwa mafunzo mwaka 2019. Ongezeko lilitokana na maboresho yaliyofanywa na Chuo kwa kuongeza aina mbalimbali za mafunzo ikiwemo udhibiti wa bidhaa zilizofungashwa na mizani za kieletroniki. Aidha, Chuo kilifanya tafiti mbili (2) na kutoa machapisho ya kitaaluma 92 katika nyanja za uchumi, teknolojia ya habari na mawasiliano, biashara na ujasiriamali ikilinganishwa na tafiti nane (8) na machapisho ya kitaaluma 56 mwaka 2019. Upungufu wa tafiti na machapisho ulitokana na ukosefu wa fedha kutoka kwa wadau wa maendeleo uliosababishwa na athari za UVIKO-19.

315. Mwaka 2020, Serikali kupitia Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania - *TanTrade* iliratibu programu 13 za mafunzo ya biashara ambapo wadau 3,223 kutoka sekta mbalimbali walishiriki ikilinganishwa na programu 12 za mafunzo kwa wadau 1,897 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 69.9. Ongezeko la wadau walioshiriki lilitokana na mwamko wa wajasiriamali kushiriki katika mafunzo ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi. Mafunzo yaliyotolewa yalihusu mbinu za upatikanaji wa masoko na ubora wa bidhaa zinazozalishwa nchini, uendeshaji wa biashara, uboreshaji wa bidhaa za kampuni shiriki, kupunguza upotevu wa mazao ya kilimo baada ya kuvuna, kujenga uelewa juu ya usafirishaji na kubainisha nyaraka muhimu zinazohitajika kwa biashara ya mazao.

316. Mwaka 2020, Mamlaka iliratibu utoaji wa huduma ya kliniki ya biashara kwa wafanyabiashara 566 ikilinganishwa na wafanyabiashara 593 waliopata huduma mwaka 2019. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na: utatuzi wa changamoto za kibiashara 161; wafanyabiashara 34 kupata mitaji yenye thamani ya shilingi milioni 700 kutoka benki ya NBC; wafanyabiashara 43 wa bidhaa za nafaka, matunda, kahawa, chai na viungo kuunganishwa na wanunuzi wa ndani na nje ya nchi; wafanyabiashara 49 kupata elimu juu ya taratibu za ulipaji kodi; na wafanyabiashara saba (7) kusajili majina ya biashara.

317. Mwaka 2020, Serikali kupitia Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania – TIRDO ilitoa mafunzo kwa wajasiriamali na wafugaji 450 wa wilaya za Meru, Monduli na Longido. Mafunzo yaliyotolewa yalihusu uongezaji thamani katika zao la uyoga na teknolojia ya uhifadhi bora wa ngozi za wanyama pasipo kutumia kemikali. Kupitia mafunzo hayo, ngozi 3,404 za wanyama zenye ubora zilizalishwa.

318. Mwaka 2020, TIRDO ilihaulisha matokeo ya tafiti saba (7) ikilinganishwa na matokeo ya tafiti tatu (3) mwaka 2019. Matokeo ya tafiti hizo yalihusu teknolojia za: uboreshaji na uhifadhi wa ngozi ambapo wafugaji 400 walipewa mafunzo na ngozi 3,250 zilisindikwa; uongezaji thamani katika zao la mwani ambapo kaushio la ukubwa wa mita saba (7) kwa nne (4) lilijengwa kisiwani Pemba na mashine yenye uwezo wa kusaga kilo 400 za mwani kwa siku ilitengenezwa; uongezaji thamani kwa mazao ya nafaka na muhogo ambapo kaushio bora la unga wa muhogo na nafaka la uwezo wa kukausha kilo 1,500 lilijengwa katika wilaya ya Chamwino, Dodoma; kutengeneza vitofali lishe vya kuzalishia uyoga na uongezaji thamani katika zao la uyoga ambapo kampuni ya *OKOA Enterprises Limited* iliyopo Kihonda, Morogoro ilipewa mafunzo na kuanza uzalishaji; kuzalisha tofali za makaa ya mawe (briketi) ambapo mashine ya kuzalisha briketi kwa ajili ya kupikia majumbani ilitengenezwa kwa ushirikiano na Shirika la Nyumbu; na utengenezaji wa vitakasa mikono ambapo lita 41,500 zilizalishwa na kuuzwa kwa Mkemia Mkuu, bohari ya dawa, mashirika/taasisi pamoja na watu binafsi.

319. Mwaka 2020, Serikali kupitia Shirika la Uhandisi na Usanifu Mitambo Tanzania - TEMDO ilitoa mafunzo kwa wahandisi wahitimu 10 na wanafunzi wahandisi 19 wa mafunzo kwa vitendo ikilinganishwa na wahandisi wahitimu watatu (3) na wanafunzi wahandisi nane (8) mwaka 2019. Ongezeko la wahandisi waliopata mafunzo lilitokana na Shirika kujitangaza zaidi kuhusu majukumu na uwezo wa kutoa mafunzo kupitia mitandao ya kijamii. Aidha, Shirika lilitoa mafunzo ya kihandisi kwa wahandisi 12 kutoka taasisi za *Gas Company Tanzania Limited* na Shirika la Viwango Tanzania. Vile vile, Shirika lilitoa huduma za kihandisi katika viwanda saba (7) mwaka 2020 ikilinganishwa na viwanda vitano (5) mwaka 2019.

320. Mwaka 2020, Shirika lilisanifu teknolojia zilizowezesha kutengeneza mashine 10 za kuzalisha bidhaa za viwanda ikilinganishwa na mashine sita (6) mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 66.7. Ongezeko lilitokana na Serikali kuliwezesha Shirika kununua mashine za kisasa za Computer *Numerical Control (CNC)* ambazo ziliiwezesha kufanya kazi kwa ubora, ufanisi na haraka. Katika kipindi hicho, mashine zilizotengenezwa ni pamoja na: mfumo wa kupooza malighafi ya *gypsum board* katika kiwanda cha *St. Gobain Lodhia Industries* Arusha; mitambo ya kuteketeza taka ngumu za hospitali; mfumo wa kuondoa vumbi katika kiwanda cha *Minjingu mines;* mashine za kukamua juisi ya zabibu; mtambo wa kukausha mazao ya muhogo; mashine ya briketi kutokana na vumbi la makaa ya mawe na mabaki ya bidhaa za kilimo.

321. Mwaka 2020, Serikali kupitia Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini - CAMARTEC ilitoa mafunzo ya ujenzi wa mitambo ya biogesi kwa vijana 181 (wanawake 65 na wanaume 116) ikilinganishwa na vijana wanawake 69 mwaka 2019. Aidha, CAMARTEC kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia

Mbeya - MUST na taasisi binafsi ya TAHUDE ilitoa mafunzo ya ujenzi wa mitambo ya biogesi kwa walimu 10 (wanawake 2 na wanaume 8) wa MUST kwa lengo la kuwajengea uwezo na ufahamu wa matumizi sahihi ya mbolea hai inayotoka kwenye mitambo hiyo.

322. Mwaka 2020, CAMARTEC ilifanya maboresho na kuzalisha aina 19 za teknolojia ikilinganishwa na aina 12 za teknolojia zilizoboreshwa na kuzalishwa mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 58.3. Aidha, teknolojia hizo ziliwezesha kutengenezwa kwa mashine 95 mwaka 2020 ikilinganishwa na mashine 52 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 82.7. Mashine zilizotengenezwa ni pamoja na: mashine 34 za kubangua korosho zinazoendeshwa kwa miguu; meza tatu (3) za kumenyea korosho zilizobanguliwa; meza tatu (3) za kupanga korosho zilizobanguliwa kwenye madaraja; mashine tano (5) za kukatakata malisho ya mifugo; mashine tatu (3) za kupukuchua mahindi; mizinga ya nyuki ya kisasa 20; mashine kumi za kukamua mafuta zinazoendeshwa kwa mkono; na matoroli sita (6) ya kubebea korosho viwandani.

323. Mwaka 2020, CAMARTEC ilifanya ukaguzi na majaribio ya aina tisa (9) za zana za kilimo kutoka nje ya nchi ikilinganishwa na majaribio ya aina 11 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 18.2. Baada ya majaribio, aina tano (5) zilithibitishwa na aina nne (4) hazikukidhi vigezo.

**Miundombinu ya Masoko ya Bidhaa za Mazao na Mifugo**

324. Mwaka 2020, Serikali kwa kushirikiana na Sekta binafsi iliendelea kuimarisha miundombinu ya masoko ya bidhaa za mazao na mifugo. Katika kipindi hicho, vituo vya kukusanyia maziwa viliongezeka na kufikia 244 kutoka 133 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 83.5. Aidha, minada ya mipakani iliongezeka na kufikia minada 11 kutoka minada 6 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 83.3. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya kilimo na mifugo na kuongezeka kwa uelewa wa wakulima na wafanyabiashara kuhusu umuhimu wa matumizi wa miundombinu hiyo.

**Jedwali Na.14.1: Mchanganuo wa Miundombinu ya Masoko Mwaka 2019-2020**

| Miundombinu ya Masoko | 2019 | 2020 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---:|---:|---:|
| Vibaraza vya Machinjio | 6,082 | 3,879 | -36.2 |
| Bucha | 9,546 | 9,676 | 1.4 |
| Banda la ngozi | 226 | 199 | -11.9 |
| Nyumba za Machinjio | 566 | 283 | -50.0 |
| Maghala | 678 | 455 | -32.9 |
| Machinjio | 78 | 74 | -5.1 |
| Minada ya Awali | 330 | 260 | -21.2 |
| Minada ya Upili | 17 | 20 | 17.6 |
| Minada ya Mipakani | 6 | 11 | 83.3 |
| Mashine za Kuchakata Nyama | 84 | 113 | 34.5 |
| Mashine za Kuchakata Maziwa | 30 | 39 | 30.0 |
| Mashine za Kuchakata Samaki | 13 | 16 | 23.1 |
| Vituo vya Kukusanyia Maziwa | 133 | 244 | 83.5 |

**Chanzo**: Wizara ya Viwanda na Biashara - *Agricultural Routine Data System*

### Usajili wa Biashara na Viwanda

325. Mwaka 2020, Serikali kupitia Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni - BRELA ilisajili kampuni 9,236 ikilinganishwa na kampuni 8,846 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 4.4. Aidha, majina ya biashara 18,555 yalisajiliwa mwaka 2020 ikilinganishwa na majina 14,764 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 25.7. Ongezeko hilo lilitokana na juhudi za Serikali kuendelea kuboresha mazingira ya biashara nchini ikiwemo kufuta na kupunguza viwango vya baadhi ya tozo katika sekta mbalimbali za kiuchumi. Vile vile, Wakala ilitoa leseni 11,105 za biashara za kundi A na leseni za viwanda 195 mwaka 2020 ikilinganishwa na leseni 12,571 kundi A na leseni za viwanda 240 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 11.7 na asilimia 18.8 mtawalia. Upungufu huo ulitokana na kusitishwa kwa shughuli za kiuchumi na baadhi ya wafanyabiashara kutohuisha leseni kutokana na athari za janga la UVIKO – 19 hususan kwa biashara zinazomilikiwa na wageni, biashara za uagizaji wa bidhaa kutoka nje na biashara zinazohudumia watalii.

326. Mwaka 2020, Wakala ilisajili alama za biashara na huduma 3,808 ikilinganishwa na alama za biashara na huduma 2,476 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 53.8. Ongezeko hilo lilitokana na Wakala kuendelea kuhamasisha uwasilishaji wa maombi hayo pamoja na kupokea sajili zilizofanyika kupitia Shirika la Kanda la Afrika linalosimamia Haki Miliki za Kitaaluma (African Regional Intellectual Property Organization – ARIPO). Aidha, Wakala ilipokea maombi 73 ya kuwekea ulinzi uvumbuzi wa sayansi na teknolojia (hataza) mwaka 2020 ikilinganishwa na maombi 59 mwaka 2019. Kati ya maombi ya hataza yaliyopokelewa, hataza 2 ziliridhiwa, maombi ya hataza 60 yalirudishwa kwa waombaji kwa ajili ya kurekebishwa na maombi ya hataza 11 yalikataliwa. Sababu za kurudishwa kwa wateja zilitokana na maandalizi hafifu ya nyaraka na baadhi ya maombi kutokidhi vigezo vya kivumbuzi. Katika kipindi hicho wafanyabiashara 500 wanaofanya biashara nje ya nchi walisajiliwa kwenye kanzidata ya wafanyabiashara ikilinganishwa wafanyabiashara 50 waliosajiliwa mwaka 2019.

### Maonesho ya Kibiashara ya Kimataifa

327. Mwaka 2020, Serikali kupitia Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania - *TanTrade* iliratibu maonesho ya 44 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam ambapo kampuni 2,837 za ndani na kampuni 43 za nje ya nchi zilishiriki ikilinganishwa na kampuni 3,250 za ndani na kampuni 520 za nje ya nchi zilizoshiriki maonesho ya 43 mwaka 2019. Aidha, nchi tano (5) zilishiriki katika maonesho ya mwaka 2020 ikilinganishwa na nchi 35 zilizoshiriki mwaka 2019. Upungufu wa washiriki ulitokana na kusitishwa kwa shughuli za kiuchumi katika baadhi ya nchi kulikosababishwa na athari za janga la UVIKO-19. Katika maonesho hayo: washiriki 60,000 walipata

huduma ya vitambulisho vya Taifa; ajira 15,912 za muda zilipatikana; pamoja na kutolewa kwa huduma za afya 2,050, huduma za kibenki 1,700, leseni za biashara 109, vitambulisho vya wajasiriamali wadogo saba (7) na leseni za vileo saba (7).

328. Mwaka 2020, Mamlaka iliratibu ushiriki wa Tanzania kwenye maonesho mawili (2) ya kimataifa yaliyofanyika mwezi Februari nchini Paris (Ufaransa) na (Ujerumani). Katika maonesho hayo, kampuni 15 za Tanzania zilipata fursa ya kushiriki katika kutangaza, kutafuta na kukuza masoko ya bidhaa mbalimbali zikiwemo nguo, vinywaji, mazao ya chakula, mbogamboga na matunda. Aidha, mikataba ya makubaliano isiyofungani ya uuzaji wa matunda na mbogamboga yenye thamani ya shilingi bilioni 8.37 ilisainiwa. Vile vile, kampuni ya Interstate ilipokea oda ya kilogramu 500 za kahawa za majaribio kutoka kampuni ya Hilton Paris Opera ya nchini Ufaransa.

329. Mwaka 2020, Mamlaka iliandaa na kuratibu Maonesho ya Tano ya Bidhaa za Viwanda vya Tanzania kwa lengo la kuongeza uelewa na hamasa ya kutumia bidhaa zinazozalishwa nchini yaliyofanyika Jijini Dar es salaam tarehe 3 – 9 Desemba. Katika maonesho hayo, wadau 596 wa sekta ya viwanda walishiriki ikilinganishwa na wadau 542 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 10.0. Ongezeko hilo lilitokana na ushirikishwaji wa wadau wa viwanda katika kuhamasisha wadau kushiriki maonesho hayo pamoja na mwamko wa wenye viwanda kutumia fursa zitokanazo na maonesho zikiwemo kuongeza maarifa, kutangaza bidhaa na huduma zinazozalishwa na kuongeza wigo wa masoko

**Udhibiti wa Ubora wa Viwango na Vipimo**

330. Mwaka 2020, Serikali kupitia Shirika la Viwango Tanzania iliandaa viwango 509 ikilinganishwa na viwango 487 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 4.5. Aidha, Shirika lilipima sampuli 25,560 ikilinganishwa na sampuli 23,910 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 6.9. Ongezeko la uandaaji wa viwango na upimaji wa sampuli lilitokana na ukuaji wa uzalishaji wa bidhaa za viwandani na kuongezeka kwa uelewa wa wazalishaji na watumiaji kuhusu umuhimu wa ubora wa bidhaa. Vile vile, vifaa 10,390 vilifanyiwa uhakiki/ugezi mwaka 2020 ikilinganishwa na vifaa 7,503 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 38.5. Ongezeko hilo lilitokana na elimu iliyotolewa kwa wadau kuhusu umuhimu wa kufanyia ugezi vifaa mbalimbali ili kuwa na uhakika wa vipimo.

331. Mwaka 2020, Shirika lilitoa leseni 526 za ubora ikilinganishwa na leseni 358 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 46.9. Ongezeko hilo lilitokana na Shirika kuendelea kutoa mafunzo kwa wazalishaji wa bidhaa na umma kwa ujumla kuhusu umuhimu wa kuzingatia ubora. Kati ya leseni hizo, leseni 217 zilitolewa kwa wajasiriamali wadogo na wa kati wanaozalisha bidhaa mbalimbali na leseni 309 kwa wajasiriamali wa kati na wakubwa. Vile vile, mafunzo ya aina 112 ya udhibiti ubora

yalitolewa kwa washiriki 12,711 mwaka 2020 ikilinganishwa na mafunzo ya aina 108 yaliyotolewa kwa washiriki 7,464 kwa mwaka 2019.

332. Mwaka 2020, Shirika lilisajili na kutoa vibali 5,616 vya chakula na maeneo ya uzalishaji ikilinganishwa na vibali 188 vilivyotolewa mwaka 2019. Katika kipindi hicho, vibali 1,452 vya bidhaa za vipodozi na maeneo ya uzalishaji vilitolewa ikilinganishwa na vibali 42 mwaka 2019. Ongezeko la vibali vilivyotolewa lilitokana na ufanisi wa mfumo wa kielektroniki uliorahisisha zoezi la usajili na utoaji vibali pamoja na kuongezeka kwa uzoefu wa watumishi katika kutoa huduma.

333. Mwaka 2020, Shirika lilikagua magari yaliyotumika 46,123 ikilinganishwa na magari 47,881 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 3.7. Aidha, bidhaa 39,690 kutoka nje ya nchi zilikaguliwa mwaka 2020 ikilinganishwa na bidhaa 44,006 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 9.8. Upungufu huo ulitokana na kufungwa kwa mipaka na kupungua kwa shughuli za kiuchumi katika baadhi ya nchi zinazofanya biashara na Tanzania kulikosababishwa na athari za janga la UVIKO-19.

334. Mwaka 2020, Serikali kupitia Wakala wa Vipimo – WMA ilihakiki vipimo 899,975 ikilinganishwa na vipimo 841,518 vilivyohakikiwa mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 6.9. Ongezeko hilo lilitokana na upatikanaji wa vitendea kazi kama magari, vifaa au mitambo ya kisasa na rasilimali watu. Aidha, Wakala iliidhinisha vipimo aina 56 toka nje ya nchi, ilitoa vibali 26 vya ugezi na leseni 290 za ufundi wa vipimo ikilinganishwa na vipimo/leseni/vibali 310 vilivyotolewa mwaka 2019. Ongezeko lilitokana na elimu na ujuzi uliotolewa kwa waundaji wa vipimo. Vile vile, Wakala ilifanya kaguzi 5,601 za kushtukiza kwenye maduka na maeneo ya biashara mwaka 2020 ikilinganishwa na kaguzi 4,000 mwaka 2019. Ongezeko hilo lilitokana na ununuzi wa magari yaliyosaidia kufikika kwa maeneo mengi.

**Usawa wa Ushindani na Udhibiti wa Bidhaa Bandia**

335. Mwaka 2020, Serikali kupitia Tume ya Ushindani - FCC ilikagua makasha 5,096 ya kusafirishia mizigo ambapo makasha 286 yalibainika kuwa na bidhaa bandia ikilinganishwa na makasha 3,260 yaliyokaguliwa mwaka 2019 ambapo makasha 114 yalibainika kuwa na bidhaa bandia.

336. Mwaka 2020, Tume ilipokea na kusajili mikataba ya walaji 44 kutoka kwenye maeneo yanayohusu masuala ya fedha, bima, nishati jadidifu na michezo ya kubahatisha ikilinganishwa na mikataba 105 iliyosajiliwa mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 58.1. Aidha, Tume ilitatua malalamiko 83 ya walaji ikilinganishwa na malalamiko 188 yaliyotatuliwa mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 55.9. Upungufu huo ulitokana na kuongezeka kwa umakini wa walaji pindi wafanyapo maamuzi ya ununuzi wa bidhaa na huduma. Vile vile, Tume ilipokea na kutoa maamuzi

kwa mashauri 54 mwaka 2020 ikilinganishwa na mashauri 46 yaliyopokelewa mwaka 2019 ambapo mashauri 43 yalitolewa maamuzi.

**Shirika la Maendeleo la Taifa**

337. Mwaka 2020, uzalishaji wa mpira mkavu katika mashamba ya Kihuhwi (Muheza) na Kalunga (Kilombero) ulifikia tani 174.1 ikilinganishwa na tani 40.3 mwaka 2019. Ongezeko hilo lilitokana na kuendelea kuboreshwa kwa usimamizi wa mashamba, kuongezeka kwa wafanyakazi hususan wa kugema utomvu na kuongezeka kwa vifaa vya ugemaji, usindikaji na ukaushaji wa utomvu.

338. Mwaka 2020, kiwanda cha URSUS kilichopo Kibaha kiliunganisha matrekta 149 ikilinganishwa na matrekta 421 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 64.6. Upungufu huo ulitokana na vifaa vya kuunganisha matrekta vilivyoagizwa kutofika kwa wakati pamoja na kampuni ya URSUS SA ya Poland kutotekeleza mkataba ipasavyo ikiwemo kukamilisha uingizaji wa matrekta 2,400, ujenzi wa kiwanda cha kuunganisha matrekta na ujenzi wa vituo nane (8) vya kuhudumia matrekta.

**Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Uwekezaji**

339. Mwaka 2020, Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Uwekezaji - EPZA ilisajili kampuni mpya saba (7) ikilinganishwa na kampuni sita (6) mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 16.7. Ongezeko hilo lilitokana na Serikali kuendelea kuhamasisha uwekezaji na kuboresha usimamizi katika Maeneo Huru ya Uwekezaji. Kampuni zilizosajiliwa ni Mwanza Precious Metals Refinery Limited, GG Refinery Limited, Fertisul Africa Limited, T. Masasi Agro Industry Limited, Abi Agro Products Limited, Cheng Xin Investment Co Limited na Al Sultan Establishment Limited.

340. Mwaka 2020, mtaji wa dola za Marekani bilioni 2.5 uliwekezwa katika Maeneo Maalumu ya Uwekezaji - EPZ/SEZ ikilinganishwa na dola za Marekani bilioni 2.4 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 3.4. Katika kipindi hicho, mauzo nje ya bidhaa za maeneo maalumu ya uwekezaji yalikuwa dola za Marekani bilioni 3.0 ikilinganishwa na dola za Marekani bilioni 2.2 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 36.0. Vile vile, ajira za moja kwa moja 58,007 zilizalishwa mwaka 2020 ikilinganishwa na ajira 57,342 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 1.2. Ongezeko hilo lilitokana na Serikali kuendelea kuhamasisha uwekezaji katika Maeneo Maalumu ya Uwekezaji.

Jedwali Na. 48 **MATUMIZI YA SARUJI NCHINI**

| Mwaka | Kutoka Nje | Uuzaji nje | Uzalishaji wa Ndani | Tani | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Matumizi Tani | Badiliko % |
| 2003 | 166,446 | 34,396 | 1,186,434 | 1,318,484 | 15.9 |
| 2004 | 125,007 | 37,655 | 1,280,851 | 1,368,203 | 3.8 |
| 2005 | 120,200 | 40,430 | 1,375,222 | 1,454,992 | 6.3 |
| 2006 | 92,711 | 98 | 1,421,460 | 1,514,073 | 4.1 |
| 2007 | 101,827 | 52,170 | 1,629,890 | 1,679,547 | 10.9 |
| 2008 | 356,468 | 99,688 | 1,755,862 | 2,012,642 | 19.8 |
| 2009 | 516,182 | 57,569 | 1,940,845 | 2,399,458 | 19.2 |
| 2010 | 566,828 | 189,321 | 2,312,055 | 2,689,562 | 12.1 |
| 2011 | 768,343 | 217,944 | 2,408,765 | 2,959,164 | 10.0 |
| 2012 | 1,013,986 | 145,793 | 2,557,798 | 3,425,991 | 15.8 |
| 2013 | 1,218,453 | 154,481 | 2,369,819 | 3,433,791 | 0.2 |
| 2014 | 1,428,995 | 142,001 | 2,795,687 | 4,082,681 | 18.9 |
| 2015 | 1,257,578 | 126,391 | 3,273,000 | 4,404,187 | 7.9 |
| 2016 | 1,306,732 | 194,338 | 4,916,400 | 6,028,794 | 36.9 |
| 2017 | 188,067 | 226,588 | 4,397,684 | 4,359,163 | -27.7 |
| 2018 | 17,259 | 206,234 | 4,766,092 | 4,577,117 | 5.0 |
| 2019[r] | 0 | 410,607 | 6,515,396 | 6,104,789 | 33.4 |
| 2020* | 757,523 | 476,560 | 6,496,044 | 6,777,008 | 11.0 |

**Chanzo**: Ofisi ya Taifa Takwimu na TRA
* Takwimu za awali
r Takwimu zimeboreshwa

Jedwali Na.49

## UZALISHAJI WA BAADHI YA BIDHAA VIWANDANI

| **Aina ya Bidhaa** | Kipimo | **2013** | **2014** | **2015** | **2016** | **2017** | **2018** | **2019** | **2020** | **Badiliko (%) 2019/20** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Biskuti & tambi | Tani | 17,440 | 18,225 | 19,204 | 15,890 | 16,451 | 16,911 | 18,113 | 22,430 | 23.8 |
| Unga wa ngano | Tani | 516,778 | 529,797 | 533,257 | 498,940 | 606,432 | 662,967 | 680,393 | 767,476 | 12.8 |
| Konyagi | 000 Lita | 20,680 | 31,963 | 29,491 | 28,754 | 25,555 | 29,335 | 32,366 | 33,287 | 2.8 |
| Bia | 000 Lita | 374,238 | 379,913 | 386,310 | 383,251 | 396,864 | 412,555 | 391,299 | 385,851 | -1.4 |
| Chibuku | 000 Lita | 19,935 | 20,301 | 23,028 | 26,513 | 22,624 | 20,819 | 20,350 | 21,712 | 6.7 |
| Sigara | Milioni | 7,710 | 8,028 | 7,837 | 8,091 | 7,412 | 7,921 | 8,369 | 7,320 | -12.5 |
| Nguo | 000 $M^2$ | 97,522 | 119,458 | 100,491 | 76,436 | 52,052 | 52,613 | 45,415 | 53,067 | 16.8 |
| Kamba za katani | Tani | 7,542 | 7,871 | 8,851 | 9,216 | 8,188 | 8,148 | 9,287 | 8,187 | -11.8 |
| Nyavu za uvuvi | Tani | 297 | 279 | 311 | 312 | 196 | 228 | 254 | 261 | 2.8 |
| Mazulia | 000 $M^2$ | - | - | 0 | 0 | - | - | - | - | - |
| Tabaka za mbao | $M^2$ | 36,935 | 38,913 | 36,317 | 34,983 | 37,302 | 37,849 | 42,563 | 34,237 | -19.6 |
| Dawa za pareto | Tani | 83 | 136 | 118 | 126 | 134 | 139 | 145 | 154 | 6.2 |
| Mbolea | Tani | - | - | 0 | 0 | - | - | - | - | - |
| Rangi | 000 Lita | 36,623 | 38,308 | 38,372 | 35,096 | 40,146 | 47,928 | 58,024 | 48,261 | -16.8 |
| Bidhaa za petrol | 000 Tani | - | - | 0 | 0 | - | - | - | - | - |
| Saruji | 000 Tani | 2,369 | 2,795 | 3,135 | 4,572 | 4,398 | 4,766 | 6,514 | 6,496 | -0.3 |
| Chuma* | Tani | 48,500 | 56,752 | 62,612 | 65,686 | 231,591 | 275,267 | 266,314 | 277,785 | 4.3 |
| Bati | Tani | 85,314 | 86,825 | 91,385 | 91,421 | 84,541 | 84,132 | 100,963 | 107,836 | 6.8 |
| Aluminium | Tani | 37 | 27 | 32 | 14 | - | - | - | - | - |
| Radio | 000 namba | - | - | 0 | 0 | - | - | - | - | - |
| Betri | Milioni | 75 | 93 | 87 | 69 | 122 | 115 | 120 | 132 | 10.0 |

**Chanzo**: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Wizara ya Viwanda na Biashara

- Hakuna uzalishaji

* Takwimu za uzalishaji wa chuma kuanzia mwaka 2008 - 2018 zimeboreshwa

Jedwali Na. 50

**VIWANDA - IDADI YA WATU WALIOAJIRIWA**

| ISIC (Rev 3) | Shughuli | Walioajiriwa | | | Wengine | | | Jumla | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **2018** | **2019** | **2020*** | **2018** | **2019** | **2020** | **2018** | **2019** | **2020** |
| 151-4 | Vyakula | 84,611 | 93,072 | 102,379 | 28,441 | 31,285 | 34,414 | 113,052 | 124,357 | 136,793 |
| 155 | Vinywaji | 9,167 | 10,084 | 11,092 | 112 | 123 | 136 | 9,279 | 10,207 | 11,228 |
| 160 | Tumbaku na Sigara | 6,761 | 7,437 | 8,182 | 8 | 9 | 10 | 6,769 | 7,446 | 8,192 |
| 171-2, 181 | Ufumaji na Ushonaji | 35,907 | 39,498 | 43,449 | 28,023 | 30,825 | 33,908 | 63,930 | 70,323 | 77,357 |
| 191 | Ngozi, bidhaa za ngozi | 1,868 | 2,055 | 2,262 | 419 | 461 | 508 | 2,286 | 2,516 | 2,770 |
| 201-202 | Mbao, Bidhaa za Mbao | 9,551 | 10,506 | 11,556 | 2,926 | 3,219 | 3,541 | 12,478 | 13,725 | 15,097 |
| 210-221-222 | Karatasi, Uchapishaji | 7,142 | 7,856 | 8,643 | 266 | 293 | 322 | 7,409 | 8,149 | 8,965 |
| 241-2 | Utengenezaji wa Kemikali na Madawa ya serikali | 9,551 | 10,506 | 11,557 | 301 | 331 | 364 | 9,852 | 10,837 | 11,921 |
| 251 | Bidhaa za mpira na Plastiki | 5,678 | 6,246 | 6,870 | 75 | 82 | 91 | 5,753 | 6,328 | 6,961 |
| 261-9 | Bidhaa za Madini yasiyo Chuma | 10,722 | 11,794 | 12,975 | 1,712 | 1,883 | 2,071 | 12,434 | 13,677 | 15,046 |
| 271-369 | Nyinginezo | 40,148 | 44,163 | 48,579 | 22,790 | 25,069 | 27,576 | 62,938 | 69,232 | 76,155 |
| | **Jumla** | **221,108** | **243,217** | **267,544** | **85,072** | **93,580** | **102,941** | **306,180** | **336,797** | **370,485** |

**Chanzo**: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

* Takwimu zimekadiriwa kutokana na utafiti wa sensa ya viwanda ya mwaka 2013 na Utafiti wa mwaka 2015 na 2016 wa Uzalishaji Viwandani

Jedwali Na. 51 **VIWANDA - GHARAMA ZA KAZI** (Shilingi Milioni)

| ISIC (Rev 3) | Shughuli | Mishahara | | | Malipo Mengine | | | Jumla | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **2018** | **2019** | **2020*** | **2018** | **2019** | **2020*** | **2018** | **2019** | **2020*** |
| 151-4 | Vyakula | 435,952 | 479,547 | 527,501 | 79,813 | 87,794 | 96,574 | 515,765 | 567,341 | 624,075 |
| 155 | Vinywaji | 267,177 | 293,895 | 323,284 | 113,550 | 124,905 | 137,396 | 380,727 | 418,800 | 460,680 |
| 160 | Tumbaku na Sigara | 119,013 | 130,914 | 144,005 | 33,284 | 36,612 | 40,274 | 152,297 | 167,527 | 184,279 |
| 171-2, 181 | Ufumaji na Ushonaji | 132,610 | 145,871 | 160,458 | 69,995 | 76,994 | 84,693 | 202,605 | 222,865 | 245,151 |
| 191 | Ngozi, Bidhaa za ngozi | 7,535 | 8,288 | 9,118 | 762 | 838 | 922 | 8,297 | 9,127 | 10,040 |
| 201- 202 | Mbao, Bidhaa za Mbao | 35,079 | 38,587 | 42,446 | 4,967 | 5,464 | 6,010 | 40,047 | 44,051 | 48,456 |
| 210-221-222 | Karatasi, Uchapishaji | 63,745 | 70,119 | 77,131 | 14,134 | 15,547 | 17,102 | 77,879 | 85,667 | 94,233 |
| 241-2 | Utengenezaji wa Kemikali na Madawa ya Binadamu | 86,538 | 95,192 | 104,711 | 13,524 | 14,876 | 16,364 | 100,062 | 110,068 | 121,075 |
| 251 | Bidhaa za Mpira na Plastiki | 44,471 | 48,918 | 53,810 | 6,540 | 7,194 | 7,913 | 51,011 | 56,112 | 61,723 |
| 261-9 | Bidhaa za Madini yasiyo Chuma | 117,146 | 128,861 | 141,747 | 35,506 | 39,057 | 42,963 | 152,652 | 167,917 | 184,710 |
| 271-369 | Nyinginezo | 193,255 | 212,580 | 233,838 | 40,217 | 44,239 | 48,663 | 233,472 | 256,819 | 282,501 |
| | **Jumla** | **1,502,522** | **1,652,773** | **1,818,049** | **412,292** | **453,521** | **498,874** | **1,914,814** | **2,106,294** | **2,316,923** |

**Chanzo**: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

* Takwimu zimekadiriwa kutokana na utafiti wa sensa ya viwanda ya mwaka 2013 na Utafiti wa mwaka 2015 na 2016 wa Uzalishaji Viwandani
Viwanda vilivyohusika ni vyenye ajira ya mtu mmoja na kuendelea (1+)

Jedwali Na. 52 **VIWANDA - MUHTASARI WA MATOKEO** (Shilingi Milioni)

| ISIC (Rev 3) | Shughuli | Pato | | | Gharama | | | Thamani iliyoongezeka | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **2018** | **2019** | **2020** | **2018** | **2019** | **2020** | **2018** | **2019** | **2020** |
| 151-4 | Vyakula | 6,615,079 | 7,276,587 | 8,004,246 | 3,040,178 | 3,344,196 | 3,678,616 | 3,574,901 | 3,932,391 | 4,325,630 |
| 155 | Vinywaji | 2,728,047 | 3,000,852 | 3,300,937 | 816,874 | 898,561 | 988,417 | 1,911,174 | 2,102,290 | 2,312,520 |
| 160 | Tumbaku na Sigara | 1,025,152 | 1,127,667 | 1,240,434 | 257,285 | 283,013 | 311,314 | 767,867 | 844,654 | 929,120 |
| 171-2, 181 | Ufumaji na Ushonaji | 800,505 | 880,556 | 968,612 | 366,463 | 403,109 | 443,420 | 434,041 | 477,446 | 525,192 |
| 191 | Ngozi, bidhaaa za ngozi | 89,846 | 98,831 | 108,714 | 60,992 | 67,091 | 73,800 | 28,855 | 31,739 | 34,914 |
| 201-202 | Mbao, Bidhaa za Mbao | 243,213 | 267,534 | 294,287 | 80,677 | 88,745 | 97,620 | 162,536 | 178,790 | 196,667 |
| 210-221-222 | Karatasi, Uchapishaji | 439,681 | 483,649 | 532,014 | 272,251 | 299,476 | 329,424 | 167,430 | 184,173 | 202,590 |
| 241-2 | Utengenezaji wa Kemikali na madawa ya Binadamu | 963,032 | 1,059,335 | 1,165,269 | 602,621 | 662,883 | 729,171 | 360,411 | 396,452 | 436,098 |
| 251 | Bidhaa za mpira na Plastiki | 989,217 | 1,088,139 | 1,196,953 | 639,628 | 703,591 | 773,950 | 349,590 | 384,548 | 423,003 |
| 261-9 | Bidhaa za Madini yasiyo Chuma | 1,263,134 | 1,389,447 | 1,528,392 | 641,032 | 705,135 | 775,649 | 622,101 | 684,312 | 752,743 |
| 271-369 | Nyinginezo | 1,942,021 | 2,136,223 | 2,349,845 | 1,127,622 | 1,240,384 | 1,364,423 | 814,399 | 895,839 | 985,422 |
| | **Jumla** | **17,098,926** | **18,808,820** | **20,689,703** | **7,905,622** | **8,696,185** | **9,565,804** | **9,193,304** | **10,112,635** | **11,123,899** |

**Chanzo**: Ofisi ya Taifa ya Takwimu
* Takwimu zimekadiriwa kutokana na utafiti wa sensa ya viwanda ya mwaka 2013 na Utafiti wa mwaka 2015 na 2016 wa Uzalishaji Viwandani
Viwanda vilivyohusika ni vyenye ajira ya mtu mmoja na kuendelea (1+)

Jedwali Na.53

**VIWANDA - MUHTASARI WA MATOKEO KIMKOA**

| Jina la mkoa | Idadi ya Wafanyakazi | | | Idadi ya Waajiriwa | | | Mishahara (TShs. Milioni) | | | Thamani Iliyoongezeka (TShs. Milioni) | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **2018** | **2019** | **2020*** | **2018** | **2019** | **2020*** | **2018** | **2019** | **2020*** | **2018** | **2019** | **2020*** |
| Dodoma | 3,313 | 3,644 | 4,009 | 2,392 | 2,631 | 2,894 | 18,802 | 20,682 | 22,750 | 116,192 | 126,546 | 139,200 |
| Arusha | 25,986 | 28,585 | 31,444 | 18,766 | 20,643 | 22,707 | 63,838 | 70,222 | 77,243 | 394,505 | 429,659 | 472,625 |
| Kilimanjaro | 19,512 | 21,463 | 23,610 | 14,091 | 15,500 | 17,050 | 80,860 | 88,946 | 97,840 | 499,696 | 544,223 | 598,647 |
| Tanga | 14,729 | 16,202 | 17,823 | 10,637 | 11,701 | 12,871 | 100,762 | 110,838 | 121,922 | 622,689 | 678,176 | 745,994 |
| Morogoro | 46,159 | 50,775 | 55,853 | 33,333 | 36,666 | 40,333 | 42,748 | 47,023 | 51,725 | 264,170 | 287,711 | 316,480 |
| Pwani, | 14,368 | 15,805 | 17,385 | 10,376 | 11,414 | 12,555 | 60,649 | 66,714 | 73,385 | 374,796 | 408,195 | 449,014 |
| Dar es Salaam | 98,793 | 108,672 | 119,542 | 71,343 | 78,477 | 86,325 | 862,752 | 949,027 | 1,043,930 | 5,331,606 | 5,806,701 | 6,387,375 |
| Lindi | 1,474 | 1,621 | 1,783 | 1,065 | 1,172 | 1,289 | 384 | 422 | 464 | 2,373 | 2,585 | 2,842 |
| Mtwara | 4,272 | 4,699 | 5,169 | 3,085 | 3,394 | 3,733 | 14,307 | 15,738 | 17,312 | 88,411 | 96,290 | 105,919 |
| Ruvuma | 2,756 | 3,032 | 3,335 | 1,991 | 2,190 | 2,409 | 2,885 | 3,173 | 3,490 | 17,831 | 19,420 | 21,362 |
| Iringa | 7,346 | 8,081 | 8,889 | 5,305 | 5,836 | 6,419 | 34,128 | 37,541 | 41,295 | 210,903 | 229,696 | 252,665 |
| Mbeya | 8,798 | 9,678 | 10,646 | 6,353 | 6,988 | 7,687 | 69,433 | 76,376 | 84,014 | 429,078 | 467,312 | 514,043 |
| Singida | 3,404 | 3,744 | 4,118 | 2,459 | 2,705 | 2,976 | 2,497 | 2,747 | 3,022 | 15,429 | 16,804 | 18,484 |
| Tabora | 1,084 | 1,192 | 1,313 | 782 | 860 | 946 | 13,772 | 15,149 | 16,664 | 85,105 | 92,688 | 101,958 |
| Rukwa | 2,267 | 2,494 | 2,744 | 1,637 | 1,801 | 1,981 | 7,955 | 8,750 | 9,625 | 49,157 | 53,538 | 58,892 |
| Kigoma | 2,760 | 3,036 | 3,339 | 1,993 | 2,192 | 2,412 | 1,341 | 1,475 | 1,622 | 8,286 | 9,024 | 9,926 |
| Shinyanga | 4,059 | 4,465 | 4,912 | 2,932 | 3,225 | 3,547 | 13,679 | 15,047 | 16,552 | 84,531 | 92,063 | 101,270 |
| Kagera | 5,288 | 5,817 | 6,399 | 3,819 | 4,201 | 4,621 | 6,369 | 7,006 | 7,707 | 39,359 | 42,867 | 47,153 |
| Mwanza | 16,193 | 17,812 | 19,594 | 11,694 | 12,863 | 14,149 | 79,976 | 87,974 | 96,771 | 494,235 | 538,276 | 592,104 |
| Mara | 5,188 | 5,707 | 6,277 | 3,746 | 4,121 | 4,533 | 6,988 | 7,687 | 8,456 | 43,182 | 47,030 | 51,733 |
| Manyara | 7,547 | 8,302 | 9,132 | 5,450 | 5,995 | 6,594 | 3,327 | 3,660 | 4,025 | 20,563 | 22,395 | 24,635 |
| Njombe | 4,039 | 4,443 | 4,887 | 2,917 | 3,209 | 3,530 | 6,350 | 6,985 | 7,684 | 39,244 | 42,741 | 47,015 |
| Katavi | 2,093 | 2,302 | 2,532 | 1,511 | 1,662 | 1,829 | 1,366 | 1,503 | 1,653 | 8,441 | 9,194 | 10,112 |
| Simiyu | 2,573 | 2,830 | 3,113 | 1,858 | 2,044 | 2,248 | 5,100 | 5,610 | 6,170 | 31,519 | 34,328 | 37,760 |
| Geita | 883 | 971 | 1,069 | 638 | 702 | 772 | 251 | 276 | 304 | 1,551 | 1,690 | 1,857 |
| Songwe | 1,296 | 1,426 | 1,568 | 936 | 1,030 | 1,133 | 2,004 | 2,204 | 2,424 | 12,381 | 13,484 | 14,834 |
| **Jumla** | **306,180** | **336,798** | **370,485** | **221,108** | **243,220** | **267,544** | **1,502,522** | **1,652,775** | **1,818,049** | **9,285,235** | **10,112,636** | **11,123,899** |

**Chanzo**: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

* Takwimu zimekadiriwa kutokana na utafiti wa sensa ya viwanda ya mwaka 2013 na Utafiti wa mwaka 2015 na 2016 wa Uzalishaji Viwandani

Viwanda vilivyohusika ni vyenye ajira ya mtu mmoja na kuendelea (1+)

## SURA YA 15

## UJENZI NA MAENDELEO YA ARDHI

### UJENZI

### Mtandao wa Barabara Nchini

341. Mtandao wa barabara zinazosimamiwa na Wakala wa Barabara nchini (TANROADS) una urefu wa kilometa 89,204. Mtandao huo unajumuisha, kilometa 12,176 za barabara kuu zinazounganisha mikoa na nchi jirani, kilometa 24,082 barabara za mikoa zinazounganisha wilaya na miji mikuu na kilometa 52,946 barabara za wilaya zinazounganisha wilaya, kata na vijiji.

342. Barabara kuu na za mikoa zenye kiwango cha lami na changarawe/udongo zilizofanyiwa tathmini zilikuwa na urefu wa kilometa 33,649.7 mwaka 2020 ikilinganishwa na kilometa 33,178 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 1.4. Ongezeko hilo lilitokana na baadhi ya barabara za wilaya kupandishwa hadhi na kuwa barabara za mikoa. Kati ya hizo, kilometa 4,256.8 zilikuwa katika hali mbaya, kilometa 16,621.7 zilikuwa katika hali ya wastani na kilometa 12,771.2 zilikuwa katika hali nzuri ikilinganishwa na kilometa 3,618, kilometa 16,693 na kilometa 12,867 mwaka 2019 mtawalia. Aidha, barabara zenye hali mbaya ziliongezeka kutokana na mvua zilizozidi wastani na kusababisha uharibifu wa miundombinu ya barabara.

343. Mwaka 2020, kilometa 10,644.8 za barabara kuu zenye kiwango cha lami na changarawe zilifanyiwa tathmini ikilinganishwa na kilometa 10,482.0 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 1.6. Kati ya hizo, kilometa 1,359.9 zilikuwa katika hali mbaya, kilometa 3,185.4 zilikuwa na hali ya wastani, kilometa 6,099.5 zilikuwa na hali nzuri ikilinganishwa na kilometa 1,164, kilometa 2,789 na kilometa 6,529 mwaka 2019 mtawalia. Ongezeko hilo lilitokana na mvua zilizozidi wastani na kusababisha uharibifu wa miundombinu ya barabara.

344. Barabara za mikoa zenye kiwango cha lami na changarawe zilizofanyiwa tathmini mwaka 2020 zilikuwa na urefu wa kilometa 23,004.9 ikilinganishwa na kilometa 22,696.0 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 1.4. Kati ya hizo, kilometa 2,896.9 zilikuwa katika hali mbaya, kilometa 13,436.3 hali ya wastani na kilometa 6,671.7 hali nzuri ikilinganishwa na kilometa 2,454, kilometa 13,904 na kilometa 6,338 mwaka 2019 mtawalia. Ongezeko la barabara zenye hali mbaya lilitokana na mvua iliyozidi wastani na kusababisha uharibifu wa mundombinu ya barabara. Aidha, barabara zenye hali nzuri ziliongezeka kutokana na barabara za kiwango cha lami kuendelea kujengwa.

**Jedwali Na. 15.1: Hali ya Mtandao wa Barabara hadi Desemba, 2020**

| | Hali ya mtandao wa barabara | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Nzuri** | | **Wastani** | | **Mbaya** | | **Jumla** |
| **Aina ya barabara** | **Km** | **%** | **Km** | **%** | **Km** | **%** | **Km** |
| Barabara kuu lami | 5,445.4 | 67 | 1,560.3 | 19 | 1,167.3 | 14 | 8,173.1 |
| Barabara kuu changarawe/udongo | 654 | 26 | 1,625.1 | 66 | 192.6 | 8 | 2,471.7 |
| **Jumla Ndogo** | **6,099.5** | **57.3** | **3,185.4** | **29.9** | **1,359.9** | **12.8** | **10,644.8** |
| Barabara za Mkoa lami | 726.9 | 44 | 436.7 | 26 | 486.5 | 29 | 1,650.1 |
| Barabara za Mkoa changarawe/udongo | 5,944.90 | 28 | 12,999.6 | 61 | 2,410.4 | 11 | 21,354.8 |
| **Jumla Ndogo** | **6,671.7** | **29** | **13,436.3** | **58** | **2,896.9** | **12.6** | **23,004.9** |
| **Jumla Kuu** | **12,771.2** | **38** | **16,621.7** | **49** | **4,256.8** | **13** | **33,649.7** |

**Chanzo:** Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Ujenzi)

## Barabara, Madaraja, Vivuko na Magari

345. Mwaka 2020, Wakala wa Barabara Tanzania – TANROADS ilitengeneza kilometa 34,706.2 za barabara kuu na mikoa ikilinganishwa na kilometa 35,813.7 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 3.1. Katika kipindi hicho, madaraja 2,482 yalitengenezwa ikilinganishwa na madaraja 3,310 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 25.0. Kupungua kwa matengenezo ya barabara na madaraja kulitokana na kusitishwa kwa utekelezaji wa baadhi ya miradi inayotumia vifaa na wakandarasi kutoka nje ya nchi kutokana na hatua zilizochukuliwa na mataifa mbalimbali ikiwemo kuzuia safari ili kujiepusha na maambukizi ya UVIKO – 19

346. Mwaka 2020, Serikali kupitia Wakala wa Ufundi na Umeme - TEMESA ilisimamia uendeshaji wa vivuko 33 ikilinganishwa na vivuko 31 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 6.5. Ongezeko hilo lilitokana na kununuliwa na kufanya kazi kwa vivuko vipya vya MV Ukara II na MV Chato II vyenye uwezo wa kubeba tani 100 kwa lengo la kuboresha huduma ya usafiri katika eneo la Bugolora-Ukara na Chato-Nkome. Katika kipindi hicho, abiria 30,290,361, magari 1,291,974 na tani 7,159.6 za mizigo ilivushwa ikilinganishwa na abiria 26,837,846, magari 1,140,855 na tani 3,585.1 za mizigo mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 13.2, asilimia 12.9 na asilimia 99.7 mtawalia. Ongezeko hilo lilitokana na kuanza kufanya kazi kwa vivuko vya MV Ilemela, MV Chato II na MV Ukara II.

347. Mwaka 2020, Wakala iliendelea kufanya ukarabati wa vivuko vyote nchini ambapo ukarabati mkubwa ulifanyika kwa vivuko vya MV Kigamboni na MV Pangani II, kuboresha miundombinu ya maegesho ya vivuko, kujenga maegesho mapya na kukarabati karakana za magari za Mbeya na Mwanza. Aidha, Wakala alitengeneza magari 30,701 mwaka 2020 ikilinganishwa na magari 29,707 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 3.3. Ongezeko hilo lilitokana na kuanzishwa kwa karakana za magari katika wilaya za Same na Kahama.

**Mtandao wa Barabara za Vijijini na Mijini**

348. Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini-TARURA uliendelea kusimamia mtandao wa barabara wenye urefu wa kilometa 108,946.2. Kati ya hizo, barabara za udongo ni asilimia 72.4 ya mtandao wote wa barabara zinazosimamiwa na TARURA. Hadi Desemba 2020, mtandao wa barabara za wilaya wenye kiwango cha lami ulifikia kilometa 2,250.7, changarawe kilometa 27,809.3 na udongo kilometa 78,886.3 ikilinganishwa na kilometa 2,025.0, kilometa 24,493.0 na kilometa 82,428.2 mwaka 2019 mtawalia. Aidha, kilometa 16,168.5 za mtandao wote wa barabara zipo katika hali nzuri, kilometa 39,027.6 hali ya wastani na kilometa 53,750.1 hali mbaya.

**Jedwali Na. 15.2: Hali ya Mtandao wa Barabara za Vijijini na Mijini Mwaka 2020**

| **Aina ya Barabara** | **Hali ya Mtandao wa Barabara (Km)** | | | **Jumla (Km)** | **Asilimia** |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Nzuri** | **Wastani** | **Mbaya** | | |
| Barabara za lami | 1,540.3 | 509.0 | 201.5 | 2,250.7 | 2.1 |
| Barabara za Changarawe | 7,555.1 | 13,266.50 | 6,987.7 | 27,809.3 | 25.6 |
| Barabara za udongo | 7,073.1 | 25,252.2 | 46,561.0 | 78,886.3 | 72.4 |
| **Jumla** | **16,168.5** | **39,027.6** | **53,750.1** | **108,946.2** | **100** |
| Asilimia | 15.0 | 36.0 | 49.0 | 100.0 | |

**Chanzo:** Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini

349. Hadi Desemba 2020, Wakala ulifanya matengenezo ya barabara za wilaya zenye urefu wa kilometa 26,201.6 ikilinganishwa na kilometa 17,688.2 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 48.1. Ongezeko hilo lilitokana na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya ujenzi na ukarabati wa barabara ikiwemo ujenzi wa barabara za lami katika Mji wa Serikali - Dodoma na halmashauri za Kilolo, Mufindi, Mbeya na Rungwe. Aidha, matengenezo hayo yalijumuisha ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilometa 225.7 kwa kiwango cha lami, ujenzi wa barabara za changarawe kilometa 3,316.2 na barabara zenye urefu wa kilometa 22,659.7 zilifanyiwa matengenezo maalumu, ya kawaida pamoja na matengenezo ya maeneo korofi. Aidha, Wakala ulijenga madaraja 19, makalavati 786, mitaro mikubwa ya maji ya mvua yenye urefu wa kilometa 89.4 na kukarabati madaraja 102.

350. Hadi Desemba 2020, Wakala kupitia miradi ya uendelezaji wa miji na majiji iliwezesha ujenzi wa madampo ya kisasa mawili (2) katika Jiji la Tanga na Mwanza, maeneo 45 ya kuweka makontena ya kukusanyia taka ngumu, maeneo matatu (3) ya mapumziko, stendi ya mabasi Dodoma na stendi ndogo Mtwara, kituo kimoja cha maegesho ya malori Dodoma, vivuko sita (6) vya waenda kwa miguu, masoko mawili ya kisasa katika Jiji la Dodoma na Manispaa ya Mtwara Mikindani.

**Mfuko wa Barabara**

351. Mwaka 2020, Serikali kupitia Bodi ya Mfuko wa Barabara ilikusanya shilingi bilioni 820.9 ikilinganishwa na shilingi bilioni 841.8 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 2.5. Hii ilitokana na kupungua kwa kiasi cha mafuta ya dizeli, mafuta ya ndege na mafuta ya taa kilichoagizwa na kutumika nchini kufuatia kupungua kwa shughuli za kiuchumi na kusitishwa kwa safari za ndege za kimataifa kulikosababishwa na janga la UVIKO -19. Bodi ilikagua miradi 647 ya barabara ikilinganishwa na miradi 606 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 6.8. Hii ilitokana na kuboreshwa kwa hadidu za rejea za ukaguzi wa miradi ambapo kila halmashauri ilipaswa kukagua miradi isiyopungua saba pamoja na kujumuisha miradi ya dharura na mipya pale inapotokea uhitaji.

**Nyumba na Majengo ya Serikali**

352. Mwaka 2020, Serikali kupitia Wakala wa Majengo Tanzania - TBA iliendelea kusanifu na kusimamia ujenzi wa miradi ya nyumba na majengo ya Serikali 484 ikilinganishwa na miradi 485 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 0.2. Upungufu huo ulitokana na kuongezeka kwa ushindani kutoka taasisi zinazotoa huduma sawa na Wakala. Taasisi hizo ni pamoja na Chuo Kikuu cha Ardhi, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Shirika la Nyumba la Taifa na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya. Aidha, Wakala ulisimamia miradi 82 ya ukarabati wa nyumba na majengo mwaka 2020 ikilinganishwa na miradi 117 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 29.9. Upungufu huo ulitokana na kushuka kwa mapato yatokanayo na mauzo ya nyumba, kodi za pango pamoja na huduma za ushauri na ujenzi.

353. Mwaka 2020, nyumba 4,929 zilipangishwa kwa watumishi wa Serikali ikilinganishwa na nyumba 1,499 mwaka 2019. Ongezeko hilo lilitokana na kupata wapangaji kwenye nyumba zilizokuwa wazi, kukamilika kwa ukarabati wa nyumba na kubadilishwa kwa matumizi ya nyumba za biashara kuwa za makazi. Kwa upande mwingine, nyumba 1,720 za biashara zilipangishwa mwaka 2020 ikilinganishwa na nyumba 4,802 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 64.2. Upungufu huo ulitokana na baadhi ya nyumba za biashara kubadilishwa matumizi na kupangishwa kwa watumishi.

**Usajili wa Makandarasi**

354. Mwaka 2020, makandarasi 907 walisajiliwa na Bodi ya Usajili wa Makandarasi ikilinganishwa na makandarasi 925 mwaka 2019. Hii inafanya jumla ya makandarasi waliosajiliwa hadi Desemba 2020 kufikia 11,729 kutoka makandarasi 10,822 Desemba 2019, sawa na ongezeko la asilimia 8.4. Ongezeko hilo lilitokana na Bodi kuendelea kutoa elimu kuhusu umuhimu wa makandarasi kujisajili na kuchukua hatua za kisheria kwa waajiri wanaotumia huduma za makandarasi wasiosajiliwa. Aidha, Bodi ilisajili miradi ya ujenzi 3,179 ikilinganishwa na miradi 3,155 mwaka 2019.

355. Mwaka 2020, Bodi ilikagua miradi 3,364 ikilinganishwa na miradi 3,717 iliyokaguliwa mwaka 2019. Kati ya hiyo, miradi 2,430 haikuwa na upungufu na miradi 934 ilikuwa na upungufu mwaka 2020 ikilinganishwa na miradi 2,633 na miradi 1,084 mwaka 2019 mtawalia. Mapungufu yaliyobainishwa kwenye miradi ni pamoja na: miradi kutekelezwa na makandarasi wasiosajiliwa; miradi kutosajiliwa; kutowekwa bango la mradi; kutozingatia sheria ya afya na usalama wa wafanyakazi na makandarasi kutekeleza miradi ambayo haiendani na fani na madaraja yao. Aidha, Bodi iliwapeleka mahakamani watuhumiwa 116 waliokuwa na makosa mbalimbali ikiwemo kutekeleza miradi kwa kutumia kampuni au watu wasio makandarasi ikilinganishwa na watuhumiwa 72 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 61.1.

**Usajili wa Wahandisi**

356. Mwaka 2020, Bodi ya Usajili wa Wahandisi ilisajili wahandisi 29,759 wa fani mbalimbali ikilinganishwa na wahandisi 26,918 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 10.6. Ongezeko hilo lilitokana na wahitimu kuendelea kujisajili kufuatia kukua kwa shughuli za kiuchumi zinazohusu taaluma ya uhandisi hususan viwanda na ujenzi wa miundombinu ya reli, barabara, bandari na viwanja vya ndege. Kati ya wahandisi waliosajiliwa, wahandisi 27,235 sawa na asilimia 91.5 walikuwa watanzania na wahandisi 2,524 walitoka nje ya nchi. Hadi Desemba 2020, idadi ya mafundi sanifu waliosajiliwa na Bodi ilifikia 465 ikilinganishwa na mafundi sanifu 359 kipindi kama hicho mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 29.5. Hii ilitokana na Bodi kuendelea kudhibiti mafundi sanifu wasiokuwa na usajili kufanya kazi kwenye miradi.

357. Hadi Desemba 2020, Bodi ilikuwa imesajili kampuni za ushauri 376 ikilinganishwa na kampuni 354 Desemba 2019, sawa na ongezeko la asilimia 6.2. Kati ya hizo, kampuni 259 zilikuwa za kitanzania na kampuni 117 za kigeni ikilinganishwa na kampuni 242 za kitanzania na kampuni 112 za kigeni mwaka 2019. Katika kipindi hicho, Bodi ilisajili wahandisi washauri 605 ikilinganishwa na wahandisi washauri 578 Desemba, 2019. Kati ya hao, wahandisi washauri 461 walikuwa watanzania na 144 wa kigeni ikilinganishwa na wahandisi washauri 439 wa kitanzania na 139 wa kigeni mwaka 2019. Ongezeko la usajili wa kampuni na wahandisi washauri lilitokana na kuongezeka kwa miradi ya kiuhandisi. Aidha, maabara za vifaa vya ujenzi na uhandisi zilizosajiliwa na Bodi zilifikia 37 mwaka 2020 kutoka maabara 34 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 8.8. Ongezeko hilo lilichangiwa na kuendelea kuhimiza na kusimamia utaratibu unaozitaka kampuni zinazotoa huduma za maabara ya vifaa vya ujenzi na uhandisi kujisajili.

358. Mwaka 2020, wahandisi 8,444 walishiriki mafunzo ikilinganishwa na wahandisi 7,259 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 16.3. Kati ya hao, wahandisi 4,067 walihitimu na kusajiliwa kama wahandisi wataalam ikilinganishwa na wahandisi 3,551 mwaka 2019, sawa ongezeko la asilimia 14.5. Ongezeko hilo lilichangiwa na

uhuishwaji wa leseni katika mafunzo hayo ambapo washiriki husajiliwa na Bodi baada ya kukamilisha mafunzo na hivyo, kuhamasisha wahandisi kushiriki mafunzo hayo katika kanda zote nchini. Aidha, Bodi ilisajili miradi ya ujenzi 567 na kukagua miradi 77 mwaka 2020 ikilinganishwa na usajili wa miradi 649 na ukaguzi wa miradi 88 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 11.3 na 12.5 mtawalia. Hii inatokana na kupungua kwa miradi ya ujenzi kufuatia athari za mlipuko wa janga la UVIKO-19.

**Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi**

359. Hadi Desemba 2020, Bodi ya Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi ilisajili wataalamu 1,170 ikilinganishwa na wataalamu 1,098 waliosajiliwa Desemba 2019, sawa na ongezeko la asilimia 6.6. Kati ya wataalamu waliosajiliwa, wataalamu 1,136 walikuwa wa kitanzania na 34 walikuwa wa kigeni ikilinganishwa na wataalamu 1,064 wa kitanzania na 34 wa kigeni mwaka 2019. Ongezeko la wataalamu waliosajiliwa lilitokana na kuongezeka kwa uelewa wa Sheria namba 4 ya Usajili ya Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi ya Mwaka 2010 inayowataka wataalamu kujisajili na kufanya kazi kulingana na matakwa ya Sheria.

360. Hadi Desemba 2020, Bodi ilisajili kampuni 406 za wabunifu majengo na wakadiriaji majenzi ikilinganishwa na kampuni 387 Desemba 2019, sawa na ongezeko la asilimia 4.9. Kati ya hizo, kampuni 397 zilikuwa za kitanzania na kampuni tisa (9) za kigeni ikilinganishwa na kampuni 378 za kitanzania na tisa (9) za kigeni mwaka 2019. Ongezeko la usajili lilichangiwa na waendelezaji majengo kuendelea kutumia huduma za wataalamu waliosajiliwa na Bodi.

361. Mwaka 2020, Bodi ilikagua miradi 1,777 ya ujenzi wa majengo ikilinganishwa na miradi 1,617 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 9.9. Hii ilitokana na kuongezeka kwa utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa majengo. Aidha, miradi 828 ya ujenzi wa majengo ilisajiliwa ikilinganishwa na miradi 816 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 1.5. Ongezeko hilo lilitokana na utekelezaji wa miradi ya ujenzi na uzingatiwaji wa Sheria Namba 4 ya Usajili ya Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi ya Mwaka 2010.

362. Mwaka 2020, idadi ya wahitimu walioshiriki mafunzo kwa vitendo katika fani ya ubunifu majengo na ukadiriaji majenzi iliongezeka na kuwa wahitimu 108 ikilinganishwa na wahitimu 47 mwaka 2019. Hii ilitokana na kuongezeka kwa fursa za mafunzo ya vitendo kwa wahitimu kulikochagizwa na ongezeko la miradi ya ujenzi wa majengo.

**Baraza la Taifa la Ujenzi**

363. Mwaka 2020, Baraza la Taifa la Ujenzi lilifanya ukaguzi wa kiufundi katika miradi 63 ya ujenzi wa barabara, madaraja na majengo ikilinganishwa na miradi 43 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 46.5. Ongezeko hilo lilitokana na kuwepo

kwa mikataba mingi ya miradi ya ujenzi iliyotekelezwa. Aidha, Baraza lilitoa ushauri wa kiufundi kwa wadau 10 wa sekta ya ujenzi ikilinganishwa na wadau nane (8) mwaka 2019. Vile vile, Baraza lilifanya usuluhishi wa migogoro 60 ya ujenzi ikilinganishwa na migogoro 78 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 23.1. Upungufu huo ulitokana na wadau kuzingatia sheria na miongozo inayotolewa na Baraza.

364. Mwaka 2020, Baraza lilitoa mafunzo kwa wadau 67 wa sekta ya ujenzi ikilinganishwa na wadau 69 mwaka 2019. Mafunzo hayo yalijumuisha usimamizi wa mikataba, usuluhishi wa migogoro na ukaguzi wa kiufundi wa miradi. Aidha, Baraza kwa kushirikiana na Shirika la Viwango Tanzania-TBS liliandaa viwango 34 vya ubora wa vifaa vya ujenzi mwaka 2020 ikilinganishwa na viwango 42 vya ubora mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 19.0. Kupungua kwa viwango vilivyopitishwa na TBS ni kutokana na viwango husika kupitwa na wakati.

**Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi**

365. Mwaka 2020, Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi ilitoa mafunzo kwa mafundi sanifu 22 wa ujenzi kuhusu teknolojia stahiki ya nguvukazi katika kukarabati na kutengeneza barabara za lami ikilinganishwa na mafundi sanifu 10 mwaka 2019. Katika kipindi hicho, Taasisi ilihamasisha matumizi ya teknolojia ya nguvukazi kwa wadau 122 wa barabara kutoka TARURA na wakurugenzi watendaji wa halmashauri ikilinganishwa na wadau 114 mwaka 2019. Ongezeko la washiriki lilitokana na kuboreshwa kwa njia za uhamasishaji kwa kuwahusisha watendaji wa sekta ya ujenzi na baadhi ya maafisa maendeleo ya jamii wa halmashauri. Aidha, Taasisi ilitoa mafunzo ya matengenezo na ukarabati wa barabara kwa makandarasi wanawake 50 ikilinganishwa na makandrasi 30 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 66.7. Ongezeko hilo lilitokana na jitihada za Taasisi kuhamasisha makandarasi wanawake kupata mafunzo hayo.

**MAENDELEO YA ARDHI**

**Utayarishaji wa Hatimiliki, Ukaguzi na Uhakiki Milki**

366. Mwaka 2020, hatimiliki 71,972 za viwanja na mashamba ziliandaliwa kwa ajili ya usajili ikilinganishwa na hatimiliki 53,872 zilizoandaliwa mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 33.6. Katika kipindi hicho, ilani 17,199 za ubatilisho zilitumwa kwa wapangaji waliokiuka masharti ya upangaji wa ardhi ikilinganishwa na ilani 2,598 mwaka 2019. Ongezeko la hatimiliki na ilani za ubatilisho lilitokana na uanzishwaji wa ofisi za ardhi katika mikoa yote Tanzania Bara na hivyo kusogeza huduma kwa wananchi na kuongeza usimamizi wa ardhi. Aidha, hatimiliki za kimila 127,116 zilitolewa kwa wananchi mwaka 2020 ikilinganishwa na hatimiliki 238,839 mwaka 2019.

**Usajili wa Hatimiliki za Ardhi na Nyaraka za Kisheria**

367. Mwaka 2020, hatimiliki na nyaraka za kisheria 133,217 zilisajiliwa ikilinganishwa na hatimiliki na nyaraka za kisheria 92,512 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 44.0. Kati ya hizo, hati za kumiliki ardhi na sehemu ya jengo zilikuwa ni 58,104 ikilinganishwa na hati 48,269 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 20.4. Ongezeko hilo lilitokana na zoezi la urasimishaji lililofanyika katika maeneo mbalimbali nchini. Aidha, katika kipindi hicho, nyaraka za kisheria 75,113 zilisajiliwa ikilinganishwa na nyaraka za kisheria 44,243 mwaka 2019.

**Jedwali Na 15.3: Usajili wa Hatimiliki za Ardhi na Nyaraka za Kisheria Mwaka 2016-2020**

| **Hati zilizosajiliwa** | **2016** | **2017** | **2018** | **2019** | **2020** |
|---|---|---|---|---|---|
| Hati za kumiliki ardhi zilizosajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Ardhi (Sura 334) | 33,257 | 21,743 | 41,522 | 47,948 | 57,180 |
| Hati za Sehemu ya Jengo chini ya Sheria ya Usajili wa Hati za Sehemu ya Jengo (*Unit Title Act No*.17/2008). | 1,410 | 827 | 844 | 321 | 924 |
| **Jumla Hatimiliki** | **34,667** | **22,570** | **42,366** | **48,269** | **58,104** |
| **Nyaraka zilizosajiliwa** | | | | | |
| Nyaraka za Kisheria zilizosajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Ardhi (Sura 334). | 34,682 | 13,821 | 27,716 | 15,018 | 35,477 |
| Nyaraka zilizosajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Nyaraka (Sura 117). | 20,525 | 13,027 | 21,807 | 26,096 | 33,938 |
| Nyaraka zilizosajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Rehani ya mali zinazohamishika (Sura 210). | 1,313 | 310 | 1,817 | 3,129 | 5698 |
| **Jumla Nyaraka za Kisheria** | **56,520** | **27,158** | **51,340** | **44,243** | **75,113** |
| **Jumla Kuu Hatimiliki na Nyaraka za Kisheria** | **91,187** | **49,728** | **93,706** | **92,512** | **133,217** |

**Chanzo**: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

**Uthamini wa Mali**

368. Mwaka 2020, Serikali iliidhinisha taarifa za uthamini 40,874 ikilinganishwa na taarifa 19,669 mwaka 2019. Ongezeko la taarifa za uthamini zilizoidhinishwa lilitokana na kuongezeka kwa miamala ya ardhi hususan katika maeneo ya uhamisho wa milki, uhuishaji wa milki, mikopo *(mortgage)*, uthamini kwa ajili ya mizania ya kimahesabu na fidia katika miradi ya kimkakati inayotekelezwa na Serikali.

**Upimaji wa Mashamba na Viwanja**

369. Mwaka 2020, ramani zenye viwanja 337,598 na mashamba 372 ziliidhinishwa katika mikoa 26 ya Tanzania Bara ikilinganishwa na ramani zenye viwanja 322,709 na mashamba 717 mwaka 2019. Kuongezeka kwa ramani zenye viwanja vilivyoidhinishwa kulitokana na kuongeza kwa kasi ya uidhinishaji wa ramani za viwanja katika maeneo mbalimbali nchini.

**Jedwali Na. 15.4: Viwanja na Mashamba Yaliyoidhinishwa Mwaka 2020**

| Na. | Mikoa | Viwanja | Mashamba | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Arusha | 19,051 | 6 | 19,057 |
| 2 | Dar Es Salaam | 19,033 | 0 | 19,033 |
| 3 | Dodoma | 90,032 | 13 | 90,045 |
| 4 | Geita | 13,468 | 0 | 13,468 |
| 5 | Iringa | 8,674 | 19 | 8,693 |
| 6 | Kagera | 9,049 | 38 | 9,087 |
| 7 | Katavi | 1,547 | 7 | 1,554 |
| 8 | Kigoma | 9,909 | 12 | 9,921 |
| 9 | Kilimanjaro | 9,545 | 21 | 9,566 |
| 10 | Lindi | 3,725 | 10 | 3,735 |
| 11 | Manyara | 10,712 | 9 | 10,721 |
| 12 | Mara | 8,945 | 1 | 8,946 |
| 13 | Mbeya | 5,713 | 19 | 5,732 |
| 14 | Morogoro | 6,222 | 151 | 6,373 |
| 15 | Mtwara | 4,383 | 4 | 4,387 |
| 16 | Mwanza | 24,073 | 0 | 24,073 |
| 17 | Njombe | 11,041 | 7 | 11,048 |
| 18 | Pwani | 19,595 | 10 | 19,605 |
| 19 | Rukwa | 3,623 | 3 | 3,626 |
| 20 | Ruvuma | 5,472 | 8 | 5,480 |
| 21 | Shinyanga | 5,097 | 0 | 5,097 |
| 22 | Simiyu | 6,675 | 12 | 6,687 |
| 23 | Singida | 12,189 | 0 | 12,189 |
| 24 | Songwe | 3,702 | 10 | 3,712 |
| 25 | Tabora | 10,210 | 7 | 10,217 |
| 26 | Tanga | 15,913 | 5 | 15,918 |
| | **Jumla** | **337,598** | **372** | **337,970** |

**Chanzo:** Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

**Mipango ya matumizi ya Ardhi**

370. Mwaka 2020, mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji 67 iliandaliwa katika wilaya 17 nchini ikilinganishwa na mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji 395 iliyoandaliwa katika wilaya 67 mwaka 2019. Kupungua kwa idadi ya vijiji vyenye mipango ya matumizi ya ardhi kulitokana na wadau wa maendeleo ya ardhi kutoshiriki katika upangaji wa matumizi ya ardhi kulikosababishwa na athari za UVIKO – 19.

**Jedwali Na. 15.5: Orodha ya Vijiji Vilivyoandaliwa Mipango ya Matumizi ya Ardhi kwa Mwaka 2020**

| **Mkoa** | **Wilaya** | **Vijiji** | **Idadi ya Vijiji** |
|---|---|---|---|
| Mbeya | Mbeya vijijini | Ngohanjapanda, Sebe, Ulenje, Italia. | 4 |
| Kigoma | Kasulu | Rungwempya, Kaguruka, Kwaga, Ngage | 4 |
| | Uyui | Ibelamalundi, Itobela | 2 |
| Iringa | Mufindi | Kilosa, Ilogombe, Kipanga, Ihanu, Igoda, Mkonge, Nandala, Ihomasa, Udumuka, | 9 |
| Iringa | Iringa | Ibangamoyo, Kibena, Mibikimitali, Msuluti, Sadani, Kikombwe, Kaning'ombe, Makongati, Lumuli, Ibumila, Ng'enza, Mangalali, Lyamgungwe, Kipera | 14 |
| Songwe | Chunya | Bitimanyanga, Kambikatoto, Mafyeko, Sipa | 4 |
| Tabora | Sikonge | Majojolo, Mwitiko | 2 |
| Dodoma | Mpwapwa | Lwihomelo, Mwanawota, Man'galiza, Kilambo, Kazania, Kiegea, Mbugani, Ng'hambi, Chitemu. | 9 |
| Mara | Serengeti | Mbalimbali, Kitunguruma, Manyata | 3 |
| Lindi | Mtama | Nteme | 1 |
| Ruvuma | Mbinga | Makoro, Kiwombi | 2 |
| Manyara | Simanjiro | Norrosoit, Irkujit, endonyongijape | 3 |
| Shinyanga | Kishapu | Mguda, Kiloleli, Mihama, Beledi | 4 |
| Singida | Itingi | Kitanula, Mwamagembe | 2 |
| Tanga | Handeni | Ghole | 1 |
| | Kilindi | Kimamba | 1 |
| Morogoro | Mvomero | Mingo, lubungo | 2 |
| **Jumla** | | | **67** |

**Chanzo:** Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

## Urasimishaji wa Makazi Holela

371. Mwaka 2020, Serikali iliandaa na kuidhinisha michoro ya mipango miji 824 katika mikoa yote ya Tanzania Bara ikilinganishwa na michoro 1,188 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 30.6. Upungufu huo ulitokana na kuanza kutumia ramani zenye uwiano wa 2500 ambazo zinajumuisha viwanja vingi na hivyo kuwa na michoro michache. Aidha, vipande 238,538 vya ardhi vilirasimishwa katika halmashauri mbalimbali nchini ikilinganishwa na vipande 232,717 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 2.5. Ongezeko hilo lilitokana na kuendelea kwa utekelezaji wa Programu ya Urasimishaji na Udhibiti wa Makazi Holela.

## Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya

372. Hadi Desemba, 2020, kulikuwa na jumla ya mashauri 48,191 (mashauri mapya yalikuwa 22,330 na mashauri 25,861 ambayo hayakufanyiwa maamuzi mwaka 2019) katika Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya ikilinganishwa na mashauri 51,951

Desemba, 2019. Kati ya hayo, mashauri 23,917 yaliamuliwa na mashauri 24,274 yaliendelea kusikilizwa. Aidha, migogoro 8,583 ya matumizi ya ardhi ilitatuliwa kiutawala mwaka 2020 ikilinganishwa na migogoro 4,186 mwaka 2019.

**Ujenzi wa Nyumba za Makazi na Biashara**

373. Mwaka 2020, Shirika la Nyumba la Taifa lilijenga nyumba 1,164 katika halmashauri mbalimbali nchini kwa ajili ya ofisi, biashara na makazi ikilinganishwa na nyumba 7,331 zilizojengwa mwaka 2019. Kati ya hizo, nyumba za bei nafuu zilikuwa 468 na bei ya kati na juu zilikuwa nyumba 696. Aidha, Kampuni ya Nyumba kwa Watumishi – WHC ilijenga nyumba 70 mwaka 2020 ikilinganishwa na nyumba 845 mwaka 2019.

## SURA YA 16

## MAWASILIANO NA UCHUKUZI

### UCHUKUZI

**Usafiri wa Barabara**

374. Mwaka 2020, idadi ya leseni zilizotolewa kwa vyombo vya usafirishaji zilifikia 215,040 ikilinganishwa na leseni 202,149 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 6.4. Ongezeko hilo lilitokana na uwepo wa wawekezaji wapya hasa katika usafirishaji wa mizigo, kuendelea kutolewa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kuwa na leseni na kufanya kaguzi katika maeneo mbalimbali nchini.

**Jedwali Na. 16.1: Leseni za Usafirishaji Zilizotolewa Mwaka 2018 - 2020**

| **Leseni** | **2018** | **2019** | **2020** | **Badiliko (Asilimia)** |
|---|---:|---:|---:|:---:|
| Mabasi ya abiria | 46,449 | 60,344 | 52,081 | -13.7 |
| Magari ya mizigo | 113,345 | 123,460 | 142,559 | 15.5 |
| Bajaji/Pikipiki | 16,488 | 18,345 | 20,400 | 11.2 |
| **Jumla** | **176,282** | **202,149** | **215,040** | **6.4** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Nchi Kavu

375. Ajali za vyombo vya usafirishaji abiria na mizigo kwa njia ya barabara zilipungua kwa asilimia 14.0 kutoka ajali 1,340 mwaka 2019 hadi ajali 1,152 mwaka 2020. Upungufu huo ulitokana na kuendelea kufanya kaguzi za mara kwa mara zilizoambatana na kufungiwa kwa mabasi yasiyo na ubora wa kutembea barabarani, kutumia mfumo wa udhibiti mwendo wa mabasi, upimaji ulevi kwa madereva na matumizi ya madereva wawili kwa safari zilizozidi saa nane.

**Jedwali Na. 16.2: Mchanganuo wa Ajali za Barabarani Mwaka 2018-2020**

| **Ajali** | **2018** | **2019** | **2020** | **Badiliko (Asilimia)** |
|---|---:|---:|---:|:---:|
| Mabasi ya abiria | 620 | 442 | 330 | -25.3 |
| Magari ya mizigo | 469 | 331 | 407 | 23.0 |
| Bajaji/Pikipiki | 876 | 567 | 415 | - 26.8 |
| **Jumla** | **1,965** | **1,340** | **1,152** | **-14.0** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Nchi Kavu

**Usafiri kwa Njia ya Reli**

**Shirika la Reli Tanzania**

376. Shirika la Reli Tanzania lilisafirisha shehena ya mizigo tani 339,671 kwa umbali wa kilometa 304,826,099 mwaka 2020 ikilinganishwa na tani 355,079 kwa kilometa 366,119,797 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 4.3. Upungufu huo ulitokana

na mafuriko yaliyosababisha kufungwa kwa njia ya reli kwa muda mrefu katika maeneo ya Kilosa-Gulwe, Mto Ugala, Ruvu-Mruazi, Mnyusi-Korogwe-Mombo, Bwiko na Muheza na kufungwa kwa njia ya reli kwa masaa 8 hadi 72 kwa wiki kutokana na ukarabati wa njia ya reli kutoka Dar es Salaam-Isaka.

377. Shirika lilisafirisha abiria 449,497 kwa njia kuu kwa umbali wa kilometa 343,842,068 mwaka 2020 ikilinganishwa na abiria 492,423 waliosafirishwa kwa umbali wa kilometa 428,739,684 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 8.7. Kwa upande wa huduma ya usafiri wa treni katika Jiji la Dar es Salaam, Shirika lilisafirisha abiria 3,069,168 kwa umbali wa kilometa 98,213,376 mwaka 2020 ikilinganishwa na abiria 3,577,313 kwa umbali wa kilometa 114,474,016 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 14.2. Upungufu huo ulitokana na sharti la kuwa na idadi maalumu ya abiria katika kila behewa ili kukabiliana na maambukizi ya UVIKO-19.

**Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia**

378. Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia - TAZARA ilisafirisha tani 182,792 za mizigo mwaka 2020 ikilinganishwa na tani 175,599 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 4.1. Ongezeko hilo lilitokana na kukarabatiwa kwa njia ya reli na kuanza kutumika kwa injini 3 zilizokarabatiwa.

**Jedwali Na.16.3: Shehena ya Mizigo Iliyosafirishwa (Tani) Mwaka 2019-2020**

| Aina ya Mizigo | 2019 | 2020 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---:|---:|:---:|
| Kwenda nje ya nchi | 68,253 | 86,526 | 26.8 |
| Kutoka nje ya nchi | 86,240 | 66,055 | -23.4 |
| Ndani ya Tanzania na Zambia (TAZARA) | 21,106 | 30,211 | 43.1 |
| **Jumla** | **175,599** | **182,792** | **4.1** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia

379. Mwaka 2020, TAZARA ilisafirisha abiria 2,727,852 ikilinganishwa na abiria 3,046,002 waliosafirishwa mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 10.4. Kati ya hao, abiria 493,799 walikuwa wa safari ndefu, abiria 420,945 wa treni ya Udzungwa na abiria 1,813,108 wa treni ya jiji la Dar es Salaam. Upungufu huo ulitokana na uhaba wa vitendea kazi na kusitishwa kwa treni kuvuka mipaka kwenda Zambia na kuja Tanzania ili kuzuia maambukizi ya UVIKO - 19.

**Jedwali Na. 16.4: Mchanganuo wa Abiria Waliosafirishwa Mwaka 2019 -2020**

| Aina ya Abiria | 2019 | 2020 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---:|---:|:---:|
| Safari ndefu | 494,059 | 493,799 | -0.1 |
| Udzungwa | 396,895 | 420,945 | 6.1 |
| Jiji la Dar es Salaam | 2,155,048 | 1,813,108 | -15.9 |
| **Jumla** | **3,046,002** | **2,727,852** | **-10.4** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia


**Usafiri wa Anga**

**Mamlaka ya Usafiri wa Anga**

380. Mamlaka ya Usafiri wa Anga nchini ilisajili kwa mara ya kwanza ndege nne (4) mwaka 2020 ikilinganishwa na ndege 15 zilizosajiliwa mwaka 2019. Katika kipindi hicho, Mamlaka ilikagua ndege 76 na kutoa vyeti vya ubora ikilinganishwa na ndege 49 zilizokaguliwa mwaka 2019. Aidha, kufikia Desemba 2020, mashirika 27 ya ndege za kimataifa yalitoa huduma kwa utaratibu wa mikataba ya usafiri wa anga baina ya Tanzania na nchi nyingine ikilinganishwa na mashirika 22 mwaka 2019.

381. Idadi ya abiria waliosafiri kwa njia ya anga ilikuwa 2,773,539 mwaka 2020 ikilinganishwa na abiria 5,487,679 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 49.5. Upungufu huo ulitokana na mashirika ya ndege kusitisha safari za ndege 22 katika kipingi cha kuanzia mwezi Machi hadi Mei 2020 kutokana na mlipuko wa UVIKO-19. Aidha, katika kipindi hicho, idadi ya abiria waliosafiri ndani ya nchi ilipungua kufikia abiria 1,830,117 kutoka abiria 2,892,701 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 58.1. Upungufu huo ulitokana na kupungua kwa idadi ya watalii kutokana na maambukizi ya UVIKO-19.


**Kielelezo Na.16.1: Idadi ya Abiria Waliotumia Usafiri wa Anga Kimataifa na Ndani ya Nchi Mwaka 2016-2020**




| | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 |
|---|---|---|---|---|---|
| KIMATAIFA | 2,216,950 | 2,756,372 | 2,593,862 | 2,594,978 | 943,422 |
| NDANI YA NCHI | 2,695,236 | 2,257,058 | 2,593,800 | 2,892,701 | 1,830,117 |
| JUMLA | 4,912,186 | 5,013,430 | 5,187,662 | 5,487,679 | 2,773,539 |


382. Mwaka 2020, kulikuwa na jumla ya safari za ndege 121,255 ikilinganishwa na safari 292,105 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 58.5. Aidha, mizigo iliyosafirishwa ilikuwa tani 24,452 mwaka 2020 ikilinganishwa na tani 28,202 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 13.3. Kupungua kwa idadi ya abiria na mizigo iliyosafirishwa kulitokana na mashirika 22 ya ndege ya kimataifa kusitisha safari na kufungwa kwa anga za nchi mbalimbali kulikosababishwa na UVIKO-19.

**Kielelezo Na. 16.2: Idadi ya Safari za Ndege Mwaka 2016-2020**




| | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 |
|---|---|---|---|---|---|
| KIMATAIFA | 41,753 | 194,405 | 202,402 | 247,803 | 17,885 |
| NDANI YA NCHI | 191,507 | 42,977 | 43,670 | 44,302 | 103,370 |
| JUMLA | 233,260 | 237,382 | 246,072 | 292,105 | 121,255 |

**Kielelezo Na.16.3: Tani za Mizigo Zilizosafirishwa Mwaka 2016-2020**




| | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 |
|---|---|---|---|---|---|
| KIMATAIFA | 24,059 | 1,967 | 2,003 | 2,230 | 20,333 |
| NDANI YA NCHI | 3,303 | 25,482 | 25,907 | 25,972 | 4,119 |
| JUMLA | 27,362 | 27,449 | 27,910 | 28,202 | 24,452 |

**Kampuni ya Ndege Tanzania**

383. Kampuni ya Ndege Tanzania - ATCL iliendelea kutoa huduma katika vituo vya ndani 10 mwaka 2020 ikilinganishwa na vituo 11 mwaka 2019. Vituo hivyo ni Bukoba, Dar es Salaam, Dodoma, Kigoma, Kilimanjaro, Mbeya, Mwanza, Tabora, Zanzibar na Mpanda. Kupungua kwa idadi ya vituo kulitokana na maboresho ya kiwanja cha ndege cha Iringa. Kabla ya kusitishwa kwa safari za ndege za kimataifa mwezi Machi 2020, safari za nje ya nchi ziliendelea kutolewa katika vituo vya Hahaya (Comoro), Entebbe (Uganda), Lusaka (Zambia), Bujumbura (Burundi), Harare (Zimbabwe) na Mumbai (India).

384. Mwaka 2020, ATCL ilisafirisha jumla ya abiria 472,374 ikilinganishwa na abiria 703,610 waliosafirishwa mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 32.9. Upungufu huo ulitokana na ATCL kusitisha safari katika vituo vyote vya nje pamoja na kupunguza idadi ya miruko kutokana na mataifa mbalimbali kufunga anga na mipaka ili

kujikinga na maambukizi ya UVIKO-19. Kwa upande mwingine, tani 1,125 za mizigo ya ndani na nje ya nchi zilisafirishwa mwaka 2020 ikilinganishwa na tani 1,710.2 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 34.2. Upungufu huo ulitokana na kusitishwa kwa safari za nje ya nchi ikiwemo India iliyokuwa inaongoza kwa usafirishaji wa mizigo ya dawa.

**Usafiri kwa njia ya Maji**

**Utoaji wa Leseni**

385. Mwaka 2020, leseni 903 za uwakala wa ugomboaji shehena ipitayo katika bandari na maeneo mengine ya kiforodha zilitolewa ikilinganishwa na leseni 824 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 9.6. Ongezeko hilo lilitokana na usajili wa mawakala wapya. Aidha, leseni 25 za uwakala wa meli zilitolewa mwaka 2020 ikilinganishwa na leseni 27 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 7.4. Upungufu huo ulitokana na kuanza kwa utekelezaji wa Sheria ya Uwakala wa Meli Tanzania ya Mwaka 2017 ambayo imeorodhesha baadhi ya aina za meli kuwa chini ya Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania.

386. Mwaka 2020, leseni za wakusanyaji mizigo zilikuwa 31 ikilinganishwa na leseni 28 zilizotolewa mwaka 2019. Aidha, leseni 47 za upimaji uzito wa makasha zilitolewa mwaka 2020 ikilinganishwa na leseni 41 mwaka 2019. Kuongezeka kwa leseni hizo kulitokana na kuimarika kwa shughuli na fursa katika utoaji huduma za usafiri na usafirishaji kwa njia ya maji.

387. Mwaka 2020, leseni 42 za bandari kavu zilitolewa ikilinganishwa na leseni 27 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 55.6. Ongezeko hilo limetokana na kunyambulishwa kwa leseni 15 za sehemu za kuhifadhia makasha nchi kavu ambazo ni leseni ya yadi ya kuhifadhia makasha matupu (Empty Container Depot - ECD), leseni ya bandari kavu (Inland Container Depot - ICD) na leseni ya yadi ya kupakia kwenye makasha (Container Freight Station - CFS) ambapo hapo awali leseni moja ilikuwa inatumika katika maeneo yote matatu.

**Jedwali Na. 16.5: Utoaji Leseni Mwaka 2019-2020**

| Na. | Aina ya leseni | 2019 | 2020 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Ugomboaji wa shehena | 824 | 903 | 9.6 |
| 2 | Uwakala wa Meli | 27 | 25 | -7.4 |
| 3 | Wakusanyaji mizigo | 28 | 31 | 10.7 |
| 4 | Wapimaji Uzito wa Makasha | 41 | 47 | 14.6 |
| 5 | Bandari Kavu | 27 | 42 | 55.6 |

**Chanzo:** Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania

## Vyombo vya Usafiri Majini

388. Mwaka 2020, vyombo 4,348 vya usafiri majini vilipewa leseni ikilinganishwa na vyombo 4,172 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 4.2. Ongezekeo hilo lilitokana na kaguzi za mara kwa mara na utolewaji wa elimu kwa wamiliki wa vyombo hivyo kuhusu umuhimu wa kuwa na leseni.

389. Mwaka 2020, Kituo cha Utafutaji na Uokozi kilitoa taarifa za matukio 10 ya ajali za majini ikilinganishwa na matukio 15 mwaka 2019. Kupungua kwa matukio ya ajali kulitokana na kutolewa kwa elimu ya usalama kupitia mikutano 454 ya uelimishaji iliyofanyika mwaka 2020 ikilinganishwa na mikutano 146 mwaka 2019. Aidha, sababu nyingine ni kuongezeka kwa kaguzi za usalama wa vyombo vya usafiri majini kwa meli zenye uwezo wa kubeba zaidi ya tani 50 ambapo kaguzi 408 zilifanyika mwaka 2020 ikilinganishwa na kaguzi 369 mwaka 2019 na kwa upande wa meli zenye uwezo wa kubeba chini ya tani 50 kaguzi 7,095 zilifanyika ikilinganishwa na kaguzi 6,539 mwaka 2019.

## Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania

390. Mwaka 2020 Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania – TPA ilihudumia Jumla ya shehena tani milioni 17.04 ikilinganishwa na tani milioni 17.11 zilizohudumiwa mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 0.5. Upungufu huo ulisababishwa na kuathirika kwa shughuli za uchumi kwa nchi zinazofanya biashara na Tanzania kutokana na athari za mlipuko wa UVIKO - 19.

**Jedwali Na. 16.6: Shehena zilizosafirishwa (Tani `000') Mwaka 2016-2020**

| Kituo (Bandari) | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | Badiliko (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Bandari Kuu za Mwambao | | | | | | |
| Dar es Salaam | 13,581 | 13,762 | 15,074 | 16,023 | 15,858 | -1.0 |
| Tanga | 587 | 527 | 581 | 571 | 475 | -16.8 |
| Mtwara | 379 | 417 | 139 | 122 | 189 | 54.9 |
| **Jumla ndogo** | 14,547 | 14,706 | 15,794 | 16,716 | 16,522 | -1.2 |
| Bandari Ndogo na Bandari za Maziwa Makuu | | | | | | |
| Kilwa, Lindi , Mafia, Bagamoyo na Pangani | 38 | 42 | 18 | 32 | 107 | 234.4 |
| Mwanza | 119 | 92 | 122 | 163 | 142 | -12.9 |
| Kigoma | 124 | 167 | 201 | 206 | 250 | 21.4 |
| Kyela | 9 | 1 | 9 | 1 | 17 | 1600.0 |
| ***Jumla ndogo*** | 290 | 302 | 350 | 402 | 516 | 28.4 |
| ***Jumla Kuu*** | 14,837 | 15,008 | 16,144 | 17,118 | 17,038 | -0.5 |

**Chanzo**: Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania

391. Mwaka 2020, makasha 717,301 yenye urefu wa futi 20 (TEUs) yalihudumiwa katika bandari za Dar es Salaam, Mtwara na Tanga ikilinganishwa na makasha 736,460 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 2.6. Katika kipindi hicho, makasha yaliyohudumiwa katika bandari ya mtwara yalipungua na kufikia makasha 19 kutoka makasha 3,695 mwaka 2019 kutokana na mabadiliko ya mfumo wa uuzaji na ununuzi wa korosho. Aidha, Kitengo cha Mizigo ya Kawaida kinachosimamiwa na Mamlaka

kilihudumia makasha 108,227 yenye urefu wa futi 20 (TEUs) ikilinganishwa na makasha 121,429 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 10.9. Vile vile, Kampuni ya Kimataifa ya Kupakua na Kupakia Makasha Tanzania – TICTS ilihudumia jumla ya makasha 601,654 yenye urefu wa futi 20 (TEUs) ikilinganishwa na makasha 605,002 yaliyohudumiwa mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 0.6. Upungufu huo ulisababishwa na kuathirika kwa shughuli za uchumi kwa nchi zinazofanya biashara na Tanzania kutokana na athari za mlipuko wa UVIKO - 19.

**Jedwali Na. 16.7: Shehena ya Makasha (TEUs) katika Bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara Mwaka 2016-2020**

| | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| TICTS | 465,848 | 482,836 | 591,776 | 605,002 | 601,654 | -0.55 |
| General Cargo | 137,442 | 134,430 | 113,455 | 121,429 | 108,227 | -10.87 |
| **Jumla Ndogo** | 603,290 | 617,266 | 705,231 | 726,431 | 709,881 | -2.28 |
| Tanga | 6,996 | 6,539 | 7,511 | 6,334 | 7,401 | 16.85 |
| Mtwara | 23,754 | 40,924 | 12,633 | 3,695 | 19 | -99.49 |
| **Jumla Ndogo** | 30,750 | 47,463 | 20,144 | 10,029 | 7,420 | -26.01 |
| **Jumla Kuu** | **634,040** | **664,729** | **725,375** | **736,460** | **717,301** | **-2.60** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania

392. Mwaka 2020, Mamlaka ilihudumia abiria 2,879,455 ikilinganishwa na abiria 2,609,567 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 10.3. Ongezeko hilo linatokana na ujenzi wa meli mpya katika maeneo hayo. Katika kipindi hicho, abiria waliohudumiwa na Mamlaka waliongezeka katika bandari za Mwanza na Kyela. Aidha, abiria waliohudumiwa katika bandari za Dar es Salaam, Tanga na Kigoma walipungua kutokana na baadhi ya meli kuwa katika matengenezo.

**Jedwali Na. 16.8: Idadi ya Abiria Waliohudumiwa Mwaka 2016-2020**

| Bandari | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Dar es Salaam | 1,734,589 | 1,662,730 | 1,501,648 | 1,994,809 | 1,639,683 | (17.8) |
| Tanga | 1,422 | 43,184 | 43,613 | 67,699 | 55,403 | (18.2) |
| Mwanza | 109,768 | 0 | 423,749 | 541,121 | 1,176,918 | 117.5 |
| Kigoma | 13,676 | 11,844 | 3,643 | 2,148 | 1,781 | (17.1) |
| Kyela | 4,627 | 890 | 1,598 | 3,790 | 5,670 | 49.6 |
| **Jumla** | **1,864,082** | **1,718,648** | **1,974,251** | **2,609,567** | **2,879,455** | 10.3 |

**Chanzo:** Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania

## Muda wa Meli Kukaa Bandarini

393. Mwaka 2020, muda wa meli kukaa bandarini ulikuwa siku 4.0 ikilinganishwa na siku 4.3 mwaka 2019. Katika Kitengo cha Makasha na Kitengo cha Mizigo ya Kawaida, muda wa meli kukaa bandarini ulikuwa siku 3.3 na 3.1 kutoka siku 3.5 na 3.6 mwaka

2019 mtawalia. Kupungua kwa siku za meli kukaa bandarini kwa kitengo cha makasha na mizigo ya kawaida kulitokana na kukamilika na kuanza kutumika kwa gati mpya ya kushusha na kupakia magari melini. Kwa upande wa kitengo cha mafuta, muda wa meli kukaa bandarini ulipungua na kufikia siku 5.6 kutoka siku 5.8 mwaka 2019. Kupungua kwa siku za meli kukaa bandarini kwa kitengo cha mafuta kulitokana na uboreshaji wa mifumo ya ushushaji katika gati za Kurasini Oil Jet -KOJ na Single Buoy Mooring - SBM.

**Jedwali Na.16.9: Muda wa Meli Kukaa Bandarini Mwaka 2016-2020**

| | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 |
|---|---|---|---|---|---|
| Makasha | 1.8 | 2 | 2.2 | 3.5 | 3.3 |
| G/C | 2.6 | 2.8 | 3.2 | 3.6 | 3.1 |
| Mafuta | 5.3 | 5.5 | 6.6 | 5.8 | 5.6 |
| **Wastani** | **3.2** | **3.4** | **4.0** | **4.3** | **4.0** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania

### Shehena za Nchi Jirani

394. Mwaka 2020 jumla ya tani 5,340,287 za mizigo ya kwenda nchi jirani zilihudumiwa katika bandari ya Dar es Salaam ikilinganishwa na tani 5,871,887 za mwaka 2019 sawa na upungufu wa asilimia 9.1. Hii ilitokana na kupungua kwa shehena za mizigo kwenda nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Zambia kulikosababishwa na athari za mlipuko wa UVIKO - 19. Hata hivyo, katika kipindi hicho shehena za mizigo kwa nchi za Burundi, Malawi na Rwanda ziliongezeka.

**Jedwali Na. 16.10: Shehena za Nchi Jirani**

| Nchi | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | Asilimia (Badiliko) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Zambia | 1,739,306 | 2,021,086 | 1,504,014 | 1,763,052 | 1,159,013 | -34.3 |
| J.D. Kongo | 1,152,747 | 1,176,764 | 1,779,617 | 1,914,138 | 1,840,657 | -3.8 |
| Burundi | 320,374 | 415,993 | 379,704 | 453,280 | 476,809 | 5.2 |
| Rwanda | 862,639 | 1,061,193 | 911,870 | 1,238,540 | 1,239,238 | 0.1 |
| Malawi | 128,722 | 276,039 | 311,138 | 336,714 | 407,472 | 21.0 |
| Uganda | 165,919 | 271,957 | 188,591 | 140,960 | 153,995 | 9.2 |
| Nyinginezo | 95,250 | 85,340 | 98,542 | 25,203 | 63,104 | 150.4 |
| **Jumla** | **4,464,956** | **5,308,372** | **5,173,477** | **5,871,887** | **5,340,287** | **-9.1** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania

### Uchukuzi Kwenye Maziwa

### Kampuni ya Huduma za Meli

395. Mwaka 2020, abiria 173,859 walisafirishwa ikilinganishwa na abiria 96,892 waliosafirishwa mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 79.4. Ongezeko hilo lilitokana na kuanza kutoa huduma baada ya matengenezo kwa meli za *New Victoria* na *New Butiama* katika Ziwa Victoria. Katika kipindi hicho, tani 19,391.0 za mizigo zilisafirishwa ikilinganishwa na tani 34,304.4 mwaka 2019, sawa na upungufu wa

asilimia 44.0. Upungufu huo ulitokana na kuharibika kwa meli za *MT Sangara* na *MV Umoja*.

**Kampuni ya Meli ya China na Tanzania**

396. Kampuni ya Meli ya China na Tanzania ilisafirisha shehena ya tani 609,000 mwaka 2020 ikilinganishwa na tani 600,000 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 1.5. Ongezeko hilo lilitokana na uhakika wa upatikanaji wa shehena baada ya meli ya *MV Changshun II* kukodishwa kwa Kampuni ya COSCO *Bulk Refines* yenye uzoefu na uwezo katika usafirishaji wa shehena duniani.

397. Makasha 50,000 yalihudumiwa na Kampuni ya Meli ya China na Tanzania katika bandari ya Dar es Salaam mwaka 2020 ikilinganishwa na makasha 47,000 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 6.4. Ongezeko hilo lilitokana na utekelezaji wa mkakati wa kutafuta masoko unaohakikisha kuwa asilimia 20 ya makasha yanayoingiza mizigo nchini yanapata mizigo ya kupeleka nje ya nchi.

**Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania**

398. Mwaka 2020, Mamlaka ya Hali ya Hewa iliendelea kutumia mfumo wa udhibiti wa ubora wa huduma ya hali ya hewa katika sekta mbalimbali zikiwemo usafiri wa anga na maji. Kupitia mfumo huo, ndege 27,348 zilihudumiwa mwaka 2020 ikilinganishwa na ndege 45,966 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 40.5. Hii ilitokana na mashirika 22 ya ndege ya kimataifa kusitisha safari na kufungwa kwa anga za nchi mbalimbali kwa lengo la kujikinga na maambukizi ya UVIKO-19.

399. Mwaka 2020, Mamlaka ilihudumia meli/boti 7,248 katika bahari ya Hindi, Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa ikilinganishwa na meli/boti 4,285 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 69.1. Ongezeko hilo lilitokana na elimu iliyotolewa na Mamlaka kwa watumiaji wa bahari ya Hindi na Maziwa Makuu kuhusu umuhimu wa kutumia huduma za hali ya hewa katika shughuli zao kwa ajili ya usalama na kuongeza ufanisi. Aidha, idadi ya wateja mahsusi waliohudumiwa na Mamlaka iliongezeka na kufikia wateja 2,582 mwaka 2020 kutoka wateja 631 mwaka 2019. Hii ilitokana na utekelezaji wa miradi mikubwa ya Serikali iliyotumia huduma ya hali ya hewa na kuongezeka kwa uelewa kuhusu matumizi ya taarifa za hali ya hewa. Vile vile, kiwango cha usahihi wa utabiri kilifikia asilimia 87.9 mwaka 2020 ikilinganishwa na asilimia 84.5 mwaka 2019 kiwango hicho ni zaidi ya asilimia 70 kinachokubalika kimataifa.

**Jedwali Na. 16.11: Viashiria vya Ufanisi katika Sekta ya Hali ya Hewa**

| Na. | Kipimo cha Utendaji (KPI) | Maelezo | Mwaka | |
|---|---|---|---|---|
| | | | 2019 | 2020 |
| 1 | Kiwango cha usahihi wa utabiri wa siku na msimu (asilimia) | Usahihi wa utabiri | 84.5 | 87.9 |
| 2 | Idadi ya wateja na watumiaji wa huduma za hali ya hewa | Sekta ya usafiri wa anga | 45,966 | 27,348 |
| | | Meli na boti | 4,285 | 7,248 |
| | | Huduma mahsusi | 631 | 2,582 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 3 | Kiwango cha watumiaji na wateja wanaoridhika na huduma za hali ya hewa (asilimia) | Kiwango cha kuridhika | 90 | 91 |

**Chanzo:** Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania

**Udhibiti wa Mionzi**

400. Mwaka 2020, Serikali kupitia Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania ilipokea na kutathmini maombi 457 ya leseni za matumizi na umiliki wa vyanzo vya mionzi ikilinganishwa na maombi ya leseni 439 yaliyopokelewa mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 4.1. Kati ya maombi hayo, maombi 455 yalipata leseni baada ya kukidhi vigezo ikilinganishwa na maombi 435 mwaka 2019. Aidha, Tume ilipima kiasi cha mionzi kwa wafanyakazi 1,982 kutoka katika vituo 436 mwaka 2020 ikilinganishwa na wafanyakazi 1,213 kutoka vituo 390 mwaka 2019. Matokeo ya upimaji huo yalionesha kuwa kiwango cha mionzi kwa wafanyakazi ndani ya miezi mitatu kilikuwa chini ya mSv 5 ambacho kinakubalika kimataifa. Hadi Desemba 2020, vituo vinavyotumia mionzi vilifikia 981 kutoka vituo 952 hadi Desemba 2019. Vile vile, Tume ilikagua vituo 608 vinavyotumia mionzi na kutoa ushauri wa maboresho ya usalama wa watumiaji na mazingira mwaka 2020 ikilinganishwa na vituo 650 vilivyokaguliwa mwaka 2019.

401. Mwaka 2020, Tume ilipima viwango vya mionzi kwenye sampuli 21,046 ambapo sampuli za mbolea zilikuwa 545, sampuli za sigara na vyakula vya wanyama 1,672 na vyakula vya binadamu 18,829 ikilinganishwa na sampuli 7,873 zilizojumuisha sampuli 143 za mbolea, sampuli 971 za sigara na vyakula vya wanyama, na sampuli 6,759 za vyakula vya binadamu mwaka 2019. Kati ya sampuli za chakula zilizopimwa, sampuli 5,735 ziliingizwa nchini na sampuli 13,094 zilisafirishwa nje ya nchi mwaka 2020 ikilinganishwa na sampuli 2,883 zilizoingizwa nchi na sampuli 3,876 zilizosafirishwa nje ya nchi mwaka 2019. Ongezeko la sampuli zilizopimwa lilitokana na kuimarishwa kwa mifumo ya udhibiti ikiwemo kujiunga na mfumo wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (Tanzania Electronic Single Window System) pamoja na kuongeza wigo wa utoaji huduma kwa kuanzisha ofisi za Tume maeneo ya mipakani.

**HUDUMA ZA MAWASILIANO**

**Huduma za Posta**

402. Mwaka 2020, Shirika la Posta Tanzania lilisafirisha barua 3,705,183 ndani ya nchi ikilinganishwa na barua 6,855,626 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 46.0. Aidha, katika kipindi hicho, barua zilizosafirishwa nje ya nchi zilikuwa 1,173,732 ikilinganishwa na barua 2,187,254 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimai 46.3. Kupungua kwa barua zilizosafirishwa kulitokana na matumizi makubwa ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano pamoja na kuongezeka kwa ushindani katika huduma za posta na usafirishaji.

403. Mwaka 2020, jumla ya vifurushi 2,828 vilisafirishwa ndani ya nchi ikilinganishwa na vifurushi 40,469 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 93.0. Upungufu huo ulitokana na ongezeko la huduma ya usafirishaji wa vifurushi kwa kutumia mabasi ya abiria. Aidha, vifurushi 1,064 vilisafirishwa nje ya nchi mwaka 2020 ikilinganishwa na vifurushi 3,304 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 67.8. Vile vile, rejesta 74,639 zilisafirishwa nchini mwaka 2020 ikilinganishwa na rejesta 160,290 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 53.4. Rejesta 6,112 zilisafirishwa nje ya nchi mwaka 2020 ikilinganishwa na rejesta 17,490 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 65.1.

404. Mwaka 2020, nyaraka na vipeto vilivyotumwa kwa njia ya haraka - EMS nchini vilikuwa 520,217 ikilinganishwa na nyaraka na vipeto 615,663 vilivyotumwa mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 15.5. Upungufu huo ulitokana na ongezeko la huduma ya usafirishaji wa vifurushi kwa kutumia mabasi ya abiria. Aidha, nyaraka na vipeto vilivyotumwa nje ya nchi kwa njia ya haraka vilikuwa 6,774 mwaka 2020 ikilinganishwa na nyaraka na vipeto 14,206 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 52.3. Kwa ujumla, huduma za posta nje ya nchi zilipungua kutokana na kusitishwa kwa huduma za usafirishaji sehemu mbalimbali duniani katika harakati za kukabiliana na maambukizo ya UVIKO – 19.

405. Mwaka 2020, idadi ya barua na nyaraka 44,065 zilipokelewa na kusambazwa kwa njia ya huduma ya usambazaji wa barua za haraka ndani ya miji - pCUM mwaka 2020 ikilinganishwa na barua na nyaraka 57,716 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 23.7. Upungufu huo ulisababishwa na ongezeko la usambazaji usio rasmi wa barua za haraka ndani ya miji kwa kutumia pikipiki.

406. Mwaka 2020, miamala ya fedha 69 ya *money gram* ilihaulishwa kwa njia ya kielektroniki ikilinganishwa na miamala 808 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 91.5. Katika kipindi hicho, miamala ya fedha 53 ilitumwa kupitia Mfumo wa Kimataifa wa Utumaji Fedha ikilinganishwa na miamala 1,211 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 95.6. Upungufu huo ulitokana na kubadilishwa kwa vigezo vya utumaji wa miamala ya *Money Gram* na kusababisha kusitishwa kwa huduma hiyo.

407. Mwaka 2020, wateja 230 walihudumiwa kupitia huduma ya kufanya malipo kwa njia ya uwakala wa *Post Giro* ndani ya nchi ikilinganishwa na wateja 18,198 waliohudumiwa mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 98.7. Kupungua kwa wateja kulitokana na Mifuko ya Taifa ya Hifadhi ya Jamii kusitisha rasmi matumizi ya huduma za *Posto Giro* kulipa pensheni ya wastaafu.

**Huduma za Simu**

408. Mwaka 2020, idadi ya kadi za simu za kiganjani zilifikia 51,220,233 kutoka kadi 47,761,520 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 7.2. Ongezeko hilo lilitokana na kupanuka kwa miundombinu ya mawasiliano iliyosababisha kukua kwa huduma za habari na mawasiliano kwa kutumia mitandao ya kijamii na matumizi ya simu za kiganjani katika kufanya miamala ya fedha. Hadi Desemba 2020, kadi za simu za kiganjani zilizosajiliwa kwa kutumia alama za vidole zilikuwa 48,745,574, sawa na asilimia 95.2 ya kadi zote. Katika kuhakikisha wananchi wenye kadi zisizosajiliwa kwa kutumia alama za vidole wanasajiliwa, Serikali kupitia Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa inaendelea kuharakisha zoezi la utoaji wa vitambulisho vya Taifa ili kuwezesha usajili wa kadi hizo. Katika kipindi hicho, kadi za simu za mezani zilipungua na kufikia 72,469 kutoka kadi 76,288 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 5.0.

409. Mwaka 2020, gharama za kupiga simu ndani ya mtandao zilipungua kwa asilimia 17.2 na kufikia shilingi 72 kwa dakika kutoka shilingi 87 mwaka 2019. Gharama za kupiga simu nje ya mtandao zilipungua kwa asilimia 22.3 na kufikia shilingi 73 kwa dakika mwaka 2020 kutoka shilingi 94 mwaka 2019. Kupungua kwa gharama kulitokana na kuongezeka kwa ushindani kwa watoa huduma.

410. Kwa upande wa simu za kimataifa, gharama za kupiga simu ndani ya Afrika Mashariki zilikuwa shilingi 1,201 kwa dakika mwaka 2020 ikilinganishwa na shilingi 732 mwaka 2019. Aidha, gharama za kupiga simu kwenda mataifa mengine zilikuwa shilingi 1,942 kwa dakika mwaka 2020 ikilinganishwa na shilingi 1,439 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 35.0. Ongezeko hilo lilitokana na gharama kubwa zinazotozwa na watoa huduma wa kimataifa.

**Huduma za Intaneti**

411. Mwaka 2020, watumiaji wa huduma za intaneti walikuwa milioni 28.5 ikilinganishwa na watumiaji wa huduma hiyo milioni 25.8 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 10.4. Ongezeko hilo lilitokana na kuendelea kupanuka kwa maeneo yaliyofikiwa na miundombinu ya huduma za mtandao wa intaneti.

**Jedwali Na. 16.12: Watumiaji wa Intaneti Nchini Mwaka 2019-2020**

| **Aina ya Huduma** | **2019** | **2020** | **Badiliko (Asilimia)** |
|---|---|---|---|
| *Fixed Wireless* | 773,837 | 510,683 | -34.0 |
| *Mobile Wireless* | 24,762,778 | 27,371,350 | 10.5 |
| *Fixed Wired* | 257,946 | 588,472 | 128.1 |
| **Jumla** | **25,794,560** | **28,470,506** | **10.4** |

**Chanzo**: Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania

**Huduma za Utangazaji**

412. Mwaka 2020, idadi ya watumiaji wa huduma za utangazaji kwa kutumia ving'amuzi walifikia 2,972,227 kutoka watumiaji 2,683,513 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 10.8. Watumiaji wa huduma za utangazaji kupita *satellite* waliongezeka kwa asilimia 22.8 mwaka 2020 na kufikia 1,341,686 kutoka watumiaji 1,092,891 mwaka 2019. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uhitaji wa huduma za habari kulikosababishwa na mabadiliko ya teknolojia.

**Jedwali Na. 16.13: Watumiaji wa Huduma za Utangazaji Mwaka 2019-2020**

| Aina | 2019 | 2020 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|
| *Digital Terrestrial Television (DTT)* | 1,432,398 | 1,472,317 | 2.8 |
| *Satellite* | 1,092,891 | 1,341,686 | 22.8 |
| *Cable* | 158,224 | 158,224 | 0 |
| **Jumla** | **2,236,577** | **2,769,841** | **10.8** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania

**Utoaji wa Leseni za Mawasiliano**

413. Mwaka 2020, Mamlaka ya Mawasiliano ilitoa leseni 1,125 za huduma mbalimbali za mawasiliano ikilinganishwa na leseni 1,507 mwaka 2019. Upungufu huo ulitokana na kupungua kwa waombaji wa leseni za V-Sat kutoka leseni 571 hadi leseni 57. Hii ilisababishwa na uombaji mkubwa wa leseni za V - Sat katika mwaka 2019 uliosababisha kupungua kwa uhitaji katika kutumia ungo ndogo kupokea mawasiliano kupitia jukwaa la Satelite (V-SAT) kwa mwaka 2020.

**Jedwali Na. 16.14: Leseni zilizotolewa Mwaka 2019-2020**

| Na. | Aina ya Leseni | 2019 | 2020 |
|---|---|---|---|
| 1 | Kusimika Vifaa vya Mawasiliano | 1 | 0 |
| 4 | Huduma za Mawasiliano Daraja B | 15 | 6 |
| 5 | Maudhui ya Redio | 22 | 15 |
| 6 | Maudhui ya Luninga | 6 | 7 |
| 7 | Ufungaji na Utengenezaji wa Vifaa vya Mawasiliano vya Kieletroniki | 67 | 33 |
| 8 | Kuingiza Nchini Vifaa vya Mawasiliano vya Kieletroniki | 42 | 30 |
| 9 | Kusambaza Nchini Vifaa vya Mawasiliano vya Kieletroniki | 23 | 12 |
| 10 | Kuuza Vifaa vya Mawasiliano vya Kieletroniki | 321 | 606 |
| 11 | Huduma ya Msingi ya Posta | 1 | 0 |
| 12 | Huduma za Kusafirisha Vifurushi na Vipeto | 90 | 39 |
| 13 | *V-SAT* | 571 | 57 |
| 14 | Maudhui ya Mtandaoni | 330 | 305 |
| 15 | Maudhui kutokana na Matumizi | 18 | 15 |
| | **Jumla** | **1,507** | **1,125** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania

**Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano**

414. Hadi Desemba 2020, Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ulifika katika mikoa yote 26 ya Tanzania - bara. Aidha, kupitia miradi mbalimbali inayotekelezwa na Serikali pamoja na watoa huduma za mawasiliano nchini, halmashauri za wilaya 163 zinatumia huduma ya Mkongo wa Taifa. Vile vile, shule za sekondari 1,172 zilifikishiwa huduma ya intaneti na kupewa vifaa vya TEHAMA. Katika kipindi hicho, vyuo vya elimu ya juu na Taasisi za Tafiti 28 viliunganishwa kwenye Mkongo wa Taifa na ofisi za wakuu wa mikoa zilifungiwa seti 43 za vifaa kwa ajili ya mikutano kwa njia ya picha jongevu - *video conference.*

## HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

**Sekta ya Habari**

415. Hadi Desemba 2020, kulikuwa na jumla ya magazeti 250, vituo vya redio 198 na vituo vya runinga 44 vilivyosajiliwa na kupewa leseni ikilinganishwa na magazeti 226, vituo vya redio 183 na vituo vya runinga 43 vilivyosajiliwa hadi Desemba 2019. Magazeti na majarida yaliyosajiliwa/kupewa leseni yaliongezeka kwa asilimia 4.3 na kufikia 24 mwaka 2020 ikilinganishwa na magazeti na majarida 23 mwaka 2019. Katika kipindi hicho, idadi ya vituo vya redio vilivyosajiliwa vilikuwa 15 na runinga kimoja (1) ikilinganishwa na vituo vya redio 21 na runinga nane (8) mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 28.6 na asilimia 87.5 mtawalia. Upungufu wa usajili wa vituo vya redio na runinga ulisababishwa na maendeleo ya sayansi na teknolojia katika sekta ya habari na utangazaji hususan uwepo wa redio na runinga za mtandaoni. Kwa upande mwingine, blogu 14 zilisajiliwa mwaka 2020 ikilinganishwa na blogu 106 zilizosajiliwa mwaka 2019. Kupungua kwa usajili wa blogu kulisababishwa na kuongezeka kwa ushindani katika vyombo vya habari vya mtandaoni.

**Jedwali 16.15: Magazeti, Vituo vya Redio na Runinga, na Blogu Vilivyosajiliwa**

| Mwaka | Idadi ya Magazeti/Majarida | Idadi ya Vituo vya Redio | Idadi ya Vituo vya Runinga | Idadi ya blogu |
|---|---|---|---|---|
| **2015** | 39 | 22 | 1 | 0 |
| **2016** | 26 | 23 | 6 | 0 |
| **2017** | 161 | 6 | 3 | 0 |
| **2018** | 42 | 8 | 3 | 0 |
| **2019** | 23 | 21 | 8 | 106 |
| **2020** | 24 | 15 | 1 | 14 |

**Chanzo:** Idara ya Habari-MAELEZO, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania

**Maendeleo ya Sanaa**

416. Mwaka 2019/20, Bodi ya Filamu Tanzania ilitoa vibali vya kutengeneza filamu na picha jongevu 114 ikilinganishwa na vibali 168 mwaka 2018/19, sawa na upungufu wa asilimia 32.1. Kati ya hivyo, vibali 26 vilitolewa kwa kampuni za ndani na vibali 88 kwa kampuni za nje ya nchi. Aidha, vibali vilivyotolewa kwa kampuni za ndani vilipungua kutoka vibali 34 mwaka 2018/19 hadi vibali 26 mwaka 2019/20, sawa na

upungufu wa asilimia 23.5. Hii ilitokana na mlipuko wa UVIKO-19 uliosababisha kupungua kwa idadi ya watengenezaji wa filamu kutoka nje ya nchi na kuathiri kazi za wazalishaji wa filamu wa ndani waliokuwa washirikiane na wa nje.

**Jedwali 16.16: Idadi ya Vibali vya Kutengeneza Filamu Vilivyotolewa Nchini**

| Mwaka | Vibali vya Wageni | Vibali vya Watanzania | Jumla |
|---|---|---|---|
| 2014/15 | 133 | 36 | 169 |
| 2015/16 | 137 | 31 | 168 |
| 2016/17 | 123 | 30 | 153 |
| 2017/18 | 137 | 46 | 183 |
| 2018/19 | 134 | 34 | 168 |
| 2019/20 | 88 | 26 | 114 |

**Chanzo:** Bodi ya Filamu Tanzania.

**Usajili wa Wabunifu na Kazi za Sanaa**

417. Mwaka 2019/20, Serikali kupitia Taasisi ya Hakimiliki Tanzania - COSOTA ilisajili wanachama wabunifu wa kazi za sanaa 1,378 ikilinganishwa na wanachama 400 mwaka 2018/19. Ongezeko hilo lilitokana na kuanza kutumika kwa mfumo wa usajili kwa njia ya mtandao na utolewaji wa elimu kuhusu hakimiliki. Katika kipindi hicho, Taasisi ilitoa vyeti vya uthibitisho wa umiliki wa hakimiliki 1,241 ikilinganishwa na vyeti 1,158 mwaka 2018/19, sawa na ongezeko la asilimia 7.2. Aidha, leseni 354 za watumiaji wa kazi zenye hakimiliki zilitolewa mwaka 2019/20 ikilinganishwa na leseni 317 mwaka 2018/19, sawa na ongezeko la asilimia 11.7.

**Baraza la Kiswahili la Taifa**

418. Mwaka 2019/20, Serikali kupitia Baraza la Kiswahili la Taifa - BAKITA lilirusha vipindi 1,020 vilivyohusu teknolojia ya lugha, sarufi na fasihi ya Kiswahili kupitia redio na runinga ikilinganishwa na vipindi 780 mwaka 2018/19, sawa na ongezeko la asilimia 30.8. Aidha, miswada ya ithibati ya lugha kwa vitabu vinavyokusudiwa kutumika shuleni iliongezeka na kuwa 213 ikilinganishwa na miswada 38 mwaka 2018/19. Ongezeko hilo lilitokana na kuwapo kwa vitabu vingi kutoka katika mashirika yanayoandaa vitabu vya watoto.

419. Mwaka 2019/20, Baraza lilitafsiri nyaraka 869 na kuhariri nyaraka 41 ikilinganishwa na nyaraka 5,061 zilizotafsiriwa na nyaraka saba (7) zilizohaririwa mwaka 2018/19. Kupungua kwa idadi ya nyaraka zilizotafsiriwa kulitokana na mlipuko wa UVIKO-19 uliosababisha kupungua kwa wageni na hivyo kushuka kwa uhitaji wa

tafsiri za nyaraka. Aidha, nyaraka zilizohaririwa ziliongezeka kutokana na kuongezeka kwa uelewa wa umma kuhusu umuhimu wa uhariri wa nyaraka mbalimbali zikiwemo nyaraka za Serikali, vitabu vya kiada na ziada.

**Jedwali Na. 16.17: Idadi ya Huduma Zilizotolewa**

| Mwaka | Vipindi vya redio na runinga | Huduma ya ithibati | Huduma ya tafsiri | Huduma ya ukalimani | Huduma ya uhariri | Makosa yaliyobainika kutumiwa katika vyombo vya habari |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **2015** | 118 | 121 | 320 | 3 | 8 | 1,200 |
| **2016** | 110 | 60 | 350 | 2 | 20 | 1,048 |
| **2017** | 87 | 61 | 268 | 3 | 10 | 805 |
| **2018** | 847 | 63 | 1,607 | 3 | 39 | 848 |
| **2019** | 780 | 38 | 5,061 | 2 | 7 | 1,081 |
| **2020** | 1,020 | 213 | 869 | 0 | 41 | 1,380 |

**Chanzo:** Baraza la Kiswahili la Taifa

**Maendeleo ya Kiswahili Katika Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika**

420. Lugha ya Kiswahili ilipitishwa kuanza kutumika rasmi katika mikutano ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika - SADC wakati wa Mkutano wa 39 wa Wakuu wa nchi na Serikali wa SADC uliofanyika Jijini Dar es salaam mwaka 2019 na kuungana na lugha za Kiingereza, Kireno na Kifaransa zinazotumiwa na nchi wanachama wa SADC. Mwaka 2020, baadhi ya nchi za SADC zilionesha juhudi za kuingiza lugha ya Kiswahili katika mitaala ya kufundishia zikiwemo Afrika ya Kusini na Namibia. Aidha, nchi za Afrika ya Kusini, Zimbambwe na Ghana zilianza kufundisha lugha ya Kiswahili katika baadhi ya shule za msingi na vyuo vikuu. Katika kuhakikisha lugha ya Kiswahili inafundishwa katika vyuo vikuu vyingi vya nchi za SADC, jitihada mbalimbali zinaendeleakuchukuliwa zikiwemo: kuandaliwa na kuchapishwa kwa kamusi ndogo ya Kiswahili - Kiingereza - Kireno itakayosaidia kubidhaisha lugha ya Kiswahili katika nchi za SADC; na kukamilika kwa maandalizi ya Muswada wa Kamusi ya Kiswahili-Kiingereza-Kifaransa.

**Maendeleo ya Michezo**

421. Mwaka 2020, vilabu vya michezo vilivyosajiliwa viliongezeka na kufikia 9,275 kutoka vilabu 9,165 mwaka 2019. Vilabu vipya 110 vya michezo vilisajiliwa mwaka 2020 ikilinganishwa na vilabu 231 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 52.4. Aidha, vyama vya michezo vilivyosajiliwa viliongezeka na kufikia 488 kutoka vyama

476 mwaka 2019. Mwaka 2020, vilabu vya michezo vilivyosajiliwa vilikuwa 12 ikilinganishwa na vilabu 18 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 66.7. Kwa upande mwingine, wakuzaji/mawakala wa michezo 88 walisajiliwa ikilinganishwa na wakuzaji/mawakala 62 mwaka 2019. Mwaka 2020, wakuzaji/mawakala walikuwa 26 ikilinganishwa na wakuzaji/mawakala 19 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 36.8. Ongezeko hilo lilitokana na wadau wa michezo kuhamasika kuanzisha shughuli za ukuzaji/uwakala wa michezo kulikosababishwa na uhamasishaji uliofanyika katika mikoa ya Arusha, Morogoro, Tanga, Kilimanjaro, Mara, Iringa na Ruvuma. Kadhalika, taasisi 10 za michezo zilisajiliwa mwaka 2020 ambapo nane (8) zipo mkoa wa Dar es salaam, moja (1) Tanga na moja (1) Ruvuma.

**Jedwali Na. 16.18: Usajili wa Vilabu, Vyama, Vituo/Shule, Wakuzaji/Mawakala wa Michezo na Taasisi za Michezo**

| Mwaka | Vilabu vya Michezo | Vyama vya Michezo | Vituo/shule za Michezo | Wakuzaji /Mawakala wa Michezo | Taasisi za michezo |
|---|---|---|---|---|---|
| **2015** | 224 | 15 | 12 | 0 | 0 |
| **2016** | 331 | 9 | 15 | 0 | 0 |
| **2017** | 288 | 29 | 13 | 14 | 0 |
| **2018** | 212 | 23 | 18 | 29 | 0 |
| **2019** | 231 | 18 | 21 | 19 | 0 |
| **2020** | 110 | 12 | 5 | 26 | 10 |

**Chanzo:** Wizara ya Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo

## SHIRIKA LA RELI TANZANIA

Jedwali Na. 54

| Maelezo | Kipimo | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Urefu wa Reli | KM | 2,707 | 2,707 | 2,707 | 2,707 | 2,707 | 2,707 | 2,707 | 2,707 |
| Magari ya Moshi: | Namba | 45 | 45 | 30 | 44 | 44 | 30 | 30 | 30 |
| Mvuke | Namba | - | - | - | - | - | - | - | |
| Dizeli: | Namba | 45 | 45 | 30 | 44 | 44 | 30 | 30 | 30 |
| Mainlain | | 38 | 38 | 21 | 40 | 40 | 28 | 28 | 28 |
| Shunting | | 7 | 7 | 9 | 4 | 4 | 2 | 2 | 2 |
| Jumla ya mabehewa: | Namba | 1,200 | 1,214 | 1,155 | 426 | 426 | 327 | 327 | 180 |
| Abiria | Namba | 91 | 91 | 56 | 56 | 56 | 71 | 71 | 115 |
| Mizigo ya kawaida | Namba | 681 | 590 | 561 | 22 | 22 | 18 | 18 | |
| Mafuta | Namba | 178 | 203 | 196 | 123 | 123 | 95 | 95 | 147 |
| Mifugo | Namba | 39 | 64 | 64 | 27 | 27 | 27 | 27 | 91 |
| Mengineyo | Namba | 211 | 266 | 278 | 198 | 198 | 116 | 116 | 27 |
| Uchukuzi | Namba | | | | | | | | |
| Abiria | 000 | 373 | 170 | 196 | 1,707 | 2,150 | 6,012 | 445 | 3,069 |
| Mizigo | Tani'000 | 185 | 127 | 283 | 102 | 170 | 357 | 374 | 340 |

**Chanzo**: Shirika la Reli Tanzania

Jedwali Na. 55 **RELI YA UHURU TANZANIA**

| **Maelezo** | **Kipimo** | **2012** | **2013** | **2014** | **2015** | **2016** | **2017** | **2018** | **2019** | **2020** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Urefu wa Reli Kuu | Km | 1,860 | 1,860 | 1,860 | 1,860 | 1,860 | 1,860 | 1,860 | 1,860 | 1860 |
| Magari ya Moshi | Namba | 13 | 15 | 16 | 17 | 21 | 21 | 18 | 18 | 17 |
| Reli Kuu | Namba | 9 | 11 | 13 | 12 | 14 | 12 | 13 | 13 | 13 |
| Ya kujongeza | Namba | 5 | 4 | 3 | 6 | 7 | 7 | 5 | 5 | 4 |
| Mabehewa ya abiria | Namba | 35 | 52 | 50 | 51 | 56 | 49 | 60 | 61 | 47 |
| Abiria | Namba | 30 | 45 | 44 | 43 | 48 | 40 | 51 | 52 | 35 |
| Chakula | Namba | 2 | 3 | 3 | 3 | 4 | 4 | 4 | 4 | 5 |
| Vifurushi | Namba | 3 | 4 | 3 | 5 | 4 | 5 | 5 | 5 | 7 |
| Mabehewa ya mizigo | Namba | 858 | 1,391 | 1,101 | 1,142 | 1,221 | 1,033 | 1,068 | 1,054 | 803 |
| Mizigo ya kawaida | Namba | 765 | 1,229 | 966 | 1,007 | 1,077 | 972 | 998 | 992 | 659 |
| Mifugo | Namba | - | - | - | - | - | - | - | - | 0 |
| Mafuta | Namba | 59 | 104 | 82 | 82 | 89 | 26 | 70 | 72 | 94 |
| Barafu | Namba | - | 5 | 5 | 5 | 5 | - | - | - | 0 |
| Mengineyo | Namba | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 2 |
| Breki | Namba | 16 | 35 | 30 | 30 | 32 | 30 | 34 | 34 | 34 |
| Ballast | Namba | 17 | 17 | 17 | 17 | 17 | 4 | 15 | 14 | 14 |
| Uchukuzi mizigo (Tani) | 000 | 259 | 245 | 33 | 81 | 96 | 171 | 268 | 155 | 224 |
| Abiria | 000 | 678 | 654 | 287 | 327 | 440 | 443 | 154 | 510 | 534 |

**Chanzo**: Mamlaka ya Reli ya Uhuru

\+ Urefu ni km. 1860.54, km 974.814 zikiwa nchini

Jedwali Na. 56 **USAFIRISHAJI KWA MELI: DAR ES SALAAM**

| Maelezo | Kipimo | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Jumla ya meli | Namba | 1,617 | 1,684 | 1,688 | 1,744 | 1,516 | 1,407 |
| Uwezo wa kubeba mizigo | 000 Tani | 31,614 | 31,278 | 31,287 | 32,513 | 31,200 | 28,532 |
| Jumla ya abiria | 000 Namba | 1,612 | 1,735 | 1,874 | 1,901 | 2,035 | 1,307 |
| Jumla ya bidhaa zote | 000 Dwt | 14,601 | 13,580 | 13,761 | 14,401 | 16,405 | 15,365 |
| **Bidhaa zilizopakuliwa** | **000 Dwt** | **11,901** | **11,260** | **11,460** | **11,682** | **13,836** | **12,473** |
| Za kawaida | 000 Dwt | 6,657 | 6,087 | 6,376 | 6,199 | 7,876 | 7,113 |
| Saruji | 000 Dwt | - | - | - | - | - | - |
| Mafuta (*Petroleum)* | 000 Dwt | 4,882 | 4,772 | 4,740 | 5,483 | 5,959 | 5,360 |
| Mengineyo[1] | 000 Dwt | 362 | 401 | 344 | - | - | |
| **Bidhaa zilizopakiwa** | **000 Dwt** | **2,700** | **2,320** | **2,301** | **2,719** | **2,550** | **2,807** |
| Za kawaida | 000 Dwt | 2,137 | 1,915 | 1,986 | 2,353 | 2,422 | 2,680 |
| Mafuta (*Petroleum)* | 000 Dwt | 362 | 116 | 59 | 99 | 82 | 127 |
| Mengineyo[1] | 000 Dwt | - | - | - | - | - | - |
| Mabadilishano (*Transhipment*) | 000 Dwt | 201 | 289 | 256 | 267 | 46 | - |

**Chanzo**: Mamlaka ya Bandari

1 Kama vile mbolea, mollasses, tallow fats n.k

\- Takwimu hazikupatikana

Jedwali Na. 56 (linaendelea) **USAFIRISHAJI KWA MELI: TANGA**

| **Maelezo** | **Kipimo** | **2015** | **2016** | **2017** | **2018** | **2019** | **2020** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Jumla ya meli | Namba | 63 | 87 | 72 | 144 | 120 | 108 |
| Uwezo wa kubeba mizigo | 000 Tani | 1,018 | 1,258 | 1,041 | 780 | 568 | 633 |
| Jumla ya abiria | 000 Namba | - | - | - | 45,820 | 68 | 49 |
| Jumla ya bidhaa zote | 000Dwt | 645 | 677 | 486 | 647 | 619 | 633 |
| **Bidhaa zilizopakuliwa** | **000Dwt** | **561** | **614** | **436** | **502** | **511** | **519** |
| Za kawaida | 000Dwt | 483 | 398 | 141 | 183 | 181 | 285 |
| Mafuta (*Petroleum)* | 000Dwt | 78 | 216 | 295 | 319 | 331 | 234 |
| **Bidhaa zilizopakiwa** | **000Dwt** | **83** | **63** | **50** | **144** | **108** | **102** |
| Za kawaida | 000Dwt | 83 | 63 | 50 | 144 | 108 | 102 |
| Mafuta (*Petroleum)* | 000Dwt | - | - | - | | - | - |
| Mabadilishano (*Transhipment*) | 000Dwt | - | - | - | | - | - |

**Chanzo**: Mamlaka ya Bandari Tanzania
- Takwimu hazikupatikana

Jedwali Na. 56 (linaendelea) **USAFIRISHAJI KWA MELI: MTWARA**

| Maelezo | Kipimo | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Jumla ya meli | Namba | 46 | 113 | 105 | 69 | 132 | 72 |
| Uwezo wa kubeba mizigo | 000 | 593 | 460 | 457 | 589 | 598 | 304 |
| Jumla ya abiria | 000 Namba | - | - | - | - | - | - |
| Jumla ya bidhaa zote | 000 DWt | 248 | 375 | 378 | 363 | 270 | 159 |
| **Bidhaa zilizopakuliwa** | **000 DWt** | **109** | **158** | **91** | **69** | **40** | **289** |
| Za kawaida | 000 DWt | 108 | 147 | 91 | 69 | 2 | 10 |
| Mafuta (*Petroleum)* | 000 DWt | 1 | 10 | - | - | 37 | 11 |
| **Bidhaa zilizopakiwa** | **000 DWt** | **139** | **218** | **286** | **294** | **230** | **134** |
| Za kawaida | 000 DWt | 139 | 218 | 286 | 294 | 230 | 134 |
| Mafuta (*Petroleum)* | 000 DWt | - | - | - | - | - | - |
| Mabadilishano (*Transhipment*) | 000 DWt | - | - | - | - | - | - |

**Chanzo**: Mamlaka ya Bandari Tanzania

- Takwimu hazikupatikana

## HUDUMA ZA POSTA

Jedwali Na. 57

| Maelezo | Kipimo | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Ofisi Ndogo Posta | Namba | 74 | 74 | 65 | 65 | 66 | 57 | 46 | 36 |
| Franchised Post Offices | Namba | 89 | 89 | 90 | 90 | 87 | 87 | 79 | 75 |
| Ofisi Kubwa | Namba | 160 | 160 | 158 | 158 | 154 | 157 | 139 | 139 |
| **Jumla** | Namba | 323 | 323 | 313 | 313 | 307 | 301 | 264 | 250 |
| Masanduku Binafsi | 000 | 173 | 142 | 160 | 160 | 161 | 161 | 145 | 140 |
| Masanduku Yaliokodishwa | 000 | 148 | 128 | 138 | 138 | 143 | 157 | 126 | 125 |
| Maombi Yasiotimizwa | 000 | 25 | 18 | 4 | 1 | 1 | 3 | 1 | 154 |
| Mifuko Pekee Iliyokodishwa | Namba | 212 | 260 | 180 | 180 | 342 | 675 | 442 | 60 |
| Barua Zilizotumwa bila Vifurushi | Mill. | 26 | 15 | 10 | 4 | 5 | 9 | 11 | 5 |
| Regista na Barua za Amana | 000 | 568 | 455 | 402 | 297 | 269 | 280 | 186 | 80 |
| Vifurushi Nchini | 000 | 29 | 12 | 17 | 36 | 51 | 63 | 32 | 3 |
| Vifurushi Nje | 000 | 9 | 5 | 9 | 2 | 3 | 4 | 3 | 1 |
| Leseni za kuuza stamp | Namba | 2,637 | 3,715 | - | - | 4,635 | 6,027 | 5,570 | 670 |
| **Huduma za Haraka, barua na vifurushi** | " | | | | | | | | |
| Ndani ya Nchi | " | 620,478 | 406,732 | 416,007 | 452,827 | 560,710 | 655,927 | 511,274 | 520,217 |
| Nje ya Nchi | " | 17,130 | 20,564 | 308,288 | 6,364 | 9,534 | 14,346 | 13,742 | 6,774 |
| EMS Money Fax | " | 550 | 745 | 748 | 272 | 18 | - | - | - |
| EMS Fax (Fax message received) | " | 544 | 1,194 | 3,844 | 2,518 | 129 | - | - | - |
| **Overnight Mail Services** | " | 115,126 | - | - | - | - | - | - | - |
| Mifuko ya Barua Iliyosafirishwa | " | 87,051 | 46,652 | 53,639 | 57,605 | 24,966 | 14,553 | 19,598 | 39,066 |
| Vifurushi vya magazeti vilivyosafirishwa | " | 18,784 | 8,700 | 9,130 | 113,448 | 2,120 | 5,346 | 7,800 | - |
| **Huduma za gari ndogo** | | | | | | | | | |
| Idadi ya Mifuko ya Barua Iliyosafirishwa | " | 849 | 714 | 9,576 | - | - | 2,919 | 2,518 | 5,320 |
| Amna za Haraka Zilizotolewa | " | 2,034 | 845 | 58,423 | 272 | 127 | 104 | 109 | 168 |
| Amana za Haraka Zilizolipwa | | 555 | - | - | - | - | | - | 107 |
| **Amana za Haraka za Nje ya Nchi** | | | | | | | | | |
| Zilizotumwa | " | 478 | 325 | 221 | 220 | 8 | 11 | 26 | 3 |
| Zilizopokelewa | " | 83 | 227 | 283 | 116 | 43 | 37 | - | - |
| Amana za Posta zilizouzwa | " | 684 | 261 | 251 | 107 | 45 | 2 | - | - |
| Amana za Posta Zilizolipwa | " | 166 | 67 | 25 | 18 | 8 | - | - | 0 |
| **Benki ya Akiba (Transaction)** | | | | | | | | | |
| Uwekaji Amana (Deposit) | " | 21,491 | 12,732 | 21,541 | 261,423 | 59,249 | 108,972 | 91,567 | - |
| Uchukuaji Amana (Withdrawal) | " | 37,556 | 12,807 | 18,098 | 45,449 | 76,926 | 133,531 | 103,958 | - |

**Chanzo**: Shirika la Posta - Takwimu hazikupatikani

Jedwali Na. 58

## IDADI YA WANAOTUMIA SIMU ZA MEZANI NA VIGANJANI

| Kampuni | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | Badiliko (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **A. Simu za Kiganjani** | | | | | | | | |
| Mobitel/Tigo | 8,624,638 | 10,639,610 | 11,677,344 | 11,044,520 | 12,583,640 | 12,572,826 | 13,032,073 | 3.7 |
| Vodacom | 11,810,064 | 12,520,645 | 12,419,425 | 12,714,297 | 14,143,657 | 15,672,390 | 15,621,457 | -0.3 |
| Airtel | 9,551,977 | 10,887,742 | 10,456,117 | 10,571,110 | 10,954,621 | 12,722,224 | 13,823,756 | 8.7 |
| Zantel | 1,730,105 | 1,563,503 | 1,083,157 | 934,991 | 1,153,623 | 1,170,085 | 1,021,409 | -12.7 |
| Benson/Smart | 528 | 528 | 803,251 | 131,501 | 132,292 | - | - | |
| TTCL Mobile | 296,618 | 165,460 | 166,383 | 175,717 | 587,191 | 981,072 | 963,384 | -1.8 |
| Sasatel | | | | | | | - | |
| Smile | | | | | | 1,222 | 12,395 | 914.3 |
| Hallotel | | | 3,438,509 | 3,799,691 | 3,942,237 | 4,641,701 | 6,818,228 | 46.9 |
| **Jumla Ndogo** | **32,013,930** | **35,777,488** | **40,044,186** | **39,371,827** | **43,497,261** | **47,761,520** | **51,292,702** | **7.4** |
| **B. Simu za Mezani** | | | | | | | | |
| TTCL | 140,391 | 140,391 | 127,112 | 127,009 | 124,220 | 76,288 | 72,469 | -5.0 |
| Zantel | 10,833 | 10,833 | 24,585 | 85 | 18 | - | - | |
| **Jumla Ndogo** | **151,224** | **151,224** | **151,697** | **127,094** | **124,238** | **76,288** | **72,469** | **-5.0** |
| **Jumla Kuu** | **32,165,154** | **35,928,712** | **40,195,883** | **39,498,921** | **43,621,499** | **47,837,808** | **51,365,171** | **7.4** |

**Chanzo**: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)

-Takwimu hazikupatikana

Jedwali Na. 59

**SHIRIKA LA NDEGE TANZANIA (ATCL)**[+]

| Maelezo | Kipimo | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Tani-Kilometa: | | | | | | | | | | |
| Zilizokuwepo | 000 | 1,932 | 6,154 | 3,052 | 60,042 | 3,937 | 863,107 | 32,095 | 32,927 | 65,968 |
| Zilizotumika | 000 | 815 | 2,503 | 117 | 30,889 | 1,756 | 89,092 | 17,526 | 18,944 | 33,655 |
| Matumizi | % | 42 | 41 | 4 | 54 | 47 | 10 | 55 | 58 | 51 |
| Viti-kilometa: | | | | | | | | | | |
| Vilivyokuwepo | 000 | 15,131 | 54,665 | 3,680 | 21,693 | 37,877 | 225,259 | 231,943 | 321,771 | 557,216 |
| Vilivyotumika | 000 | 10,209 | 27,279 | 946 | 11,472 | 20,692 | 122,532 | 158,203 | 220,433 | 347,101 |
| Matumizi | % | 67 | 50 | 26 | 53 | 56 | 54 | 68 | 69 | 62 |
| Abiria [++] | 000 | 11 | 35 | 56 | 31 | 28 | 129 | 279 | 627 | 434 |
| Mizigo ya ziada | Tani | 0 | 45 | - | 53 | 1 | 41 | 55 | 96 | 86 |
| Mizigo mingine | Tani | 5 | 35 | 45 | 42 | 7 | 50 | 220 | 696 | 438 |
| Shehena za Posta | Tani | - | 25 | 405 | 4 | - | 32 | 119 | 295 | 61 |

**Chanzo:** Shirika la Ndege Tanzania

+ Zinahusu "scheduled traffic" tu

++ Abiria waliolipa nauli kamili

\- Takwimu hazikupatikana

## SURA YA 17

## NISHATI


**Ufuaji wa Umeme**

422. Mwaka 2020, uwezo wa uzalishaji wa umeme ulifikia MW 1605.8 ikilinganishwa na MW 1,602.3 mwaka 2019. Katika kipindi hicho, umeme uliozalishwa kutoka vyanzo mbalimbali ulifikia saa za gigawati 7,862.9 ikilinganishwa na saa gigawati 7,806.4 mwaka 2019. Kati ya umeme uliozalishwa, saa za gigawati 7,677.3 zilizalishwa kwenye gridi ya Taifa na saa za gigawati 185.6 zilizalishwa kwenye vituo nje ya gridi ya Taifa ikilinganishwa na 7,617.9 na 188.5 mtawalia. Kwa upande wa umeme uliozalishwa katika gridi ya Taifa, umeme wa mitambo ya nguvu za maji ulikuwa saa za gigawati 3,139.2; gesi saa za gigawati 4,509.1; mafuta mazito na dizeli saa za gigawati 10.2; na tungamotaka saa za gigawati 18.8 ikilinganishwa umeme wa mitambo ya nguvu za maji saa za gigawati 2,481.5; gesi saa za gigawati 5,114.2; mafuta mazito na dizeli saa za gigawati 7.8 na tungamotaka saa za gigawati 14.4 mwaka 2019. Hii inatokana na Serikali kuendelea kutoa kipaumbele kwa miradi ya umeme utokanao na vyanzo vya gharama nafuu vya gesi na maji badala ya vyanzo vya mafuta ambavyo gharama zake za uzalishaji ni kubwa.

423. Mwaka 2020, umeme uliozalishwa na mitambo inayomilikiwa na TANESCO ulikuwa saa za gigawati 6,387.1 ikilinganishwa na saa za gigawati 6,039.9 zilizozalishwa mwaka 2019 sawa na ongezeko la asilimia 5.7. Vile vile, uzalishaji wa umeme kwa kampuni binafsi ulifikia saa za gigawati 1,290.2 mwaka 2020 ikilinganishwa na saa za gigawati 1,578.0 mwaka 2019, sawa na pungufu ya asilimia 18.2. Umeme ulionunuliwa kutoka nchi jirani ulikuwa saa za gigawati 114.3 mwaka 2020 ikilinganishwa na saa za gigawati 113.2 mwaka 2019, sawa na asilimia 1.5 ya umeme wote uliozalishwa mwaka 2020. Hii inatokana na kuimarika kwa uzalishaji wa umeme kupitia mitambo inayomilikiwa na TANESCO. Kwa ujumla asilimia 78.4 ya wananchi wamefikiwa na huduma ya umeme *(accessibility)* na asilimia 42 ya wananchi wameunganishiwa umeme *(connectivity)*.

424. Mwaka 2020, umeme uliouzwa kwa watumiaji mbalimbali ulikuwa saa za gigawati 6,674.3 ikilinganishwa na saa za gigawati 6,642.5 mwaka 2019 sawa na ongezeko la asilimia 0.5. Aidha, umeme uliopotea kutokana na uchakavu wa miundombinu ya kusafirishia na kusambaza umeme ulikuwa saa za gigawati 1,110.0 (sawa na asilimia 14.1 ya umeme uliozalishwa mwaka 2020) ikilinganishwa na saa za gigawati 1,085.9 kwa mwaka 2019 (sawa na asilimia 13.9 ya umeme uliozalishwa mwaka 2019.

**Kielelezo Na.17.1. Umeme Uliozalishwa kutoka vyanzo mbalimbali kwa mwaka 2020 (Saa za gigawati)**



**Jedwali Na. 60: Uwezo wa Mitambo ya Umeme na Kiasi cha Umeme Uliozalishwa kwa Vituo Mwaka 2020**

| Kituo | 2,020 | |
|---|---|---|
| | Uwezo (MW) | Umeme Uliozalishwa (GWh) |
| **Umeme kutokana na Maji** | | |
| Kidatu | 204 | 1,168.60 |
| Kihansi | 180 | 830.5 |
| Mtera | 80 | 563 |
| Hale | 21 | 31.8 |
| Nyumba ya Mungu | 8 | 67.8 |
| New Pangani Falls | 68 | 423.4 |
| Uwemba | 0.8 | 1.9 |
| Mwenga | 4 | 10.2 |
| Yovi | 1 | 2.4 |
| Tulila | 5 | 32.8 |
| Andoya | 1 | 4.3 |
| Darakuta | 0.3 | 2.1 |
| Matembwe (Ikondo) | 0.6 | 0.4 |
| **Jumla Ndogo - Maji** | **573.7** | **3,139.20** |
| **Umeme kutokana na Gesi Asilia** | | |
| Ubungo Gas PP- I | 102 | 429.6 |
| Tegeta Gas PP | 45 | 159.5 |
| Ubungo Gas PP - II | 129 | 948.7 |
| Kinyerezi I | 150 | 371.7 |
| Kinyerezi II | 248.2 | 1,290.4 |
| Songas | 189 | 1,219.2 |
| Somanga | 7.5 | 4.9 |
| Mtwara | 30.6 | 85.1 |
| **Jumla Ndogo -Gesi** | **901.3** | **4,509.1** |
| **Umeme kutokana na Mafuta** | | |
| Zuzu | 7.4 | 0.4 |
| Biharamulo | 4.1 | 4.5 |
| Ngara | 2.5 | 4.9 |
| Nyakato | 63 | 0.3 |
| Ludewa | 1.3 | 0 |
| Tunduru | 1.7 | 0.1 |
| Songea | 5.8 | - |
| Namtumbo | - | - |
| Mbinga | 1 | - |
| Madaba | 0.5 | - |
| Liwale | 0.9 | - |
| **Jumla Ndogo - Mafuta** | **88.1** | **10.2** |
| **Umeme kutokana na Tungamotaka (Biomass)** | | |
| TPC | 9 | 16.3 |
| TANWAT | 1.5 | 2.5 |
| **Jumla Ndogo - Tungamotaka** | **10.5** | **18.8** |
| **Jumla - Gridi ya Taifa** | **99** | **7,677.30** |
| **Umeme nje ya Mfumo wa Gridi ya Taifa *(Off-Grid)*** | | |
| Bukoba | 2.6 | 0.1 |
| Inyonga | 0.8 | 1.6 |
| Kasulu | 3.4 | 10.1 |
| Kibondo | 2.5 | 5.8 |
| Kigoma | 6.3 | 29.8 |
| Loliondo | 3.5 | 1.7 |
| Mafia | 3.2 | 6.4 |
| Mpanda | 5 | 15.2 |
| Sumbawanga | 5 | 0.6 |
| Umeme kutoka Nchi Jirani | | 114.3 |
| **Jumla Nje ya Gridi ya Taifa** | **32.2** | **185.6** |
| **Jumla Kuu** | **1,605.8** | **7,862.9** |

**Chanzo:** Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania

Jedwali Na.61 **Mauzo ya Umeme (Saa za Gigawati)**

| Mwaka | Tanzania Bara | | | Wateja Zanizibar | Jumla | Umeme Uliopotea | Umeme Uliozalishwa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wateja Wadogo | Wateja wa Kati | Wateja Wakubwa | | | | |
| 2013 | 280.6 | 1,747.0 | 2,560.4 | 218.7 | 4,806.7 | 1,139.6 | 5,946.3 |
| 2014 | 217.0 | 1,891.0 | 2,595.0 | 348.5 | 5,051.5 | 1,135.3 | 6,186.8 |
| 2015 | 148.8 | 2,082.7 | 2,721.1 | 344.6 | 5,297.2 | 1,119.8 | 6,417.0 |
| 2016 | 345.3 | 2,263.4 | 2,887.2 | 375.6 | 5,871.5 | 1,220.7 | 7,092.2 |
| 2017 | 301.5 | 2,371.0 | 2,893.3 | 390.4 | 5,956.2 | 1,159.1 | 7,115.3 |
| 2018 | 319.8 | 2,481.9 | 3,075.0 | 414.0 | 6,290.7 | 1,064.1 | 7,354.8 |
| 2019 | 307.2 | 2,655.7 | 3,198.0 | 481.5 | 6,642.5 | 1,064.1 | 7,806.4 |
| 2020 | 325.8 | 2,668.6 | 3,205.1 | 474.9 | 6,674.3 | 1,110.0 | 7,862.9 |

**Chanzo:** Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania

## Mauzo ya Umeme kwa Mikoa

Jedwali Na.62

| Mikoa | Umeme Uliouzwa (GWh) | Umeme Uliouzwa (GWh) | Umeme Uliouzwa (GWh) | Umeme Uliouzwa (GWh) | Umeme Uliouzwa (GWh) | Umeme Uliouzwa (GWh) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | **2015** | **2016** | **2017** | **2018** | **2019** | **2020** |
| Dar es salaam | 2,229.4 | 2,397.9 | 2,412.5 | 2,481.6 | 2,596.5 | 2,534.0 |
| Pwani | 220.1 | 260.1 | 302.1 | 393.1 | 450.7 | 517.9 |
| Dodoma | 115.9 | 136.7 | 150.4 | 161.0 | 179.7 | 177.7 |
| Morogoro | 212.2 | 239.8 | 242.8 | 274.9 | 268.0 | 266.8 |
| Singida | 47.3 | 42.6 | 43.8 | 45.7 | 49.5 | 53.1 |
| Tanga | 299.9 | 321.7 | 330.4 | 353.9 | 351.3 | 342.2 |
| Kilimanjaro | 150.9 | 181.8 | 179.4 | 181.7 | 185.2 | 183.9 |
| Arusha | 311.2 | 356.9 | 365.9 | 383.3 | 406.3 | 385.6 |
| Manyara | 25.8 | 29.5 | 31.9 | 32.4 | 34.8 | 35.2 |
| Mtwara | 50.7 | 49.4 | 48.3 | 52.8 | 55.9 | 55.9 |
| Lindi | 21.5 | 24.0 | 22.9 | 25.8 | 29.7 | 30.5 |
| Ruvuma | 30.6 | 33.7 | 35.4 | 41.9 | 50.3 | 53.7 |
| Mbeya | 163.8 | 177.4 | 177.6 | 186.9 | 201.6 | 209.9 |
| Iringa | 111.5 | 106.9 | 98.4 | 103.7 | 108.9 | 109.1 |
| Rukwa | 23.3 | 28.4 | 27.0 | 25.9 | 27.3 | 28.6 |
| Katavi | | 3.8 | 10.8 | 11.2 | 13.6 | 16.3 |
| Njombe | | 69.1 | 35.6 | 35.4 | 39.1 | 42.0 |
| Songwe | 11.4 | 4.9 | 10.1 | 29.3 | 33.2 | 40.4 |
| Mwanza | 235.9 | 262.1 | 283.2 | 287.7 | 295.2 | 300.9 |
| Kagera | 60.5 | 72.3 | 76.9 | 90.6 | 80.3 | 79.2 |
| Mara | 134.6 | 141.7 | 156.9 | 165.8 | 163.9 | 188.1 |
| Geita | | 33.5 | 42.7 | 49.2 | 53.0 | 60.8 |
| Tabora | 51.5 | 56.9 | 55.9 | 60.7 | 68.4 | 69.7 |
| Shinyanga | 416.9 | 428.2 | 371.9 | 339.5 | 354.0 | 352.2 |
| Kigoma | 27.6 | 28.5 | 34.8 | 40.2 | 40.3 | 41.0 |
| Simiyu | | 8.3 | 18.2 | 22.4 | 24.2 | 24.8 |
| **Jumla Tanzania Bara** | **4,952.5** | **5,496.1** | **5,565.8** | **5,876.6** | **6,161.0** | **6,199.4** |
| Zanzibar | 344.6 | 375.6 | 390.4 | 414.0 | 481.5 | 474.9 |
| **JUMLA** | **5,297.1** | **5,871.7** | **5,956.2** | **6,290.6** | **6,642.5** | **6,674.3** |

**Chanzo:** Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania

**Utafutaji wa Mafuta na Gesi**

**Gesi Asilia**

425. Hadi Desemba 2020, kiasi cha gesi asilia kilichogundulika kilifikia futi za ujazo trilioni 57.54. Kati ya hizo, futi za ujazo trilioni 10.41 zipo nchi kavu na futi za ujazo trilioni 47.13 ziligunduliwa katika kina kirefu cha maji baharini. Aidha, gesi iliyozalishwa ilikuwa futi za ujazo milioni 57,084.2 mwaka 2020, ikilinganishwa na futi za ujazo milioni 63,821.3 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 10.6. Upungufu huo ulichangiwa na uwepo wa mvua nyingi uliowezesha Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania kutumia zaidi maji ambayo ni gharama nafuu katika kuzalisha umeme ikilinganishwa na gesi. Vile vile, Shirika lilipunguza mahitaji ya gesi kutokana na kupungua kwa mahitaji ya umeme kutokana na athari za mlipuko wa UVIKO -19.

426. Mwaka 2020, mapato yaliyotokana na mauzo ya gesi asilia kutoka vitalu vya Songo Songo na Mnazi Bay yalikuwa dola za Marekani milioni 55.12 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 64.05 mwaka 2019 sawa na upungufu wa asilimia 13.9. Upungufu huo ulichangiwa na kupungua kwa kiwango cha gesi iliyouzwa kwa Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania.

**Jedwali Na. 17.1: Uzalishaji wa Gesi Asilia Songo Songo na Mnazi Bay**

| Mwaka | Futi za Ujazo (SCF) | | | Jumla | Badiliko |
|---|---|---|---|---|---|
| | Songo Songo | Mnazi Bay | Kiliwani North | | |
| 2020 | 33,149,940,000 | 23,934,210,000 | - | 57,084,150,000 | -10.6% |
| 2019 | 37,619,760,000 | 26,201,516,247 | - | 63,821,276,247 | 8.3% |
| 2018 | 28,510,280,000 | 30,412,535,066 | 27,784, 935 | 58,950,600,001 | 15.5% |
| 2017 | 29,496,560,000 | 17,960,300,000 | 3,597,578,168 | 51,054,438,168 | 5.7% |
| 2016 | 29,747,400,000 | 15,792,127,458 | 2,783,497,464 | 48,323,024,922 | 30.0% |
| 2015 | 31,384,100,000 | 5,792,141,976 | - | 37,176,241,976 | |

**Chanzo:** Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania

**Jedwali Na 17.2: Mapato Yaliyotokana na Mauzo ya Gesi Asilia katika Visima vya SongoSongo na Mnazi Bay (Dola za Marekani)**

| Mwaka | Songo Songo | Mnazi Bay | Kiliwani North | Jumla | Badiliko |
|---|---|---|---|---|---|
| 2020 | 20,995,963 | 34,122,450 | - | 55,118,413 | -13.9% |
| 2019 | 28,097,086 | 35,952,953 | - | 64,050,039 | 1.5% |
| 2018 | 22,406,171 | 40,671,729 | 11,359 | 63,089,259 | 49.3% |
| 2017 | 22,795,142 | 13,763,426 | 5,702,695 | 42,261,263 | -18.7% |
| 2016 | 38,172,718 | 12,216,279 | 1,602,436 | 51,991,433 | 13.6% |
| 2015 | 43,854,236 | 1,921,965 | - | 45,776,201 | |

**Chanzo:** Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania

## Uagizaji Mafuta

427. Mwaka 2020, mafuta yenye jumla ya lita za ujazo milioni 3,572.0 yaliingizwa nchini kwa matumizi ya ndani ikilinganishwa na lita za ujazo milioni 3,537.9 mwaka 2019. Kati ya hizo, mafuta ya dizeli yalikuwa lita za ujazo milioni 1,924.9, sawa na ongezeko la asilimia 1.0. petroli lita za ujazo milioni 1,467.2, mafuta ya taa lita za ujazo milioni 34.9, mafuta ya ndege lita za ujazo milioni 118.3 na mafuta mazito lita za ujazo milioni 26.8. Aidha, mafuta ya dizeli yaliyoingizwa nchini yalipungua kwa asilimia 4.8, mafuta ya taa yalipungua kwa asilimia 2.0, na mafuta ya ndege nayo yalipungua kwa asilimia 35.1. Kupungua kwa uagizaji wa mafuta ya taa kulitokana na hatua zilizochukuliwa na Serikali kudhibiti uchakachuaji wa petroli na dizeli pamoja na ongezeko la matumizi ya nishati mbadala maeneo ya vijijini ikiwemo umeme wa jua. Uagizaji wa mafuta ya ndege na dizeli ulipungua kutokana na kusitishwa kwa safari za ndege za mashirika ya kimataifa na kupungua kwa shughuli za usafirishaji kwenda nchi jirani katika jitihada za kukabiliana na athari za UVIKO - 19. Kwa upande mwingine mafuta ya petroli yaliyoingizwa yaliongezeka kwa asilimia 14.7 na mafuta mazito asilimia 35.1 ikilinganishwa na mwaka 2019 na sehemu kubwa yalitumika katika utekelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo.

**Jedwali Na 17.3 Mafuta yaliyoingizwa Nchini kwa matumizi ya Ndani Mwaka 2020 (Lita za ujazo)**

| | Dizeli | Petroli | Mafuta ya Taa | Mafuta ya Ndege | Mafuta Mazito | **Jumla** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Januari | 187,029,091 | 150,119,727 | 3,578,317 | 29,300,084 | | 370,027,219 |
| Februari | 144,502,056 | 84,954,954 | 2,580,658 | 16,263,788 | 4,527,903 | 252,829,359 |
| Machi | 71,104,865 | 96,293,221 | 7,295,989 | 15,772,347 | | 190,466,422 |
| Aprili | 136,529,687 | 123,034,254 | 3,622,106 | 16,068,957 | 4,001,259 | 283,256,263 |
| May | 149,426,486 | 82,451,690 | | | 3,861,501 | 235,739,677 |
| Juni | 76,228,966 | 50,594,426 | | | | 126,823,392 |
| Julai | 100,626,451 | 92,660,911 | | | | 193,287,362 |
| Agosti | 209,275,758 | 142,307,023 | | | 4,496,215 | 356,078,996 |
| Septemba | 208,036,580 | 115,918,591 | 1,599,310 | 8,569,392 | 4,738,255 | 338,862,128 |
| Octoba | 131,361,563 | 160,897,766 | | | | 292,259,329 |
| Novemba | 187,285,677 | 117,841,106 | 1,593,696 | 9,961,772 | | 316,682,251 |
| Decemba | 179,236,527 | 85,052,268 | 6,210,553 | 20,905,058 | 5,157,978 | 296,562,384 |
| Mafuta ya nje yaliyouzwa ndani ya nchi (Localized Transit) 2020 | 144,228,780 | 165,116,474 | 3,452,693 | 4,463,099 | 12,841 | 317,273,887 |
| Mafuta ya ndege yaliyobadilishwa matumizi kutumika kama Mafuta ya Taa (Local Downgraded IK) | | | 4,950,000 | - 3,050,000 | | 1,900,000 |
| **Jumla Kuu** | **1,924,872,487** | **1,467,242,411** | **34,883,322** | **118,254,497** | **26,795,952** | **3,572,048,669** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati

## Mafuta Yaliyoingizwa Nchini Kwenda Nchi Jirani

428. Mwaka 2020, mafuta yaliyoingizwa nchini kwenda nchi jirani yalikuwa lita za ujazo milioni 2,204.8 ikilinganishwa na lita za ujazo milioni 2,614.1 mwaka 2019 sawa na upungufu wa asilimia 15.7. Kati ya kiasi cha mafuta kilichoagizwa mwaka 2020, mafuta ya dizeli yalikuwa lita za ujazo milioni 1,392.1, petroli lita za ujazo milioni

702.5, mjumuisho wa mafuta ya ndege na mafuta ya taa lita za ujazo milioni 102.4 na mafuta mazito lita za ujazo milioni 7,844.6. Aidha, mafuta ya dizeli yamepungua kwa asilimia 12, petroli imepungua kwa asilimia 20 na mjumuisho wa mafuta ya ndege na mafuta ya taa yamepungua kwa asilimia 31ikilinganishwa na mafuta yaliyoingizwa nchini kwenda nchi jirani kwa mwaka 2019. Hii ilitokana na kupungua kwa shughuli za kiuchumi na kusitishwa kwa shughuli za kawaida katika nchi za jirani zinazoagiza mafuta kupitia bandari za hapa nchini.

**Jedwali Na 17.4: Mafuta yaliyoingizwa Nchini kwenda Nchi Jirani -2020 (Lita)**

| Mwezi | Dizeli-AGO | Petroli- PMS | Mafuta ya Taa na Ndege-JETA1/IK | Mafuta Mazito - HFO | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| Januari | 160,290,915 | 100,921,091 | 26,710,288 | | 287,922,294 |
| Februari | 108,371,069 | 71,359,796 | 14,354,233 | | 194,085,098 |
| Machi | 59,496,322 | 74,628,332 | 20,529,254 | | 154,653,908 |
| Aprili | 124,857,394 | 86,740,199 | 14,923,100 | | 226,520,693 |
| May | 102,194,099 | 51,209,478 | | 4,190,926 | 157,594,503 |
| Juni | 66,273,410 | 40,527,425 | | | 106,800,835 |
| Julai | 143,625,086 | 63,823,296 | | | 207,448,382 |
| Agosti | 110,304,665 | 73,464,172 | | | 183,768,837 |
| Septemba | 193,068,017 | 57,610,228 | 2,122,079 | 3,666,560 | 256,466,884 |
| Octoba | 86,831,700 | 91,082,313 | | | 177,914,013 |
| Novemba | 199,812,740 | 81,295,230 | 8,810,720 | | 289,918,690 |
| Decemba | 181,161,116 | 74,963,308 | 22,863,876 | | 278,988,300 |
| | 1,536,286,533 | 867,624,868 | 110,313,550 | 7,857,486 | |
| Toa-Localization(Ujanibishaji)-Jan-Dec 2020 | 144,228,780 | 165,116,474 | 7,915,792 | 12,841 | 317,273,887 |
| **Jumla Kuu** | **1,392,057,753** | **702,508,394** | **102,397,758** | **7,844,645** | **2,204,808,550** |

**Chanzo**: Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati

## Mwenendo wa Bei za Mafuta

429. Mwaka 2020, wastani wa bei ya mafuta kwa tani ulikuwa petroli dola za Marekani 426, dizeli dola za Marekani 403 na mafuta ya taa dola za Marekani 390 ikilinganishwa na petroli dola za Marekani 593, dizeli dola za Marekani 570 na mafuta ya taa dola za Marekani 589 mwaka 2019. Bei hizo zilipungua kwa asilimia 28.2 kwa mafuta ya petroli, asilimia 29.3 mafuta ya dizeli na asilimia 33.8 mafuta ya taa. Hii inatokana na kupungua kwa mahitaji kufuatia athari za UVIKO – 19 zilizosababisha kupungua au kusimamishwa kwa baadhi ya shughuli za kiuchumi duniani zikiwemo za usafirishaji na uzalishaji viwandani zinazotumia kiasi kikubwa cha mafuta.

**Jedwali Na 17.5: Bei za Mafuta katika soko la Dunia (dola za Marekani kwa tani za ujazo)**

| Aina ya Mafuta | Petroli | | | Dizeli | | | Mafuta ya Taa | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwezi/Mwaka** | **2018** | **2019** | **2020** | **2018** | **2019** | **2020** | **2018** | **2019** | **2020** |
| Januari | 574 | 635 | 592 | 530 | 606 | 552 | 570 | 644 | 574 |
| Februari | 600 | 520 | 580 | 549 | 501 | 571 | 587 | 542 | 585 |
| Machi | 599 | 496 | 578 | 581 | 516 | 551 | 587 | 543 | 572 |
| Aprili | 646 | 543 | 529 | 607 | 582 | 475 | 624 | 543 | 484 |
| Mei | 615 | 610 | 397 | 573 | 600 | 402 | 624 | 605 | 291 |
| Juni | 632 | 677 | 214 | 580 | 618 | 249 | 633 | 625 | 291 |
| Julai | 718 | 658 | 261 | 674 | 610 | 300 | 633 | 634 | 291 |
| Agosti | 710 | 597 | 389 | 655 | 546 | 367 | 691 | 570 | 291 |
| Septemba | 710 | 639 | 389 | 639 | 576 | 369 | 673 | 601 | 333 |
| Oktoba | 711 | 576 | 405 | 653 | 552 | 359 | 673 | 584 | 333 |
| Novemba | 712 | 596 | 394 | 699 | 572 | 320 | 693 | 602 | 333 |
| Desemba | 707 | 574 | 386 | 721 | 560 | 321 | 756 | 574 | 301 |
| **Wastani wa Bei** | **661** | **593** | **426** | **622** | **570** | **403** | **645** | **589** | **390** |
| **Badiliko (Asilimia)** | **22.4** | **-10.3** | **-28.2** | **28.5** | **-8.4** | **-29.3** | **28.2** | **-8.7** | **-33.8** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati

**Jedwali Na. 17.6: Mwenendo wa Bei za Mafuta katika Soko la Ndani, Mwaka 2020**

| Mwezi | Petroli (Shiling/Lita) | Dizeli (Shilingi/Lita) | Mafuta ya Taa (Shilingi/Lita) |
|---|---|---|---|
| Januari | 2,206 | 2,121 | 2,075 |
| Februari | 2,226 | 2,195 | 2,119 |
| Machi | 2,204 | 2,153 | 2,116 |
| Aprili | 2,087 | 1,989 | 1,923 |
| Mei | 1,868 | 1,846 | 1,568 |
| Juni | 1,520 | 1,546 | 1,568 |
| Julai | 1,693 | 1,716 | 1,568 |
| Agosti | 1,766 | 1,720 | 1,568 |
| Septemba | 1,852 | 1,793 | 1,692 |
| Oktoba | 1,877 | 1,778 | 1,695 |
| Novemba | 1,902 | 1,734 | 1,707 |
| Desemba | 1,865 | 1,687 | 1,621 |
| **Wastani kwa Mwaka 2020** | **1,928** | **1,862** | **1,768** |
| **Wastani kwa Mwaka 2019** | **2,200** | **2,159** | **2,114** |
| **Badiliko (Asilimia)** | **-12** | **-14** | **-16** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati

## Nishati Jadidifu

### Nishati mbadala ya Gesi inayotokana na Petroli

430. Mwaka 2020, gesi inayotokana na petroli (Liquefied Petroleum Gas - LPG) iliyoagizwa toka nje kwa matumizi mbalimbali ilikuwa tani za ujazo 194,597 ikilinganishwa na tani 166,436 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 16.9. Hii ilichangiwa na utoaji wa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kutumia gesi itokanayo na petroli katika utunzaji wa mazingira

**Nishati ya Mionzi ya Jua**

431. Uzalishaji wa umeme jua kwa mfumo wa gridi ndogo katika maeneo yaliyo nje ya mfumo wa gridi ya Taifa ulifikia megawati 9.0 mwaka 2020 ikilinganishwa na megawati 7.4 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 21. Ongezeko hilo lilitokana na kukamilika kwa miradi minne katika visiwa vya ziwa Victoria na mradi wa MW 5 wa Solawazi Nextgen Mkoani Kigoma. Aidha, matumizi ya nishati ya mionzi ya jua majumbani (Solar Home System) yaliongezeka kwa asilimia 7.6 na kufikia megawati 21 kutoka megawati 19.5 mwaka 2019. Katika kipindi hicho, umeme wa mionzi ya jua ulichangia katika maendeleo ya sekta ya kilimo ambapo kilowati 200 zilitumika katika shughuli za umwagiliaji wa mazao ya matunda na mbogamboga.

## SURA YA 18

## MAJI

**Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji**

432. Mwaka 2020, kiwango cha rasilimali za maji kilichopo na kinachofaa kwa matumizi ni wastani wa mita za ujazo bilioni 126 kwa mwaka kama kilivyokuwa mwaka 2019. Kati ya kiwango hicho, mita za ujazo bilioni 105 zilikadiriwa kuwa juu ya ardhi na mita za ujazo bilioni 21 chini ya ardhi. Aidha, wastani wa kiwango cha maji kilichopo kwa mtu kwa mwaka 2020 ulikuwa mita za ujazo 2,250 ikilinganishwa na mita za ujazo 2,300 mwaka 2019. Kiwango hicho ni juu ya wastani wa mita za ujazo 1,700 ambacho ni kiwango cha chini cha mahitaji ya maji kinachokubalika kimataifa kwa mtu kwa mwaka. Hadi Desemba 2020, mahitaji ya maji kwa matumizi mbalimbali nchini yalikadiriwa kuwa takribani mita za ujazo bilioni 60 kwa mwaka.

433. Mwaka 2020, Serikali iliendelea kutambua vyanzo vya maji vilivyo katika hatari ya kuharibiwa kutokana na shughuli za kibinadamu. Hadi Desemba 2020, vyanzo 1,213 vilitambuliwa ikilinganishwa na vyanzo 575 vilivyotambuliwa kipindi kama hicho mwaka 2019. Ongezeko la vyanzo vilivyotambuliwa lilichangiwa na zoezi maalum la utambuzi wa vyanzo vya maji lililofanywa na Bodi za Maji za Mabonde hususan katika Bonde la Rufiji, Pangani na Ziwa Rukwa. Kati ya vyanzo vilivyotambuliwa, vyanzo 133 viliwekewa mipaka kwa lengo la kuvihifadhi visiharibiwe kutokana na shughuli za kibinadamu ikilinganishwa na vyanzo 120 vilivyotambuliwa mwaka 2019.

434. Hadi Desemba 2020, vituo vya kufuatilia mwenendo wa maji juu na chini ya ardhi katika maeneo mbalimbali nchini vilikuwa 1,175 ikilinganishwa na vituo 996 katika kipindi kama hicho mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 18.0. Kati ya vituo hivyo: vituo 324 ni kwa ajili ya kupima mtiririko wa maji katika mito; vituo 28 ni vya kupima kina cha maji katika maziwa na mabwawa; vituo 189 ni vya kukusanya takwimu za mvua; vituo 152 ni vya hali ya hewa; vituo 95 ni vya kufuatilia mwenendo wa maji chini ya ardhi; vituo 33 ni vya kupima wingi wa tope katika maji; na vituo 354 ni vya kupima ubora wa maji.

435. Mwaka 2020, sampuli 6,855 za maji zilikusanywa na kuhakikiwa ubora katika vyanzo vya maji, mitandao ya usambazaji maji, taasisi mbalimbali, viwanda, vituo vya utafiti, shughuli za umwagiliaji na ujenzi ikilinganishwa na sampuli 5,252 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 30.5. Ongezeko hilo lilitokana na kuanza utekelezaji wa miongozo ya kupima ubora wa maji katika visima kwa ajili ya matumizi mbalimbali. Kati ya sampuli zilizokusanywa na kuhakikiwa, sampuli kutoka vyanzo vya maji, mitandao ya usambazaji maji na taasisi mbalimbali zilikuwa 5,830, viwandani sampuli

288, umwagiliaji sampuli 17, ujenzi sampuli 55, utafiti sampuli 98 na sampuli 567 kwa ajili ya kubaini mwenendo wa ubora wa maji katika vyanzo vya maji.

436. Matokeo ya uhakiki yalionesha kuwa sampuli 4,964 kwa ajili ya vyanzo vya maji, mitandao ya usambazaji maji na taasisi mbalimbali, sawa na asilimia 85.1 zilikidhi viwango vya ubora na usalama wa maji vinavyokubalika ikilinganishwa na asilimia 90.8 mwaka 2019. Aidha, sampuli zote za maji kwa ajili ya kubaini mwenendo wa ubora wa maji katika vyanzo vya maji, viwandani, ujenzi, umwagiliaji na utafiti zilizofanyiwa uchunguzi zilikidhi viwango vya ubora. Kwa upande mwingine, sampuli 866, sawa na asilimia 14.9 ya sampuli zilizohakikiwa kutoka katika vyanzo vya maji, mitandao ya usambazaji maji na taasisi mbalimbali hazikukidhi viwango vya ubora na usalama wa maji vinavyokubalika. Hii ilitokana na uwepo wa viwango vikubwa vya madini ya chumvi, *manganese* na chuma katika mikoa ya Lindi na Mtwara; *fluoride* katika mikoa ya Arusha, Manyara na Singida; na *nitrate* na chumvi katika mikoa ya Dodoma na Manyara (Kiteto).

437. Mwaka 2020, sampuli 328 za majitaka yanayorudishwa kwenye mazingira zilikusanywa na kuhakikiwa ikilinganishwa na sampuli 387 mwaka 2019. Kati ya sampuli hizo, sampuli 230, sawa na asilimia 70.1 zilikidhi viwango vya ubora.

**Huduma ya Maji Vijijini**

438. Mwaka 2020, Serikali iliendelea kuboresha miundombinu ya maji vijijini kwa kukarabati na kupanua miradi ya miundombinu iliyopo na kutekeleza miradi mipya. Katika kipindi hicho, miradi 695 yenye vituo vya kuchotea maji 11,841 yenye uwezo wa kuhudumia wananchi 2,960,250 ilikamilika. Hadi Desemba 2020, idadi ya vituo vinavyofanya kazi na kutoa huduma ya maji ilifikia vituo 114,354 ikilinganishwa na vituo 96,952 Desemba 2019. Kukamilika kwa miradi hiyo, kuliongeza kiwango cha upatikanaji wa huduma ya maji vijijini hadi asilimia 72.3 mwaka 2020 kutoka asilimia 70.1 mwaka 2019.

**Huduma ya Maji Mijini**

439. Mwaka 2020, wastani wa upatikanaji wa huduma ya majisafi katika miji mikuu ya mikoa ulikuwa asilimia 86 ikilinganishwa na asilimia 84 mwaka 2019. Ongezeko la kiwango cha upatikanaji wa maji lilichangiwa na kukamilika kwa baadhi ya miradi ya ukarabati wa miundombinu ya maji pamoja na kukamilika kwa miradi 67 katika miji mikuu ya mikoa, wilaya na utekelezaji wa miradi ya kitaifa. Aidha, wastani wa upatikanaji wa majisafi kwa jiji la Dar es Salaam ulikuwa asilimia 88 mwaka 2020 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 85 mwaka 2019. Vile vile, wastani wa upatikanaji wa huduma ya maji katika miji mikuu ya wilaya, miji midogo na maeneo yanayohudumiwa na miradi ya kitaifa uliongezeka na kufikia asilimia 70 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 64 mwaka 2019.

440. Hadi Desemba 2020, wastani wa wateja 1,060,700 waliunganishwa na huduma ya majisafi ikilinganishwa na wateja 943,074 Desemba 2019, sawa na ongezeko la asilimia 12.5. Aidha, mauzo ya majisafi na salama yalipungua kutoka shilingi milioni 306.6 mwaka 2019 hadi shilingi milioni 297.3 mwaka 2020. Upungufu huo ulichangiwa na kupungua kwa shughuli za kiuchumi zinazohusisha matumizi ya maji kwa wingi ikiwemo hoteli za kitalii na uzalishaji viwandani hususan katika majiji makubwa, ikiwemo Dar es salaam, Arusha, Mbeya na mkoa wa Iringa kulikochangiwa na athari za UVIKO 19.

**Uchimbaji wa Visima**

441. Mwaka 2020, jumla ya visima 853 vilichimbwa katika maeneo mbalimbali ikilinganishwa na visima 2,053 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 58.5. Upungufu huo ulisababishwa na baadhi ya kampuni za kigeni za uchimbaji wa visima kusitisha shughuli zao kutokana na janga la UVIKO-19. Kati ya visima hivyo, visima 695 vilichimbwa na kampuni binafsi na visima 158 vilichimbwa na Serikali katika mikoa ya Dodoma visima 39, Mara 19, Rukwa 15, Iringa 11, Simiyu tisa (9), Tabora tisa (9), Manyara nane (8), Songwe saba (7), Lindi saba (7), Pwani sita (6), Morogoro vitano (5), Mtwara vitano (5), Singida vitano (5), Dar es Salaam vitano (5), Mara vinne (4) na Tanga vinne (4).

**Uondoaji wa Majitaka**

442. Mwaka 2020, huduma ya usafi wa mazingira katika miji yenye mtandao wa majitaka ambayo ni Dar es Salaam, Arusha, Tanga, Dodoma, Moshi, Morogoro, Mwanza, Iringa, Songea, Mbeya na Tabora ilikuwa wastani wa asilimia 13.0 kama ilivyokuwa mwaka 2019. Hadi Desemba 2020, mtandao wa majitaka ulikuwa na urefu wa kilomita 898.6 ikilinganishwa na kilomita 892.4 katika kipindi kama hicho mwaka 2019. Aidha, idadi ya wateja waliounganishwa katika mtandao wa majitaka ilifikia wateja 51,183 kutoka wateja 51,032 mwaka 2019. Kwa upande wa miji isiyokuwa na mtandao wa majitaka, huduma ya usafi wa mazingira iliendelea kutolewa kwa njia ya magari maalum ya majitaka. Hadi Desemba 2020, Mamlaka za maji na usafi wa mazingira sita (6) za Sumbawanga, Bukoba, Musoma, Geita, Nansio na Sengerema zilianza kutumia mfumo usiounganishwa na mtandao katika uondoaji majitaka. Mfumo huo hutumia magari maalum ya ubebaji majitaka na kuyamwaga katika sehemu maalum zilizojengwa kwa ajili ya kuchakata majitaka.

## UZALISHAJI WA MAJI NA MAPATO YATOKANAYO NA MAJI MIJINI

Jedwali Na.63

| Mamlaka | 2019 | | 2020 | |
|---|---|---|---|---|
| | **Uzalishaji wa Maji (mita za ujazo)** | **Mapato (TShs)** | **Uzalishaji wa Maji (mita za ujazo)** | **Mapato (TShs)** |
| Arusha | 15,207,609 | 17,147,472,138 | 15,823,818 | 16,863,639,378 |
| Dar es Salaam | 183,960,000 | 140,781,910,096 | 2,033,740 | 2,673,483,543 |
| Babati | 2,196,128 | 2,504,075,166 | 2,748,120 | 2,284,101,436 |
| Bukoba | 2,288,913 | 2,674,430,314 | 15,493,870 | 18,093,093,316 |
| Dodoma | 15,993,293 | 18,793,945,336 | 146,437,533 | 135,380,043,912 |
| Iringa | 4,850,334 | 9,128,422,716 | 4,668,691 | 8,532,522,161 |
| Kigoma | 3,542,157 | 1,856,673,611 | 1,287,543 | 999,653,342 |
| Kahama | 4,283,787 | 9,086,230,528 | 944,570 | 609,492,500 |
| Lindi | 817,153 | 804,163,655 | 3,250,796 | 2,208,707,132 |
| Mbeya | 16,219,782 | 13,437,635,472 | 758,513 | 843,700,012 |
| Morogoro | 11,477,281 | 9,586,393,334 | 16,892,670 | 12,074,273,429 |
| Moshi | 12,288,705 | 9,850,398,091 | 12,347,306 | 10,563,745,566 |
| Mtwara | 3,569,872 | 3,722,963,282 | 11,681,145 | 10,360,287,936 |
| Musoma | 6,484,529 | 3,106,769,854 | 3,447,080 | 3,360,287,173 |
| Mwanza | 29,138,375 | 26,762,495,979 | 5,806,006 | 3,055,714,297 |
| Shinyanga | 4,339,482 | 6,697,549,150 | 28,882,933 | 25,631,493,019 |
| Singida | 2,618,508 | 3,176,653,742 | 1,748,297 | 1,842,082,283 |
| Songea | 2,862,762 | 3,212,818,561 | 272,262 | 179,187,841 |
| Sumbawanga | 2,873,643 | 1,511,067,307 | 4,216,608 | 6,545,726,499 |
| Tabora | 5,249,105 | 4,789,917,115 | 4,337,360 | 9,049,024,770 |
| Tanga | 10,732,719 | 14,451,964,945 | 2,705,150 | 3,148,496,303 |
| Mpanda | 1,013,665 | 593,542,631 | 2,910,973 | 3,041,166,043 |
| Bariadi | 214,128 | 182,050,541 | 2,448,249 | 1,520,152,181 |
| Njombe | 1,263,582 | 993,794,522 | 4,974,294 | 4,487,577,632 |
| Geita | 1,744,633 | 1,624,701,489 | 10,711,585 | 13,819,213,628 |
| Vwawa Mlowo | 677,435 | 87,585,517 | 868,142 | 86,448,413 |
| **Jumla** | **345,907,580** | **306,565,625,092** | **307,697,254** | **297,253,313,745** |

**Chanzo**: Wizara ya Maji

## MAHITAJI NA KIWANGO CHA UPATIKANAJI WA MAJI KATIKA MIJI

Jedwali Na. 64

| Mamlaka | Mahitaji ya Maji kwa Mwaka | Wastani wa upatikanaji wa huduma ya maji kwa mwaka 2020 (Asilimia) |
|---|---|---|
| Arusha | 38,984,008 | 80 |
| Babati | 3,102,500 | 88 |
| Bariadi | 2,984,605 | 59 |
| Bukoba | 4,479,300 | 85 |
| Dar es Salaam | 207,970,000 | 88 |
| Dodoma | 37,080,000 | 97 |
| Geita | 5,643,360 | 68 |
| Iringa | 5,840,000 | 98 |
| Kahama | 5,202,187 | 85 |
| Kigoma | 8,183,480 | 95 |
| Lindi | 1,728,000 | 84 |
| Mbeya | 22,995,000 | 92 |
| Morogoro | 21,570,640 | 70 |
| Moshi | 18,514,080 | 100 |
| Mpanda | 3,843,000 | 74 |
| Mtwara | 8,030,000 | 90 |
| Musoma | 8,760,000 | 95 |
| Mwanza | 44,950,115 | 95 |
| Njombe | 3,316,008 | 88 |
| Shinyanga | 7,655,760 | 90 |
| Singida | 4,680,000 | 90 |
| Songea | 5,320,440 | 96 |
| Sumbawanga | 5,920,000 | 83 |
| Tabora | 10,759,589 | 92 |
| Tanga | 10,925,816 | 97 |
| Vwawa- Mlowo | 3,593,425 | 49 |
| **Jumla** | 502,031,313 | 86 |

**Chanzo**: Wizara ya Maji

## SURA YA 19

## ELIMU MAFUNZO YA UFUNDI NA TEKNOLOJIA

### Elimu ya Awali

443. Mwaka 2020, wanafunzi 1,377,409 waliandikishwa katika elimu ya awali ikilinganishwa na wanafunzi 1,429,169 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 3.6. Kati ya hao, wasichana walikuwa 679,242 sawa na asilimia 49.3 na wavulana walikuwa 698,167. Upungufu huo ulichangiwa na kuendelea na utekelezaji wa sera ya elimumsingi bila ada ambapo wanafunzi wengi walijiunga na elimu ya awali tangu kuanza kwa utekelezaji wa Sera husika. Aidha, shule za Serikali zilikuwa na wanafunzi 1,278,886 mwaka 2020 ikilinganishwa na wanafunzi 1,334,992 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 4.2. Kati ya hao, wasichana walikuwa 631,277, sawa na asilimia 49.4 na wavulana walikuwa 647,609. Katika kipindi hicho, wanafunzi katika shule zisizo za Serikali waliongezeka kwa asilimia 4.6 na kufikia wanafunzi 98,523 ikilinganishwa na wanafunzi 94,177 mwaka 2019.

444. Mwaka 2020, idadi ya walimu wenye sifa stahiki katika shule za Serikali za elimu ya awali ilikuwa walimu 10,594 (wanaume 2,408 na wanawake 8,186) ikilinganishwa na walimu 9,592 (wanaume 2,089 na wanawake 7,503) mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 10.4. Aidha, Uwiano wa mwalimu mwenye sifa kwa wanafunzi ulikuwa 1:193 mwaka 2020 ikilinganishwa na 1:216 mwaka 2019. Uwiano huo umezidi uwiano wa 1:25 unaokubalika ambapo Serikali inaendelea kutoa mafunzo mbalimbali ya muda mrefu na mfupi kwa walimu waliopo kazini na walimu tarajari na kuajiri walimu wapya ili kupunguza tofauti iliyopo katika uwiano huo.

### Elimu ya Msingi

445. Mwaka 2020, shule za msingi zilikuwa 18,152 ikilinganishwa na shule 17,804 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 2.0. Kati ya hizo, shule za Serikali zilikuwa 16,406 mwaka 2020 ikilinganishwa na shule 16,223 mwaka 2019. Ongezeko la shule za msingi lilitokana na kuendelea kwa utekelezaji wa azma ya Serikali ya kuhakikisha uwepo wa shule ya msingi katika kila kata. Kwa upande mwingine, idadi ya shule zisizo za Serikali iliongezeka kwa asilimia 10.4 na kufikia 1,746 mwaka 2020 kutoka shule 1,581 mwaka 2019. Ongezeko hilo lilitokana na Serikali kuendelea kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji katika sekta ya elimu.

446. Mwaka 2020, kulikuwa na wanafunzi 10,925,896 katika shule za elimu ya msingi ikilinganishwa na wanafunzi 10,605,430 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 3.0. Kati ya hao, wasichana walikuwa 5,481,982 na wavulana walikuwa 5,443,914 ikilinganishwa na wasichana 5,304,648 na wavulana 5,300,782 mwaka 2019. Katika kipindi hicho, idadi ya wanafunzi katika shule za Serikali iliongezeka kwa

asilimia 2.8 kufikia wanafunzi 10,460,785 kutoka wanafunzi 10,174,237 mwaka 2019. Hii ilitokana na jitihada za Serikali za kuendelea kuimarisha mazingira ya kujifunzia na kufundishia ikiwemo ugharamiaji wa elimumsingi bila ada pamoja na ujenzi wa miundombinu.

447. Mwaka 2020, watahiniwa waliofanya mtihani wa kuhitimu darasa la saba waliongezeka kwa asilimia 9.7 na kufikia watahiniwa 1,023,950 ikilinganishwa na watahiniwa 933,369 mwaka 2019. Kati ya hao, watahiniwa 883,672 walifaulu mtihani sawa na kiwango cha ufaulu cha asilimia 86.3 ikilinganishwa na kiwango cha ufaulu cha asilimia 81.4 mwaka 2019.

448. Mwaka 2020, idadi ya walimu katika shule za msingi za Serikali za ilikuwa 170,569 (wanaume 84,673 na wanawake 85,896) ikilinganishwa na walimu 174,806 (Wanaume 86,280 na Wanawake 88,526) mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 2.4. Upungufu huo ulitokana na baadhi ya walimu kuvutiwa na taaluma nyingine, kustaafu, kuachishwa kazi na vifo. Aidha, uwiano wa mwalimu kwa wanafunzi katika shule za Serikali ulikuwa 1:61 mwaka 2020 zaidi ya uwiano unaokubalika kitaifa wa 1:45 ikilinganishwa na uwiano wa 1:58 mwaka 2019.

**Elimu ya Sekondari**

449. Mwaka 2020, idadi ya shule za sekondari iliongezeka kwa asilimia 2.8 na kufikia 5,143 kutoka shule 5,001 mwaka 2019. Kati ya hizo, shule za Serikali zilikuwa 3,863 na shule zisizo za Serikali 1,280 ikilinganishwa shule za Serikali 3, 742 na shule zisizo za Serikali 1,259 mwaka 2019. Ongezeko la shule za Serikali lilitokana na kuendelea na utekelezaji wa sera ya elimumsingi bila ada iliyosaidia kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wanaohitimu darasa la saba (7) na kujiunga na kidato cha kwanza. Aidha, Serikali imekuwa ikitenga kiasi cha shilingi bilioni 149.7 kila mwaka kwa ajili ya ugharamiaji wa sera ya elimumsingi bila ada.

450. Mwaka 2020, idadi ya wanafunzi katika kidato cha kwanza hadi cha sita ilikuwa 2,473,506 ikilinganishwa na wanafunzi 2,338,457 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 5.8. Kati ya hao wasichana walikuwa 1,284,096 na wavulana walikuwa 1,189,410, ikilinganishwa na wasichana 1,205,369 na wavulana 1,133,088 mwaka 2019. Idadi ya wanafunzi katika shule za Serikali iliongezeka kwa asilimia 4.7 na kufikia wanafunzi 2,172,257 mwaka 2020 kutoka wanafunzi 2,023,205 mwaka 2019. Ongezeko hilo lilitokana na jitihada za Serikali za kuendelea kuimarisha mazingira ya kujifunzia na kufundishia ikiwemo ugharamiaji wa elimumsingi bila ada pamoja na ujenzi wa miundombinu iliyowezesha wanafunzi wengi kujiunga na elimu ya sekondari. Katika kipindi hicho, wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi cha nne walikuwa 2,322,259 ikilinganishwa na wanafunzi 2,185,037 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 6.3. Kati ya hao, wanafunzi katika shule za Serikali walikuwa 2,062,717 ikilinganishwa na wanafunzi 1,914,735 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 7.7. Hii ilitokana na

kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wanaohitimu darasa la saba na kujiunga na kidato cha kwanza.

451. Mwaka 2020, watahiniwa 435,654 walifanya mtihani wa kuhitimu kidato cha nne (wasichana 226,686 na wavulana 208,968) ikilinganishwa na watahiniwa 473,755 mwaka 2019. Kati ya hao, watahiniwa 373,958 walifaulu (wasichana 193,672 na wavulana 180,286) sawa na kiwango cha ufaulu cha asilimia 85.8 ikilinganishwa na kiwango cha ufaulu cha asilimia 78.4 mwaka 2019. Aidha, mwaka 2020, watahiniwa 73,901 walifanya mtihani wa kidato cha sita (wasichana 32,357 na wavulana 41,544). Kati ya hao, watahiniwa 73,537 walifaulu sawa na kiwango cha ufaulu cha asilimia 99.5 ikilinganishwa na kiwango cha ufaulu cha asilimia 96.8 mwaka 2019.

**Elimu katika Vyuo vya Ualimu**

452. Mwaka 2019/2020, idadi ya wanafunzi katika vyuo vya ualimu ilipungua kwa asilimia 17.7, na kuwa wanafunzi 19,249 (wanawake 6,025 na wanaume 13,224) ikilinganishwa na wanafunzi 23,396 (wanawake 7,081 na wanaume 16,315) mwaka 2018/19. Kupungua kwa idadi ya wanafunzi katika vyuo vya ualimu kulitokana na wahitimu wengi kutoka ngazi za chini kujiunga na vyuo vya ufundi.

**Ukaguzi wa Shule na Vyuo vya Ualimu**

453. Mwaka 2019/20, Serikali ilikagua taasisi za elimu 5,166 ikilinganishwa na taasisi 8,966 mwaka 2018/19, sawa na upungufu wa asilimia 42.4. Hii ilichangiwa na upungufu wa rasilimali watu na vitendea kazi na kusababisha ukaguzi kufanyika katika taasisi zenye changamoto pamoja na mlipuko wa UVIKO - 19 uliosababisha shule kufungwa kwa muda.

**Jedwali Na. 19.1: Ukaguzi wa Taasisi za Elimu mwaka 2018/19 -2019/20**

| **Taasisi/Shule/ Vituo/Vyuo** | **Idadi iliyokaguliwa (2018/19)** | **Idadi iliyokaguliwa (2019/20)** | **Badiliko (Asilimia)** |
|---|---:|---:|---:|
| Shule za Awali na Msingi | 7,288 | 4,042 | (44.5) |
| Shule/Vituo vya Elimu Maalum | 197 | 0 | (100) |
| Shule za Sekondari | 1,436 | 1,098 | (23.5) |
| Vyuo vya Ualimu | 45 | 26 | (42.2) |
| **Jumla** | **8,966** | **5,166** | **(42.4)** |

**Chanzo**: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

**Elimu ya Ufundi na Mafunzo**

454. Mwaka 2019/20, idadi ya wanafunzi katika vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo iliongezeka kwa asilimia 33.5 na kuwa 151,379 ikilinganishwa na wanafunzi 113,427 mwaka 2018/19. Kati ya hao, wanawake walikuwa 75,045, sawa na asilimia 49.6 na wanaume walikuwa 76,334. Ongezeko hilo, lilitokana na usajili wa taasisi mpya

za ufundi, kuanzishwa na kuboreshwa kwa programu zinazoendana na soko la ajira na kukamilika kwa ukarabati na ujenzi wa miundombinu.

**Elimu ya Ufundi Stadi na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi**

455. Mwaka 2019/20, idadi ya wanafunzi katika vyuo vya ufundi stadi na vyuo vya maendeleo ya wananchi iliongezeka kwa asilimia 41.2 na kuwa wanafunzi 320,143 ikilinganishwa na wanafunzi 226,767 mwaka 2018/19. Kati ya hao, wanawake walikuwa 117,425 (asilimia 36.7) na wanaume walikuwa 202,718. Ongezeko hilo lilitokana na kuanzishwa na kuboreshwa kwa programu zinazoendana na soko la ajira na kukamilika kwa ukarabati na upanuzi wa miundombinu. Aidha, mwaka 2020 Serikali imewezesha ujenzi, ukarabati na upanuzi wa vyuo vya maendeleo ya wananchi 20 awamu ya pili na Vyuo vya Ufundi Stadi 53.

**Elimu ya Juu**

456. Mwaka 2019/20, idadi ya wanafunzi katika vyuo vikuu nchini iliongezeka kwa asilimia 4.1 na kuwa wanafunzi 189,291 ikilinganishwa na wanafunzi 181,897 mwaka 2018/19. Kati ya hao, wanawake walikuwa 79,426 sawa na asilimia 42.0 na wanaume 109,865. Ongezeko hilo, lilitokana na: kukamilika kwa ujenzi na ukarabati wa mabweni na hosteli za wanafunzi, kumbi za mihadhara na madarasa; ongezeko la programu 35 za kujifunza kwa njia ya mtandao; na juhudi za Serikali kuongeza mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu.

457. Mwaka 2019/20, Serikali kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 450.0 kwa wanafunzi 132,392 ikilinganishwa na mikopo yenye thamani shilingi bilioni 427.6 iliyotolewa kwa wanafunzi 123,329 mwaka 2018/19, sawa na ongezeko la asilimia 5.3. Kati ya wanafunzi waliopata mkopo, wanafunzi wa mwaka wa kwanza walikuwa 49,713 (wanafunzi yatima walikuwa 10,393, wenye ulemavu 415, kutoka kaya maskini 36,419 na wanafunzi waliofadhiliwa walikuwa 2,486) na wanafunzi 82,679 walikuwa wakiendelea na masomo. Aidha Serikali kupitia Bodi ya Mikopo ilikusanya marejesho ya mikopo kutoka kwa wanufaika kiasi cha shilingi bilioni 192.9 mwaka 2019/20 ikilinganishwa na shilingi bilioni 183.3 zilizokusanywa mwaka 2018/19.

**Teknolojia na Ubunifu**

458. Mwaka 2020, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (Arusha) ilikuwa na wanafunzi 722 (wanaume 472 na wanawake 250) ikilinganisha na wanafunzi 602 (wanaume 402 na wanawake 200) mwaka 2019. Aidha, wanafunzi 494 (wanaume 347 na wanawake 147) walihitimu masomo katika Taasisi hiyo mwaka 2020 ikilinganishwa na wanafunzi 373 (wanaume 280 na wanawake 93) waliohitimu mwaka 2019. Katika kipindi hicho, wanafunzi 6,137 (wanaume 4,764 na wanawake 1,373) walidahiliwa katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya ikilinganishwa na wanafunzi 5,320 (wanaume 4,199 na wanawake 1,121) mwaka 2019. Jumla ya

wanafunzi 1,203 (wanaume 952 na wanawake 251) walihitimu masomo katika Chuo hicho ikilinganishwa na wanafunzi 811 (wanaume 638 na wanawake 173) waliohitimu mwaka 2019. Vile vile, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam ilidahili wanafunzi 2,190 (wanaume 1,537 na wanawake 653) mwaka 2020 ikilinganishwa na wanafunzi 1,951 (wanaume 1,318 na wanawake 633) mwaka 2019. Idadi ya wanafunzi 604 (wanaume 466 na wanawake 138) wahitimu masomo katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam ikilinganishwa na wanafunzi 1,079 (wanaume 837 na wanawake 242) mwaka 2019.

459. Mwaka 2020, Serikali iliendesha Mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU) kwa lengo la kuchochea ubunifu na ugunduzi nchini ambapo wabunifu na wagunduzi 651 walitambuliwa ikilinganishwa na wabunifu na wagunduzi 415 mwaka 2019. Kati ya hao, wabunifu na wagunduzi 70 waliendelezwa ili kufikia hatua ya ubiasharishaji ikilinganishwa na wabunifu na wagunduzi 60 mwaka 2019. Vile vile, Serikali imetambua na kuhakiki teknolojia mpya 79 na kufanya jumla ya teknolojia zilizozalishwa nchini na zilizotambuliwa hadi sasa kufikia 310. Lengo la utambuzi huo ni kuwa na kanzidata ya kitaifa itakayorahisisha upatikanaji wa taarifa muhimu kuhusu teknolojia na ubunifu nchini.

.

## SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI: IDADI YA WANAFUNZI KWA KIDATO

Jedwali Na. 65 (Namba)

| Mwaka | I | II | III | IV | V | VI | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2003 | 52,863 | 60,643 | 36,906 | 35,653 | 7,780 | 6,885 | 200,730 |
| 2004 | 98,738 | 67,294 | 46,546 | 36,385 | 8,353 | 7,572 | 264,888 |
| 2005 | 134,963 | 109,398 | 46,188 | 46,489 | 9,710 | 8,444 | 355,192 |
| 2006 | 196,391 | 151,448 | 72,167 | 42,584 | 18,211 | 9,691 | 490,492 |
| 2007 | 401,011 | 218,060 | 105,770 | 70,796 | 21,789 | 11,668 | 829,094 |
| 2008 | 395,930 | 332,393 | 175,353 | 95,214 | 25,240 | 11,743 | 1,035,873 |
| 2009 | 480,529 | 308,131 | 159,789 | 167,355 | 31,201 | 12,695 | 1,159,700 |
| 2010 | 382,207 | 398,870 | 293,519 | 279,995 | 26,065 | 20,674 | 1,401,330 |
| 2011 | 403,873 | 396,724 | 380,528 | 279,117 | 30,265 | 25,164 | 1,515,671 |
| 2012 | 457,321 | 386,250 | 355,740 | 343,376 | 31,206 | 28,859 | 1,602,752 |
| 2013 | 444,532 | 506,036 | 193,901 | 302,963 | 30,581 | 26,698 | 1,504,711 |
| 2014 | 479,089 | 506,170 | 356,787 | 178,246 | 33,619 | 26,899 | 1,580,810 |
| 2015 | - | - | - | - | - | - | - |
| 2016 | 467,982 | 366,396 | 263,981 | 278,690 | 45,533 | 47,007 | 1,469,589 |
| 2017 | 491,535 | 443,614 | 296,034 | 236,775 | 53,749 | 43,494 | 1,565,201 |
| 2018 | 587,186 | 480,327 | 358,960 | 278,239 | 57,287 | 52,687 | 1,814,686 |
| 2019 | 637,335 | 555,087 | 388,029 | 334,284 | 52,428 | 56,042 | 2,023,205 |
| 2020 | 659,661 | 588,561 | 454,139 | 360,356 | 58,402 | 51,138 | 2,172,257 |
| Badiliko (%) 2019 - 2020 | 3.5 | 6.0 | 17.0 | 7.8 | 11.4 | -8.8 | 7.4 |

**Chanzo**: Wizara ya Elimu, Sayansi naTeknolojia
- Takwimu Hazikupatikana

**IDADI YA WANAFUNZI NA WALIMU KATIKA SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI KWA JINSIA**

Jedwali Na.65A

| **Elimu ya msingi** | **2019** | | | **2020** | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Waume** | **Wake** | **Jumla** | **Waume** | **Wake** | **Jumla** |
| Jumla ya wanafunzi wote walioandikishwa Darasa Ia I-VII | 5,300,782 | 5,304,648 | 10,605,430 | 5,443,914 | 5,481,982 | 10,925,896 |
| Jumla ya wanafunzi wanaosoma shule za binafsi Darasa Ia I-VII | 216,348 | 214,845 | 431,193 | 232,505 | 232,606 | 465,111 |
| Jumla ya walimu katika shule za msingi | 98,842 | 97,595 | 192,889 | 98,887 | 95,849 | 194,736 |
| Jumla ya walimu katika shule za msingi za Serikali | 86,280 | 88,526 | 173,851 | 84,673 | 85,896 | 170,569 |
| Jumla ya walimu katika shule za msingi za binafsi | 12,562 | 9,069 | 19,038 | 14,214 | 9,953 | 24,167 |
| **Elimu ya Sekondari** | | | | | | - |
| Jumla ya wanafunzi wote Kidato I-VI | 1,133,088 | 1,205,369 | 2,338,457 | 1,189,410 | 1,284,096 | 2,473,506 |
| Wanafunzi wanaosoma katika shule za Serikali, kidato I-VI | 982,220 | 1,040,985 | 2,023,205 | 1,045,557 | 1,126,700 | 2,172,257 |
| Wanafunzi wanaosoma katika shule za binafsi, kidato I-VI | 150,868 | 164,384 | 315,252 | 143,853 | 157,396 | 301,249 |
| Idadi ya walimu katika shule za Serikali | 53,570 | 30,536 | 84,106 | 54,221 | 30,393 | 84,614 |
| Idadi ya walimu katika shule za binafsi | 16,684 | 4,456 | 21,140 | 16,758 | 4,634 | 21,392 |
| Jumla ya Walimu katika shule za Sekondari | 70,254 | 34,992 | 105,246 | 70,979 | 35,027 | 106,006 |

**Chanzo**: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

- Takwimu Hazikupatikana

Jedwali Na. 65B **IDADI YA TAASISI ZA ELIMU**

| Aina ya Taasisi | 2019r | | | 2020 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Serikali | Binafsi | Jumla | Serikali | Binafsi | Jumla |
| Shule za Msingi | 16,223 | 1,581 | 17,804 | 16,406 | 1,746 | 18,152 |
| Shule za Sekondari | 3,742 | 1,259 | 5,001 | 3,863 | 1,280 | 5,143 |
| Vyuo vya Ualimu (Msingi na Sekondari) | 35 | 37 | 72 | 35 | 36 | 71 |
| Elimu ya Ufundi na Mafunzo | - | - | - | - | - | - |
| **Jumla** | **20,000** | **2,877** | **22,877** | **20,304** | **3,062** | **23,366** |

**Chanzo**: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia
- Takwimu hazikupatikana

Jedwali Na. 65C **MAFUNZO YA WALIMU KATIKA VYUO VYA UALIMU 2020**

| **Aina** | **2019** | | | **2020** | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Me** | **Ke** | **Jumla** | **Me** | **Ke** | **Jumla** |
| **Masomo ya Art** | | | | | | |
| Cheti (pre services) | 3,028 | 1,889 | 4,917 | 2,491 | 1,554 | 4,045 |
| Astashahada (in services) | 1,072 | 643 | 1,715 | 882 | 529 | 1,411 |
| Astashahada (pre services) | 4,243 | 2,228 | 6,471 | 3,491 | 1,833 | 5,324 |
| **Masomo ya Sayansi** | | | | | | |
| Cheti (pre services) | 164 | 115 | 279 | 135 | 95 | 230 |
| Astashahada (in services) | 598 | 355 | 953 | 492 | 292 | 784 |
| Astashahada (pre services) | 6,609 | 1,845 | 8,454 | 5,438 | 1,518 | 6,956 |
| **Elimu Maalum** | | | | | | |
| Astashahada (pre services) | 359 | 248 | 607 | 295 | 204 | 499 |
| **Jumla** | **16,073** | **7,323** | **23,396** | **13,224** | **6,025** | **19,249** |

**Chanzo**: Wizara ya Elimu, Sayansi na teknolojia

**SHULE ZA SEKONDARI ZA BINAFSI: IDADI YA WANAFUNZI KWA KIDATO**

Jedwali Na. 66

| Mwaka | I | II | III | IV | V | VI | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2004 | 48,752 | 46,167 | 33,240 | 24,476 | 8,847 | 6,229 | 167,711 |
| 2005 | 45,276 | 46,321 | 32,063 | 29,248 | 9,183 | 7,046 | 169,137 |
| 2006 | 46,968 | 48,013 | 42,878 | 29,796 | 9,569 | 7,956 | 185,180 |
| 2007 | 47,437 | 46,927 | 41,340 | 35,746 | 11,299 | 8,667 | 191,416 |
| 2008 | 42,971 | 43,232 | 43,177 | 35,980 | 12,576 | 8,594 | 186,530 |
| 2009 | 44,255 | 36,384 | 37,064 | 34,061 | 11,851 | 9,096 | 172,711 |
| 2010 | 56,620 | 57,876 | 50,778 | 46,820 | 12,269 | 13,006 | 237,369 |
| 2011 | 63,282 | 67,205 | 65,859 | 54,521 | 11,083 | 11,926 | 273,876 |
| 2012 | 65,058 | 69,403 | 64,453 | 61,209 | 9,684 | 11,713 | 281,520 |
| 2013 | 70,060 | 77,407 | 67,998 | 65,637 | 8,592 | 9,651 | 299,345 |
| 2014 | 109,784 | 96,732 | 76,574 | 66,898 | 8,865 | 7,686 | 366,539 |
| 2015 | - | - | - | - | - | - | - |
| 2016 | 70,844 | 81,499 | 72,970 | 73,231 | 21,091 | 17,731 | 337,366 |
| 2017 | 71,160 | 79,548 | 77,168 | 72,056 | 24,146 | 19,578 | 343,656 |
| 2018 | 64,844 | 71,685 | 74,932 | 74,848 | 24,030 | 23,441 | 333,780 |
| 2019 | 63,629 | 64,488 | 68,064 | 74,121 | 22,050 | 22,900 | 315,252 |
| 2020 | 63,232 | 64,727 | 64,328 | 67,255 | 20,032 | 21,675 | 301,249 |
| Badiliko (%) 2019 - 2020 | -0.6 | 0.4 | -5.5 | -9.3 | -9.2 | -5.3 | -4.4 |

**Chanzo**: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

Takwimu Hazikupatikana

# SURA YA 20

# AFYA NA MAENDELEO YA JAMII

## AFYA

### Vituo vya Kutolea Huduma za Afya

460. Mwaka 2020, Serikali iliendelea kuboresha na kusogeza huduma za afya karibu na wananchi ambapo vituo vya kutolea huduma za afya viliongezeka na kufikia vituo 9,813 kutoka vituo 9,104 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 7.8. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa uwekezaji wa Serikali, mashirika ya dini na sekta binafsi katika ujenzi wa hospitali na vituo vya afya. Kati ya vituo hivyo, Serikali ilikuwa inamiliki asilimia 64 ya vituo vyote, Mashirika ya dini asilimia 9, na vituo binafsi asilimia 27. Kwa upande mwingine, mchanganuo wa vituo vya kutolea huduma za afya unaonesha kuwa hospitali zilikuwa asilimia 4, vituo vya afya asilimia 10, zahanati asilimia 72, kliniki na “maternity homes” asilimia 14 kwa mwaka 2020.

461. Mwaka 2020, idadi ya wagonjwa waliohudumiwa walipungua kwa asilimia 9.6 na kufikia wagonjwa 44,349,923 kutoka wagonjwa 49,050,625 mwaka 2019. Kati ya hao, wagonjwa wa kulazwa walikuwa 1,696,968 na wagonjwa wa nje walikuwa 42,652,955 ikilinganishwa na wagonjwa wa kulazwa 1,852,720 na wagonjwa wa nje 47,197,905 mwaka 2019. Kupungua kwa wagonjwa waliohudumiwa kulitokana na wananchi kuwa na hofu ya maambukizi ya UVIKO-19 na kuongezeka kwa matumizi ya tiba mbadala. Kwa upande mwingine, idadi ya vitanda vya wagonjwa iliongezeka na kufikia 84,162 mwaka 2020 ikilinganishwa na vitanda 80,164 mwaka 2019.

### Huduma za chanjo kwa Watoto Chini ya Mwaka Mmoja

462. Mwaka 2020, watoto 1,823,380 walizaliwa ikilinganishwa na watoto 1,794,856 waliozaliwa mwaka 2019. Katika kipindi hicho, asilimia 98 ya watoto walipata huduma ya chanjo ya PENTA-3, Surua rubella (asilimia 98), Rota2 (asilimia 91.5), OPV 1 (asilimia 84) na OPV 2 (asilimia 75). Chanjo hizo hutolewa kwa lengo la kuzuia magonjwa ya kupooza, kuharisha, pepopunda, *pneumonia*, homa ya ini, homa ya uti wa mgongo, surua, polio na dondakoo kwa watoto walio chini ya mwaka mmoja. Aidha, Tanzania iliendelea kutoa chanjo hizo ili kukidhia vigezo vya Shirika la Afya Duniani vinavyotaka nchi kuhakikisha kuwa zaidi ya asilimia 90 ya watoto wa chini ya mwaka mmoja wanapata chanjo.

### Dawa na Vifaa Tiba

463. Mwaka 2020, Serikali iliendelea kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi katika vituo vya kutolea huduma za afya. Katika kipindi hicho, upatikanaji wa dawa muhimu zinazofuatiliwa (*30 tracer medicines*) katika vituo vya kutolea huduma za afya ulikuwa asilimia 86 ikilinganishwa na asilimia 94.4 kwa mwaka 2019.

Hali ya upatikanaji wa aina 312 za dawa muhimu na za kipaumbele ilikuwa asilimia 76 ikilinganishwa na asilimia 86 kwa mwaka 2019. Serikali iliboresha huduma za uchunguzi kwa kununua, kusimika vifaa tiba mbalimbali (*MRI*, *CT-scan*, *Fluoroscopy*, *X-ray*, *Ultrasound*) na kuanza kutoa huduma katika hospitali za Rufaa za mkoa za Mkuranga, Mwananyamala, Temeke, Amana na Kigoma.

464. Mwaka 2020, Serikali iliendelea kuimarisha huduma za uchunguzi na tiba ya Saratani nchini kwa kununua dawa za saratani na mashine mpya za kisasa za: *Positron Emmission Tomography* (PET Scan); *Tumor marker* kwa ajili ya kuchunguza matokeo ya tiba ya saratani kwa njia ya damu; *Oxygen Concentrators* 25 kwa ajili ya wagonjwa wanaolazwa wenye uhitaji maalumu wa hewa ya *oxygen*; *PCR Machine* kwa ajili ya kupima virusi mbalimbali hususan vinavyosababisha saratani; na kufunga mashine zenye uwezo mkubwa wa vipimo vya kikemia na *X-ray* ya upimaji wa matiti (*Mammography*).

**Afya ya Uzazi na Mtoto**

465. Mwaka 2020, idadi ya wajawazito 2,394,736 walihudhuria kliniki ikilinganishwa na wajawazito 2,320,559 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 3.2. Hii ilitokana na Serikali kuendelea kuhamasisha wajawazito kuanza huduma ya afya ya uzazi na mtoto kabla ya majuma 12 ya ujauzito na kuhudhuria kliniki angalau mara nne katika kipindi cha ujauzito. Aidha, asilimia 37.7 ya wajawazito walifanya hudhurio la kwanza kabla ya majuma 12 mwaka 2020 ikilinganishwa na asilimia 34 mwaka 2019. Wajawazito waliohudhuria kliniki angalau mara nne waliongezeka kutoka asilimia 80.4 mwaka 2019 hadi asilimia 90.1 mwaka 2020. Kwa upande mwingine, huduma ya kumkinga mama mjamzito dhidi ya malaria ilifikia asilimia 79 ikilinganishwa na asilimia 83.7 mwaka 2019. Katika kipindi hicho, wajawazito waliohudhuria kliniki na kupima Virusi Vya Ukimwi (VVU) walikuwa asilimia 98 ikilinganishwa na asilimia 99 kwa mwaka 2019. Kati ya wajawazito waliopima VVU, asilimia 1.8 waligundulika kuwa na VVU na asilimia 99 ya waliogundulika na VVU walianzishiwa matibabu ya ART (*Antiretoviral therapy*).

466. Mwaka 2020, idadi ya vituo vilivyokarabatiwa kwa ajili ya kutoa huduma ya upasuaji wa kumtoa mtoto tumboni iliongezeka na kufikia 487 mwaka 2020 kutoka vituo 352 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 38.4. Hii ilichangiwa na jitihada za Serikali kwa kushirikiana na wadau wa sekta binafsi kuendelea kuboresha miundombinu ya afya. Aidha, idadi ya vituo vya kutolea huduma za uchunguzi wa mabadiliko ya awali ya saratani iliongezeka na kufikia vituo 746 mwaka 2020 kutoka vituo 624 mwaka 2019, ambapo wanawake 533,780 walifanyiwa uchunguzi ikilinganishwa wanawake 413,851 mwaka 2019. Kwa upande mwingine, chanjo aina ya HPV ilitolewa kwa asilimia 81 kwa wasichana wenye umri kati ya miaka 9 hadi 14 kwa

ajili ya kuwakinga na Saratani ya Mlango wa Kizazi ikilinganishwa na asilimia 79 mwaka 2019.

**Huduma za Matibabu ya Kibingwa**

467. Mwaka 2020, Serikali imeendelea kuboresha huduma za matibabu ya kibingwa ambapo jumla ya wagonjwa 78 walipandikizwa figo ukilinganishwa na wagonjwa 15 mwaka 2019. Kati ya hao, wagonjwa 62 walipandikizwa figo katika hospitali ya Taifa Muhimbili na wagonjwa 16 katika Hospitali ya Benjamin Mkapa Dodoma ikilinganishwa na wagonjwa nane (8) walipandikizwa figo katika hospitali ya Taifa Muhimbili na wagonjwa saba (7) katika Hospitali ya Benjamin Mkapa Dodoma mwaka 2019. Aidha, watoto 34 walipata huduma ya upandikizaji wa vifaa vya usikivu katika Hospitali ya Taifa Muhimbili mwaka 2020 ikilinganishwa na watoto tisa (9) mwaka 2019.

**Udhibiti wa Malaria**

468. Mwaka 2020, Serikali iliendelea kuhakikisha kuwa vipimo vya malaria vinapatikana katika vituo vya kutolea huduma za afya ambapo vitendanishi vya malaria vipimo 40,821,350, dawa ya mseto dozi 16,514,790 na dawa ya malaria ya sindano vichupa 4,102,658 vilinunuliwa na kusambazwa ikilinganishwa na vitendanishi vya malaria vipimo 25,699,500, dawa ya mseto dozi 10,668,600 na dawa ya malaria ya sindano vichupa 1,205,876 mwaka 2019. Aidha, vyandarua 7,951,345 vilinunuliwa na kusambazwa mwaka 2020 ikilinganishwa na vyandarua 3,266,260 vilivyonunuliwa na kusambazwa mwaka 2019. Kwa upande mwingine, kiwango cha ugonjwa wa malaria kwa watoto chini ya miaka mitano kiliendelea kuwa asilimia 7.3 kama ilivyokuwa mwaka 2019 na kiwango cha malaria kwa wajawazito kilikuwa asilimia 7.8 mwaka 2020 ikilinganishwa na asilimia 6.6 mwaka 2019.

469. Mwaka 2020, Serikali iliendelea na juhudi za kukabiliana na ugonjwa wa malaria kwa kutekeleza afua mbalimbali ikiwemo ufuatiliaji na ukusanyaji wa sampuli za mbu uliofanyika katika Halmashauri 62 katika mikoa yote nchini ambapo mbu 50,268 walikusanywa. Kati ya hao, mbu 11,713 ambao ni wa aina ya anofelesi wanaoambukiza malaria walipelekwa katika Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu Muheza kwa ajili ya uchunguzi wa kimaabara.Vile vile, Serikali ilianzisha afua mpya ya ufuatiliaji wa wagonjwa wa malaria hadi ngazi ya kaya kwa mikoa yenye kiwango kidogo cha maambukizi ya malaria nchini ambayo ni Kilimanjaro, Arusha na Manyara.

**Udhibiti wa Kifua Kikuu**

470. Hadi Desemba 2020, Serikali iliendelea na mapambano dhidi ya kifua kikuu ambapo iligundua na kuwanzishia dawa wagonjwa 39,044 sawa na asilimia 86 ya lengo la wagonjwa 45,328. Hii ilitokana na kampeni za uchunguzi zilizofanyika kwa kushirikisha watoa huduma katika ngazi ya jamii. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na wadau wa sekta ya afya ilinunua Mashine 21 za *GeneXpert* mwaka 2020 ikilinganishwa

na mashine 28 mwaka 2019 na kufanya jumla ya mashine hizo kufikia 259. Vile vile, vituo vya kutolea huduma za uchunguzi na tiba ya kifua kikuu viliongezeka na kufikia 1,613 mwaka 2020 kutoka vituo 1,201 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 34.3. Hii ilichangiwa na jitihada za Serikali kwa kushirikiana na wadau wa sekta ya afya kuendelea kuboresha miundombinu ya afya.

**UVIKO - 19**

471. Ugonjwa wa homa kali ya mapafu unaosababishwa na virusi vya corona ujulikanao kama UVIKO-19 ulianzia nchini China mwishoni mwa mwaka 2019. Kwa mara ya kwanza ugonjwa huo uliripotiwa kuingia nchini katika jiji la Arusha tarehe 16 Machi, 2020 na kuendelea kusambaa kutoka maambukizi yanayoletwa na kusababishwa na watu wanaotoka nje ya nchi kuja nchini hadi kufikia maambukizi ya ndani ya jamii. Tanzania kama mataifa mengine duniani iliathirika na ugonjwa huu kiuchumi na kijamii. Hata hivyo, Serikali imekuwa ikishirikiana na wadau katika kukabiliana na mlipuko wa UVIKO -19 kwa kuhakikisha afua mbalimbali zinatekelezwa katika ngazi zote. Afua hizo ni pamoja na: kuhamasisha uvaaji wa barakoa, unawaji wa mikono na kuepuka misongamano; ufuatiliaji wa wagonjwa mipakani; na kuongeza vifaa, vifaa tiba na dawa katika vituo vya kutolea huduma ikiwemo ununuzi na usimikaji wa Mitambo ya kuzalishia Oxygeni katika Hospitali za Amana (Dar es Salaam), Ligula (Mtwara), Ruvuma, Mbeya, Geita, Manyara na Dodoma. Katika kukabiliana na UVIKO-19 Serikali ilichukua hatua mbalimbali zikiwemo; kusitisha kwa muda safari za anga nje ya nchi, shughuli za michezo na burudani; kusitishwa kwa mikusanyiko ya aina yote; kutoa elimu kwa umma kuhusu UVIKO -19; kutenga maeneo maalum kwa ajili ya kuwahudumia wagonjwa wa UVIKO -19; na kuahirisha baadhi ya matumizi yaliyopangwa katika bajeti ya 2019/20 ili fedha hizo zielekezwe kwenye mapambano dhidi ya UVIKO-19. Aidha, Serikali iliendelea kuhimiza matumizi ya tiba mbadala katika kukabiliana na UVIKO -19. Vilevile, mwaka 2020 Serikali ilikamilisha mradi wa kimkakati wa ujenzi wa maabara ya kisasa ya afya ya jamii iliyopo Mabibo, Dar es Salaam. Maabara hiyo ina uwezo wa kupima sampuli 1,800 za wagonjwa wa COVID-19 ndani ya masaa 24 ikilinganishwa na uwezo wa awali wa kupima sampuli 300 tu.

**Lishe**

472. Mwaka 2020, Serikali iliendelea kutekeleza Mpango Jumuishi wa Taifa wa Lishe (2016/17 - 2020/21) ili kukabiliana na athari za lishe duni na kuimarisha ukuaji mzuri wa mwili na akili kwa mtoto. Katika kipindi hicho, zaidi ya asilimia 90 ya watoto milioni 9 walio chini ya umri wa miaka mitano walipatiwa matone ya Vitamini A. Aidha, asilimia 91.3 ya watoto waliozaliwa katika vituo vya kutolea huduma za afya walinyonyeshwa ndani ya saa moja baada ya kuzaliwa ikilinganishwa na asilimia 89.9 walionyonyeshwa mwaka 2019. Vile vile, asilimia 5.6 ya watoto walizaliwa na uzito pungufu mwaka 2020 ikilinganishwa na asilimia 5.7 ya watoto mwaka 2019. Kwa upande mwingine, asilimia 0.9 ya wajawazito waliopimwa wingi wa damu katika

hudhurio la kwanza walikuwa na upungufu mkubwa wa damu ikilinganishwa na asilimia 1.4 mwaka 2019.

**Mafunzo katika Kada za Afya**

473. Mwaka 2020, wanafunzi waliodahiliwa katika vyuo vya afya walikuwa 35,501 ikilinganishwa na wanafunzi 25,077 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 41.6. Hii ilichangiwa na kukamilika kwa upanuzi na ukarabati wa vyuo vya afya, uanzishwaji wa vyuo vipya vya binafsi na mwitikio wa wanafunzi kujiunga na mafunzo ya kada za afya. Kati ya hao, wanafunzi 9,696 walijiunga vyuo vya Serikali na wanafunzi 25,815 vyuo binafsi katika programu za uuguzi na ukunga, sayansi shirikishi za afya na wahudumu wa afya ya jamii.

## MAENDELEO YA JAMII

**Mafunzo ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii**

474. Mwaka 2020, Serikali kupitia vyuo vya maendeleo ya jamii vya Buhare, Monduli, Mlale, Mabughai, Misungi, Ruaha, Rungemba na Uyole ilidahili jumla ya wanafunzi 4,853 (wanawake 2,982 na wanaume 1,871) ikilinganishwa na wanafunzi 3,986 (wanawake 2,438 na wanaume 1,548) mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 21.8. Ongezeko hilo lilichangiwa na kuboreshwa kwa mazingira ya kujifunza na kufundishia. Aidha, wanafunzi 3,953 wa fani ya maendeleo ya jamii walihitimu ngazi ya stashahada na astashahada mwaka 2020 ikilinganishwa na wanafunzi 3,307 waliohitimu mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 19.5.

475. Mwaka 2020, Serikali kupitia Taasisi ya Maendeleo ya Jamii – Tengeru ilidahili wanafunzi 2,492 (wanawake 821 na wanaume 1,671) ikilinganishwa na wanafunzi 1,971 (wanawake 1,350 na wanaume 621) mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 26.4. Ongezeko hilo lilichangiwa na kuboreshwa kwa mazingira ya kujifunza na kufundishia ikiwemo ukarabati wa miundombinu ya maji, umeme na TEHAMA. Katika kipindi hicho, wanafunzi 1,003 (wanaume 262 na wanawake 741) walihitimu katika fani na ngazi mbalimbali ikilinganishwa na wanafunzi 917 (wanaume 286 na wanawake 631) mwaka 2019.

476. Mwaka 2020, Serikali kupitia Taasisi ya Ustawi wa Jamii Kijitonyama ilidahili wanafunzi 2,187 (wanawake 1,434 na wanaume 753) ikilinganishwa na wanafunzi 1,799 (wanawake 1,275 na wanaume 524) mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 21.6. Ongezeko hili lilichangiwa na kuboreshwa kwa mazingira ya kujifunzia ikiwa ni pamoja na ununuzi wa viti 320 na jenereta linalosaidia kuimarisha upatikanaji wa nishati ya umeme. Katika kipindi hicho, wanafunzi 1,246 (wanaume 318 na wanawake 928) walihitimu katika fani na ngazi mbalimbali ikilinganishwa na wanafunzi 1,368 (wanaume 393 na wanawake 975) mwaka 2019.

477. Mwaka 2020, Serikali imeendelea kufanya maboresho ya utoaji wa mafunzo ya taaluma ya maendeleo ya jamii kwa kutekeleza Programu ya Uanagenzi inayolenga kuwaunganisha wanafunzi na wahitimu kwenye Taasisi, Mashirika na Makampuni ili kupata mafunzo kwa vitendo, mafunzo ya ujuzi wa kujiajiri na kuajiriwa unaoendana na soko la ajira. Katika kipindi hicho, jumla ya wanafunzi na wahitimu 219 wa taaluma ya maendeleo ya jamii waliunganishwa na taasisi, mashirika na makampuni kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo.

**Maendeleo ya Wanawake na Jinsia**

478. Mwaka 2020, Serikali kupitia dirisha la wanawake katika Benki ya Posta Tanzania iliendelea kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wajasiriamali wanawake ambapo shilingi milioni 9,994.8 zilitolewa kwa wajasiriamali wanawake 5,234 ikilinganishwa na shilingi milioni 3,586.4 zilizotolewa kwa wajasiriamali wanawake 14,271 mwaka 2019. Kiasi cha fedha kilichotolewa kwa wanawake wajasiriamali kiliongezeka kutokana na ukuaji wa mtaji mwaka hadi mwaka. Hata hivyo, idadi ya wanawake wajasiriamali waliopatiwa mkopo ilipungua kwa kuwa mwaka 2020 wanawake wajasiriamali wamepatiwa mikopo mikubwa ukilinganisha na mwaka 2019.

479. Mwaka 2020, Serikali iliwezesha kuanzishwa na kupewa mafunzo kwa Kamati 4,823 (14 ngazi ya halmashauri, 452 kata, 4,250 kijiji na 107 mtaa) za ulinzi wa wanawake na watoto ikilinganishwa na kamati 4392 (11 ngazi ya halmashauri, 309 kata, 3973 kijiji na 99 mtaa) mwaka 2019. Katika kipindi hicho, Serikali ilianzisha dawati la jinsia katika vyuo vikuu vya Dar es Salaam, Dodoma na Mzumbe, pamoja na Taasisi za Ustawi wa Jamii Kijitonyama na Maendeleo ya Jamii Tengeru.

**Huduma za Ustawi na Maendeleo ya Watoto**

480. Mwaka 2020, Serikali iliendelea kutekeleza afua mbalimbali zinazotoa fursa kwa watoto walio katika mazingira hatarishi kulelewa katika familia, ambapo jumla ya watoto 217 (wasichana 110 na wavulana 107) walio katika mazingira hatarishi walipata huduma za malezi ya kambo ikilinganishwa na watoto 65 waliopata huduma za malezi ya kambo mwaka 2019. Aidha, watoto 95 (wasichana 44 na wavulana 51) waliasiliwa mwaka 2020 ikilinganishwa na watoto 49 (wasichana 23 na wavulana 26) walioasiliwa mwaka 2019.

481. Mwaka 2020, Serikali iliendelea kutoa huduma za msingi pamoja na huduma za msaada wa kisheria kwa watoto walio katika mkinzano na sheria katika mahabusu za watoto za Mbeya, Kilimanjaro, Tanga, Arusha na Dar es Salaam. Katika kipindi hicho, jumla ya watoto 138 (wasichana 18 na wavulana 120) walio katika mkinzano na sheria walipata huduma za chakula, malazi, mavazi, huduma za matibabu na elimu ikilinganishwa na watoto 250 (wasichana 19 na wavulana 231) mwaka 2019. Aidha, jumla ya watoto 78 (wasichana 5 na wavulana 73) waliokuwa katika mkinzano na sheria

walichepushwa kutoka katika mfumo rasmi wa haki jinai kwa kuwarekebisha tabia na kuwaunganisha na familia zao mwaka 2020 ikilinganishwa na watoto 148 (wasichana 59 na wavulana 89) mwaka 2019.

482. Mwaka 2020, Serikali iliendelea kuwezesha upatikanaji wa huduma za chakula, malazi, elimu, mavazi na matibabu pamoja na marekebisho ya tabia kwa watoto waliobainika na makosa ya jinai katika shule ya maadilisho Irambo - Mbeya. Katika kipindi hicho, watoto 31 (Msichana mmoja na wavulana 30) walihukumiwa na kupelekwa katika shule ya maadilisho Irambo Mbeya ikilinganishwa na watoto 32 (wasichana 2 na wavulana 30) mwaka 2019.

483. Mwaka 2020, Serikali iliendelea na jitihada za kuhakikisha watoto walio katika mazingira hatarishi wanapata malezi bora ikiwemo, chakula, mavazi, malazi, elimu na huduma za afya katika Makao ya Taifa ya Watoto ya Kurasini Dar es Salaam na Kikombo Dodoma. Katika kipindi hicho, jumla ya watoto 80 (wasichana 40 na wavulana 40) walipatiwa huduma ikilinganishwa na watoto 75 (wasichana 42 na wavulana 33) waliopata huduma mwaka 2019. Aidha, watoto 15,290 (wasichana 7,053 na wavulana 8,237) walipatiwa huduma kupitia makao binafsi ya watoto mwaka 2020 ikilinganishwa na watoto 13,349 (wasichana 6,618 na wavulana 6,731) waliopatiwa huduma mwaka 2019.

**Huduma ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto**

484. Mwaka 2020, Serikali ilisajili vituo 134 vya kulelea watoto wadogo mchana ikilinganishwa na vituo 373 mwaka 2019 na kufanya jumla ya vituo vilivyosajiliwa kufikia 1,677. Katika kipindi hicho, jumla ya watoto 163,394 (wavulana 85,175 na wasichana 78,219) waliandikishwa ikilinganishwa na watoto 159,479 (wavulana 82,539 na wasichana 76,940) mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 2.5. Hili ilitokana na kuongezeka kwa mwamko wa wazazi kuandikisha watoto wadogo kulelewa katika vituo. Aidha, idadi ya walezi wa watoto katika vituo vya kulelea watoto wadogo mchana iliongezeka na kufikia walezi 2,878 mwaka 2020 kutoka walezi 2,563 mwaka 2019. Ongezeko hili linatokana kuongezeka kwa idadi ya vituo vya kulea watoto wadogo mchana. Kwa upande mwingine, Serikali iliendelea kuwajengea uwezo wazazi na walezi wa watoto kupitia maafisa maendeleo ya jamii ambapo vikundi 2,777 vya malezi viliundwa mwaka 2020 ikilinganishwa na vikundi 1,186 mwaka 2019. Vikundi hivyo vinalenga kuhamasisha na kuhimiza malezi chanya kwa familia na jamii.

**Huduma za Ustawi kwa Wazee**

485. Mwaka 2020, Serikali iliendelea kutoa huduma za chakula, malazi, mavazi na matibabu kwa wazee wasiojiweza katika makazi 13 ya wazee ambapo wazee 291 (wanawake 111 na wanaume 180) walipatiwa huduma hizo ikilinganishwa na wazee 383 (wanawake 179 na wanaume 204) waliopatiwa huduma mwaka 2019, sawa na

upungufu wa asilimia 24.0. Upungufu huu ulichangiwa na baadhi ya wazee kuunganishwa na familia zao.

**Mashirika yasiyo ya kiserikali**

486. Mwaka 2020, Serikali ilisajili mashirika yasiyo ya kiserikali 377 (ngazi ya kimataifa 11, kitaifa 353 na kimkoa 13) ikilinganishwa na mashirika yasiyo ya kiserikali 1,402 (ngazi ya kimataifa 133, kitaifa 1,251, kimkoa 9 na wilaya 9) yaliyosajiliwa mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 73.1. Hii ilitokana na mwaka 2019 kuanza kwa utekelezaji wa Sheria ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali Na. 24 ya Mwaka 2002 na Kanuni zake za mwaka 2019 iliyowataka mashirika yote kujisajili upya chini ya sheria husika.

487. Mwaka 2020, Serikali ilifanya ufuatiliaji wa utendaji wa mashirika 206 ikilinganishwa na mashirika 113 mwaka 2019. Aidha, mikataba ya fedha 130 ya mashirika yasiyo ya kiserikali, yenye thamani ya jumla ya shilingi bilioni 118.4 ilipokelewa na kukaguliwa. Vile vile, wasajili wasaidizi 89 kutoka katika mikoa ya Dodoma, Singida, Kilimanjaro, Arusha, Manyara na Tabora walipatiwa mafunzo juu ya usajili na uratibu wa shughuli za mashirika yasiyo ya kiserikali.

.

Jedwali Na. 67

## IDADI YA VITUO VYA KUTOLEA HUDUMA ZA AFYA

| Aina ya Vituo | 2018 | | | | 2019 | | | | 2020 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Binafsi | Serikali | Dini | Jumla | Binafsi | Serikali | Dini | Jumla | Binafsi | Serikali | Jumla |
| Zahanati | 986 | 5,055 | 659 | 6,700 | 1,235 | 5,136 | 871 | 7242 | 1768 | 5395 | 7163 |
| Vituo vya Afya | 127 | 551 | 156 | 834 | 153 | 587 | 170 | 910 | 281 | 645 | 926 |
| Hospitali | 50 | 127 | 108 | 285 | 57 | 121 | 116 | 294 | 184 | 185 | 369 |
| Nyinginezo* | 225 | 21 | - | 246 | 168 | 4 | 434 | 606 | 1355 | 1 | 1356 |
| Maternity/Nursing Homes | 52 | 2 | - | 54 | 49 | 1 | 2 | 52 | - | - | - |
| **Jumla** | **1,440** | **5,756** | **923** | **8,119** | **1,662** | **5,849** | **1,593** | **9,104** | **3,588** | **6,226** | **9,814** |

**Chanzo**: Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto
* Ni pamoja na kliniki
- Takwimu hazikupatikana

**IDADI YA WAGONJWA KATIKA VITUO VYA KUTOLEA HUDUMA ZA AFYA**

Jedwali Na. 68

| Mwaka | Wagonjwa wa Nje | | | Jumla ya Wagonjwa waliolazwa |
|---|---|---|---|---|
| | Hospitali | Zahanati | Vituo vya Afya | |
| 2002 | 1,328,395 | 19,695,356 | 3,258,520 | 701,568 |
| 2003 | 1,491,909 | 22,935,688 | 3,659,615 | 1,390,273 |
| 2004 | 1,532,028 | 23,552,460 | 3,758,027 | 2,125,388 |
| 2005 | 1,619,700 | 24,900,276 | 3,973,085 | 2,237,146 |
| 2006 | 1,754,925 | 26,979,136 | 4,304,787 | 2,837,252 |
| 2007 | 1,842,671 | 28,328,093 | 4,520,026 | 2,979,115 |
| 2008 | 1,934,805 | 29,744,498 | 4,746,027 | 3,128,071 |
| 2009 | 2,128,286 | 32,718,948 | 5,220,630 | 3,440,870 |
| 2010 | 2,341,114 | 35,990,843 | 5,742,693 | 3,784,957 |
| 2011 | 2,622,048 | 39,917,117 | 6,431,816 | 4,239,152 |
| 2012 | 2,815,529 | 41,333,522 | 6,657,817 | 4,388,108 |
| 2013 | 2,903,275 | 42,682,479 | 6,873,056 | 4,529,971 |
| 2014 | 5,910,725 | 14,008,692 | 475,295 | 1,665,935 |
| 2015 | 4,480,781 | 25,072,487 | 6,006,466 | 1,858,956 |
| 2016 | 4,984,645 | 20,859,281 | 6,515,219 | 1,775,835 |
| 2017 | 5,266,252 | 21,115,639 | 7,050,725 | 1,650,224 |
| 2018 | 4,675,045 | 27,473,506 | 8,903,461 | 1,359,264 |
| 2019 | 9,821,148 | 26,500,182 | 10,153,322 | 1,852,720 |
| 2020 | 10,150,504 | 22,154,653 | 9,741,820 | 1,852,720 |

**Chanzo**: Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

Jedwali Na. 69. **IDADI YA VITANDA KATIKA HOSPITALI ZOTE NCHINI**

| **Aina ya Huduma** | **2019** | | | | **2020** | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Serikali** | **Shirika la kujitolea/Dini** | **Binafsi** | **Jumla** | **Serikali** | **Shirika la kujitolea/Dini** | **Binafsi** | **Jumla** |
| Hospitali za Mikoa | 6,692 | 1,033 | 480 | 8,205 | 7,307 | 898 | 420 | 8,625 |
| Hospitali za Wilaya | 9,919 | 6,154 | 2,911 | 18,984 | 10,328 | 7,629 | 409 | 18,366 |
| Hospitali nyingine | 1,420 | 6,865 | 1,108 | 9,393 | 1,820 | 8,753 | 1,559 | 12,132 |
| Vituo vya Afya | 15,221 | 5,373 | 3,674 | 24,268 | 16,211 | 6,223 | 2,225 | 24,659 |
| Zahanati | 11,818 | 4,979 | 2,517 | 19,314 | 13,549 | 3,712 | 3,119 | 20,380 |
| **Jumla** | **45,070** | **24,404** | **10,690** | **80,164** | **49,215** | **27,215** | **7,732** | **84,162** |

**Chanzo**; Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto

**UDAHILI WA WANAFUNZI KATIKA TAASISI ZA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII**

Jedwali. Na. 70

| | Ngazi ya Elimu | 2019 | | | 2020 | | | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Me | Ke | Jumla | Me | Ke | Jumla | |
| **Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru** | Astashahada | 324 | 115 | 439 | 870 | 357 | 1227 | 179.5 |
| | Stashahada | 542 | 152 | 694 | 229 | 83 | 312 | -55 |
| | Shahada | 367 | 262 | 629 | 553 | 366 | 919 | 46.1 |
| | Stashahada ya Juu ya Maendeleo ya Jamii | 117 | 92 | 209 | 19 | 15 | 34 | -83.7 |
| | **Jumla Ndogo** | **1,350** | **621** | **1,971** | **1,671** | **821** | **2,492** | **26.4** |
| **Taasisi ya Ustawi wa Jamii Kijitonyama** | Astashahada | 249 | 671 | 920 | 375 | 545 | 920 | 0 |
| | Stashahada | 48 | 177 | 225 | 145 | 402 | 547 | 143.1 |
| | Shahada | 207 | 404 | 611 | 221 | 469 | 690 | 12.9 |
| | Stashahada ya Juu | 15 | 10 | 25 | 8 | 12 | 20 | -20 |
| | Shahada ya Uzamili | 5 | 13 | 18 | 4 | 6 | 10 | -44.4 |
| | **Jumla Ndogo** | **524** | **1,275** | **1,799** | **753** | **1,434** | **2,187** | **21.6** |
| **Vyuo vya Maendeleo ya Jamii** | Stashahada | 307 | 572 | **879** | 357 | 843 | **1,200** | 36.5 |
| | Astashahada | 1241 | 1,866 | **3,107** | 1514 | 2,139 | **3,653** | 17.6 |
| | **Jumla Ndogo** | **1,548** | 2,438 | **3,986** | **1,871** | 2,982 | **4,853** | **21.8** |

**Chanzo**: Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto